

Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 29 Mei, 2014

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na :-

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

AIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE. JEROME D. BWANAUSI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014

Nakala ya Mtandao (Online Document)

na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE. MOSES J. MACHALI (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa Wizara ya Nishati na Madini Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, leo ni maswali kwa Waziri Mkuu bahati ninamwona Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, kama ilivyo kwa mujibu wa Kanuni zetu yeye ndiye atakayeanza kumwuliza Maswali Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu Maswali. Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati unahitimisha hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ultanabaHisha kwamba, uchaguzi wa Serikali za Mitaa utafanyika kama ilivyo kawaida mwisho wa mwaka huu 2014.

Vilevile, ulilifahamisha Taifa kwamba, wakati huo huo zoezi la uandikishaji wapiga kura katika utaratibu mpya wa biometric utakuwa unatumika.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uzoefu wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Mwaka 2004 na zaidi Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2009 ambao ulisimamiwa na Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura ya 287 na Sheria ya Serikali za Miji, Sura ya 288, Uchaguzi huu uligubikwa na vurugu nydingi sana.

Pia uliishawahi kutoa kauli huko nyuma kwamba, Serikali itaangalia upya sheria ile ili pengine kuifanya marekebisho ya msingi kabla ya uchaguzi wa mwaka huu 2014 ili matatizo yale yasijirudie tena.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni miezi michache imebakia kabla ya Uchaguzi huo. Unaliambia nini Taifa kuhusu maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Vijiji mwisho wa mwaka huu? (Makofii)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba tu kueleza kwa ufupi kwamba, mambo ambayo tumeishaanza kuyafanya kazi; kwanza ni maandalizi tu ya kibajeti ambayo tulizungumza wakati wa kuhitimisha Bajeti ya Waziri Mkuu.

Pili, huwa tunakuwa na utaratibu wa kushirikisha wadau wote wakati wa kuandaa Kanuni ambazo tunafikiria zinaweza zikasaidia katika kusimamia vizuri zoezi hili. Kwa hiyo, nalo tumeishaanza kuliangalia kwa maana ya kutafuta Kanuni za mara ya mwisho turekebishe mahali gani ili tuweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, tatu ni hili ambalo amelieleza. Ni kweli kwamba tulitoa hiyo kauli na tumeishaomba watu wa TAMISEMI waangalie kama kuna maeneo hasa ambayo tunafikiria pengine yangeweza kufanyiwa marekebisho kabla ya Uchaguzi Mkuu. Sasa kama yatabainika basi tutaleta hiyo rai mbele yetu.

Wakati huo huo labda niseme tu kwamba, kwa sababu na ninyi ni wadau wakubwa kwa maana ya vyama vya Upinzani, ni rai yangu tu kwamba na ninyi mngeanza kulitazama vilevile kama kuna maeneo ambayo mnafikiria yangeweza kupendekezwa ili na yenyewe tuweze kuyachukua wakati tunajaribu kutazama na sisi upande wetu, tutashukuru vilevile. (Makofii)

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru kwa majibu yako ya awali.

Ni kweli sisi kama wadau muhimu yako maeneo mengi sana ambayo yanalamikiwa katika Kanuni hizi ambazo mara ya mwisho zilitungwa mwaka 2009 na ni dhahiri tutatoa mapendekezo mengi tu ya mabadiliko katika Kanuni hizi ili kuufanya uchaguzi huu uwe huru na amani zaidi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hata hivyo, tatizo hapa siyo mapendekezo yetu, ila ni utayari wenu wa kukubali mapendekezo ambayo wadau watayatoa, kwa sababu tukikumbuka katika uchaguzi wa mwaka 2009 yako mapendekezo kadha wa kadha ambayo yalitolewa kwa Serikali lakini ikayapuuza na matokeo yake uchaguzi ule ukaghubikwa na vurugu nydingi.

Sasa badala ya kusubiri wadau wapendekeze bila utaratibu unaoeleweka unaonaje kama leo utalipa Taifa taarifa kwamba, unakusudia kuita kikao cha wadau mapema sana ili mambo haya yajadiliwe mapema kabla hujafika hatua ya kumaliza Kanuni wewe na TAMISEMI ambao ni washindani katika zoezi hili? (Makofii)

Nakala ya Mtando (Online Document)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, mnaweza vilevile mkawa na Kanuni nzuri sana, lakini kama watu wenyewe ambao tunahusika na zoezi dhamira zetu nazo si nzuri, bado hiyo haiwezi kuwa ni tiba. (Makofii)

Kwa hiyo, nadhani rai ya msingi hapa ni kwamba, sisi wote ambao ni washirika wakubwa katika zoezi hili pande zote mbili; upande wa Chama cha Mapinduzi, upande wa vyama vya Upinzani tufike mahali tuone kwamba, jambo hili ni letu wote na pale ambapo hapastahili kuwa na vurugu hakuna sababu ya kuwa na vurugu, vinginevvo nadhani rai yako kwangu haina tatizo hata kidogo.

Tutajitahidi kuona wakati mwafaka, na hata ikibidi pengine kuanza na mawasiliano formal hivi, brain storming ya Kanuni zenyewe kwa ujumla wake halafu baadaye twende katika hatua sasa ya kuona ni maeneo gani ambayo tunafikiri tunaweza tukayafanya.

Tutajitahidi kupitia TAMISEMI tuone wakati ambao tungeweza tukafanya hilo zoezi. (Makofii)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kumjibu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Ninatamani wote walioamka asubuhi wamalizike na inawezekana tu kama maswali yetu yatakuwa mafupi na hoja zetu fupi na zingine siyo lazima ku-repeat. Kwa hiyo, ninaanza na Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwaka 1997 Serikali ilichukua uamuzi wa kuvunja Jiji la Dar es Salaam na liliendeshwa na Tume baadaye yakaja mapendekezo ya uanzishwaji wa Manispaa za Kinondoni, Ilala na Temeke. Hivi sasa kuna mkanganyiko mkubwa sana kwenye utekelezaji wa maamuzi kati ya Halmashauri hizo na Jiji.

Je, ni lini Serikali itachukua uamuzi wa kuondoa mkanganyiko huu na kuweka mfumo ambao utasaidia kutekeleza majukumu ya Manispaa hizi kama inavyotakiwa? (Makofii)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ni kweli suala la mfumo au muundo wa Jiji na uhusiano wake na manispaa zile tatu kwa muda mrefu limekuwa ni tatizo

Nakala ya Mtando (Online Document)

ambalo linajitokeza mara kwa mara na ndiyo maana Serikali kwa nyakati imajaribu kuona ni muundo gani pengine ungeweza ukafaa.

Mtakumbuka mara ya mwisho tulijaribu lakini yale mapendekezo bado hayakuweza kutatua lile tatizo na tukalazimika kurejea tena kwenye utaratibu huu wa sasa.

Mheshimiwa Spika, sasa nafikiri ushauri wangu ingekuwa, tuombe Manispaa zile tatu ambazo ndiyo wadau wakubwa, pamoja na Jiji lenyewe pengine mngekuwa ndiyo chanzo cha kuibua fikra ambazo mnadhani zinaweza zikafaa kwa ajili ya muundo wa Jiji la Dar es Salaam.

Mnaweza mkafanya hivyo, kwa kujaribu kutengeneza timu kwanza ya Wataalam, baadaye mkajaribu kutengeneza timu ya Madiwani lakini wa maeneo yote, lakini mtumie na uzoefu pengine wa maeneo mengine duniani kuona mifumo ya miji au majiji yalivyo na kuweza kuona ni namna gani nzuri tunaweza tukajaribu kuitumia hapa Dar es Salaam.

Nadhani tukifanya hilo pengine litakuwa mwanzo mzuri kwa sababu ninyi ndiyo wadau wakubwa, badala ya kuanzia juu na kushuka chini. Tuanzie chini ili tuyalete juu tuone baadaye kama litakubalika. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Mangungu swali la pili, fupi kabisa.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru sana kwa majibu mazuri yenye matumaini. Ningependa tu kujua kwamba, uko tayari kusimamia mwongozo na usimamizi wa jambo hili kwa maana hizo zitakuwa ni mamlaka ambazo mpaka sasa zinasuguana kama tunavyoona Jiji la Dar es Salaam linazidi kuwa chafu, mifereji ya maji machafu imefurika, kila mamlaka inasema hili ni jukumu la mwингine.

Sasa kwa kipindi hiki cha mpito. Je, unatoa agizo gani na utayari wako wa kiasi gani kuweze kuzikutanisha mamlaka hizi na kulismamia hili jambo chini ya ofisi yako?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ofisi yangu ndiyo kiongozi wa shughuli zote za Serikali za Mitaa, ndiyo maana ninalisema hili kwa sababu Manispaa hizi ziko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Jiji lenyewe liko chini ya Ofisi Waziri Mkuu.

Rai yangu ya msingi ni hiyo tu kwamba, tulianzishe kule chini ili muweze kubainisha maeneo ambayo mnayatazama kwamba, kwanza ni tatizo katika

Nakala ya Mtando (Online Document)

utekelezaji, tatizo kimfumo na kumuundo, yapande juu baada ya mjadala mpana kwene mabaraza yote pamoja na Jiji lenyewe kama tunavyofanya tunapoanzisha maeneo mapya popote pale.

Mheshimiwa Spika, mimi natamani hili lifanyike zaidi na pengine hata wadau nje kabisa ya mabaraza haya ili kuweze kuwa na ushiriki mpana zaidi tuweze kuona namna gani tutaweza kulifanya hili jambo.

Sisi ofisi yetu na TAMISEMI kwa ujumla bado tutakuwa ndiyo wasimamizi pale mtakapokuwa mmeonesha nia hiyo na namna ambavyo mngependa zoezi hili liendelee.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye sijamwuliza swali muda mrefu sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunaelewa kwamba, nchi nyingi duniani zinakopa na sisi Tanzania hatuna budi kukopa kwa Maendeleo yetu. Hata hivyo, kumekuwepo na trend katika kipindi kirefu sasa kukopa na inaonekana miradi yote mikubwa tunakopa kutoka *Exim Bank* ya China. Sababu hizo zinajulikana kwa sababu ya unaifuu wa riba, masharti na urafiki tulionao na China.

Nini hatima ya nchi yetu ukizingatia kwamba, huko nyuma kuna mikopo mingi tumeshindwa kulipa ikabidi tusamehewe na ukitazama pia na siasa au msimamo wetu wa kutofungana na upande wowote?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Ndugu yangu Mheshimiwa Mnyaa, ingawa swali lake kidogo nadhani hakulitafiti tafiti sana. Ungelifanya utafiti ungembana Waziri Mkuu vizuri sana.

Iko sheria ambayo inasimamia suala zima la ukopaji pamoja na madeni. Sheria ile ndiyo inaisaidia Serikali muda wote kuzingatia yale ambayo yanastahili.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Ni kweli nyuma tulikopa, pia ni kweli kwamba mikopo ile ni mikubwa lakini zoezi lile lililoendeshwa na vyombo vyta Kimataifa lilikuwa ni zoezi la jumla katika kujaribu kusaidia hizi nchi maskini kuziondolea mzigo wa kuja kulipa madeni hayo baadaye ali mradi ukidhi vigezo fulani. Tanzania tulikidhi na ndiyo maana tukapata ule msamaha, ulikuwa ni wa jumla na siyo sisi tu, nchi nyingi zilipata hiyo nafuu.

Kwa hiyo, basi nataka nikuhakikishie tu kwamba, mimi kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali, faraja niliyo nayo ni moja tu kwamba, kwa vigezo vyote sisi kama nchi bado tuna sifa nzuri sana ya kuendelea kukopa kwa sababu uwezo huo wa kuweza kulipa haujakiuka yale masharti ya msingi kwa mujibu wa sheria hiyo.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa jibu hilo zuri la Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Nitakuwa na swali moja tu dogo kwamba, uzoefu tulionao Tanzania katika miradi ambayo imetekelawa kwa msaada wa Ndugu zetu wa China huko nyuma, iwe ya viwanda, hospitali na miradi mingine ya kijamii. Mifano iko ya TAZARA, URAFIKI, hospitali kule Zanzibar, Kiwanda cha Sukari Zanzibar na kadhalika.

Baada ya muda kumalizika na wao kuondoka, miradi hii tukaachiwa wenyewe utakuta miradi hii mingi imetupatia na kuleta taabu, na mingine imetushinda. Pamoja na sababu zetu za kiutawala katika kuendesha hiyo miradi lakini kuna sababu za standardization ya zile mashine au materials, iwe umeme au mashine nyingine.

Tumejiandaa vipi sasa na hii miradi yote ambayo tunakopeshwa na inajengwa kwa msaada wa China (fedha au materials zinazotoka China) ili ziwe sustainable baadaye baada ya kutuachia wenyewe? Tanzania tunajiandaa vipi?

SPIKA: Bahati yako, karibu niseme ni swali jipya. Mheshimiwa Waziri Mkuu! (Makofi/Kicheko)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ni dhahiri swali ni pana sana, lakini labda tutumie mifano michache tu, maana hapa nadhani anazungumza mikopo ya China.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Nichukue kwa mfano ujenzi wa bomba la Gesi kutoka Mtwara kwa sababu ule mkopo ni mkubwa. Tulicho fanya katika zoezi hili wakati huu tunaendelea kujenga hilo bomba, of course tutakuwa na vijana ambao tumewajiri mle. Watabakia na sehemu ya uwezo wa kuweza kusaidia kuelewa mambo yale madogo madogo ambayo yanaweza kujitokeza katika usimamizi wa bomba hilo.

Lakini kupitia Nishati na Madini, tumeagiza vilevile kwamba mradi huu ni mkubwa sana na bomba hili litahitaji kusimamiwa vizuri. Ni vizuri katika wale vijana ambao tumpata fursa ya kuwapeleka nje kwenda kujifunza mambo mbalimbali kuhusu gesi moja ya eneo ambalo tulipe umuhimu mkubwa ni namna tunavyoweza kusimamia suala zima la mkopo huu unaotuwezesha kuwa na gesi kutumia bomba la Mtwara.

Hivyo itatusaidia vile vile kwenye mabomba mengine ambayo yatajitekeza kwa sababu bomba hili halishii Dar es Salaam tuna ndoto za kwenda Kaskazini, kwenda hata mpaka Kanda ya Ziwa. Kwa hiyo ni lazima tuwe na wataalamu watakaotuwezesha kusimamia jambo hili vizuri. Hili tunalo na tume shaliingiza katika utaratibu wa kuanza kutoa mafunzo kwa vijana. (Makofij)

SPIKA: Naomba tuendelee na Mheshimiwa Assumpter Mshama.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali moja.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumekuweko mgogoro mkubwa sana katika maeneo ya ardhi hasa maeneo ambayo yamegawiwa kwa wawekezaji. Katika Tanzania nzima ikiwemo na Misenyi wananchi walikuwa wanamiliki maeneo yao lakini NARCO ikaamua kuuza hayo maeneo kwa wawekezaji.

Lakini wawekezaji wengine wamechukua maeneo makubwa kuliko mahitaji yao na matokeo yake wameacha Watanzania wengi wakihangaika hawana mahali pa kulishia wanyama wao na ardhi yao imechukuliwa bila utaratibu wowote na wakauziana watu ndani ya vitalu vile.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa wewe ndio msimamizi wa mambo yote ya Serikali hili suala kwa Wizara ya Ardhi limeshindikana unaonaje ukiingilia kati zikafutwa zile hati wananchi wakarudishiwa maeneo yao na matokeo yake tukapata amani katika Taifa letu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba maelezo yako.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ni kweli analolisema Mheshimiwa Assumpter Mshama kwamba pale Kagera tunayo maeneo ambayo ni mashamba ambayo zamani yalikuwa yanamilikiwa na NARCO na baadaye tukayatengenezea utaratibu ambao tulifikiri ungejibu haja ya Serikali ya kuendeleza ufugaji wa kisasa katika maeneo hayo na kwa njia hiyo tuweze kuboresha mifugo yetu.

Lakini ni kweli vilevile kwamba uamuzi ule na utekelezaji wake havikuenda kama tulivyokuwa tumetarajia. Kwa hiyo tulichofanya Serikalini nimeagiza Wizara kadhaa ambazo sekta hizo zinahusiana kwa karibu sana.

Tupitie kwenye maeneo yote ya mashamba ya NARCO kuweza kubaini matatizo kwa kila shamba na tuone ni maeneo yapi kwa kweli yanaweza yakaondolewa katika utaratibu ule. Pengine tukawapa wakulima au wafugaji kama watakuwepo wafugaji wadogo maana lengo ilikuwa ni kuyatumia kwa ajili ya kuboresha mifugo.

Sasa ndani yake ofcourse ipo Wizara ya Kilimo, Ardhi, watu wetu wa TAMISEMI, tumeweka Maliasili na Utalii vilevile kwa sababu hawa wanahusiana kuna maeneo mengine ambapo tutahitaji utaalamu wao kidogo.

Kwa hiyo, hiyo timu tunafikiri itakapomaliza hilo zoezi nadhani inaweza ikanisaidia kuweza kushauri au kumshauri Mheshimiwa Rais vizuri zaidi juu ya jambo hili.

SPIKA: Mheshimiwa Mshama kwa kifupi sana.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Inawezekana labda Mheshimiwa Waziri Mkuu hawakuambii ukweli, kwa sababu mpaka sasa hivi kwetu zimekuwepo Kamati zaidi ya saba na moja nilikuwemo mle na uamuzi Waziri wa Mifugo mwaka jana alituambia kwamba wameamua sasa kurudisha vitalu.

Je, lini utawaambia wananchi hasa wa Misenyi kwamba sasa ni mwisho na sasa tunakwenda kwenye utaratibu huu?

WAZIRI MKUU: Ziko efforts za Wizara inayohusika. Mimi ninachokisema hapa nimepanua tu hili wazo, sababu tatizo hili si Kagera tu, mashamba ya NAFCO yako sehemu mbali mbali, ndiyo maana tukasema tusiachie Wizara hii peke yake tuhusishe na Wizara nyingine ili baadaye tuweze kuwa na kauli pamoja kwa sababu TAMISEMI wanahusika sana.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Kama hawatakuwa sehemu ya uamuzi kesho na kesho kutwa TAMISEMI wanaweza wakajikuta tena kupitia Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya hawaelewi kinachoendelea ni nini.

Kwa hiyo, nataka nikuhakikishie tu kwamba zile jitihada za Wizara kwenye maeneo ambayo tayari walikuwa wameanza hatukuziingilia sisi lakini tumetaka tupanue zoezi sasa tuweze kuchukua maeneo yote ya NARCO kwa upana wake na tuone namna tunavyoweza kuwasaidia. (Makof)

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, suala langu haliko mbali sana na suala ambalo ameliuliza Mheshimiwa Assumpter Mshama, ila mimi nitazungumzia zaidi katika madhaifu katika usimamizi wa rasilimali za Taifa hasa nikizingatia uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Waziri Mkuu Tanzania ina eneo la misitu ambalo halipungui ekari milioni 33 na wastani wa ukataji miti ndani ya nchi yetu kwa mwaka haupungui ekari 403,000.

Mheshimiwa Waziti Mkuu, na ukataji huu wa miti ndio ambao unasababisha uchafuzi mkubwa wa mazingira. Wakataji hawa mara nyingi wanakuwa ni wakataji haramu au huwa hawafanyi kutokana na mipango ambayo imewekwa na Serikali. Naomba tu kutoka kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu, kauli ya Serikali juu ya ukataji huu mkubwa wa miti nchini.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ukataji wa miti au misitu hapa nchini ni kweli ni tatizo na lipo. Lakini lazima vilevile tukubali kwamba hiyo ni changamoto ambayo lazima tuijibu kwa kutumia mbinu mbalimbali.

Nitoe mfano tu wananchi wetu wengi vijijini wengi wanatumia nishati ya kuni na baadhi ya makabila wanapenda kukata miti hii kabla hata haijakauka anaikausha baada ya kukata ili aweze kujianaa vizuri. Ni ukataji haramu kama unavyosema, lakini ni ukataji ambao haukwepeki katika mazingira ya sasa kwa sababu nishati ile kwa mwananchi yule ni ya lazima.

Lakini uko ukataji miti ambao unatokana na matumizi ya mbao na hapo unaweza ukachukua mifano ya shule zote ulizojenga, zahanati zote ulizojenga, nyumba zote tunazojenga zote tunatumia miti. Ni ukataji ambao kwa upande mwingine haukwepeki.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Madawati yote wanayokalia watoto wetu yote ni mbao ambazo zimetokana na miti. Unaweza ukauita ukataja haramu lakini bado changamoto yake ni lazima itafutiwe njia mbadala ya namna ya kushughulika na jambo hili.

Kwa hiyo kwa ufupi nataka kusema nini, nakubali kwamba changamoto ipo lakini nadhani kama Serikali na sisi wote kama wadau wakubwa wa tatizo hili ni lazima tuweke vichwa pamoja tuone namna gani tutashughulikia jambo hili.

Moja tamaa niliyonayo ni kwamba pengine gesi hii ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia tuone namna tutakavyoitumia kikamilifu ili sisi wote wakazi wa mijini kwanza maana ndio watumiaji wakubwa sana wa mkaa tuondokane na matumizi ya mkaa tuingie katika matumizi ya gesi tutakuwa tumepunguza sana ile sulubu ya sasa ya mkaa kuja mijini.

Lakini ukifanya hivyo peke yake bado haisaidii ndiyo juhudzi za Serikali ni kujaribu kutumia kila aina ya mbinu. Kuna matumizi ya majiko banifu katika jitihada za kujaribu kupunguza matumizi ya ukataji wa miti vijijini.

Lakini nadhani tunakokwenda kama nchi zingine zilivyofanya nyingi ni lazima vilevile gesi hii tuitafutie utaratibu wa kuweza kuifikisha mpaka kwenye maeneo yale ambayo sasa yanakuwa kimiji ili na yenyewe kutusaidia kuzidi kupunguza jambo hili.

Lakini mwisho kwa ujumla ni elimu, tunahitaji elimu kubwa kwa Watanzania kwa sababu wengine wanakata wakati mwingine hana sababu anaona tu limti linamkera tu. Wakati mwingine watu wanakata kwa sababu wanataka mifugo ipite sehemu ambako akiona anaona ng'ombe badala ya kuona miti anachohitaji huyu mtu ni elimu tu.

Kwa hiyo kwa ujumla nadhani tutahitaji interventions au njia mbalimbali kuweza kujaribu kutatua hili tatizo ambalo kimsingi ni kubwa sana.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu amenipa ambayo kwa kweli ni mazuri.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hata hivyo ni asilimia nne (4) tu ya ekta hizo ambazo nimezitaja ndani ya nchi yetu ambazo zimewekewa mipango mizuri ya matumizi. Asilimia 96 bado Serikali haijaweka msimamo mzuri wa matumizi ya eneo hili na hii ndiyo inayosababisha hata hivi vita ambavyo sasa hivi tunaviona vya wafugaji kuingia katika maeneo ambayo yametengwa na mambo mengine.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini kwa upande wa Wizara ya Maliasili wanasema kwamba asilimia 57 ya mapato ambayo yanatokana na mazao ya misitu hayakusanywi. Sasa kweli wananchi wana shida wana matatizo yao mambo ya kuni, madawati lakini je katika eneo hili ambalo la usimamizi wa upatikanaji wa fedha na matumizi mazuri haya maeneo Serikali inasemaje?

SPIKA: Haya sekta hii halafu unaingia kwenye particular haya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Rajab fundi sana wa kuunganisha mambo.

Mheshimiwa Spika, analosema Mheshimiwa Rajab ni kweli bado kuna udhaifu katika eneo hili na utaona hata katika Bajeti yetu moja ya eneo ambalo hatukufanya vizuri sana ni hilo la maduhuli na Wizara ya Maliasili na Utalii wana eneo kubwa ambalo tunadhani lingeweza kuwa la msaada sana katika kuongeza Bajeti yetu.

Serikalini tulikaa kujaribu kuona tunafanya nini na hili tatizo la maduhuli kutokukusanywa kwa mujibu wa Bajeti iliyowekwa. Imefika mahali watu wanafikiria kwamba pengine tungakuwa na chombo maalum au timu maalum ambayo kazi yake iwe ni kufuatilia tu maduhuli kwa kila Wizara na kwa kila taasisi ambayo imepewa jukumu la kukusanya hizo fedha. Kwa hiyo katika

Bajeti ya mwaka huu tutajaribu sana kuona namna ya kuja na utaratibu wa jambo hili kusimamiwa hatutakuwa ni chombo kwa maana ni chombo cha kisheria kama TRA ilivyo.

Lakini tumedhani kwamba ndani ya Wizara hizi sisi wenyewe tutatafuta timu ambayo tutataka tuipe jukumu la ufuatiliaji wa makusanyo wa maduhuli na hili unalolisema linaweza kuwa ni namna moja pengine ya kuweza kupata kile ambacho kwa sasa hivi tunakikosa.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa nimwulize swali moja dogo la nyongeza.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Waziri Mkuu hivi karibuni kumelipuka ugonjwa wa homa

SPIKA: Hebu vipi la nyongeza kwa nani?

MHE. MOSES J. MACHALI: Hapana swali moja.

SPIKA: Aaa!!! Okay okay.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni kumejitokeza ugonjwa ambao unaonekana kutishia watu wengi hapa nchini ugonjwa wa homa ya dengue.

Taarifa ambazo zinatajwa na watu ambazo nimezisikia ni kwamba kulikuwa kuna utafiti ambao unafanywa hapa nchini na wataalamu wetu wa Wizara ya Afya wakitafuta mbu ambao watakuja kuangamiza mbu wa Malaria. Sasa katika majaribio hayo, wale mbu ndio wamepelekwa matokeo yake yanaleta janga hili.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilikuwa naomba kauli ya Serikali kuhusiana na taarifa hizi ni sahihi kiasi gani ili kuweza kuondoa hofu iliyoko mionganoni mwa Watanzania?

SPIKA: Au umesikia yule Mchungaji. (Makofi/Kicheko)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Machali hakunitendea haki. Swali angemwuliza Waziri wa Afya angefanya vizuri zaidi kuliko mimi. Lakini ni kweli sasa hivi tuna tatizo la homa ya dengue.

Lakini wakati huo huo ugonjwa wa malaria nao upo. Sasa kama gonjwa hili limetokana na hizo tafiti au hapana siwezi kulisema kwa sasa maana sjui. Lakini ninachojua ni kwamba homa hiyo inasababishwa na mbu aina ya aedes maana tuna aina tatu za mbu. Chanzo chake ni mbu anaitwa aedes.

Sasa huyu mbu yupo muda wote wala sio kwamba ameibuka leo, hapana. Ni kwamba tu hapa katikati pengine jitihada zilikuwa nzuri tukaweza kudhibiti akakosa kupanua uwezo wake wa kueneza ugonjwa na utaona imejitokeza sambamba na mafuriko makubwa yaliyojitokeza.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Kwa hiyo inawezekana pengine katika kuzaliana walikuja wakapata upenyo hivi na ndiyo maana tatizo hili likajitokeza. Lakini labda niseme tu kwamba pengine nitakuwa sikukutendea haki mimi nadhani labda nitamwomba Waziri wa Afya kwa sababu ni jambo kubwa pengine angekuja na kauli ya Serikali ili aweze kulieleza vizuri zaidi kwa manufaa ya Watanzania wote.

SPIKA: Ahsante sana kwa kuokoa muda, sasa nimwite Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Tulikuwa na muda wa kuwasilisha.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nikuulize swali moja.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi sana za walipa kodi kwa ajili ya kutengeneza miundombinu ya barabara hapa nchini.

Hata hivyo Mheshimiwa Waziri Mkuu barabara hizi kwa sehemu kubwa, kiasi kikubwa zilikuwa zinaharibiwa pamoja na kuwepo na sheria lakini wanyabiashara wasiokuwa na uzalendo wamekuwa wakizidisha mizigo kwenye magari yao na hivyo kuonekana barabara zote zimeharibika na tumeshuhudia migomo mikubwa kwenye barabara zote.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, wafanyabiashara wengi wamefanikiwa hata kuishinikiza Serikali pale sheria inaposimamiwa wamegoma na hivyo Serikali kuruhusu uharibifu wa barabara kuendelea. Naomba kauli ya Serikali, nini kauli ya Serikali kuhusiana na barabara kuharibiwa na huku wanaona na huku Watanzania wanaendelea kuteseka? Ahsante sana. (Makofii)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu sjui kama umelielewa hili swali?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, zaidi ya asilimia 80 ya usafirishaji wa mizigo na abiria hapa unategemea barabara. Kwa hiyo, ndio uhalisia wake kwa sasa. Ni hali ambayo inaikumba nchi yetu kwa sababu bado reli haijaweza kutoa jibu kwa tatizo hili, tutakapokuwa tumeimarisha reli chini ya Dkt. Harrison Mwakyembe inawezekana kabisa tatizo hili tukaanza kulipunguza.

Lakini pili, barabara zetu hizi za lami zinatengenezwa kwa mfumo wa kitu kinaitwa surface dressing. Life span yake uwezo wake wa kuishi ni kati ya miaka 10 mpaka 15. Hatutumii concrete asphalt hapana, tumejaribu kwenye barabara tu ya TANZAM ndio tuliweza kutumia kigezo hicho kwa historia yake.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Kwa hiyo barabara zote hizi ni za aina hiyo. Sasa unapokuwa na barabara hizi kwa mfumo huo ambao una mizigo mikubwa hiyo ni tosha kabisa kuwezesha barabara hizi kutohimili kwa muda mrefu.

Tatu, magari yetu hapa nchini uzito tulioruhusu ni tani 56, nchi nyingi hawakufika huko ni tani thelathini na thelathini na kitu hivi. Kwa uhalisia wa kutokuwa na miundombinu ya reli, miundombinu ambayo ingeweza ikasaidia kupunguza huu mizigo Serikali ilijikuta ikaweka utaratibu huo kwa maana ya kusaidia tu kuweza kubeba mizigo hiyo kwa urahisi na kwa kutumia magari haya ambayo tungefikiri yangekuwa ni machache badala ya kuwa na magari mengi na hivyo kuzidi kuongeza tatizo la msongamano. Lakini kwa kufanya hivyo bado hatujasaidia sana.

Lakini, nne niseme hili unalolisema kwa bahati mbaya sana jambo hili halikueleweka vizuri, tatizo hakuna anayesema mtu azidishe mizigo zaidi ya tani 56, hakuna. Si mimi, si Waziri Magufuli si mtu mwengine yoyote na wenyewe malori na mabasi wanajua hilo tatizo hapa lipo wapi? Ni kwamba katika kupima uzito wa magari tunatumia axleload weight ya gari.

Gari inaweza kuwa na excel hizi mbili, tatu, nne, kinachotokea gari hili katika kubeba huo mizigo unashuka milima unapanda kuna sehemu nyingine kuna matuta unaruka unashuka.

Kwa hiyo, inawezekana kabisa mizigo ambao umeupima una tani 56 ukasogea kwenye excel ya mbele na kugandamiza ile excel ya mbele. Au wakati unapanda mlima mizigo uka-slide back, nyuma na kugandamiza ile excel ya nyuma unapokwenda kupima wanapima hiyo excel weight kinachotokea inawezekana katika kutereza kwa ule mizigo ukajikuta ule uzito umeongezeka kwenye excel hiyo kwa kiwango kile ambacho wanasema hakizidi asilimia 5 au nyuma kwa kiwango hicho.

Sasa sheria nyingi duniani unapokuwa na hiyo allowance wanairuhusu kwa nini, kwa sababu hujazidisha tani 56 inaruhusiwa na unachofanya pale unapopima wakakuta kuna hilo tatizo nchi nyingi wanakuambia hebu park gari jaribu kuona kama unaweza ukapanga hii mizigo tena vizuri halafu uendelee.

Lakini magari mengine ni mizigo ambao ni transit good huwezi ukafungua. Ndio maana wanakwambia inapotokea situation hiyo park gari lakini ukubali kulipa faini kidogo kwa sababu itakubidi tukuruhusu uendelee ingawa excel ya mbele ina uzito zaidi kuliko inavyotakiwa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, sasa ubishi ulikuwa katika hiyo allowed percentage ndiyo ililetu ule ubishi ndiyo maana mimi nikaingilia kati nikasema jambo hili linachohitaji ni ueleweshwaji na Kanuni hii kuiweka vizuri ili iweze kueleweka kwa sababu ilionekana kutokueleweka vizuri, tukaomba ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, akasema ni kweli Kanuni hiyo inahitaji kuandikwa vizuri.

Vinginevyo mizigo hii isinge kuwa inasafiri inaingia Zambia, mizigo hii ikasafiri ikaingia Burundi kama utakuwa umeweka uzito zaidi ya kiwango kinachotakiwa. Ndiyo maana nikaingilia kati kwasababu niliona ugomvi ule haukuwa na tija sana kwa sababu malori yale ndiyo jukumu la kusafirisha mizigo na hali ilishakuwa mbaya.

Kwa hiyo, hatukupishana na magufuli ingawa watu wanaweza kusema angalia Waziri Mkuu ameruhusu mizigo ibebe zaidi ya tani 56 hapana tulikuwa tunazungumza allowable percentage wheather mtu ashushe afanye nini au vinginevyo ni hilo tu ambalo nimeona nimalizie katika ku-clarify. (Makofii)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Kanuni hazinilamishi kumwambia mtu aulize swalii la nyongeza. Kwa hiyo, tunakushukuru kwa majibu mengine yalikuwa ni ya kitaalam hasa hili la mwisho na ninawashukuru. Kanuni hazinilazimishi, muda umepita. Kwa hiyo, tunaendelea Katibu!

MASWALI NA MAJIBU

Na.148

Mkakati wa Kupunguza Maambukizo ya Ukimwi

MHE. MBAROUK SALIM ALI aliuliza:-

Ukimwi bado ni tishio na taarifa zinaonyesha kuwa maambukizi bado ni makubwa hasa kwa baadhi ya maeneo hapa nchini.

Je, Serikali ina mkakati gani mahsusii wa kupunguza maambukizi katika maeneo yaliyoathirika zaidi?

Nakala ya Mtando (Online Document)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba kujibu swali la Mhe. Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Wete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Ukimwi bado ni tishio hasa Katika makundi maalumu kama vile wanaofanya biashara ya ngono, wanaojidunga sindano wanafanya ngono nzembe na wanaofanya ngono kinyume cha maumbile.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mikakati kadhaa mahususi ya kupunguza maambukizi hasa katika maeneo yaliyoathirika zaidi. Baadhi ya mikakati hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kupitia mkakati wa kudhibiti Ukimwi kwa kipindi cha mwaka 2008-2012 na kuandika mkakati mpya kwa kipindi cha mwaka 2013-2018.

(ii) Kupitia Sera ya Taifa ya Ukimwi ya mwaka 2001 na kuboresha ili kutoa miongozo bora zaidi ya kupunguza maambukizi.

(iii) Serikali imeandaa mwongozo wa kuelekeza Mikoa namna ya kuandaa mpango kazi wa Mkoa na kipaumbele ni kuzuia maambukizi kwa kubainisha viashiria au vichocheo kwa kila Mkoa, Wilaya, Kata, Kijiji na mtu mmoja mmoja.

(iv) Serikali ina andaa mpango wa kuwa mwitikio wa Ukimwi kwa mfumo wa Kikanda ambapo Wakuu wa Mikoa wa Kanda watacaa pamoja na kuwa na mikakati ya pamoja.

(v) Kuimarisha huduma za kinga katika Mikoa yenyе maambukizi makubwa.

(vi) Kupitia mkakati wa kinga 2009-2012 ili kuhakikisha mkakati wa Taifa kuhusu Kinga inawekwa kwenye mkakati huu na baadae kutumika katika maeneo yote hususan maeneo yenyе maambukizi makubwa.

(vii) Kuendelea kutoa elimu ya Ukimwi na kubadili tabia kupitia kwa wadau mbalimbali na vyombo vya habari hususan radio.

(viii) Mifumo ya uratibu usimamizi wa huduma za ukimwi imeimarishwa katika ngazi za Halmashauri.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuipongeza Pemba kwa kuzingatia mikakati ya kupunguza maambukizi ambapo viwango vya maambukizi kwa Pemba ni vya chini Kitaifa ni kati ya 0.1% hadi 0.4%.

MHE. MBAROUK SALIM ALI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru na pia nimshukuru Waziri kwa majibu yake ingawa amaenda zaidi ki mikakati ya Kisera kuliko ile mikakati mahususi ambayo nilitegemea niipate lakini pamoja na hayo ninapenda kumuuliza mawili madogo.

Kwa sasa Serikali imejikita zaidi kupunguza maambukizi ya Mama kwa Mtoto na pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri ametaja makundi mengi hapa ambayo ni tishio kwa magonjwa haya sasa nimuulize. Mheshimiwa Waziri kwamba ana kauli gani. Serikali inasemaje kuhusiana na mkakati wa sifuri tatu ifikapo 2015 ambapo bado kama miezi sita. malengo hayo yatafikiwaje ikiwa bado Serikali imejikita zaidi katika kipengele cha kuzuia maambukizi ya Mama na Mtoto.

Lakini lingine nimwulize Mheshimiwa Waziri kwamba inaonyesha kwamba katika baadhi ya maeneo kuna baadhi ya makabila hasa katika maeneo ambayo yana maambukizi makubwa, kuna tatizo sugu la tohara kwa wanaume, kwamba hawataki kufanyiwa tohara na watu wengi hawajafanyiwa tohara.

Hili ni tatizo kubwa lakini pia kuna sumu kali inayoenewa na makabila hayo hayo kuwa iwapo watu watakubali kufanyiwa tohara ni kuingizwa katika Uislamu.

Je, Waziri ana kauli gani kuhusiana na suala hilo? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kupata nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ningepeda kuongezea jibu la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kuhusu suala la sifuri tatu, kwa maana ya kwamba kuna suala zima la unyanyapaa, kuna suala zima la maambukizi mapya na suala zima la vifo kutokana na ukimwi. Mkakati uliopo kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Afya imeandaa maelezo maalumu ambayo tumeshasambaza nchi nzima kuitia vituo vyote ambavyo tunatoa huduma ya Afya.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Nitumie fursa hii kuwaeleza Watanzania kazi kubwa ambayo imefanyika kutokana na tafiti za viashiria katika ngazi ya jamii yaani indicator survey 2008 hali ya ukimwi nchini ilikuwa ni 5.7% lakini katika matokeo ya 2012 ambayo Mheshimiwa Rais alizindua tarehe 27 Machi, 2013 tafiti hizi zimeonyesha hali ya ukimwi kushuka na kufikia 5.1% katika nchi.

Kwa hiyo, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge nyaraka hizi na miongozo na mafundisho ambayo tumetoa nchi nzima kupitia vikao vya maamuzi vya Mikoa ikiwamo Kamati ya Sheria yaani RCC na ngazi ya Hamashauri katika Baraza yaani Full Council tufuatilie kuhusu utekelezaji unakwendaje ili tuweze kuangalia hali ya jamii itakuwaje mwaka 2015/2016.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa nchi swalii la pili.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Ni kweli lile alilolisema Mheshimiwa Mbarouk kwamba utafiti umeonyesha hata kwa Tanzania kwamba wale ambao hawajapata tohara na wale waliopata tohara wanaoweza kupata maambukizi kwa haraka ni wale ambao hawajapata tohara.

Utafiti umeonyesha, ndiyo maana hivi sasa kuna jitihada maalum za Serikali na kampeni hii imeanza kufanikiwa vizuri sana katika Mikoa ambayo imeoekana ina maambukizi makubwa sana ya Ukimwi.

Labda niseme tu kwamba Mikoa ambayo inaongoza sasa hivi kwa kiwango cha juu ni Njombe ambayo ni 14.8%, Iringa 9.1%, Mbeya 9%, Shinyanga 7.4%, Ruvuma 7%, Dar es salaam 6.9% Katavi 5.9% na Pwani ni 5.9% tumeanza kampeni ya makusudi ya kuhakikisha kwamba watu kwa hiari yao wanakwenda kufanya tohara bila ya gharama na zoezi hili limefanikiwa sana. (Makofij)

Kwa hiyo, ninataka kutoa wito tu kwa wananchi hasa wanaume wajitokeze kwa umri wowote ili kuweza kufanya jambo hili kwa sababu limeonekana kwamba ina faida na inaweza kuwasaidia katika kupunguza maambukizi.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuuliza swalii moja la nyongeza.

Kwa kuwa, sasa hivi takwimu zinaonyesha kwamba maambukizi ya Ukimwi yanaongezeka sana katika makundi maalumu ikiwamo watumiaji wa madawa ya kulevya.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Je, ni lini Seerikali italeta Muswada wa Sheria wa kudhibiri Madawa ya Kulevyo?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri ninaomba uende kwenye meza ndiyo utaratibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, swalii la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kweli Serikali pamoja na marekebisho makubwa ya Sera na Sheria hayo anayoyasema Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, Serikali tunafanya maandalizi pamoja na Sera ili kuhakikisha kwamba tuna dhibiti na kuimarisha mapambano dhidi ya madawa ya kulevyo.

SPIKA: Tunaendelea swalii mnalipenda hilo badilisheni tabia. Mheshimiwa Suleiman Nchambi.

Na. 149

Ujenzi wa Vituo Afya na Zahanati Kishapu

MHE. SULEIMAN N. SULEIMAN aliuliza:-

Vituo vingi vya Afya pamoja na Zahanati katika Jimbo la Kishapu vimefikia lenta katika Ujenzi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza vituo hivyo ili wananchi wapate huduma?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Suleiman Nchambi Suleiman, Mbunge wa Jimbo la Kishapu, kama ifuatavyo:-

Nakala ya Mtando (Online Document)

Miradi ya ujenzi wa zahanati na vituo vya Afya huibuliwa na wananchi wenyewe kupitia mpango wa Fursa na Vikwazo katika Maendeleo (O&OD) na unatekelezwa kwa ubia kati ya wananchi na Halmashauri. Halmashauri huchangia gharama ndogo za utekelezaji wa miradi hiyo kwa kuwezesha upatikanaji wa vifaa pamoja na usimamizi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu vipo vituo vya Afya 6 na Zahanati 26 ambazo ujenzi wake umeanza na haujakkalimika. Ujenzi wa vituo na zahanati ulianza mwaka 2012/2013 kwa gharama ya shilingi milioni 77.7 hadi sasa jumla ya Zahanati 6 zipo katika hatua ya lenta ambazo ni Mangu, Mwaweja, Mwamashimba, Isagala, Busongo na Msagala na kituo kimoja cha Afya cha Bubiki na vituo vya afya vya Dulisi na Ng'wanghalanga vimepanuliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Halmashauri iliidhinishiwa shilingi milioni 215.8 kutoka katika Mfuko wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) kati ya fedha hizo kiasi kilichopokelewa ni shilingi milioni 187.5 sawa na 87% ya Bajeti Halmashauri imetumia fedha hizi katika ujenzi wa majengo ya wagonjwa wa nje (OPD) katika vituo vya Afya vya Dulisi na Ng'wanghalanga.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2014/2015 Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ilitengewa milioni 149.8 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya MMAM. Kipaumbele cha Halmashauri katika matumizi ya Fedha ni katika kukamilisha ujenzi wa OPD na kujenga nyumba moja (*two in one*) katika kituo cha afya cha Dulisi.

Serikali itaendelea kutenga Bajeti kila mwaka ili kuhakikisha majengo hayo yanakamilishwa kwa kushirikisha nguvu za wananchi ili Sera ya afya ya kuwa na kituo cha afya kila Kata na Zahanati kila kijiji iweze kutekelezwa kikamilifu.

Aidha, ninachukua fursa hii kuzikumbusha Halmashauri zote kuhakikisha kuwa kipaumbele kinawekwa katika kumalizia miradi ya zamani kabla ya kuanza miradi mipyä. (*Makofî*)

MHE. SULEIMAN N. SULEIMAN: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwanza ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kupitia Wizara yake ya TAMISEMI kupitia Wizara yake kwa ushirikiano anaotupa wananchi wa Kishapu na Halmashauri yetu, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Kwa kufuata utaratibu wa Bajeti ya milioni mia mbili na mia moja na hamsini na kwa kuwa Halmashauri ya Kishapu inayo miradi takribani 26 ya Zahanati za 2013/2014 na Vituo vya Afya zaidi ya kumi kwa 2013/2014.

Sasa swalilangu ni hili. Kwa kuwa Vituo vya Afya vitakuwa na thamani ya zaidi ya shilingi bilioni tatu na Zahanati zitakuwa na thamani ya takribani bilioni tatu. Kama tutafuata utaratibu wa Bajeti ni wazi kuwa tutakamilisha baada ya miaka isiyopungua ishirini.

Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari kupokea maombi maalum kama ulivyo fanya katika Hospitali yetu ya Wilaya ukatusaidia?

Kwa kuwa Kishapu miradi ya Zahanati na Vituo vya Afya na hospitali ya Wilaya inakwenda kwa kasi kama nilivyoeleza kuwa watu wa Kishapu ni sharp Mbunge wao sharp, na wananchi wote ni sharp.

Je, Wizara iko tayari kutuandalia Wafanyakazi ili tunapokamilisha mara moja wafanyakazi wawepo ili wananchi wa Kishapu wanufaikie na Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi (CCM) makini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri ninaomba ujibu kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa pongezi zake ambazo amezitoa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Lakini la pili la ushuhuda huyu Kiongozi anayezungumza hapa amefanya mambo makubwa katika Wilaya yake amehakikisha wamepata Ambulance tano pale, amehakikisha kwamba amesaidia hospitali ya Wilaya ikafikia hatua hiyo anayozungumzia hapa.

Amehakikisha kwamba amechangia mifuko 4,000 katika hiyo Halmashauri yake kwa ajili ya kujenga hiyo Hospitali ya Wilaya. It is my judgment kama Member wa Parliament kusema kwamba huyu Mbunge ni Mbunge serious anajua anachofanya katika Halmashauri yake.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Sasa kuhusu hizi hela anazozzungumza hapa huyu Bwana anazungumza habari ya shilingi nbillioni sita ndizo zinazungumzwa hapa hela za mwaka huu tunaokwenda nao ni shilingi bilioni moja na themanini na saba ndizo walizotengewa kwa ajili ya Bajeti yote kwa mambo ya afya.

Mwaka huu tunaokwenda nao tumewatengea shilingi milioni mia tisa na hamsini na tatu *Development* ni shilingi milioni mia mbili na hamsini na *Development* kwa mwaka huu tunaokwenda nao ambayo imepitishwa hapa ni mia moja na arbabaini na saba.

Tutakachofanya hapa tutakwenda kuangalia hiyo *special request* anayozzungumza. *Special request* ikiombwa na ili watu wengine wajue, Halmshauri inaambiwa kuwa wewe *special request* yako uliyoomba umekubaliwa kiasi hiki. Tutakwenda kuangalia kwenye *special request* na kwa kipaumbele chao kwa maana ya (*O&OD*), tutapeleka huko kama anavyotaka kushauri Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

Na. 150

Ucheleweshaji wa Kupandishwa Daraja Wakufunzi wa Vyuo vya Elimu.

MHE. MARTHA M. MLATA (K.n.y. DIANA M. CHILOLO) aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko ya wakufunzi wa vyuo vya Ualimu nchini kuhusu kucheleweshwa kupandishwa madaraja.

- (a) Je, hadi sasa ni wakufunzi wangapi wa vyuo vya Ualimu nchini hawajapandishwa madaraja?
- (b) Je, Serikali gani ina mkakati gani wa kuhakikisha malalamiko hayo yanamalizwa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA
aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge, lenye sehemu(a) na (b), kama ifuatavyo:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(a) Mheshimiwa Spika, Watumishi hupandishwa vyeo kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa katika miundo ya maendeleo ya Utumishi, Ikama iliyodhihirishwa, Fedha za kulipa mishahara ya Vyeo vipyta na utendaji mzuri wa kazi hakuna sababu ya Watumishi kukaa kwenye Cheo Kimoja kwa muda mrefu endapo ametimiza vigezo hivi.

(b)

Katika mwaka wa fedha 2013/2014 Serikali ilipanga kuwapandisha vyeo wakufunzi 696 na hadi kufikia mwezi Machi, 2014 wakufunzi 282 walikuwa wamepandishwa vyeo wakufunzi 414 hawakupandishwa cheo na kati yao wakufunzi 247 hawakutimiza masharti ya muundo wao wa maendeleo ya Utumishi na wakufunzi 167 hawakuleta taarifa zao kiutendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, idara ya Utumishi wa walimu (*TSD*) imewahimiza waajiri wa wakufunzi hao kuwasilisha taarifa zao ili nao waweze kupandishwa vyeo.

(c) Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na malalamiko ya wakufunzi wa vyuo vya Elimu nchini Serikali imepanga mikakati ifuatayo:-

(i) Kusafisha taarifa za kiutumishi na mishahara ya wakufunzi wa vyuo vya elimu sambamba na Watumishi wengine wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı ili kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi analipwa mshahara sahihi kulingana na cheo chake cha sasa.

(ii) Kurekebisha mishahara ya wakufunzi hawa kwa wakati kuitia Mfumo wa Taarifa za kiutumishi na mishahara (*HCMIS*) pale wanapopandishwa cheo ili kuepuka madai ya malimbikizo ya mshahara.

(iii) Kuwataka Wakuu wa Vyuo kujaza mkikataba ya utendaji kazi (Performance Contract) kila mwanzo wa mwaka wa fedha (Mwezi Julai) kufanya tathimini ya nusu mwaka (Mid-year Performance Review) mwezi Desemba kwa kufanya tathimini ya ya mwisho wa mwaka (Annual Performance Review) mwezi Juni kwa wakati ili kuepuka uwezekano wa baadhi ya wakufunzi kukosa taarifa za utendaji kazi wakati wa zoezi la kuwapandisha vyeo.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwahimiza wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu kuhakikisha kuwa wanasoma na kuelewa sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa Muundo wao wa Utumishi.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, lakini naomba nimuulize tu maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, matatizo ya Walimu pamoja na Wakufunzi wote yanatokana na kutokuwa na chombo maalum cha kushughulikia matatizo yao na kwa sababu Mheshimiwa Waziri aliahidi kuitisha kikao maalum cha wadau

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwa ajili ya kushughulikia na kuhakikisha chombo hicho kinapatikana, naomba alieleze Bunge hili na Watanzania wote, je, hatua hiyo imefikia wapi?

Mshahara anaopata Mkuu wa Chuo yeyote anaoufahamu yeye Mheshimiwa Waziri pamoja na Wakuu wa Vyuo hao. Je, unastahili kulingana na wadhifa huo walionao?

Mheshimiwa Spika, ahsante. (Makofii)

SPIKA: Haya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, hicho chombo kina hoja inakuja.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:

Mheshimiwa Spika, ni kweli niliahidi hapa Bungeni kwamba tutawaita wadau kuhusu kuanzishwa kwa chombo maalum cha kushughulikia masuala ya Walimu, lakini nilikaa pamoja na Mwenyekiti wa Kamati yako ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Mama Sitta, tumekaa pamoja, tulishauriana, akaomba kwanza kabla ya kuwaita wadau, mimi na ofisi yangu twende kwanza tukajifunze kwa wenzetu Kenya kama walivyofanya wao na baada ya hapo ndio tuite kikao cha wadau. Kwa hiyo, tumeshaelewana kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, suala kuhusu mshahara wa Wakuu wa Vyuo hivi vya Wlimu. Mshahara wa Mkuu wa Chuo cha Walimu unaendana na muundo wa utumishi wa wakufunzi wa vyuo hivyo. Kwa hiyo, mshahara ule anastahili na ni kulingana na muundo wao wa utumishi na pia kuna nyongeza ambayo anapata kama Mwalimu au kama Mkuu wa Chuo cha Ualimu.

SPIKA: Ngoja tuendelee na swali lingine muda umekwenda. Tunakwenda Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Profesa Kahigi atauliza swali hilo.

Na. 151

Ukosefu wa Umeme Shule za Bukombe

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI aliuliza:-

Ukosefu wa umeme katika shule za Msingi na Sekondari katika Wilaya ya Bukombe ni kikwazo kikubwa katika ufundishaji na kujifunza mashulenii:-

Je, ni lini mradi wa Umeme Vijijini utapeleka umeme katika shule hizo ili kuboresha huduma ya utoaji na upokeaji elimu ikiwa ni pamoja na elimu ya TEHAMA?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI, (MHE. CHARLES M. KITWANGA)
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Bukombe (Ushirombo) pamoja na Vijiji/ maeneo ya jirani kupitia mradi wa Electricity "v", ambao ni miongoni mwa miradi iliyopata ufadhili wa Benki ya Manedeleo ya Afrika (AFDB), Mradi huo unahusu kupeleka umeme kwenye Vijiji/maeneo zaidi ya 25 Wilayani Bukombe.

Mheshimiwa Spika, umeme katika Mradi huu utaunganishwa kutokea kituo cha kupozea umeme katika Kijiji cha llogi kutoka kwenye kituo kikubwa cha kupozea umeme cha Bulyankulu. Kazi za Mradi zitahusisha; Ujenzi wa laini yenye urefu wa kilometra 190 yenye msongo wa kilovoti 33 kutoka Kijiji cha llogi hadi Ushirombo; ufungaji wa vipoza umeme 41; ujenzi wa laini za umeme wa msongo wa volti 400/230 zenye urefu wa kilometra 88; na kuunganisha wateja wa awali wapatao 5000.

Mradi huu utagharimu kiasi cha Dola za Marekani 10,328,228. Hatua iliyofikiwa kwa sasa ni pamoja na vifaa vya ujenzi wa mradi kufika Ushirombo na Mkandarasi (*Eltel Networks*) anaendelea na ujenzi wa laini ya msongo wa kilovoti 33. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2014.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia itatekeleza mradi wa umemenuru katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwemo Wilaya ya Bukombe kupitia Mradi wa SSMP II (*Sustainable Solar Market Programme II*) utakaoanza kutekelezwa mwezi Julai, 2014. Katika Wilaya ya Bukombe, Mradi utanufaisha wakazi wa vijiji 52, vituo vya afya viwili (2), dispensary kumi (10), shule 13 na vituo vya Polisi vitatu (3). Gharama ya utekelezaji wa Mradi kwa loti ya Bukombe ni jumla ya Dola za Marekani 1,277,023.68 na Mradi unategemewa kukamilika mwezi Juni, 2016.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Profesa Kahigi, swali la nyongeza.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu ambayo yanatia matumaini, lakini tatizo kubwa la miradi hii ya umeme ni kwamba, ama inachelewa kuanza au inachelewa kukamilika. Mradi huu alioutaja wa electricity five kwamba ulikuwa ukamlike Juni mwaka huu, lakini taarifa nilizonazo asubuhi hii ni kwamba, bado upo katika hatua za mwanzo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Swali langu la kwanza, Mradi huu utakamilika lini? Maana ultakiwa ukamilike Juni mwaka huu.

La pili, umesema kwamba umemenuru utapelekwa Bukombe kuanzia Julai mwaka huu, naomba tu majina ya Shule kumi na tatu ambazo umesema kwamba zitapelekewa umeme.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI(MHE. CHARLES M. KITWANGA):

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swalii la msingi kwamba mradi huu utakamilika Septemba mwaka huu na mkataba ndivyo ulivyo.

Swali lake la pili, naomba mpatie majina ya shule ambazo anazihitaji kwa sababu siwezi kuyataja yote hapa.

SPIKA: Ahsante naomba muangalie muda na nina swalii langu moja Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Josephine Chagula atauliza swalii hilo!

Na. 152

Mlipuko wa Malaria Mkoa wa Geita

MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA aliuliza:-

Mkoa wa Geita una tatizo kubwa sana la maambukizi ya malaria yanayosababishwa na mashimo makubwa yalioachwa wazi baada ya uchimbaji wa madini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti uharibifu huo wa mazingira katika Mkoa huo na kuondoa tatizo la mlipuko wa malaria?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Josephine Thabita Chagula, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Geita ilipewa hadhi ya kuwa Mkoa Julai, 2011. Takwimu za matokeo ya utafiti wa Taifa katika ngazi ya kaya (*Tanzania HIV, Malaria Indicator Survey- THMIS*), za mwaka 2011/2012, zilionesha kiwango cha

Nakala ya Mtando (Online Document)

maambukizi ya *malaria* Mkoa wa Geita kuwa ni asilimia 33. Kwa takwimu hizi, ni dhahiri Mkoa wa Geita una kiwango kikubwa cha maambukizi ya *malaria* kuliko Mikoa yote nchini, utafiti unaofuata utafanyika 2015/2016 kwani tafiti hizi hufanyika kila baada ya miaka minne.

Mheshimiwa Spika, mashimo yaliyoachwa wazi baada ya kuchimba madini husababisha maji kutuama na kuwa chanzo cha mazalio ya mbu. Vyanzo vingine vya mbu kuzaliana ni vidimbwi, matairi chakavu ya magari, mashimo ya vyoo na kadhalika. Sheria ya Uchimbaji wa Madini namba 14 ya 2010, pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya 2004 na Kanuni zake za Athari kwa Mazingira za 2005, zinawataka wachimbaji kuonesha “Mining Closure Plan,” lengo likiwa kuwabana kisheria wenyewe migodi kufukia mashimo baada ya uchimbaji wa madini kumalizika. Upande wa mazingira, mwekezaji anahitajika kufanya tathmini ya athari za mazingira (*environmental impact assessment*) na kuacha mazingira yakiwa salama.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Wizara inazitaka Mamlaka ya Usimamizi katika mikoa yote kuhakikisha zinasimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria hizi na kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukubwa wa tatizo la *malaria* katika Mikoa yote ya Kanda ya Ziwa, ikiwemo Geita, hatua zinazochukuliwa kupunguza maambukizi ya *malaria* ni:- upulizaji wa dawa ya ukoko katika majumba ili kudhibiti mbu wapevu wa *malaria*; kuongeza matumizi ya vyandarua kwa kipitia kampeni ya ugawaji kwa watu wa kaya (*Replacement Universal Mass Campaign* kama utakavyofanyika mwakani 2014/2015, Geita watapata vyandarua vipatavyo 900,000.

Mheshimiwa Spika, aidha, mpango wa kuangamiza mazalio ya mbu kwa kutumia viuatilifu vya kibaiolojia (*bioarvicides*) katika Mitaa ya Mji wa Geita utaanza mara baada ya Kiwanda cha Kuzalisha Viuatililafu iliyojengwa Kibaha kwa kushirikiana na Serikali ya Cuba kuanza uzalishaji.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Josephine Chagula, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Nashukuru sana kwa majibu ya Naibu Waziri lakini nina swali moja tu. Kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kwamba, Mkoa wa Geita unaongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi sana wa *malaria* na hii ni kutokana na mashimo mengi yayoachwa wazi kwa muda mrefu na wachimbaji wa madini.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Je, Serikali sasa haioni kuna haja ya kuleta Sheria ambayo itawataka wachimbaji hawa wa madini kufukia mashimo yao ya awali kabla ya kuanza tena kuchimba mashimo mengine, ili tuweze kunusuru afya na maisha ya wananchi wa Mkoa wa Geita? (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, suala hili la mazingira kulingana na *Mining Closure Plan* ambayo kisheria inabidi wenyewe migodi watimize masharti haya. Ndio sababu inalazimu kuainisha bayana kabisa suala zima la tafiti ya mazingira (*Environmental Impact Assessment*) ambayo inakuwa katika mpango mzima. Lakini kwa kushirikiana na Wizara ya Madini na Nishati, suala hili tutashirikiana kufuatilia ili kuona taratibu zote za kisheria zimefuatwa.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge najua mnapenda kuuliza maswali, lakini muda wenyewe umekwisha. Kwa hiyo, niwatambue wageni waliopo humu ndani.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo amba ni Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wenyeviti wa Bod, Maafisa kutoka Wizarani na Watumishi kutoka Asasi mbalimbali zilizo chini ya Wizara hiyo. Yupo anayeongoza timu hiyo ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Sihaba Nkinga, asimame alipo! Halafu pia yupo na Naibu Katibu Mkuu Profesa Elisante Ole Gabriel. (Makofi)

Tuna Wageni wa Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo (Mheshimiwa Juma Nkamia), amba ni Mkurugenzi wa *Steps Entertainments and Steps Solar* huyo Ndugu Dileshi Solanky. Kama nime-mess up the names I am sorry.

Halafu kuna Ndugu Juma Mtetwa-TBC-Ulimwengu wa filamu, asimame alipo. Okay ahsante, yupo upande huu hapa. (Makofi)

Yupo ndugu Francis Robert ambaye ni Mkurugenzi wa Radio Five. (Makofi)

Tuna wageni wengine wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ni wanafunzi nane kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Wasimame walipo. (Makofi)

Nakala ya Mtando (Online Document)

Wageni wa Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba ambao ni wanafunzi 20 kutoka Shule ya Sekondari Tumaini, Singida wakiongozwa na Walimu wao Ndugu Atupele Mbila Joel na Ndugu Khard Mtoi. Wasimame wanafunzi hawa kama wapo ndani! Ahsante sana karibuni naomba msome kwa bidii. (Makofii)

Kuna Mkurugenzi Mtendaji wa Mwananchi Communication, Bwana Tido Mhando alipo asimame! Yeye amekosa nafasi? Okay alikosa nafasi labda, halafu tuna wageni 27 wa Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbewe, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Bungeni pamoja nao yupo Diwani wa CHADEMA, Ndugu Sinock Olenairuko, nimesema vibaya? Wameniandikia CHADEMA. (Makofii)

Halafu wameniandikia pia na Ndugu Tehera Kipara, Mwenyekiti wa CCM Kata, hawakusema! Naomba hawa wageni wawili wasimame walipo kama nimembatiza Chama basi Kiongozi wao, ahsanteni sana. Kwa hiyo, inaonesha Kiongozi wa Kambi ya Upinzani hana ubaguzi. (Makofii)

Nina wageni wa Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, ambaye ni Waziri Kivuli, Sera, Uratibu na Bunge ambao ni Wanakwaya wa kwaya ya Mtakatifu Joseph Mfanyakazi Chuo Kikuu. Haya msimame wanakwaya nyie, ahsante sana. Ahsante sana sijui Kwaya ya kitu gani hiyo. (Makofii)

Kuna wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Anthony Mbassa kutoka Bihalamuro Magharibi wakiongozwa na Ndugu Severine Stephano. Huyu yupo wapi? Wageni wako wapi? Haya Zephine yupo pale na wageni wengine wasimame. (Makofii)

Kuna wageni wa Mheshimiwa Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi ambao ni Mwenyekiti wa Riadha Mkoa wa Singida ambaye ni Ndugu Elia Nollo na Mwenyekiti wa CCM mstaafu Kata ya Sanjaranda, Ndugu Hassan Kashinje naomba wasimame walipo, kuna wengine watakosa nafasi. (Makofii)

Kuna Mheshimiwa Profesa Msolla wa Kilolo ambao wanaongozwa na ndugu Sifuni Makongwa, Mwenyekiti wa UVCCM, Kilolo. Wasimame hao wageni. Ahsanteni sana. (Makofii)

Kuna wageni wa Mheshimiwa Ester Bulaya ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma na wenyewe wasimame walipo. Ahsanteni sana msome kwa bidii. (Makofii)

Tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Waziri Kivuli Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo wakiongozwa na Ndugu John Mwambigija,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mwenyekiti wa CHADEMA, Mbeya Mjini. Wasimame hao wote walipo. Ahsanteni sana. (Makofii)

Nina wageni waliokuja Bungeni kwa ajili ya mafunzo hawa ni wanafunzi 42 na Walimu watatu kutoka Chuo cha Red Cross, Makole. Naomba wasimame wote walipo, okay ahsante sana na tunawatachia kazi njema. (Makofii)

Tuna wanafunzi 31 kutoka Chuo cha Mipango, Dodoma, naomba msimame mlipo kama mpo. Ahsante sana msome kwa bidii. (Makofii)

Tuna wageni watatu kutoka Aseki Business School wakiongozwa na Ndugu Omari Kiputiputi, Mkuu wa Chuo cha Aseki hiyo, wasimame walipo. Ahsanteni karibuni sana na wageni wengine ambaao hamkukaribishwa mnakaribishwa. (Makofii)

Matangazo ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Sitta, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na Kikao katika ukumbi wa Pius Msekwa C.

Pia mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo mchana watakuwa na Kikao chao ambacho kitafanyika ukumbi wa Hazina ndogo Na.125.

Waheshimiwa Wabunge, tumekula sana muda, naomba tuendelee!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mwongozo baadaye.

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa
Mwaka 2014/2015 – Wizara ya Habari,
Vijana, Utamaduni na Michezo**

Nakala ya Mtando (Online Document)

SPIKA: Sasa namwita Mtoa hoja!

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2014/2015 Kama Ilivyosomwa Bungeni

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kutumia fursa hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunilinda na kuniipa nguvu ya kutekeleza majukumu yangu na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Wabunge wapya waliochaguliwa hivi karibuni kwa ushindi wa kishindo amba ni Mheshimiwa Yusuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani; Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Jimbo la Kalenga; na Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge wa Jimbo la Chalinze. (Makofisi)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kuwapa pole familia za wanahabari, wasanii na wanamichezo pamoja na tasnia nzima za Habari, Utamaduni na Michezo kwa kuondokewa na wapendwa wetu. Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo kwenye Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Asasi zake kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu imegawanyika katika maeneo makuu matano kama ifuatavyo:-

Eneo la kwanza, ni Utangulizi; eneo la pili ni Majukumu ya Wizara; eneo la tatu ni Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2013/2014; eneo la nne ni Mpango na Bajeti kwa mwaka 2014/2015; na eneo la tano ni Hitimisho.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara; Wizara yangu inatekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera za Sekta za Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo;

Nakala ya Mtando (Online Document)

- (ii) Kuratibu na kusimamia masuala ya maendeleo ya vijana ili kuwawezesha kujitambua, kujajiri, kuajirika, kuwajibika na kujitegemea;
- (iii) Kuwa Msemaji Mkuu wa Serikali na kusimamia vyombo vya Habari nchini; Kuratibu na kusimamia maendeleo ya utamaduni nchini;
- (iv) Kuratibu na kusimamia maendeleo ya michezo nchini;
- (v) Kusimamia utendaji kazi wa Asasi, Miradi na programu zilizo chini ya Wizara; na
- (vi) Kuendeleza, kuwezesha na kuratibu masuala ya kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ilipanga kukusanya mapato ya jumla ya shilingi milioni mia nane themanini na mbili, mia mbili na tatu elfu (882,203,000) kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2014, jumla ya shilingi milioni mia sita sitini na tatu, ishirini na tisa elfu, mia tano sitini na tisa (663,029,569) zilikusanywa ambazo ni sawa na asilimia sabini na tano (75%) ya lengo la makusanyo kwa mwaka. Kwa upande wa fedha za Matumizi ya kawaida, Wizara ilitengewa jumla ya shilingi bilioni kumi na saba, milioni mia sita ishirini na nane, arobaini na tano elfu (17,628,045,000).

Mheshimiwa Spika, fedha hizo zilijumuisha Mishahara ya Wizara; shilingi bilioni mbili, milioni mia sita kumi na saba, mia tano tisini na nane elfu (2,617,598,000) na Asasi ni Shilingi bilioni sita, milioni mia sita thelathini na tisa, mia tano ishirini na saba elfu (6,639,527,000). Matumizi Mengineyo ya Wizara ni Shilingi bilioni nne, milioni mia tisa arobaini na moja, mia tisa ishirini elfu (4,941,920,000) na Asasi ni shilingi bilioni tatu, milioni mia nne ishirini na tisa (3,429,000,000).

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili, 2014, jumla ya shilingi bilioni kumi na tatu, milioni mia mbili tisini na mbili, mia tano thelathini na tisa elfu, mia nne tisini na nane (13,292,539,498) za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo Matumizi Mengineyo ni shilingi bilioni nne, milioni mia saba arobaini, mia tisa hamsini na saba elfu (4,740,957,000) na Mishahara ni shilingi bilioni nane, milioni mia tano hamsini na moja, mia tano themanini na mbili elfu, mia nne tisini na nane (8,551,582,498).

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, Wizara ilitengewa jumla ya shilingi bilioni kumi na mbili, milioni mia saba

Nakala ya Mtando (Online Document)

(12,700,000,000). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2014 jumla ya shilingi bilioni nne, milioni mia tatu ishirini na saba, mia tano elfu (4,327,500,000) zilipokelewa ambazo ni sawa na asilimia 34 na shilingi bilioni mbili, milioni mia tatu na kumi na ishirini na moja elfu (2,310,021,000) zilitumika.

Miradi iliyotekelawa ni pamoja na Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Ujenzi wa Ofisi - BAKITA, Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Habari; katika mwaka 2013/2014, Wizara ilikabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na baadhi ya Vyombo vy'a Habari kukiuka sheria kwa kuandika na kurusha habari ambazo hazingatii kanuni na maadili ya taaluma ya habari. Pia ongezeko la mifumo na njia za mawasiliano kama mitando ya kijamii ambayo mingine imetumiwa kuathiri maudhui ya habari zinazotolewa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto hizo kwa kutoa onyo na kufungia baadhi ya vyombo vy'a habari viliyokiuka maadili. Wizara pia imeelekeza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kutekeleza kikamilifu mpango wa kusajili wamiliki wote wa mitando hiyo. Aidha, Wizara inaendelea kutoa elimu na kuwaelekeza wamiliki na Wahariri wa vyombo vy'a habari kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyowekwa. Wizara inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kukataa kutumia fursa hizi za mitando ya kijamii kueneza chuki, uchochezi na vijiwe vy'a udaku.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara imekamilisha maandalizi ya Muswada wa Sheria ya Kusimamia Vyombo vy'a Habari na sasa uko katika hatua nzuri za mwisho. Kwa kuzingatia utaratibu uliopo, Muswada huu utafikishwa katika Bunge lako Tukufu lijalo la kutunga Sheria.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kuimarisha njia za mawasiliano kati ya Serikali na wananchi wake, Wizara yangu inafanya maboresho ya Tovuti ya Wananchi ili kuweza kuimarisha mifumo na muonekano wa Tovuti hiyo. Maboresho hayo yakikamilika, yatawawezesha wananchi popote walipo kuwasiliana na Serikali kwa kutumia njia za kisasa. Aidha, itawapunguzia wananchi gharama za kuwasilisha kero, hoja na maoni mbalimbali katika taasisi za Serikali. Kazi ya kujengwa upya na kuimarisha Tovuti hiyo ili kuwa na muonekano mpya unaokidhi mabadiliko ya sasa ya sayansi na teknolojia inatarajiwa kukamilishwa mwisho wa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Wizara, imendelea kukusanya habari, kupiga picha za matukio mbalimbali ya Serikali na kuzihifadhi katika maktaba; pamoja na

Nakala ya Mtando (Online Document)

kuzisambaza kwenye vyombo mbalimbali vya habari kwa lengo la kutoa habari na kuelimisha jamii. Wizara kama Msemaji Mkuu wa Serikali ilifafanua masuala na hoja mbalimbali zinazohusu Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia Vitengo vya Mawasiliano Serikalini kwa lengo la kutoa habari na kuelimisha umma juu ya utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Wizara imetoa mwongozo ulioainisha taratibu za kuendesha vitengo hivyo na kuhimiza Wizara na Asasi zote za umma kuajiri Maafisa Mawasiliano Serikalini.

Mheshimiwa Spika, jumla ya mikutano 255 ya wasemaji wa Asasi za Serikali na Vyombo vya Habari ilifanyika kuwaelimisha wananchi kuhusu shughuli mbalimbali za Serikali zinazofanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Vyombo vya Habari katika vikao vya Bunge vilivyofanyika Dodoma na pia kuhakikisha inawapatia vitambulisho waandishi wa habari wa ndani na nje wenye sifa za taaluma ya Uandishi wa Habari.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kuititia TCRA ilikamilisha awamu ya kwanza ya uhamaji wa kutoka katika mfumo wa utangazaji wa analogia kwenda dijiti. Baada ya zoezi hili tathmini imefanyika ambayo ilionesha mwitikio mzuri wenye mafanikio. Hivi sasa zoezi hili limeingia katika awamu ya pili iliyoanza tarehe 31 Machi, 2014 na inatarajiwa kukamilika kabla ya tarehe 30 Juni, 2015.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na TCRA imesajili vituo nane (8) vya redio na vituo viwili (2) vya televisheni na hivyo kuwezesha Tanzania kuwa na jumla ya vituo tisini na tatu (93) vya redio na ishirini na nane (28) vya televisheni. Pia uhamaji kutoka mfumo wautangazaji wa analogi kwenda mfumo wa dijiti umesaidia kupanua wigo wa masafa na kuongeza ubora wa matangazo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Kamati ya Maudhui ilipokea na kushughulikia malalamiko saba ya vituo vya televisheni na redio kutokana na kurusha vipindi ambavyo vilikiuka maadili ya utangazaji. Kituo binafsi cha televisheni kilicholalamikiwa kwa kurusha kipindi kilichokiuka kanuni na maadili ya utangazaji kilipewa onyo. Pia vituo sita vya redio viliviyolalamikiwa kwa kurusha vipindi vilivyoikiuka kanuni za utangazaji na maadili ya uandishi wa habari vilipewa onyo na vingine kutozwa faini kati ya shilingi laki mbili (200,000) na shilingi milioni tano (5,000,000).

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) imeendelea kuimarisha upanuzi wa usikivu wa Redio na Televisheni ya Taifa. *TBC* ilirusha pia matangazo ya vikao vya Bunge moja kwa moja, pamoja na matangazo ya Bunge Maalum la Katiba kwa lugha za alama, kwa ajili ya watu wenyewe mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi hizo, *TBC* inakabiliwa na tatizo la uchakavu wa vifaa vya kurushia matangazo. Uchakavu huo wakati mwingine umesababisha tatizo la kukatika kwa matangazo yakiwemo matangazo ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge wawe wavumilivu kwani Wizara imejipanga katika kuendelea kutatua changamoto hizo ili kuboresha huduma zitolewazo na *TBC*. Kupitia Bunge lako Tukufu niwaombe Waheshimiwa Wabunge watuunge mkono kufanikisha malengo tuliyojiwekea ya kuimarisha *TBC*.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kutatua changamoto za *TBC*, mwezi Aprili, 2014, imepokea gari jipyga la kisasa la matangazo kutoka Serikali ya Watu wa China. Gari hili litasaidia sana kuongeza nguvu katika kutatua tatizo la uchakavu wa vifaa. Sambamba na hatua hizo, wataalam watano (5) wa *TBC* walipelekwa nchini China kupata mafunzo maalum ya namna ya kutumia gari hilo pamoja na vifaa husika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Kampuni ya Magazeti ya Serikali (*TSN*) imeendelea na mkakati wa upanuzi wa Kiwanda cha Uchapaji. Katika Mkakati huo, Makubaliano na Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*) yamekamilika ambapo *TIB* itaipatia *TSN* mkopo wa shilingi bilioni 2.7 kwa ajili ya kujenga jengo la kitega uchumi. Hatua hii itasaidia Kampuni kuongeza uzalishaji na kuweza kufikisha huduma kwa wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kupanua wigo wa mapato, *TSN* na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) wameingia mkataba wa ubia wa kuendeleza kiwanja kilichopo Kitalu Na. 27, Central Business Park, Dodoma, kwa ajili ya kujenga jengo la kupangisha. Maandalizi ya ujenzi yameanza. Ukamilishaji wa Miradi huu utasaidia Kampuni kujiongezea mapato zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha usambazaji wa magazeti, Kampuni imepata pipipiki 20 toka Serikali ya Watu wa China kwa ajili ya usambazaji wa mijini. *TSN* pia imeingia makubaliano na kampuni za usafirishaji ili kusafirisha magazeti ndani na nje ya nchi ili kuwezesha upatikanaji wa habari za ukweli kwa wakati.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maendeleo ya Vijana; katika kushughulikia masuala ya vijana mwaka 2013/2014, changamoto mbalimbali zimejitokeza ambazo ni pamoja na baadhi ya Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya kutokuajiri Maafisa Vijana.

Uelewa mdogo wa vijana katika kubuni na kutayarisha maandiko ya miradi, kuanzisha na kutekeleza miradi endelevu, vijana wengi kukosa ujuzi na maarifa ya ujasiriamali na biashara ikiwa ni pamoja na kukosa ujuzi wa matumizi sahihi ya fedha za mikopo wanazopata kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na vijana kushindwa kujitambua na kufanya maamuzi sahihi kuhusu maisha yao.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maendeleo ya Vijana chini ya Wizara yangu ina vitengo mahsusи vya kushughulikia hizi changamoto za Vijana. Vitengo hivi ni Uratibu na Uwezeshaji wa Vijana Kiuchumi; Ushauri Nasaha, Makuzi na Maongozi, pamoja na Mafunzo na Maendeleo ya Ujuzi. Hii ni kwa mujibu wa instrument ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia vitengo hivi na kushirikiana na Wadau mbalimbali kama muundo na majukumu ya Wizara yangu yanavyoelekeza, Wizara yangu imeendelea kuwajengea vijana uwezo wa kiuchumi kwa kuwapa mafunzo na ujuzi katika maeneo ya ujasiriamali, uanzishaji wa miradi endelevu ya uzalishaji mali, uongozi, stadi za maisha na matumizi sahihi ya mikopo kwa kushirikiana na Benki ya NMB. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya Viongozi wa vikundi vya vijana 457 na Watendaji 211 kutoka Wilaya na Mikoa yote nchini wamenufaika na mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana hasa wanaomaliza Vyuo Vikuu na Vyuo vya Kati, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya vijana na Wizara mbalimbali kama vile Kilimo na Ushirika; Ufugaji; Madini na Nishati na Viwanda imeendelea kuhamasisha vijana kuunda makampuni binafsi ya biashara na vikundi vya kuzalisha mali ili waweze kujiajiri na kuajiri wengine na kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara inaendeleza mpango wa kutafutia kazi za kujitolea vijana hawa ili kuwawezesha kupata uzoefu kabla ya ajira. Mpango umeanzia Dar es Salaam, mfano ambapo vijana 27 wanafanya kazi sehemu mbalimbali kwa kujitolea. Wizara pia imehamasisha vijana wa Vyuo Vikuu kujitolea mashuleni kufundisha kwa kusaidiana na Walimu husika.

Mheshimiwa Spika, Wizara vile vile kwa kushirikiana na Shirika la IYF imeendelea kuandaa kambi za mafunzo yenye lengo la kubadilisha fikra za vijana nchini kwa malengo chanya ya kujituma, kupenda kazi, kushirikiana, kupendana, kupenda nchi na kutii sheria. Kwa mfano, mwaka 2013 vijana 800

Nakala ya Mtando (Online Document)

kutoka Mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani walihudhuria kambi ya Kimataifa iliyofanyika mjini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, naendelea kutoa wito na kuhimiza wadau wote wa maendeleo ya vijana nchini, tuendelee kushirikiana katika kuhakikisha kuwa vijana wetu wanapata uwezo wa kuwajibika na kuchangia katika maendeleo ya maisha yao na ya Taifa kwa ujumla. Wizara inaendelea kuhimiza Wakuu wa Mikoa kutenga maeneo kwa kazi za vijana na muitikio unaendelea kuwa mzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Maendelo ya Vijana; napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mwongozo wa kusimamia Mfuko huu umeandaliwa na kusambazwa kwa Makatibu Tawala wa Mikoa yote tangu mwezi Agosti, 2013. Kulingana na Mwongozo huu, kila Halmashauri inahitajika kuanzisha SACCOS ya Vijana ambayo itashughulikia utoaji wa mikopo hii. Hadi kufikia Aprili, 2014, Halmashauri 22 kati ya 151 zimeanzisha SACCOS za Vijana. Nawapongeza sana wale wote walioweza kufanikisha uanzishaji wa SACCOS hizi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2013/2014, jumla ya Shilingi bilioni 6.1 zilitengwa kwa ajili ya Mfuko huu. Hadi Aprili, 2014, Wizara imepokea kiasi cha shilingi bilioni mbili (2,000,000,000). Kati ya fedha hizo zilizokopeshwa ni shilingi milioni mia moja sabini na mbili, mia sita na tisa elfu (172,609,000) kwa Miradi ya vikundi vya vijana 25. Hata hivyo, Wizara inaendelea na uchambuzi wa maombi ya vikundi 1,178 yenye thamani ya shilingi bilioni nane, milioni mia nne ishirini na moja, mia sita na sita elfu, mia saba hamsini (8,421,906,750) ili kuweza kuvikopesha vikundi vitakavyotimiza vigezo vilivyobainishwa kwenye mwongozo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2013, Mbio za Mwenge wa Uhuru zilizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 5 Mei, 2013 katika Kijiji cha Chokocho, Mkoani Kusini Pemba na kufikia kilele Mkoani Iringa tarehe 14 Oktoba, 2013 na Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuititia mbio hizo, jumla ya miradi ya maendeleo 1,229 yenye thamani ya shilingi bilioni mia moja hamsini na nane, milioni mia tano themanini na saba, mia sita sitini na saba elfu, mia sita kumi na tatu na senti arobaini (158,587,667,613.40) ilizinduliwa au kuwekewa mawe ya msingi. Uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2014 umefanyika tarehe 2 Mei, 2014 Mkoani Kagera; na Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, dhamana ya kuhakikisha hili linafanyika vizuri wamepewa vijana. Mbio hizi zinalenga kuhamasisha maendeleo ya wananchi,

Nakala ya Mtando (Online Document)

kudumisha umoja, amani, upendo na mshikamano wa Kitaifa. Hivyo basi, hatuna budi sisi sote kuthamini na kuenzi Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na maadhimisho ya kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru, Wizara iliratibu maadhimisho ya Wiki ya Vijana Kitaifa ambayo yalianza tarehe 8 hadi 14 Aprili, 2013, Mkoani Iringa. Maonyesho katika Wiki ya Vijana yalishirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Ofisi za Mikoa 10, Idara za Serikali 16, Halmashauri za Wilaya 21, Asasi za Kiraia 14, Vikundi vya Vijana Wajasiriamali 53, Vyuo Vikuu vya Elimu vitatu na Taasisi za Kibenki tatu.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Wiki hiyo, Vijana 300 kutoka makundi mbalimbali ya Vijana walishiriki katika midahalo ambapo pia walipatiwa mafunzo ya aina tofauti yenye lengo la kuwajengea uelewa wa masuala mbalimbali ya maendeleo ya vijana. Kwa mfano, umuhimu wa kuwa na Wiki ya Vijana kila mwaka, ujasiriamali, dhana ya uwajibikaji, umuhimu wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni; katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Wizara ilikabiliana na changamoto zilizotokana na athari za utandawazi na maendeleo yenye kasi kubwa ya sayansi na teknolojia, mmomonyoko wa maadili kwa watu wa rika mbalimbali, wizi wa kazi za wasanii kutokana na upatikanaji kirahisi wa kurudufu kazi husika. Malalamiko makubwa yamekuwa kwamba, hali hii imekuwa ikiwaneemeshaa mapromota na wasambazaji wa bidhaa za filamu na muziki ambao sio wasanii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizi, Wizara kuitia Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni:- imeimarisha ukusanyaji na uhifadhi wa takwimu za tasnia ya utamaduni; imetoa mafunzo ya namna ya kuainisha namba za misimbo (code numbers) za sekta ya utamaduni ambazo zitatumika Kitaifa na Kimataifa; imefanya tafiti za maktabani za lugha za jamii 10 na utafiti wa uwandani katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ili kuhifadhi sarufi, misamiati na istilahi za lugha ya Taifa – Kiswahili; imefanya utafiti wa kina kuhusu mila za jando na unyago miongoni mwa jamii za Wamakonde, Wamakua na Wayao.

Mheshimiwa Spika, utafiti huo umewezesha kukamilisha maandalizi ya pendekezo la elementi ya urithi usioshikika ambao hatimaye Serikali itaomba urithi huo uingizwe kwenye orodha ya urithi wa utamaduni wa dunia unaotambuliwa na UNESCO. Elementi hiyo ni ya ngoma ya “Nankachanga” kutoka Kijiji cha Namahonga, Wilaya ya Tandahimba, Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, iliratibu zoezi la

Nakala ya Mtando (Online Document)

kuwapata Watanzania wenyе sifa stahiki ili kunufaika na fursa zinazotokana na Tanzania kuwa Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Fursa za ajira katika Kamisheni zitashindaniwa na nchi zote wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, hivyo ni muhimu kwa Tanzania kuwa na wagombea sadifu ili kuhimili vishindo vya kinyang'anyiro hicho. Wizara hizi mbili zitaendelea kusimamia zoezi hili kuhakikisha fursa zilizopo zinatumika ipasavyo na Watanzania wetu wanapata hizo fursa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, kazi ya ukusanyaji wa kumbukumbu za mapambano ya kupigania uhuru nchini iliendelea kufanywa kwa kushirikiana na Maofisa Utamaduni wa Mikoa na Wilaya. Jumla ya kumbukumbu 63 zimerekodiwa katika kanzidata ya Programu. Aidha, Washirika katika Programu hii kutoka Namibia, Afrika Kusini na Msumbiji walikuja nchini kujifunza namna Tanzania ilivyotekeleza shughuli za uhifadhi na utunzaji wa kumbukumbu za kihistoria za Ukombozi wa Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, Programu hii ni muhimu sana katika kutunza na kuhifadhi kumbukumbu za Ukombozi wa Bara la Afrika kwa vizazi vijavyo. Ni Programu kubwa na Wizara inaendelea kutafuta ufadhilli kufanikisha malengo ya Programu hii.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2013/2014, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA):- liliandaa na kurusha vipindi 52 vya 'Lugha ya Taifa', vipindi 52 vya 'Kumepambazuka' vipindi 52 vya 'Ulimwengu wa Kiswahili'; lisoma jumla ya Miswada 24 ya vitabu vya taaluma na kuvipatia ithibati ya lugha; limeratibu na kutoa huduma ya tafsiri kwa Asasi 14 za Serikali, Mashirika ya Umma, pamoja na watu binafsi; limetoa huduma ya ukalimani kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika huko Addis Ababa, Ethiopia, mwezi Julai, 2013 na mwezi Januari, 2014 na ukalimani kwenye Mkutano wa Bunge la Afrika nchini Afrika Kusini mwezi Novemba, 2013 na Machi, 2014.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA):- limeendesha midahalo 52 ya Jukwaa la Sanaa kwa wasanii, waandishi wa habari na wadau wa sanaa 3,850; limeendesha mafunzo ya utambaji wa hadithi, ngoma za asili kwa watoto 200 wa shule za msingi katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa lengo la kuibua na kuendeleza vipaji vyao katika fani husika na limeendelea kuingiza taarifa muhimu za wasanii na wadau wa sanaa za muziki katika mfumo wa kielektroniki unaouanganisha Taasisi za TRA, COSOTA, Bodi ya Filamu na BASATA. Aidha, Baraza limeendelea na hatua za awali za uandaaji wa mfumo wa kanzidata za wasanii mahiri na kukusanya

Nakala ya Mtando (Online Document)

taarifa zao muhimu. Wizara pia imeendelea kuhamasisha watoto, vijana na wananchi kwa ujumla kujenga utamaduni wa kujisomea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Bodi ya Filamu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), imeendelea kuhimiza matumizi ya stempu za kodi. Hadi sasa, jumla ya wadau 86 wamechukua Stempu 4,380,000 zilizotolewa kwa upacha (*duplicate*) kwa ajili ya kuweka kwenye kazi za filamu na muziki. Kati ya hizo 3,810,000 ni kwa kazi za filamu na 570,000 ni za muziki.

Mheshimiwa Spika, Bodi imepitia Miswada 139 ya kutengenezea filamu kwa watengenezaji wa ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia Aprili, 2014, jumla ya filamu 1,206 sawa na CD 2,412 zilikaguliwa na kuwekewa madaraja ambapo filamu 127 zilifanyiwa marekebisho na filamu saba hazikuruhusiwa kuoneshwa hadharani. Aidha, Kati ya filamu 215 za nje zilizowasilishwa, filamu mbili zilelekezwa kufanyiwa marekebisho na filamu tano za nje zilizuiliwa kuonyeshwa hadharani.

Mheshimiwa Spika, aidha, Bodi imekagua na kuidhinisha maeneo 13 ya uzalishaji wa filamu. Bodi imeendelea kutoa elimu kuhusu urasimishaji wa tasnia ya filamu kupitia matangazo kwenye magazeti, vipeperushi, mabango ya barabarani, maadhisho na sherehe mbalimbali, vipindi mbalimbali vya TV, Redio na vikao vya wadau.

Mheshimiwa Spika, Bodi ilihamasisha wadau kushiriki katika tuzo mbalimbali za filamu Kitaifa na Kimataifa ambapo hadi kufikia Aprili, 2014, jumla ya filamu 10 ziliingia katika tuzo mbalimbali na filamu ya Mdundiko ya Kitanzania ilishinda katika tuzo ya Kimataifa huko Marekani. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa):- iliendesha mafunzo ya stashahada kwa wanachuo wapatao 238 na mafunzo ya muda mfupi kwa wasanii 255 walio kazini; ilisimamia na kuendesha tamasha la 32 la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania na ilishiriki mikutano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ilioitishwa kujadili mustakabali wa vituo vya Jumuiya vyenye ubora uliotukuka (Centre of Excellency).

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maendeleo ya Michezo, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara imekabiliana na changamoto mbalimbali zikiwemo uchache wa wataalam waliobobea katika fani mbalimbali za michezo, upungufu wa miundombinu, mwamko mdogo wa jamii kushiriki katika michezo na udhaifu wa uongozi katika baadhi ya Vyama mbalimbali vya Michezo.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo, Wizara kupitia Chuo cha Maendeleo ya Michezo, Malya, Mkoani Mwanza imeendelea kutoa mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Ufundishaji Michezo na Stashahada ya Uongozi wa Utawala kwa wanachuo 40. Vilevile, imeendesha Mafunzo ya muda mfupi ya fani mbalimbali za michezo kwa vijana 200, Walimu 100 wa shule za Msingi, Walimu 100 wa shule za Sekondari, Viongozi wa Michezo na Makocha 102 katika Vituo vya Michezo vya Kanda ya Kaskazini (Arusha) na Kusini (Songea).

Mheshimiwa Spika, hivi sasa zaidi ya asilimia 50 ya Walimu ambao hushiriki katika uendeshaji na ufundishaji wa michezo kwa ajili ya mashindano ya shule za msingi (UMITASHUMTA) na shule za sekondari (UMISETA) ni wahitimu wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, Vituo vya Michezo na Mpango wa Michezo kwa Jamii. Wizara bado inahimiza kila Halmashauri na Mkoa kuajiri Maafisa Michezo.

Mheshimiwa Spika, mafunzo yaliyotolewa katika Vituo vya Arusha na Songea yaliwashirikisha pia jumla ya vijana watatu wenyewe Ulemavu wa Walimu 42 wanaofundisha michezo kwa vijana wenyewe ulemavu wa aina mbalimbali chini ya utaratibu jumuishi ujulikanao kwa Kiingereza kama *Inclusion*.

Mheshimiwa Spika, katika kutafuta maeneo mapya ya ushirikiano wa Kimataifa, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, imekamilisha hatua za awali za kujenga miundombinu ya Mchezo wa kupanda Majabali (*Rock Climbing*) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Aidha, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, Wizara iliendesha Kongamano la Kimataifa la Viongozi Wanawake wa Michezo liliofanyika Dar es Salaam tarehe 16 – 18 Desemba, 2013 na kushirikisha jumla ya nchi 17 za Bara la Afrika na Ulaya.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Vyama vya Michezo, imeendelea kufanya maandalizi ya timu ya Taifa zitakazoshiriki kwenye michezo ya Jumuiya ya Madola itakayofanyika Glasgow, Scotland, mwezi Julai, 2014. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, timu sita za Taifa za mchezo wa Riadha, Ngumi, Kuogelea, Judo, Kunyanya Vitu Vizito na Mpira wa Meza zimepata fursa za kuweka kambi za mazoezi nchini Uturuki, Ethiopia na New Zealand kwa ajili ya maandalizi ya michezo ya Jumuiya ya Madola. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia ukamilishaji wa ukarabati wa Uwanja wa Uhuru ambao ni sehemu ya eneo Changamani la Michezo lilioloko Dar es Salaam. Ukarabati huu unatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2014.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Wizara ilitoa huduma ya Kinga na Tiba kwa wanamichezo na wadau wa michezo 108,000 kwa timu za michezo mbalimbali. Wizara kwa kutumia matukio ya michezo imeendelea na upimaji na utoaji wa elimu kwa wanamichezo kuhusu udhibiti wa matumizi ya dawa na mbinu haramu za kuongeza nguvu katika michezo. Hadi kufikia Aprili, 2014 wanamichezo 27 walichukuliwa vipimo. Hata hivyo, hakuna aliyegundulika kutumia dawa na mbinu haramu baada ya majibu ya maabara.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Baraza la Michezo la Taifa (BMT), kwa kushirikiana na "UK Sport" na "British Council", kupitia mradi wa "*International Inspiration*", limekamilisha uandaaji wa mifumo rasmi ya Elimu na Ithibati ya Ufundishaji wa Michezo Nchini; Michezo Shirikishi kwa Jamii; Ufuatiliaji na Tathmini ya Maendeleo ya Michezo Nchini; na Utambuzi na Ukuzaji wa Vipaji vya Michezo Mionganoni mwa Vijana. Pia limeendesha mafunzo ya utawala bora kwa Vyama vya Michezo 17 na kusimamia uchaguzi kwa Vyama na mashirikisho ya michezo 14.

Mheshimiwa Spika, Baraza, limeendesha mafunzo ya michezo kwa jamii kwa Walimu 76 wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Mtwara Vijijini kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na pia liliandaa na kuendesha Kongamano la Kimataifa kuhusu Mfumo wa Elimu ya Michezo kwa Jamii kwa Nchi za Kanda ya V ya Michezo Barani Afrika. Kongamano hilo lilifanyika mwezi Novemba, 2013 huko Arusha na kuhudhuriwa na nchi saba ambazo ni Uganda, Kenya, Rwanda, Ethiopia, Misri, Zimbabwe na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha, Baraza limeendesha mafunzo ya uamuzi na ukocha kwa Walimu na wanafunzi 761, kati ya hao Walimu ni 421 na wanafunzi ni 340. Mafunzo haya, yaliyo katika majoribio ya mradi wa *International Inspiration* yamefanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Ruvuma, Mwanza na Mjini Magharibi, Zanzibar. Aidha, jumla ya wanafunzi 50 wenye ulemavu na Walimu 32 wanaofundisha michezo kwa watu mbalimbali walishiriki katika mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, utawala na menejimenti ya rasilimali watu, katika kipindi cha mwaka 2013/2014, watumishi 51 wamehudhuria mafunzo katika fani mbalimbali kama ifuatavyo:- watumishi thelathini na wawili (32), mafunzo elekezi; watumishi kumi na saba (17) mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi na watumishi wawili (2) mafunzo ya muda mrefu nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeandaa na kuendesha vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi ili kuimarisha Utawala Bora na ushirikishwaji watumishi sehemu za kazi. Aidha, watumishi 32 waliostahili wamepandishwa vyeo na watumishi 32 kwa kuzingatia miundo ya kada zao, Sera ya Menejimenti na Ajira

Nakala ya Mtando (Online Document)

katika Utumishi wa Umma, toleo la mwaka 1999 na 2008 pamoja na taarifa za Upimaji Kazi wa Wazi (OPRAS).

Mheshimiwa Spika, mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2014/2015, Wizara yangu kupitia Idara za Kisekta za Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo pamoja na Asasi chini ya sekta hizo imejipanga kutekeleza majukumu yake kama ilivyoainishwa kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 32 hadi ukurasa wa 42 kwa rejea na ufahamu wa kina.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; Wizara itaendelea kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika Sekta inazosismamia ili ziweze kuchangia zaidi katika maendeleo ya nchi yetu katika kuongeza ajira, kipato, kulinda mazingira, kudumisha amani na mshikamano katika jamii. Wizara itaendelea kukabiliana na changamoto zilizoainishwa katika hotuba hii ili zipatiwe ufumbuzi ili fursa zinazopatikana katika Sekta za Wizara ziweze kutumika ipasavyo katika kuleta maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikisha wananchi kwamba, Wizara ina nia thabiti ya kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizopo hatua kwa hatua kwa kushirikiana na Wizara mbalimbali na wadau mbalimbali wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani za dhati kwa wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 katika kutimiza malengo yetu. Ushirikiano huu utaendelezwa na kuimarishwa zaidi kwa manufaa ya Taifa ili kuhakikisha kuwa umma wa Watanzania unapata taarifa za kina na za uhakika na za ukweli. Vijana wanaendelea kujitambua, kujajiri na kuajirika, maadili na utamaduni wa Mtanzania unazingatiwa, pamoja na kuwa Taifa lenye afya na ufanisi kupitia michezo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yamewezekana kutohana na ushirikiano uliopo mionganoni mwa viongozi na watumishi wa Wizara na wadau wengine walio nje ya Wizara. (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu za pekee ziende kwa Mheshimiwa Alhaj Juma Suleiman Nkamia, Mbunge, Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ambaye amekuwa msaada mkubwa kwangu. Bibi Sihaba Nkinga, Katibu Mkuu; na Prof. Elisante Ole Gabriel, Naibu Katibu Mkuu. Ninawashukuru kwa uchapakazi wao mahiri na ushirikiano mkubwa walionipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Watendaji Wakuu wa Asasi, Wataalam na Watumishi wote wa Wizara kwa

Nakala ya Mtando (Online Document)

juhudii walizofanya kuhakikisha kwamba tunatimiza ipasavyo majukumu tulyokabidhiwa na Taifa. Nawashukuru pia familia yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Bodii za Asasi zilizo chini ya Wizara kwa jinsi wanavyofanya kazi kwa kushirikiana na Wizara. Asasi hizo zimefanya kazi kwa karibu sana na mimi na nawaomba waendelee kufanya kazi kwa uadilifu na weledi mkubwa ili kuhakikisha Wizara yetu inafikia malengo yake.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa nitumie fursa hii tena kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo ambaao wametuunga mkono wakati wote na kutekeleza majukumu ya Wizara nikitarajia kuwa wataendelea na moyo huo. Siyo rahisi kuwataja wote, lakini nitaje wachache ambaao ni Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Finland, Uingereza, Denmark, Japan, Sweden, Norway, Iran, Cuba, Ethiopia, New Zealand, Turkey, Korea ya Kusini, Marekani, Ujerumani pamoja na Mashirika ya Kimataifa ya UNESCO, UNICEF, UNFPA, IYF, UNDP, ILO, Forum - SYD, BRAC, Balton Tanzania Limited, JICA, CYP, ESAMI, RALEIGH INTERNATIONAL, VSO, AMREF, Restless Development and BRITISH COUNCIL. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, napenda kuvishukuru sana vyombo vyote vya habari nchini ambavyo vimefanya kazi nzuri ya kutoa habari, kuelimisha na kuburudisha umma. Naamini kwamba vyombo hivyo vitaendelea na kazi hiyo kwa kuzingatia maadili na weledi. Aidha, nimshukuru sana Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha hotuba hii kwa wakati, bila kuvisahau vituo vya Televisheni na Redio ambavyo kwa namna ya pekee vinarusha hotuba hii hewani moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Mapato, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni moja, milioni mia arobaini na tisa na nane elfu (1,149,008,000) kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara imetengewa jumla ya shilingi bilioni ishirini milioni mia tatu sabini na moja mia nane arobaini na nne elfu (20,371,844,000) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo Matumizi Mengineyo shilingi bilioni tisa milioni mia tatu sabini mia tisa ishirini elfu (9,370,920,000) na Mishahara shilingi bilioni kumi na moja na mia tisa ishirini na nne elfu (11,000,924,000) na Miradi ya Maendeleo shilingi bilioni kumi na tano (15,000,000,000).

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Maombi ya Fedha kwa Ajili ya Kutekeleza Mpango wa Mwaka 2014/2015. Ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka wa fedha 2014/2015, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya jumla ya shilingi bilioni thelathini na tano milioni mia tatu sabini na moja mia nane arobaini na nne elfu (35,371,844,000) ambapo kati ya hizo, fedha za Matumizi ya Kawaida ni shilingi bilioni ishirini, milioni mia tatu sabini na moja, mia nane arobaini na nne elfu (20,371,844,000) na Fedha za Miradi ya Maendeleo ni shilingi bilioni kumi na tano (15,000,000,000). Mchanganuo wa fedha hizi upo katika viambatisho viliviyotajwa hapo awali ambavyo ni sehemu ya Hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante sana, hoja hiyo imeungwa mkono.

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2014/2015 Kama Ilivyowasilishwa Mezani

**HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO, MHE.
DKT. FENELLA E. MUKANGARA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2014/2015**

A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo kwenye Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii sasa naomba kutoa hoja ya kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Asasi zake kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.
2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunilinda na kunipa nguvu ya kutekeleza majukumu yangu na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha bajeti hii.
3. **Mheshimiwa Spika**, kwa heshima na taadhima nitumie fursa hii kuwapongeza Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano

Nakala ya Mtando (Online Document)

wa Tanzania na Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wao thabiti ambao umeendelea kudumisha amani na mshikamano wa Taifa letu. Tunajivunia pia matunda ya Waasisi wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao mwaka 2014 umetimiza miaka 50. Uongozi wao umetuwezesha kufikia maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa tuliyonayo hivi sasa.

4. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Makamu wa Rais, Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal na Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Peter Pinda (Mb.), kwa kazi nzuri wanazozifanya za ujenzi wa nchi yetu. Aidha, nikushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, Mhe. Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mnaonipa ambao unaniwezesha kutekeleza kikamilifu majukumu niliyokabidhiwa ya kulitumikia Taifa letu.
5. **Mheshimiwa Spika**, katika maandalizi ya hotuba hii, Wizara imezingatia maudhui yaliyotolewa katika Bunge lako Tukufu kupitia Hotuba ya Mhe. Mizengo Peter Pinda (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, hotuba yangu imezingatia pia maelekezo na malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2014/2015.
6. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na mabadiliko ya uongozi yaliyotokea, natumia fursa hii kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali.
7. **Mheshimiwa Spika**, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wa Bunge Maalumu la Katiba kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kujadili, kuchambua na kuboresha Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni matumaini yangu kuwa baada ya kukamilika wananchi watapata fursa ya kupiga kura za maoni kama ilivyopangwa ili Taifa letu liweze kupata Katiba Mpya iliyo bora.
8. **Mheshimiwa Spika**, kipekee napenda kuwapongeza wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuishauri Wizara katika maeneo mbalimbali. Wizara itaendelea kuzingatia na kutekeleza ushauri unaotolewa. Shukrani na pongezi zangu ziende kwa viongozi wapya waliochaguliwa kuongoza Kamati hii yaani, Mwenyekiti wa Kamati, Mhe. Saidi Mtanda (Mb.) na Makamu Mwenyekiti, Mhe. John Damiano Komba (Mb.). Nawapongeza pia wajumbe walioteuliwa kuunda Kamati hii. Ushauri wao ndio umefanikisha maandalizi ya hotuba hii.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

9. **Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru aliyejekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mhe. Jenista Joachim Mhagama (Mb.), kwa kazi nzuri aliyoifanya katika Kamati hii.
10. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa pongezi kwa Wabunge wapya waliochaguliwa hivi karibuni kwa ushindi wa kishindo ambaao ni Mhe. Yusuf Salim Hussein, (Mbunge wa Chambani), Godfrey William Mgimwa, (Mbunge wa Jimbo la Kalenga) na Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, (Mbunge wa Jimbo la Chalinze).
11. **Mheshimiwa Spika**, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawapongeza wanahabari pamoja na wadau wote wa sekta ya habari kwa kazi nzuri ya kutoa habari na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kuuelimisha umma wa Watanzania. Aidha, napenda kutambua mchango mkubwa wa vijana wote katika kuinua uchumi kwa kuwa wao ni takriban asilimia 70 ya nguvu kazi ya Taifa letu. Vilevile, niwapongeze wanamichezo wote ambaao wameshiriki katika kuliletea heshima taifa kupitia mashindano ya michezo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kwa namna ya pekee nachukua fursa hii, kutoa pongezi za dhati kwa Timu ya Mpira wa Miguu ya Watoto wanaoishi katika mazingira magumu kutoka Mkoa wa Mwanza iliyotwaa Kombe la Dunia la Watoto wa Mitaani nchini Brazili. Hali kadhalika nawapongeza kwa dhati kabisa wasanii wote ambaao wamekuwa kioo cha jamii katika kulitangaza taifa letu ndani na nje ya nchi yetu. Nawapongeza hasa kwa jinsi walivyoshiriki kikamilifu katika kuhamasisha jamii kushiriki katika Maadhimisho ya Miaka 50 ya Muungano wa Tanzania.
12. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia nafasi hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia na wananchi wa Jimbo la Kalenga na Jimbo la Chalinze kwa kuondokewa na Wabunge wao, Marehemu William Augustao Mgimwa aliyejekuwa Waziri wa Fedha, ambaye alifariki tarehe 01 Januari 2014 nchini Afrika Kusini na Marehemu Said Ramadhani Bwanamdogo aliyesfariki tarehe 22 Januari 2014. Aidha, ninawapa pole Watanzania wote waliopoteza ndugu zao kutokana na ajali, majanga na maradhi mbalimbali. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amina!
13. **Mheshimiwa Spika**, hotuba yangu imegawanyika katika maeneo makuu matano kama ifuatavyo: eneo la kwanza ni Utangulizi, eneo la pili ni Majukumu ya Wizara, eneo la tatu linahusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2013/2014, eneo la nne linahusu Mpango na Bajeti kwa mwaka 2014/2015 na eneo la tano ni Hitimisho.

B. MAJUKUMU YA WIZARA

14. Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza majukumu ya msingi yafuatayo:-

- i) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera za Sekta za Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo;
- ii) Kuratibu na kusimamia masuala ya maendeleo ya vijana ili kuwawezesha kujajiri, kuajirika na kujitegemea;
- iii) Kuwa Msemaji Mkuu wa Serikali na kusimamia vyombo vya habari nchini;
- iv) Kuratibu na kusimamia maendeleo ya utamaduni nchini;
- v) Kuratibu na kusimamia maendeleo ya michezo nchini;
- vi) Kusimamia utendaji kazi wa Asasi, miradi na programu zilizo chini ya Wizara na
- vii) Kuendeleza, kuwezesha na kuratibu masuala ya kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara.

C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mapato na Matumizi

15. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ilipanga kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi **882,203,000** kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2014 jumla ya Shilingi **663,029,569** zilikusanywa ambazo ni sawa na asilimia 75 ya lengo la makusanyo kwa mwaka. Mchanganuo wa makusanyo upo kwenye **Kiambatisho Na. I.**

16. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ilitengewa jumla ya Shilingi **17,628,045,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizo zilijumuisha Mishahara shilingi **9,257,125,000** (Wizara ni Shilingi **2,617,598,000** na Asasi ni Shilingi **6,639,527,000**). Matumizi Mengineyo (OC) shilingi **8,370,920,000** (Wizara ni Shilingi **4,941,920,000** na Asasi ni Shilingi **3,429,000,000**). Hadi mwezi Aprili, 2014 jumla ya Shilingi **13,292,539,498** za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na kutumika ambapo kati ya fedha hizo Matumizi Mengineyo ni Shilingi **4,740,957,000** na Mishahara ni Shilingi **8,551,582,498**.

Miradi ya Maendeleo

Nakala ya Mtandao (Online Document)

17. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ilitengewa jumla ya **Shilingi 12,700,000,000** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2014 jumla ya **Shilingi 4,327,500,000** zilipokelewa ambazo ni sawa na asilimia 34 na Shilingi **2,310,021,000** zilitumika. Miradi iliyotekelawa ni pamoja na Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Ujenzi wa Ofisi - BAKITA, Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

SEKTA YA HABARI

18. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea na utendaji wa kazi zake huku ikikabiliana na changamoto mbalimbali. Miongoni mwa changamoto hizo ni baadhi ya vyombo vya habari kukiuka sheria kwa kuandika na kutangaza habari ambazo hazingatii kanuni na maadili ya taaluma ya uandishi wa habari. Aidha, kuongezeka kwa mifumo na njia za mawasiliano kama mitando ya kijamii kwenye "internet" kumeathiri maudhui ya habari zinazotolewa.

19. Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo, Wizara imechukua hatua mbalimbali za kukabiliana nazo, zikiwemo kutoa onyo na kufungia baadhi ya vyombo vya habari vilivyokiuka maadili. Wizara pia imeelekeza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kutekeleza kikamilifu mpango wa kusajili wamiliki wote wa mitando hiyo. Vilevile, Wizara inaendelea kutoa elimu na kuwaelekeza wamiliki na wahariri wa vyombo vya habari kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyowekwa.

20. Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara imekamilisha maandalizi ya Muswada wa Sheria ya kusimamia Vyombo vya Habari na sasa uko katika hatua nzuri. Kwa kuzingatia utaratibu uliopo, Muswada huu utafikishwa katika Bunge lako Tukufu lijalo la kutunga Sheria.

21. Mheshimiwa Spika, ili kuweza kuimarisha njia za mawasiliano kati ya Serikali na Wananchi wake, Wizara inafanya maboresho ya Tovuti ya Wananchi ili kuweza kuimarisha mifumo na monekano wa Tovuti hiyo. Maboresho hayo yakikamilika, yatawawezesha Wananchi popote walipo kuwasiliana na Serikali kwa kutumia njia za kisasa. Aidha itawapunguzia wananchi ghamama za kuwasilisha kero, hoja na maoni mbalimbali katika Taasisi za Serikali. Kazi ya kuijenga upya na kuimarisha Tovuti hiyo ili kuwa na muonekano mpya unaokidhi mabadiliko ya sasa ya Sayansi na Teknolojia inatarajiwa kukamilishwa mwisho wa mwaka wa fedha 2013/2014.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

- 22. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kukusanya habari, kupiga picha za matukio mbalimbali ya Serikali na kuzihifadhi katika maktaba; pamoja na kuzisambaza kwenye vyombo mbalimbali vya habari kwa lengo la kutoa habari na kuelimisha jamii. Wizara kama Msemaji Mkuu wa Serikali, ilifafanua masuala na hoja mbalimbali zinazohusu Serikali.
- 23. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia Vitengo vya Mawasiliano Serikalini kwa lengo la kutoa habari na kuelimisha umma juu ya utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Wizara imetoea mwongozo ulioainisha taratibu za kuendesha Vitengo hivyo na kuhimiza Wizara na Asasi zote za umma kuajiri Maafisa Mawasiliano Serikalini. Hali kadhalika, Wizara imeratibu jumla ya mikutano 255 ya wasemaji wa Asasi za Serikali na Vyombo vya Habari. Mikutano hii imesaidia kuwaelimisha Wananchi kuhusu shughuli za Serikali zinazofanyika kwa maendeleo yao.
- 24. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa vyombo vya habari katika vikao vya Bunge vilivyofanyika Dodoma na pia kuhakikisha inawapatia vitambulisho waandishi wa habari wa ndani na nje wenye sifa za taaluma ya uandishi wa habari.
- 25. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kupitia TCRA, ilikamilisha awamu ya kwanza ya uhamaji wa kutoka katika mfumo wa utangazaji wa analogi kwenda dijiti. Baada ya zoezi hili tathmini imefanyika ambayo ilionesha mwitikio mzuri wenye mafanikio. Hivi sasa zoezi hili limeingia katika awamu ya pili iliyoanza tarehe 31 Machi 2014. Ni matarajio yetu kwamba uhamaji huu utakamilika kwa kuzingatia ratiba iliyopangwa kabla ya tarehe 30, Juni 2015.
- 26. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na TCRA imesajili vituo nane (8) vya redio na vituo viwili (2) vya televisheni na hivyo kuwezesha Tanzania kuwa na jumla ya vituo **93 vya redio na 28 vya televisheni**. Aidha uhamaji kutoka mfumo wa utangazaji wa analogi kwenda mfumo wa dijiti umesadia kupanua wigo wa masafa na kuongeza ubora wa matangazo.
- 27. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Kamati ya Maudhui ilipokea na kushughulikia malalamiko 7 ya vituo vya televisheni na redio kutokana na kurusha vipindi ambavyo vilikiuka maadili ya utangazaji. Kituo binafsi cha televisheni kilicholalamikiwa kwa kurusha kipindi kilichokiuka kanuni na maadili ya utangazaji kilipewa onyo. Aidha, vituo 6 vya redio vilivyalalamikiwa kwa kurusha vipindi vilivyokiuka kanuni za utangazaji na maadili ya uandishi wa habari vilipewa onyo na vingine kutozwa faini kati ya Shilingi 200,000 na Shilingi 5,000,000.

- 28. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, TBC imeendelea kuimarisha upanuzi wa usikivu wa Redio na Televisheni ya Taifa. TBC pia ilirusha matangazo ya vikao vya Bunge moja kwa moja. Aidha, TBC ilirusha matangazo ya Bunge Maalum la Katiba kwa lugha za alama kwa ajili ya watu wenyewe mahitaji maalum. Pamoja na kazi hizo, TBC inakabiliwa na tatizo la uchakavu wa vifaa vya kurushia matangazo. Uchakavu huo wakati mwingine umesababisha tatizo la kukatika kwa matangazo yakiwemo matangazo ya Bunge.
- 29. Mheshimiwa Spika**, naomba waheshimiwa wabunge wawe wavumilivu kwani Wizara imejipanga katika kuendelea kutatua changamoto hizo ili kuboresha huduma zitolewazo na TBC. Kupitia Bunge lako Tukufu niwaombe Waheshimiwa Wabunge watuunge mkono kufanikisha malengo tuliojivekea.
- 30. Mheshimiwa Spika**, katika kuendelea kutatua changamoto za TBC, mwezi Aprili, 2014 imepokea gari jipya la kisasa la matangazo kutoka Serikali ya Watu wa China. Gari hili litasaidia sana kuongeza nguvu katika kupunguza tatizo la uchakavu wa vifaa. Sambamba na hatua hizo, Wataalamu watano (5) wa TBC walipelekwa nchini China kupata mafunzo maalum ya namna ya kutumia gari hilo pamoja na vifaa husika.
- 31. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) imeendelea na mkakati wa upanuzi wa kiwanda cha uchapaji. Katika mkakati huo, makubaliano na Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB) yamekamilika ambapo TIB itaipatia TSN mkopo wa Shilingi bilioni 2.7 kwa ajili ya kujenga jengo la kitega uchumi.
- 32. Mheshimiwa Spika**, katika kupanua wigo wa mapato, TSN na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) wameingia mkataba wa ubia wa kuendeleza kiwanja kilichopo Kitalu Na. 27, Central Business Park, Dodoma, kwa ajili ya kujenga jengo la kupangisha. Maandalizi ya ujenzi yameanza.
- 33. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha magazeti, TSN imeongeza kurasa za habari katika magazeti ya 'Daily News' na Habari Leo. Vilevile, imeongeza weledi katika uhariri wa taarifa ndani ya magazeti hayo. Uchapaji wa magazeti hayo unazingatia sera na maadili ya uandishi wa habari.
- 34. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha usambazaji wa magazeti, Kampuni imepata pikipiki 20 toka Serikali ya Watu wa China kwa ajili ya usambazaji wa mijini. Aidha, TSN, imeingia makubaliano na kampuni za usafirishaji kusafirisha

Nakala ya Mtandao (Online Document)

magazeti ndani na nje ya nchi ili kuwezesha upatikanaji wa habari kwa wakati.

SEKTA YA MAENDELEO YA VIJANA

35. **Mheshimiwa Spika**, katika kushughulikia masuala ya vijana mwaka 2013/2014, Wizara imekabiliana na changamoto mbalimbali zikiwemo, baadhi ya Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya kutokuajiri Maafisa Vijana, uelewa mdogo wa vijana katika kubuni, kutayarisha maandiko ya miradi, kuanzisha na kutekeleza miradi endelevu.
36. **Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine ni vijana wengi kukosa ujuzi na maarifa ya ujasiriamali na biashara ikiwa ni pamoja na kukosa ujuzi wa matumizi sahihi ya fedha za mikopo wanazopata kuititia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.
37. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto hizi, Wizara imeendelea kuwajengea vijana uwezo wa kiuchumi kwa kuwapa mafunzo na ujuzi katika maeneo ya ujasiriamali, uanzishaji wa miradi endelevu ya uzalishaji mali, uongozi, stadi za maisha na matumizi sahihi ya mikopo. Mafunzo haya yametolewa kwa vijana **668** katika ngazi ya Mikoa na Wilaya katika mwaka wa fedha 2013/2014.
38. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na kupungua kwa nafasi za ajira katika sekta rasmi ikilinganishwa na idadi ya vijana wanaoingia katika soko la ajira kila mwaka, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya vijana imeendelea kuhamasisha vijana kuunda makampuni binafsi ya biashara na vikundi vya kuzalisha mali ili waweze kujajiri. Mpango huu utasaidia kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana.
39. **Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha na kuongeza mitaji katika miradi na kampuni za vijana zinazoanzishwa, Wizara imeratibu mpango wa kuanzisha Benki ya Vijana na tayari Mshauri Mwelekezi amepatikana. Mshauri huyo anaendelea na upembuzi yakinifu wa uanzishwaji wa Benki hiyo.
40. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Mfuko wa Maendelo ya Vijana, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba mwongozo wa kusimamia Mfuko huu umeandaliwa na kusambazwa kwa Makatibu Tawala wa Mikoa yote tangu mwezi Agosti 2013. Kulingana na Mwongozo huu, kila Halmashauri inahitajika kuanzisha SACCOS ya Vijana ambayo itashughulikia utoaji wa mikopo hii. Hadi kufikia Aprili, 2014, Halmashauri 22 kati ya 151 zimeanzisha SACCOS za Vijana.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

- 41. Mheshimiwa Spika**, jumla ya Shilingi bilioni 6.1 zilitengwa kwa ajili ya Mfuko huu. Hadi Aprili, 2014, Wizara imepokea kiasi cha Shilingi **2,000,000,000**. Kati ya fedha hizo zilizokopeshwa ni Shilingi **172,609,000** kwa Miradi ya vikundi vya vijana 25. Hata hivyo, Wizara inaendelea na uchambuzi wa maombi ya vikundi 1,178 yenye thamani ya Shilingi **8,421,906,750** ili kuweza kuvikopesha vikundi vitakavyotimiza vigezo vilivyobainishwa kwenye mwongozo.
- 42. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya "Elimu ya Stadi za Maisha kwa vijana walio nje ya shule". Katika kipindi hiki, Wizara imeandaa mafunzo kwa waelimishaji 75 wa kitaifa ambao watatoa mafunzo kwa waelimishaji rika kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Kata. Programu hii itawasaidia vijana kujitambua na kufanya maamuzi sahihi yanayohusu maisha yao.
- 43. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhamasisha maendeleo ya wananchi, kudumisha umaja, amani, upendo na mshikamano wa kitaifa kupitia Mbio za Mwenge wa Uhuru. Kwa mwaka 2013, Mbio za Mwenge wa Uhuru zilizinduliwa tarehe 5 Mei, 2013 katika kijiji cha Chokocho, Mkoani Kusini Pemba ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Maadhimisho ya kilele cha mbio hizo yalifanyika mkoani Iringa tarehe 14, Oktoba, 2013 na Mgeni Rasmi alikuwa Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia mbio hizo, jumla ya miradi ya maendeleo **1229** yenye thamani ya Sh. **158,587,667,613.40** ilizinduliwa au kuwekewa mawe ya msingi. Uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2014 umefanyika tarehe 2, Mei 2014 Mkoani Kagera; na Mgeni Rasmi alikuwa Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- 44. Mheshimiwa Spika**, sambamba na maadhimisho ya kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru, Wizara iliratibu maadhimisho ya Wiki ya Vijana kitaifa ambayo yalianza tarehe 8 Oktoba na kuhitimishwa tarehe 14 Oktoba, 2013 mkoani Iringa. Lengo la maadhimisho hayo ni kuwakutanisha vijana kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini na kuwapa fursa ya kubadilishana uzoefu, ujuzi, kuonesha vipaji na ubunifu wa kazi zao, pamoja na kujenga mtandao na wadau mbalimbali wa maendeleo ya vijana.
- 45. Mheshimiwa Spika**, Maonesho katika Wiki ya Vijana yalishirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na ofisi za mikoa 10, Idara za Serikali 16, Halmashauri za Wilaya 21, Asasi za Kiraia 14, Vikundi vya Vijana Wajasiriamali 53, Vyuo Vikuu vya Elimu 3 na Taasisi za Kibenki 3. Jumla ya watu waliotembelea mabanda ya maonesho ya Wiki ya Vijana ilikuwa ni 39,361. Aidha, katika Wiki hiyo, Vijana 300 kutoka makundi mbalimbali ya Vijana walishiriki katika midahalo ambapo pia walipatiwa mafunzo ya aina tofauti

Nakala ya Mtandao (Online Document)

yenye lengo la kuwajengea uelewa wa masuala mbalimbali ya maendeleo ya vijana.

46. Mheshimiwa Spika, washiriki wa Wiki ya Vijana pia walipata fursa ya kupewa huduma ya ushauri nasaha na upimaji wa VVU/UKIMWI kwa hiari kupitia taasisi zinazojihusisha na afya zilizoshiriki katika maadhisho hayo, kama vile WAMATA, AMREF – ANGAZA, HOSPITALI YA RUFAA IRINGA na JHPIEGO - UHAI CT. Jumla ya Vijana 613 walipima afya zao wakiwemo wanawake 397 na wanaume 216, kati yao vijana 27 sawa na asilimia 4.4 waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU. Vijana waliogundulika kuwa na maambukizi walipatiwa huduma ya ushauri wa namna ya kuishi vizuri na kwa matumaini na jinsi ya kuendelea kupata huduma za afya.

SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

47. Mheshimiwa Spika, athari za utandawazi na maendeleo yenye kasi kubwa ya sayansi na teknolojia vimeendelea kuwa ni changamoto kubwa inayokabili Maendeleo ya Utamaduni. Mmomonyoko wa maadili ulio dhahiri nchini, sio tu mionganoni mwa watoto na vijana bali pia hata baadhi ya watu wazima, ni matokeo ya athari hasi za utandawazi na maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia yanayoambatana na matumizi mapana ya televisheni na mitandao anuwai ya kijamii. Kwa upande mwingine, upatikanaji kirahisi wa mitambo ya kurudufu kazi za wasanii, hasa wa filamu na muziki, umeendeleza dhuluma ya kipato kwa wasanii wengi huku ukiwaneemesha mapromota na wasambazaji wa bidhaa za filamu na muziki ambao sio wasanii.

Pamoja na changamoto hizi, Wizara kupitia Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni imetekeleza kazi zifuatazo katika mwaka wa fedha wa 2013/2014.

48. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ukusanyaji na uhifadhi wa takwimu za tasnia ya utamaduni, Maofisa wawili walipata mafunzo ya namna ya kuainisha namba za misimbo (code numbers) za sekta ya utamaduni ambazo zitatumika kitaifa na kimataifa. Aidha, Wizara ilifanya tafiti za maktabani za lugha za jamii 10 na utafiti wa uwandani katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ili kuhifadhi sarufi, misamiati na istilahi za lugha ya Taifa - Kiswahili.

49. Mheshimiwa Spika, mintaarafu utafiti wa mila na desturi, Wizara ilifanya utafiti wa kina kuhusu mila za jando na unyago mionganoni mwa jamii za Wamakonde, Wamakua na Wayao. Utafiti huo umewezeesa kukamilisha maandalizi ya pendekezo la elementi ya urithi usioshikika ambao hatimaye Serikali itaomba urithi huo uingizwe kwenye orodha ya urithi wa utamaduni

Nakala ya Mtandao (Online Document)

wa Dunia unaotambuliwa na UNESCO. Elementi hiyo ni ya ngoma ya "Nankachanga" kutoka kijiji cha Namahonga, Wilaya ya Tandahimba, Mkoa wa Mtwara.

- 50. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa Tanzania inanufaika ipasavyo na fursa za ajira zinazotokana na nchi yetu kuteuliwa kuwa Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika hili, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, iliratibu zoezi la kuwapata Watanzania wenyewe sifa stahiki za kuajirika katika Kamisheni hiyo. Ajira katika Kamisheni zitashindaniwa na nchi zote wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, hivyo ni muhimu kwa Tanzania kuwa na wagombea sadifu ili kuhimili vishindo vya kinyang'anyiro hicho.
- 51. Mheshimiwa Spika**, kuhusiana na Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, kazi ya ukusanyaji wa kumbukumbu za mapambano ya kupigania uhuru nchini iliendelea kufanya kwa kushirikiana na Maofisa Utamaduni wa Mikoa na Wilaya. Kwa kipindi cha mwaka 2013/2014, jumla ya kumbukumbu 63 zimerekodiwa katika kanzi data ya Programu. Programu hii ni muhimu sana katika kutunza na kuhifadhi kumbukumbu za Ukombozi wa Bara la Afrika. Wizara inaendelea kutafuta ufadhilli kufanikisha malengo ya Programu.
- 52. Mheshimiwa Spika**, Wizara ilifanya kikao cha Makatibu Wakuu wa Wizara ambazo ni wadau wakuu ili kujenga uelewa zaidi wa Programu. Aidha, washirika katika Programu hii kutoka Namibia, Afrika Kusini na Msambiji walikuja nchini kujifunza namna Tanzania inavyotekeleza shughuli za uhifadhi na utunzaji wa kumbukumbu za historia ya Ukombozi wa Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika.
- 53. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2013/2014, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) liliandaa na kurusha vipindi 52 vya '**Lugha ya Taifa**' kuititia TBC Taifa, vipindi 52 vya '**Kumepambazuka**' kuititia Radio One na vipindi 52 vya '**Ulimwengu wa Kiswahili**' kuititia Televisheni ya Taifa-TBC1. Vilevile, Baraza liliisoma jumla ya miswada 24 ya vitabu vya taaluma na kuvipatia ithibati ya lugha.
- 54. Mheshimiwa Spika**, Baraza limeratibu na kutoa huduma ya tafsiri kwa Asasi 14 za Serikali, Mashirika ya Umma, pamoja na watu binafsi. Aidha, huduma ya ukalimani ilitolewa kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika huko Addis Ababa, Ethiopia, mwezi Julai, 2013 na mwezi

Nakala ya Mtando (Online Document)

Januari, 2014. Vilevile, ukalimani ulifanyika kwenye Mkutano wa Bunge la Afrika nchini Afrika Kusini mwezi Novemba, 2013 na Machi, 2014.

- 55. Mheshimiwa Spika**, Baraza limeendelea kufuatilia matumizi ya Kiswahili na kubaini jumla ya makosa 75 yaliyofanywa na vyombo vya habari na watumiaji wengine wa Kiswahili kwa kusahihisha na kutoa ushauri wa matumizi stahiki. Baraza katika kuijimarisha, limeongeza wigo wa kiutendaji kwa kuandaa Kamusi Kuu ambapo fafanuzi za maneno (utomeshaji) zimeingizwa na warsha tatu za kuhakiki zimefanyika.
- 56. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) limeendesha midahalo 52 ya Jukwaa la Sanaa kwa wasanii, waandishi wa habari na wadau wa sanaa 3,850. Vilevile, Baraza kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sanaa, limeendesha mafunzo ya utambaji wa hadithi, ngoma za asili kwa watoto 200 wa shule za msingi katika Mkoa wa Dar es Salaam kati ya Februari na Machi, 2014 kwa lengo la kuibua na kuendeleza vipaji vyao katika fani husika.
- 57. Mheshimiwa Spika**, Baraza limeendesha mafunzo na kuhamasisha watumishi 34 wa Baraza, wasanii na wadau 98 kuititia Jukwaa la Sanaa kuhusu umuhimu wa kujikinga na maambukizi ya VVU na UKIMWI. Baraza limeendelea kuingiza taarifa muhimu za wasanii na wadau wa sanaa za muziki katika mfumo wa kielektroniki unaouunganisha Taasisi za TRA, COSOTA, Bodi ya Filamu na BASATA. Hii itaimarisha urasimishaji wa tasnia ya muziki. Aidha, Baraza limeendelea na hatua za awali za uandaaji wa mfumo wa kanzi data za wasanii mahiri na kukusanya taarifa zao muhimu.
- 58. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Bodi ya Filamu imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza pamoja na Kanuni zake. Bodi, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), imeendelea kuhimiza matumizi ya stempu za kodi. Hadi sasa, jumla ya wadau 86 wamechukua Stempu 4,380,000 zilizotolewa kwa upacha (duplicate) kwa ajili ya kuweka kwenye kazi za filamu na muziki. Kati ya hizo 3,810,000 ni kwa kazi za filamu na 570,000 ni za muziki.
- 59. Mheshimiwa Spika**, Bodi imepitia miswada 139 ya kutengenezea filamu kwa watengenezaji wa ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia Aprili, 2014, jumla ya filamu 1,206 sawa na CD 2,412 zilikaguliwa na kuwekewa madaraja. Kati ya filamu hizo, 127 zilifanyiwa marekebisho. Filamu 7 hazikuruhusiwa kuonyeshwa hadharani. Aidha, kati ya filamu 215 za nje zilizowasilishwa, filamu 2 zilielekezwa kufanyiwa marekebisho. Jumla ya filamu 5 za nje zilizowasilishwa zilizuiliwa kuonyeshwa hadharani. Aidha, Bodi imekagua na kuidhinisha maeneo 13 ya uzalishaji wa filamu.

- 60. Mheshimiwa Spika**, Bodi imeendelea kutoa elimu kuhusu urasimishaji wa tasnia ya filamu kupitia matangazo kwenye magazeti, vipeperushi, mabango ya barabarani, maadhimisho na sherehe mbalimbali, vipindi mbalimbali vya TV na Redio na vikao vya wadau.
- 61. Mheshimiwa Spika**, Bodi ilihamasisha wadau kushiriki katika tuzo mbalimbali za filamu kitaifa na kimataifa ambapo hadi kufikia Aprili 2014, jumla ya filamu 10 ziliingia katika tuzo mbalimbali na filamu ya Mdundiko ya Kitanzania ilishinda katika tuzo ya kimataifa huko Marekani.
- 62. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) iliendesha mafunzo ya stashahada kwa wanachuo wapatao 238 na mafunzo ya muda mfupi kwa wasanii 255 walio kazini. Vilevile, inaendelea na kazi ya kukamilisha mitaala ya shahada ya kwanza ya sanaa za maonyesho na ufundi.
- 63. Mheshimiwa Spika**, TaSUBa ilisimamia na kuendesha tamasha la 32 la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania ambapo vikundi 40 vya sanaa za maonyesho na vikundi 12 vya sanaa za ufundi vya ndani na nje ya nchi vilishiriki. Aidha, TaSUBa ilishiriki mikutano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyoitishwa kujadili mustakabali wa vituo vya Jumuiya vyenye ubora uliotukuka (Centre of Excellence), ambapo TaSUBa ni kimojawapo cha vituo hivyo.

SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO

- 64. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara imeendelea kukabiliana na changamoto mbalimbali zikiwemo uchache wa wataalamu waliobobea katika fani mbalimbali za michezo, upungufu wa miundombinu inayokidhi mahitaji ya sasa, mwamko mdogo wa jamii kushiriki katika michezo na udhaifu wa uongozi katika baadhi ya vyama mbalimbali vya michezo.

Pamoja na changamoto hizo, Wizara katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2013/2014 imetekeleza kazi zifuatazo.

- 65. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Ufundishaji Michezo na Stashahada ya Uongozi na Utawala kwa wanachuo 40 katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo, Malya, mkoani Mwanza. Aidha, Wizara imeendesha Mafunzo ya muda mfupi ya fani mbalimbali za michezo kwa vijana 200, walimu 100 wa shule za Msingi, walimu 100 wa shule za Sekondari, Viongozi wa Michezo na Makocha 102 katika Vituo vya Michezo vya Kanda ya Kaskazini (Arusha) na Kusini (Songea). Hivi sasa zaidi ya asilimia 50 ya walimu ambao hushiriki katika uendeshaji na ufundishaji wa michezo kwa ajili ya mashindano ya shule za

Nakala ya Mtando (Online Document)

msingi (UMITASHUMTA) na shule za sekondari (UMISETA) ni wahitimu wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, Vituo vya Michezo na Mpango wa Michezo kwa Jamii.

- 66. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutafuta maeneo mapya ya ushirikiano wa kimataifa na kufuatilia utekelezaji wa Mikataba kati ya nchi marafiki na Tanzania katika Sekta ya Michezo. Kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Wizara imekamilisha hatua za awali za kujenga miundombinu ya Mchezo wa kupanda Majabali (Rock Climbing) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Aidha, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, Wizara iliendesha Kongamano la Kimataifa la Viongozi Wanawake wa Michezo lilofanyika Dar es Salaam tarehe 16 – 18 Desemba, 2013 na kushirikisha jumla ya nchi 17 za Bara la Afrika na Ulaya.
- 67. Mheshimiwa Spika**, Wizara, kwa kushirikiana na Vyama vya Michezo, imeendelea kufanya maandalizi ya timu za Taifa zitakazoshiriki kwenye michezo ya Jumuiya ya Madola itakayofanyika Glasgow, Scotland, mwezi Julai, 2014. Timu za Michezo ya Riadha, Ngumi, Kuogelea, Mieleka, Baiskeli, Judo, Paralimpiki na Mpira wa Meza zinatarajiwaa kushiriki katika mashindano hayo. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, timu sita za Taifa za mchezo wa Riadha, Ngumi, Kuogelea, Judo, Kunyanya Vitu vizito na Mpira wa Meza zimepata fursa ya kuweka kambi za mazoezi nchini China, Uturuki, Ethiopia na New Zealand kwa ajili ya maandalizi ya michezo ya Jumuiya ya Madola.
- 68. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kusimamia ukamilishaji wa ukarabati wa Uwanja wa Uhuru ambao ni sehemu ya eneo Changamani la Michezo lililoko Dar es Salaam. Ukarabati huu unatarajiwaa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2014.
- 69. Mheshimiwa Spika**, Wizara ilitoa huduma ya Kinga na Tiba kwa wanamichezo na wadau wa michezo 108,000 wa timu za michezo mbalimbali. Vilevile, Wizara imeendelea na upimaji na utoaji wa elimu kwa wanamichezo kuhusu udhibiti wa matumizi ya dawa na mbinu haramu za kuongeza nguvu katika michezo.
- 70. Mheshimiwa Spika**, katika juhudi za kupambana na dawa na mbinu haramu za kuongeza nguvu michezoni, Wizara imeendelea kutumia matukio ya michezo kama vile Ligi Kuu ya Vodacom, Kambi za Timu za Taifa na Mashindano ya Riadha na Ngumi ya Kitaifa na Kimataifa, kuchukua sampuli mbalimbali (damu, mate, jasho n.k) za wanamichezo kwa ajili ya vipimo vya matumizi ya dawa za kuongeza nguvu katika michezo kwa uchunguzi zaidi kwenye maabara zilizoko nchini Afrika Kusini. Hadi kufikia Aprili, 2014

Nakala ya Mtandao (Online Document)

wanamichezo 27 walichukuliwa vipimo. Hata hivyo, hakuna aliyegundulika kutumia dawa na mbinu haramu baada ya majibu ya maabara.

- 71. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Baraza la Michezo la Taifa (BMT), kwa kushirikiana na "UK Sport" na "British Council", kupitia mradi wa "International Inspiration", limekamilisha uandaaji wa mifumo rasmi ya Elimu na Ithibati ya Ufundishaji wa Michezo Nchini; Michezo Shirikishi kwa Jamii; Ufuatiliaji na Tathmini ya Maendeleo ya Michezo Nchini; na Utambuzi na Ukuzaji wa Vipaji vya Michezo Miiongoni mwa Vijana. Mifumo hiyo inalenga kuinua maendeleo ya michezo nchini na inaendelea kufanyiwa majoribio kwa ajili ya utekelezaji.
- 72. Mheshimiwa Spika**, Baraza limeendesa mafunzo ya utawala bora kwa vyama vya michezo 17, na kusimamia uchaguzi kwa vyama na mashirikisho ya michezo 14. Aidha, kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Baraza, limeendesa mafunzo ya michezo kwa jamii kwa walimu 76 wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Mtwara Vijijini.
- 73. Mheshimiwa Spika**, Baraza liliandaa na kuendesha Kongamano la Kimataifa kuhusu Mfumo wa Elimu ya Michezo kwa Jamii kwa Nchi za Kanda ya V ya Michezo Barani Afrika. Kongamano hilo lilikuwa na lengo la kuangalia namna ya kuwa na mfumo mmoja wa utoaji wa Elimu ya Michezo kwa Jamii miiongoni mwa nchi wanachama. Kongamano hilo lilitanyika mwezi Novemba, 2013 huko Arusha na kuhudhuriwa na nchi saba ambazo ni Uganda, Kenya, Rwanda, Ethiopia, Misri, Zimbabwe na Tanzania.
- 74. Mheshimiwa Spika**, Baraza limeendesa mafunzo ya uamuzi na ukocha kwa walimu na wanafunzi 761, kati ya hao walimu ni 421 na wanafunzi ni 340. Mafunzo haya, yaliyo katika majoribio ya mradi wa "International Inspiration" yamefanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Ruvuma, Mwanza na Mjini Magharibi, Zanzibar.
- 75. Mheshimiwa Spika**, Baraza, kwa kushirikiana na Asasi ya Kimataifa ya "Tackle Africa" inayojishughulisha na utoaji wa elimu ya kinga dhidi ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kwa kutumia mchezo wa soka, limeendesa mafunzo kwa wanawake 140 na wasichana 8,000 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Lindi.

UTAWALA NA MENEJIMENTI YA RASILIMALI WATU

- 76. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2013/2014, watumishi 51 wamehudhuria mafunzo katika fani mbalimbali. Kati ya hao, watumishi thelathini na wawili (32), wamehudhuria mafunzo elekezi ambayo

Nakala ya Mtandao (Online Document)

yaliandaliwa na Wizara kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali za Serikali. Aidha, watumishi kumi na saba (17) wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi na watumishi wawili (2) wanahudhuria mafunzo ya muda mrefu nje ya nchi.

77. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha Utawala Bora na ushirikishwaji watumishi sehemu za kazi, Wizara imeandaa na kuendesha vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi pamoja na kusimamia uendeshwaji wa vikao mbalimbali vya kiutawala katika kuimarisha utendaji kazi.

78. Mheshimiwa Spika, katika usimamizi wa haki na maslahi ya watumishi, Wizara imewapandisha vyeo watumishi 32 wanaostahili kwa kuzingatia miundo ya kada zao, Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma toleo la mwaka 1999 na 2008 pamoja na taarifa za Upimaji Kazi wa Wazi (OPRAS).

D: MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014 / 2015

79. Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2014/2015 umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 – 2015/2016; Malengo ya Taifa ya MKUKUTA II; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya mwaka 2010 – 2015; Mpango Mkakati wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo 2011/2012 – 2015/2016; Maagizo ya Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoyatoa kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa nyakati tofauti; Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2014/2015 na ushauri uliotolewa na Bunge pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwa nyakati tofauti.

SEKTA YA HABARI

80. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Kuisemea Serikali katika masuala muhimu yanayohitaji ufanuzi kwa wananchi;
- (ii) Kukusanya habari mbalimbali za matukio ya kiserikali na kuyasambaza kwa wananchi;
- (iii) Kuratibu Vitengo vya Mawasiliano Serikalini;

Nakala ya Mtando (Online Document)

- (iv) Kusajili magazeti na machapisho;
- (v) Kuandaa jarida la Nchi Yetu na kulisambaza;
- (vi) Kuratibu waandishi wa habari katika shughuli za kitaifa na kimataifa na
- (vii) Kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Habari kwa Umma.

81. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) linakusudia:-

- (i) Kurusha matangazo ya vikao vya Bunge;
- (ii) Kulipia huduma ya kukodi "satellite" kwa ajili ya matangazo ya moja kwa moja ya televesheni;
- (iii) Kuhamisha na kujenga mitambo miwili (2) ya FM katika maeneo ya StarMedia (T) Ltd ili kuboresha usikivu wa matangazo ya redio. Maeneo yatakayohusika na zoezi hilo la uhamishaji wa mitambo yake ya FM ni Iringa na Dodoma;
- (iv) Kujenga mtambo mpya mmoja (1) wa FM redio kwa ajili ya kuboresha usikivu wa matangazo katika eneo la Ngorongoro mkoani Arusha na
- (v) Kujenga studio mbili (2) za redio katika Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma pamoja na kufunga vifaa vya kisasa.

82. Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) kwa mwaka 2014/2015 imepanga kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Kukamilisha mradi wa upanuzi wa kiwanda cha uchapaji na
- (ii) Kuendelea na mchakato wa kuendeleza kiwanja kilichopo Kitalu Na. 27, Central Business Park, Dodoma, kwa ubia na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

83. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Wizara kuitia Kamati ya Maudhui ya Utangazaji imepanga kutekeleza yafuatayo:-

Nakala ya Mtando (Online Document)

- (i) Kupitia na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria na Kanuni za Utangazaji;
 - (ii) Kutengeneza rasimu ya kanuni ndogo za maudhui ya Utamaduni wa Mtanzania;
 - (iii) Kutengeneza mwongozo wa udhamini wa matangazo (Codes of Advertising and Sponsorship);
 - (iv) Kuanzisha utaratibu wa kutoa motisha (Incentive scheme) kwa watengenezaji na vituo vya utangazaji vitakavyorusha vipindi vyenye maudhui bora ya Mtanzania;
 - (v) Kuendesha warsha za mashauriano na wadau wa maudhui wa kujitegemea na
 - (vi) Kusimamia awamu ya pili ya uhamaji kutoka mfumo wa analogi kwenda mfumo wa dijiti katika miji yote ambayo haijafikiwa na mfumo huu mpya.
- SEKTA YA MAENDELEO YA VIJANA**

84. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kuratibu mafunzo ya Ujasiriamali; Uanzishaji na Uendeshaji wa Miradi na Kampuni Endelevu, Uongozi na Stadi za Maisha kwa viongozi wa vikundi vya vijana vya uzalishaji mali na asasi za vijana ili kuwajengea uwezo wa kujajiri na kuajirika, hivyo kujikimu kiuchumi na kijamii;
- (ii) Kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru ili kuhamasisha wananchi kudumisha amani, upendo na mshikamano wa kitaifa. Aidha, Wizara itaratibu maadhisho ya Wiki ya Vijana ili kuwapa fursa za kubadilishana uzoefu, ujuzi, kuonesha vipaji na kazi zao za uzalishaji mali, ubunifu pamoja na kuwawezesha kujenga mitando baina yao na wadau mbalimbali;
- (iii) Kuendelea na maandalizi ya uanzishwaji wa Benki ya Vijana ili kuwezesha vijana pamoja na SACCOS za vijana kupata mitaji kwa ajili ya shughuli zao za kiuchumi;

Nakala ya Mtando (Online Document)

- (iv) Kuendelea kuwezesha Vijana kiuchumi kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili waweze kujiajiri wenyewe na hivyo kupunguza tatizo la ajira mionganii mwao na umaskini kwa ujumla na
- (v) Kuimarisha vituo vitatu vya mafunzo ya vijana ili viweze kutumika ipasavyo katika kutoa mafunzo ya ujasiri, ujasiriamali, uongozi na stadi za maisha.

SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

85. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara itatekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kuratibu mjadala wa Kitaifa kuhusu maadili ya Mtanzania;
- (ii) Kukuza na kuendeleza matumizi sanifu na fasaha ya lugha ya Kiswahili na kufanya utafiti wa msamati wa lugha za jamii;
- (iii) Kuratibu mikutano, matamasha ya sanaa na ushiriki wa wasanii katika Sherehe za Kitaifa;
- (iv) Kuratibu utafiti, uhifadhi na uorodheshaji wa urithi wa utamaduni na
- (v) Kuratibu utekelezaji wa miradi ya Ujenzi wa Jumba la Utamaduni na Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika.

86. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) limepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kuandaa na kurusha vipindi 52 vya '**Lugha ya Taifa**' katika TBC Taifa, vipindi 52 vya '**Kumepambazuka**' katika Radio One na vipindi 52 vya '**Ulimwengu wa Kiswahili**' katika Televisheni ya Taifa (TBC1) ili kuhamasisha na kuelimisha matumizi sahihi ya Lugha ya Kiswahili;
- (ii) Kusoma Miswada ya vitabu vya taaluma na kuipatia ithibati ya lugha;
- (iii) Kuratibu na kutoa huduma za tafsiri na ukalimani katika mikutano ya kitaifa na kimataifa, shughuli za mashirika, makampuni na watu binafsi;

Nakala ya Mtando (Online Document)

- (iv) Kuchunguza makosa ya Kiswahili yanayofanywa na vyombo vyaa habari na watumiaji wengine na kufanya masahihisho ya makosa hayo;
- (v) Kuandaa Kamusi Kuu ya Kiswahili Sanifu;
- (vi) Kuchapisha Kitabu cha Furahia Kiswahili (Kiswahili kwa Wageni) na
- (vii) Kukarabati majengo ya ofisi yaliyonunuliwa kutoka Shirika la Bima la Taifa.

87. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) limepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kuendesha mafunzo ya utambaji hadithi, ngoma za asili na uigizaji kwa watoto 200 wa shule za msingi 5 za Mkoa wa Dar es salaam kwa lengo la kuibua na kuendeleza vipaji vyaa watoto katika fani husika;
- (ii) Kuendesha mafunzo ya sanaa na ujasiriamali kwa wasanii 100 katika mkoa wa Tabora;
- (iii) Kuendesha midahalo 30 kwa wasanii, waandishi wa habari na wadau wa sanaa 3,000;
- (iv) Kusajili wasanii na wadau wanaojishughulisha na shughuli za sanaa katika Mikoa ya Dar es salaam, Arusha, Mwanza, Morogoro na Mbeya;
- (v) Kusanifu, kuboresha na kuhifadhi maelezo ya wasanii katika kanzi data ya BASATA;
- (vi) Kutoa elimu ya urasimishaji wa tasnia ya muziki kwa wadau wa sanaa na
- (vii) Kuendelea na ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa sanaa na mafunzo.

88. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, Bodii ya Filamu imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo;

- (i) Kuendelea na Urasimishaji wa Tasnia ya Filamu;
- (ii) Kukagua na kuweka madaraja ya filamu 600;
- (iii) Kupitia miswada 150 ya kutengeneza filamu na kutoa vibali 150 vyaa kutengeneza filamu kwa waombaji wa ndani na nje ya nchi;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(iv) Kuendelea kutoa elimu ya kulinda Maadili ya Mtanzania kupitia tasnia ya filamu na

(v) Kufanya utafiti wa masuala ya filamu na kuendesha mafunzo ya kujenga weledi kwa wadau 150 wa filamu.

89. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kuendesha mafunzo ya stashahada kwa washiriki 250 na mafunzo ya muda mfupi kwa wasanii 270 walio kazini;
- (ii) Kusimamia na kuendesha Tamasha la 33 la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania na
- (iii) Kuboresha studio ya picha jongefu na kununua vifaa vya muziki.

SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO

90. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara itatekeleza yafuatayo:-

- (i) Kuratibu ushiriki wa timu za Taifa kushiriki Michezo ya Jumuiya ya Madola itakayofanyika Glasgow, Scotland, mwezi Julai 2014;
- (ii) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Ufundishaji wa Michezo na Stashahada ya Utawala na Uongozi wa Michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya;
- (iii) Kutoa huduma ya tiba na kinga kwa wanamichezo na kuendelea na juhudzi za kudhibiti matumizi ya dawa na mbinu haramu za kuongeza nguvu katika michezo;
- (iv) Kuendesha mafunzo ya muda mfupi ya fani mbalimbali za michezo kwa wadau 200 katika Vituo vya Michezo vya Kanda ya Kusini (Songea) na Kaskazini (Arusha);
- (v) Kusajili Vyama na Vilabu vya Michezo;
- (vi) Kuimarisha uendeshaji wa michezo shulen na ubora wa mashindano ya UMITASHUMTA na UMISETA kwa kutoa nafasi zaidi kwa walimu wa shule za msingi na sekondari kupata mafunzo ya ufundishaji wa michezo mbalimbali katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, Vituo vya

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Michezo vya Arusha na Songea na fursa nyingine kwa kadri zitakavyopatikana;

- (vii) Kuratibu ukamilishaji wa Uboreshaji wa Uwanja wa Uhuru na
- (viii) Kuratibu uendeshaji wa Uwanja wa Taifa na uboreshaji wa miundombinu katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya.

91. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Baraza la Michezo la Taifa (BMT) litatekeleza yafuatayo:-

- (i) Kuandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa walimu 200 wa michezo kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali za serikali za mitaa kupitia Mpango wa Michezo Jumuishi kwa Jamii “Integrated Community Sports”;
- (ii) Kutoa mafunzo ya Utawala Bora katika Sekta ya Michezo kwa viongozi wa Mashirikisho na Vyama Vya Michezo katika ngazi mbalimbali;
- (iii) Kuratibu na kusimamia chaguzi za Vyama Vitano (5) vya Michezo na
- (iv) Kuhamasisha wadau mbalimbali wa Michezo kushiriki katika majaribio ya kutumia mifumo rasmi ya michezo katika kutekeleza Programu zao za Maendeleo ya Michezo nchini.

UTAWALA NA MENEJIMENTI YA RASILIMALI WATU

92. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa kuzingatia makundi ya kada zao. Mafunzo hayo yatalenga katika kuimarisha utendaji kazi. Aidha, Wizara itatoa elimu ya maadili kwa watumishi ili kuimarisha nidhamu ya kazi;
- (ii) Kuendelea kuhamasisha watumishi kukubali kupimwa UKIMWI ili kutambua hali zao. Aidha, Wizara itaendelea kutoa msaada wa chakula na lishe kwa watumishi wanaoishi na VVU na UKIMWI ambao wamejitokeza;
- (iii) Kuhakikisha watumishi wanaostahili wanapandishwa vyeo kwa kuzingatia miundo ya kada zao, Sera ya Menejimenti katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999 na 2008 pamoja na taarifa za Upimaji Kazi wa Wazi (OPRAS) ; na

Nakala ya Mtando (Online Document)

(iv) Kuendelea kuimarisha utawala bora na ushirikishwaji watumishi sehemu za kazi kwa kuendesha vikao vya Baraza la Wafanyakazi pamoja na vikao vingine vya kiutawala ili kuimarisha utendaji kazi.

E: HITIMISHO

93. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendeleza mafanikio yaliyopatikana katika Sekta inazosimamia ili ziweze kuchangia zaidi katika maendeleo ya nchi yetu. Hii ni pamoja na kuongeza ajira, kipato, kulinda mazingira, kudumisha amani na mshikamano katika jamii. Wizara itaendelea kukabiliana na changamoto zilizoainishwa katika hotuba hii ili zipatiwe ufumbuzi ili fursa zinazopatikana katika Sekta za Wizara ziweze kutumika ipasavyo katika kuleta maendeleo ya nchi. Napenda kuwahakikisha wananchi ya kwamba Wizara ina nia thabiti ya kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizopo hatua kwa hatua kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo.

SHUKRANI

94. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani za dhati kwa wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 katika kutimiza malengo yetu. Ushirikiano huu utaendelezwa na kuimarishwa zaidi kwa manufaa ya Taifa ili kuhakikisha kuwa umma wa Watanzania unapata taarifa za kina na za uhakika, vijana wanaendelea kujajiri na kuajirika, maadili na utamaduni wa Mtanzania unazingatiwa, pamoja na kuwa Taifa lenye ufanisi kupitia michezo. Mafanikio ya utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yamewezekana kutokana na ushirikiano uliopo mionganoni mwa viongozi na watumishi wa Wizara na wadau wengine walio nje ya Wizara.

95. Mheshimiwa Spika, shukrani zangu za pekee ziende kwa **Mhe. Alhaji Juma Suleiman Nkamia** (Mb.), Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ambaye amekuwa msaada mkubwa kwangu, **Bibi Sihaba Nkinga**, Katibu Mkuu na **Prof. Elisante Ole Gabriel**, Naibu Katibu Mkuu. Ninawashukuru kwa uchapakazi wao mahiri na ushirikiano mkubwa walionipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, nawashukuru Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Watendaji Wakuu wa Asasi, Wataalamu na Watumishi wote wa Wizara kwa juhudhi walizofanya kuhakikisha kwamba tunatimiza ipasavyo majukumu tuliyokabidhiwa na Taifa.

96. Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru Wenyeviti na wajumbe wa Bodi za Asasi zilizo chini ya Wizara kwa jinsi wanavyofanya kazi kwa kushirikiana na Wizara. Asasi hizo zimefanya kazi kwa karibu sana na mimi na nawaomba

Nakala ya Mtandao (Online Document)

waendelee kufanya kazi kwa uadilifu na weledi mkubwa ili kuhakikisha Wizara yetu inafikia malengo yake.

97. Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa nitumie fursa hii tena kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo ambao wametuunga mkono wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Wizara. Shukrani hizi ziwaendee wahisani waliotusaidia, nikitarajia kuwa wataendelea na moyo huo. Siyo rahisi kuwataja wote lakini nitaje wachache ambao ni Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Finland, Uingereza, Denmark, Japan, Sweden, Norway, Iran, Cuba, Ethiopia, New Zealand, Turkey, Korea ya Kusini, Marekani na Ujeruman pamoja na Mashirika ya Kimataifa ya UNESCO, UNICEF, UNFPA, IYF, UNDP, ILO, Forum - SYD, BRAC, Balton Tanzania Limited, JICA, CYP, ESAMI, RALEIGH INTERNATIONAL, VSO, AMREF, Restless Development na BRITISH COUNCIL.

98. Mheshimiwa Spika, napenda kuvishukuru vyombo vyote vya habari nchini ambavyo vimefanya kazi nzuri ya kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha umma. Ninaamini kuwa vyombo hivyo vitaendelea na kazi hiyo kwa kuzingatia maadili na weledi. Aidha, ninamshukuru sana Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha hotuba hii kwa wakati, bila kuvisahau vituo vya Televisheni na Redio ambavyo kwa namna ya pekee vinarusha hotuba hii hewani moja kwa moja.

MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mapato

99. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara imepanga kukusanya jumla ya **Shilingi 1,149,008,000** kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Mchanganuo wa makusanyo kifungu kwa kifungu kwa mwaka 2013/2014 na Makadirio kwa mwaka 2014/2015 upo katika **Kiambatisho Na. I.**

Matumizi ya Kawaida

100. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara imetengewa jumla ya **Shilingi 20,371,844,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Matumizi Mengineyo na Mishahara), fedha hizo zinajumuisha:-

- (i) Mishahara ya Wizara Sh. **3,151,654,000**
- (ii) Mishahara ya Asasi Sh. **7,849,270,000**

Nakala ya Mtando (Online Document)

(iii) Matumizi Mengineyo
ya Wizara - Sh. **5,830,920,000.**

(iv) Matumizi Mengineyo
ya Asasi Sh. **3,540,000,000.**

Mchanganuo wa makadirio ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara na Asasi upo katika **Kiambatisho Na. II**. Matumizi ya Kawaida kwa Wizara peke yake rejea **Kiambatisho Na. III** na kwa Asasi rejea **Kiambatisho Na. IV**.

Miradi ya Maendeleo

101. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara imetengewa jumla ya **Shilingi 15,000,000,000** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo kamili upo katika **Kiambatisho Na. V**.

MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA MPANGO WA MWAKA 2014/2015.

102. Mheshimiwa Spika, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka wa fedha 2014/2015, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya jumla ya **Shilingi 35,371,844,000** ambapo kati ya hizo, fedha za Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 20,371,844,000** na Fedha za Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 15,000,000,000**. Mchanganuo wa fedha hizi upo katika viambatisho vilivyotajwa hapo awali ambavyo ni sehemu ya Hotuba hii.

103. Mheshimiwa Spika, napenda nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya: www.habari.go.tz na www.tanzaniangovernment.blogspot.com

104. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Wizara hiyo. Namwona Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kapteni John Damiano Komba. (Makofii)

Taarifa ya Upinzani kuhusu bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2014/2015 kama ilivyosomwa Bungeni

MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII): Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari,

Nakala ya Mtando (Online Document)

Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, nachukua fursa hii kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ilikutana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Jijini Dar es Salaam tarehe 4 Mei, 2014. Katika kikao hicho Kamati ilipokea na kujadili kwa kina utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Aidha Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa Wizara ambapo kwa sehemu kubwa maagizo hayo yametekeliza ingawa kuna changamoto kubwa ya kupokea fedha kutoka Hazina ili kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajetiy Mwaka 2013/2014. Katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Kamati ilitoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, maoni na ushauri wa Kamati kwa sehemu kubwa yametekeliza na Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Wizara ilipangia bajeti ya shilingi bilioni 30.3, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 9.2 zinajumuisha mishahara na shilingi bilioni 8.3 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Shilingi 12,700,000,000/= kwa ajili ya Miradi mbalimbali ya Maendeleo zote zikiwa ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, hadi Kamati ilipokutana na Wizara mwezi Mei, 2014 fedha zilizokuwa zimetolewa ni shilingi 16.5 tu ya fedha zote sawa na 50% ambazo ni fedha za ndani. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 7.8 ni mishahara, shilingi 4.4 ni Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni 4.3 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali ikamilishe utoaji wa fedha hizi kwa kipindi kilichosalia ili Wizara iweze kutekeleza majukumu ilijoipangia kwa ufanisi wa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kamati iliagiza Serikali kuongeza bajeti ya Wizara ambayo ilikuwa ndogo kwa mwaka 2013/2014. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali imeiongezea Wizara fedha kutoka shilingi bilioni 30.3 mpaka shilingi bilioni 35.3. Naiomba Serikali itoe fedha hizi kwa wakati ili Wizara iweze kutekeleza majukumu iliyojipangia.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Katika mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2014, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo mbalimbali hasa kwenye maeneo yanayohusu:-

Kulijengea uwezo Shirika la Utangazaji (TBC) ili liweze kujitegemea. Sheria ilioanzisha Baraza la Kiswahili la Taifa ifanyiwe marekebisho ili kukidhi haja ya wakati uliopo na pia liweze kutekeleza maagizo yaliyomo katika Kamisheni ya Kiswahili kwa nchi za Afrika Mashariki. Kuongeza fedha katika Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) kuhakikisha linajikita zaidi katika kuhuisha na kuhimiza maendeleo ya uzalishaji ya kazi za wasanii. Wizara pamoja na mambo mengine ikamilishe ujenzi wa eneo la changamani la michezo ili hatimaye Baraza la Michezo la Taifa (BMT) lipate ofisi za kisasa na mwisho, kuitumia sekta binafsi katika ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa, hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kutekeleza ushauri wa Kamati kwenye maeneo ambayo bado hayajafanyiwa kazi.

Mhesimiwa Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara imekadiria kukusanya jumla ya shilingi bilioni 1.15 zitakazokusanya kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ikilinganishwa na lengo la sh. 882,203,000 la mwaka 2013/2014 sawa na ongezeko la asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara inatarajia kupokea jumla ya shilingi bilioni 35 kwa ajili ya matumizi ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 20.3 ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida yaani mishahara na matumizi mengineyo na shilingi bilioni 15 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na maombi ya fedha yanayojuisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2014/2015, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Ukichukua taarifa za Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara utaona kwamba, kwa zaidi ya miaka mitatu mfululizo Kamati imekuwa ikitaka Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya Wizara hii. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, bajeti iliyotengwa imeongezeka kutoka shilingi bilioni 30.3 hadi kufikia bilioni 35.3, ingawa bado kiasi hiki hakitoshi katika changamoto za kukabiliana na majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na kuboresha maendeleo ya vijana nchini.

Mheshimiwa Spika, Ajira kwa Vijana; Taifa lililo na vijana wengi wasio na kazi maalum ni hatari sana kwani vijana hawa huweza kujingiza katika vitendo vya uvunjifu wa amani na kutumika katika vitendo vya uhalifu na hata kutumika na watu wasioitakia mema nchi yetu, Waswahili husema ‘ishara inamtosha mtambuzi’ makundi ya vijana yaliyojibatiza majina ya “Panya Road, Watoto wa Mbwa Mwitu” na mengineyo ni ishara ya uwepo wa vijana wengi wasio na kazi maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hili na takwimu kwamba kwa kila mwaka zaidi ya wahitimu milioni moja na laki mbili kutoka kwenye ngazi mbalimbali za taaluma wanaingia kwenye soko la ajira, soko ambalo lina uwezo wa kuhudumia wahitimu laki mbili tu, ni hatari kwa nchi. Kutokana na hali hiyo, vijana wanaomaliza elimu ya juu kutoka vyuo mbalimbali hapa nchini wamekuwa wakiaswa kuacha kutegemea ajira kutoka Serikalini na mashirika mbalimbali na badala yake wajajiri wenyewe na kuajiri vijana wengine ili kuihuisha dhana ya ajira na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ndiyo yenyeye jukumu la kuandaa mazingira wezeshi ya kuwasaidia vijana kwa kuwawezesha kiuchumi na kuwajengea uwezo ili kuweza kujajiri na kuajirika. Kiasi hiki cha bajeti kilichotengwa ni kidogo na hakitoshelezi mahitaji halisi yaliyopo Wizarani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kutenga bajeti ndogo, Kamati inaitaka Wizara kuandaa mpango maalum wa makusudi wa kuwawezesha vijana kama njia mojawapo ya kupunguza tatizo la ajira kwa vijana nchini. Kamati inaamini kuwa kuwepo kwa mpango wa makusudi wa kupunguza tatizo la vijana nchini kutapelekea sekta ya habari, vijana, utamaduni na michezo kuchochea ukuaji wa uchumi kuititia rasilimali vijana.

Mheshimiwa Spika, pengine suala hili la vijana wengi wasio na kazi maalum linahitaji mjadala wa Kitaifa.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Mfuko huu ulianzishwa mwaka 1993 kwa lengo la kutoa mikopo midogo midogo yenye gharama nafuu itakayowawezesha vijana kujajiri na kuajiriwa. Suala la kuwawezesha vijana kujajiri kuitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ni changamoto kubwa inayolikabili Taifa kwa sasa na hii ni kutokana na ukweli kwamba vijana ndiyo nguzu na nguvu kazi ya Taifa na ndiyo kundi kubwa katika jamii. Kama ilivyoainishwa na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 kuwa zaidi ya asilimia 60 ni vijana.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa katika kuwawezesha vijana ni ukosefu wa rasilimali fedha ambayo ingetumika kutoa mikopo, mafunzo ya ujasiriamali na ufuatiliaji wa shughuli za vijana nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuwaendeleza vijana kwani kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Wizara imetengewa jumla ya shilingi bilioni nne tu kwa ajili ya Mfuko huu ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2013/2014 ambapo Serikali ilitenga shilingi bilioni 6.1 kwa ajili ya mikopo ya vikundi kwa vijana vya uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, hadi Kamati inakutana na Wizara, fedha zilizokuwa zimepelekwa ni shilingi bilioni mbili tu kwa ajili ya kuwakopesha vijana. Hata hivyo, fedha hizi zimepokelewa Wizarani hivi karibuni na Wizara sasa imeanza kuwakopesha vijana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, Kamati inaitaka Serikali kupeleka fedha zote zilizosalia ili kuifanya Wizara kuweza kutekeleza majukumu iliojipangia kwa mwaka huu unaoishia tarehe 30 Juni, 2014 kwani Kamati inaamini fedha hizi zilizokwishatolewa ni kidogo ikilinganishwa na idadi kubwa ya vijana ambao wanahitaji kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*). Jengo la Shirika la Utangazaji. Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) ni chombo cha habari cha umma kinachomiliki mitambo ya Redio na Televisheni ambayo ipo maeneo mbalimbali ya nchi. Moja ya majukumu ya kuanzishwa kwa Shirika hili ni kuhakikisha kuwa matangazo ya Redio na Televisheni yanasi kika nchi nzima na yanakuwa hewani kwa saa ishirini na nne.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) mpaka sasa limeshindwa kukamilisha ujenzi wa jengo lake tangu limewekewa jiwe la msingi tarehe 10 Aprili, 1995 na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili Mheshimiwa Alhaj Ali Hassan Mwinyi. Jengo hilo lilikuwa likitengewa fedha za ujenzi katika Mfuko wa Maendeleo, lakini baadaye fungu hilo lilisitishwa.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia kukamilika kwa ujenzi wa jengo hilo, Menejimenti ya TBC ilifanya makubaliano na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ili kupatiwa mkopo kwa utaratibu wa kudhaminiwa na Serikali kwa asilimia mia moja. Wizara ya Fedha imeshindwa kutoa tamko la kudhamini mkopo huo kwa asilimia mia moja na kuahidi kutoa dhamana ya asilimia 75 tu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuliangalia upya jambo hili kwa jicho la huruma na kudhamini mkopo utakaoweza kukamilisha ujenzi wake kwani kutokukamilika kwa ujenzi wa jengo hilo kwa muda mrefu sasa ni fedheha kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, gari la Matangazo la Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC). Napenda niipongeze Serikali kwa jitihada ambazo zimevezesha Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kupata gari jipya la kurushia matangazo (*Outside Broadcasting Van - OB Van*) na la kisasa. Gari hili lina uwezo kwa kazi hiyo ya urushaji matangazo hapa nchini pengine kuliko gari lolote. Haya ni mapinduzi mazuri kifikra na katika tasnia nzima ya habari. Ni imani ya Kamati kuwa OB-Van hiyo itaboresha matangazo hasa ya moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Kamati inalishauri shirika kulitumia ipasavyo kwa misingi iliyokusudiwa na kwa uangalifu mkubwa ili liweze kudumu na kwa maana hiyo kuwa kiunganishi kizuri cha habari baina ya Serikali na jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Wadeni wa TBC. Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) linawadai watu na taasisi mbalimbali za Serikali deni kubwa ambalo lingelipwa kwa wakati TBC ingeweza kutatua baadhi ya matatizo yake ikiwa ni pamoja na kuifanya ukarabati mitambo yake iliyochakaa sana.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa ushauri kwa Serikali kuititia TBC kufuatilia kwa ukaribu madeni yake na ikibidi kuwaweka hadharani wadaiwa wote. Aidha Kamati inalishauri Shirika hilo kutotoa huduma nyingine kwa mdaiwa yeoyote mpaka atakapomaliza deni lake la awali.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Urithi na Ukombozi wa Afrika. Programu ya Ukombozi wa Bara la Afrika ilianzishwa kwa lengo la kutambua mchango wa nchi za Afrika zilizoshiriki katika kulikombua Bara hili. Kati ya nchi hizo Tanzania inatambulika kuwa na mchango mkubwa sana katika ukombozi wa Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 jumla ya shilingi bilioni 200 zilitengwa kwa ajili ya uendelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi

Nakala ya Mtando (Online Document)

wa Bara la Afrika. Hadi Machi, 2014 shilingi bilioni 200 zimetolewa na shilingi bilioni ishirini na tisa milioni mia tisa ndiyo zimetumika.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeona thamani ya mchango wa Tanzania kutambulika Kimataifa katika ukombozi wa Bara la Afrika hivyo basi, Kamati inashauri fedha zote zinazotengwa kwa matumizi ya programu hii zisitumike katika malengo mengine isipokuwa yaliyokusudiwa ili kuendelea kutunza na kuthamini umuhimu wa programu hii.

Mheshimiwa Spika, Vazi la Taifa. Kwa miaka mingi kumekuwa na mjadala kuhusu Vazi la Taifa na hata kusababisha Serikali kuunda Kamati kuhusu suala hili. Vazi au uvaaji huweza kuelezea asili ya mtu, jinsia, imani na pia wakati mwagine huakisi tabia yake. Kwa kifupi uvaaji ni lugha ya kimavazi inayomtambulisha mvaaji katika jamii fulani.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kwamba, wazo la kuwa na Vazi la Taifa lilikuwa zuri kwa maana ya kupata vazi litakalotumika katika matukio muhimu ya Kitaifa na Kimataifa ukizingatia mavazi ni sehemu muhimu ya utamaduni wa Taifa husika.

Mheshimiwa Spika, ni kwa muktadha huu iliundwa Kamati ili kuratibu zoezi hili la kupata Vazi la Taifa na kwa taarifa kupitia mitando ya kijamii ni kwamba Kamati hiyo iliyasilisha taarifa yake kwa aliyekuwa Waziri katika Wizara ya Habari, Utamaduni Ajira na Vijana juu ya vazi hilo la Taifa. Kamati ingependa kupata taarifa kama kuna mchakato wowote unaoendelea juu ya jambo hili au laa na kama kweli bado tuna uhitaji wa vazi hilo au lilikuwa ni suala la kujifurahisha tu.

Mheshimiwa Spika, mafunzo kwa Waandishi wa Habari. Kwanza tunawapongeza waandishi wa habari kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwapasha habari mbalimbali Watanzania ikiwa na kile kinachojiri hapa Bungeni kila siku. Hata hivyo, bado kuna waandishi wa habari wachache hawajui historia ya nchi yetu na pia masuala mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa. Hali hii huchangia upotoshaji wa masuala muhimu ya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa ushauri kwa Serikali na wamiliki wa vyombo vya habari kuwapatia mafunzo ya mara kwa mara waandishi wa habari ili kuwajengea uwezo na hivyo kuwa weledi katika kazi zao. Kamati inaamini kuwa waandishi wa habari ni kama Walimu kwa jamii. Hivyo kama hawatajibidiisha kupata maarifa ya kutosha au kuwawezesha kitaaluma wanaweza kuwa wapotoshaji badala ya kuwa waelimishaji.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Waandishi na Lugha ya Kiswahili. Bado kuna waandishi wengi wa habari wanafanya makosa katika lugha kwa kutozingatia ufasaha na usanifu wa lugha ya Kiswahili. Ni aibu kwa mwandishi wa habari wa Kitanzania kufanya makosa hasa ukizingatia kuwa Watanzania ndiyo tunaoonekana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa kuifahamu vyema lugha hii adhimu na aushi ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa ushauri kwa waandishi wa habari kujibidiisha kujifunza Kiswahili fasaha ili wawe makini wanapoandika makala na taarifa kwa matukio mbalimbali. Kwa kufanya hivi kutawasaadid Kutumia lugha iliyosanifu na iliyofasaha ili wasomaji wapate habari zilizo sahihi na za kweli badala ya kuchanganya maneno kwa kutofahamu lugha ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Uhuru wa Vyombo vya Habari na Haki ya Kupata Habari. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa wanahabari na wadau wa habari wote nchini kwa kuwa mstari wa mbele kuelimisha jamii licha ya kuwa katika mazingira magumu. Pamoja na mambo mengine, mazingira hayo magumu huchangiwa na kutokuwepo kwa sheria nzuri zinazolinda haki na uhuru kamili wa wanahabari na vyombo vyao.

Mheshimiwa Spika, suala la kuleta Bungeni la Muswada wa Sheria ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, limechukua muda mrefu sana. Wadau na wanahabari hawaridhishwi na kusuasua kwa Serikali juu ya Muswada huu na wanaona kama vile hawatendewi haki. Serikali imekuwa ikitoa ahadi kwamba Muswada huu utaletwa na kila hatua inayohitajika imekamilika, lakini matokeo yake Muswada huu hauletwi Bungeni. Aidha, Serikali imeahidi kuleta Bungeni Muswada wa Haki ya Kupata Habari kwani maandalizi yake wanasema yamekamilika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kufanya haraka sana ili Miswada hii muhimu katika tasnia ya habari iweze kuleta Bungeni na ikiwezekana Serikali itoe muda maalum (*timeframe*) wa kuleta Bungeni kwa Miswada hiyo, ili hatimaye yapatikane mazingira bora ya uhuru wa kupata habari ikiwa ni pamoja na kusimamia haki za wanahabari na vyombo vyenyewe vya habari.

Mheshimiwa Spika, Vijana na UKIMWI. Taarifa iliyotolewa hivi karibuni na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani kuhusu hali ya watu ulimwenguni imebainisha kuwa pamoja na kuongezeka kwa idadi ya watu wenye umri mdogo ulimwenguni, vijana wamekuwa katika hatari zaidi ya kuathiriwa na ugonjwa wa UKIMWI. Taarifa hiyo imeeleza kwamba, hivi sasa kwa kila dakika moja kuna vijana wanne wanaambukizwa virusi vya ugonjwa wa UKIMWI wengi wao ni vijana wa kike.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, takwimu hizo pia zinaonesha kwamba idadi ya vijana wenyе umri wa miaka 15 hadi 24 ni zaidi ya vijana bilioni moja ikiwa ni asilimia 20 ya jumla ya idadi ya watu ulimwenguni ambao asilimia 90 ya idadi hiyo wapo katika nchi zinazoendelea. Aidha, vijana wenyе umri wa chini ya miaka 25 imechukua asilimia 50 ya jumla ya idadi ya watu ulimwenguni.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini idadi ya vijana kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 ni zaidi ya asilimia 60 ya Watanzania. Pamoja na kiwango cha maambukizi kupungua kutoa 5.7% mwaka 2008/2009 hadi kufikia 5.1% kwa mwaka 2010/2011, bado vijana wengi sana wanaathirika na ugonjwa huo wa UKIMWI. Kizazi hiki ambacho ndiyo nguvukazi ya nchi kinahitaji kulindwa kutokana na ugonjwa huu ili nacho kisimamie vizuri kizazi kijacho.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kupitia taasisi zake kutoa elimu ya kutosha kwa vijana kuhusu janga hili la UKIMWI. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kupitia Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) kuwa na kauli mbiu ya salamu angalizo kwa kila Tamasha linalokutanisha vijana hususan matamasha yaitwayo Fiesta na mengineyo ambayo hufanyika katika kila mkoa na hukusanya vijana wengi sana kwa wakati mmoja ili kutoa angalizo kwa vijana hao kupata burudani huku wakichukua tahadhari kubwa kwa afya zao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza timu yetu ya Taifa (*Taifa Stars*) kwa ushindi wa bao moja kwa sifuri dhidi ya Zimbabwe. Mechi iliochezwa katika Uwanja wa Taifa Jijini Dar es Salaam tarehe 18 mwezi wa Tano mwaka huu, 2014 kuwania kufuzu kucheza Kombe la Mataifa ya Afrika yatakayofanyika mwaka 2015 nchini Morocco. Tunaiombea Mungu timu yetu iweze kushinda tena katika mchezo wa marudiano utakaochezwa nchini Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaipongeza Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuwawezesha vijana 45 kwenda kuweka kambi nje ya nchi ili kuijandaa na michezo ya Jumuuya ya Madola. Wizara imefanya hivyo kupitia mpango wake wa Diplomasia ya Michezo ambayo imewawezesha wanamichezo hao kupata nafasi za kwenda kujifua katika nchi mbalimbali kama New Zealand, Ethiopia, China na Uturuki tayari kwa kushiriki michezo ya Madola mwezi Julai.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi Kamati ingeona fahari kama Wizara ingeipeleka Timu ya Taifa pia angalau nchi moja kati ya hizi ili nayo ijifue vyema badala ya kuiachia kuweka Kambi Jijini Mbeya kwa kisingizio cha hali ya hewa kufanana na hali ya hewa ya Zimbabwe wakati Mbeya kwenyewe hakuna kiwanja cha mpira chenye hadhi ya Kimataifa. (Makofii)

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inatoa pongezi za dhati kwa watoto wa Mitaani wa Tanzania kushinda Kombe la Dunia. Kwa kweli watoto hawa wametupa faraja kubwa na imekuwa fahari kwa Tanzania nzima, kwani wameipeperusha vyema bendera ya Taifa letu. Kamati inaishauri Serikali na pia Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania, kuziona juhudzi za watoto hao na kutumia vipaji vyao walivyonavyo ili waweze kujajiri kwa manufaa yao na kwa Taifa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa pole kwa misiba ya wasanii waliopoteza maisha kama Marehemu Muhidin Maalim Gurumo, Marehemu Adam Phillip Kuambiana, Marehemu Amina Nguluma na wengineo. Mwenyezi Mungu awalipe ujira wao na awasamehe makosa yao.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inatumia fursa hii kuwaomba wasanii kutunga nyimbo nzuri zenyne mafundisho kama ambazo alitunga na kuzimba Marehemu Muhidin Maalim Gurumo wakizingatia maadili ya Kitanzania.

Kamati inapenda kuwashauri wasanii wa Tanzania kujituma na kuwa na mipango endelevu ili sanaa yao iweze kunyaanya maisha yao au iweze kuwatoa kama wenyewe wanavyosema

Mheshimiwa Spika, wapo wasanii wazuri sana hapa nchini ambao kama wangeweza kuongeza juhudzi wangekuwa wa Kimataifa, lakini bahati mbaya wamebweteka na sifa chache wanazozipata hapa nchini. Kamati inawashauri wasanii hawa kujitathmini upya na pia kupanga mikakati ya namna ya kuinua tasnia zao ili ziweze kuwaletea maendeleo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kutumia fursa hii kukupongeza kwa umahiri na busara zako katika uendeshaji wa Vikao vya Bunge. Nawapongeza pia Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi wanavyokusaidia wewe kuendesha vikao vya Bunge. Kwa niaba ya Kamati, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Fenella Ephraim Mukangara, Mbunge na Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mbunge; Katibu Mkuu, Ndugu Sihaba Nkinga; Naibu Katibu Mkuu, Profesa Elisante Ole-Gabriel na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii kwa ushirikiano wao mkubwa waliounesha wakati tunatekeleza shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi hapa hatutajwi, umesema tusitajwe; siku nyingine tutajwe.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati, Ndugu Charles Mloka; Makatibu wa Kamati, Ndugu Hanifa Masaninka, Ndugu Abdallah Hancha na Ndugu Aziza Makwai, kwa ushauri na uratibu wa Kamati hadi kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumalizia, naomba niwashukuru wapigakura wangu na wana Jimbo langu la Mbinga Magharibi au Nyasa kwa ushirikiano wao hadi tumeweza kufanikiwa na kuipata Wilaya Mpya ya Nyasa. Wito wangu kwao ni kwamba Nyasa itajengwa na Wananyasa wenyewe, na mkataa kwao ni mtumwa. Sote tuhamasike kujenga Nyasa yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, na ninaomba kuwasilisha. (Makofii)

SPIKA: Ahsante! Hayo ya mwisho ni ya kwako, siyo maoni ya Kamati.

Taarifa ya Kamati Kuhusu Maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2014/2015 - Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Kama Ilivyowasilishwa Mezani

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014 PAMOJA NA MAONI YA KAMATIKUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2014/2015

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, nachukua fursa hii kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ilikutana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Jijini Dar es Salaam tarehe 04 Mei, 2014. Katika kikao hicho Kamati ilipokea na kujadili kwa kina utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Aidha Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa Wizara ambapo kwa sehemu kubwa maagizo hayo yametekelawa ingawa kuna changamoto kubwa ya kupokea fedha kutoka Hazina ili kutekeleza majukumu yake.

2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2013/2014

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 Kamati ilitoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, maoni na ushauri wa Kamati kwa sehemu kubwa yametekelawa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Wizara ilipangia bajeti ya shilingi **30,328,045,000/=** kati ya fedha hizo shilingi **9,257,125,000/=** zinajumuisha mishahara na shilingi **8,370,920,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Shilingi **12,700,000,000/=** kwa ajili ya Miradi mbalimbali ya Maendeleo zote zikiwa ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, hadi Kamati ilipokutana na Wizara mwezi Mei, 2014 fedha zilizokuwa zimetolewa ni shilingi **16,544,000,119/=** tu ya fedha zote sawa na 50% ambazo ni fedha za ndani. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi **7,806,736,134/=** ni mishahara, shilingi **4,409,763,985/=** ni Matumizi Mengineyo na shilingi **4,327,500,000/=** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali ikamilishe utoaji wa fedha hizi kwa kipindi kilichosalia ili Wizara iweze kutekeleza majukumu iliyojipangia kwa ufanisi kwa Mwaka wa Fedha **2013/2014**.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Kamati iliiagiza Serikali kuongeza bajeti ya Wizara ambayo ilikuwa ndogo kwa mwaka 2013/2014. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Serikali imeiongezea Wizara fedha kutoka shilingi **bilioni 30.3** mpaka shilingi **bilioni 35.3**. Naiomba Serikali itoe fedha hizi kwa wakati ili Wizara iweze kutekeleza majukumu iliyojipangia.

3.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2014, Kamati ilioa maoni na ushauri kwenye maeneo mbalimbali hasa kwenye maeneo yanayohusu:-

- Kulijengea uwezo Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ili liweze kujitegemea.
- Sheria iliyoanzisha Baraza la Kiswahili la Taifa ifanyiwe marekebisho ili kukidhi haja ya wakati uliopo na pia liweze kutekeleza maazimio yaliyomo kwenye Kamisheni ya Kiswahili kwa nchi za Afrika Mashariki.
- Kuongeza fedha katika Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.
- Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) kuhakikisha linajikita zaidi katika kuhuisha na kuhimiza maendeleo ya uzalishaji ya kazi za wasanii.
- Wizara pamoja na mambo mengine ikamilishe ujenzi wa eneo changamani la michezo ili hatimaye Baraza la Michezo la Taifa (BMT) lipate ofisi za kisasa.
- Kuitumia sekta binafsi katika ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa, hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kutekeleza ushauri wa Kamati kwenye maeneo ambayo bado hayajafanyiwa kazi.

4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2014

4.1 Makadirio ya Mapato

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara imekadiria kukusanya jumla ya shilingi **1,149,008,000/=** zitakazokusanya kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ukilinganisha na lengo la shilingi **882,203,000/=** la mwaka 2013/2014 sawa na ongezeko la asilimia 30.

4.2 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara inatarajia kupokea jumla ya shilingi **35,371,884,000/=** kwa ajili ya matumizi ambapo kati ya fedha hizo shilingi **20,371,884,000/=** ni kwa ajili ya matumizi

Nakala ya Mtando (Online Document)

ya Kawaida yaani mishahara na matumizi mengineyo na shilingi **15,000,000,000/=** kwa ajili ya Mirasi ya Maendeleo.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na maombi ya fedha yanayojumuisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2014/2015, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuataao:-

5.1 Bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

Mheshimiwa Spika, ukichukua taarifa za Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii utaona kwamba kwa zaidi ya miaka mitatu mfululizo Kamati imekuwa ikitaka Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya Wizara hii. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 bajeti iliyotengwa imeongezeka kutoka shilingi **bilioni 30.3** hadi shilingi **bilioni 35.3**, Ingawa bado kiasi hiki hakitoshi kutekeleza changamoto za kukabiliana na majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na kuboresha maendeleo ya vijana nchini.

5.2 Ajira kwa Vijana

Mheshimiwa Spika, Taifa lililo na vijana wengi wasio na kazi maalum ni hatari sana kwani vijana hawa huweza kuijingiza katika vitendo vya uvunjifu wa amani na kutumika katika vitendo vya uhalifu na hata kutumika na watu wasioitakia mema nchi yetu, waswahili husema ‘ishara inamtosha mtambuzi’ makundi ya vijana yaliyojibatiza majina ya “Panya Road” “Watoto wa Mbwa Mwit” na mengineyo ni ishara ya uwepo wa vijana wengi wasio na kazi maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hili na takwimu kwamba kwa kila mwaka zaidi ya wahitimu milioni moja na laki mbili (1,200,000) kutoka kwenye ngazi mbalimbali za taaluma wanaingia kwenye soko la ajira, soko ambalo lina uwezo wa kuhudumia wahitimu laki mbili (200,000) tu ni hatari kwa nchi. Kutokana na hali hiyo, vijana wanaomaliza elimu ya juu kutoka vyuo mbalimbali hapa nchini wamekuwa wakiaswa kuacha kutegemea ajira kutoka Serikalini na mashirika mbalimbali na badala yake wajajiri wenyewe na kuajiri vijana wengine ili kuihuisha dhana ya kukuza ajira na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ndiyo yenyе jukumu la kuandaa mazingira wezeshi ya kuwasaidia vijana kwa kuwawezesha kiuchumi na kuwajengea uwezo ili kuweza kujajiri na kuajirika.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Kiasi hiki cha bajeti kilichotengwa ni kidogo na hakitoshelezi mahitaji halisi yaliyopo ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kutenga bajeti kidogo, Kamati inaitaka Wizara kuandaa mpango maalum na wa makusudi wa kuwawezesha vijana kama njia mojawapo ya kupunguza tatizo la ajira kwa vijana nchini. Kamati inaamini kuwa kuwepo kwa mpango wa makusudi wa kupunguza tatizo la vijana nchini kutapelekea sekta ya habari, vijana, utamaduni na michezo kuchochaea ukuaji wa uchumi kupitia rasilimali vijana.

Mheshimiwa Spika, pengine suala hili la vijana wengi wasio na kazi maalum linahitaji mjadala wa kitaifa.

5.3 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ulianzishwa mwaka 1993 kwa lengo la kutoa mikopo midogo midogo yenye gharama nafuu itakayowawezesha vijana kujajiri na kuajiriwa. Suala la kuwawezesha vijana kujajiri kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ni changamoto kubwa inayolikabili Taifa kwa sasa na hii ni kutokana na ukweli kwamba vijana ndiyo nguzo na nguvu kazi ya Taifa na ndiyo kundi kubwa katika jamii. Kama ilivyobainishwa na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 kuwa zaidi ya asilimia 60 ni vijana.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa katika kuwawezesha vijana ni ukosefu wa rasilimali fedha ambayo ingetumika kutoa mikopo, mafunzo ya ujasiriamali na ufuatiliaji wa shughuli za vijana nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudini zinazofanywa na Serikali katika kuwaendeleza vijana kwani Mwaka wa Fedha 2014/2015 Wizara imetengewa jumla ya shilingi **bilioni nne tu (4,000,000,000/=)** kwa ajili ya mfuko huu ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2013/2014 ambapo Serikali ilitenga shilingi **6,100,000,000/=** kwa ajili ya mikopo ya vikundi kwa vijana vya uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, hadi Kamati inakutana na Wizara, fedha zilizokuwa zimepelekwa ni shilingi **2,000,000,000/=** tu kwa ajili ya kuwakopesha vijana. Hata hivyo fedha hizi zimepokelewa Wizarani hivi karibuni na Wizara sasa imeanza kuwakopesha vijana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, Kamati inaitaka Serikali kupeleka fedha zote zilizosalia ili kuifanya Wizara kuweza kutekeleza majukumu iliyojipangia kwa mwaka huu unaoishia tarehe 30 Juni, 2014 kwani Kamati

Nakala ya Mtandao (Online Document)

inaamini fedha hizi zilizokwishatolewa ni kidogo ikilinganishwa na idadi kubwa ya vijana ambao wanahitaji kuendelezwa.

5.4 Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

5.4.1 Jengo la Shirika la Utangazaji Tanzania

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ni chombo cha habari cha umma kinachomiliki mitambo ya Redio na Televisheni iliyopo maeneo mbalimbali ya nchi. Moja ya majukumu ya kuanzishwa kwa Shirika hili ni kuhakikisha kuwa matangazo ya Redio na Televisheni yanasi kika nchi nzima na yanakuwa hewani kwa saa ishirini na nne (24).

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) mpaka sasa limeshindwa kukamilisha ujenzi wa jengo lake tangu limewekewa jiwe la msingi tarehe 10 Aprili, 1995 na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili Mheshimiwa Alhaj Ali Hassan Mwinyi. Awali jengo hilo lilikuwa likitengewa fedha za ujenzi katika mfuko wa maendeleo lakini baadaye fungu hilo lilisitishwa.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia kukamilika kwa ujenzi wa jengo hilo, Menejimenti ya TBC ilifanya makubaliano na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ili kupatiwa mkopo kwa utaratibu wa kudhamini na Serikali kwa asilimia mia moja. Wizara ya Fedha imeshindwa kutoa tamko la kudhamini mkopo huo kwa asilimia mia moja na kuahidi kutoa dhamana ya asilimia 75 tu. Kamati inashauri Serikali kuliangalia jambo hili kwa jicho la huruma na kudhamini mkopo utakaoweza kukamilisha ujenzi wake kwani kutokukamilika kwa ujenzi wa jengo hilo kwa muda mrefu sasa ni fedheha kwa Taifa.

5.4.2 Gari la Matangazo la Shirika la Utangazaji (TBC)

Tanzania

Mheshimiwa Spika, napenda niipongeze Serikali kwa jitihada ambazo zimevezesha Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kupata gari jipya la kurushia matangazo (*Outside Broadcasting Van - OB Van*) na la kisasa. Gari hili lina uwezo kwa kazi hiyo ya urushaji matangazo hapa nchini pengine kuliko gari lolote. Haya ni mapinduzi mazuri kifkra na katika tasnia nzima ya habari. Ni imani ya Kamati kuwa OB-Van hiyo itaboresha matangazo hasa ya moja kwa moja (*live*).

Mheshimiwa Spika, Kamati inalishauri shirika kulitumia ipasavyo kwa misingi iliyokusudiwa na kwa uangalifu mkubwa ili liweze kudumu na kwa maana hiyo kuwa kiunganishi kizuri cha habari baina ya Serikali na jamii ya Watanzania.

5.4.3 Wadeni wa TBC

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) linawadai watu na taasisi mbalimbali za Serikali deni kubwa ambalo kama lingelipwa kwa wakati TBC ingeweza kutatua baadhi ya matatizo yake ikiwa ni pamoja na kuifanyia ukarabati mitambo yake iliyochakaa sana.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa ushauri kwa Serikali kupitia TBC kufuatilia kwa ukaribu madeni yake na ikibidi kuwaweka hadharani wadaiwa wote. Aidha Kamati inalishauri Shirika kutotoa huduma nyingine kwa mdaiwa ye yeyote mpaka atakapomaliza deni lake la awali.

5.5 Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika

Mheshimiwa Spika, Programu ya Ukombozi wa Bara la Afrika ilianzishwa kwa lengo la kutambua mchango wa nchi za Afrika zilizoshiriki katika kulikombua Bara hili. Kati ya nchi hizo Tanzania inatambulika kuwa na mchango mkubwa sana katika ukombozi wa Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 jumla ya shilingi **200,000,000/=** zilitengwa kwa ajili ya uendelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika. Hadi Machi, 2014 shilingi **200,000,000/=** zimetolewa na shilingi **29,912,000/=** ndiyo zimetumika.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeona thamani ya mchango wa Tanzania kutambulika kimataifa katika ukombozi wa Bara la Afrika hivyo basi, Kamati inashauri fedha zote zinazotengwa kwa matumizi ya programu hii zisitumike katika malengo mengine isipokuwa yaliyokusudiwa ili kuendelea kutunza na kuthamini umuhimu wa programu hii.

5.6 Vazi la Taifa

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi kumekuwa na mjadala kuhusu Vazi la Taifa la hata kusababisha Serikali kuunda Kamati kuhusu suala hili. Vazi au uvaaji huweza kuelezea asili ya mtu, jinsia, imani na pia wakati mwingine huakisi tabia yake. Kwa kifupi uvaaji ni lugha ya kimavazi inayomtambulisha mvaaji katika jamii fulani.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kwamba, wazo la kuwa na Vazi la Taifa lilikuwa zuri kwa maana ya kupata vazi litakalotumika katika matukio muhimu ya kitaifa na kimataifa ukizingatia mavazi ni sehemu muhimu ya utamaduni kwa Taifa husika.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, ni kwa muktadha huu iliundwa Kamati ili kuratibu zoezi hili la kupata Vazi la Taifa na kwa taarifa kupitia mitandao ya kijamii ni kwamba kamati hiyo iliwasilisha taarifa yake kwa aliyekuwa Waziri katika Wizara ya Habari, Utamaduni Ajira na Vijana juu ya vazi hilo la Taifa. Kamati ingependa kupata taarifa kama kuna mchakato wowote unaoendelea juu ya jambo hili au laa na kama kweli bado tuna uhitaji wa vazi hilo au lilikuwa ni suala la kujifurahisha tu.

5.7 Mafunzo kwa Waandishi wa Habari

Mheshimiwa Spika, kwanza tunawapongeza waandishi wa habari kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwapasha habari mbalimbali Watanzania ikiwa na kile kinachojiri hapa Bungeni kila siku. Hata hivyo, bado kuna waandishi wa habari wachache hawajui historia ya nchi yetu na pia masuala mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Hali hii huchangia upotoshaji wa masuala muhimu ya kitaifa na kimataifa. Kamati inatoa ushauri kwa Serikali na wamiliki wa vyombo vya habari kuwapatia mafunzo ya mara kwa mara waandishi wa habari ili kuwajengea uwezo na hivyo kuwa weledi katika kazi zao. Kamati inaanini kuwa waandishi wa habari ni kama walimu kwa jamii. Hivyo kama hawatajibidiisha kupata maarifa ya kutosha au kuwezeshwa kitaaluma wanaweza kuwa wapotoshaji badala ya waelimishaji.

5.8 Waandishi na Luga ya Kiswahili

Mheshimiwa Spika, bado kuna waandishi wengi wa habari wanafanya makosa katika lugha kwa kutozingatia ufasaha na usanifu wa lugha ya Kiswahili. Ni aibu kwa mwandishi wa habari wa Kitanzania kufanya makosa haya hasa ukizingatia kuwa Watanzania ndiyo tunaoonekana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa kuifahamu vyema lugha hii adhimu na aushi ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa ushauri kwa waandishi wa habari kujibidiisha kujifunza Kiswahili fasaha ili wawe makini wanapoandika makala na taarifa kwa matukio mbalimbali. Kwa kufanya hivi kutawasaidia kutumia lugha iliyosanifu na iliyofasaha ili wasomaji wapate habari zilizosahihi na za kweli badala ya kuchanganya maneno kwa kutofahamu lugha ipasavyo.

5.9 Muswada wa Uhuru wa Vyombo vya Habari na Haki ya Kupata Habari

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wanahabari na wadau wa habari wote nchini kwa kuwa mstari wa mbele kuelimisha jamii licha ya kuwa katika mazingira magumu. Pamoja na mambo mengine, mazingira hayo magumu yanachangiwa na kutokuwepo kwa sheria nzuri zinazolinda haki na uhuru kamili wa wanahabari na vyombo vyao.

Mheshimiwa Spika, suala la kuletwa Bungeni kwa Muswada wa Sheria ya Uhuru wa Vyombo vya Habari limechukua muda mrefu sana kuletwa Bungeni. Wadau na wanahabari hawaridhishwi na kususua kwa Serikali juu ya Muswada husika na wanaona kama vile hawatendewi haki. Serikali imekuwa ikitoa ahadi kwamba Muswada huo utaletwa na kila hatua inayohitajika imekamilika lakini matokeo yake Muswada huo hauletwi Bungeni. Aidha, Serikali pia imeahidi kuleta Bungeni Muswada wa Haki ya Kupata Habari kwani maandalizi yake yamekwishakamilika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kufanya haraka sana ili Miswada hii muhimu katika tasnia ya habari iweze kuletwa Bungeni na ikiwezekana Serikali itoe muda maalum (*timeframe*) wa kuletwa Bungeni kwa Miswada hiyo ili hatimaye yapatikane mazingira bora ya uhuru wa kupata habari ikiwa ni pamoja na kusimamia haki za wanahabari na vyombo vyenyewe vya habari.

5.10 Vijana na UKIMWI

Mheshimiwa Spika, taarifa iliyotolewa hivi karibuni na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani kuhusu hali ya watu ulimwenguni imebainisha kuwa pamoja na kuongezeka kwa idadi ya watu wenye umri mdogo ulimwenguni, vijana wamekuwa katika hatari zaidi ya kuathiriwa na ugonjwa wa UKIMWI. Taarifa hiyo imeeleza kwamba, hivi sasa kwa kila dakika moja kuna vijana wanne wanaambukizwa virusi vya ugonjwa wa UKIMWI wengi wao ni vijana wa kike.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizo pia zinaonesha kwamba idadi ya vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 24 ni zaidi wa vijana bilioni moja ikiwa ni asilimia 20 ya jumla ya idadi ya watu ulimwenguni ambao asilimia 90 ya idadi hiyo wapo katika nchi zinazoendelea. Aidha, vijana wenye umri wa chini ya miaka 25 imechukua asilimia 50 ya jumla ya idadi ya watu ulimwenguni.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini idadi ya vijana kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 ni zaidi ya asilimia 60 ya Watanzania. Pamoja na kiwango cha maambukizi kupungua kutoa 5.7% mwaka 2008/2009 hadi kufikia 5.1% kwa mwaka 2010/2011 bado vijana wengi sana wanaathirika na ugonjwa huo wa UKIMWI. Kizazi hiki ambacho ndiyo nguvukazi ya nchi kinahitaji kulindwa kutohana na ugonjwa huu ili nacho kisimamie kizazi kijacho.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kupitia taasisi zake kutoa elimu ya kutosha kwa vijana kuhusu janga hili la UKIMWI. Aidha Kamati inaishauri Serikali kupitia Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) kuwa na kauli mbiu ya ‘salamu angalizo’ kwa kila Tamasha linalokutanisha vijana hususan matamasha

Nakala ya Mtando (Online Document)

yaitwayo Fiesta ambayo hufanyika katika kila mikoa na hukusanya vijana wengi sana kwa wakati mmoja ili kutoa angalizo kwa vijana hao kupata burudani huku wakichukua hadhari kubwa kwa afya zao.

5.11 Michezo na Muziki

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza timu yetu ya Taifa (*Taifa Stars*) kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Zimbabwe, mechi iliyochezwa katika Uwanja wa Taifa, Jijini Dar es Salaam tarehe 18/5/2014 kuwania kufuzu kucheza Kombe la Mataifa ya Afrika yatakayofanyika mwaka 2015 nchini Morocco, tunaiombea timu yetu iweze kushinda tena katika mchezo wa marudiano utakaochezwa nchini Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaipongeza Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuwawezesha wanamichezo 45 kwenda kuweka kambi nje ya nchi ili kuiandaa na michezo ya Jumuiya ya Madola. Wizara imefanya hivyo kuititia mpango wake wa Diplomasia ya Michezo ambayo imewawezesha wanamichezo hao kupata nafasi za kwenda kujifua katika nchi mbalimbali kama New Zealand, Ethiopia, China na Uturuki tayari kwa kushiriki michezo ya Madola mwezi Julai.

Pamoja na pongezi hizi Kamati ingeona fahari kama Wizara ingeipeleka Timu ya Taifa walau nchi moja katika hizi ili nayo ijifue vyema badala ya kuiachia kuweka kambi Jijini Mbeya kwa kisingizio cha hali ya hewa kufanana na hali ya hewa ya Zimbabwe wakati Mbeya hakuna kiwanja cha mpira chenye hadhi ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inatoa pongezi za dhati kwa watoto wa mitaani wa Tanzania kushinda Kombe la Dunia. Kwa kweli watoto hawa wametupa faraja kubwa na imekuwa fahari kwa Tanzania nzima kwani wameipeperusha vyema bendera ya Taifa letu. Kamati inaishauri Serikali na pia Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kuziona juhudi za watoto hawa na kutumia vipaji walivyonyavyo watoto hawa ili kuwawezesha kujajiri kwa manufaa yao na Taifa kwa ujumla wake.

5.12 Sanaa na Wasanii

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa pole kwa misiba ya wasanii waliopoteza maisha kama Marehemu Muhidin Maalim Gurumo, Marehemu Adam Phillipo Kuambiana, Marehemu Amina Nguluma na wengineo. Mwenyezi Mungu awalipe ujira na awasamehe makosa yao.

Mheshimiwa Spika, aidha Kamati inatumia fursa hii kuwaomba wasanii kutunga nyimbo nzuri zenye mafundisho kama ambazo alitunga na kuziimba Marehemu

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Muhidin Maalim Gurumo wakizingatia maadili ya Kitanzania. Aidha Kamati inapenda kuwashauri wasanii wa Tanzania kujituma na kuwa na mipango endelevu ili sanaa yao iweze kunyanya maisha yao au iweze kuwatoa kama wanavyosema wenyewe wasanii.

Mheshimiwa Spika, wapo wasanii wazuri sana hapa nchini kama wangeweza kuongeza juhudhi wangekuwa wa Kimataifa lakini bahati mbaya wamebweteka kwa sifa chache wanazopata hapa nchini. Kamati inawashauri wasanii hawa kujitathmini upya na pia kupanga mikakati ya namna ya kuinua tasnia zao ili ziweze kuwaletea maendeleo.

5.12.1 Wizi wa Kazi za Wasanii

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni jambo la kawaida kwa makampuni ya simu nchini kutumia miito ya simu kwa kutumia nyimbo za wasanii bila makubaliano yoyote baini ya msanii na kampuni. Kwa kutokuwepo makubaliano baina ya pande mbili kwa maana ya makampuni na wasanii huu unakuwa ni wizi wa wazi wa kazi za wasanii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Wizara ya Viwanda na Biashara kukutana na Shirikisho la Wasanii ili kupata namna bora ya kuwawezesha kupata ujira mzuri kwa kila wimbo wa msanii husika utakapotumika. Aidha kuwe na utaratibu wa TCRA kuweza kubaini kupitia njia za kieletroniki mara ngapi wimbo huo umetumika.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kukupongea kwa umahiri na busara zako katika uendeshaji wa Vikao vya Bunge. Nawapongea pia Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi wanavyokusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Kwa niaba ya Kamati, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Fenella Ephraim Mukangara (Mb) - Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; Naibu Waziri - Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia (Mb); Katibu Mkuu - Ndugu Sihaba Nkinga; Naibu Katibu Mkuu - Prof. Elisante Ole-Gabriel na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii, kwa ushirikiano mkubwa waliounesha wakati tunatekeleza shughuli za Kamati.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano mkubwa walionipatia katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

- | | |
|---|----------------|
| 1. Mhe. Said Mohamed Mtanda, Mb | - Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Capt. John D. Komba, Mb | - M/mwenyekiti |
| 3. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb | - Mjumbe |
| 4. Mhe. Mohamed Said Mohamed, Mb | - Mjumbe |
| 5. Mhe. Nasib Suleiman Omar, Mb | - Mjumbe |
| 6. Mhe. Mustafa Haidi Mkulo, Mb | - Mjumbe |
| 7. Mhe. Salum Halfan Barwany, Mb | - Mjumbe |
| 8. Mhe. Kiumbwa Makame Mbaraka, Mb | - Mjumbe |
| 9. Mhe. Salvatory Naluyaga Machemli, Mb | - Mjumbe |
| 10. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb | - Mjumbe |
| 11. Mhe. Moza Abedi Saidy, Mb | - Mjumbe |
| 12. Mhe. Agness Elias Hokororo, Mb | - Mjumbe |
| 13. Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb | - Mjumbe |
| 14. Mhe. Mary Pius Chatanda, Mb | - Mjumbe |
| 15. Mhe. Juma Othman Ali, Mb | - Mjumbe |
| 16. Mhe. Jaddy Simai Jaddy, Mb | - Mjumbe |
| 17. Mhe. Dkt. Maua Abeid Daftari, Mb | - Mjumbe |
| 18. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb | - Mjumbe |
| 19. Mhe. Rose Kamili Sukum, Mb | - Mjumbe |
| 20. Mhe. Joshua Samweli Nassari, Mb | - Mjumbe |
| 21. Mhe. Rosemary Kasimbi Kirigini, Mb | - Mjumbe |
| 22. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb | - Mjumbe |

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashillilah na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Ndugu Charles Mloka, Makatibu wa Kamati, Ndugu Hanifa Masaninka, Ndugu Abdallah Hancha na Ndugu Aziza Makwai, kwa ushauri na uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumalizia naomba niwashukuru wapigakura na wananchi wa Jimbo langu la Mbinga Magharibi/Nyasa kwa ushirikiano wao nami hadi tumeweza kufanikiwa na kuipata Wilaya Mpya ya Nyasa. Wito wangu kwao ni kwamba Nyasa itajengwa na Wananyasa wenywewe, na mkataa kwao ni mtumwa. Sote tuhamasike kuijenga Nyasa yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na ninaomba kuwasilisha.

Capt. John Damiano Komba, Mb

Nakala ya Mtando (Online Document)

MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII

29 Mei, 2014

SPIKA: Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Maoni ya Kambi juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2014/2015 - Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Kama Ilivyosomwa Bungeni

MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini kabla sijaendelea, siungi mkono hoja kwa sababu Wizara hii haina fedha na haitapata fedha hata walizoomba mwaka huu kutekeleza yale wanayosema watafanya.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nisome hotuba ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema na kwa kunitumia kama chombo cha mabadiliko katika kutetea haki za wanahabari, vijana, wanamichezo na wasanii. Namshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Freeman Mbewe kwa kuendelea kuwa na imani nami katika kuisimamia Serikali katika Wizara hii na kunitfea tena.

Aidha, napongeza hatua ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuungana kwa pamoja kwa maslahi ya wananchi wa Tanzania. Pia napongeza UKAWA kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwaelimisha wananchi nchi nzima. (Makofii)

Napenda kuchukua nafasi hii kutoa salamu za rambirambi kwa wasanii nchini kwa vifo vya waigizaji Adam Kuambiana na Rachel Haule vilivyotokea hivi karibuni na Marehemu wengine wote, Mungu azilaze Roho zao mahali pema peponi, Amen.

Mheshimiwa Spika, naomba kuanza hotuba hii kwa kumnukuu kwa kirefu mmoja wa viongozi wetu ambao wamejipambanua kwa namna ambayo wanastahili sifa za kuitwa statesmen. Mtu huyu sio mwingine bali ni Jaji Mark Bomani, ambaye hivi karibuni wakati akitoa hotuba kuadhimisha Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani, alinukuliwa na vyombo vya habari akisema:

Nakala ya Mtando (Online Document)

"Inasikitisha kuona kuwa hali ya Mtanzania inazidi kudidimia au kubaki pale pale katika sehemu nyingi hasa vijiji ni katika kipindi cha miaka 40 iliyopita kwa kukosa fursa muhimu za maendeleo na viongozi hawalioni hilo."

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari vilimnukuu zaidi Jaji Bomani akisema: "nchi itaendeshwa kwa kusimamia haki na ukweli na kuwataka wanahabari wasichoke kuisimamia haki na uhuru wa nchi yao bila uwoga, kwani bila kufanya hivyo, nchi itaongozwa kiimla. Ni aibu kuona Muswada wa sheria ya habari umekwama kwa zaidi ya miaka 10 kwa sababu ambazo hadi leo hazijaeleweka."

Mheshimiwa Spika, namnukuu Jaji; akawataka waandishi wa Habari wasikate tamaa na badala yake waendelee na kupambana kuhakikisha kwamba harakati za kupata Sheria ya Haki ya Kujua inafanikiwa ili kupunguza matukio ya manyanyaso, kupigwa, kuteswa, kufungwa kwa vyombo vya habari na kuuawa. Haki haiombwi, simamieni haki zenu na songeni mbele.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie kuhusu miaka 10 ya mapambano na ahadi za uongo uliofikia ngazi ya Kimataifa. Naomba kuchukua nafasi hii kuzungumzia vyombo vya habari. Kwanza, napenda kuvishukuru kwa kazi kubwa inayofanywa na muhimili huu usio rasmi katika kuimarisha demokrasia na kupigania umuhimu wa uongozi nchini kwetu.

Vyombo vya habari vimeduwa mstari wa mbele kuibua na kuweka bayana vitendo vya rushwa, ubadhirifu wa mali ya Umma na matumizi mabaya ya madaraka licha ya sheria mbaya na kandamizi ambazo zinaendelea kuminya uhuru wa habari na haki ya kupata habari kwa wanahabari na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa Kambi ya Upinzani Bungeni tumezungumza kwa kirefu, tukishauri, kutoa angalizo, kuonya na kuelekeza kwa mapana na mrefu kuhusu kufuta sheria kandamizi zilizopo zinazominya uhuru wa habari na kupata taarifa na badala yake zitungwe sheria nyingine ambazo zitaimarisha uhuru huo na kusaidia kukomaza demokrasia nchini. Mapambano haya ya wananchi kupigania uwepo wa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari na Haki ya Kupata Habari, siyo ya leo, yameanza tangu mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, katika namna ya kipekee ambayo ilipaswa kuungwa mkono na Serikali hii kama ingelikuwa ni sikivu, wadau wa habari kwa jitihada za kulisaidia Taifa lao, walichukua jukumu la kukusanya mawazo na mapendekezo ya wadau mbalimbali wa habari kuhusu namna ya kuboresha Miswada ambayo ilikuwa imeandaliwa na Serikali. Mapendekezo hayo yaliwasilishwa

Nakala ya Mtando (Online Document)

Serikalini tangu mwaka 2007 kwa Sheria ya Haki ya Kupata Habari na 2008 kwa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari.

Hatuna haja ya kurudia kusema juu ya danadana ambazo Serikali hii ya CCM imezifanya tangu wakati huo hadi nchi hii imeshindwa kuwa na sheria nzuri kama ilivyopendekezwa na wadau. Mwaka jana, 2013 wananchi walifarijika walipomsikia Rais, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete akitoa ahadi kwa maneno mazito mbele ya Mkutano wa Kimataifa kuwa Serikali ingeleta Muswada wa Sheria wa Haki ya kupata Taarifa ifikapo mwezi Aprili mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Kikwete alikuwa akihutubia Mkutano wa Kimataifa wa Serikali Uwazi ulioitishwa na Waziri Mkuu wa Uingereza, David Cameroun ambaao ulijadili masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwazi katika manunuzi ya Umma, uwazi katika mikataba, haki ya kupata habari, uwazi katika ukaguzi wa fedha za Umma, uwazi wa Serikali na vyombo vya habari, uwazi katika mikataba ya maliasili na uwazi katika maendeleo ya nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, watu wengi hawajui kuwa kabla ya kutoa ahadi hiyo nchini Uingereza ambako Rais Kikwete aliitangazia dunia kuwa Tanzania itatunga Sheria ya Uhuru wa Habari na kupata taarifa yenye viwango vya Kimataifa, pia aliwahi kutoa ahadi ya namna hiyo kwenye Mkutano kama huo nchini Brazil mwaka mmoja kabla, ambapo alisema hivi, nanukuu:

"Ninaahidi kuwa tutafanya kadri ya uwezo wetu wote kutimiza matarajio ya ushirikiano huu ili kuhamasisha uwazi na uwajibikaji wa Serikali yetu kwa wananchi wa Tanzania. Napenda kuwahakikisha kwamba, utashi wetu wa kisiasa kufanikisha malengo ya OGP hayatakwama kwa sababu dhana ya Serikali "Uwazi" iko kwenye moyo wa mkataba kati ya dola na wananchi." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Mwandishi katika gazeti la *The Guardian* aliandika akisema: "Je Tanzania inaweza kusimama imara kutekeleza maneno haya mazito?" Swali hilo linaweza kujibiwa na Viongozi wa Serikali hii ya CCM ambaao sasa siyo kwamba wanaweza kutoa ahadi za papo kwa papo na kuwahadaa Watanzania pekee, bali sasa wamevuka mipaka ya nchi na kutoa ahadi za uongo dunia nzima ikiwasikiliza. (Makof)

Siyo tu kwamba hawaoni tatizo kuahidi, bali sasa hawaoni shida hata kutotekeliza kila wanachoahidi. Hii ni dalili ya wazi ya ukosefu wa dhamira na uwezo wa kukidhi matarajio ya watu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, katika hali ambayo kwa kweli wadau wa habari nchini wanapaswa kuanza kumjua adui yao halisi kwenye mapambano ya kupata

Nakala ya Mtando (Online Document)

sheria hizi mbili muhimu, ni kitendo cha CCM kupitia kwenye vikao vyake vya ndani kutoa maelekezo kwa Wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba wanaotokana na Chama hicho na washirika wake ambayo kwa ujumla yanapingana na dhana nzima ya uwepo wa sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, hali hii siyo tu kwamba inawachanganya wananchi, lakini inaibua munkari wa kuhoji iwapo Mheshimiwa Rais Kikwete kupitia Serikali yake, wanayo dhamira ya kuheshimu na kutambua mchango wa vyombo vya habari na umuhimu wa wananchi kuwa na taarifa juu ya namna nchi yao inavyoendeshwa.

Ni suala linalochanganya na kuibua maswali mengi yasiyokuwa na majibu kuona Mheshimiwa Rais Kikwete anatoa ahadi Kimataifa kuhusu kukuza uwazi na uwajibikaji kwa kuimarisha uhuru wa habari na kupata taarifa, lakini wakati huo huo akiwa hapa nchini, Serikali yake kushindwa kutimiza ahadi hiyo, anasimamia vikao vya Chama chake ambacho kinapinga maoni ya Watanzania wanaotaka Katiba Mpya izingatie uwazi, uadilifu na uwajibikaji. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majibu ya Serikali yaliyotolewa hapa Bungeni kwenye Mkutano huu wa Kumi na Tano, Kikao cha Kumi na Sita kuhusu Miswada ya Sheria hizi mbili na Mwongozo ulioombwa na Mbunge wa Ubungo, Mheshimiwa John Mnyika na Serikali ikashindwa kutoa majibu ya kuridhisha; inazidi kudhihirisha kuwa Serikali haina dhamira ya dhati kutekeleza ahadi ya kuleta Muswada wa Habari na Sheria za Haki ya Kupata Taarifa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inalaani kwa nguvu zote, Sheria kandamizi zinazonyima vyombo vya habari uhuru wa kufanya kazi zake kwa ufanisi za kufichua maovu kama rushwa, ubadhifuru wa mali za Umma na hujuma za rasilimali za Taifa. Sheria hizo zinatishia uhuru wa uhariri na kuleta uwoga wa kushitakiwa kwa makosa ya jnai.

Mheshimiwa Spika, tuna wasiwasi mkubwa na nia ya Serikali ya kufanya mabadiliko stahiki. Tunaona hakuna dhamira ya dhati ya kuleta sheria bora. Hili limedhihirishwa na hatua ya Serikali ya mwezi Novemba, 2013 ya kuleta Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali (*Miscellaneous Ammendment Act*) ambayo ndani yake ilikuwa na mapendekezo ya Sheria ya Magazeti 1976, Sheria ya Filamu na Michezo ya Jukwaa na Sheria ya Kanuni za Adhabu ambazo zilikuwa na lengo ya kuongeza adhabu kubwa kwa makosa ya kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu uhuru wa uhariri, vitisho kwa waandishi na habari za utatu hatarishi. Katika hali ambayo imezidi kudhihirisha kuwa Serikali ya CCM inawalazimisha Watanzania kuendelea kuishi zama za

Nakala ya Mtando (Online Document)

mawe, mwezi Septemba, 2013, tasnia ya habari ilipata dhahama kubwa baada ya Serikali kupitia Wizara husika na Habari Maelezo, katika hali ambayo hadi sasa haijulikani ilikuwa kwa maslahi ya nani, ilihamua kufungia magazeti mawili ya Mtanzania na Mwananchi. Tunasema ni zama za mawe kwa sababu, vitendo vya kufungia vyombo vya habari kwa namna ambayo imekuwa ikifanywa na Serikali ya CCM ikitumia sheria zilizopitwa na wakati, ikiwa ni sehemu ya kubana uhuru wa maoni na utoaji wa fikra mbadala, vilifanywa enzi zile ambapo dunia ilikuwa inaaminishwa kuwa ina muundo wa meza siyo dunia duara.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ambayo iliendelea kutuanika namna tulivyokumbatia ukoloni na ukaburu, Serikali ya CCM ilijigeuza mlalamikaji, Polisi mkamataji, mwendesha mashtaka, Hakimu na kisha Askari Magereza mfungajji kisha kulifungia Gazeti la Mtanzania siku 90 na Mwananchi siku 14. (Makofii)

Kambi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kupitia kauli ya Serikali hapa Bungeni, mtindo huu wa udikteta unaofanywa na Serikali hii inayojiita sikivu inayoshughulikia vyombo vya habari, utaendelea hadi lini? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa sasa zipo fikra mionganini mwa wadau wa vyombo vya habari kwamba uhuru wa habari nchini unazidi kuwambwa msalabani kwa sababu ya utatu wa hatari amba ometengenezwa na Serikali ya CCM, kwenye Wizara ya Habari, Vijana, Michezo na Utamaduni. Utatu huu hatari unaundwa na Waziri mwenyewe Dkt. Fenela Mukangara ambaye mbali ya kwamba sio mwanahabari, sio mwanasanaa, sio mwanamuziki wala sio mwanamichezo na wala sio mwanasiasa, taarifa zinaonesha kuwa amekuwa na dhamira ya kupambana na vyombo vya habari, amba ni wadau wake tangu alipoteuliwa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Mkurugenzi wa Habari Maelezo kufanya maamuzi makubwa ya kuyatisha magazeti ya Mwananchi na Rai, kutimiza wajibu kuendelea kuhabarisha, kwanza bila kuwa na msingi wowote wa kisheria na bila kuwasiliana na wakubwa wake wala wasaidizi wake, kama ilivytamkwa na aliye kuwa Naibu Waziri Mheshimiwa Amos Makala, ni jambo ambalo linathibitisha jinsi alivyo sehemu ya utatu huu tunaouzungumzia hapa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, aliye kamilisha utatu unaoweka uhuru wa habari na uhariri kwenye hatihati ni Naibu Waziri, Mheshimiwa Alhaji Juma Nkamia. Kwa kauli zake mwenyewe hapa hapa Bungeni akisikiwa na Watanzania wote, wakiwemo wadau wa habari, alithibitisha jinsi alivyo na chuki dhidi ya waandishi wa habari.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, wakati Katibu Mkuu kiongozi anataja mabadiliko ya Baraza la Mawaziri Ikulu tarehe 19 Januari, 2014, akiwa amezungukwa na Wanahabari kutoka vyombo mbalimbali vya habari, wakati akitaja jina la Naibu Waziri Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Juma Nkamia; wanahabari hao waliguna na kucheka ikiwa ni ishara ya kutoridhishwa na uteuzi huo.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaungana na wana habari wote kwa kuguna na kuchekeshwa na uteuzi wa Mheshimiwa Juma Nkamia, ambaye ni dhahiri hana wala habari, bali ameitumia tasnia ya habari kama daraja lake la kufanikisha maslahi yake binafsi ya kisasa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, tarehe 17 Novemba, 2013, Baraza la Habari la Tanzania lilioneshwa kusikitishwa na kauli za Mheshimiwa Nkamia ambaye alitoa kauli ya kulikashifu Baraza hilo wakati akiwa katika vikao vya Bunge wakati yeye akiwa ni mmoja watu walionufaika na Baraza hilo. Akichangia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Nkamia alitamka kuwa MCT na TEF, yaani Baraza la Habari la Tanzania na Jukwaa la Wahariri Tanzania, ni sawa na asasi zisizo za Kiserikali NGO's, lakini zimekuwa zikijipa kazi ya kusimamia waandishi wa habari nchini.

Mheshimiwa Spika, ni kuwa kauli ya Mheshimiwa Nkamia ilikuwa ni ya kudharau dhidi ya wanahabari, dharau dhidi ya tasnia ya habari, dharau dhidi ya vyombo hivyo ambavyo kwa nyakati tofauti kabla na hata baada ya kupata Ubunge, Naibu Waziri alikuwa akizitambua na kushirikiano nazo.

Kwa kumbukumbu rasmi ni kuwa MCT na TF ndizo Taasisi zinazoendelea kupigania maslahi ya wanahabari dhidi ya uonevu unaofanyiwa Serikali hasa kwa wale ambao wana misimamo na msingi wa uadilifu, kwani vyombo hivyo ndivyo vilivyounda timu maalum ya uchunguzi kuchunguza mazingira yaliyopelekeea kuuawa kwa mwandishi wa habari, David Mwangosi Septemba 2, 2012, katika kijiji cha Nyololo, Wilaya ya Mufindi, Mkoani Iringa ambapo ripoti yake ilifichia kuwepo kwa mahusiano mabaya baina ya Waandishi wa Habari na aliyekuwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa ambaye aliulizwa maswali magumu na Marehemu Mwangosi ikiwemo ni kwanini Chama Tawala cha CCM kiko huru kufanya Mikutano ya Siasa wakati Chama cha Upinzani kama CHADEMA kinawekewa vikwazo na Polisi kila wakati?

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri amesahau kuwa anazoziita Taasisi hizo za Kiserikali ndizo zilizochangia kwa mapinduzi katika Sekta ya Habari nchini kwa kufanikisha mambo muhimu ikiwemo kusimamia maadili ya Waandishi wa Habari, kuandaa mitaala kuwafundishia Waandishi wa Habari ambayo imepitishwa na Baraza la Elimu la Taifa. Pia kutumiwa na Viongozi Wakuu wa

Nakala ya Mtando (Online Document)

Serikali na wanasiasa kama kwa aliyejikuwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Omar Ali Juma na Mawaziri Wakuu waliopita; Mheshimiwa Edward Lowassa, pamoja na Mheshimiwa Fredrick Sumaye katika kusuluuhisha migogoro inayohusiana na tasnia ya habari. Inakuwaje yeye binafsi avipuuze vyombo hivyo muhimu na ndiyo maana kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri kuliwashangaza wanahabari na wadau wa habari.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa nyakati tofauti Naibu Waziri amekuwa akiwaita Waandishi wa Habari kuwa ni waandishi makanjanja naye kujinasibu kuwa ni mwandishi mwenye weledi na taaluma. Kambi Rasmi ya Upinzani ina ushahidi kuwa Mheshimiwa Nkamia amelidanganya Bunge na Taifa kwa ujumla kwa kutuaminisha kuwa yeye alikuwa ni mfanyakazi mwajiriwa wa Shirika la Habari la Uingereza BBC kitengo cha Propaganda, wakati Tirdo Muhandi ambaye amefanya kazi na Shirika hilo kwa takriban miaka 20 alikana kujua uwepo wa kitengo hicho katika Shirika hilo na zaidi kueleza kuwa Mheshimiwa Nkamia hakuwa mwajiriwa wa kitengo hicho bali aliitwa kwenda kusoma taarifa za habari tu kama kibarua jambo ambalo hajawahi kusema hadharani. (Makofij)

Hivyo mbwembwe zote za Naibu Waziri zilikuwa ni kumhadaa Mheshimiwa Rais Kikwete ili apate uongozi kwa sifa asizostahili. Kambi Rasmi Bungeni inauliza: Je, waandishi wa habari wakiitwa makanjanja ninyi viranja wao ni nani? (Makofij)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaikumbusha Serikali na Waheshimiwa Wabunge kwamba, Sera ya zamani ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 1999 ilitamka kwamba kutaanzishwa Baraza la vijana na suala hilo kurudiwa katika sera mpya ya mwaka 2007. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikikwepa kuhakikisha kwamba matakwa hayo ya sera tajwa yanatekelezwa pamoja na kuwa suala hilo linahusu mustakabali wa maendeleo ya vijana nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani inaikumbusha pia kwamba katika llani za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 Vyama mbalimbali viliahidi kuhakikisha kwamba Baraza la Vijana la Taifa linaundwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji ni kwanini kwa mwaka wa fedha 2013/2014 jumla ya fedha zilizopelekwa kwenye vikundi mbalimbali kwa kupitia Mfuko wa Vijana ni Shilingi bilioni 72 tu, sawa na asilimia 2.82 kati ya Shilingi bilioni 6.1 ambazo Serikali mwaka 2013 iliwasanganya vijana kuwa itatenga. Huku taarifa ikionyesha kwa kiasi cha Shilingi bilioni mbili sawa na asilimia 32.7 pekee ndizo zilizokuwa zimepokelewa hadi kufikia Aprili, 2014. Je, kiasi cha Shilingi bilioni 827.4 zimetumikaje? (Makofij)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Je, Serikali itaacha lini kuwahadaa vijana kuwa wanatenga mabilioni ili kuwanyamazisha katika kudai haki zao, huku ikijua kuwa haiwezi kuwasaidia hata kwa kile wanachostahili? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, lingine ni sanaa na usanii kutambuliwa kama sekta ya uchumi, ulinzi wa wamiliki bunifu kuboreshwa kuinua vipato vyta wasanii na mapato kwa nchi.

Kambi ya Rasmi Bungeni ina taarifa juu ya maoni ambayo wasanii waliwasilisha mbele ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba na baadaye kwa baadhi ya Wabunge ikiwemo upinzani kutaka wasanii watambuliwe kama kundi maalum katika Katiba mpya kama ilivyo kwa wafugaji, wakulima na fani au tasnia nyingine. Aidha, wasanii wamependekeza kwamba Rasmu ya Katiba mpya itaje mmiliki bunifu, yaani *intellectual property right*.

Mheshimiwa Spika, kutokana umuhimu wa mapendelekezo ya wasanii hao waliyoyatoa kupitia mashirikisho yao manne; shirikisho la filamu, shirikisho la muziki, shirikisho la sanaa na maonesho na shirikisho la sanaa za ufundi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa maoni kwa Serikali kwamba haipaswi kusubiri mpaka mchakato wa mabadiliko ya Katiba bali marekebisho ya msingi ya kisheria yanapaswa kuharakishwa kuwezesha sanaa na usanii kuchangia katika kuongeza ajira, kuboresha maisha ya wasaani na kuchangia kwa kiwango kikubwa katika mapato ya Serikali na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitazama sanaa kama suala la burudani zaidi badala ya kuitazama kama ni sekta muhimu ya kiuchumi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuzingatia kwamba wasanii sio wanamuziki tu, wasanii wapo karibu katika kila kaya Tanzania, wakiwepo wafinyazi, wasusi, wapambaji, wanamuziki, waigazaji, mafundi mbalimbali wa ushonaji, ujenzi na kadhalika. Wako wengi wala hata wao hawajitambui kama ni wasanii kutokana na mazingira waliyonayo.

Mheshimiwa Spika, kuna hasara nyingi ambazo hupatikana kama nchi haina ulinzi wa miliki bunifu, yaani *intellectual property right*. Mifano michache hapa Tanzania ni kama kupoteza kwa miliki bunifu wa jina Tanzanite ambayo licha ya kuwa inachimbwa Tanzania tu, lakini jina linamilikiwa na Kampuni ya Afrika Kusini.

Vazi la kikoi pamoja na kuwa ni la asili ya Tanzania, miliki bunifu imesajiliwa Kenya; staili ya michoro maarufu ya Tingatinga, miliki bunifu yake iko Japan. Haya ni machache ambayo yameshtukiwa; miliki bunifu ikifuatiwa vizuri ndipo hasa ukubwa wa tatizo utakapo julikana. (Makofii)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kuna ulazima mkubwa wa kutaja miliki bunifu katika sheria zote muhimu na kuainisha ulazima wa kulinda na kuendeleza na kuwezesha wabunifu wa nchi kwa manufaa kwa ya kizazi hiki na vizazi vijavyo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeendelea kuona umuhimu wa Taifa kuwekeza katika viwanja vya michezo ili kuweza kupanua wigo wa Taifa kujitangaza na kukusanya mapato yanayotokana na viwanja vya michezo nchini. Labda Wizara mpaka sasa haijaweza kujua hasara ambazo kama Taifa tunapata kutokana na kutotumia nafasi zinazojitokeza na kutowekeza vya kutosha katika kuboresha michezo nchini.

Mheshimiwa Spika, enzi za Chama kimoja majengo na maeneo yote ya Umma yalikuwa chini ya Serikali. Ujenzi na uendelezaji wa maeneo hayo ulifanywa na Serikali kupitia kodi za wananchi, michango, fedha za wananchi na hisani mbalimbali. Hata baada ya uwepo wa Vyama vingi, uendelezaji wa miradi yote iliyokuwa chini ya Chama kimoja ilifanywa kuwa ni jambo la kitaifa.

Kwa namna isiyoeleweka, baadhi ya maeneo ambayo CCM imeshindwa kuyarudisha kwa wananchi na kuwa mali ya Umma na kuyafanya ni mali ya Chama chao, ni pamoja na uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza; Uwanja wa Samora, Iringa; Uwanja wa Sokoine, Mbeya; Sheikh Amri Abeid Arusha; Majimaji, Songea; Kaitaba, Kagera; na Kadhalika. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, pamoja na CCM kuendelea kuhodhi viwanja hivi imeshindwa kuviedeleza na matokeo yake ni kuwanyima fursa wananchi wa maeneo husika kushuhudia michezo mbalimbali kwa kuwa viwanja hivyo huwa viwango vya ubora vya michezo, hali inayofanya michezo mingi mikubwa ikiwemo ya Kimataifa kufanyika Dar es Salaam pekee.

Kambi Rasmi ya Upinzani inarudia tena kuitaka Serikali kuvirudisha viwanja vyote vinavyohodhiwa na CCM kwa wananchi ili viendelezwe kwa kupitia mamlaka ya viwanja vya michezo nchini kama tulivyopendekeza mwaka 2013. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kitendo cha mechii ya Taifa Stars na Zimbambwe kuhamishwa kutoka uwanja wa Sokoine Mbeya tarehe 18 Mei, 2014 na kuhamishiwa uwanja wa Taifa Dar es Salaam; kwanza, kimewavunja moyo mashabiki wa mpira na wakazi wa Mbeya ambao walijiandaa kuonyesha uzalendo kwa Taifa lao.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Kutokana na kitendo cha mechi hii kuhamishwa, wana Mbeya tulikoseshwa fursa ya kujitangaza kiutalii na hatimaye kuchangia katika uchumi kulikosababishwa na Serikali ya CCM kuendelea kuhodhi viwanja vya michezo nchini. Rudisheni viwanja vya wananchi ili viendelezwe kuwanufaisha wananchi. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu kambi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikipingana na utumiaji wa fedha za walipa kodi na kitendo cha Serikali kuendelea kuwatoza wananchi kwa mashinikizo bila ridhaa zao kuchangia shughuli za mbio za Mwenge wa Uhuru.

Ni kweli kuwa Mwenge wa uhuru ni hazina ya Taifa letu, jambo ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani inakubaliana nalo kwa na muda mrefu tumepeendekeza mwenge wa uhuru uwekwe katika makumbusho ya Taifa ili kuweza kuwapatia fursa wananchi kuweza kujifunza kutoka hapo.

Mheshimiwa Spika, suala la kuenzi la utamaduni wa Taifa hili ni la lazima lakini kuendelea kutumia gharama kubwa kwa jambo hili wakati Watanzania wengi hawana huduma muhimu ni dharau kubwa.

Aidha, katika kipindi hiki ambacho mwenge wa uhuru unapitishwa katika sehemu mbalimbali za nchi, Chama Tawala nacho kinapita katika maendeleo mbalimbali na kuangalia utekelezaji wa ilani jambo ambalo ni pamoja na kuzindua miradi ya maendeleo ya wananchi.

Huu ni usanii ukubwa unaofanywa na Seriakli ya Chama cha Mapinduzi kwa dhumiuni ya kuwanyonya wananchi masikini kwa kigezo cha kuwa wanachangia shughuli za maendeleo wakati ukweli ni kuwa Watanzania wanachangishwa mpaka fedha kwa ajili ya malazi na chakula kwa wakimbiza Mwenge kama alivyojibu Waziri Mkuu juzi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara, wafanyakazi wa Serikali na hasa Walimu sehemu mbalimbali nchini kuwa wanalazimishwa kuchangia Mwenge bila ridhaa yao na kama CCM inataka bado, mambo ya mbio za mwenge, basi wagħaramie wenywew kwa asilimia 100 na siyo kuwalazimisha wananchi kuchangia hasa ukizingatia kuwa Waziri Mkuu alitoa kauli wiki hii kuwa kuchangia mbio za mwenge wa uhuru ni hiari.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaendelea kusitiza kuwa ni wakati muafaka Mwenge wa Uhuru kupelekwa jumba la makumbusho ya Taifa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuhitimisha hoja za Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kulitaka Bunge lako Tukufu sasa kuishinikiza Wizara hii kutekeleza maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambayo Wizara hii imekuwa ikiyakubali kwa muda wa miaka mitatu mfululizo sasa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, alutakotinyua! Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (Makofii)

SPIKA: Ahsante. Hotuba zinazosema watu mara nyingi zinakuwa kidogo na kasoro! Kusema watu katika Bunge, tena afadhali mseme walio nje, maana yake malalamiko ya watu walio nje kulalamika kama Bunge langu linawatukana ni mengi. Nafikiri siyo tabia njema kusema watu.

Kwa hiyo, tutakuwa na wachangiaji wafuatao, tutakuwa na AnnaMaryStella, yupo nafikiri, atakuwepo Mheshimiwa Ester Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Catherine Magige na wengine nitawataja kadiri muda utakavyoruhusu. AnnaMaryStella yupo? Okay!

Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2014/2015 - Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kama ilivyowasilishwa Mezani

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI MHESHIMIWA JOSEPH O.
MBILINYI (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA
HABARI, VIJANA,
UTAMADUNI NA MICHEZO KWA MWAKA WA
FEDHA 2014/2015**

*(Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya kanuni
za Bunge toleo la mwaka 2013)*

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema na kwa kunitumia kama chombo cha mabadiliko hasa katika

Nakala ya Mtando (Online Document)

kutetea haki za wanahabari, vijana, wanamichezo na wasanii. Namshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Mhe. Freeman A. Mbwe kwa kuendelea kuwa na imani nami katika kuisimamia Serikali katika wizara hii. Aidha, napongeza hatua ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuungana kwa pamoja kwa maslahi ya wananchi wa Tanzania. Napongeza UKAWA kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwaelimisha wananchi nchi nzima. Napenda kuchukua nafasi hii kutoa salamu za rambirambi kwa wasanii nchini kwa vifo vya waigizaji Adam Kuambiana na Rachel Haule vilivyotokea hivi karibuni. Mungu azilaze Roho za Marehemu mahali pema peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika **naomba kuanza hotuba hii kwa kumnukuu kwa kirefu mmoja wa viongozi wetu ambao wamejipambanua kwa namna ambayo wanastahili sifa za kuitwa 'statesmen'**, mtu huyu si **mwingine bali ni Jaji Mark Bomani, ambaye hivi karibuni wakati akitoa hotuba kuadhimisha Siku ya Uhuru wa Vyombo Duniani, alinukuliwa na vyombo vya habari akisema;**

"Inasikitisha kuona kuwa hali ya Mtanzania inazidi kudidimia au kubaki pale pale katika sehemu nyingi hasa vijijini katika kipindi cha miaka 40 iliyopita kwa kukosa fursa muhimu za maendeleo na viongozi hawalioni hilo."

Vyombo vya habari vilimnukuu zaidi Jaji Bomani akisema "nchi itaendeshwa kwa kusimamia haki na ukweli na kuwataka wanahabari wasichoke kuisimamia haki na uhuru wa nchi yao bila woga kwani bila kufanya hivyo nchi itaongozwa kiimla.

"Ni aibu kuona mswaada wa sheria ya habari umekwama kwa zaidi ya miaka 10 kwa sababu ambazo hadi leo hazijaeleweka." Akawataka waandishi wa habari,

"wasikate tamaa na badala yake waendelee na kupambana kuhakikisha kwamba harakati za kupata Sheria ya Haki ya Kujua inafanikiwa ili kupunguza matukio ya manyanyaso, kupigwa, kuteswa, kufungwa kwa vyombo vya habari na kuuwawa."

"Haki haiombwi simamieni haki zenu na songeni mbele."

2.0 MAENDELEO YA SEKTA YA HABARI NCHINI

2.1 Miaka 10 ya mapambano na ahadi za uongo uliofika ngazi ya kimataifa

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuzungumzia vyombo vya habari. Kwanza napenda kuvishukuru kwa kazi kubwa inayofanywa na 'mhimili'

Nakala ya Mtando (Online Document)

huu usio rasmi katika kuimarisha demokrasia na kupigania umuhimu wa uongozi nchini kwetu.

Vyombo vya habari vimeduwa mstari wa mbele kuibua na kuweka bayana vitendo vya rushwa, ubadhirifu wa mali ya umma na matumizi mabaya ya madaraka licha ya sheria mbaya na kandamizi ambazo zinaendelea kuminya uhuru wa habari na haki ya kupata habari kwa wanahabari na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa Kambi ya Upinzani Bungeni tumezungumza kwa kirefu, tukishauri, kutoa angalizo, kuonya na kuelekeza kwa mapana na marefu kuhusu kufuta sheria kandamizi zilizopo zinazominya uhuru wa habari na kupata taarifa na badala yake zitungwe sheria zingine ambazo zitaimarisha uhuru huo na kusaidia kukomaza demokrasia nchini. Mapambano haya ya wananchi kupigania uwepo wa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari na Haki ya Kupata Habari si ya leo. Yameanza tangu mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, katika namna ya kipekee ambayo ilipaswa kuungwa mkono na serikali hii kama ingelikuwa ni sikivu, wadau wa habari kwa jitihada za kulisaidia taifa lao, walichukua jukumu la kukusanya mawazo na mapendekezo ya wadau mbalimbali wa habari kuhusu namna ya kuboresha miswada ambayo ilikuwa imeandalishiwa na serikali. Mapendekezo hayo yaliwasilishwa serikalini tangu mwaka 2007 kwa sheria ya Haki ya Kupata habari na 2008 kwa sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari.

Hatuna haja ya kurudia kusema juu ya danadana ambazo Serikali hii ya CCM imezifanya tangu wakati huo hadi sasa nchi imeshindwa kuwa na sheria nzuri kama ilivyopendekezwa na wadau. Mwaka jana wananchi walifarijika walipomsikia Rais Jakaya Kikwete akitoa ahadi kwa maneno mazito mbele ya mukutano wa kimataifa kuwa serikali ingeleta muswada wa Sheria wa Haki ya kupata Taarifa ifikapo mwezi Aprili mwaka huu!

Mheshimiwa Spika, Rais Kikwete alikuwa akihutubia Mkutano wa Kimataifa wa Serikali Uwazi ulioitishwa na Waziri Mkuu wa Uingereza, David Cameroun ambao ulijadili masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwazi katika manunuvi ya umma, uwazi katika mikataba, haki ya kupata habari, uwazi katika ukaguzi wa fedha za umma, uwazi wa Serikali na vyombo vya habari, uwazi katika mikataba ya maliasili, uwazi katika maendeleo ya nchi zinazoendelea.

Akizungumza kwenye mukutano huo Alhamis ya Oktoba 31, Rais Kikwete si tu kwamba aliwaahidi Watanzania bali pia alitumia jukwaa hilo la kimataifa kuitangazia dunia nzima kuwa Serikali yake tayari inafanya kazi utungaji wa

Nakala ya Mtando (Online Document)

Sheria ya Kupata Taarifa, kwa ajili ya kuwapatia wananchi haki ya kupata taarifa kutoka serikalini.

Vyombo vya habari mbalimbali, vya ndani na nje ya nchi, vilimnukuu Rais Kikwete akitoa ahadi hiyo, kwa kusema;

"Kama watu wanataka kupata taarifa kuhusu namna gani dawa zinagawanywa, kama wanataka kupata taarifa kuhusu bajeti za shule zao za msingi, wanastahili kuwa na haki ya kuzipata. Kama watu wanataka kupata taarifa kuhusu lini watasambaziwa maji wanapaswa kuwa na haki hiyo. Pale watu wanapotaka kupata taarifa, haipaswi kuonekana kuwa wanaingia mahali ambapo hapawahuusu."

Gazeti la The Guardian likiandika kuhusu ahadi hiyo ya Serikali ya CCM, lilisema hivi;

"Ahadi hii inawakilisha moja ya hatua kubwa kuelekea haki ya kupata taarifa na suala la Serikali Uwazi nchini Tanzania. Hata hivyo, kama ilivyo ada siku zote, jaribio halisi litakuwa ni katika utekelezaji (wa ahadi hiyo)."

Watu wengi hawajui kuwa kabla ya kutoa ahadi hiyo nchini Uingereza ambako Rais Kikwete alitangazia dunia kuwa Tanzania itatunga sheria ya uhuru wa habari na kupata taarifa yenye viwango vya kimataifa, pia aliwahi kutoa ahadi ya namna hiyo hiyo kwenye mkutano kama huo, nchini Brazil mwaka mmoja kabla ambako alisema hivi;

"Ninaahidi kuwa tutafanya kadri ya uwezo wetu wote kutimiza matarajio ya ushirikiano huu ili kuhamasisha uwazi na uwajibikaji wa serikali yetu kwa wananchi wa Tanzania. Napenda kuwahakikisha kwamba utashi wetu wa kisiasa kufanikisha malengo ya OGP hayatakwama kwa sababu dhana ya Serikali Uwazi iko kwenye moyo wa mkataba katika dola na wananchi."

Mwandishi katika Gazeti hilo la The Guardian akamalizia kwa kusema:

"Je Tanzania inaweza kusimama imara kutekeleza maneno haya mazito?"

Swali hilo linaweza kujibiwa na viongozi wa Serikali hii ya CCM ambao sasa si kwamba wanaweza kutoa ahadi za papo kwa papo za kuwahadaa Watanzania pekee, bali sasa wamevuka mipaka ya nchi na kutoa ahadi za uongo dunia nzima ikiwasikiliza. Si tu kwamba hawaoni tatizo kuahidi, bali sasa

Nakala ya Mtando (Online Document)

hawaoni shida hata kutoteketeza kila wanachoahidi. Hii ni dalili ya wazi ya ukosefu wa dhamira na uwezo wa kukidhi matarajio ya watu.

Mheshimiwa Spika, katika hali ambayo kwa kweli wadau wa habari nchin wanapaswa kuanza kumjua adui yao halisi kwenye mapambano ya kupata sheria hizi mbili muhimu, ni kitendo cha CCM kuititia kwenye vikao vyake vya ndani kutoa maelekezo kwa Wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba wanaotokana na chama hicho na washirika wake, ambayo kw aujumla yanaingana na dhana nzima ya uwepo wa sheria hizo.

Katika waraka wake wa siri ambao umeripotiwa mara kadhaa na vyombo mbalimbali vya habari, CCM imeamua kujandikia rasimu nyingine ambayo chama hicho ndiyo kinataka eti Katiba Mpya ya nchi. Katika nyaraka hiyo, vikao vya CCM ambavyo vinaongozwa na Mwenyekii wake Jakaya Kikwete, kimepinga dhana za uwazi, uadilifu na uwajibikaji kama ambavyo zimependekezwa na wananchi ili ziwe sehemu ya tunu za taifa ndani ya katiba.

Mheshimiwa Spika, hali hii si tu kwamba inawachanganya wananchi, lakini inaibua munkari wa kuhoji iwapo Rais Kikwete kuititia serikali yake, wanayo dhamira ya kuheshimu na kutambua mchango wa vyombo vya habari na umuhimu wa wananchi kuwa na taarifa juu ya namna nchi yao inavyoendeshwa! Ni suala linalochanganya na kuibua maswali mengi yasiyokuwa na majibu kuona Rais Kikwete anatoa ahadi kimataifa kuhusu kukuza uwazi na uwajibikaji kwa kuimarisha uhuru wa habari na kupata taarifa, lakini wakati huo huo akiwa hapa nchini bali ya serikali yake kushindwa kutimiza ahadi hiyo, anasimamia vikao vya chama chake ambacho kinapinga maoni ya Watanzania wanaotaka Katiba Mpya izingatie uwazi, uadilifu na uwajibikaji!

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majibu ya Serikali yaliyotolewa hapa bungeni kwenye mkutano huu wa 15 kikao cha 16 kuhusu miswada ya sheria hizi mbili na mwongozo ulioombwa na Mbunge wa Ubungo John Mnyika na Serikali ikashindwa kutoa majibu ya kuridhisha, inazidi kudhihirisha kuwa hakuna dhamira ya dhati kutekeleza jambo hili. Sasa maelezo ya Mheshimiwa waziri wa Sheria na Katiba, Dr. Asha Rose Migiro katika hotuba ya Makadirio ya wizara yake ni kuwa waraka wa kupeleka kwenye Baraza la Mawaziri wa kupendekeza kutungwa kwa Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa umeandaliwa.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitarajia Serikali ya CCM kutambua umuhimu wa kutekeleza ahadi zake hapa bungeni kwa miaka 7 lakini zaidi ya hapo kutimiza ahadi iliyotolewa na Rais Kikwete ili kumwokoa na aibu ya kusema uongo kwenye mkutano mkubwa wa kimataifa wa Open Government Partnership, mjini London. Tulitarajia Serikali hii ingelikuwa sikivu, ingetambua kuwa sheria hizo ni mtambuka na inahusu wananchi wote katika haki ya kupata

Nakala ya Mtando (Online Document)

na kutoa taarifa kama ilivyoelekezwa na Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inalaani kwa nguvu zote, sheria kandamizi zinazonyima vyombo vya habari uhuru wa kufanyakazi zake kwa ufanisi, za kufichua maovu kama rushwa, ubadhirifu wa mali za umma na hujuma za raslimali za taifa. Sheria hizo zinatishia uhuru wa uhariri na kuleta woga wa kushtakiwa kwa makosa ya jinai.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa ahadi ya kuleta Bungeni muswada wa sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ambazo zitasimamia utendaji kazi wa vyombo vya habari nchini. Wote tunafahamu kuwa sheria zilizopo zinazosimamia vyombo vya habari ni mbaya, ni kandamizi na hazina nafasi katika nchi inayojinadi kuwa ni ya kidemokrasia. Sheria hizi zinavifanya vyombo vya habari na wanahabari kutekeleza majukumu yao katika mazingira magumu. Katika vikao vya bunge kwa takriban miaka saba sasa, tumekuwa tukisikia ahadi za serikali ya kubadilisha sheria hizi kandamizi ambazo kwa kiasi kikubwa zinakiuka Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tunawasiwasi mkubwa wa nia ya serikali ya kufanya mabadiliko stahiki. Tunaona hakuna dhamira ya dhati ya kuleta sheria bora. Hili limedhihirishwa na hatua ya serikali ya mwezi Novemba mwaka 2013 ya kuleta mabadiliko ya sheria mbalimbali (Miscellaneous Ammendment Act) ambayo ndani yake ilikuwa na mapendekezo ya Sheria ya Magazeti 1976, Sheria ya Filamu na Michezo ya Jukwaa na Sheria ya Kanuni za Adhabu ambazo zilikuwa na lengo ya kuongeza adhabu kubwa kwa makosa ya kitaduma.

Ni muhimu sana kwa Serikali kuacha kutoa ahadi hewa hapa Bungeni na kwingineko na badala yake tudhihirishe utashi wetu kwa kutekeleza kwa vitendo. Ahadi zinazotolewa na mawaziri miaka nenda miaka rudi hapa Bungeni bila kutekelezwa zinashusha hadhi ya Bunge na Taifa letu machoni mwa watanzania na dunia kwa ujumla. Ni jambo lisilopendeza na ni la aibu kwa kweli kwani inaonyesha dhahiri kuwa ama utendaji kazi ni hafifu sana katika serikali hii au la basi Serikali hii haina nia njema ya kufanya marekebisho ya kimfumo ili tuwe na sera na sheria nzuri ambazo zitastawisha demokrasia, uwazi na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inawataka mawaziri husika wawe jasiri na watimize ahadi walizotoa kwenye Bunge hili tukufu za kuleta miswada ya sheria za Haki ya Kupata Taarifa na ule wa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari. Wadau wa habari wameshafanya kazi kubwa kwa kutoa mapendekezo yao serikalini. Wayatumie mapendekezo hayo kuandika miswada hiyo na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wadau wa habari wamejipanga kuboresha na kuinua hali ya uwajibikaji na maadili katika vyombo vya habari. Tuwaunge mkono kwa dhati kwenye hilo. Kupitia Baraza lao la habari wamepitisha Azimio la Dar es Salaam ambalo linazungumzia haki na wajibu wa vyombo vya habari katika kuimarisha weledi, maadili na uhuru wa uhariri.

Napenda niongeze kwa lengo ya kuweka msisitizo kuwa Haki ya Kupata Taarifa ni muhimu na ya msingi sana, kwani ni sheria mtambuka na inahusu haki ya msingi ya kupata habari ambayo ni haki inayolindwa kikatiba. Ni ukweli wa uhakika kuwa utawala ulioshamiri katika mila za usiri ndio ulioifikisha Tanzania yetu mahali hapa pabaya. Ndio chanzo cha mikataba mibovu na kushindwa kwa uwajibikaji kwa sababu tu watendaji wabovu wanaweza kujificha katika kinga ya usiri. Kambi Rasmi ya Upinzani tunaitaka Serikali kuleta Bungeni muswada wa sheria ya Haki ya Kupata Habari ndani ya mwaka huu kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasisitiza tena kuwa uwepo wa sheria nzuri za vyombo vya habari ambayo itakuwa kwa manufaa ya wananchi na serikali. Wakati wananchi wanasubiri sheria mpya ya Huduma za Vyombo vya Habari, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuleta Bungeni Muswada wa kufuta Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 pamoja na kufanya marekebisho sheria nyingine 17 zenye vipengele kandamizi kwa vyombo vya habari kwa kuwa sheria hizo ni kinyume na Katiba ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Pia sheria hizo zinaendeleza utamaduni wa usiri amba kama nilivyosema awali unasaidia sana kufanya viongozi wasiwajibike ipasavyo na kufanya mambo yasiyostahili kwa kujificha kwenye kinga ya usiri.

2.2 Uhuru wa uhariri, vitisho kwa waandishi wa habari na utatu hatarishi

Mheshimiwa Spika, katika hali ambayo imezidi kudhihirisha kuwa Serikali ya CCM inawalazimisha Watanzania kuendelea kuishi 'zama za mawe', Mwezi Septemba mwaka jana, tasnia ya habari ilipata dhahama kubwa baada ya Serikali kupitia wizara husika na Habari Maelezo, katika hali ambayo hadi sasa haijulikani ilikuwa kwa maslahi ya nani, iliamua kufungia magazeti mawili ya Mtanzania na Mwananchi. Tunasema ni zama za mawe kwa sababu, vitendo vya kufungia vyombo vya habari kwa namna ambayo imekuwa ikifanywa na Serikali ya CCM ikitumia sheria zilizopitwa na wakati, ikiwa ni sehemu ya kubana uhuru wa maoni na utoaji wa fikra mbadala, vilifanywa enzi zile ambapo dunia ilikuwa inaaminishwa kuwa ina muundo wa meza.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ambayo iliendelea kutuanika namna tunavyokumbatia ‘ukoloni na ukaburu’, Serikali ya CCM ilijigeuza mlalamikaji, polisi (mkamataji), mwendesha mashtaka, hakimu na kisha askari magereza (mfugaji) kisha kulifungia Gazeti la Tanzania siku 90 na Mwananchi siku 14. Kambi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kupitia kauli ya serikali hapa bungeni, mtindo huu wa udikteta unaofanywa na serikali hii inayojiita siku inayoshughulikia vyombo vya habari, utaendelea hadi lini?

Mheshimiwa Spika, kwa sasa zipo fikra mionganini mwa wadau wa vyombo vya habari kwamba uhuru wa habari nchini unazidi ‘kuwambwa msalabani’ kwa sababu ya utatu wa hatari ambao umetengenezwa na Serikali ya CCM, kwenye Wizara ya Habari, Vijana, Michezo na Utamaduni. Utatu huu hatari unaundwa na waziri mwenyewe Dk. Fenella Mukangara ambaye mbali ya kwamba si mwanahabari, si mwanasanaa, si mwanamziki wala si mwanamichezo, taarifa zinaonesha kuwa amekuwa na dhamira ya kupambana na vyombo vya habari, ambao ni wadau wake, tangu alipoteuliwa.

Mheshimiwa Spika, Akiandika kwenye safu yake, mmoja wa waandishi waandamizi nchini, alikuwa na haya ya kusema juu ya Dk. Mukangara;

“Waziri mwenye dhamana Dk. Fenella Mukangara kwa muda mrefu amekuwa na nia ovu dhidi ya vyombo vya habari. Julai mwaka jana (akimaanisha 2012) tukiwa Hotelki ya Dodoma mjini Dodoma, wakati tunafanya mazungumzo rasmi na Waziri Mukangara, walikuwepo Theophil Makunga, Pili Mutambalike, Neville Meena na marehemu Alfred Mbogola na wengine, Dk. Mukangara alitoa kauli iliyotushtua wengi na sasa ndipo tunaona inatekelezeka kwa vitendo.”

Mwandishi huyo aliongeza kwa kunukuu maneno ya Waziri Mukangara ambaye amenukuliwa akisema;

“Nikipata fursa Mwananchi nitalifuta, mimi linanikera sana. Tena na Nipashe nao naona wanakuja, ikibidi nitawafungia tu, mimi siogopi kitu.” Hayo ni maneno ya Waziri anayetakiwa kuwa mlezi wa vyombo vya habari!

Mwandishi huyo katika makala yake akaendelea kuandika hivi;

“Baada ya kauli hii tulienendelea na mazungumzo mengine, lakini Meena akatwambia kuwa Dk. Mukangara aliwahi kutoa kauli kama hii ofisini kwake walipokwenda akina Jesse Kwayu, Meena na Absalom Kibanda

Nakala ya Mtando (Online Document)

kuomba Gazeti la Mwanahalisi lifunguliwe. Mwanahalisi alilifungia kwa muda usiojulikana...”.

Mheshimiwa Spika, si Waziri Mukangara mwenyewe wala mtu mwingine ye yote kwa niaba yake, amewahi kukanusha maneno hayo aliyonukuliwa akiyasema hadharani mbele ya wadau ambao yeye anapaswa kuwa kiongozi na mlezi wao. Kuto kana na mwenendo wa Waziri Mukangara wa kupamabana na vyombo vya habari, unaofumbiwa macho na mamlaka iliyomteua, labda kwa bahati mbaya au sehemu ya mkakati wa serikali hii ya CCM. Uhusiano wa waziri na vyombo vya habari ulifikia hatua mbaya zaidi, baada ya wadau wa habari waliokutana Oktoba 9 mwaka jana, kufikia maazimio kadhaa, ikiwemo lile linalosema;

“Kusitisha kuandika, kutangaza na kupiga picha shughuli zozote zitakazowahuishaa au kuratibiwa na Mheshimiwa Fenella Mukangara na Assah Mwambene hadi hapo itakapotangazwa vinginevyo. Adhabu hiyo inaanza mara moja kuanzia leo.”

Mheshimiwa Spika, hapo juu kwenye moja ya maazimio ya wadau wa habari, ametajwa Assah Mwambene, huyu ni Mkurugenzi wa Habari Maelezo. Mkurugenzi huyu ambaye amewahi kufanya kazi kwenye vyombo vya habari kama mwandishi, pamoja na kwamba kwa majukumu yake hayo alipaswa kuwa mtu wa karibu kama mwelekezi na kiongozi kwa wadau wake, kwa kushirikiana na Waziri Fenella Mukangara, amekuwa ni mwiba kwa utendaji wa vyombo hivi, akihusika kuuweka uhuru wa habari na uhariri katika sintofahamu kubwa.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Mkurugenzi wa Habari Maelezo kufanya maamuzi makubwa ya kuyatisha magazeti ya Mwananchi na Rai, kutimiza wajibu wa kuendelea kuhabarisha, kwanza bila kuwa na msingi wowote wa kisheria na pili bila kuwasiliana na wakubwa wake wala wasaidizi wake, kama ilivyotamkwa na aliyekuwa Naibu Waziri Amos Makala, ni jambo ambalo linathibitisha jinsi alivyo sehemu ya utatu huu tuna ozungumza hapa.

Mheshimiwa Spika, anayekamilisha utatu unaoweka uhuru wa habari na uhariri kwenye hati hati ni Naibu Waziri Juma Nkamia. Kwa kauli zake mwenyewe hapa hapa bungeni akisikiwa na Watanzania wote, wakiwemo wadau wa habari, alithibitisha jinsi alivyo na chuki dhidi ya waandishi wa habari.

2.3 Kauli za Dharau Dhidi ya Wanahabari

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, wakati katibu mkuu kiongozi anataja mabadiliko ya baraza la mawaziri ikulu tarehe 19 Januari Mwaka huu, akiwa amezungukwa na wanahabari kutoka vyombo mbalimbali vya habari, wakati akitaja jina la Naibu waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Mhe. Juma Nkamia, wanahabari hao waliguna na kucheka ikiwa ni ishara ya kutoridhishwa na uteuzi huo. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, inaungana na wana habari wote kwa kuguna na kuchekeshwa na uteuzi wa Mhe. Juma Nkamia ambaye ni dhahiri hana maslahi na wana habari bali ameitumia tasnia ya habari kama daraja lake la kufanikisha maslahi yake binafsi ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 17 Novemba mwaka 2013, Baraza la Habari la Tanzania lilioneshwa kusikitishwa na kauli za Mhe. Nkamia ambaye alitoa kauli ya kulikashifu baraza hilo wakati akiwa katika vikao vya Bunge wakati yeye akiwa ni mmoja watu walionufaika na Baraza hilo. Akichangia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mhe. Nkamia alitamka kuwa , MCT(Baraza la Habari Tanzania) na TEF (Jukwaa la wahariri Tanzania) ni sawa na asasi zisizo za Kiserikali (NGOs) lakini zimekuwa zikijipa kazi ya kusimamia waandishi wa habari nchini.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa kauli ya Mhe. Nkamia ilikua ni ya dharau dhidi ya wana habari, dharau dhidi ya tasnia ya habari na dharau dhidi ya vyombo hivyo ambavyo kwa nyakati tofauti, kabla na hata baada ya kupata ubunge, Naibu Waziri alikua akizitambua na kushirikiana nazo. Na kwa kumbukumbu rasmi, ni kuwa MCT na TEF ndizo taasisi zinazoendelea kupigania maslahi ya wana habari dhidi ya uonevu unaofanywa na Serikali hasa kwa wale amba wana misimamo na misingi ya uadilifu kwani vyombo hivyo ndivyo vilivyounda timu maalum ya uchunguzi kuchunguza mazingira yaliyopelekea kuuawa kwa mwandishi wa habari Daudi Mwangosi Septemba 2, 2012 katika kijiji cha Nyololo, wilaya ya Mufindi, mkoani Iringa ambapo ripoti yake ilifichua kuwepo kwa mahusiano mabaya baina ya waandishi wa habari na aliyekua kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa ambaye aliulizwa maswali magumu na Marehemu Mwangosi ikiwemo ni kwanini chama tawala cha CCM kiko huru kufanya mikutano ya kisiasa wakati chama cha upinzani kama Chadema kinawekewa vikwazo na polisi kila wakati.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri amesahau kuwa anazoiita asasi zisizo za kiserikali, ndizo zilizochangia kwa mapinduzi katika sekta ya habari nchini kwa kufanikisha mambo muhimu ikiwemo kusimamia maadili ya waandishi wa habari, kuandaa mitaala ya kufundishia waandishi wa habari ambayo imepitishwa na Baraza la Elimu la Taifa (NACTE) na pia kutumiwa na viongozi wakuu wa Serikali na wanasiasa kama aliyekua Makamu wa Rais, Dkt. Omar Ali Juma, mawaziri wakuu waliopita Edward Lowassa na Fredrick Sumaye katika

Nakala ya Mtando (Online Document)

kusululuhisha migogoro inayohusiana na tasnia ya habari, inakuaje yeye binafsi avipuuze vyombo hivyo muhimu? Na ndio maana kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri kuliwashangaza wanahabari na wadau wa habari.

Mheshimiwa Spika, aidha kwa nyakati tofauti Naibu waziri amekua akiwaita waandishi wa habari kuwa ni waandishi makanjanja na yeye kujinasibu kuwa ni mwandishi mwenye weledi na taaluma. Kambi Rasmi ya Upinzani, ina ushahidi kuwa Mhe. Nkamia amelidanganya bunge na taifa kwa ujumla kwa kutuaminisha kuwa yeye alikua ni mfanyakazi mwajiriwa wa Shirika la Habari La Uingereza BBC, kitengo cha Propaganda wakati Bwana Tido Mhando ambaye amefanya kazi na Shirika hilo kwa takribani miaka 20, alikana kujua uwepo wa kitengo hicho katika Shirika hilo na zaidi kueleza kuwa Mhe. Nkamia hakua muajiriwa wa Shirika hilo bali aliiwtwa ili kwenda kusoma taarifa za habari tu kama kibarua jaambo ambalo hajawahi kusema hadharani. Hivyo mbwembwe zote za Naibu waziri zilikua ni kumuhadaa Rais Kikwete ili apate uongozi kwa sifa asizostahili. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inauliza, je wakiitwa waandishi makanjanja, Kiranja wao ama mwalimu wao mkuu ni nani?

3.0 MAENDELEO YA VIJANA

3.1 Baraza la Vijana la Taifa, Benki ya Vijana na Mustakabali wa Maendeleo ya Vijana Nchini

Mheshimiwa Spika; Kifungu 6002 Idara ya Maendeleo ya Vijana ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo katika mwaka wa fedha 2014/2015 inaombewa jumla ya Sh. 995, 234,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Fedha hizo kwa kiwango kikubwa ni za matumizi yasiyo ya lazima yanayohusiana na Mbio za Mwenge yasiyokuwa na uhusiano moja kwa moja na maendeleo ya vijana nchini. Ikumbukwe kwamba siku chache zilizopita tarehe 27 Mei 2014 katika kikao cha kumi na tisa kwenye Mkutano huu wa Bunge, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ilijibu kwa mfano mwaka 2012 Jumla ya Tsh 650,000,000 zilitengwa kwa ajili ya kuadhimisha Uzinduzi na Kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru.

Hali hii inajidhihirisha katika uchambuzi wa kasma za idara hii ya maendeleo ya vijana ambapo kwenye matumizi ya kawaida kasma 210314 kumetengwa posho za vikao Sh 20,100,000 katika mwaka wa fedha 2014/2015 kwa ajili ya "vikao vya uanzishwaji wa Baraza la Vijana, Benki ya Vijana pamoja na tathmini ya Mbio za Mwenge wa Uhuru".

Mheshimiwa Spika; Hali hii inadhihirisha Wizara haiweki kipaumbele katika kazi muhimu zinazohusu uanzishaji uanzishwaji wa vyombo viwili muhimu kwa ajili ya vijana: Baraza la Vijana la Taifa na Benki ya Vijana ambavyo Kambi Rasmi ya

Nakala ya Mtando (Online Document)

Upinzani imehojoji kwa nyakati mbalimbali kutaka utekelezaji uharakishwe. Kitendo cha kutenga rasilimali kidogo kwa ajili ya kazi hizo, huku rasilimali hizo zikielekeza katika posho za vikao na vikao hivyo vikiwa na ajenda nyingi nyingine zikiwa tofauti na masuala ya msingi ya maendeleo ya vijana kinaashiria udhaifu mkubwa wa Serikali inayoongozwa na CCM katika masuala yanayohusu vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa vyovvye vile, chini ya makada wa CCM posho hizo zitatumika kujadili kuhusu mbio za Mwenge kuliko masuala ya msingi ya uanzishwaji wa Baraza la Vijana la Taifa na Benki ya Vijana kwa kuzingatia namna Serikali ya CCM ilivyojibu bungeni kubariki Mwenge huo kutumika kwa ajili ya propaganda potofu za Serikali mbili kuelekea kura ya maoni ya mabadiliko ya katiba. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa mwito kwa uongozi wa Bunge na Wabunge katika mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kuhakikisha mamlaka na madaraka ya wabunge kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba ya Nchi yanatumika vizuri zaidi kuwezesha kuharakishwa kuundwa kwa Baraza la Vijana la Taifa na Benki ya Vijana kwa ajili ya Maendeleo ya Vijana nchini.

Mheshimiwa Spika; Katika Mkutano wa 14 Kikao cha 15 tarehe 21 Disemba 2013 ulisomwa Bungeni Muswada Binafsi wa Mbunge wa Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa wa mwaka 2013. Baada ya muswada huo, Bunge lilielezwa pia na Mheshimiwa Spika,

“ Waheshimiwa wabunge, muswada binafsi wa Mheshimiwa Zitto Kabwe sasa utaanza kuwepo kwenye website ya Bunge na utakuwa public mpaka utakapopangiwa tarehe ya kujadiliwa na utapelekwa kwenye kamati zitakazohusika wakati muafaka”.

Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa mwito kwa Spika: Mosi, kuweka kumbukumbu sawa kwa kulieleza Bunge kwamba muswada binafsi wa mbunge uliwasilishwa na Mheshimiwa John Mnyika; Pili, kulieleza Bunge sababu ya maelekezo yake ya muswada huo kuwepo kwenye tovuti ya bunge kwa ajili ya kuwa wazi kwa umma mpaka sasa kutokutekelezwa, Tatu, ni lini muswada huo utapangiwa tarehe ya kujadiliwa; Nne, ni kwanini mpaka sasa muswada huo haujapelekwa kwenye kamati zinazohusika; Tano, ni upi wakati muafaka alioutaja kwenye maelezo yake.

Mheshimiwa Spika; Kambi Rasmi ya Upinzani inawahimiza wabunge kuzingatia kwamba kutokuwepo kwa chombo kinachowaunganisha vijana wote bila kujadili itikadi kufuatilia masuala ya maendeleo ya vijana kunafanya Wizara mbalimbali za kisekta kutokuzingatia masuala yaliyokipaumbele kwa maendeleo ya vijana. Mathalani, katika Mkutano huu wa Bunge katika Fungu la

Nakala ya Mtando (Online Document)

65 la Wizara ya Kazi na Ajira Kitabu cha Nne Cha Miradi ya Maendeleo Kifungu cha 2002, pamoja na wabunge na vijana kupewa matumaini kwamba zimepitishwa bilioni tatu kwa ajili ya mikopo na mitaji kwa vijana ukweli ni kwamba fedha hizo zimepangija matumizi ambayo kusipokuwa na chombo cha kuyafuatilia kutakuwa na udhaifu, ufisadi na ubadhirifu kama ilivyojitokeza katika fedha za mifuko ya maendeleo ya vijana kati ya mwaka 1993/1994 mpaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika; Kwa mujibu wa Kasma za Kifungu hicho cha 2002 cha Bajeti iliyopitishwa ya Fungu 65 Wizara ya Kazi na Ajira, fedha hizo zinazopaswa kuwa za mikopo na mitaji kwa vijana zitatumika milioni 700 kwa ajili ya kulipia utaalamu elekezi (consultancy fees) kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa vijana 200 tu; milioni 150 zitatumika kununulia magari Wizarani, milioni 60 zitatumika kwenye matangazo na orodha ndefu nyingine ya matumizi yasiyo ya lazima ambayo kutohata na ufinyu wa muda sitaendelea kuyataja. Aidha, katika mjadala wa bajeti hiyo wabunge waliweka bayana kwamba kiwango kinachotengwa katika Mifuko ya Maendeleo ya Vijana iwe ni kwa Serikali Kuu na hata Halmashauri ni kidogo ukilinganisha na uwezo wa nchi, mahitaji ya vijana na mafungu mengine yasiyo na matumizi muhimu yanavyotengewa fedha nyingi katika baadhi ya Wizara.

Mheshimiwa Spika; Hivyo, ili Baraza la Vijana la Taifa na Benki ya Vijana ambavyo ni vyombo muhimu kwa maendeleo ya vijana viweze kuanzishwa kwa wakati, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa mwito kwa Spika wa Bunge kuelekeza muswada binafsi uliokwisha wasilishwa kwa Bunge kwa kamati zinazohusika kwa ajili ya kuanza kuujadili. Aidha, Spika arejea ratiba ya Bunge ambapo imetajwa bayana kwamba kati ya tarehe 5 Juni 2014 na 11 Juni 2014 ratiba ya Bunge haitahusu uwasilishaji wa Bajeti za Serikali. Ratiba imetaja bayana kwamba "Shughuli nyingine yoyote kama itavyokuwa imeelekezwa na Spika" inaweza kuingizwa kwenye ratiba; hivyo, fursa hiyo itumike kuleta muswada huu Bunge kusomwa kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika; Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Bunge kuingilia kati suala hili na kuvisimamia Serikali kwa kuzingatia kwamba katika majumuisho ya Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2013/2014 tarehe 21 Mei 2013 mkutano wa 11 kikao cha 30; Serikali ilitumia kisingizio kwamba 'ni bunge la bajeti' kukwepa kuwasilishwa kwa muswada Bunge. Hata hivyo, ahadi ya Serikali ya kuwasilisha muswada haikutekelezwa kwenye mikutano mitatu uliyofuatia ya 12, 13 na 14; hivyo mkutano huu wa 15 ni muafaka kuwezesha maamuzi kufanyika kwa ajili ya maendeleo ya vijana nchini.

Mheshimiwa Spika; Kambi Rasmi ya Upinzani inaikumbusha Serikali na wabunge kwamba Sera ya zamani ya maendeleo ya vijana ya mwaka 1996 ilitamka kwamba kutaanzishwa Baraza la Vijana na suala hilo kurudiwa katika Sera

Nakala ya Mtando (Online Document)

mpya ya mwaka 2007; hata hivyo Serikali imekuwa ikiwepa kuhakikisha kwamba matakwa hayo ya sera tajwa yanatekelezwa pamoja na kuwa suala hilo linahusu mustakabali wa maendeleo ya vijana nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani inakumbusha pia kwamba katika ilani za uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 vyama mbalimbali viliahidi kuhakikisha kwamba Baraza la Vijana la Taifa linaundwa. Ili kuwahadaa na kujipatia kura za vijana CCM kwa kupitia ilani yake katika kipengele 80 (k) inasema

"Kuhamasisha ushiriki wa vijana katika ngazi mbalimbali za maamuzi ikiwa ni pamoja na kukamilisha uanzishaji wa Baraza la Vijana".

Mheshimiwa Spika; Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inatarajia kwamba wabunge wa pande zote katika suala hili la kuanzishwa kwa Baraza la Vijana la Taifa kuungana kuwa kitu kimoja kuisimamia Serikali na kutumia madaraka ya Bunge kutunga sheria wakati wa Mkutano huu wa Bunge unaoendelea. Serikali na wabunge mzingatie kwamba zaidi ya miaka 18 ahadi za kukamilisha mchakato wa kuanzishwa kwa baraza la Vijana la Taifa; bila utekelezaji kamili na wa haraka. Baraza la Vijana litawezesha vijana kuanzia kwenye vijiji/mitaa mpaka taifa kuweza kuwa na vyombo vya kuwaunganisha vijana kwa kike na wa kiume kwa ajili ya maendeleo yao na ya taifa.

Mheshimiwa Spika; Aidha, Baraza hilo litafuatilia pia kwa karibu utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya vijana kwenye Halmashauri, Serikali kuu, katika vyombo mbalimbali vya maendeleo na wadau wa maendeleo. Pia, Baraza la Vijana litafuatilia kwa karibu utendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kuhakikisha kwamba fedha zinatengwa za kutosha na kufika kwa walengwa kuwawezesha vijana kujiajiri, kukuza vipaji vyao na kushughulikia maendeleo yao kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, aidha Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji ni kwa nini kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 Jumla ya fedha zilizopelekwa kwenye vikundi mbalimbali kwa kupitia mfuko wa vijana ni **shilingi milioni 172.6 tu** sawa na **asilimia 2.8** tu, kati ya Shilingi **Bilioni 6.1** ambazo Serikali mwaka jana iliwardanganya vijana kuwa itatenga, huku taarifa ya wizara ikionesha kuwa kiasi cha shilingi **Bilioni 2** sawa na **asilimia 32.7** pekee ndizo zilizokua zimepokelewa hadi kufikia April 2014. Je, kiasi cha shilingi **milioni 827.4**, zimetumikaje tumikaje? Je, Serikali itaacha lini kuwahadaa vijana kuwa wanatenga mabilioni ili kuwanyamazisha katika kudai haki zao huku ikijua kuwa haiwezi kuwasaidia hata kile wanachostahili?

4.0 UTAMADUNI

4.1 UTAMADUNI: KIELELEZO CHA HISTORIA YA TAIFA

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, imekua ikishauri Serikali juu ya umuhimu wa kutunza maeneo na majengo ya kale ili kuweza kuonesha urithi wa utamaduni wa taifa letu. Ni dhahiri kuwa maeneo mengi ya kihistoria yameachwa na kuwa magofu na mengine yanaendelea kubomolewa kwa ujenzi mpya hali inayofanya historia ipotee, jambo ambalo pia linalikosesa taifa mapato yanayotokana na utalii. Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kujua mikakati ya wizara kuhakikisha kuwa maeneo na majengo ya kale yanahifadhiwa na kuachwa katika hali yake kwa mwaka huu wa fedha wa 2014/2015.

4.2 BARAZA LA SANAA TANZANIA (BASATA)

Mheshimiwa Spika, Baraza la Sanaa nchini lina dhamana kubwa kuhakikisha kuwa sanaa ya mtanzania haipoki wala kudhalilisha maadili pamoja na kuiendeleza sanaa hapa nchini. Ni jambo la kushangaza kuona kuwa Baraza hili hufanya kazi kwa kuzinduka tu usingizini huku athari za uporomokaji wa maadili kwa kupitia sanaa katika jamii zinakua kubwa.

Mheshimiwa Spika, ngoma ya Kigodoro haikua maarufu katika sehemu kubwa za nchi kutoptaka na ngoma hiyo kuchewza katika sehemu chache. Lakini, baada ya kutolewa kwa filamu ya Kidogoro ambayo kwa kiasi kikubwa ilihamasisha jamii kutaka kujua maana ya kidogoro na hivyo ngoma hiyo kuzidi kupata umaarufu katika sehemu kubwa ya jamii ya watanzania hata kwa watanzania wanaoishi nje ya nchi. Mara baada ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuelezea athari za ngoma hii katika maadili ya watanzania BASATA ghafla ikazinduka usingizini na kupiga marufuku ngoma hiyo, huku filamu ya Kigodoro ikiwemo katika soko la filamu na ikiendelea kuuzwa huku ikiambatana na ujumbe amba si tu unahamasisha uvunjifu wa maadili ya kitanzania bali unatoa taswira ya jamii isiyostaarabika. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka wizara hii kuisimamia BASATA ipasavyo pamoja na kuipa uwezo wa kifedha ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kuutunza na kuutangaza utamaduni wa mtanzania kwa kupitia kazi za sanaa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka BASATA kuacha uvivu na kutekeleza majukumu yake kwa ubunifu ili kulinda na kuutangaza utamaduni wa Mtanzania ili hatimaye navyo vitoe mchango katika taifa kutoptaka na mapato yanayotokana na mauzo ya kazi za sanaa na utamaduni.

4.3 WASANII NA HARAKATI MBALIMBALI

Mheshimiwa Spika, katika mapambano ya kudai haki za wasanii duniani popote, wasanii huongozwa na dhamira ya kutumia sanaa zao ili kuleta mabadiliko ya kweli na si kukubali kutumika kuwa faraja kwa watu wengine kufanikisha malengo yao na mwishowe haki wanazozipigania kuonekana kama kelele za chura.

Mheshimiwa Spika, kila mtu ana uhuru wa kufanya maamuzi yake hasa maamuzi ya msimamo wa kisiasa. Ila kwa muda mrefu sasa, wasanii wa Kitanzania tumeshindwa kuwa mabalozi wa kweli wa haki katika kuhakikisha kuwa tunatumia kazi zetu za sanaa tunapigania haki na usawa ili kulikomboa taifa. Matokeo yake, baadhi ya wasanii wamekua wakitumika kama chambo na baadhi ya wanasiasa ili kuweza kutimiza maslahi ya wanasiasa, ambayo kwa kifupi baada ya kutumika, hata maslahi ya wasanii ambayo wanapigania huwa hayapewi kipaumbele. Mfano mzuri kwetu wasanii ni jinsi ambavyo tumetumika sana katika harakati za kisiasa lakini katika mchakato wa katiba, tumesahulika. This is a wake up call kwa wasanii wote ambao wamekubali kutumika kwa maslahi ya muda mfupi bila kuangalia mustakabali wa sekta ya sanaa katika taifa letu. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, inawataka wasanii kuacha kutumika na kujenga umaja imara utakaotetea maslahi yao kwa ujumla bila ya kufuata mashinikizo ya kisiasa ili kuleta mapinduzi ya kweli katika sanaa.

4.3.1 SANA NA WASANII KUTUMIKA KWENYE UFISADI NA UFICHAJI WA MGONGANO WA MASLAHI

Mheshimiwa Spika, Katika Maoni yetu kwa hoja hii ya mwaka jana, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu ilizungumzia kwa kirefu jinsi ambavyo Serikali hii ya CCM imeshindwa kulinda haki za wasanii licha ya kuwepo kwa Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki tangu mwaka 1999. Tulielezea jinsi ambavyo, licha ya masharti ya Sheria hiyo na licha ya kuwepo kwa Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA) tangu mwaka 2007, nyimbo za wasanii nchini zimeendelea kutumiwa kwenye matangazo ya vyombo vya habari, hasa vya Serikali kama vile Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC1 na TBC2) bila wasanii waliozitunga au kuziimba nyimbo hizo kupata malipo yoyote.

Mheshimiwa Spika, Ni haki na wajibu kwa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu kupiga kelele dhidi ya unyonyaji huu wa wasanii wetu, hasa wanamuziki vijana wa kizazi kipyaa ambao wanajihangaikia kutafuta maisha na kuendeleza vipaji vyao. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inawaahidi wasanii wetu kwamba itaendelea kutimiza wajibu wake kwa kutetea haki na maslahi yao hadi watakapotendewa haki.

Hata hivyo, Mheshimiwa Spika, ni haki na wajibu kwa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu kuwakemea na kuwakosoa vijana pale wanapojingiza katika vitendo vinavyochafua sanaa na sifa zao kama wasanii na wa-Tanzania. Kama inavyofahamika na wananchi na hata kwa Bunge lako tukufu, wasanii kadhaa wa ki-Tanzania wamekamatwa katika nchi za nje wakiwa na madawa ya kulevyia. Wasanii wa aina hii, wanaokubali kutumiwa kama punda wa mizigo

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ya madawa ya kulevyaa na mitandao haramu ya biashara hiyo, hawastahili chochote kutoka kwa wa-Tanzania zaidi ya dharau na adhabu kali zilizowekwa na sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kutumia umaarufu wao ili kuficha ushiriki wao katika biashara haramu ya madawa ya kulevyaa sio tatizo pekee la baadhi ya wasanii wetu. Sasa limejitokeza tatizo la baadhi ya wasanii wetu, hasa wanamuziki maarufu wa Bongo Fleva, kujingiza – kwa kujua au kwa kutumiwa na wajanja bila ya wao kujua – kwenye ‘dili’ za kifisadi za kuiba fedha za umma. Wajanja hao hujificha katika kivuli cha makampuni yanayotajwa kuwa na malengo ya kuendeleza wasanii na sanaa kumbe ni vichaka vya kuficha ufisadi, mgongano wa kimaslahi na matumizi mabaya ya madaraka ya baadhi ya viongozi wa umma dhidi ya fedha za umma wanazopaswa kuzisimamia.

Utaratibu unaotumika kutekeleza dili hizi za kifisadi unafanana kwa kiasi kikubwa na utaratibu uliotumika kuiba mamia ya mabilioni ya fedha za umma kutoka kwenye akaunti ya madeni ya nje ya Benki Kuu ya Tanzania (EPA) mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 13 Agosti, 2012, Msajili Msaidizi wa Makampuni katika Wakala wa Usajili wa Makampuni na Leseni (BRELA) alitoa Hati ya Usajili (*Certificate of Incorporation*) kwa kampuni inayoitwa Leka Dutigite Limited. Kwa mujibu wa nyaraka za BRELA, Leka Dutigite Ltd. ina ofisi zake katika ghorofa ya kwanza ya jengo la City House lililoko katika Mtaa wa Mkweju, Dar es Salaam. Mheshimiwa Spika, Katiba, yaani *Memorandum and Articles of Association*, ya kampuni ya Leka Dutigite Ltd. iliyosajiliwa BRELA tarehe 13 Agosti, 2012 inaonyesha kwamba mwenye hisa nyingi katika kampuni hiyo ni kampuni nyingine inayoitwa Gombe Advisors Ltd. ya Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa za kibenki ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu imezipata, mnamo tarehe 10 Desemba, 2012, Hifadhi ya Taifa ya Saadani ilihamisha jumla ya shilingi 12,200,000 kwenda kwenye akaunti na. 0150357447800 iliyoko CRDB Bank tawi la Pugu Road, Dar es Salaam, inayomilikiwa na Leka Dutigite Ltd. Hifadhi ya Taifa ya Saadani inamilikiwa na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA), ambayo ni shirika la umma. Siku moja baadae, fedha hizo zilitolewa kwa pesa taslimu kutoka kwenye akaunti hiyo.

Baada ya hapo, kati ya tarehe 14 Januari na 7 Februari, 2013, akaunti ya Leka Dutigite Ltd. iliringiziwa jumla ya shilingi 28,600,000. Fedha hizo zote ziliingizwa kama fedha taslimu na mtu aitwaye Mchange (shilingi 3,600,000 tarehe 14 Januari, 2013) na Leka Dutigite (shilingi 25,000,000 tarehe 23 Januari na 7 Februari, 2013). Kufikia tarehe 7 Februari, 2013, fedha hizo zote zilikwishatolewa benki.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Tarehe 28 Februari, 2013, akaunti ya Leka Dutigite Ltd. iliingiziwa shilingi 32,367,000 na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF). Kwa mujibu wa taarifa za kibenki, siku hiyo hiyo, fedha hizo zilitolewa kwenye akaunti hiyo. Siku nne baadae, yaani tarehe 4 Machi, 2013, NSSF ilifanya malipo mengine kwenye akaunti ya Leka Dutigite Ltd., kwa mikupuo miwili, ya jumla ya shilingi 46,663,000. Siku hiyo hiyo, fedha hizo nazo zilitolewa kutoka kwenye akaunti hiyo kwa mikupuo miwili. Kwa hiyo, katika kipindi cha miezi mitatu katika ya tarehe 10 Desemba, 2012 na 4 Machi, 2013, Leka Dutigite Ltd. ililipwa shilingi 119,930,000 kwa utaratibu huo huo wa ingiza na toa fasta. Kati ya fedha hizo, shilingi 12,200,000 zililipwa na TANAPA na shilingi 79,027,000 zililipwa na NSSF.

Mheshimiwa Spika, Katika mazingira ya kawaida, sio kitu cha ajabu kwa mashirika ya umma kama NSSF na TANAPA kufanya biashara na watu au taasisi mbali mbali kama makampuni binafsi. Ukweli ni kwamba, kwa upande wa malipo yaliyofanywa na TANAPA, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu imeweza kupata nakala ya mkataba unaohusu *Maandalizi ya Filamu (Documentary)* kwa Ajili ya Kuhamasisha Shughuli za Utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Saadani kwa Kutumia Wasanii Kutoka Kigoma. Mkataba huo umesainiwa tarehe 5 Desemba, 2012, kati ya Hifadhi ya Taifa ya Saadani na Leka Dutigite Ltd. na una thamani ya shilingi 12,200,000, kiasi kile kile kilicholipwa na Hifadhi hiyo.

Hata hivyo, Mheshimiwa Spika, mazingira ya malipo haya sio ya kawaida. Hii ni kwa sababu ya uwepo wa kampuni ya Gombe Advisors Ltd. Kwa mujibu wa nyaraka za BRELA, kampuni hii ilisajiliwa tarehe 24 Novemba, 2011. Kwa mujibu wa nyaraka hizo, ofisi za Gombe Advisors Ltd. ziko kwenye jengo la City House, Mtaa wa Mkwepu, Dar es Salaam, ziliko ofisi za Leka Dutigite Ltd. Kwa mujibu wa nyaraka hizo, wakurugenzi wa Gombe Advisors Ltd. ni Zitto Zuberi Kabwe ambaye kazi yake inatajwa kuwa 'mchumi', na Raphael Ongangi ambaye anatajwa kuwa 'mchambuzi wa fedha na vitega uchumi' (Financial and Investment Analyst). Bwana Ongangi aliwahi kutajwa na gazeti la kila wiki la Mawio la tarehe 26 Desemba 2013 kuwa ni mmoja wa washauri wa Zitto Zuberi Kabwe na anasemekana kuwa msaidizi wake.

Mheshimiwa Spika, Zitto Zuberi Kabwe sio 'mchumi' anayetajwa katika nyaraka za BRELA zinazoihusu kampuni ya Gombe Advisors Ltd. pekee, bali pia ni Mbunge, tangu mwaka 2005, wa Bunge lako tukufu. Kama Mbunge, Mheshimiwa Zitto Kabwe ni 'kiongozi wa umma' kwa mujibu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, 1995. Sheria hii inawalazimu viongozi wa umma, wanapokuwa madarakani, kuwa "waadilifu, wenyewe huruma, utulivu, umakini na watakaoendezea viwango vya juu vya maadili ili kujenga na kuendeleza imani ya umma kwa uadilifu wa Serikali."

Nakala ya Mtando (Online Document)

Aidha, viongozi wa umma "... watawajibika kutekeleza wajibu wao kwa umma na kuendesha shughuli zao binafsi kwa namna ambayo itaonekana na kuthibitika kuwa ni wazi kwa umma na haitatosheleza kwao kutekeleza wajibu wao kwa kufuata sheria tu." Vile vile, kuhusiana na maslahi binafsi, Sheria hii inaelekeza kwamba "... viongozi wa umma hawatakuwa na maslahi binafsi ambayo yanaweza kuathiriwa na maamuzi ya serikali wanayoshiriki katika kuyafanya."

Mwisho, kuhusiana na maslahi ya umma, viongozi wa umma wanatakiwa, pale wanapochaguliwa au kuteuliwa, kupanga masuala yao "kwa namna itakayozua migongano ya maslahi ya wazi, iliyojificha au inayoonekana kuwepo na pale ambapo migongano hiyo inatokea kati ya maslahi binafsi na maslahi ya umma basi itatatuliwa kwa kuangalia zaidi maslahi ya umma." Kwa kadri ya ufahamu wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu, Mheshimiwa Zitto Kabwe hajawahi kutangaza maslahi aliyonayo kwenye mikataba ya Gombe Advisors Ltd. na Leka Dutigite Ltd. na NSSF na TANAPA.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe sio tu ni Mbunge anayebanwa na masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, bali pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha za Serikali (PAC). Kwa mujibu wa kipengele cha 12 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako tukufu, mojawapo ya majukumu ya PAC ni kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara na Mashirika ya Umma yaliyoainishwa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. NSSF na TANAPA ni baadhi tu ya Mashirika ya Umma yaliyo chini ya usimamizi wa kibunge wa PAC.

Kwa maana hiyo, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Zitto Kabwe, kwa kutumia makampuni yake ya Leka Dutigite Ltd. na Gombe Advisors Ltd., amefanya biashara na TANAPA, shirika la umma analolisimamia kama Mbunge na Mwenyekiti wa PAC. Mheshimiwa Zitto Kabwe na wanamuziki washirika wake, kwa kutumia makampuni ya Gombe Advisors Ltd. na Leka Dutigite Ltd., wamelipwa fedha za umma za TANAPA na NSSF.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo juu ya madai ya ukiukwaji wa Sheria uliofanywa na viongozi wa umma na mashirika ya umma katika kashfa hii. Pamoja na maelezo yatayotolewa, Kambi Rasmi ya Upinzani inataki Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalum juu ya matumizi ya fedha zilizotolewa na TANAPA na NSSF; msukumo uliofanya fedha hizo zitolewe na matumizi ya fedha hizo kwa kuzingatia masharti yanayosimamia fedha za umma na utawala bora katika usimamizi wa fedha za

Nakala ya Mtandao (Online Document)

umma. Aidha, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ifanye uchunguzi juu ya malipo na matumizi husika kwa kurejea masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Sheria nyininge zinazohusika. Kwa upande mwingine, kwa kuwa suala hili linahusu mbunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge inayohusika na usimamizi wa fedha za umma, Kamati ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge nayo ifanye uchunguzi wake juu ya madai ya masharti ya Katiba ya Nchi, Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge na Kanuni za Bunge juu ya maadili ya kiongozi wa umma ikiwemo yahusuyo utangazaji wa maslahi.

Mheshimiwa Spika; Mwisho, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inatoa rai kwa wanamuziki na wasanii wengine wote nchini kuwa waangalifu na watu wanaotaka kutumia umaarufu wao kama wanamuziki na wasanii kwa lengo la kufanikisha dili za kifisadi. Bila kuchukua tahadhari ya kutosha, wasanii hao wanaweza kujikuta wakipoteza sifa na umaarufu wao ambao wameujenga kwa jitihada zao wenye.

4.4 MCHAKATO BUTU WA VAZI LA TAIFA

Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Vijana na Michezo, wakati huo chini ya Waziri Dk. Emmanuel Nchimbi, ilifanya uteuzi wa wajumbe wa Kamati ya Kubuni Vazi la Taifa mwezi Desemba 15, 2011. Kamati hiyo iliyokuwa na watu wanane, Mwenyekiti ni Joseph Kusaga na Katibu ni Angela Ngowi, pamoja na wajumbe wa kamati hiyo ni Habib Gunze, Joyce Mhaville, Mustafa Hassanali, Makwaia Kuhenga, Ndesambuka Merinyo na Absalom Kibanda, ambaye baadaye alitangaza kuijweka kando. Desemba 22, 2011, kamati hiyo ikazinduliwa rasmi na aliyekuwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Mhe. Emmanuel Nchimbi, tayari kuanza kazi ya kubuni Vazi la Taifa, mchakato ambao ulipaswa kukamilika ndani ya siku 75 tangu siku ya kuzinduliwa kwake. Mhe. Nchimbi aliahidi kuwa mara baada ya kamati hiyo kukamilisha kazi hiyo ikiwamo kuainisha mapendekezo mbalimbali ya vitambaa vinavyoweza kufaa, Watanzania watakuwa wamepata Vazi la Taifa. Siku hiyo Waziri Nchimbi alisema kazi ya kamati hiyo si kuanza mchakato mpya wa Vazi la Taifa, bali ni kumalizia mchakato wa kupata vazi la mwanamume na mwanamke ulioanza mwaka 2004. Hata hivyo, baada ya mabadiliko ya baraza la mawaziri, tarehe Septemba 10, 2012, Kamati ya Vazi la Taifa chini ya Ndugu Kusaga ilikabidhi ripoti kwa Waziri Mukangara aliyekuwa na naibu wake, Amos Makalla. Uwasilishaji wa ripoti hiyo ulifanywa na Katibu wa Kamati ya Vazi la Taifa Angela Ngowi, akiwa na wajumbe wa kamati hiyo, Joyce Mhaville, Mustafa Hassanali na Ndesambuka Merinyo. Angela akasema katika mchakato wa kupata vazi hilo, walipokea zaidi ya michoro 200 kutoka kwa wasanii 88 na kuitisha michoro sita iliyokuwa imekidhi vigezo na kuikabidhi kwa wataalamu wa vitambaa kwa ajili ya kutoa uamuzi wao. Waziri Mukangara alionesha

Nakala ya Mtando (Online Document)

shauku yake ya kuona vazi hilo linapatikana haraka na kwamba lingevaliwa katika maadhimisho ya miaka 51 ya Uhuru wa Tanganyika ya Desemba 9, mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, ikiwa inakaribia kuwa miaka takribani miwili sasa tangu Waziri Mukangara apokee ripoti hiyo, hakuna vazi lililopatikana wala maelezo mapya juu ya hatima ya vazi hilo. Kwa vile vazi la taifa limekuwa likisubiriwa kwa shauku kubwa na Watanzania tangu mchakato huo ulipoanzishwa kwa mara ya kwanza mwaka 2004, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka maelezo ya kina kutoka kwa Waziri ni nini kimeukwamisha mchakato huo?

4.5 SANAA NA USANII KUTAMBULIWA KAMA SEKTA YA KIUCHUMI NA ULINZI WA MILIKI BUNIFU KUBORESHWA KUINUA VIPATO VYA WASANII NA MAPATO KWA NCHI

Mheshimiwa Spika; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina taarifa juu ya maoni ambayo Wasanii waliyawasilisha mbele ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba na baadaye kwa baadhi ya wabunge ikiwemo wa upinzani kutaka wasanii watambuliwe kama kundi maalum katika katiba mpya kama ilivyo kwa wafugaji, wakulima na fani au tasnia nyingine. Aidha, wasanii wamependekeza kwamba rasimu ya katiba mpya itaje miliki bunifu (intellectual property).

Mheshimiwa Spika; Kutokana na umuhimu wa mapendelekezo ya wasanii hao waliyoyatoa kupitia mashirikisho yao manne Shirikisho la Filamu, Shirikisho la Muziki, Shirikisho la Sanaa za maonyesho na Shirikisho la Sanaa za ufundi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa maoni kwa Serikali kwamba haipaswi kusubiri mpaka mchakato wa mabadiliko ya katiba bali marekebisho ya msingi ya kisheria yapaswa kuharakishwa kuwezesha sanaa na usanii kuchangia katika kuongeza ajira, kuboresha maisha ya wasanii na kuchangia kwa kiwango kikubwa katika mapato ya Serikali na Uchumi wa Nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika; Serikali imekuwa ikitazama sanaa kama suala la burudani zaidi badala ya kuitazama kama ni sekta muhimu ya kiuchumi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuzingatia kwamba Wasanii sio wanamuziki tu, wasanii wapo karibu katika kila kaya Tanzania. Wafinyanzi, wasusi, wapambaji, wanamuziki waigizaji, mafundi mbalimbali wa ushonaji ujenzi na kadhalika, wako wengi wala hata wao hawajitambui kama ni wasanii kutokana na mazingira waliyomo.

Mheshimiwa Spika; Katika ripoti mojawapo ya BASATA ya mwaka 2006, idadi ya wasanii nchini wakati huo ilikuwa ni milioni 6, ni wazi kuwa idadi hiyo kwa sasa itakuwa imepanda. Katika miaka ya karibuni vijana wengi wamekuwa

Nakala ya Mtando (Online Document)

wanaongezeka kuijunga na kundi hili kwani katika sanaa kumekuwa na uwezekano wa kujipatia ajira, tena isiyokuwa na ukomo. Na hivyo sanaa kwa sasa si utamaduni peke yake bali ni sehemu muhimu ya uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika; Wasanii ni sehemu muhimu katika sekta ya Hakimiliki, takwimu za ripoti ya WIPO(World Intellectual Property Organisation) ya mwaka 2010, kuhusu mchango wa sekta ya hakimiliki katika uchumi wa Tanzania, inaonaonyesha kuwa sekta hii, kati ya 2007-2010 ilichangia kati ya asilimia 3-4.6% ya gross domestic product(GDP). Na kiasi cha kati ya TSH 38.930 bilioni na 86.686 billion kilipatikana kama kipato cha walioajiriwa katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika; Kati ya watu 28, 202 na 44, 331 walioajiriwa rasmi, na hiyo ilikuwa kati ya asilimia 4.5 na 5.2% ya kundi zima la waajiriwa wa Taifa hili. Kwa kipimo cha GDP, sekta hii ilikuwa zaidi ya sekta ya madini, ambayo wote ni mashahidi imekuwa katika mazungumzo kila kona ya nchi. Na katika ajira sekta hii ilikuwa juu zaidi ya sekta nyingi zikiwemo madini, usafirishaji, mawasiliano, afya na ustawi wa jamii, maji, gesi, na hata ujenzi. Kwa mchango wa sekta hii wa 3.2% katika GDP kwa mwaka 2009 , umeweka sekta hii kuwa bora kuliko sekta za aina yake katika nchi kama Croatia 3%, Singapore 2.9%, Latvia 2.9%, Lebanon 2.5%, Kenya 2.3%. Na katika mchango wa ajira sekta hii ilikuwa juu ya Romania, Bulgaria, Lebanon, Jamaica, Colombia, Kenya na Ukraine.

Mheshimiwa Spika; kwa upande wa Tanzania, Takwimu hizi hazijionyeshi katika takwimu za Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kuwa sanaa bado inaonekana ni burudani tu, na thamani yake katika uchumi haitiliwi uzito. Kutambuliwa kwa kundi hili kutawezesha kutungwa sheria na taratibu za kuwezesha Wasanii kuongeza ajira na mapato, na Taifa kufaidika na uchumi wa raslimali hii.

Mheshimiwa Spika; Kambi Rasmi ya Upinzani inataka marekebisho makubwa kwenye sheria za nchi yetu kuwezesha kutajwa kwa miliki bunifu katika sanaa, usanii na sekta zote nyingine muhimu za kiuchumi. Ni muhimu Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Serikali kwa ujumla ikazingatia kwamba mali ziko za aina tatu. Kuna mali zinazohamishika, mali zisizohamishika na mali zitokanazo na ubunifu. Aina mbili za kwanza zimetajwa katika katiba na ulinzi wake hujulikana na ni wa jadi. Lakini hii aina ya tatu ya mali huwa ni ngumu kuilinda kutookana na mfumo wake kuwa haushikiki hivyo sheria maalumu hutungwa kulinda aina hii ya mali (IP Laws).

Mheshimiwa Spika; Mali zitokanazo na ubunifu kwa sasa ndio mali zenyе kipa umbele duniani. Uvumbuzi wa teknolojia mbalimbali, ugunduzi wa njia mbalimbali za kuboresha maisha, sanaa na mengi yanayolindwa na

Nakala ya Mtando (Online Document)

milikibunifu, vimeweza kutoa ajira kubwa na kutoa mchango mkubwa wa kipato kwa wagunduzi na nchi ambazo wagunduzi hao wamekuwa wakiishi au kuzisajili kazi zao. Kama wasanii, haki zetu katika milikibunifu zinajulikana kama Hakimiliki, lakini kama Watanzania tunaona ni muhimu kulinda haki zote za Milikibunifu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika; Nchi zote ambazo zimeweka taratibu imara za kulinda Milikibunifu duniani, zimewesha wabunifu wake kubuni mambo ambayo yameweza kubadilisha maisha ya binadamu wengine duniani kote. Marekani iliweka kipengele cha Ulinzi wa hakimiliki katika katiba yake tangu mwaka Agosti 1787, na kazi za wagunduzi wa Marekani tunaziona kila wakati katika kazi za sanaa na teknolojia. Korea kusini ilinakiri sehemu ya katiba ya Marekani kuhusu ulinzi wa Milikibunifu kuanzia mwaka 1948, kwa wakati huu wote ni mashahidi wa bidhaa kama Samsung, Ld Daewoo, Hyundai na kadhalika.

Mheshimiwa Spika; Milikibunifu pamoja na kulinda haki katika kazi za sanaa ambazo picha ndogo ya mapato yake zimetajwa hapo juu, Milikibunifu italinda haki za wabunifu wetu, tafiti za wasomi wetu, ugunduzi mbalimbali, taratibu mbalimbali za mambo yetu ya kiasili, dawa za asili za miti yetu, na taratibu za matumizi ya dawa hizo, na mali asili zetu nyingine nyingi tunazozifahamu na ambazo bado hatujazifahamu.

Mheshimiwa Spika; Kuna hasara nyingi ambazo hupatikana kama nchi haina ulinzi wa Milikibunifu, mifano michache hapa Tanzania, ni kupoteza kwa Milikibunifu ya jina Tanzanite, ambayo licha ya kuwa inachimbwa Tanzania tu lakini jina linamilikiwa na kampuni ya Afrika ya Kusini. Vazi la kikoi, pamoja kuwa ni la asili ya Tanzania, milikibunifu imesajiliwa Kenya, staili ya michoro maarufu ya Tingatinga milikibunifu yake iko Japan. Na haya ni machache ambayo yameshtukiwa Milikibunifu ikifuatiwa vizuri ndipo haswa ukubwa wa tatizo utakapo julikana. Kuna ulazima mkubwa wa kutaja Milikibunifu katika sheria zote muhimu na kuanisha ulazima wa kulinda kuendeleza na kwezesha wabunifu wan chi kwa manufaa ya kizazi hiki na vizazi vijavyo.

6.0 SEKTA YA MICHEZO NCHINI

6.1 UENDELEZAJI WA VIWANJA VYA MICHEZO NCHINI

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, imeendelea kuona umuhimu wa taifa kuwekeza katika viwanja vya michezo ili kuweza kupanua wigo wa taifa kujitangaza na kukusanya mapato yanayotokana na viwanja vya michezo nchini. Labda, wizara mpaka sasa haijaweza kujua hasara ambazo kama taifa tunapata kutokana na kutotumia

Nakala ya Mtando (Online Document)

nafasi zinazotokea na kutowekeza vya kutosha katika kuboresha michezo nchini.

Mheshimiwa Spika, enzi za chama kimoja, majengo na maeneo yote ya umma yalikuwa chini ya Serikali. Ujenzi na uendelezaji wa maeneo hayo ulifanya na Serikali kupitia kodi za wananchi, michango, fedha za wafadhili na wahisani mbalimbali. Hata baada ya uwepo wa vyama vingi, uendelezaji wa miradi yote iliyokuwa chini ya Chama kimoja ilifanywa kuwa ni jambo la kitaifa. Kwa namna isiyoeleweka baadhi ya maeneo ambayo CCM imeshindwa kuyarudisha kwa wananchi na kuwa mali ya umma na kuyafanya ni mali ya chama ni pamoja na Uwanja wa CCM Kirumba (Mwanza), Samora (Iringa), Sokoine (Mbeya), Sheikh Amri Abeid (Arusha), Majimaji (Songea), Kaitaba (Kagera) n.k.

Mheshimiwa Spika, pamoja na CCM kuendelea kuhodhi viwanja hivi imeshindwa kuviendezea na matokeo yake kuwanyima fursa wananchi wa maeneo husika kushuhudia michezo mbalimbali kwa kuwa viwanja hivyo huwa havikidhi viwango vya ubora vya michezo hali inayofanya michezo mingi mikubwa ikiwemo ya kimataifa kufanyika Dar Es Salaam pekee. Kambi rasmi ya upinzani inarudia tena kuitaka Serikali kuvirudisha viwanja vyote vilivyohodhiwa na CCM kwa wananchi ili viendelezwe kwa kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Michezo nchini kama tulivyopendekeza mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Mechi ya Taifa Stars na Zimbabwe kuhamishwa kutoka uwanja wa Sokoine Mbeya tarehe 18 Mei na kuhamishiwa uwanja wa Taifa Dar Es Salaam, kwanza kimewavunja moyo mashabiki wa mpira na wakazi wa Mbeya ambao walijandaa kuonesha uzalendo kwa taifa lao. Kutokana na kitendo cha mechi hii kuhamishwa, Wanambeya walikoseshwa fursa za kujitangaza kiutalii na hatimaye kuchangia katika uchumi kulikosababishwa na Serikali ya CCM kuendelea kuhodhi viwanja vya michezo nchini. Rudisheni viwanja vya wananchi ili viendelezwe na kuwanufaisha wananchi.

6.2 KASUMBA YA MPIRA WA MIGUU KUWA MCHEZO PEKEE WA KIPAUMBELE.

Mheshimiwa Spika, kama Waziri kivuli mwenye dhamana ya kuisimamia Serikali katika masuala ya habari, vijana, utamaduni na michezo. Lakini ni dhahiri kuwa Wizara hii imeshindwa kusimamiwa ipasavyo katika sekta ya michezo, huku soka peke yake ikifanywa kuwa ni michezo unaopewa kila aina ya msaada na kuidharau michezo mengine. Kwa kifupi ni kuwa, Tanzania ina hazina kubwa ya wanamichezo ambao hawajatumika ipasavyo na wala Serikali haijawekeza vya kutosha katika kuhakikisha kuwa aina nyengine za michezo zinapewa kipaumbele. Kwa mfano, Filbert Bayi ni mwanariadha wa Tanzania ambaye alililettea taifa sifa kubwa kwa kushinda medali ya dhahabu mwaka 1974,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

tunaye mchezaji wa mpira wa kikapu nchini Marekani Hasheem Thabit anayechzeza NBA.

Mheshimiwa Spika, kama taifa kushindwa kuwa na orodha ya wana michezo ambao wamefanya vizuri katika medani ya michezo duniani na kuweza kuwahesabu kwa uchache wao, kunazua maswali mengi sana si kwetu tu bali hata kwa wadau wa michezo nchini ikiwa Serikali ina nia ya dhati ya kuendeleza michezo kwa ujumla.

6.3 MAKOCHA WA KIGENI NA MUSTAKABALI WA MICHEZO NCHINI

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu tumekua tukionesa wasiwasi kwa uamuzi wa Serikali kuendelea kuwaabudu makocha wa kigeni katika michezo. Hali hii si tu kuwa inadumaza soka, bali pia inavunja nguvu makocha wazawa pamoja na kuwakatisha tamaa vijana ambao wamekua na ndoto za kuwa makocha hapa nchini. Hii imekua ni Kasumba ambayo ina athari katika maendeleo ya michezo hapa nchini.

Pamoja na makocha wa kigeni kuabudiwa na baadhi ya viongozi wa michezo na wa kitaifa, makocha hawa wamekuwa na dharau kwa makocha wa nyumbani hali ambayo inadumaza maendeleo haya ya michezo. Imekuwa ni kawaida hata kwa baadhi ya viongozi wa soka wa klabu zetu na hata timu ya taifa kuwathamini na kuwatetemekeea makocha kutoka nje pamoja na kwamba tuna zaidi ya miaka 15 sasa na mlolongo mrefu wa makocha wa kigeni, lakini hawajaweza kuleta mafanikio makubwa yanayostahili majina makubwa ya klabu zetu na timu zetu za taifa.

Mheshimiwa Spika, umeshuhudia mara nydingi makocha kutoka nje wakiletwa nchini na kupokelewa na maandamano na shangwe na wanachama na wapenzi wa klabu husika kukifuatwa na kupewa mishahara minono, usafiri wa uhakika na nyumba za kisasa za kuishi. Kuna kocha wa timu mojawapo kubwa ya Tanzania alitaka nyumba atakayopewa kuishi lazima iwe na bwawa la kuogelea, na akapewa. Hii ni sawa na kuwa mtumwa ndani ya nyumba yako mwenyewe. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji ni nini ambacho makocha wa kigeni wanancho ambacho makocha wazawa hawana kinachofanya Serikali itenye kiasi cha **shilingi Bilioni 1.6** kwa ajili ya malipo ya makocha wa kigeni kwa timu za taifa na matumizi ya kawaida ya BMT bila mchanganuo?

Je, kwanini Serikali inaendelea kuajiri makocha wa kigeni wakati nchi kuna makocha wenyewe uwezo wa kufundisha timu za taifa? Je, ni kwanini serikali na wizara hii inasita kuwafadhili kimasomo makocha wazawa nje ya nchi ili waweze kutumikia taifa lao pindi wakimaliza masomo na mafunzo yao?

6.4 MWENENDO WA MCHEZO WA RIADHA

Mheshimiwa Spika: Tanzania imewahi kupata heshima kubwa kimataifa kutokana na mchezo wa riadha. Hata hivyo, katika mchezo huu pia nchi yetu iko katika ‘chumba cha wagonjwa mahututi’. Hali hiyo, inachangiwa na udhaifu wa kiuongozi, kisera, kimikakati na kioganzesheni kwenye mchezo wa riadha nchini kuanzia ngazi za chini mpaka taifa.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kwamba taifa letu linaweza kutolewa ‘kimasomaso’ na mchezo huu iwapo katika mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2013/2014 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2014/2015 riadha itapewa kipaumbele katika mjadala.

Mheshimiwa Spika: Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imekuwa ikitoa maelezo bungeni kwamba riadha nchini inaendelezwa kupitia wadau mbalimbali ikiwemo Chama Cha Riadha Tanzania (RT). Hata hivyo, Wizara haijawahi kutoa majibu kamili bungeni namna inavyoshughulikia migogoro na matatizo ya kiuongozi na kiutendaji katika chama tajwa hali ambayo inaathiri mustakabali mwema wa mchezo wa riadha nchini.

Kambi Rasmi ya Upinzani inataarifa kwamba kabla na hata baada ya uchaguzi wa Chama Cha Riadha Tanzania (RT) uliofanyika Morogoro tarehe 20 Mei 2012 kwa nyakati mbalimbali kumekuwepo malalamiko ya wadau wa mchezo huo juu ya uhalali wa uchaguzi huo pamoja na hali tete ya maendeleo ya mchezo huu. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ujibu bungeni maswali muhimu yafuatayo kuhusu mustakabali mwema wa riadha nchini:

Mheshimiwa Spika: Mosi, Baada ya kufanya vibaya katika mashindano ya Olimpiki yaliyofanyika London 2012 zilitolewa kauli na ahadi mbalimbali na Wizara na Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC) ya kufanya maandalizi bora kuelekea 2016 Rio De Janeiro Olympics; Wizara na Baraza la Michezo Tanzania (BMT) wanалиhakikishia vipi bunge kwamba maandalizi yamekamilika kuondoa ‘ukame’ wa medali na ‘aibu’ kwa taifa?

Mheshimiwa Spika: Pili, Kambi Rasmi ya Upinzani inafahamu kwamba kama sehemu ya diplomasia ya michezo Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa alilieleza bunge kwamba kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Vijana na Michezo ilipeleka vijana 50 pamoja na walimu wao kwenye makambi ya mafunzo katika nchi mbalimbali ikiwemo New Zeland. Baadhi ya vyombo vya habari viliripoti kwamba mwanariadha Atson Mbugi na Kocha Samwel Tupa nao wapo nchini New Zeland kwenye mazoezi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Hata hivyo, taarifa zilizoifikia Kambi Rasmi ya Upinzani ni kwamba wapo Tanga na Arusha. Je, ni kwanini wameachwa, wakina nani wamepelekwa badala yao na ni kwanini taarifa za uongo zilitolewa kwenye vyombo vya habari? Ni muhimu kwa Bunge kupewa taarifa kwa kuzingatia kuwa kwa nyakati mbalimbali zimekuwepo kashfa za wanamichezo wasio na viwango kupewa nafasi za wenyе vipaji na hatimaye kwenda kulisababishia aibu taifa. Aidha zimekuwepo pia kashfa za wengine kupernezwa kwenye misafara ya wanamichezo kwa ajili ya kubeba biashara haramu yakiwemo madawa ya kulevyo.

Tatu; Wizara na Baraza la Michezo Tanzania (BMT) walichukua hatua gani baada kupokea tahadhari ya wanariadha na wataalamu wa riadha juu ya madai ya uchaguzi wa chama hicho kuelekea kufanyika kinyume na Sheria na. 12 ya Baraza la Michezo ya mwaka 1967 kabla ya Mwenyekiti wa BMT Dionis Malinzi na Mkurugenzi wa Michezo Leonard Thedeo kwenda kusimamia Uchaguzi huo?

Mheshimiwa Spika; Nne; mara baada ya uchaguzi huo yapo malalamiko ambayo yaliwasilishwa kwa Waziri yenye kuwasilisha maelezo na vielelezo kuhusu namna uchaguzi huo ulivyokiuka sheria; je, ni sababu zipi zilizoifanya Wizara kutokutoa majibu yoyote juu ya madai hayo?

Tano; Inadaiwa kwamba viongozi wa Chama cha Riadha Tanzania (RT) walisaini Makubaliano ya Maelewano (MOU) mbele ya Viongozi wa Wizara na BMT kwamba marekebisho bora ya katiba ya chama hicho yangefanyika ndani ya siku tisini ambazo zilimalizika tarehe 20 Agosti 2012. Hata hivyo, taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani imeelezwa ni kwamba marekebisho hayo yaliyopaswa kuwezesha mustakabali mwema wa riadha nchini hayajafanyika. Je, Wizara imechukua hatua gani kwa chama hicho na viongozi wake kwa kwenda kinyume na makubaliano hayo?

Mheshimiwa Spika; Sita; Chama Cha Riadha Tanzania (RT) kimekuwa kikipokea fedha za maendeleo ya mchezo wa riadha kutoka Shirikisho la Riadha Duniani (IAAF) kwa ajili ya mashindano ya kitaifa na kimataifa. Aidha, Kamati ya Olimpiki (TOC) nayo imekuwa ikipokea fedha kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya pamoja na mambo mengine maandalizi ya wanariadha kwa ajili ya mashindano hayo. Kwa ujumla riadha imekuwa pia ikichangiwa kwa ajili ya maandalizi ya All African Games. Hata hivyo, pamoja na vyanzo hivyo, RT imeburuzwa katika mahakama ya Temeke kwa deni la milioni ishirini ambalo maelezo yake yana utata. Hali hii inaacha maswali kuhusu mapato na matumizi katika RT na TOC. Je, Wizara na BMT wako tayari kuwasilisha nakala ya taarifa zote za mapato na matumizi yaliyokaguliwa ya RT na TOC ya miaka ya fedha 2012/2013 na 2013/2014?

Mheshimiwa Spika; Kwa hali hiyo tete na tata ya kifedha ambayo inasababisha hata wakati mwagine wanariadha wa Tanzania kukosa vifaa vinavyostahili, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo kutoka kwa Wizara na BMT, ni nini kilisababisha udhamini wa kampuni ya Lining ya China kwa RT na wanariadha wetu wa toka mwaka 2007 kusitishwa? Je, uamuzi wa TOC kuingia mkataba mwagine na PUMA bila kujadili masharti ya mkataba mwagine uliokuwepo uliathiri vipi mkataba wa awali kwa kuzingatia kwamba yapo madai ya baadhi ya wadau wa riadha kwamba ilikuwa mikataba ya 'mtaka yote mkosa yote'?

Mheshimiwa Spika; Kwa kuzingatia uzito wa maswali hayo, pamoja na majibu yatakayotolewa na Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo katika majumuisho; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ifanye uchunguzi wa masuala haya na mengine yanayohusu RT na TOC ili kuwezesha mustakabali mwema wa mchezo wa riadha nchini. Hata hii italiwezesha bunge kupokea taarifa na kuitisha maazimio yatakayorudisha heshima ya taifa letu kimataifa katika mchezo wa riadha.

7.0 MBIO ZA MWENGE

Mheshimiwa Spika, kwa mufa mrefu Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekua ikipingana na utumiaji wa fedha za walipa kodi na kitendo cha Serikali kuendelea kuwatoza wananchi kwa mashinikizo bila ridhaa zao kuchangia shughuli za mbio za Mwenge wa Uhuru. Ni kweli kuwa Mwenge wa uhuru ni hazina kwa taifa letu jambo ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakubaliana nalo na kwa muda mrefu tumependekeza Mwenge wa uhuru uwekwe katika makumbusho ya taifa ili kuweza kuwapatia fursa wananchi kuweza kujifunza hapo.

Mheshimiwa Spika, Suala la kuenzi utamaduni wa Taifa ni la lazima lakini kuendelea kutumia gherama kubwa kwa jambo hili wakati Watanzania wengi hawana huduma muhimu ni dharau kubwa.

Aidha, katika kipindi hiki ambacho mwenge wa uhuru unapitishwa katika sehemu mbalimbali za nchi, chama tawala nacho kinapita katika maeneo mbalimbali ya nchi kuangalia utekelezaji wa ilani yake pamoja na kuzindua miradi ya maendeleo ya wananchi. Huu ni usanii mkubwa unaofanywa na Serikali ya CCM kwa dhumi la kuwanyonya watanzania masikini kwa kigezo cha kuwa wanachangia shughuli za maendeleo wakati ukweli ni kuwa watanzania wanachangishwa mpaka fedha kwa ajili ya malazi na chakula kwa wakimbiza mwenge kama alivyojibu Waziri Mkuu. Na kwa kuwa kumekua na

Nakala ya Mtandao (Online Document)

malalamiko kutoka wa wafanyabiashara, wafanyakazi wa Serikali na hasa walimu sehemu mbalimbali nchini kuwa wanalazimishwa kuchangia mwenge bila ridhaa yao. Na kama CCM inataka bado mambo ya mbio za mwenge basi wagharamie wenyewe kwa asilimia 100 na si kuwalazimisha wananchi kuchangia hasa ukizingatia kuwa Waziri Mkuu alitoa kauli wiki hii kuwa kuchangia mbio za mwenge wa uhuru ni hiyari.

Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kusitiza kuwa sasa ni wakati muafaka mwenge wa uhuru kupelekwa jumba la Makumbusho ya Taifa.

8.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha hoja za Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na michezo kwa kulitaka Bunge lako tukufu kuishinikiza Wizara kutekeleza maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambayo Wizara imekua ikiyakubali kwa muda wa miaka mitatu mfululizo.

Aluta Continua.

Mheshimiwa Spika, Baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha

.....

Joseph Osmund Mbilinyi (Mb)

**Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-Wizara ya Habari, Vijana,
Utamaduni na Michezo**

29.5.2013

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Wizara hii nyeti. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliye asili ya mema yote, aliye niwezesha afya na nguvu ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, vijana ndiyo nguzo ya Taifa na bila vijana hatuwezi kuwa na Taifa lililo imara. Kwa hiyo, ninapozungumzia vijana, nazungumzia nguvu kazi ya Taifa. Vijana hawa wamekuwa na changamoto nydingi na wao ndio wajenzi wa Taifa letu. Naomba Serikali ingewaangalia sana vijana na iweke mikakati imara ya kuwawezesha vijana waondokane na umasikini na usumbufu walionao sasa hivi.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, nikianza na huu Mfuko wa Maendeleo wa Vijana, ambao ni asilimia tano katika Halmashauri zote nchini. Mfuko huu naona unatolewa labda kwa baadhi ya vijana lakini siyo kwamba unawanufaisha vijana wote. Vijana wamekuwa wakilalamika nao sana na wengi hawaelewi maana ya mfuko huu. Sasa Serikali ingetuambia, huu mfuko unatolewa kwa vijana wa aina gani? Kila Bunge la Bajeti, ingekuwa inatolewa taarifa jinsi mgao wa fedha hizi unavyokuwa kwa vijana waliozipata; wamezipata vijana wangapi? Wanatoka maeneo gani na wakatajwa majina yao ili wananchi wote wawe wanaelewa huu mfuko uliishia kwa vijana gani? Kwa sababu wengi hawajui mfuko unatumika na vijana gani?

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba sasa hivi Wizara ya Elimu imetambua kwamba somo la ujasiriamali ni muhimu sana kurudisha mashulenii. Kwa sababu ukiangalia kuhangai kwa vijana, kunatokana na mfumo mbovu wa elimu ambao hauelengi kumkomboa kijana Mtanzania. Vilevile ajira, kwa sababu elimu imekuwa inalenga kuwafundisha vijana wetu wategemee kuajiriwa na siyo kujajiri wenyewe, ndiyo mfumo wetu wa elimu ulivyowajenga. Sasa naomba Wizara ya Utamaduni ikae pamoja na Wizara ya Elimu kuhakikisha ni jinsi gani wanawasaidia vijana wa Tanzania kujikomboa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vijana nimemaliza, naingia kwenye sekta ya utamaduni.

Mheshimiwa Spika, utamaduni ni utambulisho wa asili wa Mtanzania kupitia kabile, mavazi, mpaka vyakula. Lakini leo ukiangalia asilimia kubwa ya Watanzania, yaani tumekuwa tuna-base zaidi kwenye utamaduni wa nchi za wenzetu kuliko utamaduni wetu sisi wenyewe. Nailaumu sana Serikali, imetufikisha mahali pabaya, maadili ya nchi yamemong'onyoka, tunaishi ili mradi tupo, hatujui tunafanya nini na tunakwenda wapi na vizazi vyetu. Inasikitisha na inatia uchungu sana kuona vizazi vyetu havina mwelekeo sasa hivi kutokana na sisi wakubwa tumeshindwa kuonyesha njia namna ya kulea vijana wetu au watoto wetu na vizazi vyetu vinavyokuja.

Nikienda upande wa mavazi, tangu tumeanza kusikia kuna vazi la Taifa litaonyeshwa lakini mpaka hivi leo kimya. Kwa hiyo, sasa hivi Watanzania tunavaa tu ili mradi tupo tunavaa. Ukienda madukani, mwanamke anaweza kuchukua saa nzima anachagua nguo, anatafuta vazi la mwanamke halionekani. Nguo tunaletewa za wenzetu nje, utakuta magauni ya akina mama ni mikono ya shumizi tu; mikanda imeenea mabegani, nyama zetu migogo iko wazi. Tunavaa nguo zisizokuba na heshima mbele ya watoto wetu, tutafanya nini ndizo tulizoandaliwa madukani? (Makof)

Nakala ya Mtando (Online Document)

Vazi la mjamzito sasa hivi halithaminiki, limepoteza kabisa thamani yake. Unakuta mwanamke ni mjamzito, mama mzima kama Mheshimiwa Anna Mallac hapa, lakini anavaa suruali, anafinya tumbo lake wakati lile tumbo linatakiwa liachiwe nafasi na yule mtoto wa ndani apumue. Lakini suruali imebana, mama kavaa kishati cha kubana kafunga na mkanda jamani. Tunakwenda wapi na Maafisa utamaduni wanaona? Hawa Maafisa Utamaduni kazi yao ni nini? Kazi yao ni kukaa Ofisini?

Mheshimiwa Spika, naomba Maafisa Utamaduni kama kweli wapo, wajue kazi yao jamani, watembelee wananchi, wajichanganyie katika jamii kuelimisha jamii. Hali ni mbaya tunakokwenda, itatutesa tunakokwenda. Leo watoto wetu wa kike ukiwaona, hawana mavazi, *tight* ndiyo limekuwa vazi. Ile *tight* mimi naifananisha na nguo ya ndani. Unakuta mama mtu mzima, mnene, amevaa *tight* imebana, nyama zimegawanyika! Jamani, ni aibu! Ni aibu jamani! Inabidi wewe unayemwangalia ndio unasikia uchungu moyoni, lakini huwezi kutoka ukamweleza kwa sababu Viongozi wetu wa Serikali yetu ya sasa wamekosa ubunifu na wanaangalia.

Kwa hiyo, naomba hilo Serikali iangalie sana katika mavazi. Tutawasemaje mabinti wetu au vijana wetu wanaovaa nguo zisizokuwa na heshima wakati sisi ndio mavazi yetu wakubwa? Kwa hiyo, inabidi ukiangalia unaishia kunyamaza. Naomba Serikali ilisimamie sana hilo. Maafisa Utamaduni wasikae Ofisini.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye suala la wanahabari; naomba Serikali ipitie upya sheria zake, itoe uhuru kwa wana habari kupata habari sehemu nyingi ikiwemo Magereza na Mahakamani ili waweze kuwahabarisha wananchi jinsi tunavyokwenda. Kwa sababu sehemu kama hizo waandishi wa habari hawaingii Magereza na kule ukiangalia kuna wananchi wenzenet hata kama wako kwenye sehemu ya kujifunza, lakini nao wana maoni yao ambayo wanaweza kuyatoa kwa wanahabari na wanahabari wakatuhabarisha.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali ijipange kuboresha upya sheria zake. Wanahaba... (Makofi)

(*Hapa kengele illilia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji*)

SPIKA: Ahsante, muda umekwisha. Sasa namwita Mheshimiwa Ester Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Rage.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara ambayo inanihu sana, kama mwakilishi wa vijana, lakini na mimi kama mwandishi wa habari.

Mheshimiwa Spika, ningependa kwanza kutoa pole kwa Waandishi wenzangu kwa kupotelewa na mpiga picha Max wa Kituo cha Mlima TV, tunamwombe Mungu amemlaze mahali pema peponi. Lakini pia natoa pole kwa Bongo Movie kwa kuendelea kupotelewa na wasanii pamoja pia na kumpoteza mzee wetu Gurumo.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waandishi wenzangu kwa kufanya kazi katika mzingira magumu na mimi kama mwandishi mwenzao, nimo humu ndani, nitaendelea kuwatetea kwa nguvu zangu zote pamoja na kudai haki za msingi za kupata habari na kuhakikisha Muswada wa Waandishi wa Habari unaletwa ambaa utajali maslahi yao na kuweka misingi mizuri ya kutokiuka maadili ya uandishi wa habari. Tuko pamoja nitaendelea kuwapigania.

Mheshimiwa Spika, mimi sina kawaida sana ya kutaka kujibu au ku-question vitu ambavyo pia vinasemwa na wenzetu ambaa pia wanasaidia kuboresha mawazo mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi anachangia kuminya uhuru wa vyombo vyahabari kwa vikao vyahabari, siyo kweli. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, leo hii tukiuliza, Rais ambaye amehakikisha kila mtu ana uwezo wa kusema anachotaka, kuandika anachotaka, ni Rais, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Ametoa mwanya kwa watu kutoa maoni yao, mawazo yao bila kushurutishwa. Tunatambua kuna changamoto mbalimbali. Kama Wabunge, kama Viongozi, tuweze kukaa katika Bunge hili Tukufu kuhakikisha tunaweka mazingira gani mazuri ya kuhakikisha waandishi wanapata habari na wanapata uhuru wa kutoa habari. Hilo ndiyo jambo la misingi! Lakini ndiye Rais wa kwanza ambaye amehakikisha kwamba kuna uhuru mkubwa wa kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, unaposema CCM kinaminya au hakitaki kuhakikisha kuna uhuru wa vyombo vyahabari. Bunge lilllopita, Mheshimiwa Peter Serukamba, mimi, tukishikiriana na baadhi ya wenzetu kutoka opposition Mheshimiwa Tundu Lissu tulimzuia Mwanasheria hapa Bungeni ili Sheria ambayo ilikuwa inakandamiza Waandishi wa Habari isipite. Kweli Mwanasheria hakufanikiwa kupita.

Leo hii unaposema Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi au Chama cha Mapinduzi hakipendi uhuru wa vyombo vyahabari, *it is quite*

Nakala ya Mtando (Online Document)

unfair. Lazima tuwe wakweli! Tulishirikiana wote humu kuhakikisha sheria ile haipiti, tukasema uje Muswada kamili utakaojali Waandishi wa Habari na utakaoweka mazingira mazuri ya kuhakikisha Waandishi wa Habari wanafuata ethics za uandishi wa habari. (Makofij)

Narudia waandishi wenzangu, nitakuwa wa mwisho kuwasaliti katika kuhakikisha haki zenu zinaminywa, kwa sababu nimeanzia katika u-correspondent na nitahakikisha haki zenu zinapatiwa ufumbuzi ndani ya Bunge hili Tukufu, lakini sitakuwa wa kwanza kuhakikisha kuna taarifa zinapotoshwa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kuweka hayo sahihi. Pande zote mbili tunajua umuhimu wa Waandishi wa Habari na tutawatetea kuhakikisha haki zao za msingi zinapatikana. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, pia waandishi wa habari wengi wanafanya kazi katika mazingira magumu, wengine hawana mikataba, wengine wanateseka pamoja na kupata taabu na Waajiri kutowapa ajira na kuwalipa malipo madogo. Hayo ni mambo ya msingi ambayo yanatakiwa yazingatiwe katika huo Muswada utakaoletwa. Mimi nasema nilianzia huko, najua shida ya Waandishi wenzangu wanayopata.

Kwa hiyo, hayo yote Mheshimiwa Fenella nakuomba katika Muswada wa Wandishi wa Habari yazingatiwe, wapate malipo stahiki pamoja na haki ya msingi ya kupata habari lakini vilevile tunahakikisha tunafuata maadili yetu.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia suala zima la Wizara hii kupewa bajeti ndogo. Tumekuwa tukisema, vijana ni asilimia 61. Mwaka 2013 wameombwa hela, hamkuwapa. Mfuko wa vijana hauna fedha! Leo hii mnatumbia mmewaongezea Shilingi bilioni 35, hizo ni kiini macho, hazitoki! Tunaomba fedha za vijana zitoke! Kama kweli mnaona sisi ni asilimia 61 ya Watanzania, ndio wapiga kura wenu tegemezi! Tunaomba fedha za vijana zitoke. Tumechoka kuwa mnatenga fedha ambazo hazitoki!

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Vijana haina hela, SACCOS za vijana hazina hela; kila siku mnatuambia mnatenga fedha! Kutenga fedha ni jambo lingine na fedha kutoka kwa ajili ya vijana, ni jambo lingine.

Mheshimiwa Spika, nahakikisha nitakuwa mkali, fedha zinazokwenda kwa vijana mara mia ziwekewe *ring fence* ili tujue zinakwenda. Lakini mambo ya kutuambia mnatenga Shilingi bilioni sita, halafu wanapata Shilingi bilioni moja, haiwezekani, kwani vijana hawana ajira. Vijana wako wanarandaranda Mtaani!

Mheshimiwa Spika, katika hili nitakuwa mkali. Mheshimiwa Waziri, nakwambia nitakamata Shilingi. Fedha za vijana mtakazozitenga tunaomba

Nakala ya Mtando (Online Document)

mzitoe. Tumechoka kutengewa fedha hewa, haziendi; vijana vijijini wanalamika hawana hela. Hilo ni jambo la msingi.

Kagine, tunaomba shirika la TBC mlipe fedha. Mnawatengea Shilingi biloni sita, mnawapa moja, halafu mnawategemea watarusha matangazo nchi nzima! Wapi? Hiki ni chombo cha Taifa, ni aibu! Ukienda mwisho sometimes unakuja kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma, katikati husikii kitu. Halafu mnataka warushe; warushe wapi? Wapeni hela!

Mheshimiwa Spika, Serikali inaongoza kudaiwa na TBC! Muwalipe! Walipeni! Mnataka habari zenu zirushwe, zitarushwaje kule vijijini wakasikia? Mitambo inakatakata! Tunalamika hapa, ooh TBC imekata. Imekata kwa sababu hawana hela. Vifaa vyao vibovu, kila sehemu vimefungwafungwa halafu mnategemea watafanya kazi nzuri hapa ya Taifa kuhabarisha Umma? Wapeni hela! Hilo ndiyo jambo la msingi.

Mheshimiwa Spika, Bunge pia mnadaiwa, Ofisi yako, walipeni TBC. (Kicheko/Makofii)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Kwa hiyo, umenidai, na mimi nimekuzimia microphone! Muda wake ulikuwa umekwisha jamani, sijamzimia. (Kicheko)

Sasa namwita Mheshimiwa Ismail Rage, atafuatiwa na Mheshimiwa Rebecca Mgodo.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ningependa kukushukuru na ningependa kuchukua nafasi hii kuwaomba wanachama wa Simba watulie, waache vurugu ili utaratibu wao wa uchaguzi uende katika utaratibu mzuri na hatimaye wapate viongozi wazuri.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuunga mkono bajeti ya Wizara hii. Pia nilikuwa napenda kutoa mapendekezo yangu.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Michezo la Taifa lilita sheria Bungeni hapa, Na. 12 ya mwaka 1967, halafu ikaletwa tena Sheria ya kufanyiwa marekebisho Na. 6 ya mwaka 1971, sasa tuko mwaka 2014. Baraza hili limepitwa na wakati, sheria zile zimepitwa na wakati. Ujisoma katika baadhi ya kanuni katika zile sheria, mojawapo inasema; ukitaka kuwa mgombea, lazima uwe mwanachama wa TANU chombo ambacho hakipo sasa hivi. Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa kwamba iko haja sheria hii iletwe tena hapa Bungeni ili tuweze kuifanya marekebisho makubwa.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu sasa hivi kuna mabadiliko makubwa katika nyanda za michezo hapa duniani. Kwa mfano, *TFF* ni mwanachama wa *FIFA*. Kwa mujibu wa Sheria za *FIFA* Serikali hairuhusiwi kuingilia masuala ya michezo. Masuala ya michezo hayaruhusiwi kupelekwa Mahakamani.

Kwa hiyo, ili tutende haki, Katiba ya Jamhuri ya Muungano inasema wazi kwamba kila Mtanzania ana haki ya kwenda Mahakamani. Kwa hiyo, iko haja sasa Sheria ya Baraza la Michezo ifanyiwe marekebisho na yenyewe iingize kwamba wanamichezo hawaruhusiwi kupeleka masuala yao katika Mahakama ya Sheria isipokuwa wafuate utaratibu unaokubalika. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na matatizo, ndugu zetu wa Zanzibar wana hamu ya kuijunga na *FIFA*. Mimi huko nyuma nimepata bahati ya kuwa Katibu Mkuu wa *TFF* na Makamu wa Rais. Ukweli kwa mujibu wa Katiba ya *FIFA*, nchi ambayo inaruhusiwa kuwa mwanachama ni nchi mwanachama wa *United Nation with exception* ya zile nchi zilizoanzisha *FIFA* yaani Scotland, Wales ndiyo zinaingia kama wao peke yao, lakini kwa nchi nyingine, ukitaka kuwa mwanchama wa *FIFA* ni lazima uwe mwanachama wa *United Nations* kwanza.

Kwa hiyo, kwa kuwa Zanzibar siyo mwanachama wa *United Nations*, nilikuwa naomba, hakuna haja ya kila wakati kumzonga Waziri kwamba asaidie Zanzibar kuwa wanachama wa *FIFA*. Ukweli ni huo, ndiyo Katiba inasema hivyo. Hata Wajumbe wanaokwenda kwenye Mkutano wa *FIFA*, mnaweza kwenda watu zaidi ya watano, lakini kwa mujibu wa Katiba ya *FIFA*, anayeruhusiwa kupiga kura ni Rais wa *TFF*, ana vote moja na wengine wote wanakwenda kama observers tu, wala kuchangaia, hawachangii. Watakaa mle ndani kama sanamu.

Kwa hiyo, nilitaka tu kuliweka hili mapema ili Mheshimiwa Waziri asipate taabu tena ya kuulizwa masuala haya. Sasa nini tufanye ili kuleta uwakilishi halali kati ya Tanzania Bara na Visiwani? Ni wakati muafaka sasa, *Tanzania Olympic* iko pande zote mbili, kwa maana tuna Chama kimoja tu cha Tanzania, kule Zanzibar hakuna na Rais wake sasa hivi anatoka Zanzibar na Katibu Mkuu anatoka Bara.

Sasa hivi ni wakati muafaka kati ya *TFF* na *ZFA* kuungana na kufanya chama kimoja ili tuepushe ile dhana ya kwamba misaada inayoletwa *FIFA* labda wenzetu wa Zanzibar hawapati au nini? Kwa hiyo, tuungane kati ya *TFF* na *ZFA* tupate Chama kimoja ambacho kitakuwa kinahudumia nchi zote mbili, yaani Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, ningependa vilevile kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri yeye mwenyewe binafsi kwa juhudhi yake kubwa ya

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kuanzisha na kusaidia kundi za vijana mbalimbali. Pale Igunga katika Mkoa wa Tabora, kwa juhudzi zake ameweza kutusaidia, kuna vijana wasomi wameanzisha mashamba yao, tena wale wote ni graduates, wana mashamba mazuri, wanaendelea vizuri. Kutohaka na juhudzi zake, ameweza kuwasaidia pale wakapata trekti.

Kwa hiyo, mimi naomba aendelee, kwa sababu sasa hivi tuna Kambi ya Vijana pale Sikunge kwa ndugu yangu, Mheshimiwa Said Nkumba, hakuna mfano wake. Kuna vijana 100 na wote wanajengewa nyumba za kisasa ili waweze kuishi pale pale kijiji; watakuwa na mashamba yao. Kwa hiyo, nadhani kazi yetu sisi isiwe kupiga kelele ndani ya Bunge hili tuongezewe hela, kazi ya Wabunge ni kwenda kuanzisha miradi ya vijana na kuomba hela na hela zinapatikana. Hiyo, ndiyo njia rahisi ya kuweza kuisaidia Serikali yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, pale Manispaa ya Tabora Mjini tuna kambi ya vijana tumeanzisha katika Kata ya Ikomwa na mimi nimejitolea, nawapatia trekti langu na vifaa vya kulimia bure kabisa. Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Waziri atakapoanza kukumbuka kusaidia vijana, basi na hawa vijana wa kule Tabora watakumbukwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante sana. Hongera kwa initiative hiyo. Sasa nimwite Mheshimiwa Rebecca Mngodo, atafuatiwa na Mheshimiwa Catherine Magige, na Mheshimiwa Neema Hamid Mgaya ajiandae.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimshukuru sana Mungu kwa sababu ameifanya siku hii ili tupate kuifurahia na tupate kuishangilia. (Makofii)

Kwa kuanza nataka niwapongeze sana watoto walio under 15 ambao wamejitahidi sana kufanya michezo hata katika Mikoa ile ambayo premium league hairuhusiwi, kwa mfano, kule Kigoma. Hivyo, naiomba Serikali na hasa Wizara iangalie jambo hilo. (Makofii)

Pia, Tanzania tulikuwa na sifa kubwa katika ile miaka ya 1970 ambapo Mtanzania wa kwanza, Filbert Bayi aliweza kuvunja record ya kukimbia mita 1500 kwa dakika tatu na sekunde 32 nukta moja sita. (3:32.16). Dunia nzima mpaka leo miaka 40 baadaye, bado inamuenzi Filbert Bayi. Lakini kwa hapa Tanzania ninasikitika sana kwamba Filbert Bayi anajikwamua yeye mwenyewe kwa kuanzisha mashule na kujitangaza mwenyewe, lakini Wizara au Idara katika

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Wizara inayohusika na Wanariadha, sioni kama kuna jambo lolote linalotendeka. (Makofi)

Mungu ametupa upendeleo katika nchi yetu; katika Bonde la Ufa kuna makabila ambayo wao kimaumbile wanaweza kukimbia masafa mrefu, lakini hatuna chochote! Nchi yetu haifanyi chochote kuwaendeleza vijana katika Bonde la Ufa ambao wao kimaumbile wanaweza kukimbia masafa mrefu! Haiwezekani tuwe na Filbert Bayi mmoja tu tangu miaka ya 1970 mpaka leo. Tunahitaji kuona Wizara ikifanya jambo. Tunahitaji kuona Wizara, Serikali ikitengeneza Filbert Bayi wa leo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzungumzia Kiswahili, Kiswahili ni mali. Wenzetu wa Kenya wanalifahamu hilo na kwa sababu hiyo, wao wanajinadi, wanajuza katika masoko ya dunia. Napendekeza kwamba na sisi Watanzania hasa wale wenye fani ya Kiswahili wajinadi wao wenyewe, wasisubiri Serikali kwa sababu kimsingi Serikali au Wizara haiwasaidii lolote. Watu wamezungumza sana, lakini hakuna kinachoendelea. Kwa hiyo, wajinadi wao wenyewe. Pia, Serikali katika Mikutano ya Kimataifa, itumie Kiswahili katika kutoa taarifa zao ili kutoa nafasi zaidi kwa watafsiri na wakalimani ili wapate ajira.

Sambamba na lugha ya Kiswahili, ningependekeza pia lugha ya Kiswahili iendane na lugha ya kimavazi. Kwa sababu ukimwona Mnigeria utamjua ni Mnigeria kwa kuona mavazi aliyovaa. Watanzania tunatambulika kwa Kiswahili kwa kuongea Kiswahili sanifu. Pia tuwe na lugha ya kimavazi ili tuweze kuendelea zaidi kutangaza lugha yetu na mavazi yetu ulimwenguni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye tasnia ya habari ambayo inafanya kazi nzuri sana hapa Tanzania, inafanya kazi ya kuhabarisha, inafanya kazi ya kuelimisha na inafanya kazi ya kuburudisha, lakini katika mazingira magumu sana. Kwa miaka saba, Muswada wa kurekebisha sheria ile kandamizi ya mwaka 1976, ambayo imeendelea kukandamiza Waandishi wa Habari.

Hapa katika ukurasa wa tisa, Mheshimiwa Waziri anasema kwamba Wizara yake imekamilisha maandalizi ya Muswada wa Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari na sasa uko katika hatua nzuri. Nasikitika kusema kwamba maelezo haya yalikuwepo katika kitabu cha mwaka 2013, yalikuwa hivi hivi kwamba Wizara imeshakamilisha na kwamba sasa wako tayari kuleta Muswada Bungeni.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012 nilipata bahati ya kwenda na Kamati ya Maendeleo ya Jamii kule India. Tulikwenda kujifunza Baraza la Habari la India linavyofanya kazi na bahati nzuri Mheshimwia Nkamia ndiye aliyekuwa Mkuu wa msafara ule na ninaamini kwamba atasimamia vizuri kwa yale tuliojifunza kwa sababu tulikuwa pamoja naye. Mambo tuliojifunza ni ya msingi sana, kwa

Nakala ya Mtando (Online Document)

sababu yanasaidia siyo tu Waandishi wa Habari kuwa na uhuru wa kupata na kutoa habari, lakini pia na Serikali kuwajibika kwa wananchi. Wananchi wanakuwa na uhuru wa kuiwajibisha Serikali kwa yale ambayo hayajafanyika, lakini pia kuondoa mawazo mgando ya Serikali pale ambapo wanashindwa kuwashirikisha wananchi wajue wajibu wao na hivyo walete maendeleo katika nchi yetu. Ndiyo tulijifunza kule India.

Tulijifunza pia kwamba waliojitihadi kuleta Muswada ule walikuwa ni watu wa kawaida kabisa na ndio waliopigania ule Muswada mpaka ukafanywa sheria, ambapo kila mwananchi wa India ana haki ya kupata habari. Tunataka ulinzi kwa wanatasnia wa habari, tunataka ulinzi kwa wananchi, tunataka wananchi wapate taarifa ya jinsi ya kutumia kwa mfano, mbolea. Tunataka wapate taarifa na wasikae tu mbumbumbu. Kwa sababu wanapozidi kuwa mbumbumbu wanazidi kuwa mtaji wa CCM; wanazidi kuwa mtaji wakati wa kura kwa sababu hawaelewi na tunataka wapate habari kwa wakati na ninaomba sana isiwe kama ilivyoandikwa kwamba tayari sasa utaletwa katika Bunge lijalo la Katiba.

Mheshimiwa Spika, naomba kwamba Wizara iangalie umuhimu wa kuwaharakisha ili Muswada huu uweze kuletwa na Sheria iweze kuletwa na kutungwa ili kulinda wanahabari ambao kimsingi wanafanya kazi katika mazingira magumu sana.

Napenda kuzungumzia pia waandishi wa habari kwamba wanahitaji kuwa na Bima ya Maisha yao ili waweze kupata fidia pale ambapo wanakuwa wameumia kazini au wamepoteza maisha kama vile Daudi Mwangosi aliyeuliwa kule Iringa lakini tunahitaji kwamba waandishi wapatiwe Bima.

Vile vile ili pia kupunguza makanjanja ambao wanaingilia tasnia ya habari, kuwepo na vitambulisho maalum. Wanahabari wawe na vitambulisho, wanapokuwa kazini tujue kwamba huyu ni mwanahabari. Hii itasaidia sana kupunguza na kuondoa makanjanja ambao mara nyingi tumelalamika kwamba habari imepotoshwa, habari haijafanyiwa utafiti, habari haina uwiano. Inakuwa hivyo kwa sababu hakuna sheria ya kuwabana. Lakini pale ambapo sheria itakuwepo, basi tutaona kazi inafanywa kwa kufuata maadili ya kazi ya uandishi wa habari.

Mheshimiwa Spika, napenda pia sasa nizungumzie kuhusu mavazi; nadhani nimeshazungumzia mavazi, na ninaomba niishie hapo. (Makof)

SPIKA: Umeshazungumzia mavazi. Mheshimiwa Catherine Magige, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Hamid.

Nakala ya Mtando (Online Document)

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Awali ya yote, napenda kupongeza hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana Utamaduni na Michezo, ambayo ameitoa, kweli ni hatuba nzuri ikifuatiliwa na bajeti yake ikiwekwa vizuri. (Makofii)

Vilevile naomba niipongeze Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na Taasisi zake likiwemo Shirika la Habari la Utangazaji la TBC ingawa Wizara hii imekuwa ikitengewa bajeti kidogo sana tofauti na shughuli zao. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Shirika la Habari la TBC linahitaji kuwezeshwa. Mwaka 2013 lilitengewa bajeti ya Shilingi bilioni sita, lakini hadi sasa hivi, fedha ambayo wameshapata ni Shilingi bilioni 1.7, ambayo kwa changamoto ambazo wanazo TBC, na kwa matatizo mengi ambayo yanalikabili Shirika hili pamoja na watangazaji wake ni fedha ndogo sana. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nakuwa sielewi, kwa sababu hapa Bungeni tunapitisha fedha zote hizo, lakini hazifiki kwa walengwa. Tunakaa wakati mwingine tunamlaumu Mheshimiwa Waziri, lakini Serikali kwa nini inakuwa haipeleki fedha hizi? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naomba commitment ya Serikali, katika Shilingi bilioni sita hizi ambazo zilitengwa, wamepewa bilioni 1.7, hizi fedha nydingine TBC watapewa lini? Mheshimiwa Waziri, naomba wakati wa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, unipatie jibu hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba moja kwa moja niende katika suala la zima la ajira kwa vijana. Suala la ajira kwa vijana lisipopewa kipaumbele, litavuruga amani ya nchi yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, vijana wakikosa ajira wanafanya mambo ya uhalifu. Kama vijana wangu wa Mkoa wa Arusha; hawana ajira, ndio maana hata maandamano yakiitwa wanakimbilia kuandamana. Naomba Serikali iangalie vizuri suala hili kwani vijana wanateseka sana. Tumeona vijana wanatumikishwa kwenye mambo ya uhalifu, vijana wanabebeshwa madawa ya kulevyia. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa ajira kunaharibu maisha ya vijana. Tusipochukua tahadhari, Taifa lijalo litakuwa na vijana wavuta bangi, litakuwa na vijana wauza madawa, kwa kweli tutawaachia kizazi kijacho Taifa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

lisiloeleweka. Tunaomba Serikali ijipange, iweke mikakati, ni jinsi gani itawasaidia vijana ili waweze kujajiri. (Makof)

Mheshimiwa Spika, tumeona vijana ndio wanajiingiza kwenye masuala ya madawa ya kulevyo. Naomba nitoe pongezi zangu nyingi kwa msanii Rehema Chalamila (*Ray C*); msanii huyu alikuwa anatumia madawa ya kulevyo, lakini alijitambua, ameacha kutumia madawa ya kulevyo na sasa hivi ameanzisha Taasisi yake ambayo inawasaidia vijana wajitambue, waweze kuacha kutumia madawa ya kulevyo na waweze kupata dawa za kuwasaidia. (Makof)

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali iangalie ni jinsi gani itamuunga mkono msanii huyu, kwa sababu kazi anayoifanya ni kubwa, na kama tunavyojuu, wasanii ni kioo cha jamii, kwa kuitia ye ye tutaokoa vijana wetu wengi sana. Naomba sana Serikali iangalie suala hili. (Makof)

Mheshimiwa Spika, vile vile nilikuwa naomba wazazi waangalie vijana wao wanapopata matatizo haya, wajaribu kukaa nao karibu wawashauri kama alivyofanya mama yake huyu msanii. Kwa sababu tunapowatupa vijana ndiyo wanaenda wanakuwa wadokozi, wanakuwa vibaka huko, tunakuwa tuneshaharibu vijana wetu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja katika suala la wasanii wetu. Kwanza kabisa naungana na Waheshimiwa wenzangu ambaa wamepita, kutoa pole nyingi sana kwa wasanii kwa misiba iliyotokea, na hata leo kuna baadhi ya msanii mmoja nadhani wanamzika leo. Mungu awalaze mahali pema Peponi, nawapeni pole sana. (Makof)

Mheshimiwa Spika, wasanii wetu wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana, wamejiajri, wamepunguza kiasi kikubwa cha tatizo la ajira. Tumeona wasanii wana maisha mazuri sana, nawapongeza kwa hilo; lakini sasa naomba Serikali iendelee kuwabana wale wanaowabana wasanii, na wanaowatumia wasanii kujinufaisha wenyewe. Naomba Serikali isimamie vyema haki za wasanii ili wasanii hawa waweze kuwa wasanii wakubwa na wenyе fedha kama tunavyoona wasanii wengine nje ya nchi. Nina imani Serikali ikitilia mkazo, tunaweza. (Makof)

Mheshimiwa Spika, naomba moja kwa moja niongelee waandishi wa habari. Wandishi wa Habari, wanaishi katika mazingira magumu sana, wanafanya kazi katika mazingira hatarishi, lakini Serikali tunaomba mliangalie hilo, nadhani hamlioni, wasaidieni Waandishi wa Habari. Vilevile tunaomba Muswada wa Sheria wa vyombo vyaya habari uharakishwe, uletwe haraka hapa Bungeni ili Waandishi wa Habari waweze kujua pia maadili yao.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, tumeona waandishi wa habari wanafanya kazi nzuri, lakini kuna baadhi hawafuati maadili ya uandishi wa habari, wamekuwa wakiandika habari za uchochezi, za ugombanishi na za kutunga. Kwa hiyo, utakapoletwa Muswada wa Sheria wa Vyombo vya Habari, utasaidia sana, na wenyewe watakuwa wana mipaka yao, na vilevile watakuwa na haki zao ili tulete heshima kwenye tasnia nzima hii ya habari. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuiomba Wizara hii ya Habari, Vijana, Michezo na Utamaduni, washirikiane kwa karibu na Wizara ya Kazi na Ajira ili kuangalia wimbi hili la vijana wanaomaliza Vyuo watakwenda wapi; kuwasaidia waweze kupata ajira. Maana wamekuwa wanazunguka Mitaani sana, matokeo yake ndiyo wanajiingiza kwenye uhalifu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana Serikali ishirikiane na Wizara hizi mbili, wanaweza; wawasaidie vijana hawa ili wasidhurure Mitaani. Hata wasipopata ajira, waangalie ni jinsi gani ya kuweza kujiajiri. (Makofii)

Tumeona mfano Igunga pale kwa yule Mkuu wa Wilaya Ndugu Kingu, tumeona vijana walivyosaidiwa na Serikali, wakajiajiri, wanapata mapato makubwa sana. Mimi najua Mheshimiwa Waziri tunaweza tukafanya vile Arusha, Shinyanga, kila Mkoa tunaweza tukafanya vile. (Makofii)

Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iangalie na Mikoa mingine na Wilaya nyingine zote hapa nchini, kuwasaidia vijana ili tukwepe hatari inayokuja. Baada ya miaka kadhaa tuwe na vijana ambao hawataki utegemezi, watakuwa wanaweza kujitumikisha wenyewe, kujiajiri, kufanya kazi, ili baadaye hata tuwe katika historia, tuwe tumemaliza tatizo hili la ajira na tuwe na vijana ambao wanaelewa wanafanya nini na kuongeza uchumi wa Taifa letu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante. (Makofii)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Neema Hamid Mgaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali.

MHE. NEEMA M. HAMID: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Habari, Vijana, Michezo na Utamadauni. Nianze kwa kusema kwamba Wizara hii tumeipangia bajeti ndogo sana. Shilingi bilioni 33.5, kwa kuzingatia unyeti na umuhimu wa Wizara hii ni ndogo sana. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kwamba Wizara hii inashuhulikia maendeleo ya vijana na vijana tuko zaidi ya asilimia 60. Hivyo kwa wingi wetu, hamtutendei haki kwa Wizara hii nyeti inayotuhusu sisi vijana kututengea Shilingi

Nakala ya Mtando (Online Document)

bilioni 35.3. Wakati huo huo katika hizo fedha ukiangalia, ni Shilingi bilioni 15 tu ndiyo ambazo zinakwenda kwenye maendeleo mbalimbali. Nasi vijana kwenye maendeleo ya vijana tuko humo humo ndani ya hayo maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mfuko wa vijana, mwaka 2013 mlitutegea Shilingi bilioni sita, lakini mpaka Aprili, 2014, mmetupatia Shilingi bilioni mbili tu. Mwaka huu katika bajeti hii ya maendeleo ya vijana imepangiwa Shilingi bilioni nne tu. Sasa sijui tutakuja kupata Shilingi bilioni moja! Maana yake tulipopangiwa Shilingi bilioni sita tulipewa Shilingi bilioni mbili; sasa hatujui mwaka huu katika Shilingi bilioni nne sijui mtatupa moja, au mtatupa nusu bilioni! (Makof)

Mheshimiwa Spika, lazima Serikali iangalie umuhimu wa mfuko huu, sababu mfuko huu unatumika kukopesha vijana ambao tunasema wako zaidi ya asilimia 60 ya Watanzania. Vile vile, mfuko huu unatumika kuelimisha vijana katika masuala mbalimbali ya ujasiriamali na jinsi gani ya kuendesha biashara zao. (Makof)

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali iangalie kwa ukaribu mfuko huu wa maendeleo ya vijana, kwa sababu unalenga asilimia kubwa ya Watanzania, kwa sababu sisi vijana ni wengi Tanzania. Kwa wingi wetu basi, tunaomba mfuko huu muungalie kwa ukaribu na tupewe fedha nydingi za kutosha ili vijana tuweze kujikwamua katika matatizo ya ajira. (Makof)

Mheshimiwa Spika, napenda pia nizungumzie suala la Maafisa vijana. Kwa kweli Afisa kijana katika Wilaya ni kiungo muhimu sana kati ya vijana na Wizara. Kwa sababu Wizara inajitahidi kuanzisha programs mbalimbali za uvuvi, za kilimo, huko Wilayani, lakini sasa programs zile hazi hazifanikiwi na wala haziwezi kuendelea kwa sababu hawa Maafisa Vijana, hawapo. Ni katika Mikoa 14 tu kati ya 31 ya Tanzania ndiyo ambayo ina Maafisa Vijana. (Makof)

MBUNGE FULANI: Duh!

MHE. NEEMA M. HAMID: Mheshimiwa Spika, vilevile, katika bajeti iliyopita niliombwa Serikali iangalie suala zima la out growers katika mashamba makubwa yaliyoko Mikoani kwetu. (Makof)

Kuna mashamba makubwa, kama ya tumbaku kule Tabora; Njombe kuna chai; Kanda ya Ziwa kuna pamba; na Singida kuna alizeti. Niliiombwa Serikali ianzishe program ya out growers kwa vijana kwa sababu vijana watakuwa na uhakika wa mbegu, mbolea, lakini vilevile watakuwa na uhakika wa masoko.

Vilevile hata kama Serikali ikianza kushughulikia suala hili, pasipokuwa na Afisa Vijana wa Wilaya, ni nani atakayesimamia vijana hawa katika kuhakikisha

Nakala ya Mtando (Online Document)

kwamba programs hizi zinaendelea vizuri na zinafanikiwa kwa kiwango kikubwa?

Naiomba Serikali ihakikishe kwamba Maafisa Wilaya wa Vijana wawepo katika Wilaya zote za Mikoa ya Tanzania. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Sawa sawa!

MHE. NEEMA M. HAMID: Mheshimiwa Spika, sasa naomba pia nizungumzie suala la habari. Mheshimiwa Spika, TBC ni chombo cha Umma, ni television ya Umma. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Naam!

MHE. NEEMA M. HAMID: Watu wengi, Watanzania wanategemea kupata habari kwa kupitia chombo hiki cha TBC. Lakini inasikisha sana na inatia aibu kuona kwamba wakati mwingine habari zinakwama, wakati mwingine mtu hatokei, unaona giza tu; sauti haitokei!

Kwa hiyo, kutokana na changamoto zote hizi na wachangiaji wengi waliopita wamelizungumzia tatizo hili, mimi namwomba Mheshimiwa Waziri, aniambie, kwani fedha kiasi gani wanahitaji watengewe ili kuweza kumaliza tatizo hili? Tujue, ili waweze kupatiwa ufumbuzi wamalize tatizo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, siku moja hapa, kuna Mheshimiwa mmoja, Mheshimiwa Maryamu aliniambia, ninyi mmezidi CCM, mkimwona Mheshimiwa Tundu Lissu anaongea, mnazima mitambo. Inaleta ugomvi baina ya Chama tawala na Wapinzani.

Mheshimiwa Spika, naomba tatizo hili liishe, isionekane kama sisi tunawafanya wenzetu hiana, hapana. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, vilevile nilikuwa nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuweza kufuatilia hivi vyombo vyahabari ambavyo vinatoa habari ambazo siyo za kweli. Mheshimiwa Waziri kajitahidi kulishughulikia, kama alivyosema kwenye hotuba yake. Lakini ningependa Mheshimiwa Waziri aniambie kwamba, hii Sheria ya Vyombo vyahabari, italetwa lini hapa Bungeni ili tuweze kuweka mambo sawa kila mtu apate haki yake stahiki?

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuzungumia suala la utamaduni, lakini vilevile katika suala la utamaduni nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Michezo na Utamaduni, pamoja na Naibu wake na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kuweza kurasimisha kazi za wasanii na kuweza kuwapatia stamp. Hii inasaidia wasanii kuweza ku-control kazi zao, hivyo sasa wake promoters hawatakuwa wafaidika peke yao, wasanii nao waafaidika. (Makof)

Mheshimiwa Spika, vilevile nizidi kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kufanya kazi kwa ukaribu na kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, lakini vilevile na Wizara ya Fedha. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. (Makof)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nizungumzie suala la filamu ambazo hazina maadili. Kumekuwa na filamu ambazo hazina maadili.

Nimesikia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, anajitahidi kupambana na filamu hizo zisitoke, lakini bado Mheshimiwa Waziri una kazi kubwa sana, hakikisha kwamba hizi filamu ambazo hazina maadili zisiweze kutoka, kwani zinapotosha maadili. Utakuta wazazi wamekaa wanaangalia filamu na watoto, yanakuja kutokea mambo ya ajabu, haipendezi; siyo utamaduni wetu Watanzania. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nimalizie tena kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuhamasisha wasanii kuweza kujipatia elimu inayohusiana na masuala ya sanaa, lakini vilevile kuhamasisha katika kununua hisa. (Makof)

Mheshimiwa Spika,...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji*)

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa fursa, lakini pia nitambue mchango wa wadau wa michezo ndani ya Bunge. Namwona Mheshimiwa Comrade Kassim Majaliwa, kocha wa timu ya Bunge, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, captain wa timu ya Bunge, pia na ndugu yangu Mheshimiwa Ismail, Rais wa Simba aliyemaliza muda wake. (Makof)

Mheshimiwa Spika, naanza hoja yangu kwa kusema kwamba, kwa kuhakikisha haki inatendeka na inapatikana katika michezo mbalimbali duniani,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Chama cha Mpira wa Miguu cha Uingereza (FA), pia FIFA, wameamua kuanzisha teknolojia mpya ambayo imetoa matokeo ya kihistoria katika Barclays Premium League ya Uingereza, teknolojia ya *goldline technology*.

Sasa, na pia FIFA wana mpango wa kutumia teknolojia hiyo katika Kombe la Dunia linalokuja. Je, Serikali kupitia TFF ina mpango gani wa ku-install *goldline technology* katika uwanja wa Taifa wa Dar es Salaam ambao unatumika kwa mashindano mbalimbali ya Kimataifa. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, la pili, niliguswa na ndugu yangu Mheshimiwa Ismail Aden Rage wakati akizungumza kwamba tusimwulize Waziri juu ya swali la FIFA, kuhusu Zanzibar kujinga na FIFA, na akatuonya kwamba tusifanye hilo kwa sababu Waziri hana uwezo nalo.

Mheshimiwa Spika, mtu ambaye alikuwa hasa aambilie maneno hayo, ilikuwa ni Rais wa TFF. Nanukuu taarifa ya utekelezaji wa llani ya Uchaguzi wa Rais wa TFF, kifungu cha 9(1) kama kinavyozungumza.

Mheshimiwa Spika, Rais wa TFF anasema, mahusiano na Zanzibar; TFF na Chama cha Mpira Zanzibar (ZFA), zimekaa kuimarisha kufuatilia ziara mbalimbali walizozifanya kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Anasema timu zetu za Taifa za wakubwa, za vijana na za wanawake, zinafanya kazi kwa pamoja, juhudhi mbalimbali zinachukuliwa.

Juhudi ya kuhakikisha Zanzibar inajunga na FIFA zinaendelea kupita wahusika kwa mazungumzo na wahusika wenywewe.

Sasa Rais wa TFF ndiye anayesema kwamba juhudhi za kuhakikisha Zanzibar inajunga na FIFA zinafanya. Sasa Mheshimiwa Rage kwenye hili labda ukamwambie Rais wa TFF, asiseme maneno hayo.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu, ambalo ni muhimu ni kuhusu Baraza la Michezo la Taifa. Baraza la Michezo la Taifa limeanzishwa na Sheria ya Bunge Na. 12 ya mwaka 1997, pamoja na marekebisho yake ya Sheria Na. 6 ya mwaka 1971.

Mheshimiwa Spika, hili Baraza majukumu yake makubwa ni kuhakikisha kwamba linasimamia na linaimarisha michezo kwa kadri inavyokwenda. Lakini

Nakala ya Mtando (Online Document)

kwa bahati mbaya sana Baraza la Michezo halijasimamia mchezo wowote ambao sasa Tanzania tunajivunia.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano TOC, katika mashindano ya Olympic zaidi ya miaka 32 Tanzania haijapata medali yoyote, hata medali ile ya mtu kurusha tufe. Tunao watu wakubwa, Wasukuma tunao chungu nzima, tunashindwa kuwaandaa wakarusha tufe! Leo tuna watu wakubwa kama kina Abdallah Sharia tunawatumia kupiga vigelegele kwenye Bunge la Katiba, watu kama wale wanetusaidia sana katika kurusha tufe. (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, TBC inafanya kazi vizuri. Wakati ule wa Mkurugenzi Tido Mhando ilikuwa tunaiona TV wapi inaelekea lakini leo TV hii imekuwa ya ajabu sana. Tunahitaji TBC iwe kama CNN, Reuters, BBC, iwe na matukio, mtu unakwenda unatazama taarifa ya habari baada ya saa moja au masaa mawili lakini leo unataka kutazama habari unamkuta John Komba, number one, number one, number one nini, anakaa kwenye TV. Kwa hiyo, mambo kama haya TBC lazima mrekebishe vipindi vyenu isiwe TV ya kishamba. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda hautoshi, medali ya mwisho iliyopatikana na Tanzania katika mashindano ya Olympic imepatikana mwaka 1980...

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Margareth Mkanga atafuatiwa na Mheshimiwa Kapt. John Komba.

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii. Niunge mkono hoja lakini baada ya kuwa nimejibowi vizuri hayo mengine yote ambayo nitayazungumzia. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kuwapongeza walioko mbele ya Wizara hii, Waziri na wenzake wote kwa kazi nzuri wanayojitahidi kuifanya pamoja na kwamba fedha kama bajeti ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, nashukuru katika hotuba yao nimeona kwamba wanamichezo wenyewe ulemavu kuitia Paralympic, ni moja ya timu ambazo zinaandaliwa na Wizara hii huko nje kusudi wakashiriki vizuri kabisa, kama ilivyo desturi yao kwenye michezo ijayo ya Jumuia ya Madola itakayofanyika mwezi wa sita huko Scotland. (Makofij) -

Mheshimiwa Spika, lakini nataka kufahamu, katika timu sita ambazo Serikali ikishirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje zimepeleka timu hizo kwenda

Nakala ya Mtando (Online Document)

kujifunza au kuweka kambi zao nje ya nchi, je, katika timu hizo sita timu za watu wenyewe ulemavu kupitia *Paralympic* nazo ziko huko au wao wameachwa hapa nchini waweze kujipigapiga tu wenye? (Makof)

Mheshimiwa Spika, la pili, pamoja na kwamba watu wenyewe ulemavu wanamichezo huwa wanajitahidi kila wanaposhiriki michezo kimataifa, ndiyo timu pekee zinazoleta medali za dhahabu, fedha na shaba, tofauti hata na timu za watu wazima ambao si wenyewe ulemavu. Hata hivyo, katika maandalizi timu hizi zimekuwa na matatizo kwa muda mrefu. Moja, hakuna vifaa, pili, jinsi ya kufika kwenye mazoezi matatizo, jinsi ya kupata lishe sahihi ya wanamichezo, maana si kula tu, wanamichezo wanapaswa kulishwa sawasawa ili wakaweze ku-perform huko mbele ya safari, inakuwa ni matatizo, wanajitegemea wenye? Mimi chama nachokifahamu kinawashughulikia watu hawa ni hicho cha *Paralympic* kilichoanzishwa na mlemavu mwenzao, mnafikiri pesa na huduma zinatoka wapi? Serikali haijiingizi sana kuwaandaa hawa lakini ndio wanaojitahidi kuitoa aibu nchi yetu, kuleta medali. Shukrani ya Serikali hapo iko wapi? Mimi leo nataka nifahamishwe, hivi hawa wanasaidiwa na wanaenziwa vipi na wanalelewa vipi ili waendelee kujitolea? (Makof)

Mheshimiwa Spika, nikiishia hilo napenda kuongelea suala la vyombo vya habari na umuhimu wa kuwa na wakalimani wa lugha ya alama. Niishukuru Serikali wakati wa Bunge Maalum hapa TBC ililetu watu hao. Jambo hili ni la msingi sana kwa sababu wenzetu walemavu viziwi bila tafsiri ya wakalimani wa lugha ya alama hawaelewi kitu, wanaangalia vitu kwenye viio humu kama mchezo tu hivyo hivyo. Naiomba Serikali, hili suala lichukuliwe kwa umuhimu wake kabisa kwamba si katika Bunge Maalum tu, hata na Sheria hiyo ya Vyombo vya Habari ambayo mnasema mnaileta hiyo. Mimi naomba kabisa pawe na msisitizo, TV stations zote lazima ziwaajiri wakalimani wa lugha ya alama kuwasaidia wenzetu viziwi kuweza kuelewa nini kinafanyika. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kuna Mfuko hapa wa Maendeleo ya Vijana, nafurahi Serikali imesema imetoa mwongozo wa jinsi ya kuendesha Mfuko huu kupitia SACCOs. Sijui kumewekwa nini kuhakikisha vijana wenyewe ulemavu, Maafisa Vijana wa Wilaya na Mikoa, ambao nimesikia kumbe hata hawapo sasa sijui itakuwaje huko; wameelekezwa vipi kuhakikisha katika uhamasishaji na vijana wenyewe ulemavu wanajunga kwenye SACCOs hizi ili na wao waweze kufaidika, vinginevyo wanabaki nyuma na wao ndio masikini zaidi ya masikini kuliko hata vijana wenzao ambao hawana ulemavu wa namna yoyote. Watu hawa watasaidiwa katika Mfuko huo? (Makof)

Mheshimiwa Spika, kuhusu vazi la taifa. Ni miaka mingi tangu nimekuweko hapa nasikia kuhusu vazi hili, mashindano yalikuwepo, hivi vazi hili linapatikana lini? Hilo ambalo litatusaidia kujipambanua sisi na mataifa mengine licha ya

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kiswahili kama mchangiaji mmoja alivyozungumza hapa. Mimi nashauri, ili kuweza kujipambanua na wenzetu wa nchi nyingine tuvae basi scarf za taifa kwenye shingo zetu ili angalau tueleweke kwamba hawa ni Watanzania, kwani hilo nalo ni baya? Maana naona tunachelewachelewa, basi tuanze na kitu rahisi kwanza, kwamba tunafanyaje kabla hatujafikia hilo vazi rasmi ambalo tunalitaka na Kiswahili cheti tukakikoleza hapo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nisingependa kugongewa kengele lakini naomba sana SACCOs zitakazotokana na Mfuko wa Maendeleo, vijana wenyе ulemavu wawemo humo. Hawa wanamichezo wenyе ulemavu ambaо wanahenya kwa nguvu zao wakirudi hapa nyumba, mimi sijaona hata wakipongezwa, sijaona hata wakiletwa hapa kwamba hawa wamepata vikombe, mbona wengine wanapongezwa? Jamani wakati umefika wa kuhudumia kikundi hiki kwa sababu kinatutoa kimasomaso katika michezo mingi ambayo wanashiriki. Nashukuru sana, nadhani wakati wa majibu nitaelezwa kwamba kuna mikakati gani vinginevyo hapa tusiulizane mambo ya kutoa shilingi. Ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante lakini ya kutuambia tuvae kama Nchomba hatukubali. (Kicheko/Makofi)

Sasa nimuite Mheshimiwa Kapteni Komba.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi lakini nianze na kuwapa pole sana Waziri wangu na Naibu Waziri kwa matusi mliyoyapata kutoka kwa jamaa hawa. Ni kawaida yao kila siku kuwaandama watu bila makosa, badala ya kuweka point hadharani, kutoa hoja unaandama watu binafsi. Mheshimiwa Waziri unafaa, unafaa, unafaa. Naibu wako Nkamia unafaa, unafaa, unafaa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, rafiki yangu Mheshimiwa Juma Ngwali pale anasema kila akifungua TBC anakuta sijui CCM nambari one, ndiyo inayowatoeni kila siku hiyo. Ukisikia nambari one ndiyo inayokutoa kila siku, out, out, kwa sababu nambari one ndiyo kila kitu. Kwa hiyo, isikuume sana maana itabidi uvumilie tu. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo Mheshimiwa Juma Ngwali amelisema hapa kwamba Zanzibar ikubaliwe kuwa mwanachama wa FIFA, hebu jifunzeni kutoka TOC, TOC wameungana Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara wameungana, iko moja. Kwa hiyo, kwa kweli ushauri alioutoa Mheshimiwa Rage ndio ushauri wa msingi huo, hamtapata peke yenu. Kwa hiyo, ZDFA na TFF wakiungana pamoja ndipo Zanzibar itakuwa mle ndani inawakilishwa kama

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Tanzania, si kama Zanzibar, hakuna Zanzibar hapa, nchi ni moja na Serikali ni mbili.

Mheshimiwa Spika, tatizo letu kubwa hasa mimi kule nakotoka ni *TBC* na *TBC* hata kama nikii laumu sana kwa mwendo wa Serikali inavyofanya sasa hivi haiwezi kuwa effective. Kwa sababu, hebu fikiria, mwaka jana walipewa shilingi bilioni sita lakini fedha iliyotoka ni shilingi bilioni moja na milioni mia saba. Hiyo ni hela kidogo sana, hata wangejitätahidi vipi, hata wangejitätahidi vipi, *TBC* haiwezi kuwa effective. Serikali naomba, tena Waziri Mwigulu yuko hapa, jitahidi sana mwezi huu mmoja bilioni zile zilizobaki wapewe ili *TBC* ifike Unyiramba kule, ifike Nyasa, ifike maeneo mengine yote. Naomba sana isaidieni *TBC*, imebaki peke yake. Vituo vingine vyote vinaamua kutanga nchi vikipenda lakini *TBC* inalazimika kutangaza nchi yetu, kutangaza sera za nchi yetu, kuwatangazia Watanzania lakini vituo vingine vyote wanatangaza wanapopenda. Wikipenda kutuchafua wanatuchafua, wikipenda kututukana wanatutukana lakini *TBC* iko pale kusafisha nchi yetu iwe safi, wapeni haki yao *TBC*. -(Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi hapa mnaponiona nazungumza sasa hivi wale watu wangu hawawezi kuniona. Hawanioni kabisa yaani kule wanamuona yule mama aliyeshindwa juzi, ndio wanayemuona kila siku na aliyeshinda jana wanamuona kila siku lakini mimi Mbunge wao hawanioni. Hata nilivyosoma taarifa pale hawana habari.

MBUNGE FULANI: Pole sana.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Sasa hii inasaidia nini, isaidieni *TBC* ili mimi nikaonekana kwetu. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Pole sana, pole ndugu yangu.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Spika, kwa sababu mengi nimeyazungumza kwenye taarifa yangu ile ya Kamati, nafikiri haya niliyoyasema yawe nyongeza ya yale ambayo nimezungumza. Ahsante sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Tukirudi naomba hawa nitakaowataja wawayi yuko Mheshimiwa Martha Mlata na Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar. Ajabu yenyewe ya Wizara hii sijui akina mama kwa nini wamekuwa wengi, sijajua ni siri gani. Kwa hiyo, naomba muwahi.

Nina tangazo kidogo, nadhani hata wenyewe ninaowatangazia siwaoni. Tumeamua kwamba Kamati ya Uongozi kwa maana ya Wenyeviti wa Kamati

Nakala ya Mtando (Online Document)

za Kudumu tukutane baada ya saa mbili usiku, tukahirisha hapa, tutakuwa na kikao cha muda mfupi kuweka mambo vizuri.

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi.

(Saa 6.53 mchana Bunge *lilisitishwa*
mpaka Saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge *lilirudia*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Mheshimiwa Martha Mlata atafuatiwa na Mheshimiwa Faida Bakar.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi lakini pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatakie kheri wazazi wangu ambapo wote wanaumwa na wamelazwa. Naomba Mwenyezi Mungu awape uponyaji pale walipo. Pia nimkumbuke na kumweka mikononi mwa Mungu mma yake Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto ambaye naye hali yake siyo nzuri. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, baada ya sala hizo, naomba niipongeze Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya na kubwa lakini ni ngumu sana kwa sababu bajeti wanayotengewa, ni kweli kuna majukumu mengi lakini fedha wanazopewa Wizara hii, zimekuwa ni kidogo sana. Labda tu niseme sitasema mengi, nitasubiri kwenye bajeti kuu, tunaweza tukaelewa ni sababu zipi, Wizara hii inakuwa ikipewa fedha kidogo na wakati majukumu yake ni mengi sana. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri wanayoifanya, nimpongeze pia Mheshimiwa Nkamia kwa kuteuliwa na nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuliona hilo, kuwa Naibu Waziri katika Wizara hii. Pamoja na madongo yote ambayo amekuwa akishushiwa hasa leo, nakutuhumiwa lakini ni Mtanzania wa kwanza na ni Mwfrika wa kwanza kutangaza Ligi Kuu ya Uingereza na fainali kwa lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, mimi nampongeza sana. Hata Ndugu Tido Mhando kama yupo anaweza akawa ni shahidi kwa sababu ndiye aliyekuwa bosi wake. Pia ni Mtanzania ambaye amewahi kufanya kazi Voice of America akitangaza kwa Kiswahili. Kwa hiyo, mimi nampongeza sana, madongo hayo Mheshimiwa Nkamia usiyasikilize. (Makofii)

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimuulize Mheshimiwa Waziri kuhusu TFF, kumekuwa na sintofahamu, hivi kulikuwa na tatizo gani linalopelekea jina la *Taifa Star* kwamba linafanyiwa mchakato eti libadilishwe kwani kuna tatizo gani? Kingine hata zile sare kwa maana ya jezi za *Taifa Star* ambazo zimezoleka, ni utambulisho wetu lakini naona zinabadilishwa yaani imeletwa rangi fulanifulani hivi ya ajabuajabu ambayo haieleweki, kulikuwa na tatizo gani? Hivi tatizo ni kubadilisha jina *Taifa Stars* na jezi au tatizo ni kukaa na kuangalia namna gani ya kuweza kupandisha kiwango cha timu ile kufikia kiwango cha mataifa?

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri zoezi lile lisimamishwe, waangalie ni namna gani watapandisha viwango vya timu ile na siyo jezi. Halafu jina la *Taifa Starts*, jina lililoananzisha na Waasisi wetu unabadiishi nini? Kama tutaingia huko basi itafikia wakati ataingia Rais mwingine hapa atasema jina la Tanzania halifai ngoja tubadilishe, tuache kubadilishabadiishi majina. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nirudi kwenye upande wa fani yangu. Mimi naomba ni-declare *interest* kwamba mimi pia ni msanii wa Muziki wa Injili, kwa hiyo ni mdau katika tasnia hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikizungumza sana kuhusu suala la sanaa na mambo yake mengi lakini kuna mambo ambayo mimi yananitatiza kidogo naomba Mheshimiwa Waziri uyachukue. Nitakuja kuomba pia niwe na Maeleo Binafsi, labda nikitoa yale Maeleo Binafsi, yanaweza yakaisaidia Wizara hii kuona ni namna gani inaweza ika-deal na fani hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza Sera yenyewe ya Sanaa. Ukirudi kwenye upande wa Sera, sisi tulitafuta mtaalam akatusaidia ni namna gani Sera ya Sanaa iwe hasa katika upande wa filamu lakini Wizarani wakasema watachukua mambo mawili, matatu. Ukirudi TRA, zile sticker za kutoza ushuru, wao wanatoza ushuru kwenye Makampuni ya kibiashara lakini kazi zetu hazijatambuliwa kisheria na bado tunalipa ushuru. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini nataka kuomba pia, pamoja na kwamba kweli TBC hawapati fedha kutoka Serikalini lakini wanakusanya fedha kutoka kwa wafanyabiashara mbalimbali kwenye matangazo na wanapotumia kazi zetu. Naiomba TCRA ambao wao naamini wako makini na wamekuwa very smart katika utendaji wao wa kazi wasimamie suala hili kwa sababu wao ndio wanawapa leseni vyombo vya utangazaji, televisheni zote pamoja na redio ili waweze kulipa mirabaha ambayo wanatakiwa wailipe.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kuhusu vazi la Taifa. Hapa unaponiona bado naweza nikawa nimekamilika pamoja na kwamba unasema ni bendera ya Taifa. Ghana, bendera yao ya Taifa kwenye vitenge tunavivaa mpaka hapa. Kwa hiiyo, naomba sana lisimamiwe na Asia ambaye amenipendezesha leo, abuni zaidi ya hapa ili tunapotoka, tuweze kuwa na utambulisho wetu wa Taifa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, vijana sasa hivi, kama alivyo kama yangu Mwigulu Nchemba, kule vijiji wote wameamua kuva scarf ambazo wanao ndiyo utambulisho wao. Kwa hiyo, kweli Watanzania wana kila sababu ya kutafuta utambulisha wao. Hapa tunavivaa vitenge vyta Ghana ambavyo vina bendera ya Ghana, kwa nini tusiwe na vitenge vyetu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Kwanza, naomba Mheshimiwa Mwigulu Nchemba uondoe hiyo scarf. (Makofii)

MBUNGE FULANI: Tena!

*(Hapa Mheshimiwa Mwigulu
N. Madelu aliondoa scarf aliyokuwa amevaa)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mohammed Bakar.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpa pole Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto kwa kukuuguliwa na mama yake mpenzi na Mwenyezi Mungu amjalie aweze kupona haraka sana, *Inshallah*. Pole sana Mheshimiwa Zitto, tuko pamoja. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, napenda sana kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo inaifanya, hata kama bajeti yao ni ndogo lakini Mawaziri hawa wanajitahidi. Mheshimiwa Waziri Fenella hongera, Mheshimiwa Naibu Waziri Juma Nkamia, hongera, wala msitetereke na msibabaishwe na maneno ya Wapinzani, ya kukaa hapa katika Bunge hili na kusema hamfai, mnafaa, mnatosha ndiyo maana Mheshimiwa Rais akawateua. (Makofii)

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, napenda sana kuwashukuru Wanahabari wote wa Tanzania kwa jitihada zao kubwa, wanafanya kazi usiku na mchana, hawachoki. Pamoja na kwamba hawana vifaa ama nyenzo nzuri za kufanya kazi lakini Waandishi wa Habari wa Tanzania wengi wao ni wazalendo na wanafanya kazi vizuri, hongereni sana Waandishi wa Habari. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria wa Kusimamia Vyombo vya Habari. Kama tunavyojuu bila ya sheria kitu chochote hakiwezi kwenda. Tunaweza tukakaa hapa tukawalaumu Waandishi wa Habari kama wanaandika vibaya, wanaongea vibaya lakini kwa vile hawana sheria yao ambayo inawasimamia, ambayo inatetea haki zao hapa tutakuwa tunawalaumu bure. Mheshimiwa Waziri, huu si mwaka wa kwanza, wa pili au wa tatu, ni miaka karibu saba sasa hivi kila siku mnasema mtaleta Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari lakini hadi tarehe ya leo hamjauleta. Naomba kuuliza Serikali italeta lini Muswada huu wa Sheria ili tuupitie hapa na tuwawekee Waandishi wa Habari sheria zao waweze kujitawala.

Mheshimiwa Spika, bila kupata hii sheria, Waandishi wa Habari wanabughudhiwa sana. Wanakosa sana haki zao msingi kama vile bima ya maisha yao, bima za ajali, mishahara na posho zao ni duni, kwa sababu ndani ya sheria hiyo yatakuwemo mambo yote yanayowahusu Waandishi wa Habari na ambayo yatawaendeleza katika kazi zao za uandishi wa habari, lakini bila sheria haiwezekani. Naiomba Serikali, Bunge hili likiisha, tunaomba Muswada huu uletwe hapa Bungeni tuweze kuupitisha ili Waandishi wa Habari wawe huru katika kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, hujuma dhidi ya Waandishi wa Habari. Wandishi wa Habari wengi sana, hata kama siyo wengi sana lakini baadhi yao wanahujumiwa kutokana na kutenda haki katika kazi zao. Pengine kigogo fulani huko au mtu yeyote, sio lazima kigogo, akiona kama Mwandishi wa Habari kaandika kitu kinachomhusu ambacho pengine ni kweli, kimefanyiwa utafiti, kakifanya kweli lakini Mwandishi wa Habari akikiandika hicho basi ni lawama, Waandishi hao watabughudhiwa, wengine watafanyiwa hujuma ya kuuliwa, wengine wanapata vilema vya maisha na tunajua. Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali na wananchi waelewe kwamba Waandishi wa Habari ni watu muhimu sana katika kuelimisha jamii, tuwaheshimu. Kwa upande mwingine na wao pia, kwa wale ambao hawaifiati maadili baadhi yao, wale tunaowaita Makanjanja wanaharibu fani hii muhimu sana. Kwa hiyo, wasiwe na wao wanajiandikia mambo ambayo hawayajafanya utafiti, nasema ni baadhi yao.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari vya Tanzania na maadili yake. Vyombo vya habari kama magazeti, majarida mbalimbali na kadhalika na

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Iakini kuna vyombo vingine kama TBC vimekuwa na maadili mazuri sana, yanaelimisha jamii iakini kuna vyombo vya habari vingine jamani tunaomba sana mchukue juhudhi Serikali kuvionya vyombo vingine, ama magezeti mengine kuandika mambo ambayo siyo. TBC tuipe nguvu, tuisaidie, ni shirika la Serikali ya Tanzania hii lazima lifike hadi vijijini. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, sanaa na uchoraji. Tunakuwa na michezo mbalimbali iakini sanaa tunaidharau na tunaona kama sanaa si kazi, ama sanaa siyo ajira iakini sanaa za uchoraji ni ajira, ni kazi ambayo vijana wanafanya na kujipatia maslahi yoo. Kuna kikundi fulani nimeonana nacho hapo nje, wamechora sura zetu hata Wabunge, ukienda Mheshimiwa Spika hata na wewe pengine wamekuchora, ni wewe mwenyewe jinsi ulivyo, wanauza Sh.150,000/= kwa kila picha moja. Wale vijana wana vipaji vizuri, wanajihusisha na sanaa za uchoraji iakini watu wengine wanadharau kwamba sanaa za uchoraji siyo sanaa. Naiomba Serikali iwasaidie vijana hawa, wanatoka kikundi cha *Wisdom Eyes* ya Arusha. Naomba Serikali mkitoka muwaone hapo nje. Mheshimiwa Dkt. Fenella wamekuchora wewe kama ulivyo na nywele zako hizo, umependeza kama nini. Kwa hiyo, hawa vijana wana vipaji, tuwaenzi na tuwasaidie kuwapa mikopo na misaada mbalimbali. Vijana wale mmoja anaitwa Erick na mwingine anaitwa Gerald na hawa wamemaliza Chuo Kikuu, mmoja kasomea sheria na mwingine amemaliza UDOM. Kwa hiyo, ni vijana wasomi tu iakini wamejunga katika sanaa zao za uchoraji kwa sababu wanaendesha maisha yao kwa njia hiyo na wanajilipia pango la shule kutokana na sanaa. Kwa hiyo, tuwasaidie vijana hawa na wengine kama hawa ambao wako wengi hapa Tanzanznia.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (Makofii)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. KASSIM M. MAJALIWA: Mheshimiwa Spika, nasikitika kukujulisha kuwa Mikoa ya Lindi na Mtwara hasa Wilaya za Ruangwa, Liwale, Nachingwea, Nanyumbu, Masasi na kadhalika hazipati matangazo ya TBC Radio. Tunaomba kujua tatizo hili litatatuliwa lini maana wananchi wanakosa fursa ya kupata taarifa za Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili ni la muda mrefu na hakuna ufumbuzi. Nitafurahi kama wananchi watapata majibu ya ufumbuzi wa lini matangazo hayo yataanza.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

Nakala ya Mtando (Online Document)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba/bajeti ya Wizara hii hasa kwa kuzungumzia suala zima la wajibu wa vyombo vya umma kuihabarisha jamii juu ya yote yanayoendelea ndani ya chombo muhimu cha kutunga sheria (mhimili wa Bunge). Mara kadhaa nimekuwa nikizungumzia juu ya mwenendo wa vyombo vya umma vya TBC TV na TBC radio. Ni wazi wakati wa Bunge TBC TV hutangaza vipindi vyote vya Bunge tangu asubuhi hadi usiku, hii inatoa fursa kwa Watanzania wachache sana wanaomiliki TV na ambao wanakuwa muda wote kwenye TV (runinga) kupata habari za Bunge lakini hii ni kinyume kabisa na TBC radio ambayo imekuwa ikirusha matangazo ya Bunge wakati wa kipindi cha maswali tu na baada ya hapo hukata matangazo na kuweka vipindi vingine. Nimeshauzila juu ya suala hili zaidi ya mara tatu hadi sasa Serikali inasema inashughulikia.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kuwa Watanzania zaidi ya asilimia 70 ni maskini wasiokuwa na uwezo wa kumiliki TV lakini pia kada ya Watanzania wanaofanya kazi hawana fursa ya kuangalia TV, hata wafanyabiashara hawana fursa ya kuona TV, kuna asilimia yao vilevile ni wakulima, ukizingatia ukuwaji wa teknolojia ambapo mawasiliano ya radio hupatikana hata kwenye simu za viganjani, kuna radio ndogo kama simu ambazo Watanzania wangeweza kupata fursa hii ya kufuatilia Bunge ili kujua mambo mbalimbali yanayozungumzwa ndani ya Bunge. Ikumbukwe ni asilimia ndogo sana ya nchi yetu ndio wana nishati ya umeme na hivyo kwao ni ndoto kumiliki TV. Hii kwangu naona kama vile ni njama ya kuendelea kuwaficha Watanzania juu ya nini wawakilishi wao wanachokisema Bungeni. Hivyo basi, nataka kujua ni kwa nini Serikali imeshindwa kabisa kuhakikisha TBC radio inarusha matangazo yake muda wote hasa wakati wa bajeti na vikao vingine pia. Nataka kujua ni lini TBC radio itarusha matangazo ya Bunge lote likiwa hewani kwa kuzingatia mahitaji na miundombinu ya mawasiliano ni duni. Napenda kujua juu ya hili leo maana zimekuwa ni porojo tu.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni juu ya fedha zinazotolewa na FIFA kila mwaka kwa ajili ya kuendeleza michezo Tanzania, mfano mwaka jana ilitoa dola laki tano kwa ajili ya kuweka nyasi bandia. Sasa nimejua pia kuna fedha zimekuja kwa ajili ya kukarabati viwanja ila nasikia zinapelekwa Bukoba (Kantaba). Nahitaji kujua ni vigezo vipi vinatumika ku-allocate fedha hizo. Mfano sisi Musoma (Mara) tuna viwanja duni sana, ni lini sasa tutapata fungu la FIFA kwa ajili ya kukarabati uwanja wa Musoma? Vilevile kwa nini gawio hilo la FIFA kwa ajili ya mafunzo kwa Makamisaa hazipelekwi Mikoani maana katika ngazi ya Mkoa/Wilaya hazitufikii. Naomba kupata majibu ya ufasaha katika haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, gazeti la Tanzania Daima mara nyingi linaandika habari za kuleta uchochezi. Naomba liangaliwe kwa jicho makini.

Mheshimiwa Spika, michezo nchini inaweza kuwa mizuri kwa kuhakikisha kila shule ya msingi ina timu za kila aina, sio lazima watumie muda mwingi lakini itakuwa namna ya kugundua vipaji. Maafisa Utamaduni wa Wilaya wanaweza kutumia wazazi, wafanyabiashara walioko Wilayani kudhamini michezo hii kwa kununua hata jezi tu.

Mheshimiwa Spika, vyuo vikuu nchini vinaweza pia kuwa na timu nzuri za michezo hasa football. Mchezaji mwenye elimu atacheza vizuri kuliko asiyekuwa nayo. Nidhamu ya kukaa kambini, kupata *technics* za mchezo, mwanafunzi aliyeleo chuoni atafanya better. Hivyo Serikali ihamasishe vyuo vianzishe timu za mpira wa miguu.

Mheshimiwa Spika, private sector inaweza sana kudhamini na kuunda timu zao na zikafanya vizuri mfano ni Azam FC. Vilabu vilivyoko nchi zilizoendelea vimenunuliwa na kutunzwa na private sector. Hata hivyo, vinaleta mapato mazuri as long as management inakuwa nzuri na si mfano wa Yanga na Simba. Wazalendo kama mfanyabiashara aliyetunza na kuiweka timu ya watoto wa mtaani walioshinda kombe la dunia inatakiwa Serikali iwa-support na kuhamasisha wengine wafanye kama wao.

Mheshimiwa Spika, Serikali za Mikoa zitafute namna ya kuendeleza na kutengeneza kiwanja kimoja katika Mkoa ili ku-encourage mashindano ya michezo katika kila Mkoa. Wakuu wa Mikoa wanaweza kuhakikisha hili linafanyika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri kwa kusoma hotuba vizuri.

Mheshimiwa Spika, matangazo ya redio Tanzania kutofika kule Kusini Lindi, tunaomba Serikali itusaidie ili tusikie matangazo yote ya redio Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Lindi unapenda sana michezo. Kwa miaka ya nyuma wana Lindi waliweza kucheza timu mbalimbali kama Kombe la Gossage, Sunlight, Yanga, Simba, Majimaji, wachezaji wengi walikuwa wanatoka Lindi. Nachotaka kusema ni kwamba, Serikali ifanye jitihada za

Nakala ya Mtando (Online Document)

makusudi kabisa ili kuwaenzi wana michezo hao na kujenga uwanja wa Lindi (Ilulu Stadium).

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kuwa kabla ya kupata Uhuru, Tanzania kulikuwa na viwanja vitatu tu ambavyo Tanganyika wakati huo wakichezea mpira katika Afrika Mashariki ambavyo ni Tanga –Mkwakwani, Dar es Salaam - Karume na Lindi Stadium kilijengwa mwaka 1957. Viwanja hivi tunaiomba Serikali ivikarabati hasa uwanja wa Stadium Lindi ulijengwa mwaka 1957 na Sir Edward Twinning, ulikuwa na taa, mpira wa Afrika Mashariki wakicheza usiku. Tunaiomba Serikali watusaidie Lindi kujenga uwanja wa Lindi ambao sasa unaitwa Ilulu Stadium.

Mheshimiwa Spika, kuendeleza vipaji vya watoto mapema wakiwa bado shulenii. Nashauri vipaji vya watoto viendelezwe wakati wakiwa shulenii, vipaji vya sanaa, michezo mbalimbali ya mpira, *netball*, *football*, *uchoraji* na *uimbaji*.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kuweza kutimiza na kutekeleza Sheria No.7 ya 1999 ya urekebishaji wa Sheria ya Hatimiliiki ili kukabiliana na tatizo la uharamia wa kazi za usanii. Wameweza kutambua kazi za wasanii kwa kuweka stamp; zamani kazi za wasanii karibu asilimia 87.50% zilikuwa hazilipwi, zikilipwa 12.50%, kwa hiyo, hongera kwa kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyowekwa kwa kitengo cha TBC ni ndogo sana ndio maana hawamalizi kujenga jengo lao wala kutengeneza miundombini na ndio maana redio hazisikiki katika Mikoa ya pembezoni. Tunaomba Wizara hii waongezewe pesa, ni shilingi bilioni 30 tu hazitatosha kwa mambo mengi. Tunaomba wapewe fedha ili waweze kulimalizia jengo la TBC ambalo ni la muda mrefu.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, Naibu Waziri Mheshimiwa Juma Nkamia, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanazozifanya katika ujenzi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, ajira kwa vijana bado ni changamoto kubwa kwa Serikali, mikakati inayowekwa haitekelezwi, programme zinazoandalisha kwa ajili ya kuwainua vijana kiuchumi zimebaki kwenye makabati maofisini. Sheria inazitaka Halmashauri kutenga 5% ya mapato yao kwa ajili ya kuwakopesha vijana, Wakurugenzi wa Halmashauri hawatekelezi sheria hiyo na hawachukuliwi hatua yoyote. Aidha, vijana wanaokopeshwa hawapewi elimu ya ujasiriamali kabla ya kukopeshwa matokeo yake fedha hizo hupotea. Kama hatuwezi kusimamia sheria tulizojiwekea, hatutaweza kutatua matatizo yanayotukabili.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, wananchi waishio vijijiini hutegemea sana redio Tanzania kupata habari mbalimbali. Cha ajabu ni kwamba pamoja na redio hii kuwa kongwe kuliko redio zote nchini haisikiki maeneo mengine ya nchi yetu. Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, Serikali inaua vyombo vyake vya habari kwa makusudi kwa mfano, TBC 1 inadai taasisi mbalimbali kiasi kikubwa cha fedha kwa kurusha matangazo yake. Ifike wakati TBC iache kabisa kurusha matangazo ya taasisi za Serikali zisizolipa madeni.

Mheshimiwa Spika, Serikali inathamini sana TFF kuliko CHANETA. Hii inadhihirika katika kipindi cha mashindano ya michezo hiyo, CHANETA hawana wadhamini kama TFF, je, Serikali imeshindwa kuwatafutia wadhamini wa kueleweka kwa mashindano ya mpira wa peta kwa wanawake? Naomba maelezo ya Waziri katika hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kusitiza kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara hii wapewe zote kwani bajeti yao ina kiasi kidogo sana cha fedha.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja *but with few observations below*.

Mheshimiwa Spika, ajira kwa vijana, vijana ndio Taifa na nguvu kazi ya Taifa la leo lakini vijana wengi hawana ajira na kusababisha kujikita kwenye michezo michafu, kuwa na chuki kwa Serikali iliyopo madarakani na kadhalika. Hata kazi za kujajiri hakuna. Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha vijana hawa? Tumekuwa tukilisikia fungu/mfuko wa vijana kwa maneno lakini *implementation* yake imekuwa ikisuasua.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Habari, hili limekuwa ni jambo muhimu lakini limechukua muda mrefu sana, tatizo ni nini? Tukumbuke kuwa media ndio mhimili wa nne wa nchi ambao si rasmi hivyo katika kuelimisha, kuhabarisha na kuburudisha ni muhimu sana hili likazingatiwa na kufanyiwa kazi. However, ethics za uandishi zinapaswa sana kufuatwa na hatua kali za kivitendo zichukuliwe pasipo kuona haya kwa wale wote wasiofuata maadili ya uandishi na kutumika ovyo hususan na wanasiasa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Magazeti ya 1976 iliyopitwa na wakati lini itakuwa *reviewed*? Tukumbuke pia kuwa sasa hivi kuna *online news*, hivyo kufungia magazeti ambayo bado yataendelea kutoa habari zake *online*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

hakuna tija yoyote? Waandishi wa Habari wengi hawana mikataba ya kazi, mishahara mibovu kulikoni?

Mheshimiwa Spika, vazi la Taifa ni kielelezo muhimu na kamili katika kuenzi na kuthamini utaifa. Nampongeza Mheshimiwa Waziri/Serikali kwa kuunda Kamati ya Mchakato wa kutafuta vazi la Taifa. Napenda kujua mchakato umefikia wapi? *Innovations mojawapo hii imefikiwa wapi?*

Mheshimiwa Spika, diplomasia ya michezo, niipongeze Serikali kwa hatua nzuri ambayo inafanya katika diplomasia hii ya michezo, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni! Tumeona mafanikio mbalimbali katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, TBC ni chombo kinachopaswa kuwa cha umma lakini utendaji wake wa kazi hususani kwenye TV upo questionable. Nashauri sana wafuate/waangalie competences zaidi wasi-personalise. Naamini katika hili naeleweka without exploring much.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Spika, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) liliundwa na Bunge la Tanzania kwa Sheria Na. 12 ya mwaka 1967 na marekebisho yake Na. 6 ya mwaka 1971. Hali ya michezo imebadilika lakini sheria hii inakinzana na Sheria za Kimataifa. Naomba Waziri atakapokuwa anajibu hoja mbalimbali aeleze ni lini Wizara italeta sheria mpya ya BMT ili iendane na hali halisi?

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itachukua jukumu la kusaidia timu ya Taifa Stars kwani kazi hiyo sio ya TFF peke yake.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri na uvumilivu wa mazingira duni ya kazi kutokana na ufinyu wa bajeti. Kwa zaidi ya miaka mitatu, usikivu wa TBC 1 na TBC 2 ni wa shida kupita kiasi. Wananchi wa Kilwa wanasumbuka kupata matangazo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iruhusu TBC kutumia rasilimali zake ikiwemo ardhi na majengo katika kuwekeza na kuboresha miundombinu yake badala ya kutegemea bajeti ambayo haitoshelezi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itumie rasilimali zake kuwekeza katika michezo badala ya kusubiri matunda ya miti wasiyopanda.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Spika, naanza kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wa Wizara kwa kutekeleza kazi zao katika hali ngumu ya kifedha inayotokana na bajeti finyu inayopewa Wizara hii. Kwa kweli kupangiwa kiasi cha shilingi 20.3 bilioni ni sawa na kuiua Wizara hii. Hata hivyo, naomba kuchangia katika maeneo yafutayo:-

Mheshimiwa Spika, michezo ya riadha, ni kitu gani kimetokea hapa Tanzania kilichoua ari ya wakimbajji? Ni Serikali, waendesha michezo (sport administrator) au kukosekana kwa vituo vijana wetu wasikimbie? Wako wapi warithi wa kina Bayi, Juma Ikangaa, Shahanga, Nyambui na kadhalika? Inakuwaje Wizara inashughulikia sana mpira wa miguu ambao haujawahi kushinda popote badala ya riadha?

Mheshimiwa Spika, uhuru wa magazeti, mimi ni kati ya wale watu wanaopenda sheria ifuatwe kama ilivyokusudiwa. Pamoja na kutokubaliana na kashfa magazetini lakini vilevile naamini kwamba kama kuna shutuma inabidi ifanyiwe uchunguzi wa kina na hatimaye mwenye makosa kuadhibiwa. Hata hivyo, inakuwaje Serikali imekuwa ikifungia magazeti bila kufanya utafiti wa kina kwa malalamiko dhidi ya magazeti husika?

Mheshimiwa Spika, mchango wa mwenge, kama nilielewa vizuri majibu ya Serikali juu ya swali kuhusu uhiari wa michango ya mwenge lililoulizwa Bungeni, mchango huu ni wa hiari jambo ambalo mimi nakubali. Sasa inakuwaje Wakurugenzi wa Halmashauri wanaagiza Walimu Wakuu wa Shule za Msingi wachangie kwa lazima? Mfano wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mbulu amewaita Walimu Wakuu wa Shule za Msingi kwamba wawaeze Walimu wao kwamba mchango ni lazima. Naomba Serikali iwaeze Wakurugenzi hao kwamba michango ni ya hiari, hii itaongeza ari ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia pamoja na wenzangu kutoa salam za pongezi kwa kaka yetu Bwana Nderumaki. Ni hakika kazi nzuri aliyofanya akikaimu Ukurugenzi Mkuu ataendelea nayo na kuboresha zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu, Tasnia ya Filamu imekuwa kwenye majonzi makubwa hasa kutokana na kukosekana kwa mwongozo wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, kwanza niwape pole kwa misiba inayotokea, hii yote ni kazi ya Mungu. Ninachowaomba, muwe wenye imani kubwa mbele ya Mungu kwa maana mbele yao, nyuma yetu. Poleni sana.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Serikali kwa kuja na utaratibu wa kuweka stamp za TRA katika kazi za wasanii, lakini bado ulinzi ni mdogo sana, kazi zimeendelea kuuzwa bila ya utaratibu na pia wasanii wenyewe kutopata faida ya kazi zao, upande mmoja na Serikali kukosa mapato.

Mheshimiwa Spika, mamilioni ya JK na maendeleo ya Vijana. Tupongeze Serikali kwa maamuzi hayo, lakini nikiri kwamba malengo haya mazuri hayajafanikiwa, Wizara imepanga kufanya Mafunzo ya Ujasiriamali, uanzishaji na uendeshaji wa miradi na kampuni endelevu. Tatizo hapo ni upatikanaji wa Vijana na usimamizi. Kuna watu wanaitwa Maafisa Vijana sasa wawe huru na sio wawe chini ya Idara za Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, sekta ya habari ni duniani inaendelea kukua (duniani) ilihali nchini Tanzania sekta hii inazidi kudorora kwa Vyombo vya Habari kutokuwa huru na kukandamizwa na Serikali. Hata hivyo, uhuru sharti uwe na mipaka na hivyo si kwa utashi wa Waziri mwenye dhamana kuweka mipaka bila utaratibu wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, je ni lini Muswada wa Vyombo vya Habari utaletwa Bungeni? Mara nyingi majibu ya Wizara yamekuwa ni wapo katika hatua za mwisho? Ni lini majibu haya yatakwisha? Tunataka Wizara itupe *time frame* ya lini Mswada utafika Bungeni?

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda kutoa wito kwa vyombo vya Habari kuzingatia maadili katika utendaji kazi wao ili jamii ipate habari sahihi na za ukweli.

Mheshimiwa Spika, utamaduni wa Mtanzania ni muhimu kulindwa na kutunzwa kwa gharama yoyote ile kwa kuwa utamaduni wetu ndio Utaifa wetu. Utamaduni ni pamoja na mavazi, mila na vyombo vyote vya makabila yote hapa nchini. Mambo yote haya ni muhimu kulindwa, kutunzwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya vizazi vijavyo. Hata hivyo, napenda kutoa ushauri kwa Wizara kufanya uratibu wa maonyesho ya tamaduni na makabila mbalimbali hapa nchini angalau kila mwaka mara moja na pawepo na mzunguko wa kikanda.

Mheshimiwa Spika, suala la Vijana naunga mkono hoja Kambi ya Upinzani Bungeni kuhusu suala la vijana hasa kuhusu Mfuko wa maendeleo ya vijana na benki ya Vijana nchini. Hata hivyo, pamoja na fedha ndogo zilizotengwa kuhusu Mfuko wa Vijana ni vyema fedha hizo zikatengwa na kuwafikia vijana

Nakala ya Mtando (Online Document)

wengi walio vijijini na suala hilo liwe endelevu ili kuwasaidia vijana zaidi kwa siku zijazo.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Spika, napongeza kwa hotuba nzuri ya Wizara hii, naomba kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Waandishi wa Habari wengi hapa nchini hawana ajira za uhakika na hivyo kuchangia waandishi wachache wamekuwa wakirubuniwa ili waandike habari kwa maslahi ya wale wanaotaka kuandika habari zao kwa matakwa yao.

Mheshimiwa Spika, mmomonyoko wa maadili umeshamiri sana, naomba Wizara hii ihakikishe kwamba inajimarisha kudumisha utamaduni wa nchi yetu na sio tamaduni za Kimagharibi.

Mheshimiwa Spika, naomba vijana waanzishiwe Kituo Maalum cha Kukuza Uzoefu baada ya kuhitimu masomo yao ili waweze kuwa washindaji wazuri katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. KHATIBU SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika bajeti hii ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ikamilishe ahadi yake ya kuleta Muswada wa vyombo vyaa habari ili kuondoa malalamiko yaliyopo ndani ya nchi kwamba kuna ukandamizaji wa vyombo vyaa habari.

Mheshimiwa Spika, jambo hili sasa limekuwa la muda mrefu na limezua mijadala mingi, hivyo naomba jibu la Serikali, ni lini Muswada huo wa Vyombo vyaa Habari utaletwa hapa Bungeni ili Bunge liujadili na kuweka mazingira bora ya habari hapa chini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuiomba Serikali tamko la hatua inazochukua kukabiliana na magazeti yanayoendeleza tabia chafu ya kuchapisha machapisho yasiyo na maadili katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna magazeti mengi hapa nchini ambayo yamebatizwa jina la magazeti ya udaku, mfano Ijumaa, Champion, Risasi na kadhalika ambayo yamefikia hatua ya kuandaa mafumanizi bandia na kuwaweka watu wakiwa uchi kusudio lao ni kupata picha za kuweka katika magazeti yao. Hili jambo halikubaliki na naomba tamko la Serikali juu ya hatua inazochukua kukabiliana na aibu hii kubwa kwa Taifa letu.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itueleze faida halisi zinazopatikana kutokana na ushiriki wa vijana wa Tanzania katika *Big Brother Africa*. Mimi kwa maoni yangu, mashindano haya hayana tija kwa Taifa na naomba yasitishwe vijana wetu kushiriki katika *Big Brother Africa*.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Serikali iangalie upya faida za kuendelea kukimbiza Mwenge katika nchi yetu. Je, bado iko haja ya kuendelea kuwepo kwa mbio za Mwenge au la? Kama faida zipo zinalingana na mahitaji ya wakati huu tulionao?

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nakupongeza Naibu Waziri kwa umahiri wako katika kuiongoza vyema Wizara hii, vijana wa Tanzania wana matumaini makubwa kwako.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mbozi kuna kesi kati ya Chama cha Mapinduzi na wananchi waliojenga vibanda (maduka) katika uwanja unaodaiwa kuwa ni mali ya Chama cha Mapinduzi, lakini wananchi walipewa viwanja na vibali vyta kujenga katika eneo hilo na Halmashauri ya Wilaya, lakini mpaka sasa kuna ugomvi uliopelekea wananchi kupeleka kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, uwanja huo upo eneo la Vwawa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi. Hivyo basi, katika kuhitimisha tunataka ufanuzi toka kwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ili tujue haki za wananchi hao waliojenga vibanda vyao kwa mikopo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR: Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri. Naunga mkono hotuba hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni ya TBC. TBC inadai fedha nyingi Serikalini, taasisi za Serikali, taasisi binafsi na mashirika na watu binafsi. Inasikitisha sana kuwa bado fedha nyingi hazijalipwa ingawa pesa kidogo tu zimelipwa. Katika bajeti ya mwaka jana tulipendekeza kuwa fedha zinazodaiwa Wizara na taasisi za Serikali zikatwe moja kwa moja na bajeti zao.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zikilipwa zitaweza kusaidia sana TBC kwa kununua vipuri, vifaa na hata kulipia gharama nyingine.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, TBC vile vile inadaiwa fedha nyingi. Lazima hatua zichukuliwe pamoja na mpango wa kuhakikisha kuwa deni hili linalipwa haraka kama inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Makocha wa kigeni. Serikali inachangia kulipa mshahara wa kocha wa mpira wa miguu. Mbali kuwa fedha nyingi zinatumika kumlipa kocha, bado mpira wa miguu haujaendelea kwa kiwango cha kuridhisha. Hivyo, Wizara bora ijipange upya na hasa kutumia makocha wazalendo kwa ajili ya kuleta maaendeleo katika mpira wa miguu.

Mheshimiwa Spika, itakuwa vyema kuwapatia mafunzo makocha wazalendo na hawa ndio watakaoleta maendeleo katika mpira.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii. Wizara hii ni muhimu sana kwa Ustawi wa Taifa letu kwa sababu inahudumia sehemu muhimu sana ya jamii yetu vijana, lakini pia Wizara hii inahudumia habari ambayo ni muhimu sana kwa amani na utulivu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, michezo na afya, ajira lakini pia inaweka mahusiano mazuri ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu habari. Habari ni eneo muhimu sana kwa kupasha watu habari, lakini ni lazima kuwe na sheria ili kuhakikisha sekta hii haitumiki kuleta mtifaruku bali unaendeleza amani na utulivu nchini.

Mheshimiwa Spika, kuna waandishi ambao siyo waadilifu, lakini pia hupotosha maudhui ya habari. Leo hii kuna waandishi ambao hujaribu kupindisha habari kwa maslahi binafsi au kwa rushwa.

Mheshimiwa Spika, mauaji mengi katika nchi nyingi mfano ya Kimbari yamechochewa na vyombo vya habari na mara nyingine hata kutia petrol kwenye moto. Hii ni hatari sana na Wizara ifanye kila liwezekanalo kuhakikisha vitendo kama hivyo havina nafasi nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vijana. Nchi nyingi zimeingia kwenye mchafuko kwa sababu ya vijana kutokuwa na ajira na hivyo kukata tamaa. Wizara iamue sasa kujenga mfumo imara kuhakikisha inawasaidia vijana kujajiri, hii ni pamoja na kilimo, biashara na michezo.

Mheshimiwa Spika, tuelezwe fedha za vijana ilikuwaje hazikutolewa. Ni kwa nini Serikali isizitoe kabla ya mwisho wa mwaka huu ili fedha hizo ziwekwe kwenye mabenki ili wakopeshwe mara tatu na hivyo tuweze kukopesha vijana

Nakala ya Mtando (Online Document)

wengi. Mheshimiwa Waziri nini hatua ya Benki ya vijana, kwa nini mpaka leo Serikali haijaanzisha Benki hii muhimu. Mheshimiwa Waziri ni kwa nini Serikali/Wizara yako isisimamie asilimia tano (5%) inayopaswa kutolewa na Manispaa zote ili kuwe na uhakika na fedha hizo kutolewa na pia kwenda kwa walengwa ningependa kupata jibu la hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo. Michezo siyo tu afya na burudani bali pia ajira. Tumeshuhudia nchi nyingi vijana wakipata kipato kikubwa na kuwa hata mabilionea.

Mheshimiwa Spika, ningependa kupata taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, ni mkakati gani Wizara inayo kufanya michezo kuwa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, vijana wa mtaani wanaonyakua Kombe la Dunia na kutoa ujumbe kuwa mtaani kuna vipaji vingi ambavyo pengine hata kwenye mifumo rasmi havipo. Wizara ina mkakati gani wa kuanza kuwaendeleza hao vijana, lakini pia ni vipi imejipanga kuibua vipaji vipyta na kuendeleza vilivyopo.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi sana wanaharibiwa na madawa ya kulevyta, ni jinsi gani Wizara imojiandaa kulinda vijana wetu dhidi ya madawa ya kulevyta.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nampongeza Mwenyekiti wa TFF kwa kuchaguliwa, lakini pia kwa kunteua mjumbe wa Trustee, nakuhakikisha utumishi bora. Ahsante.

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Spika, nianze na habari kumekuwa na tatizo kwa waandishi wa habari kunyimwa uhuru wa kupata taarifa muhimu, hasa maeneo ambayo wanapaswa kuhakikisha kama haki inatendeka, mfano, Mahakama pia Magereza.

Mheshimiwa Spika, sehemu hizi waandishi wa habari wamekuwa wakinyimwa haki ya kupata habari na kama kweli haki inatendeka ni kwa nini waandishi wa habari wanazuiliwa kuchukua habari?

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuangalia sheria upya kuhusu uhuru wa vyombo vyta habari kwa maeneo haya ili kuruhusu wananchi kupata habari.

Mheshimiwa Spika, pia kuhusu ajira kwa waandishi, wamekuwa wakifanya kazi kwa ujira mdogo na kazi zao hazina mkataba maalum. Naiomba Serikali kuangalia upya namna ya kusimamia maslahi yao waandishi hawa.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, suala la vijana ni suala pana sana nchini. Vijana hawa ndiyo nguvu kazi ya Taifa nchini, lakini tatizo kubwa ni ajira namna ya kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi ni elimu wanayoipata imelenga kuwaandaa vijana katika mazingira ya kuajiriwa badala ya kuwaandaa katika kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la mikopo kwa vijana kutoka katika Halmashauri asilimia tano kwa kila Halmashauri nchini, ningependa kujua ni vijana wa namna gani wanaopaswa kupewa fedha hizo? Kwani vijana huishia kuzisikia tu, kwa maneno matamu kupewa yasiyo na matekelezo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika.

- Ukosefu wa ajira kwa vijana ni tatizo.
- Mfumo wa elimu kumkomboa kijana wa Kitanzania ni tatizo.
- Utolewaji wa mikopo kwa elimu ya juu kukosa mfumo sahihi ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utamaduni. Utamaduni ni utambulisho wa asili ya jamii kuitia makabila nchini kwa ujumla. Nasikitika kuona utamaduni wa Mtanzania unapotea siku hadi siku. Maafisa Utamaduni tunao, lakini hatuoni jitihada za kuendeleza au kulinda utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, utamaduni sasa umepotea kuanzia kwenye mavazi, lugha hadi nyimbo. Mfano, Mheshimiwa Spika

(a) Vazi la mjamzito limepoteza thamani kabisa mama mjamzito anashauriwa kuvala nguo pana ambayo haibani tumbo, lakini unakuta mwanamke anavaa kisuruali na nguo iliyombana tumbo, anafunga na mkanda. Naiomba Serikali iwe na meno makali kuhusu mavazi holela na sheria kali ziwekwe.

(b) Mheshimiwa Spika, lugha kumekuwa na tabia kwa wananchi wengi hasa wanafunzi wa sekondari na vyuo kuongea maneno ya kuchanganya *English* na Kiswahili hata wakati wa usaili mbalimbali na kujifanya hawajui lugha yao ya Kiswahili. Huo ni ulimbukeni.

Mheshimiwa Spika naiomba Serikali kuitia Baraza la Kiswahili nchini kuhakikisha elimu inatolewa mashulenii na kwenye vyombo vyaa habari kuhusu ubora wa lugha ya Kiswahili badala ya Kiswahili kipigwe marufuku.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu nyimbo nashauri Serikali iweke somo la muziki mashulenii kwani wanafunzi tuliosoma miaka ya nyuma tulisoma somo la muziki na kujifunza nota na tuliiimba nyimbo za kupendeza sana tofauti na sasa. Serikali isifanye mzaha na hili.

Mheshimiwa Spika, nawakilisha.

MHE. CELINA O. KOMBANI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Kwanza napenda niipongeze Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya hasa katika kutoa elimu kwa vijana ili wajajiri wenyewe. Katika Jimbo langu nina vikundi vya vijana ambao wamekwishajajiri, vikundi hivyo ni pamoja na umoja wa maendeleo bodaboda Vigoi (UWA) ambao hadi sasa wana pikipiki 15 kati ya vijana 32, vijana hao tatizo lao ni elimu ya usajiliamali tu.

Mheshimiwa Spika, kikundi cha pili kinaitwa “Machinga Complex” ambacho kinajishughulisha na kilimo, vijana hao wameomba msaada katika Wizara yako, lakini hawajapata majibu yoyote.

Mheshimiwa Spika, kikundi cha tatu kinajishughulisha na kilimo cha pamba, kwa kuanzia niliwasaidia kama mtaji sh. 5,000,000/= wamelima ekari 100, vijana hao baada ya mavuno wanahitaji elimu ya ujasiriamali na trekta tu. Ninachoomba Naibu Katibu Mkuu aende Wilaya ya Ulanga, akawatembelee vijana hao kuwapa moyo ili waweze kueleza changamoto zinazowakabili, mimi kama Mbunge nitashirikiana na Wizara kuendelea kuanzisha vikundi vya vijana ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, bajeti iliyotengwa kwa Wizara hii ni ndogo sana. Kiwango cha jumla ya Sh. 35,371,884,000/= hakitaweza kukidhi shughuli zote za Wizara hii kwa ufanisi. Serikali iongeze bajeti ya Wizara hii ili yale yote yaliyopangwa yatekelezwe kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, nashauri Shirika la Habari la Taifa litengewe fedha za kutosha kuliendesha lakini pia ikumbukwe kwamba Shirika hili linaendeshwa kwa kodi za Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, iweje leo Shirika hili halitangazi hata siku moja Mikutano ya hadhara ya upinzani? Kwani Wapinzani hawalipi kodi?

Mheshimiwa Spika, sheria pekee itakayoweza kusawazisha jambo hili ni kuletwa hapa Bungeni Muswada wa Sheria ya Uhuru wa kutoa na kupata

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Habari. Ni haki ya kila Mtaanzania kupata Habari bila upendeleo kwa habari zinazotolewa.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa nane wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna maelezo kwamba Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama baadhi ya vyombo vya habari kukiuka sheria kwa kuandika na kutangaza habari ambazo hazizingatii kanuni na maadili ya taaluma ya Uandishi wa Habari.

Mheshimiwa Spika, endapo sheria ambayo wanatasnia wa habari wameipigia kelele kwa muda mrefu ingetungwa kwa kukubali Muswada kuletwa Bungeni, leo hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri pengine isingekutana au kukabiliwa na changamoto. Hivyo, tayari sheria ingewabana wale wanahabari wote wanaokwenda kinyume na maadili ya habari waliyofundishwa shulenii.

Hivyo basi, kama nilivyochangia kwa kuzungumza, Sheria ya Uhuru wa Kutoa na Kupata Habari, nasisitiza ifanyiwe kazi kwa umuhimu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache naomba kuwasilisha.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu nimeletta kilio cha wananchi wa Jimbo la Rombo kwamba hatupati matangazo ya radio ya Taifa (TBC) pamoja na Television ya Taifa. Majibu ya miaka yote minne ambayo nimekuwa hapa Bungeni ni kwamba kituo kitajengwa ili kuimarisha usikivu wa vyombo hivi. Naomba wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri atupe kauli ya Serikali, ni lini kazi hiyo itaanza?

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ni kwamba hapa Bungeni kumekuwa na lawama kwa Serikali kwamba haidhibiti vyeti feki. Zipo taarifa kwamba vilabu vingi vya michezo vina viongozi amba wana vyeti feki.

Mheshimiwa Spika, mfano ni kwamba Kamati ya Uchaguzi wa Simba imetoa taarifa kwamba waliochukuwa fomu kwa ajili ya kuomba nafasi mbalimbali wengi wao wana vyeti feki na mionganini mwao wamo wenye majina makubwa.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inasemaje kuhusu tuhuma hii ya viongozi wanaoharibu michezo? Je, Serikali iko tayari kuingiza Kamati ya Uchaguzi ya Simba kukabidhi vyeti hivyo kwa mamlaka sahihi kwa ajili ya uchunguzi ili kudhibiti hali hiyo?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Spika, deni la TBC ni la muda mrefu sasa na dhamira ya kweli kulipa deni hili hasa kwa Taasisi za Serikali ni kizungumkuti.

Mheshimiwa Spika, naitaka Serikali ianze sasa kulipa deni hili ili kuiwezesha TBC kumudu gharama zake. Usikivu wa TBC pamoja na kuwa na utitiri wa vyombo vya habari, lakini Serikali lazima iwe na chombo chake cha habari muhimu kwa Taifa lolote duniani.

Mheshimiwa Spika, TBC haisikiki katika maeneo mengi nchini. Ni vyema Serikali ielezee na kwa namna gani inaweza kumaliza tatizo hili? Kwa sasa ni vema ikatoa tamko rasmi kwa Umma.

MHE. DKT. PINDI H. CHANA – NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Njombe hawana Mwakilishi wa TBC; je, ni lini Mkoa wa Njombe utapata mwakilishi wa TBC?

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba Bodi ya Filamu Basata wapewe mafungu ya kutosha na attention na watumishi wa kutosha ili kuboresha maeneo yao.

MHE. ABUU H. JUMAA. Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ya mwaka wa fedha 2014/2015.

Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam wake kwa bajeti yake nzuri yenye malengo na mikakati mizuri yenye kuleta tija kwa Taifa letu. Bajeti hii imelenga kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa kuweka mikakati mizuri ya nchi katika kukuza utamaduni, Michezo na kuboresha Sekta ya habari na Vijana nchini.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuanza kwa kuzungumzia suala zima la Sekta ya Habari hapa nchini. Uhuru wa habari ni kitu kizuri sana, uhuru huo umekuwa ukivipa vyombo vya habari uhuru wa kutosha juu ya kupata habari na hivyo kuwafikisha wananchi, kwa kuwa mtu wa mwisho ni mwananchi ambae naye ana uhuru wa kupata habari, ila tumekuwa tukijiona mara nyingi vyombo vya habari vikifanya upotoshaji mkubwa katika mambo mbalimbali kwa jamii.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 18 ya Katiba inasema: "(1) Kila mtu yuko huru kuwa na maoni yoyote na kutoa nje mawazo yake, kufuata, kupokea na kutoa habari na dhana zozote kupitia chombo chochote bila ya kujali mipaka ya nchi na pia ana uhuru wa mawasiliano yake kutoingiliwa kati."

Sasa imekuwa kawaida kwa baadhi ya vyombo vyahabari hususan magazeti kuandika habari katika kurasa za mbele zenyetengano, uchochezi pamoja na upotoshaji mkubwa wa aina hiyo. Sasa najiuliza, uhuru huu wa habari ambao vyombo hivi wanavyo na jinsi wanavyoutumia: Je, huo uhuru zaidi na kutaka Sheria ya Vyombo vyahabari iboreshwe, ikipitishwa kweli tutakuwa salama? Ni mambo ya kujiliza kwa mapana yake kabla ya kufanya maamuzi yoyote juu ya jambo hili.

Ni lazima wahariri/wana habari wawe na uzalendo na kutambua kuwa vyombo vyahabari vina nguvu kubwa sana kwa jamii kwani wananchi walio wengi wanategemea kupata habari kutoka katika vyombo hivi na wamekuwa wana imani navyo kwa asilimia kubwa sana. Kwa hiyo, upotoshaji wowote utakaofanyika, basi ni moja kwa moja utaathiri Taifa letu. Hivyo basi, napenda kuviasi vyombo vyahabari kuwa makini katika utendaji wao kwani kuibomoa nchi ni rahisi sana na ugumu unakuja kwenye kuijenga.

Nashauri kwamba vyombo vyahabari visiangalie faida tu kwa kuandika habari za uwongo ama uchochezi ili wapate kuuza magazeti yao au station zao ziweze kupata waangaliaji wengi, kwani kufanya hivyo ni kukiuka sheria na miiko ya uandishi wa habari. Ushauri wangu kwa Serikali ni kuzidi kuchukua hatua kali zaidi na kuongeza adhabu ili iwe fundisho kwa wote watakaogundulika kufanya upotoshaji wa aina yoyote kwa jamii ama uchochezi.

Pia kuwachukulia hatua wale wote wanaotumia vyombo vyao vyahabari kwa manufaa yao yenyewe binafsi badala ya kuelimisha jamii au kuonyesha/ kuandika habari zenyetengano kwa jamii; wamiliki hawa naomba wachukuliwe hatua kali sana kwani kufanya hivyo ni makosa makubwa.

Pamoja na maendeleo yaliyopatikana katika Sekta ya Habari na Utangazaji, utoaji wa huduma katika sekta umekuwa siyo wa kuridhisha kutoeleza kwa ufasiha nafasi ya Sekta ya Habari na Utangazaji katika maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Matokeo yake ni kwamba bado kuna baadhi ya watu wenye mtazamo wa kuona chombo cha habari kuwa nyenzo ya kufanikisha malengo yao binafsi, badala ya yale ya utoaji wa huduma kwa

Nakala ya Mtando (Online Document)

jamii. Aidha, baadhi ya wamiliki wa vyombo vya habari wamekuwa wakijali zaidi kupata faida bila kuzingatia maslahi ya Taifa. Baadhi ya vipengele vya Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 na Sheria ya Utangazaji ya mwaka 1993 vina upungufu mkubwa ambao umesababisha malalamiko mengi.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama wa mtando ni dhahiri bado jitihada za dhati zinahitajika kuweza kuleta mabadiliko na kupata Tanzania salama kmtandao, afrika na dunia kiujumla. Ili kuleta mabadiliko chanya, jukumu la kutoa elimu halipaswi kubaki kwa mtu mmoja au kundi fulani la watu, bali ni lazima kuwe na kuunganisha nguvu ya pamoja na kutoka katika kila mtu mmoja mmoja. Miiongoni mwa jitihada zinazoonekana kwa vyombo vya habari na makundi mbalimbali nchini, Tanzania tumeanza kuona umuhimu wa masuala ya ulinzi mtando ili kupata Taifa salama kmtandao. Jitihada zaidi bado zinahitajika ili jamii iendelee kujua zaidi ni nini hasa umuhimu wa kujenga tabia ya kutumia mitando kiusalama ili kuweza kuliweka Taifa kuwa salama kmtandao.

Aidha, bado naendelea kutoa wito kwa vyombo vya habari kuendeleza jitihada katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii ili kujua athari na nini kifanyike ili kupata Taifa salama kmtandao kwani ni dhahiri kuwa vyombo vya habari vina habari, vina nafasi kubwa kuweza kuhamasisha jamii kujua umuhimu wa usalama mtando.

Kwa upande mwingine, Tasnia za sanaa pia zina nafasi kubwa sana katika kuleta mabadiliko katika jamii, kwani nchi kubwa zimekuwa zikitumia sana tasnia za uigizaji kupitia tamthilia na movie mbalimbali kupata fursa ya kuingiza vipengele vyenye kugusa moja kwa moja suala la kutoa elimu katika jamii na masuala ya ulinzi mtando.

Mheshimiwa Spika, tunajadiliana namna ya fikra inavyobadilisha mtazamo, pamoja na kuambiwa kuwa takribani bilioni moja ya watu wanaoishi duniani ni vijana na kwamba asilimia 85 ya vijana hao wanaishi katika nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania. Vijana wa Afrika wanafikia asilimia 14 ya idadi ya vijana wote duniani. Kufukia mwaka 2025, kutakuwa na asilimia 89.5 ya vijana. Kuna nguvu kubwa inayolingana na idadi ya vijana ambayo kwa vyovyote vile kuipuza ni kujenga mazingira ya vurugu, vita na ukosefu wa amani. Hawa ndio nguvukazi na ndio wenye sehemu kubwa ya maono ya Afrika na dunia nzima kwa ujumla. Katika kipindi hiki nchini na dunia nzima kumekuwa na vuguvugu la vijana kutaka mabadiliko ambayo kimsingi ni kweli yanahitajika.

Ni mabadiliko ambayo yana mrengo wa kuweka mazingira yenye tija katika maisha yao, mustakabali wa maisha yao uwe endelevu na wenye ustawi.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Leo hii umaskini wa vijana ni wa kutisha. Vijana wengi wanapita kipindi kigumu cha kukosa ajira, kubaguliwa katika kupata huduma na kukosa mwelekeo wa maisha kutokana na fursa mbalimbali za kielimu, kiuchumi, kisiasa na kijamii. Pamoja na takwimu kuonyesha idadi ya vijana hao, bado kuna changamoto ya kifikra inayowakabili vijana wengi ambaa wanashindwa kufanya maamuzi yanayoweza kuleta mtazamo chanya.

Wapo vijana ambaa fikra waliyonayo ni kuwa, kama wakipata nafasi ya kwenda Ulaya, tutawasahau, na hawataweza kurudi kwa sababu hiyo ndiyo fikra waliyonayo. Kumbe wanajidanganya kwa kuwa hata huko Ulaya bado kuna vijana wanakabiliwa na matatizo kama yaliyopo Afrika. Ndiyo maana natumia nafasi hii kuwaeleza kuwa kuna haja ya kubadilika kimtazamo. Mfano mwagine ni kuwepo kwa vijana wengi wanaopenda mafanikio ya haraka, lakini hawapendi kujishughulisha.

Vijana wanapenda kupata pesa lakini hawataki kuwa wabunifu wa kazi. Ni lazima kundi hili lifahamu kuwa maisha yana kanuni zake na endapo tutashinda kuzifuata inaweza kusababisha kufika mahali ambapo katika maisha hukutegemea. Ni muhimu vijana wakaelewa kuwa fikra tulizonazo zina umuhimu katika maendeleo na ukuaji wa uchumi, maendeleo au katika mahusiano. Ni jambo jema kama tutaweka uelewa kuwa siku, miezi na miaka itabadi, lakini kama hatutabadi, fikra zetu, tutabaki kuwa wale wale katika kila mwaka.

SikU ya muhimu katika maisha yako ni ile utakayochukua uamuzi wa kubadilisha fikra zako. Ukatili na maovu yanayoendelea katika ulimwengu wa leo ni kwa sababu fikra za watu zimechafuka. Hivyo, kutokana na ukatili huo, hata Magereza yatajaa kama fikra za watu hazitabadi, kwani fikra ndiyo zinazojenga tabia na hisia za mtu. Kwa mfano, leo ukimsafirisha kuku na kumpeleka Marekani, hatabadi, kuwa bata, atabaki kuku.

Mheshimiwa Spika, wengi wanaamini labda hatua ya kuzaliwa Afrika ndiyo chanzo cha umasikini wao na haya yote tunayoyapitia, lakini ni fikra zetu tulizojengea ndiyo zinazotufunga. Tukibadilisha fikra zetu, kila kinachotuzunguka kitabadi.

Mheshimiwa Spika, asilimia 72 ya vijana wanaishi Afrika, Kusini mwa jangwa la Sahara wanaishi katika hali ya umasikini wa kutisha, hali inayotokana na kukosa misingi mizuri ya kuwajengea vijana mipango endelevu inayoongeza fursa za kuijendeleza na fursa wanazopewa na hata kuwa na fikra za kujitambua ili waweze kuleta mabadiliko chanya wao wenyewe bila kuwa tegemezi. Kwa hali hiyo, Serikali haina budi kuchukua hatua za haraka katika kuwajengea vijana wetu ambaa ndio Taifa la kesho na kuwatoa katika fikra hizo

Nakala ya Mtando (Online Document)

ambazo hazina tija na kuwarudishia imani na nchi yao na kuweka mambo wazi. kuwawezesha vijana.

Jambo ambalo linazungumziwa sana na vijana ni kutokupata fursa ambazo nyingi wameona hupatiwa wazee na hivyo kuwafanya kukata tamaa. Ni jukumu la Sekali kuwalinda watoto na vijana dhidi ya ukatili wa aina yoyote kwa mujibu wa sheria za nchi na mikataba mbalimbali ya Kimataifa. Sheria hizi pamoja na mikataba zinasema kuwa vijana wana haki, ikiwemo haki ya kulindwa dhidi ya ukatili wa aina yoyote.

Wazazi, familia, Walimu, Polisi na jamii nzima wana jukumu la kuwalinda vijana na watoto. Hata hivyo jambo la kusikitisha ni kwamba wakati mwengine watu wanaotakiwa kuwalinda vijana wanashiriki kuwafanya ukatili. Kwa mfano, hapa nchini ni halali kisheria kutoa adhabu ya viboko kwa vijana, iwe shuleni au majumbani. Baadhi ya wazazi huamini kuwa viboko vitawafanya watoto wawe na adabu. Hata hivyo ukweli ni kwamba, viboko havisaidii, na ni ukiukaji wa haki ambayo inatakiwa kulindwa.

Mheshimiwa Spika, uvumbuzi wa utamaduni unamaanisha uvumbuzi wowote mpya na unaopatikana kuwa manufaa kwa kikundi cha watu na unaelezewa katika tabia zao, lakini haupo kama kitu kinachoonekana. Watu wako katika ulimwengu unaoharakisha mabadiliko ya utamaduni kiwakati, wakisukumwa na kupanuka kwa biashara kimataifa, vyombo vyya habari, na kuongezeka kwa idadi ya watu mionganoni mwa mambo mengine.

Tamaduni zinaathiriwa na nguvu zinazoleta mababiliko na zile zinazopinga madabiliko. Nguvu hizi zina uhusiano na miundo ya kijamii na matukio halisi na zinajihusisha katika kuendeleza mawazo na matendo ya kitamaduni ndani ya miundo ya sasa ambayo nayo inabadilika.

Mizozo ya kijamii na maendeleo ya kiteknolojia yanaweza kusababisha mabadiliko katika jamii kwa kubadili mikiki mikiki ya kijamii kwa kukuza ruwaza mpya za utamaduni kwa kuwezesha tukio zalishi. Hii mihamisho ya kijamii huweza kuandamana na mihamisho ya kiti kadi na aina nyingine za mabadiliko ya kitamaduni. Kwa mfano, Muungano wa Kifeministi wa Kimarekani ulihusisha matendo mapya yaliyosababisha uhamisho katika mahusiano ya kijansia, kubadilisha jinsia na miundo ya kiuchumi. Hali ya kimazingira inaweza kuchangia mabadiliko kuhusisha kufuata nguli wa kienyeji katika filamu. Kwa mfano, misitu ya kitropika ilirejea tena mwishoni mwa enzi ya theluji.

Mimea iliyofaa kwa kilimo ilikuwepo, ikasababisha kuvumbuliwa kwa kilimo, ambacho kilisababisha uvumbuzi wa kitamaduni na mihamisho ya mikiki mikiki ya kijamii. Tamaduni huathiri kutoka nje kuitia kwa mwengiliano baina ya

Nakala ya Mtandao (Online Document)

jamii ambazo pia zinaweza kutoa au kuzuia mihamisho ya kijamii na mabadiliko katika matendo ya kitamaduni.

Vita au ushindani juu ya rasilimali unaweza kuathiri maendeleo ya kiteknolojia na mikiki mikiki ya kijamii. Kuongezea mawazo kitamaduni yanaweza kuhama kutoka jamii moja hadi nyingine kupitia kwa kuenea na kwa mabadiliko ya uigaji wa utamaduni fulani.

Katika kuenea kwa hali ya kitu (siyo lazima maana yake) hutoka utamaduni mmoja hadi mwingine. Kwa mfano, humburgers ambazo ni za kawaida Marekani zilioneekana kuwa ngeni zilipoanzishwa Uchina. Kuenea kunakoacha athari (kubadilishana mawazo) hurejelea elements za utamaduni mmoja kusababisha kuwepo kwa uvumbuzi au kusambazwa kwa mwingine. Uokoaji wa moja kwa moja kwa upande mwingine hurejea kuenea kwa wakati kiteknolojia au kuenea kuoneekana kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine. Nadharia ya kuenea kwa uvumbuzi, huwasilisha ruwaza ya utafiti wa kwa nini na lini watu na tamaduni huwasilisha mawazo mapya, matendo na bidhaa.

Mheshimiwa Spika, michezo ni nguzo kubwa sana duniani kwani michezo inaleta amani, hukutanisha watu pamoja na kubadilishana mawazo, pia ni burudani. Naipongeza Serikali kwa kuweka juhudzi zake kubwa katika kukuza michezo hapa nchini, lakini kumekuwa na changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta nzima ya michezo hapa nchini.

Serikali katika jitihada zake imekuwa ikiwekeza zaidi katika baadhi ya michezo na kuacha michezo mingine jambo ambalo siyo zuri, kwani baadhi ya michezo iliyoachwa na kama Serikali ingewekeza vizuri kama ifanyavyo katika michezo mingine, basi ingeweza kuleta tija kubwa hapa nchini.

Sekta hii ya Michezo inahitaji ufuatiliaji wa hali ya juu kwani kuna baadhi ya Viongozi wa Vyama vya Michezo wamekuwa sio waaminifu kwa kufuja mali na fedha za wafadhili na Serikali na hivyo kufanya juhudzi zote za Serikali katika michezo kuzidi kuzorota. Kwa mfano, juzi hapa kuna jambo lilitokea katika Chama cha Michezo ya Olimpiki baada ya kupitisha majina ya wanamichezo watakaokwenda kutuwakilisha nje na kuyapeleka Serikalini na Serikali kuyarudisha kama yalivyo, ila kuna baadhi ya wanamichezo walipigiwa simu na kuambiwa kuwa Serikali imekata majina yao, hivyo hawatakwenda ilhali Serikali haikukata majina hayo. Huu ni ujisadi na wizi wa wazi kwa viongozi hawa. Hivyo Serikali haina budi kuwachukulia hatua kali watu hawa na kuwafikisha Mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

Naiomba Serikali izidi kuunga mkono masuala ya michezo kwani imekuwa ikiwapa ajira vijana wetu hivi sasa na hivyo kujikwamua kiuchumi na

Nakala ya Mtando (Online Document)

kuondokana na tatizo la ajira nchini kwa vijana kama liliyvo hivi sasa. Vilevile kuna suala zima la filamu zetu hapa nchini, filamu zinazotengenezwa na vijana wetu hakika wamekuwa wakiibiwa sana na kupata faida ndogo. Serikali sasa haina budi kulifanyia kazi suala hili ili wasanii wetu waweze kupata fedha kupidia sanaa zao, pia Serikali iweze kupata fedha kwa kukusanya kodi kupidia mauzo ya kazi hizo. Jinsi ya kudhibiti hali hiyo inawezekana kabisa kwa kushirikiana na vyombo vya usalama pamoja na TRA, maana sekta imekuwa na wapenzi wengi ambao hununua kazi za wasanii wetu, hivyo kuna fedha nyingi sana hupotea kwa Serikali kutowafuatilia kwa kupata kodi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, taarifa mbalimbali zinaonesha kila mwaka wahitimu 1,200,000 wanahitimu vyo mbalimbali, ambapo ni wahitimu 200,000 tu ndiyo wanapata ajira. Hivyo, Serikali imekuwa ikiwahamasisha vijana kujiajiri.

Kupitia Hotuba mbalimbali za Viongozi Wakuu akiwemo Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete na Waziri Mkuu Mizengo Pinda, wametoa maelekezo Halmashauri zetu kupidia Wakuu wa Wilaya, kutenga maeneo ya kilimo kwa vijana. Utekelezaji wake tumeanza kuuona kwenye baadhi ya Wilaya kama vile Igunga na Tabora Mjini, Mkoa wa Pwani kuna Mradi wa Kufyatuta Matofali na Wilaya ya Mvomero.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua ni Wilaya ngapi hadi sasa zimetekeleza na hatua walizofikia katika kushirikisha vijana kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe kipaumbele kwenye kuwuezesa Mfuko wa Maendeleo wa Vijana, kwani vijana wengi hawana mali za kuweka dhamana katika mabenki waweze kukopesheka. Kupitia Mfuko huu, vijana inakuwa rahisi kuwuezesa kukuza mitaji yao.

Mwaka 2013/2014 Serikali ilitenga bilioni 6.1 kwa ajili ya mkopo kwa vijana, lakini cha kusikitisha sana, Serikali ilitoa shilingi billioni mbili tu. Naomba Serikali ipeleke fedha zilizobaki ziwawezeshe vijana. Mwaka 2014/2015 zimetengwa bilioni nne kwenye Mfuko huu, jambo ambalo fedha zinashuka kila mwaka badala ya kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, Serikali inawafukuza Wamachinga huko mijini, inawazuia vijana wa bodaboda kutofanya kazi zao katikati ya mijji, lakini kama hakutakuwa na dhamira ya dhati ya kuwajengea uwezo wa mafunzo na

Nakala ya Mtando (Online Document)

kuwapa mikopo ya riba nafuu, vijana wataendelea na biashara zisizo halali ikiwemo wizi na ujambazi. Hivyo, Serikali lazima iuwezeshe Mfuko wa Maendeleo wa Vijana kifedha na kuendelea kuhamasisha vijana kujunga na vikundi vya ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Spika, jitihada gani zinazofanywa na Wizara ya Vijana kuendeleza ustawi wao kwa kushirikiana na Wizara nyingine kama Kilimo na Ushirika, Elimu ya Juu, Ajira na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali italeta Muswada wa Baraza la Vijana Bungeni ili ujadiliwe na ni kiasi gani cha pesa kimetengwa kufanikisha uundwaji wa Baraza la vijana?

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati gani kufanya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kuwanufaisha vijana zaidi kuliko fedha zinatengwa kutumika kwenye posho, vikao, safari uhamasishaji wa uanzishwaji wa SACCOS, ufuutiliaji, kujenga uwezo na kadhalika, mfano vijana waliokopeshwa imetumika Sh. 172,609,000, fedha zilizobaki Sh. Bilioni 1,827,391,000, kutumika kwa shughuli nyingine kama ufuutiliaji, uhamasishaji, kujenga uwezo, uratibu na usimamizi, kubainisha vikundi na safari. Je, Wizara hamwoni kwamba fedha hizo hazifiki kwa walengwa?

Nawashauri kuwa, fedha hizo ziwekwe Benki ya NMB ili wao ndiyo watoe hiyo mikopo. Serikali itenye fedha zaidi kwa ajili ya maendeleo ya vijana ili zisaide kutoa ajira zaidi.

Mheshimiwa Spika, asilimia 75 ya vijana inajihuisha na kilimo; je, Idara ya Vijana ina mkakati gani kuendeleza kundi hili ili vijana wengi zaidi wajajiri kama kutafuta masoko?

Fedha nyingi zinazotolewa na wahisani mbalimbali hazionekani kwenye bajeti; je, Serikali haioni sasa haja ya kujumuisha pesa hizo zinazolenga vijana kwenye bajeti ili vijana watambue fursa na misaada hiyo ili kuitumia kikamilifu?

Mheshimiwa Spika, Maadhimisho ya Mwenge wa Uhuru yatazamwe upya kwani yana gharama kubwa ambazo zingebanwa zingesaidia kundi la vijana; kwani matumizi na michango inayotolewa hailengi maendeleo bali starehe tu.

MHE. ABASI Z. MTEVU: Mheshimiwa Spika, Viwanja viwili vya Michezo vya Taifa viwo Temeke, Kata ya Miburani. Je Manispaa ya Temeke haipati mapato yoyote kutohana na Viwanja hivyo?

Nakala ya Mtando (Online Document)

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, Jimbo la Manyoni Magharibi, Wilaya ya Manyoni, hadi sasa Wananchi wake wanashindwa kupata matangazo ya TBC. Tatizo hili nimeliwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa muda mrefu sasa na hata kwenye Vikao vya RCC *but to date nothing doing; niende wapi?*

Naomba kuiuliza Serikali kupitia Wizara hii ni lini Wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi watapata *live broadcasting* kutoka TBC?

Nipatiwe majibu ya kina mitambo hiyo itawekwa lini kupanua matangazo ya TBC; vinginevyo, nitalazimika kutumia haki yangu kwa kutumia Kifungu cha 103 cha Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa vitendo vya wizi wa kazi za wasanii imekuwa ni maumivu kwa wasanii kwa kuwa wanakosa mapato wanayostahili kuyapata. Kuendelea kuwepo kwa malalamiko ya wizi wa kazi za wasanii pamoja na maduka na wachuuzi wanaoendelea kuuza kazi za wasanii fake, inaonesha kuwa kazi hizi za wasanii hazilindwi ipasavyo. Kwa hiyo, ni wajibu wa Serikali na Wizara kuendelea kupiga vita wizi wa kazi za wasanii kila kukicha bila ya kupumzika ili wasanii wanufaike na kazi zao.

Mheshimiwa Spika, suala la uporomokaji wa maadili katika filamu za wasanii wa Kitanzania na kazi mbalimbali za muziki, kunaendelea kupoteza utamaduni wa Mtanzania. Leo hii filamu za Kitanzania zinaongoza kwa wasanii kuvaa nguo nusu uchi, zinaongoza kwa kutotumia Kiswahili fasaha na zinaongoza kwa kuiga utamaduni wa Magharibi, ambao si kweli kuwa unaawaongezea soko wasanii bali unalishushia Taifa letu hadhi yake katika Jumuiya za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, uhuru wa vyombo vya habari na masilahi ya waandishi wa habari ni jambo ambalo linatakiwa kupewa kipaumbele hasa ili kuikuza tasnia hii. Leo hii wanahabari wanafanya kazi katika mazingira magumu huku wakiambatana na sheria kandamizi zinazoua uhuru wao. Lazima Serikali ituambie ni mkakati gani umewekwa wa kuhakikisha kuwa wanahabari wanapewa kipaumbele katika kuboreshewa masilahi na mazingira ya kufanyia kazi ili kukuza sekta hii ya habari.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Taifa kuhakikisha kuwa, michezo yote inapewa kipaumbele. Ni dhahiri kuwa, michezo mingi nchini imepewa kisogo. Kwa minajili hii ni kuwa tutaendelea kuwa wasindikizaji katika michezo ya kimataifa ikiwemo Olympics na michezo ya Jumuiya ya Madola.

Mheshimiwa Spika, suala la kuajiri makocha wa kigeni limeshazungumzwa sana hapa nchini, lakini inavyoolekea bado Serikali haielewi. Mwaka huu kumetengwa pesa kwa ajili ya Baraza la Michezo na kulipa makocha wa kigeni, ni lini hasa makocha wa kigeni wameweza si tu kuifikisha mbali Timu ya Taifa na ku-sensitize michezo ngazi za chini?

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuitaka Wizara kuweka mikakati kuhakikisha kuwa, miji mikongwe kama Stone Town, Bagamoyo na Kilwa, haipotezi historia zake. Hii ni kwa kudhibiti ujengaji holela unaofanywa kupoteza utambulisho wa miji hii. Thamani ya utamaduni wetu ilindwe hata ikiwa ni kwa kuwekeza pesa nyingi katika ku-preserve uhalisia wa majengo na miji yenye. Leo hii ukienda Makumbusho ya Taifa, unakuta magari aliyoyatuma Baba wa Taifa yakiwa katika hali ile ile ya ukuukuu. Ukienda katika nchi za wenzetu pamoja na kuwa magari yaliyotumiwa na Viongozi wao yapo makumbusho lakini yamewekwa vizuri katika hali inayoyafanya yadumu zaidi na zaidi.

MHE. ABDUL R. MTEKETA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kidogo katika Wizara yako hususan kuhusu wachezaji wa zamani wa Taifa, ambao wengi wamelitumikia sana Taifa kwa miaka mingi na hali zao ni duni na wanatia huruma kwa kuwa Taifa limewatupa. Tofauti na nchi za wenzetu kuwa wanapatiwa heshima kubwa kwa kuwashirikisha katika mambo mbalimbali ya kuendeleza soka. Kutokana na mtindo wetu wa Tanzania wa Soka la kutokulipwa wachezaji hao wa zamani, kwa hiyo, wanapoacha Soka hali yao ya maisha inakuwa ngumu sana.

Naomba basi tuwafanyie mchango kwa mfano: kwenye Mechi kati ya Simba na Yanga mapato yote wapatiwe wachezaji wa zamani ambao hali zao ni mbaya sana, kama vile Aloo Mwita, Jela Mtangwa, Shabani Baraza, Kitwana Manara na wengine wengi. Pia kuhusu Timu yetu ya Taifa, naomba kocha wa timu hiyo akipatikana, awe huru na apewe muda wa kutosha ili apate fursa ya kufanya alichonacho bila kuingiliwa. Tuache tabia kuwa na wafundishaji wengi wakiwa waandishi wa habari na wapenzi wa Soka kuingilia kazi yake.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa sina uhakika kama Watanzania wanatambua utamaduni wao ni upi. Vielelezo vya utamaduni ni kama vile ngoma, nyimbo, ngonjera, mashairi na muziki wa dansi, ukijumuisha Vazi la Taifa. Kwa namna gani Wizara hii imefanya juhudzi za kuutambulisha Utamaduni wa Mtanzania? Tanzania ina makabila mengi sana; ni kwa kiasi kikubwa kila kabilalina utamaduni wake mfano, ngoma na nyimbo?

Kwa nini Watanzaia wanaendelea kuiga ngoma na midundo ya tamaduni ya nchi zingine ilhali wanaweza kuendeleza ngoma na midundo ya tamaduni zao? Si jambo geni sasa kuona vikundi vya ngoma vikicheza ngoma kwa kuiga midundo na style ya ngoma ya Botswana (Dume lang'u), mbele ya Viongozi Wakuu wa Nchi. Wizara haioni umuhimu wa kuvizezesha vikundi vya ngoma za makabila mbalimbali mfano: Sindimba – Mtwara na Wamakonde, Wasukuma, Wanyaturu (kuna Ngoma nzuri sana ya Mawindi na Ikuda) na kadhalika na kuvikopesha vifaa vya kisasa vya muziki ili kuboresha ngoma zao?

Kwa kufanya hivyo, si tu Taifa litatangaza utamaduni (Ngoma) wake Kimataifa kwa vionjo vya kisasa, bado litaongeza kipato kwa Wananchi wa Taifa lake.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Vijana, hauwanufaishi vijana kwa ujumla wao, kwani fedha zinazotengwa licha ya kuwa hazitoshi, pia hazitolewi kwa wakati. Uzingatia vijana ni 60% ya watu wote, mikopo haiwafikii vijana wengi hususan wa vijijini. Lazima Serikali itoe mkakati ni kwa namna gani itakabiliana na bomu hili la ukosefu wa mikopo kwa vijana ambalo linategemea kulipuka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wasanii wetu wa Filamu, kumekuwa na kasoro nyingi zinazoambatana na uandaaji wa Filamu hizi kwa mfano: utakuta Filamu nyingi zinatambulishwa kwa Kiingereza ilhali zinaoneshwa kwa Kiswahili. Kwa nini Wasanii kuwa hawatambulishi (*Title*) Filamu zao kwa Lugha ya Taifa (Kiswahili)? Kama hiyo haitoshi, Filamu inapochezwa, kuna maandishi yanayotafsiri kwa Kiingereza kile kinachozungumzwa. Cha kushangaza ni kwamba, hicho Kiingereza kinachoandikwa ni aibu kwa Taifa letu; ni Kiingereza kibovu ambacho anayesoma hasa yule asiyejua Kiswahili, hawezi kuelewa ni kitu gani kilichoandikwa. Kwa nini BASATA inafumbia macho hili? Kwa nini hatutafuti mtu au kampuni inayoshughulikia Kiingereza sanifu ili kuweza kufanya kazi hii ya tafsiri? Ni aibu kuendelea na tabia hii kwani inalitia aibu Taifa letu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kuhusu TBC na magazeti ya Serikali, vyombo vya habari vinavyomilikiwa na Serikali na kuendeshwa kwa kodi za Watanzania wote, vimekuwa vikifanya kazi kwa ubaguzi mkubwa na hivyo kulalamikiwa na wadau wengi. TBC na magazeti ya Serikali vimekuwa ni vyombo vya kufanya propaganda za kisiasa kwa kupendelea CCM na kuwaponda Vyama vya Upinzani. Hii tabia siyo nzuri na ni busara sasa kwa Wizara kuonya jambo hili ingawa nayo inahusika kwa ubaguzi huu Watanzania wote wakiwemo Wapinzani wanatoa kodi zinazoendesha vyombo hivi na si CCM peke yake. Hii tabia iachwe kwa mustakabali wa usawa na imani ya nchi yetu bila kupendelea chama kimoja au dini moja.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inajumuisha mambo nyeti pamoja mfano, Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Kulingana na majukumu mazito ya Wizara hii, bajeti inayotengwa ni ndogo sana na hata hivyo haitolewi kwa wakati. Kwa namna gani Wizara inaweza kutimiza majukumu yake sawasawa kwa mambo yote haya ambayo ni mazito kwa bajeti ndogo namna hiyo? Ni muhimu sasa Serikali ikaona umuhimu wa kutenganisha mambo ya vijana kwenye Wizara hii. Wizara inayoongoza vijana inatakiwa iwe peke yake ili masuala yao yaweze kushughulikiwa kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na danadana ya kuuleta Muswada wa Sheria wa Vyombo vya Habari hapa Bungeni. Kwa nini Serikali inaona ugumu wa kuuleta Muswada huu? Lini Muswada huu utaletwa Bungeni ili kuwatendea haki waandishi wa habari ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu sana?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kueleza masikitiko yangu kwamba, Wizara hii yenye majukumu makubwa, mara zote imekuwa ikipewa bajeti isiyotosheleza sekta zote katika Wizara hii; Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, zinahitaji uwekezaji mkubwa ili kupata mafanikio ya maana. Hili ni jambo ambalo Serikali inapaswa kulifikiria sana. Katika michango yangu ya nyuma nimezungumza sana kuhusu utamaduni na mchango wake katika kukuza uzalendo na uchumi.

Serikali ya Tanzania baada ya Uhuru ilitambua hili, ndiyo maana waasisi walineni kuwa utamaduni ni roho ya Taifa. Utamaduni kwa tafsiri ya kawaida hujumuisha vitu vyote vinavyoundwa au kuumbwa na binadamu katika mapambano yake mbalimbali ya maisha. Sanaa (katika upana wake), fasihi, lugha, makumbusho, filamu, muziki, ngoma za kijadi, mila, dini za kijadi na sekta ya vitabu ni sehemu ya utamaduni.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mataifa mengi huwekeza fedha nyingi katika kukuza sekta mbalimbali za utamaduni kujenga Utaifa, kukuza uchumi wa kitamaduni na kueneza utambulisho huo kwenye duru za Kimataifa. Kwa kutambua umuhimu wa kutangaza Utaifa kwenye duru za Kimataifa, Mataifa mbalimbali yameanzisha asasi zinazosimamia utamaduni wao kama vile *British Council* (Uingereza), *Goethe Institute* (Ujerumani), *Alliance Francaise* (Ufaransa), Taasisi ya Confucius (China) na kadhalika.

Tanzania ina fursa nzuri ya kujitangaza Kimataifa kutumia Kiswahili, muziki, fasihi, sanaa, vitabu, utalii wa kitamaduni na kadhalika. Juhudi na uwekezaji zaidi vinahitajika ili mafanikio ya maana yaonekane. Wakati tukisubiri uwekezaji zaidi katika sekta hii, Wizara ifikirie kusaidia yafuatayo:-

Kwanza, kusaidia vyama vinavyokuza vipengele mbalimbali vya utamaduni. (a) Vyama vya Uandishi (UWAVITA). (b) Chama cha Wachapishaji (PATA). (c) Chama cha Washairi (UKUTA). Vyama hivi vina mchango mkubwa katika fasihi na sekta ya vitabu. Ingefaa kuwe na fungu maalumu kwa ajili ya kusaidia vyama hivi na sekta ya vitabu. Ifahamike kwamba, bila Serikali kufanya hivyo itakuwa vigumu kujenga utamaduni wa kusoma na kuandika vitabu vya ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inabeba jukumu la kukuza Kiswahili kupitia BAKITA. Tunaipongeza Serikali kwa kuipatia BAKITA ofisi za uhakika. Kinachohitajika sasa ni kuiwezesha itimize majukumu yake ya kuratibu ukuzaji na uendeshaji wa Kiswahili katika vipengele vyake vyote. Pamoja na mambo mengine, Wizara iiwezeshe BAKITA ifanye yafuatayo:- (a) kuendelea na juhudi za uundaji wa istilahi katika Nyanja za Sayansi na (b) kuchapisha majorida na vitabu na kuvieneza katika vyuo na shule mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, iko rai kwamba, Wakenya wanawapiku Watanzania katika kupata nafasi za kufundisha Kiswahili nje ya nchi. Kama hii ni kweli, basi Wizara kupitia BAKITA na asasi nyingine kama Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu, Dar es Salaam (TATAKI), iliangalie hili na kuanza kuchukua hatua stahiki. Naomba Waziri anifahamishe hatua ambazo Serikali itachukua kusahihisha jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa sana la upungufu wa wakalimani wenye weledi wa kutosha, hasa wafahamu vizuri Kiswahili na lugha nyingine kama Kiingereza, Kifaransa, Kichina na kadhalika. Tatizo hili linafahamika kwa muda mrefu, wakati umefika Wizara kwa kushirikiana na Idara za Lugha (TATAKI) na Idara ya Lugha za Kigeni na Isimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo hili kwa kuanzisha somo la ukalimani linaloweza

Nakala ya Mtando (Online Document)

kufundishwa katika taasisi ya taaluma za Kiswahili. Ingekuwa bora kama ukalimani ungeundiwa Idara kamili katika taasisi hiyo ili lifundishwe kwa mapana zaidi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Watendaji na Wataalamu Wazalendo, wanaofanya kazi katika mazingira magumu ya bajeti finyu. Nashauri kwamba, wataalamu hawa watumie taaluma na uzalendo wao kupitia Sera ya Utamaduni (1997) na kuandaa Muswada wa Sheria itakayosimamia Sekta nzima ya Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na nawatakia kila la heri.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, TBC ni Televition ya Taifa ambayo inatakiwa kuwa ya mfano kwa huduma, vitendea kazi na ubora wa huduma. Vitendea kazi vya TBC vinatia aibu, tukianzia na vilivyoko hapa Bungeni Dodoma. Wafanyakazi wanafanya kazi katika mazingira magumu sana na hali zao za maisha ni duni wakati wanafanya kazi kwenye Shirika kubwa la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ieleze Bunge ni kwa nini Watumishi wa TBC 1 hawajalipwa madai yao ya malimbikizo mbalimbali kwa miaka minne sasa?

Mheshimiwa Spika, watumishi hawa walijaza fomu za kulipwa tangu Februari, 2012 Makao Makuu na wengine hawajajaza mpaka leo. Hata wale waliojaza Serikali imekaa kimya.

Mheshimiwa Spika, tunataka maelezo ya kina ni kwa nini haki zao zimekaliwa na Serikali kwa muda wote huo bila maelezo yoyote?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze mchakato wa Vazi la Taifa umefikia wapi? Ni mwaka wa tano sasa hadithi imekuwa nydingi na Serikali imeahidi kukamilisha zoezi hilo, lakini haitekelezi. Vazi la Taifa ni heshima na fahari kwa Taifa; sjui kama Serikali inatambua hili? Tunataka majibu ya kina kuhusu suala hili muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ieleze sasabu za kuchelewesha kuleta Muswada wa kuangalia haki za Wanahabari. Kuna nini kinafichwa hapa? Serikali haioni umuhimu wa Sheria hii? Serikali haitambui umuhimu wa mhimili wa vyombo vya habari hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, tunapata mashaka hili linafanywa kwa makusudi, kuendelea kubinya haki za Watanzania kwa kuona vyombo vya habari na kufanya kazi zao kwa maelezo ya uongozi wa juu. Hili linawatieni aibu na kila leo mnaleta porojo hapa Bungeni na danadana kama vile Wabunge ni watoto

Nakala ya Mtando (Online Document)

wadogo. Leo tunataka maelezo ni lini Sheria au Muswada huu muhimu utaletwa hapa?

Mheshimiwa Spika, sheria inayompa mamlaka Waziri wa Wizara hii kufungia vyombo vya habari kwa kisingizio yameandika habari za uchochezi ni mbovu na inanyima uhuru wa magazeti. Nani anathibitisha kwamba habari hizo ni za uchochezi? Kwa nini wahariri wa habari hizo wasifkishwe kwenye vyombo vya sharia au mahakamani ili ikithibitika ni kweli wachukuliwe hatua za kisheria?

Mheshimiwa Spika, watoto wana haki ya kucheza kwa ajili ya afya zao, watengewe maeneo ya michezo kuanzia mashulen na kwenye makazi yao. Serikali ilieleze Bunge kwa mwaka 2012/2013 ni maeneo mangapi yametengwa hapa nchini kwa ajili ya watoto kukuza vipaji vyao. Hatua gani imefikiwa kurudisha viwanja vya michezo vilivyo chukuliwa na Taasisi na watu binafsi kwa ajili ya shughuli tofauti.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeeleza mara nyingi hapa Bungeni kuhusu watoto wadogo kutoshirikishwa kwenye filamu na sanaa mbalimbali. Kwa nini bado watoto wanaendelea kushiriki kwenye filamu mbalimbali? Serikali haioni huku ni kuharibu mitazamo ya watoto na hivyo kupoteza ndoto zao za maisha yao ya baadaye?

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu na Katibu Mkuu kwa utumishi uliotukuka wenyе utendaji mzuri kuliko.

Mheshimiwa Spika, shukrani kwa mambo yote yaliyofanywa Dar es Salaam pamoja na kulipa fidia wananchi waliokuwa jirani na mtambo wa umeme wa Ubungo.

Mheshimiwa Spika, maboresho ya umeme yamefanyika kama bajeti iliyopita ilivyo elekeza. Changamoto; Kilwa Energy ni tatizo, iwalipe wale waliofanyiwa uthamini. Walipwe na kama hakuna uwezekano basi wananchi waambiwe.

Mheshimiwa Spika, mradi wa umeme uendao Kimbi mpaka Pemba Mnazi, sasa ufike na kule Kibamba Kibwegele, umefika Kanisani bado upande wa pili uwafikie. Mgogoro uliopo pale hauhusiani na wananchi kupata umeme. Umeme ni huduma, naomba nao wapelekewe.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja asilimia mia.

MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri. Naomba kuishauri Serikali kuelekeza nguvu yake katika sekta ya umeme

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwa wananchi vijiji hasa waishio katika maeneo magumu yasiyo na uwezo wa kiuchumi ili kuwakwamua wananchi waweze kupata uwezo wa kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mfano wa Vijiji vya Tarafa ya Mwambao wa Ziwa Nyasa Wilayani Ludewa na Kyela, ni Vijiji vyenye wananchi maskini kabisa. Naomba wananchi hao walau wangepewa teknolojia ya umeme wa solar ambao ungetumika pia kukaushia samaki na dagaa badala ya usumbufu wa kuni wanaopata hivi sasa. Njia wanazotumia haziwasaidii kabisa kiuchumi na zinachangia uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, shida nyingine ni kutokuwa na Sera ya *renewable energy* ambayo ingewasaidia wawekezaji kuyaanisha maeneo ambayo yanahitahi umeme badala ya kukosa umeme wa Gridi. Nashauri sera hii ya *renewable energy* itoke haraka kwa manufaa na kwa maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Wilaya ya Mbarali, Mbeya Vijiji na Mbozi ni maarufu sana kwa uchimbaji wa marble na yanachimbwa kwa wingi. Tatizo kubwa ni wawekezaji hao kuacha mashimo makubwa yenye sura ya mahandaki. Nashauri, wataalam wa Wizara hii wafuatilie na kuwataka wahusika wayafukie mara moja. Kwa mazingra yetu huo ni uharibifu mkubwa sana. Kama mikataba hiyo haina masharti hayo, basi utaratibu ufanyike ili yawekwe ndani ya mikataba.

Mheshimiwa Spika, Baada ya hayo machache, naunga mkono hoja hii. Nawatachia heri katika utekelezaji wa kazi.

MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu pamoja na wataalamu wote wa Wizara hii kwa kasi nzuri ya kutekeleza majukumu yao ya kusambaza umeme.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kusambaza umeme katika Jimbo la Mpwapwa na maeneo yote yaliyofikiwa mpaka sasa. Naushukuru sana mradi wa REA pamoja na Manager wa TANESCO Mpwapwa, hadi sasa kazi inaridhisha sana. Isipokuwa kuna maeneo ya taasisi, Vituo vya Afya, Makanisa na kadhalika, tunaomba REA II na Manager wa TANESCO Mpwapwa waendlee:-

(i) Chisalu - (Folk Development Centre) Chuo cha maendeleo ya Jamii.

(ii) Mgoma - Kituo cha Afya.

Nakala ya Mtando (Online Document)

- (iii) Chunyu - Sekondari na mradi wa Maji (World Bank).
- (iv) Ng'hambi - Anglican Church na nyumba za wachungaji.
- (v) Mazae -Kituo cha Afya na Shule ya Sekondari ya Wasichana.
- (vi) Mima- Shule ya Sekondari.

Mheshimiwa Spika, hatua hii na juhudhi hii naomba iendelee kumalizia.

Mheshimiwa Spika, eneo la Kiyegesa na Kazania linapakana na Mkoa wa Dodoma, wenzetu wa eneo la Dodoma umeme umefika, lakini sisi kwenye maeneo haya ya Kiyegesa na Kazania yaliyoko mpakani hayajapata umeme bado. Ningombaa kero hii ipungue kabisa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru, nangoja vitendo na kauli ya Waziri, Naibu Waziri, Semeni wananchi wa Jimbo la Mpwapwa wasikie wenyewe.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, Wizara hii inafanya kazi vizuri laiti ingepata fedha za kutosha kila Tanzania angepata umeme. Nawapa hongera Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara iwe makini na uchimbaji wa gesi. Sheria iwe wazi na sera iwe nzuri ili gesi iwe neema kwa Watanzania. Nchi ya Qatar ilikuwa maskini, sasa hivi kwa sababu ya gesi ni nchi tajiri, sana. Gesi isiwe kama mafuta ya Nigeria. Nashauri Serikali iweke mikataba vizuri isiyokuwa na madhara kwa Taifa. Tulifanya makosa katika mikataba ya zamani ya madini, Serikali iwe makini tusirudi huko.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie uwezekano wa kutwaa maeneo ya madini mfano dhahabu ambayo hayana potential gold ili wapewe wachimbaji wadogo kwa mpango maalum, ili nao walipe kodi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ijitahidi kusomesha wataalam wetu (wanafunzi waliomaliza Kidato cha Sita) ili baadaye tupate geologists wa kutosha kuendesha na kusimamia miradi hii ya gesi na mafuta.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya tabia nchi yanazidi kutuathiri kwa sababu ya deforestation ambayo imeshika kasi ili kupata mkaa. Gesi ikisambazwa katika miji mikubwa mfano Dar es Salaam, Arusha, Moshi na kadhalika ukataji miti utapungua, hifadhi za taifa zitanusurika, na nchi itapata mvua ya kutosha. Nashauri iwepo mkakati madhubuti wa kusambaza gesi miji mikubwa mapema iwezekanavyo.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, tunashukuru *ration* ya umeme imekwisha/pungua. Nashauri Serikali iendelee kuweka vyanzo hivi vya umeme vizuri (*maintenance*) na kuendelea kuvumbua vingine ili kuliondolea taifa tabu ya ukosefu wa umeme.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie uwezekano wa kuruhusu private sector kutengeneza umeme mdogo mdogo katika maeneo yao na hatimaye kutumia katika jamii inayowazunguka na ziada kuuziwa TANESCO kwa bei nafuu. Yako maeneo yana mito yenye maji mengi, viko viwanda vya miwa viwe encouraged kutengeneza umeme hata kama Watts ni chache (TPC – Mkoani Kilimanjaro inatengeneza).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Manaibu Waziri, na Katibu Mkuu kwa kazi kubwa wanayoifanya (*tirelessly*).

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri ukurasa 18, Mradi wa North - West Grid KV 400, umeme unatoka Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma hadi Nyakanazi. Na kwamba bilioni 1.0, fedha hizi zinaombwa kwa ajili ya kukamilisha upembusi yakinifu wa mradi unaotarajiwa kukamilika 2016/2017. Kwa mantiki hiyo na kwa muda huu (*time frame*) Naipongeza Wizara, kwa sababu *timeline* hii itawezesha Wizara, Wabunge na wananchi wa Mikoa husika kufanya tathmini na kuangalia kama tunakwenda vizuri au la na ili turekeibishe. Hongera kwa kutuwekea *time frame*.

Mheshimiwa Spika, REA (Mradi wa Umeme Vijiji) unatakiwa upewe pesa zote zinazoombwa. (*REF*) mfuko huu uwezeshwe kwa pesa zote zilizoombwa ili vijiji vyote vya Mkoa wa Rukwa tukianza na Wilaya mpya ya Kalambo ili wananchi wakulima, wafugaji na wavuvi waweze kunufaika na umeme huo kwa kujinulzia uchumi kwani wananchi wa Rukwa kutokana na mazao ya kilimo na uvuvi, wana uwezo wa kuanzisha na kuendeleza viwanda.

Mheshimiwa Spika, REA, umeme vijiji, utasaidia kuwezesha utoaji bora wa huduma hospitalini, vituo vya afya na zahanati, lakini pia katika shule za sekondari huko kuna maabara zinahitaji umeme na kutumika usiku wakati wa *studies*. Pia watu binafsi mmoja mmoja na kwa makundi wanahitaji umeme kwa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Waziri wa Fedha, fedha zote zilizoombwa kwa ajili ya utekelezaji na kumalizia mradi wa North-West Grid, lakini na mradi wa REA katika muda uliopangwa 2016/2017. Rukwa Ruka!!!

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa a130%.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na kuipongeza kazi nzuri ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mbunge Jimbo la Mbogwe, ninatoa shukrani za dhati kwa Wizara ya Nishati na Madini, Shirika la Umeme nchini (TANESCO) na Wakala wa Umeme Vijiji (REA).

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imelitendea haki Jimbo la Mbogwe kwa kutupatia miradi miwili kabambe ya kutandaza umeme Kata kumi na tano kati ya kumi na sita, yaani Ushirika, Mbogwe, Nanda, Nyakafuru, Lugunga, Nghomolwa, Bukandwe, Iponya, Ngemo, Ilolangulu, Isebya, Lutembela, Ikunguigazi, Ikobe na Masumbwe. Kata ya Nyasato pekee ndiyo iliyobaki. Kwa hiyo, naiomba Wizara, TANESCO na REA kuhakikisha Kata hii nayo iwekwe katika utekelezaji wa REA ili kuwepo na ulinganifu katika kupiga hatua kimaendeleo kwa kupata huduma ya umeme kama ilivyo kwa Kata zingine.

Mheshimiwa Spika, Aidha niongeze kuomba kuwa Vijiji vyote katika Kata zote za Wilaya na Jimbo la Mbogwe kwani japo Kata kumi na tano zimepata kuingizwa katika miradi ya Electricity V na REA bado kuna Vijiji vingi vimeachwa nje. Basi Serikali iendelee kuiangalia Wilaya ya Mbogwe kwa jicho la pekee kwani ni Wilaya mpya na ilikuwa haijawahi kupata huduma ya umeme tangu nchi ipate uhuru.

Mheshimiwa Spika, sekta ndogo ya madini inazo changamoto kubwa katika Jimbo la Mbogwe ambako kuna madini ya dhahabu katika maeneo ya Nyakafuru, Bukandwe, Lugunga na Msumbwe (Shenda).

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ione uwezekano wa kuwatengea maeneo wachimbaji wadogo wadogo ili waweze kuendesha shughuli za uchimbaji ili kuepusha migogoro baina ya wachimbaji wadogo wadogo na watafiti kwa ajili ya uwekezaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika naunga mkono hoja.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, aidha, niipongeze Wizara kwa kuendelea kutekeleza miradi ya umeme kupitia miradi ya REA na Electricity V jimboni na wilayani Sengerema.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara na taasisi zake, naiomba Wizara kupitia REA itekeleze miradi ya umeme katika vijiji vifuatavyo vilivyoko Jimbo la Sengerema:- Kaningu, Nyasigu, Lubungo, Nyabila, Isome, Ikoni, Lugongo, Lukumbi, Kafundikile, Bungonya na Nkumba shule ya msingi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mungu kwa kutujalia uzima na kutuwezesha kukutana mahali hapa, pia nami niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini ya mwaka 2014/2015.

Vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalamu wake kwa kuandaa bajeti nzuri yenye mikakati ya kumaliza matatizo ya nishati ya umeme, madini hapa nchini pamoja na matatizo yaliyopo katika taasisi zake zote zilizopo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa Mwenyezi Mungu ametujalia nchi yenye utajiri mkubwa wa rasilimali za asili, ametujalia ardh kubwa yenye rutuba, madini ya aina mbalimbali, misitu na mbuga za wanyama wa kila aina, hali ya hewa nzuri, Bahari, Maziwa makubwa, Mito mingi, watu wengi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, rasilimali hizi, kwa tabia yake inatakiwa zitumiwe vizuri kuboresha hali na maisha ya Watanzania wote sawia na kwa miaka mingi na hata milele. Vinginevyo rasilimali hizi zinaweza kugeuka kuwa chanzo cha mifarakanano, magomvi na mauaji, zinaweza kuwa balaa na kuleta maanganizi nchini badala ya kuwa baraka na neema.

Mheshimiwa Spika, ipo mifano ya nchi mbalimbali duniani zilizojikuta zina migogoro na vita vyatanya wenyewe kwa wenyewe kutokana na kugombania utajiri wa rasilimali za asili. Watu wa nchi hizo wanajuta kuwa na rasilimali ambazo zimekuwa chanzo cha kuhatarisha amani, utulivu, usalama na hata uhai wao. Kwa hapa Tanzania tunashukuru Mungu rasilimali hazijageuka kuwa balaa na tunaomba hilo lisitokee.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, tangu Tanganyika ipate Uhuru na Zanzibar kufanya Mapinduzi Matakatifu na hatimaye nchi zetu mbili kuungana na kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali za awamu zote zimesimamia kwa makini rasilimali za nchi yetu ili ziwanufaishe Watanzania wote. Tumetunga sheria na sera mbalimbali kuhakikisha kuwa lengo hilo linatimia. Hata hivyo, usimamizi wa sheria hizo na utekelezaji wa sera zetu nzuri umekuwa unakabiliwa na changamoto mbalimbali kwa nyakati mbalimbali. Mpaka hapa tulipofika ni umahiri wa viongozi wetu ndiyo uliotuwezesha kuzuia mambo yasiharibike na kugeuka kuwa matatizo makubwa. Tumefanikiwa kiasi chake ingawaje hatujaweza kuzuia kabisa matatizo yasitokee hapa na pale. Taarifa za kugombea rasilimali zimekuwa zinasikika na nyingine zikiwa zimesababisha watu kupoteza maisha, kujeruhiwa na mali kuharibiwa.

Tufanye nini kukomesha hali hiyo isijitokeze? Ni jambo ambalo sisi kama Taifa, yaani Serikali, wanainchi na wadau mbalimbali wakiwemo viongozi wa dini hatuna budi kulizungumza na kulipatia ufumbuzi. Mwaka 1980 ikatungwa sheria ya utafutaji wa uzalishaji wa mafuta kwa nia ya kuweka masharti na utaratibu wa makampuni kushiriki katika utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi nchini. Pia unatoa mwongozo wa mgawanyo wa mapato baina ya makampuni na Serikali.

Sheria hiyo imeendelea kufanyiwa maboresho kwa nyakati mbalimbali kulingana na mahitaji ya wakati husika. Kuanzia mwaka 2007 shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia ziliongezeka kwa nguvu na kasi kubwa. Juhudi hizo zilizaa matunda mwaka 2010 kwa uvumbuzi wa kwanza wa gesi katika Bahari kuu uliofanywa na kampuni za *Orphir* na *British Gas*. Baada ya hapo ugunduzi umeendelea hadi kufikia futi za ujazo trilioni 46.5 za rasilimali ya gesi nchini mpaka sasa. Utafiti unaendelea na matumizi ya kupata gesi zaidi yapo.

Kufuatia ugunduzi huo, Tanzania sasa ni moja ya nchi zinazohesabiwa kuwa na gesi nyingi duniani na nchi inayovutia wawekezaji wengi katika sekta ya gesi. Kwa sababu hiyo, tukaamua kufanyia mapitio Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji wa Mafuta na Gesi. Mwaka 2013 tumetunga Sera ya Gesi na kurekebisha masharti ya mkataba wa kugawana mapato yatokanayo na gesi (*Production Sharing Agreement*) na kuongeza mgao wa Serikali. Sera ya Gesi Asilia iliyopitishwa mwezi Oktoba, mwaka jana (2013) imeeleza wazi tena kwa lugha nyepesi kuwa gesi ya Tanzania ni mali ya Watanzania wote na itatumika kwa manufaa ya Watanzania wote wa kizazi hiki na kijacho.

Katika matumizi ya gesi, kipaumbele kitakuwa matumizi ya ndani. Msingi wa sera hii ni ule ukweli kwamba ukiuza nje gesi yote unapata mapato peke yake, lakini unakosa faida nyinginezo. Ukiitumia ndani unapata mapato na faida nyingine nyingi, kwa mfano, uzalishaji wa umeme, matumizi ya majumbani

Nakala ya Mtando (Online Document)

kwenye magari na viwandani kuzalisha bidhaa mbalimbali. Hivyo basi mnapoitumia ndani gesi inakuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo ya nchi yetu. Vilevile Serikali ipo katika mchakato wa kuandaa sera ya kuwashirikisha zaidi Watanzania (*Local Content Policy*) ili wanufaikie zaidi na rasilimali yao ya gesi ambayo ni rasilimali adimu hapa duniani.

Mheshimiwa Spika, ukiachia mbali vijana wapatao ishirini (20) ambaao Serikali imewapeleka katika nchi za Uchina na Brazili ili kupata elimu ya gasi na mafuta, ila Taifa letu bado tunahitaji wataalamu wengi katika fani za mafuta na gesi, si chini ya wataalamu 200. Pia Tanzania tunahitaji wataalamu wa masuala ya uchumi wa mafuta, gesi na wahasibu wa sekta hiyo, ni lazima tukubaliane kuwekeza katika elimu ili tupate wataalamu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto mbalimbali zinazokabili Wizara; changamoto kuu katika Wizara ya Nishati na Madini ni kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika na kuendeleza sekta ndogo ya gesi. Changamoto nydingine zilizopo ni kuendeleza vyanzo mbadala vya nishati ya umeme badala ya kutegemea maji, ambayo uzoefu unaonesha wakati wa kiangazi uzalishaji umeme unapungua kutohana na kina cha maji kupungua. Changamoto nydingine ni kuongeza uwezo endelevu wa sekta ya gesi na kuwekeza katika miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme na kudhibiti upotevu wa umeme wakati wa kuusafirisha na kuutumia.

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu ya Nishati na Madini ni mionganini mwa Wizara zilizopo katika Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now - BRN*) katika sekta ya nishati. Ili kuutekeleza ipasavyo tunahitaji wataalamu wazalendo waliobobeza katika fani za mafuta na gesi. Kuna hofu ya kupoteza soko kwa makampuni ya kigeni yanayozalisha umeme dhidi ya makampuni ya Kitanzania. imetajwa kuwa chanzo cha vita dhidi ya kampuni yaufuaji umeme ya *Independent Power Tanzania Limited (IPTL)* kwa zaidi ya muongo mmoja, Kampuni za Kigeni zimekuwa zikipata faida kubwa kwa kuzalisha umeme na kuuza kwa bei ya juu Nchini. Kampuni ya IPTL ambayo inamilikiwa na kampuni ya Kizalendo, Pan African Power Solutions Tanzania Limited (PAP) ilishtua dunia mwishoni mwa mwaka jana pale ilipotangaza dhamira yake ya kushusha bei zake kutoka senti za Kimarekani 26 na 30 ya sasa mpaka senti za Kimarekani sita (6) na nane (8) kwa kila *unit*, pale itakapobadilisha mitambo yake kuweza kutumia gesi badala ya mafuta, katika hali hiyo ni lazima ushtuke kwani ni punguzo kubwa sana kutokea katika biashara yoyote.

Kwa sasa, makampuni mengine katika soko yanatoza kati ya senti za Kimarekani 38 na 60 kwa kila *unit*. "Watanzania wasidanganywe na taarifa zilizotolewa na baadhi ya vyombo vya habari kuwa IPTL ilinunuliwa na PAP bila

Nakala ya Mtando (Online Document)

kufuata sheria. Kuna kampuni ya kupakana matope kwa tamaa ya kuzalisha umeme Watanzania kutokana na biashara hii kuwa na faida kubwa katika sekta hii muhimu kiuchumi. Aidha kampuni ya PAP katika taarifa yake kwa vyombo vya habari iliyotolewa Jijini Dar es Salaam, imesema kuwa kampuni imeshtushwa na baadhi ya wawekezaji katika sekta hiyo pamoja na wanasiasa kuanzisha vita dhidi yao mara baada ya kutangaza kupunguza gharama za umeme.

Uongozi wa kampuni hiyo umesema kuwa Watanzania watafurahia gharama hizo za chini baada ya utekelezaji wa mkakati wao wa utatuzi na ubadilishaji wa mfumo wa mitambo yao ambayo utaongeza uwezo wa uzalishaji wa umeme kutoka mega wati 100 za sasa mpaka mega wati 500. Inasemekana kuwa kampuni hiyo IPTL/PAP imekuwa ikikumbana na changamoto ambazo zinajaribu kuzorotesha jitihada za uongozi mpya za kuleta mabadiliko ambayo yataapelekea kampuni hiyo kuanza kuzalisha umeme wenye gharama nafuu kwa Watanzania wote. Lakini taarifa hiyo imetolewa baada ya machapisho mbalimbali ya vyombo vya habari yanayoishutumu kampuni hiyo kutoa hongo kwa wajumbe wa kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kulinda matakwa yao au kuwalinda dhidi ya tuhuma mbalimbali wanazo husishwa nazo.

Nanukuu sehemu fupi ya taarifa ya kampuni hiyo ikisema (Tukiwa kama kampuni ya ufuaji umeme, tunaelewa faida za kiuchumi zitokanazo na umeme wa gharama nafuu kwa mteja mmoja mmoja na kwa maendeleo ya kiuchumi ya Nchi nzima. Kwa sababu hiyo ndiyo maana sasa tumeelekeza jitihada zetu katika kuona ni jinsi gani ya kuzalisha umeme wa gharama nafuu ambao utasaidia kuleta mabadiliko ya kiuchumi ya nchi hii, pasipo kuingia malumbano ambayo yataturudisha nyuma na kushindwa kutekeleza lengo letu la kuwekeza vilivyo katika sekta hii muhimu," ilisomeka taarifa hiyo).

Mheshimiwa Spika, Nishati ya gesi ipunguzwe kuepusha janga. Hali ya uhifadhi wa misitu Nchini imeteteleka. Maelfu ya ekari za misitu yanateketea kila mwaka kutokana na shughuli za kibinadamu. Hivi sasa kuna hatari kubwa ya wazi ya kukabiliwa na jangwa katika miaka michache ijayo. Na tishio hili siyo la kufikirika, ni matokeo ya taarifa za kitaalamu kwa mujibu wa Wakala wa huduma za misitu Tanzania (TFS), ekari 400,000 za misitu huteketezwa kila mwaka kwa sababu tu ya ukataji miti ovyo kwa ajili ya matumizi ya Nishati ya mkaa, katika taarifa iliyoripotiwa, TFS walisema kuwa miongoni mwa ekari za misitu zinazoteketezwa kwa mwaka nusu yake kwa maana ya ekari 200,000 hutokana na athari za matumizi ya mkaa katika Jiji la Dar es Salaam peke yake. Imeelekezwa zaidi kuwa kiasi hicho cha misitu inayoangamizwa kutokana na mkaa unaotumika Dar es Salaam peke yake ni sawa na roho ya misitu yote inayoteketezwa Nchi nzima kwa mwaka, kwa hesabu za haraka hii maana yake

Nakala ya Mtando (Online Document)

ni kwamba kwa nchi nzima ekari 800,000 za misitu huangamizwa kutokana na mkaa na vyanzo vingine mbalimbali.

Kwenye mapendekezo yao, TFS walisema kuwa ni vyema bei ya gesi ikashushwa zaidi kuliko iliyopo sasa ili kuwapa fursa wananchi wengi zaidi kutumia Nishati hiyo kwa ajili ya kupikia badala ya mkaa ambaa madhara yake ni pamoja na hayo ya kukaribisha jangwa. Mimi naungana na TFS kwa asilimia mia moja, tukiamini kwamba hakuna njia nyingine ya mkato katika kupunguza uharibifu huu mkubwa wa mazingira kwa njia ya mkaa isipokuwa ni kwa kuandaa mazingira mazuri ya matumizi ya nishati mbadala kama gesi, umeme utokao katika gridi ya Taifa na jua. Hakuna ubishi hata kidogo kuwa matumizi ya mkaa siyo rafiki kwa mazingira.

Miti mingi hukatwa, tena bila kujali kasi ya upandaji wa miti mingine ili kuziba pengo linalochwa. Uzoefu unaonyesha kuwa wadau wa biashara ya mkaa, kwa maana ya wachomaji, wasafirishaji, wauzaji wa jumla na reja reja na hata watumiaji huwa hawana nafasi hata kidogo ya kutekeleza kivitendo kauli mbiu ya "kata mti panda mti." Bali kinachoonekana ni kushamiri kwa biashara hiyo yenye kuingiza fedha nyingi kwa baadhi ya watu. Watumiaji pia huridhishwa na namna mkaa unavyoivisha vyema vyakula vyao na pia kufanikisha matumizi mengine mbalimbali ya nishati hiyo. Kwa mwenendo huu, na kwa takwimu zilizotolewa na TFS, naona kuwa ni wazi kwamba sasa ni wakati muafaka kwa Serikali kuingilia kati jambo hili.

Baadhi ya maeneo ya nchi yatabaki kuwa jangwa kama TFS wanavyobashiri, mimi naamini kwamba njia mojawapo nzuri ya kupunguza athari hizi mbaya zitokanazo na matumizi ya mkaa ni kwa wataalamu wa Wizara inayoshughulikia mazingira, Wizara ya Fedha na Wizara ya Nishati na Madini kuketi pamoja na kuangalia ni kwa namna gani wanaweza kupunguza zaidi għarama kubwa za kununua vifaa vinavyowezesha kutumia gesi na nishati nyingine badala ya mkaa. Hivi sasa watumiaji wa nishati ya gesi, umeme na jua ni wachache sana kulinganisha na wale wanaotegemea mkaa. Bei ya umeme imekuwa ikipandishwa kila uchao, bei ya vifaa vya umeme jua pia iko juu sana na wananchi wengi hushindwa kumudu.

Għarama za mitungi ya gesi, majjiko ya gesi na gesi yenyewe ni mtihani mwiegħine mkubwa kwa wananchi wa kawaida ambaa ndio waliokuwa wengi na ndio wanaotumia nishati hiyo mbadala ya mkaa ambayo ina madhara makubwa kwa Taifa letu baadaye. Binafsi natambua kuwa hata sasa, Serikali imefanya maamuzi kadhaa ya kupunguza ġħarama za gesi. Hata hivyo, nadhani kwamba jitihada hiso hazitoshi kwani bei ya nishati hiyo bado iko juu na wananchi wengi wanashindwa kuimudu. Kwa mfano, katika maeneo mengi jijini Dar es Salaam, mtungi wa gesi wa kilo sita huuzwa kwa bei ya kuanzia Sh.

Nakala ya Mtando (Online Document)

55,000/= na bei ya gesi ya ujazo wa mtungi wa aina hiyo huwa ni kati ya Sh. 23,500/= na 26,000/= kulingana na mahala inakouzwa kwa maana nyingine, mtu anayeamua kugeukia gesi badala ya mkaa, akitumia mtungi huo mdogo wa kilo sita hutakiwa awe na fedha za kuanzia walau Sh 80,000/= hapo achilia mbali jiko lenyewe, kiwashio na vifaa vingine katika mazingira kama haya, ni wazi kwamba matumizi ya gesi yatabaki kuwa ndoto kwa wananchi wengi wa kipato cha chini. Na kwa sababu watu hao hawawezi pia kumudu ghamra za nishati ya umeme katika kupikia, ni wazi kuwa mkaa unabaki kimbilio la wengi.

Njia pekee nzuri na nyepesi ya kuiepushia nchi jangwa kwa kulinda misitu yetu ni kubuni mikakati endelevu ya kupunguza bei ya nishati mbadala kama ya gesi na vifaa vyake na pia kuuelimisha umma juu ya faida za kutumia nishati hiyo ili wapunguze matumizi ya mkaa. Harakati za kupunguza ghamra za gesi zianze sasa kabla ya nchi haijageuka kuwa jangwa kama tunavyojionea katika nchi za jirani.

Mheshimiwa Spika, tunataka sheria mpya kuondoa usiri katika utoaji wa leseni za mafuta na gesi. Mswada huu wa gesi unapaswa kueleza bayana jukumu la maofisa wa Serikali katika majadiliano na haki na wajibu wa wawekezaji na Serikali pale mkataba unapokubaliwa. Sheria zilizopo, Sheria ya Ugunduzi wa Petroleamu na uzalishaji ya mwaka 1980 inajumuisha lugha tata na kukosa mwongozo ya kina kwa uingiaji zabuni na mkakati ambayo itahakikisha uwazi na uwajibikaji. Serikali tayari imeshatoa leseni 26 za ugunduzi na uzalishaji chini ya sheria zilizopo, ambazo zimeiweka Serikali katika uchunguzi mkali. Hatua ya 4 inayokuja ya utoaji leseni katika Bahari karibu na ufukweni nchini Tanzania imepingwa na wanasiwa na baadhi ya wataalamu wa viwanda kwa sababu inaegemea katika sheria ya mwaka 1980 kunadi majengo tisa yaliyo Baharini kwenye kina kirefu mkabala na majengo yanayotarajiwa kuidhinishwa.

Napenda kutoa wito kwa Serikali kusimamisha utoaji leseni kwa makampuni binafsi hadi sheria mpyaitakapowekwa. Ukiangalia kwa mapana nchi haijajiandaa kwa upanuzi wa shughuli za ugunduzi kwa kuwa Serikali inakosa taasisi na sera kutoa mwongozo na kudhibiti mapato kutoka katika sekta hiyo. “ kuendelea na hatua nyingine mpya ya utoaji leseni kabla ya sera kukamilika ni kutowajibika.

Serikali inapaswa kutekeleza usitishaji wa muda wa miaka 10 wa utoaji wa leseni na uzalishaji ili kutoa fursa kwa nchi kutengeneza sera madhubuti na taasisi kusimamia tasnia hii na kuweza kuwajibika kudhibiti mapato ya fedha. Sheria zilizopo sasa zinasababisha upotevu mkubwa na rushwa katika usimamizi wa futi za mraba trilioni 43 za maeneo ya gesi ambayo yamedunduliwa nchini

Nakala ya Mtando (Online Document)

Tanzania, yeye thamani ya shilingi za Tanzania trillioni 675 (Dola za Marekani billion 430), isipokuwa sera mpya zitakapowekwa.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa awali wa kijiolojia ulifanyika kwa mara ya kwanza mwaka 1988 katika eneo la Kata ya Mbesa Wilayani Tunduru Mkoani Ruvuma umebaini kuwepo kwa madini mengi aina ya shaba ya bluu (*Bluue copper*). Madini yeye thamani kubwa aina ya shaba ya bluu (*Bluue copper*) yamegundulika katika Kata ya Mbesa Tarafa ya Nalasi Wilayani Tunduru Mkoani Ruvuma. Kugundulika kwa madini hayo kunaifanya Wilaya ya Tunduru kuwa ndiyo Wilaya pekee nchini na Afrika Mashariki na kati kuwa na madini ya shaba ya bluu. Utafiti unaonyesha kuwa Tarafa nzima ya Nalasi ina utajiri wa madini hayo ambayo yanaweza kuchangia kuinua uchumi wa Wilaya hiyo, Mkoa wa Ruvuma na Taifa kwa ujumla wake “utafiti umebaini kuwepo kwa madini ya shaba ya bluu karibu Tarafa nzima ya Nalasi hadi Mto Ruvuma mpakani na Nchi jirani ya Msumbiji na pia madini hayo yamesambaa hadi mpakani na Wilaya ya Namtumbo hii ni shaba yeye thaman kubwa” Wataalamu wa madini wanaelekeza kuwa madini ya shaba ya bluu yana thamani kuzidi madini ya shaba aina nyingine zote ikiwemo shaba nyekundu ambayo inachimbwa katika nchi jirani ya Zambia.

Hivi sasa wachimbaji wadogo wadogo wa madini hayo wapo katika eneo hilo la madini tangu mwaka 2010 na kwamba utafiti kuhusiana na madini hayo bado unaendelea kabla ya Serikali kupitia Wizara ya nishati na madini kuanzisha rasmi mgodi wa madini hayo. Utafiti huo ulifanywa na wakala wa jiolojia Tanzania (GST) umeonyesha kuwepo kwa madini aina ya shaba ya bluu ambapo utafiti wa karibuni umebaini ubora wa mashapo ya shaba ya bluu katika eneo hilo. Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya nishati na madini, utafiti umebaini kuwa madini ya shaba ya bluu yanaweza kuchimbwa kwa faida kubwa na kwamba hatua hii ya utafutaji madini inahitaji utaalam, vifaa vya kisasa na fedha nyingi. Aidha naiomba Serikali iendelee kuimarisha STAMICO ili iweze kuwa na uwezo wa kufanya shughuli hizo za utafutaji na uchimbaji madini kwa maslahi ya Taifa badala ya kutegemea zaidi kampuni binafsi. Hata hivyo Serikali Wilayani Tunduru imetoa maelekezo kwa kampuni ya IGA & MWAKI CO. LTD ambayo inafanya shughuli za uchimbaji wa madini hayo katika kijiji cha Mbesa Wilayani humo kukamilisha taratibu za kisheria ili iweze kufanya kazi zake pasipo shaka kwani vitendo vya kuendesha uchimbaji huo vinafanyika bila kuwa na vibali vya utafutaji wa madini. Utaratibu uliokiukwa na wamiliki wa mgodi huo kampuni ya IGA & MWAKI CO.LTD imekuwa ikiendesha shughuli hizo bila kufanya tathimini za athari kwa mazingira (*Environment Impact Assessment*) pamoja na kutokuwa na mikataba ya kisheria kati ya kampuni na kijiji cha Mbesa ambacho ndiyo mmiliki wa eneo linalochimbwa madini hayo. Taratibu nyingine ambazo zimekiukwa na kampuni hiyo kuwa ni pamoja na kutowapatia wachimbaji wao vifaa vya kujikinga na madhara mbalimbali (*Protective gears*)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

yatokanayo na uchimbaji madini hayo hali ambayo inahatarisha afya zao. Ifahamike kwamba kutokana na kampuni yeyote kutotimiza vigezo hivyo inakiuka kanuni zinazo simamia sheria ya mazingira namba 20 ya mwaka 2004 ya uendeshaji wa shughuli za migodi hiyo naiomba Serikali kuwataka viongozi wa kampuni kuwasiliana na ofisi za idara ya mazingira ya Halmashauri na ofisi za Baraza la mazingira la Taifa kanda ya Mtwara inayosimamia mazingira ili kukamilisha taratibu hizo. Mkoa wa Ruvuma ni mionganoni mwa Mkoa nchini ambayo ina utajiri mkubwa wa madini mbalimbali ambayo yakichimbwa kwa vifaa vya kisasa yanaweza kuufanya Mkoa kupanda juu kiuchumi na wananchi wake wakaondokana na umasikini.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya sera za kiuchumi yaliyofanyika miaka ya 1990 na sera ya madini ya mwaka 1997 yaliweka vivutio vya uwekezaji kwenye sekta ya madini na kuharakisha ukuaji wake. Matokeo ya uwekezaji huo ni kuanzishwa kwa migodi saba mikubwa ya dhahabu iliyoanzishwa kati ya mwaka 1998 na 2009. Migodi hiyo ni:- *Golden Pride* uliopo Nzega, Geita uliopo Geita, Bulyanhulu uliopo Kahama, North Mara uliopo Tarime, Buhemba uliopo Musoma vijijini, Tulawaka uliopo Biharamulo na Buzwagi uliopo Kahama, Mrabaha mi tozo inayotozwa na kulipwa Serikalini kwa makampuni yote yanayozalisha na kuuza madini kabla ya kusafirisha madini hayo. Viwango vya mrabaha (Sheria ya madini ya mwaka 2010)

- Vito, almasi na urani – 5%
- Vito iliyokatwa na kusanifiwa – 1%
- Chumvi na madini ya ujenzi 3%
- Madini mengine ikiwemo dhahabu – 4%

Kuna manufaa yatokanayo na uchimbaji huo, kwa mfano kuanzia mwaka 1999 hadi 2010 kiasi cha TZS 341,567.259,805 kililipwa Serikalini na migodi mikubwa kama mrabaha, pia wamiliki wa migodi mikubwa wanatakiwa kulipa kodi mbalimbali kama kodi ya mapato, kodi ya zuio (WHT) kodi kwenye mishahara (PAYE), ushuru wa stempu, kodi ya kuendeleza ufundi stadi (SDL) ushuru wa barabara na ushuru wa forodha. Pia kuna manufaa yatokanayo na uchimbaji kutokana na shughuli za uchimbaji zinazoendelea nchini zimepatia Tanzania manufaa makubwa ya kiteknolojia (*technoligytransfer*), manufaa ya kiteknolojia yaliyopatikana nipamoja na kukuza ujuzi wa waajiri wazawa kwa kiwango cha Kimataifa katika ujuzi wa kijiolojia, Uhandisi, uchimbaji na ujenzi wa migodi. Kueneza teknolojia rahisi ya kuchenjua makapi/marejeo ya udogo madini na kuongeza mapato na ajira. Pia Tanzania imefaidika na teknolojia ya kutumia vifaa vya usalama migodini (PPE) pamoja na mbini/njia muafaka za kutunza mazingira katika maeneo ya uchimbaji. Kwa kuwepo vifaa vya kisasa vya uchimbaji kumechochea uzalishaji wa vifaa vya aina hiyo hapa nchini. Hizo ni baadhi ya faida zitokanazo na uchimbaji wa madini hapa nchini kwetu ingawa kuna malalamiko mengi

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, mionganini mwa malalamiko ya wananchi ni pamoja na hali inayoonekana ya sekta ya madini kutochangia vya kutosha katika maendeleo ya nchi hasa ya kiuchumi na kijamii. Pia imeonekana kuwa mikataba ya madini inapendelea zaidi makampuni makubwa ya uwekezaji katika madini, huku kukiwepo na usiri mkubwa wa mikataba hiyo. Katika siku za karibuni, malalamiko makubwa zaidi yamekuwa juu ya mfumo wa kodi ambapo kumekuwa na hisia kuwa kampuni za madini hazilipi kodi kiasi cha kutosha, huku kampuni zote zinazojishughulisha na uchimbaji wa dhahabu na almasi zikidai hazijapata mapato yanayostahili kulipa kodi. Aidha kumekuwa na lawama kuhusiana na wananchi waliohamishwa kutoka maeneo yao ya asili ili kupitsha uchimbaji mkubwa kutolipwa fidia ya ardhi zao. Pia wananchi wanaotoka Wilaya zenye migodi wanalamika kutopota sehemu ya mrahaba licha ya maisha yao kuathiriwa na shughuli za uchimbaji wa madini katika maeneo yao.

Baadhi ya kero za wananchi ni pamoja na zile za mazingira ambapo inasemekana kuwa mazingira yanaharibiwa sana. Vilevile wafanyakazi wa Kitanzania katika migodi wanalamika athari za kifaya wanazopata na ujira mdogo kulinganisha na wafanyakazi wageni. Baadhi ya wananchi wanalamika udhaifu katika usimamizi wa sekta yakiwemo masuala ya usafirishaji wa mchanga wa dhahabu nje ya Nchi, kuchenjuliwa na kutotolewa kwa taarifa sahihi za gharama za uwekezaji na uzalishaji.

Vilevile kumekuapo malalamiko makubwa ya wananchi kwamba viongozi wao wanafaidika binafsi kutoka kwa wawekezaji, zikiwemo tuhuma za rushwa katika mikataba. Madini yanayoweza kupatikana nchini Tanzania yamegawanyika katika makundi matano: kundi la jamii ya madini ya metali linalojumuisha dhahabu, chuma, nikeli, shaba, kobalti na fedha, kundi la jamii ya vito linalojumuisha almasi, tanzanite, yakuti, garnets na lulu, kundi la jamii la madini ya viwandani linalojumuisha chokaa, magadi soda, jasi, chumvi na fosfeti, madini yanayozalisha nishati kama makaa ya mawe na uranium, na madini ya ujenzi kama vile kokoto, mchanga na madini kwa ajili ya terezo. Mchanganuo wa hazina ya madini iliyothibitishwa nchini ni kama ifuatavyo:-

AINA YA MADINI

- Dhahabu
- Nikeli
- Shaba
- Chuma (Iron ore)
- Almasi
- Tanzanite
- Limestone

KIASI

- | |
|--------------------|
| Tani 2,222 |
| Tani million 209 |
| Tani million 13.65 |
| Tani million 103.0 |
| Tani million 50.9 |
| Tani 12.60 |
| Tani million 313.0 |

Nakala ya Mtando (Online Document)

· Magadi soda	Tani million 109
· Jasi (gypsum)	Tani million 3.0
· Fosfeti (Phosphate)	Tani million 577.04
· Makaa ya mawe	Tani million 911.0

Ila kutokana na utajiri tuliokuwa nao ambao tumepewa na Mungu kuna uwezekano tukawa na aina nyingine nyingi tofauti za madini hapa nchini kwetu, pamoja na kuweka hazina hii kubwa, mchango wa sekta hii katika uchumi wa Taifa na maendeleo ya jamii unaonekana kutokidhi matarajio ya wananchi ikilinganishwa na sekta nyingine za uchumi, wananchi wamekuwa wakilalamika sana jinsi mikataba inavyosainiwa mfano, kati ya mwaka 1994 – 2007 mikataba ya madini sita imesainiwa, yote ikiwa ni ya migodi mikubwa ya dhahabu. Migodi hiyo na mikataba ni:-

Bulyanhulu uliosainiwa tarehe 5 Agosti, 1994, Golden Pride ulioko Nzega uliosainiwa tarehe 25 Juni, 1997, Geita Gold Mine uliopo Geita uliosainiwa tarehe 24 Juni, 1999, North Mara uliopo Tarime uliosainiwa tarehe 24 Juni, 1999, tulawaka uliopo Biharamulo uliosainiwa tarehe 29 Desemba 2003, Buzwagi uliopo Kahama uliosainiwa tarehe 17 Februari, 2007. Tatizo linakuja kwamba kwa mujibu wa kifungu cha 10 (1) cha sheria ya madini, Waziri mwenye dhamana ya madini ndiye mwenye mamlaka ya kuingia katika mkataba wa uendelezaji wa mgodi na mwekezaji kwa niaba ya Serikali, hali hii ndio imekuwa ikituingiza katika mikataba mibovu ambayo hatunufaiki nayo sisi kama Taifa lenye rasilimali kubwa hapa Duniani.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya malalamiko yamekuwa yakitolewa na wachimbaji wadogo ikiwemo kunyang'anywa maeneo yao na wachimbaji wakubwa kwa msaada wa Serikali kwa kutumia vyombo vyatoka vya dola kama vile polisi. Maeneo madogo wanayopewa yanakuwa na matatizo ya kuchimba bila kuingiliana kwa mfano Mirerani ambako eneo walilotengewa wachimbaji wadogo ni mita 50x50 ukilinganisha na kitalu C. Walilopewa wachimbaji wakubwa. Vilevile wachimbaji wadogo wamejikuta wakifanya kazi katika mazingira ya hatari na yasiyo salama ikiwemo kutobozana na ajali za mara kwa mara kama zinavyotokea maeneo mbalimbali hapa nchini kwetu. Vilevile inapotokea wachimbaji wadogo wametoboa mgodi wa mwekezaji mkubwa wamekuwa wakipigwa, kuteswa kwa kuumwa na mbwa, kumwagiwa maji na hata kupigwa risasi na mchimbaji mkubwa.

Wachimbaji wadogo wamelelemika kuwa Serikali haiwajali kwa kutowawekea mazingira ya kupata mitaji, ushauri wa kitaalamu, na masoko ya mazao yao. Na hawapati misamaha ya kodi kama ilivyo kwa kampuni za uchimbaji mkubwa, wachimbaji wadogo wangkuwa wanapewa kipaumbele ili kuwawezesha waweze kukua kimitaji na kufanya uchimbaji wa kisasa, pia

Nakala ya Mtando (Online Document)

naishauri Serikali kutotoza kodi kwa vitu vinavyoagizwa kutoka nje na wachimbaji wadogo ili kuwarahisishia waweze kuchimba kisasa.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuzungumzia hali ya Jimboni kwangu Kibaha vijijini. Tunakabiliwa na tatizo la kukosa nishati hii muhimu ya umeme maeneo mengi na hivyo kufanya shughuli nyingi za kimaendeleo kurudi nyuma pamoja na uchumi wa mtu mmoja mmoja kuzidi kushuka siku hadi siku, kwani wananchi wanashindwa kufanya shughuli zao ambazo zingewaletea maendeleo ya haraka kwa kupata umeme tu.

Maendeleo hufuatana na umeme, hivyo kukosa umeme hali inazidi kuwa mbaya. Katika ziara ya Mheshimiwa Rais Jimbo la Kibaha vijijini alipokuja pia nae alituhakikishia miradi yetu ya umeme itakamilika, katika ziara hiyo aliambatana na Mheshimiwa Waziri nae pia kwa mapenzi makubwa na wana Kibaha vijijini alituhakikishia kuwa miradi yote itakamilika kwa awamu na hivyo kuniahidi mimi kuwa Januari mwaka huu ningezindua kwa kuweka jiwe la msingi mradi wa umeme Chalinze Magindu, ila mpaka leo hii ahadi hiyo bado haijatekelezeka na ikizingatiwa ahadi hiyo ilitolewa mbele ya wananchi, hivyo basi wananchi nao pia wanasubiri ahadi hiyo ya uwekwaji wa jiwe la msingi katika mradi huo. Tuna miradi ya umeme ambayo bado haijatekelezeka ya Ruvu, Magindu, Chalinze, Kwala Dutumi, Kikongo Ruvu Station, Mwanabwito, Vikuge, Msufini, Boko Mpiji, Mlandizi, Kibwende, Janga, Ngeta, miradi hii ya umeme ikikamilika itakuwa na faida kubwa kwa wakazi wa Kibaha vijijini kwani wana muda mrefu sana wakisubiri umeme, suala la umeme kwao limekuwa kama ni ndoto kwao. Sasa naomba kujua miradi hii itakamilika lini, vilevile naomba miradi hii ipewe kipaumbele katika bajeti ya mwaka huu. Kupelekwa umeme katika maeneo hayo niliyoyataja hapo awali kutasaidia kuleta maendeleo ya haraka na kupandisha uchumi wa wakazi wa Jimbo la Kibaha vijijini.

Mheshimiwa Spika, kauli iliyotolewa na Tanesco kuwa wanataka kuanzisha kampeni maalumu ya ukusanyaji wa madeni, ikiwemo kuwakatia umeme watakaoshindwa kulipa. Njia hizi kwangu naona kama danganya toto na kuzidi kulea kidonda ambacho baadaye kitakuja kuwa saratani na kukosa matibabu yake, jambo ambalo sitaki tufike huko, sababu zinazosabaisha nione kama kauli za TANESCO ni danganya toto, ni kutangaza kubeba mzigo wa madeni sugu ya Serikali na taasisi zake pamoja na kampuni bninagsi, kwani si jambo geni, kuwa na madeni na yamekuwa yakitajwa humu Bungeni na waheshimiwa Wabunge tangu mwaka 2011, 2012 na 2013. Kama kweli Mkurugenzi alikuwa na nia ya kukisafisha chombo hiki alitakiwa kutangaza hatua alizochukua badala ya kuendelea kuzunguka katika eneo ambalo limeshazungumzwa na inashangaza kuona jambo hilo la muda mrefu sasa ndiyo analitolea tangazo kwa wadaiwa.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Jambo linalonisababisha nipaye wakati mgumu wa kuamini kama kweli watendaji wa chombo hiki watawashughulikia wadeni sugu wote ni kutokana na kukataa kwake kutaja majina ya wadeni sugu, hivyo naamini kunaweza kukafanyika ukiritimba katika ulipaji wake, mwakani tena watajikuta wakiwaelezea wananchi kuhusu hizo hizo sababu ya kutajwa hadharani wadaiwa sugu wa muda mrefu inasaidia wananchi kuwafahamu na hapo baadaye kuja kuhoji hatua iliyofikiwa iwapo kama taasisi hizo zitaonekana zikiendelea kutumia umeme wakati wakiwa hawajalipa madeni yao.

Sifahamu sababu ya shirika hilo lililo chini ya Wizara hii kukaa kimya na kuwaficha wadeni sugu, ikiwamo kushindwa kuwadai na kusababisha mzigo mkubwa kuwaangukia wananchi na walipa kodi amba ni walalahoi, wanaoishi chini ya dola moja kwa siku bila huruma. Kwani mabadiliko ya muundo, mfumo wa shirika hilo unapaswa kuchukuliwa na mamlaka nyininge ikiwemo Wizara ya Nishati na Madini na ofisi ya Rais. Nimeshangazwa hivi karibuni kusikia kuwa bei ya umeme inaweza kushuka baada ya kuwepo kwa ongezeko la matumizi ya gesi kutoka zaidi ya asilimia 42 ya sasa, kauli ambayo naiona haina ukweli wowote. Kama kweli kauli hii haichezi na akili za Watanzania kwanini wakati TANESCO inaomba kupandisha bei ya umeme kutokana na kulemewa na madeni hakutoa mwongozo kwa shirika hilo kudai madeni ambayo yangeweza kufidia huo wa bei ya umeme? Kwa mtazamo wangu, kama Serikali inawapenda wananchi, ihakikishe inaondoa sheria ya kuwabana wafanyabiashara wenyewe uwezo wa kuendesha biashara ya umeme ili waweze kutoa huduma ya ushindani.

Hilo likifanyika itasaidia watu wengi kupata huduma bora na kwa bei nafuu zaidi ya ilivyo sasa, hata kama tukiwezesha gesi, maji umeme hali itaendelea kuwa hivyo hivyo. Jambo la msingi ni kuachia biashara hiyo kuwa huria kama Serikali ilivyo fanya kwa shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) na kuwawezesha Watanzania kupiga simu hata kwa mkopo, hivyo naamini iwapo wakiruhusu mashirika binafsi kufanya nao ushindani upo uwezekano wa kupata umeme kwa bei nafuu na itakuwa changamoto kwa wafanyakazi wa TANESCO kuwa na nidhamu kama TTCL kwa sasa baada ya kuwepo kwa makampuni mengi ya kutoa huduma za simu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Nakala ya Mtando (Online Document)

SPIKA: Sasa nitamuita mmoja wa watoa hoja, wana dakika sabini na tano, wamegawana Waziri dakika 45 na Naibu Waziri dakika 30, Mheshimiwa Naibu!

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA UTAMADUNI NA MICHEZO:

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataallah, kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kunituea kuwa Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, naomba niwashukuru Mheshimiwa Waziri, Dkt. Fenella Mukangara, Katibu Mkuu wa Wizara, Bibi Sihaba Nkinga, Naibu Katibu Mkuu Profesa Elisante Ole-Gabriel, Wakurugenzi wa Idara zote za Wizara, Wakuu wa vitengo na Taasisi zote chini ya Wizara kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa tangu nimeingia katika Wizara hii. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimshukuru Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda, Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii na vilevile nimshukuru Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, maarufu Mr. Sugu, ambaye ni Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Vilevile niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mazungumzo au kwa maandishi. Naamini wote hao michango yao ina lengo la kuboresha utendaji wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuwashudumia Watanzania kujitafutia maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, naomba uniruhusu nimshukuru pia mke wangu Bi. Amina na wanangu wawili Kassim na Hassan, kwa uvumiliivu wao. Niwashukuru pia wapiga kura wangu wa Jimbo la Kondoa Kusini katika Wilaya ya Chemba kwa ushirikiano wanaonipa kwa kazi hii ambayo nimekabidhiwa na Mheshimiwa Rais, naamini tutaendelea kushirikiana kwa maendeleo na mstakabali wa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, yamezunguza mambo mengi, niende moja kwa moja kwenye hoja kwa sababu muda wenyewe ni mdogo. Waheshimiwa walioandika na walichangia kwa kuzungumza hapa Bungeni, wamezungumza sana kuhusu suala la ukiukwaji wa maadili ya taaluma ya Uandishi wa Habari, maslahi duni kwa Wanahabari, bima ya tahadhari na kukithiri kwa Waandishi wa Habari ambao siyo Waandishi wa Habari hasa katika tasnia ya habari.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Muswada wa Kusimamia Vyombo vyatya Habari, ndiyo utakaokuwa suluhisho la haya yote tuyoyazungumza. Kwanza, Muswada huu utazingatia kwa kiasi kikubwa hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu uanzishwaji wa Bodi huru ya kusimamia vyombo vyatya habari itakayokuwa na wajibu kuangalia masuala yote ya ukiukwaji wa maadili ya taaluma ya uandishi wa habari, maslahi duni katika vyombo vyatya habari na kukithiri kwa Waandishi wa Habari ambao kwa hakika wengi wao si Waandishi wa Habari na kwa kutambua kila mwana taaluma ya habari na kufuatilia maudhui ya vyombo vyatya habari, siyo hilo tu, pia hata mazingira ambayo Waandishi wa Habari wanafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyotolewa ni kuhusu Waandishi wa Habari kuzingatia matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili. Serikali inakubaliana na maoni ya Kamati kuwa tatizo lipo. Katika kutatua tatizo hilo, Baraza la Kiswahili la Taifa, tayari limeendesha vipindi vyatya radio na televisheni kuhusu matumizi fasaha ya lugha ya Kiswahili. Aidha, kama mkakati wa muda mrefu, BAKITA inaandaa programu ya mafunzo ya muda mfupi, kwa makundi yenye uhitaji maalum wa ufasaha wa Kiwahil, ikiwa ni pamoja na Waandishi wa Habari wenyewe. Vilevile Serikali inawahimiza Waandishi wa Habari kujenga utamaduni wa kutumia Kamusi za Kiswahili zilipo kwa sababu tunaamini ni bora na wataimarisha Kiswahili chao.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni suala la kuhimiza Wasanii kuwa wabunifu na kujituma zaidi katika kazi zao. Kwa hakika Serikali inatambua na inakubaliana na maoni ya Kamati, umuhimu wa wasanii kuwa wabunifu, kufanya kazi zao kwa kujituma na kuwa na ragbha ya kuijendeleza kielimu. Aidha, Wizara inawahimiza Wasanii kuzingatia maadili katika utendaji wa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limejitokeza, ni kuhusu Makampuni ya Simu kutumia miito ya simu ya nyimbo za Wasanii bila makubaliano baina yao. Wizara inakubaliana na ushauri wa Kamati na tayari Wizara kupitia Kamati ya Urasimishaji inayoundwa na Bodi ya Filamu, BASATA, COSOTA na TRA, imeshakutana na wataalam na asasi zenye ujuzi wa kudhibiti usambazaji na uuzaji wa kazi za Wasanii wa Filamu na Muziki kwa kutumia Tehama. Upembuzi wa kisheria umeshaanza kufanyika, ukamilishaji asasi zenye ujuzi wa kazi hii zitapewa vibali vyatya usambazaji kwa njia zilizo wazi na halali ili kulinda pato la wanamuziki na wenyewe waone kweli kazi wanayoifanya inawaletea tija wao na familia zao.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kuhusu timu ya kandanda ya Tanzania, Taifa Stars, amezungumza Mheshimiwa Martha Mlata, nampongeza sana kwa kazi nzuri anayoifanya kufuatilia maendeleo ya timu yetu ya Taifa ya

Nakala ya Mtando (Online Document)

Tanzania. Pia umezungumzia suala la ubadilishwaji wa jezi pamoja na jina kama ilivyoripotiwa na TFF. Wakati mwingine maelezo ambayo tulipata mapema kutoka TFF kwamba jezi ambayo tulikuwa tukiitumia mwanzo, unapokwenda kwenye picha za televisheni, inaonekana *blue* zaidi, kwa hiyo *back ground* ya picha inakuwa na matatizo. Nadhani ndiyo maana TFF wanajaribu kuangalia ni namna gani wapate jezi ambayo itakuwa bora zaidi kwenye picha za televisheni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ubadilishwaji wa jina la Taifa ya Tanzania, sisi kwa upande wa Serikali tunawaagiza TFF kwamba waache jambo hilo mara moja. Hakuna ya kubadilisha jina kikubwa zaidi ni kubadilisha mchezo wenyewe ili twende sambamba na dunia ya sasa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni suala la BMT. Amezungumza Mheshimiwa Aden Rage kwamba BMT imepitwa na wakati, ni kweli kwamba inawezekana sheria ile lakini kinachofanyika pale wala si kubadilisha bali ni kufanya marekebisho kidogo tu katika Sheria ya BMT ili iweze kwenda sambamba na hali halisi ya sasa.

Mheshimiwa Spika, hoja ambayo kwa kweli imechukua mjadala mkubwa sana, ni suala la kucheleweshwa kuletwa hapa Bungeni Muswada wa Sheria ya Haki ya Kupata Habari. Mimi ni mdau wa habari na ningependa sana kuona Waandishi wa Habari wanafanya kazi kwenye mazingira mazuri, Waandishi wa Habari wananyonywa na hasa kwenye vyombo vya habari vya binafsi, ni kama wanatumikishwa tu, wengine wanacheleweshewa kulipwa mishahara kwa sababu mikataba yao haieleweki. Mimi naamini sheria hii itakapokuja, itatengeneza mazingira ambayo yatawasaidia Waandishi wa Habari kuheshimika katika Taifa lao na hata nje ya Taifa lao. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, niombe tu Waheshimiwa Wabunge tuwe na subira kwani Muswada wa sheria hii unakuja lakini hauwezi kuja tu ni lazima tufanye utafiti na utafiti umesrafanyika kwenye nchi za Afrika Kusini wanao-practice, India na mimi mwenyewe nilikwenda India na Mheshimiwa Mngodo na Wajumbe wengine wa Kamati wakati ule, Uingereza na tumejifunza wenzetu wanaendeshaje jambo hili. Unapofanya utafiti unakuwa na uhakika kwamba usiige tu jambo lakini ni vizuri ukalifanya utafiti ili unapokwenda kulianzisha liwe na tija zaidi na jambo hili limesrafanyika hivyo tuwe na subira.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyokuja ni hatua ya Serikali kuvifungia baadhi ya vyombo vya habari. Ni kweli Serikali ilitoa adhabu ya kuyafungia Magazeti ya Mwananchi Tanzania Limited siku 14 na Gazeti la Mtanzania kwa siku 90 kwa kuchapisha habari za uchochezi ikiwemo kuchapisha taarifa zinazoichonganisha Serikali na waumini wa dini ya Kiislam kwa kuoanisha picha

Nakala ya Mtando (Online Document)

ya mbwa na Ibada ya Kiislam huku Mhariri akijua fika kabisa kwamba mbwa ni najisi kwa mujibu wa dini ya Kiislam. Chombo cha habari makini kama gazeti la Mwananchi na Mkurugenzi wake Mkuu makini, Bwana Tido Mhando, walitakiwa kuwa wa kwanza kubaini unyeti wa Ibada ya Kiislam na mbwa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, gazeti la Mtanzania lilikiri kufanya makosa ya kitaaluma ambayo Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kwa bahati mbaya ameyatetea lakini simlaumu inawezekana ni *typing error*. Njia pekee itakayotusaidia kuondokana na vitu kama hivi ni huu Muswada wa Huduma ya Vyombo vya Habari (*Media Service Law*). (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni tuhuma za dharau dhidi ya wanahabari. Awali ya yote, napenda kutambua kazi nzuri inayofanywa na vyombo vya habari. Natambua umuhimu mkubwa sana wa Media Council of Tanzania (MCT), natambua umuhimu mkubwa wa Jukwaa la Wahariri, wanafanya kazi nzuri sana na sisi kwa upande wa Serikali tunaendelea kushirikiana nao ili taaluma ya habari iwe na mashiko kuliko ilivyo sasa. Pia ni imani yangu kwamba taaluma, weledi na maadili ya Uandishi wa Habari ndiyo tija pekee kwa Mwandishi wa Habari. Nachukua fursa hii, kama ambavyo nimeendelea kusema kwamba nchi hii ni yetu sote, ikitokea machafuko watakaoumia ni pamoja na Wanahabari wenyewe na vyombo vyao, Serikali haitavumilia kuona vyombo vya habari vyenye nia ya kuleta uchochezi katika Taifa letu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nieleze masikitiko yangu kwamba Serikali pamoja na kuwa wavumilivu katika masuala mengi ya kiuchochodzi bado wenzetu wameendelea kutukana matusi ya nguoni na kudai uhuru wa vyombo vya habari usio na wajibu wala staha kwa watu binafsi na nchi yetu. Mimi binafsi kama Juma sijawahi kudharau na sitegemei kudharau na wala kufanya hivyo, hata kuota ndoto tu ya kudharau vyombo vya habari. Ni vema ikaeleweka kwamba dhana ya vyombo vya habari kuwa mhimili wa nne kivuli hauhalalishi vyombo ya habari kwenda kinyume na miiko ya uandishi wa habari. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni uwekezaji duni katika miundombinu ya michezo, viwanja vya CCM kurejeshwa Serikalini, mchezo wa Taifa Stars na Zimbabwe kuhamishwa Dar es Salaam baada ya kutoka Mbeya, soka kupewa kipaumbele kuliko michezo mingine.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada zake za kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo kulingana na uwezo wake. Kwa sasa kipaumbele katika kuendeleza eneo la Changamani na Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya tunatilia mkazo.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la viwanja vya CCM, kimsingi wenye mamlaka ni CCM wenyewe, wanaweza kulizungumzia suala hili kwa sababu wao ndiyo wamiliki. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuhamishwa kwa mchezo kutoka Mbeya, alipokuja Musonye kama Kamisaa wa FIFA alipokwenda kukagua uwanja wa Sokoine Mbeya alikuta kuna upungufu kwa usalama wa wachezaji, usalama wa mashabiki na usalama wa waamuzi. Hili limetokea si Mbeya tu, michezo mingi imewahi kuhamishwa, siyo Tanzania tu bali duniani kote, angalieni kumbukumbu mtajua.

Mheshimiwa Spika, ajira kwa Makocha wa kigeni, kuvunja moyo wa Makocha wazalendo, maendeleo ya mchezo wa riadha, BMT kuondoa ukame wa medali Jumuia ya Madola, Makocha, mchezaji Aston Mbugi kuachwa kwenye kambi ya mazoezi na fedha za RT na TOC kukaguliwa.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba si Tanzania peke yake ambapo makocha wa kigeni wanakuja kufundisha soka ama michezo mingine. Kocha wa timu ya Taifa ya Japan wa sasa hivi wanaokwenda kwenye kombe la dunia anatoka Italia. Sven Goran Eriksson alikuwa kocha wa timu ya taifa ya Uingereza akitoka Sweden. Tunachosisitiza sisi kwa upande wa Serikali ni kuhakikisha kwamba makocha hawa wageni wanapokuja wanatoa mafunzo kwa makocha wazalendo ili watakapoondoka ujuzi ule ubaki hapa nyumbani. Hilo ni jambo ambalo tumekuwa tukilisisitiza na tumekuwa tukiwaeleza vizuri sana TFF na wao naamini wanazingatia jambo hili na wasipozingatia tutafuutilia. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni ya Mheshimiwa Christowaja juu ya kuutambulisha utamaduni wa Mtanzania. Niseme tu kwamba Wizara kwa kweli imekuwa ikielimisha jamii kupitia semina mbalimbali, makongamano na mkutano mkuu wa sekta ya utamaduni kuhusu umuhimu wa kulinda na kuendeleza utamaduni wa Taifa ikiwemo ngoma za asili, hivyo kuheshimu na kuthamini mila na desturi za kitanzania. Hata hivyo, suala la kuheshimu na kuzingatia mila na desturi mbalimbali ni mtambuka na linagusa sekta mbalimbali kama vile Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na jamii kwa ujumla. Sera ya Utamaduni inasisitiza kwamba malezi yanaanza ngazi ya kaya, hivyo nasisitiza wazazi au walezi kuwalea vijana wao katika kuheshimu, kukuza na kuenzi mila na desturi nzuri za taifa letu.

Mheshimiwa Spika, suala la mmomonyoko wa maadili pia limezungumzwa sana na Waheshimiwa AnnaMallac, Mheshimiwa Seleman Jafo, Mheshimiwa Neema Hamid Mgaya, Mheshimiwa Magdalena Sakaya na

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Rebecca Mngodo. Katika kudhibiti suala la mmomonyoko wa maadili si suala la Wizara peke yake bali ni suala la Taifa zima. Sisi kwa upande wa Serikali tumeendelea kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuva mavazi yenye staha na pia kuzuia ngoma zinazozingatia maadili ya Tanzania kama vile kigodoro na khanga moja, ndembendembe laki si pesa, wanaokaidi na kukiuka maagizo haya tunawachukulia hatua. Suala la maadili kama nilivyosema ni mtambuka, linagusa kila mwanajamii. Kwa hiyo, Wizara inasisitiza kwamba malezi yanaanza ngazi ya kaya kama nilivyosema na sisi Waheshimiwa Wabunge ni wajibu wetu tutoe mchango wetu ili kuhakikisha kwamba jamii yetu inakuwa katika maadili mema.

Mheshimiwa Spika, kwa nini wasanii hawatambulishi majina ya filamu zao kwa lugha ya taifa ya Kiswahili? Mimi naamini Wasanii wanafanya hivyo kwa kiwango kikubwa sana na nichukue fursa hii kuwapongeza sana watu ambao wanashiriki katika kuhakikisha kwamba wanatambulisha sanaa ya Tanzania. Yapo matatizo, kuna pirates wengi lakini sisi kwa upande wa Serikali tushirikiane na wadau hawa. Ndugu Alex Msama anafanya kazi nzuri na nachukua nafasi hii kumpongeza, watu wa STEPS wanafanya kazi nzuri sana lakini upo umuhimu tukae chini watu wa COSOTA, TRA na produces ili tuone mustakabali mzima wa filamu ya Tanzania inakoelekea.

Mheshimiwa Spika, leo si ajabu unaweza kupanda basi kutoka Bukoba mpaka Dar es Salaam unangalia filamu ndani ya basi, ukifika Dar es Salaam unapouziwa ile filamu huwezi kununua kwa sababu tayari umeshaiona lakini je, huyu aliyeitoa ile filamu anafaidika? Ukienda nchi nyingine mfano Marekani, Mswahili anaweza akaja akanunua CD moja tu hapa lakini akienda kule ana *duplicate*, kila ukienda nyumba ya Mswahili unaangalia filamu ya Tanzania lakini je, huyu mwanafilamu wa Tanzania amefaidika? Ni vitu ambavyo lazima tukae chini sasa tuangalie ni namna gani tunaweza ku-sort out problem hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali kusaidia vyama mbalimbali vinavyochangia katika maeneo ya Kiswahili mfano Chama cha Waandishi wa Vitabu (UWAVITA), Chama cha Wachapishaji (PATA), Chama cha Ushairi Tanzania (UKUTA) na kadhalika. Serikali inatambua umuhimu wa kusaidia vyama hivyo na Wizara iko tayari kusaidia vyama hivyo pale tu bajeti itakaporuhusu. Hoja hii ameitoa sana Prof. Kulikoyela Kahigi, naye ni mtaalam wa Kiswahili na amekuwa akitoa mchango mkubwa sana kwenye ukuzaji wa Kiswahili na juzi amesema anasaidia wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambapo na mimi bahati nzuri nasoma kule, nakupongeza sana Mzee wangu, *keep it up!* (Makofii)

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Wizara inaelewa umuhimu wa Kiswahili na imekuwa ikiwezesha BAKITA kwa mfano kutimiza jukumu hilo kutegemeana na uwezo wake wa kibajeti.

Mheshimiwa Spika, ufundishaji wa Kiswahili nje ya nchi. Serikali kupitia BAKITA ambayo ndiyo asasi inayoratibu ustawishaji wa Kiswahili nchini imeendelea kukuza maendeleo ya Kiswahili kwa ujumla kupitia Waandishi wa Sarafu, uchapishaji wa Kamusi mbalimbali, kutoa ithibati ya vitabu vya Kiswahili, tafsiri na ukalimanu, uanzishwaji wa kozi za umahiri na uzamivu katika ngazi za elimu ya juu na elimu ya ujumla kupitia vyombo habari, utengenezaji wa filamu za Kiswahili na kadhalika kimataifa na Wizara kwa kweli tumekuwa tukishiriki katika kuanzisha Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ambapo matarajio ni Kamisheni kuanza rasmi katika mwaka wa fedha 2014/2015. Vilevile, vimeanzishwa vituo na idara za ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika nchi za nje. Mathalani, kituo cha Kiswahili cha Addis Ababa - Ethiopia, idara za Kiswahili katika vyuo vikuu vya Namibia, Zimbabwe, Kwazulu Natal, Chuo Kikuu cha Sebha Libya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Kiswahili kiuzwe kimataifa, amezungumza Mheshimiwa Rebecca Mgodo na mimi nikupongeze Mheshimiwa unafuatilia kwa ukaribu sana suala la ukuzaji wa Kiswahili. (Makof)

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba suala la kukuza Kiswahili nje ya mipaka ya Tanzania linafanyika na hoja hii imekuwa ikisemwasemwa sana ndani ya Bunge kwamba inawezekana pengine wenzetu nchi jirani wanafaidika zaidi na wataalam wao wa Kiswahili nje kuliko sisi Tanzania, wakatoa mfano labda vyombo vya habari. Mimi niseme tu kwamba leo ukienda BBC, Mkuu wa Idhaa ya Kiswahili Mzanzibar, Ally Sahele, Mtanzania. Karibu nusu ya wafanyakazi pale ni Watanzania, lazima tujisifu. Ukienda Deutsche Welle, Mkuu wa Idhaa ile ni Mkomoro mwenye asili ya Zanzibar. Ukienda Voice of America, Mwamoyo Hamza ni Mdigo wa Tanga, ndiyo Mkuu wa Idhaa ya Kiswahili, Mkenya pale ni Esther Githui Ewart peke yake lakini wengine wote ni Watanzania. Vipo vyuo vikuu mbalimbali duniani ambapo Watanzania wanafanya kazi. Kazi yetu sisi ni kujaribu kuhimiza tu ili Watanzania waendelee kutumia fursa hizo, siyo kazi ya Serikali kuwatafutia kazi, sisi kazi yetu ni kutafuta fursa ili inapotokea lazima wataalam wetu wachacharike. (Makof)

Mheshimiwa Spika, ulinzi wa haki na maslahi ya wasanii, amezungumza Mheshimiwa Catherine Magige na Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa. Kama nilivyosema kwamba haki na maslahi ya wasanii vinalindwa na Sheria Na.7 ya mwaka 1999 ya Hakimiliki na Hakishiriki, Sheria Na.4 ya Filamu na Michezo ya Kuigiza ya mwaka 1976 na Sheria Na.23 ya Baraza la Sanaa la Taifa 1984

Nakala ya Mtando (Online Document)

ambapo Wizara inasilitiza wasanii kusajili kazi zao ili ziweze kulindwa na sheria hizi. Hata hivyo, nasisitiza wasanii wawe walini wa kwanza wa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, labda niende sasa kwenye suala la hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge wengine hasa kuhusu usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania TBC. Wengi wamelizungumzia jambo hili kwa mfano Mbunge wa Manyoni, Mheshimiwa Joseph Selasini na Waheshimiwa Wabunge wengine. Serikali ingependa kuona TBC inasikika nchi nzima bila kelele wala mikwaruzo. Kwa upande wa Serikali tunajaribu kutafuta namna gani ambavyo TBC iwezeshwe kifedha ili iweze kufanya kazi zake vizuri na kuwa na mashine za kisasa pamoja na mitambo ambayo itafanya kazi ya kuhakikisha kwamba TBC inaboreka.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi TBC kwa sheria ya TCRA, unapokuwa na mtambo wa FM wa 2kilowatts, coverage yake haiwezi kuwa kubwa tofauti na mtambo wa 5kilowatts, ile radius. Kwa mfano, ukienda Bukoba, mtambo uliopo pale wa kilowatts 5, ni vigumu sana kufika Ngara, kwanza umepigwa radi nydingi sana. Kwa hiyo, ile radius coverage yake na sote ni lazima tufahamu kwamba mitambo ya FM usafiri wake ni tofauti na mitambo ya MW, kwamba hii ya FM inakwenda flat inapokuja mlima inapita juu ya mlima lakini hii mitambo mingine ambayo tumekuwa tukiitumia zamani, mitambo hii inakwenda undulating, kwa hiyo, ni rahisi kufika maeneo yote lakini juhudini zinafanyika kuhakikisha kwamba TBC inafika katika maeneo yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu hiki ndiyo chombo chetu cha umma. Njombe kwa Mheshimiwa Spika nako kuna matatizo amezungumza Mheshimiwa Pindi Chana pia. Tayari TBC imeshapeleka mwakilishi Mkoani Njombe, kama report Njombe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika ufurahi na wewe ukifika nyumbani muite pale ajue uko Njombe. Vilevile TBC imempatia vifaa vyote mwakilishi aliyepo Njombe, camera na computer yaani laptop.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Wilaya ya Manyoni wanashindwa kupata matangazo ya TBC. Kama nilivyosema, TBC inafahamu tatizo la usikivu na sisi sote tungependa TBC ifike Tanzania nzima. Hata hivyo, kutohana na ufinyu wa bajeti TBC pia wanashindwa kukamilisha baadhi ya vitu ambavyo vingesaidia kusikika Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba hivi sasa mafundi wa TBC wako katika kazi ya ukarabati wa mtambo uliopo Mndemu, Mkoani Dodoma ambao ulipata hitilifu hivyo kuathiri usikivu katika eneo kubwa la nchi ikiwemo Wilaya ya Manyoni. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge wa Manyoni mtambo ukikamilika wakati wowote matangazo hayo yatarejea kama kawaida.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, tatizo hilo halipo Manyoni tu lakini pia liko hata hapa Dodoma, Singida na baadhi ya maeneo ya Mikoa ya jirani kutokana na hitilafu ya mtambo wa Mndemu. Kwa hakika tu Serikali itaendelea kujenga mitambo mipy ya redio katika Wilaya mbalimbali nchini kama Mkinga, ameshanieleza Mheshimiwa Mbunge na sisi tunazungumza na watu wa TBC.

Mheshimiwa Spika, hoja nyine ni kukamilika kwa jengo la TBC Mikocheni kupitia mkopo wa NSSF ambao udhamini wake umekwama Serikalini, kutokamilika kwa jengo hilo ni fedheha kwa Taifa. Wizara imeielekeza TBC kukutana na uongozi wa NSSF na mimi nina imani kwamba kwa busara, hekima, weledi na uelewa wa Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Dkt. Ramadhani Dau jambo hili litafikia tamati. Ninaamini hivyo na sisi kwa upande wa Serikali tutaendelea ku-push. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumewaomba TBC kwa upande mwingine kwamba TBC wana viwanja maeneo yote ya Tanzania, watafute namna gani watu wawekeza ama ni makampuni ili wapate fedha nyine ambazo zitasaidia kuendesha TBC. Kuendesha redio na televisheni ni gharama kubwa sana. Umeme ni gharama kubwa na mimi naamini TBC kama watafanya *investment* katika viwanja walivyonyavyo *its absolutely kwamba tatizo hili linaweza kuwa limepungua kwa kiwango kikubwa sana.*

Mheshimiwa Spika, suala la vyombo vyaya habari kuwa na wakalimani wa lugha ya alama. Ni kweli wakati wa Bunge la Katiba walikuwepo wakalimani walitoka Zanzibar walisaidia sana. Mimi niseme tu kwamba tutahakikisha wakalimani wa alama wanatafutwa haraka iwezekanavyo. Kwa bahati nzuri leo nimezungumza na watu wa Lushoto kwenye Chuo cha Kulola, nadhani na wao walikuwa wanasiliza hoja za Wabunge, wako tayari kutoa wakalimani kwa ajili ya TBC. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimalizie hoja ya timu ya Taifa ya Tanzania kupelekwa nje kupata mafunzo. Kila inapowezekana Wizara itafanya jitihada za kutafuta fursa za kwenda kwenye mafunzo timu ya Taifa ya soka na timu nyine kama ilivyo sasa kwamba wanamichezo wanaojiandaa na michezo ya Commonwealth wako nje wanafanya mazoezi na hawafanyi mazoezi kwa ajili ya michezo ya Commonwealth tu bali tunawajengea uwezo ili michezo mingine kwa mfano ya Olympic itakapokuja waweze kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la kukaguliwa kwa fedha za RT na TOC. Wizara inaendelea na jitihada za kuendeleza michezo kama nilivyosema na sisi tunaomba kwamba, vyama hivyo vikaguliwe ili tuwe na majibu sahihi. (Makofi)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ismail Aden Rage, nimeshajibu hoja yake kwamba, Sheria za BMT zimepitwa na wakati. Hili suala la Manispaa ya Temeke kupata mapato kutohana na Uwanja wa Taifa kuwa pale kama alivyosema Mheshimiwa Mtemvu, tutalifutilia kwa watu wa TFF tujue hali inakwendaje, kwamba, kuna Uwanja wa Uhuru na Uwanja wa Taifa pale kwa nini Manispaa ya Temeke haipati mapato.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya mchezo wa riadha na juhudi za kukuza na kuendeleza vipaji vya michezo na uwekezaji kwenye michezo, niseme tu Serikali inafanya juhudi kubwa sana za kufufua uendelezaji wa vipaji vya michezo sambamba na urejeshaji wa mashindano ya michezo ya UMITASHUMTA na UMISETA. Hili ni jambo ambalo tunalifanya vizuri sana. Mheshimiwa Akunaay amezungumzia suala hilohilo. Pia Waheshimiwa Sabreena Sungura, Murtaza Mangungu, Rebecca Mngodo, Betty Machangu halikadhalika Mheshimiwa Faida Bakari wamezungumzia kwa kina sana juu ya suala hili.

Mheshimiwa Spika, sasa kuhusu suala la fedha za FIFA na uanachama wa ZDFA ndani ya FIFA. FIFA ina-deal na sovereign state, hakuna sovereign country. Kwenye International Laws, hakuna sovereign country, kuna sovereign state. Sasa sovereign state ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini watu wa TFF wamefanya juhudi kuhakikisha kwamba Zanzibar inaingia kuwa Mwanachama wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF). Mheshimiwa Ngwali analifahamu hili na imeshiriki mara tatu mfululizo sasa katika michezo hii ya CAF, kwa bahati mbaya hakuna timu hata moja iliyovuka round ya kwanza. Tuombe Mungu katika siku zijazo pengine Zanzibar nao, mimi kama Juma nitafurahi tu wakiingia FIFA lakini kama nilivyosema FIFA wana-deal na sovereign states. (Makof)

Mheshimiwa Spika, suala la fedha za FIFA, nenda Uwanja wa Gombani-Pemba, mradi uliokarabati ule uwanja kuweka ile pitch ni fedha ya FIFA. Kwa hiyo, FIFA wanatoa fedha kulingana na project locations ambazo zinakuja kwa kila nchi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Juma Ngwali, naomba hilo alielewe vizuri sana. Hata hivyo, TFF na ZDFA wana uhusiano mzuri sana, wanashirikiana na inapokuja kwenye mikutano mbalimbali wanakwenda pamoja. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwanza kwa kumshukuru sana Mwenyekiti wa BMT, anafanya kazi nzuri sana, Ndugu Dioniz Malinzi, Rais wa TFF Ndugu Jamal Malinzi, wanafanya kazi nzuri sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

Nakala ya Mtando (Online Document)

SPIKA: Nafikiri ni kengele yako ya pili hiyo!

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:
Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (Makofii)

SPIKA: Kabla sijamuita mto hoja, naomba niwasomee Kanuni, maana wengine wanafikiri huwa tunasema maneno tu. Kanuni ya 99(14) inasema hivi, bila ya kuathiri masharti ya Kanuni ya 154, ambayo inasema kama Spika akimpongeza ama akitoa pole kwa upande wa Bunge wengine wasifanye hivyo. Upande wa Serikali kama Kiongozi Mkuu wa Serikali akisema wengine wasifanye hivyo. Hivyohivyo, kama Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ametoa pongezi au pole ya rambirambi wengine wasifanye hivyo, hiyo ndiyo Kanuni ya 154. Sasa hii ya 99(14) inasema bila kuathiri maneno ya Kanuni ya 154 ni kwamba maneno yoyote ya utangulizi, utambulisho, salamu za pole, pongezi au shukrani pamoja na kutaja majina ya Wabunge waliochangia hoja havitarhusiwa kwa Mbunge au Waziri wakati wa kujadili hotuba ya Bajeti. Kwa hiyo, siyo kwamba ni hiari, ni Kanuni na ilikuwa na sababu. Sizungumzii wewe Nkamia, nazungumzia watakaofuata. (Kicheko/Makofii)

Mheshimiwa mto hoja, una dakika 45.

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha tena kusimama hapa siku hii nikiwa na afya njema.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao ambayo ilijikita katika ushauri, maelekezo na maswali yaliyolenga kupata ufanuzi mbalimbali kwa maslahi na ustawi wa wananchi lakini pia kuhusiana na hotuba ya bajeti na makadirio ya matumizi ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, jumla ya wachangiaji walikuwa ni 51, wachangiaji 39 walichangia kwa maandishi na 12 kwa kuzungumza. Orodha ya majina ya Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia ipo na ninaomba iingizwe katika Hansard.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Saidi Mtanda, Mbunge wa Jimbo la Mchinga na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii. Niwashukuru kwa ushirikiano mkubwa walioutoa kwa Wizara yangu kwa kipindi chote cha mwaka wa fedha 2013/2014 wakati Wizara ikitekeleza majukumu yake. Naishukuru hasa Kamati kwa maelekezo mbalimbali

Nakala ya Mtando (Online Document)

waliyoyatoa yenyе lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara na hivyo kuleta mafanikio yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niihakikishie Kamati na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kuwa, maoni, mapendekezo na michango yote iliyotolewa tutaizingatia na kuifanya kazi kadri ya uwezo wetu kama Wizara kwa kushirikiana na wananchi na wadau wetu mbalimbali wa maendeleo kwa kuwa mambo mengi yaliyojadiliwa hapa ni mtambuka.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake na mchango wake kutoka Kambi ya Upinzani. Niseme tu kwamba yale yenyе tija tutayatumia kuboresha utendaji kazi katika sekta ninazozismamia. Hata hivyo, niombe tu kwamba Mheshimiwa Mbilinyi asione haya kusifia kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ikiwemo msukumo wa makusudi wa kuwafikia wananchi kwa malengo chanya. Hili tunalifanya kwa kutumia vyombo vy'a habari na waandishi wa habari kama kiungo muhimu cha kuwafikia wananchi kwa maendeleo yao na ya nchi kwa ujumla. Kwa ufupi Serikali haina ugomvi na vyombo vy'a habari. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali katika taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani na wakati Waheshimiwa Wabunge wakichangia, zimejitokeza hoja mbalimbali zikihitaji ufanuzi lakini pia Waheshimiwa wengine walitoa ushauri, maelekezo na mapendekezo.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii nianze kwanza kwa kujibu baadhi ya hoja kwa ujumla wake hususan zile zilizogusiwa na wachangiaji wengi ikiwemo Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii na Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, hoja kubwa iliyobebwa hasa na Kambi ya Upinzani ni kuhusu haki na uhuru wa vyombo vy'a habari na haki ya kupata taarifa. Mheshimiwa Mbilinyi (Sugu) anazungumzia hoja hii ndani ya dhana kwamba Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliahidi haki ya uhuru wa vyombo vy'a habari na haki ya kupata taarifa na kwamba mpaka leo hatujitekeleza. Suala hili ameliunganisha na dhana ya uwazi kama tunu ya Taifa katika Bunge la Katiba.

Mheshimiwa Spika, hili la kuunganisha na suala la uwazi na kuwa ni matakwa ya wananchi katika katiba mpya hapa siyo mahali pake. Suala la rasimu ya Katiba iliyowasilishwa kwenye Bunge la Katiba na maboresho yake tungoje tulifanyie kazi katika sehemu yake ndani ya Bunge la Katiba. Nitumie tu

Nakala ya Mtando (Online Document)

nafasi hii niwahimiza Wabunge wenzetu hao wenye kuiita UKAWA, Bunge la Katiba lipo, rudini tumalizie kazi tulioianza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niseme tu hili la uhuru wa habari na haki ya kupata taarifa siyo geni na halihitaji shinikizo kutoka Kambi ya Upinzani. Kama alivyosema Mheshimiwa Rais kuitia dhana hiyo ya utawala bora, ndiyo misingi tunayojijengea kama nchi. Niseme Mheshimiwa Rais alilisemea, ni mahali pake na kimsingi ili kupata habari kwa taratibu na kanuni sahihi lazima mifumo sahihi iwepo ya utambuzi chanya ya masuala ya habari.

Mheshimiwa Spika, nimesema hili si jipya kwani ni suala ambalo Serikali imekuwa inalifanyia kazi na kuendana na mazingira yetu tupo katika hatua nzuri. Katika bajeti ya 2013/2014, suala hili la uhuru wa kupata habari lilijitokeza na nililieleza kwa sasa tunashughulikia Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari wakati Wizara ikiendelea kupata uzoefu wa nchi nydingine wanashughulikia vipi suala la uhuru wa vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, katika hili MCT (*Media Council of Tanzania*) waliwezesha pia Wabunge kwenda India na sehemu mbalimbali. Kimsingi, Wizara imekuwa inalifanyia kazi kwa kuhakikisha kwanza, masuala ya msingi yanayohusu habari yawe yamewekwa sawa ikiwemo uelewa sahihi kuhusu habari au taarifa kwa ujumla. Tafsiri ya *ki-dictionary* ya kiurahisirahisi tu habari ni processed data. Takwimu iliyochakatwa ni habari, taarifa na taarifa tunayoizungumzia si kwa wanahabari tu, haiishii kwenye kamera na kalamu. Wizara imekuwa ikitambua jukumu kubwa na muhimu tulilonalo kama Wizara na Msemaji Mkuu wa Serikali na kuwezesha Serikali kuwafikia wananchi na kuwasiliana ndani ya Serikali na kuboresha utendaji kazi wake.

Mheshimiwa Spika, tuliamua kuanza na Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari ambayo kimsingi katika kuitengeneza na kuikamilisha inatengeneza pia misingi na mazingira chanya ya upatikanaji wa habari na taarifa. Haya mazingira ni pamoja na uelewa sahihi wa masuala ya habari. Kwanza, habari ni rasilimali yenye kubeba mahitaji mapana ya kitaaluma ili kuweza kuwa yenye manufaa kwa nchi na wananchi wake kwa ujumla. Tunapozungumzia masuala ya habari kwa mapana yake, tunazungumzia upangaji wa habari, kusimamia au kushughulikia uendeshaji wa teknolojia ya habari (*handling of information technology*), rasilimali usinifu wa habari (*information resources*).

vyanzo vya habari na huduma za habari (*information sources & services*), mifumo ya habari (*information systems*), uandishi wa habari (*journalism*), huko ndiko Waandishi wa Habari waliko, rasilimali za habari (*information resources*), watu wenyewe ustadi wa habari (*information related skilled individuals*), teknolojia ya habari (*information technology*), mfano nakala mango (*hardware*), nakala tepe (*software*), mkongo na programu za kompyuta. Vyanzo vya habari

Nakala ya Mtando (Online Document)

(information sources) ni pamoja na rasilimali za habari ndani ya Wizara zetu, asasi zetu pamoja na sekta binafsi, maabara za habari na kadhalika.

Huduma za habari kwa maana ya shughuli yoyote ile inayosaidia kuchakata na kuhuulisha habari. Sasa hii mifumo ya habari ambayo ni *information systems* uhulishwaji wa takwimu na taarifa za mifumo madhubuti, hivyo tunapozungumzia masuala ya upatikanaji wa habari au taarifa au haki ya kupata taarifa, haya pia ni muhimu tuyawkee maamuzi kwamba utekelezaji wake kwa usahihi na ufanisi utategemea kwa kiasi kikubwa kiwango cha utekelezaji wa haya yote kuhusu habari au taarifa na si kwa mtazamo wa habari wa kiuandishi wa habari tu. Kwa kuzingatia hili na kwa kuzingatia msukumo uliopo wa Serikali iliyo wazi kwa wananchi, Serikali inafanya kazi maelekezo ya Mheshimiwa Rais pamoja na haki ya kupata taarifa. Waraka wa suala hili kwa mtazamo wa haki unashughulikiwa katika ngazi ya maamuzi ya Serikali. Kwa hiyo, hivi ninavyozungumza tayari Waraka wa kushughulikia haki ya kupata habari au taarifa, uko katika ngazi ya matekelezo ndani ya Serikali.

Sasa suala lingine ambalo limezungumziwa na wachangiaji mbalimbali ni sekta ya maendeleo ya vijana. Jukumu kubwa la Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, katika sekta ya maendeleo ya vijana kama tulivyzungumza ni kuwawezesha vijana kukua katika maadili mema, kuwapa mafunzo na kuendeleza ujuzi wao pamoja kuwawezesha kuendelea kiuchumi kwa kuandaa sera, mipango, mikakati na programu za kitaifa pamoja na kufuatilia, kusimamia na kutathmini utekelezaji wake.

sasa ukosefu wa ajira kwa vijana umeanza na umejitokeza na Wabunge wengi wamelizungumzia kwa michango yao mbalimbali ambayo imeonesha ni kwa jinsi gani wanaguswa na tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana. Waheshimiwa pia wametoa ushauri mzuri wa jinsi ya kuwasaidia vijana kukabiliana na changamoto hii. Tumeupokea ushauri huo na tutaufanyia kazi kadri tutakavyoweza.

Waheshimiwa waliochangia suala hili pia wamekuja na suala la uwezekano wa kuwepo mpango maalum wa kuwawezesha vijana kupata ajira. Waheshimiwa waliochangia ni pamoja na Mheshimiwa Felister Bura, Dkt. Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa Catherine Magige, Mheshimiwa Celina Kombani, Cecilia Paresso, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac. Wote hawa napenda kusema Wizara ina mpango maalum wa kuyawezesha makundi yote ya vijana ambao unatekelezwa sambamba na Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano 2011 – 2016.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango huo, Wizara inafanya masuala yafuatayo:-

Nakala ya Mtando (Online Document)

(i) Kuwawezesha vijana kupata mitaji ya kuendeleza miradi yao kuitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

(ii) Kuendelea na mchakato wa kuanzishwa kwa Benki ya Vijana ili vijana waweze kupata chombo chao cha kitaifa cha kuwapa huduma za kifedha.

(iii) Kuendelea kuzihimiza taasisi na sekta zote kuingiza masuala ya maendeleo ya uchumi katika mipango ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kuwatenglea maeneo maalum ya biashara na kilimo.

(iv) Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI inaendelea kuwahamasisha vijana kujunga katika vikundi vyta uzalishaji mali ili waweze kuanzisha, kuunganisha mitaji na kutambuliwa kwa urahisi kisheria.

(v) Kuendelea kuhimiza Halmashauri zote nchini kutenga percent tano ya mapato yake kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya vijana.

(vi) Kuendelea kutoa elimu ya ujasiri amali, uongozi, ujasiri na kilimo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

(vii) Wizara pia imevihamasisha vyuo vikuu kuingiza somo la ujasiri amali katika programu zao za masomo ya kuwahimiza wahitimu wa vyuo vikuu kuanzisha makampuni yao kulingana na taaluma zao.

(viii) Kwa kushirikiana na TAMISEMI, Wizara inaendelea kuhimiza Sekteratieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya kuajiri Maafisa Vijana ili kuwasaidia vijana pamoja na mambo mengine kuanzisha miradi ya kuwawezesha kuajiri wenye.

Mheshimiwa Spika, sasa jukumu la Wizara yangu kama Wizara yenye dhamana ya kushughulikia maendeleo ya vijana kama nilivyotoka kueleza na majibu mbalimbali ambayo nimekwishayatoa, ni kusimamia utekelezaji wa Sera hii ya Maendeleo ya Vijana. Mambo muhimu ambayo yamepewa msukumo na makusudi katika utekelezaji wa sera hii ni kama hayo ambayo tumeyapangia na kuweza kuyaweka katika Mpango Maalum wa kuendeleza maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limejitokeza na ambalo wachangiaji mbalimbali wamelizungumzia ni kuhusu ushirikishwaji wa vijana katika masuala ya maendeleo na hasa limejikita katika uwezeshaji wa kuwa na Baraza la Vijana la Taifa. Hili limeandikiwa na Mheshimiwa Mnyika pamoja na wachangiaji wengine, niseme tu kwamba, Wizara inaendelea na utaratibu wa

Nakala ya Mtando (Online Document)

kuanzisha hili Baraza la Vijana la Taifa ili kuwapa vijana fursa pana ya kushiriki katika maendeleo ya nchi na kuwa na chombo chao cha kuwaunganisha na kuwawakilisha katika ngazi za kitaifa na kimataifa.

Muundo wa Baraza hili ni kuanzia ngazi ya taifa hadi kijiji. Waraka wa kuomba kuundwa kwa Baraza hili umeandaliwa na kwa sasa uko katika ngazi ya Baraza la Mawaziri kwa ajili ya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Vijana wa Afrika wa mwaka 2006 uliridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2012 kwa lengo la kuiwezesha Serikali na wadau wengine kuwashirikisha kikamilifu vijana katika michakato yote ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi. Kwa sasa Serikali inaanda Muswada wa Sheria ya Utekelezaji wa mkataba huo. Mkataba huo pia unahitaji kuwe na Baraza la Vijana. Kwa hiyo, Baraza la Vijana ni jambo ambalo kiserikali na sisi tunalifanyia kazi kwa karibu baada ya kwenda nchi jirani na kuweza kujifunza wanavyofanya kazi zao. Tumejitahidi kuhakikisha kwamba, Baraza tutakaloliunda litawashirikisha vijana wa ngazi zote kutoka vijiji mpaka Taifa na litakuwa katika ngazi tofauti, ngazi ya Kitaifa lakini pia ngazi ambayo itaweza kusimamiwa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, hoja nyiningine iliyojitokeza ni kuhusu maadili ya vijana yameporomoka lakini sanasana siyo kwa vijana ila tu ni kwa jamii na viongozi kutotumia lugha safi pia. Suala la maadili ni muhimu sana katika maendeleo ya ustawi wa Taifa lolote duniani. Maadili ni nyenzo muhimu katika ujenzi na usalama wa Taifa. Maadili yetu kama Watanzania yanajikita zaidi katika masuala ya upendo, ushirikiano, utii wa sheria, kuvumiliana, kujitegemea, kuwa wamoja na kulinda misingi ya amani walijotuachia Waasisi wetu.

Maadili mema kwa wananchi na viongozi hujengwa kuanzia katika ngazi za familia zetu tangu katika umri mdogo kabisa. Mazingira, tabia za walezi, wazazi na viongozi wa ngazi zote katika jamii ni vigezo muhimu katika kujenga tabia za watoto na vijana. Kwa tabia zinazooneshwu na baadhi ya wazazi na viongozi katika jamii, hususan kauli zisizokuwa na staha, zilizajaa matusi, uwongo na uchochezi kutoka kwa watu ambao jamii imewapa dhamana ya kuwaongoza ni ishara tosha ya mmomonyoko mkubwa wa maadili katika Taifa letu. (Makofii)

Athari zake zinawakumba watoto na vijana; hivyo, tunatengeneza Taifa la watu wasioheshimiana na kuona matusi, uongo, uchochezi, kejeli, kama mtaji wa kisiasa. Kizazi kisichokuwa adilifu na hata katika maeneo ya kazi na hivyo kuathiri uchumi wa Taifa. Kizazi kisichoheshimu sheria za nchi na hivyo kufanya kazi ya kuliongoza Taifa kuwa ngumu kwa kupoteza muda mwingi kupambana na watu wanaovunja sheria kwa makusudi badala ya kuwekeza katika shughuli

Nakala ya Mtando (Online Document)

za kuwaleta Wananchi maendeleo. Sasa niwaombe Viongozi mbalimbali, basi tujikite tutumie muda wetu na talanta zetu kwa malengo chanya.

Mheshimiwa Spika, mifano iko mingi na wachangiaji mbalimbali wameisemea. Leo wamefikia hatua ya kuwadharau na kuwabeza Waasisi wa Taifa hili, tukidhani *fashion* ndiyo uhuru wa mawazo na kutumia nafasi adhimu na muhimu ya Bunge kufanya hivyo. Jambo hili halikubaliki kabisa na mimi kama Waziri mwenye dhamana ya masuala ya utamaduni, yanayobeba dhamana ya kuhimiza, kujenga na kusimamia maadili ya jamii yetu, niseme tu ni jambo la hovyo, hatukubaliani nalo na mwenendo huu ni muhimu kabisa Viongozi wote tuukatae kwa nguvu zote. Hii ni tabia isiyokuwa na tija na haipendezi katika jamii na si sura ya Mtanzania na hasa si sura ya Kijana wa Kitanzania. (Makofii)

Naomba nichukue nafasi hii kuiomba jamii ya Watanzania wote kutoka pande zote mbili za Muungano; Zanzibar na Tanzania Bara, tuwakatae Viongozi wa namna hiyo. Viongozi wa namna hiyo ni sumu kali kwa ustawi wa Taifa, ni wa binafsi na ni wakala wa mabwana wakubwa wasiolitakia mema Taifa letu. Tusitumie pia vyombo vya habari kuvunja maadili ya Mtanzania na kusambaza uchochezi katika jamii hasa matamshi ya hovyo hovyo kutoka kwa Viongozi. La muhimu ni Kiongozi kupima kama anachosema ni busara na pia hata kama ni busara, kukisema hapo anapokisema na mahali anapokisemea hicho kitu anachokisema. (Makofii)

Wito wangu kwa Viongozi, Wazazi, Walezi na Wananchi wote kwa ujumla, kama kioo cha jamii ni lazima tuwe wenye maadili na kusimamia uadilifu. Tuepuke kauli zisizokuwa na staha mbele za watoto, vijana na jamii kwa masilahi ya Taifa letu na kizazi chetu cha sasa na baadaye na hasa kwa wale ambao tunakamia kuwa Viongozi au ambao tayari ni Viongozi. Kila mtu kwa nafasi yake katika ngazi ya familia, taasisi za dini, vyombo vya habari na hata hapa Bungeni, tuhakikishe tunasimamia maadili na kuwa mstari wa mbele kwa uadilifu katika uongozi.

Sasa hoja nyingine ambayo ilijitokeza ni kuhusu malezi, ushauri na nasaha za maongozi. Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, inaendelea kutoa huduma ya malezi. Napenda niseme tu kwa wale waliochangia katika nafasi hii kwamba, Idara inaendelea kutoa huduma za malezi, ushauri na nasaha na maongozi kwa vijana kupitia kwenye programu yake ya elimu ya stadi ya maisha kwa vijana walio nje ya shule. Lengo la programu hii ni kuwawezesha vijana wajitambue, waweke malengo na kufanya maamuzi sahihi kuhusu mustakabali wa maisha yao. Kupitia programu hii, Wizara inawaandaa waelimishaji na stadi rika za maisha watatu wa kitaifa kwa kila

Nakala ya Mtando (Online Document)

mkao, ambao watatoa elimu hii kwa waelimishaji rika katika kila wilaya na kata zote nchini na hatimaye kuwafikia vijana katika maeneo na rika zao.

Wizara inaendelea kuhimiza Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya zote nchini, kuajiri Maafisa Vijana. Hatua hii inalenga kuwa na watendaji wa moja kwa moja wanaoshughulikia masuala ya maendeleo ya vijana katika ngazi za Mkoa wa Halmashauri. Niseme tu kwamba, hadi sasa ni mikoa 16 na Halmashauri 33 zilizokwishaajiri maafisa hao. Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, inaendelea kuwahimiza wale ambao hawajaajiri Maafisa Vijana katika maeneo yao, basi wafanye hivyo.

Ili kuhakikisha Maafisa Vijana wenyewe weledi na taaluma ya masuala ya vijana wanapatikana katika soko la ajira la ndani, Wizara imeanza mazungumzo na Chuo Kikuu cha Mzumbe, kuangalia uwezekano wa kuanzisha Kozi ya Maendeleo ya Vijana katika ngazi ya stashahada ya kwanza na ya pili. Kwa hiyo, niseme kwamba, Wizara yangu katika kutekeleza majukumu yake vizuri, tunaendelea kuhimiza Mikoa, Wilaya na Halmashauri za Wilaya nchini, kuajiri Maafisa Vijana, Michezo, Utamaduni na Maafisa Habari ili wawe chachu ya kusaidia maendeleo ya vijana kuititia fursa za utamaduni, michezo, habari na mawasiliano na nyingine zikiwemo katika maeneo yao hasa ndani ya jamii zao.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambazo zilijitokeza kuhusu uandishi wa habari kuzingatia matumizi sahihi ya Lugha ya Kiswahili, hii hoja imekwishazungumziwa na Mheshimiwa Nkamia.

Suala lingine lililojitokeza ni kuhusu mustakabali wa Vazi la Taifa. Suala hili niseme tu ni la muda mrefu, nakubaliana na aliyetoea hoja hii. Ni la muda mrefu kutoptaka na umuhimu wake, baada ya majadiliano kuhusu mkabala wa vazi lenyewe wa ama ushonaji au kitambaa, mapendekezo yaliyopo sasa ni ya mkabala wa kitambaa na yapo ngazi ya uamuzi Serikalini. Kwa kiasi kikubwa, lile jopo lililowekwa kushughulia hili, baada ya mwaka mmoja na nusu waliweza kuleta mapendekezo na nakumbuka tuliyatangaza vizuri katika vyombo vya habari mbalimbali na tuliendelea kuyazungumzia. Uchaguzi wa vitambaa viwe vya namna gani tayari tulikwishachagua na vilishapita katika ngazi za utekelezaji katika Serikali, kwa sasa hivi ziko katika ngazi ya maamuzi, nadhani sitokuwa nakosea kusema kwamba, ipo ndani ya Baraza la Mawaziri. Tukikutana likipangwa katika Mpango na Mheshimiwa Rais, tunaweza tukalizungumzia na kumalizana nalo hili.

Mfano mmoja mmeuona wa ubunifu wa kuweza kutumia ile dhana tu ya kuweza kutumia kitambaa na kuweza kuku-identify, Mheshimiwa Mlata

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ameivaa hapo, nimshukuru sana mwanamitindo maarufu ameweza kuja na hilo suala na leo ningeweza kuwa nayo nadhani ingezidi kuvutia Watanzania wakaona tunavyoweza kujitambulisha hata kwa kutupia mtandio wenye kitambaa tu kwa kiasi fulani. (Makofi)

Kuhimiza wasanii kuwa wabunifu na kujituma zaidi, hoja nyingine hii ilitolewa. Wizara inakubaliana na maoni ya Kamati, mintarafu umuhimu wa wasanii kuwa wabunifu, kufanya kazi zao kwa kujituma na kupenda kuijendeleza kielimu. Aidha, Wizara inawahimiza wasanii kuzingatia maadili katika utendaji wa kazi zao. Katika hili Mheshimiwa Neema amezungumzia, Mheshimiwa Ritta Kabati ameligusia, Mheshimiwa Catherine amelizungumzia na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali na hasa Mheshimiwa Martha Mlata amelizungumzia na kuonesha kabisa na yeye ni mmojawapo kati ya wanaoonesha mfano mzuri wa wasanii wenye kujua kutumia nafasi zao vizuri, lakini pia kutambua kwamba, baada ya usanii wao pia kuna umuhimu wa kuijendeleza katika hizo fani zao za usanii. Katika kulizungumzia hili, niseme tu Wizara imekuwa inawahimiza kwa kiasi kikubwa hata wale wasanii ambao wamekwishatengeneza fedha za kutosha, basi wajifunze umahiri na umakini wa kuhakikisha wanaziweka katika hisa, wanawunua hisa na wanawekeza vizuri katika kuhakikisha baada ya siku zikiisha huko, wasije wakajikuta wanabaki bila kuwa na kitu.

Hili la kutumia mijo ya simu nyimbo za wasanii, Mheshimiwa amekwisha lizungumzia. Utunzaji wa urithi wa utamaduni, hili pia limejitokeza. Niseme tu Serikali imekuwa ikihimiza jamii mbalimbali za Watanzania, kuhakikisha kuwa wanahifadhi na kulinda mila na desturi zao, ikiwa ni njia ya kutunza na kuendeleza urithi wa utamaduni wetu. Aidha, Serikali imesharidhia Mikataba ya UNESCO inayohusu utunzaji wa urithi wa utamaduni. Kwa kupitia Mikataba hiyo, Serikali imo mbioni kufanya taratibu za kuorodhesha baadhi ya urithi wetu na utamaduni katika Orodha ya Urithi wa Dunia. Katika hili asubuhi katika mazungumzo yetu, nakumbuka nimezungumzia kuhusu hii element ambayo tunataka kuitumbukiza katika UNESCO ili tuweze kutambulika na hawa wenye urithi rasmi wakiwa wanatokea huko Mtwara.

Haki za wasanii, hili limezungumzwa na Mheshimiwa Mlata, limezungumzwa na Mheshimiwa Neema na Mheshimiwa Catherine, wote wamezungumzia. Haki na masilahi ya wasanii vinalindwa na Sheria Na. 7 ya Mwaka 1999 ya Hatimiliki na Hatishiriki Sheria Na. 4 ya Filamu na Michezo ya Kuigiza ya Mwaka 1975 na Sheria Na. 3 ya Baraza la Sanaa la Taifa ya Mwaka 1984, ambapo Wizara yangu huwasitiza wasanii kusajili kazi zao ili ziweze kulindwa na sheria hizo. Kwa hiyo, si kwamba sheria hazipo, sheria zipo, bado tunaendelea na tupo katika mkakati wa kuhakikisha tunashughulikia Sera ya Utamaduni iweze kupita ili tuweze kushughulikia kubadilisha hizi sheria mbalimbali ambazo zimepitwa na wakati. Kwa hiyo, katika Sera ya Utamaduni

Nakala ya Mtando (Online Document)

tumebeba kabisa suala muhimu la kuhakikisha haki za wasanii zinalindwa na ni namna gani sheria itaweza kutungwa kuhakikisha hizo haki za wasanii zinaendelea kulindwa.

Hivi sasa Serikali kama mlivyozungumza na Mheshimiwa Martha Mlata amelizungumzia kwa umakini, utaratibu na urasimishaji wa tasnia ya filamu na muziki ambapo kazi za wasanii hawa zimewekewa stempu na TRA na hivyo kuzuia wizi wa kazi. Zoezi la urasimishaji litaendelezwa kwa fani nyingine za sanaa. Kama mnavyofahamu, fani zipo nyingi nyingi za sanaa mbalimbali. Kuna mashirikisho mbalimbali yanayosimamia sanaa mbalimbali. Kuna wachangiaji mbalimbali waligusia hapa ikaonekana kana kwamba tunavyofikiria masuala ya sanaa, tunafikiria ngoma na muziki.

Tunayo mashirikisho na hata Viongozi, Mheshimiwa Spika hukuwataja tu, tuna Viongozi mbalimbali wamekuja hapa wa mashirikisho mbalimbali ya sanaa. Mashirikisho ya filamu, sanaa za maonesho, sanaa za ufundi, sanaa za muziki, zote hizi ni fursa mbalimbali na uelewa sahihi uliopo katika Serikali yetu ya kuhakikisha tunawapanga sawa sawa hawa na kuwaweka katika hali nzuri ya kuhakikisha Serikali inawajali na kuweza kuwaongoza vizuri na hasa kwa kuzingatia kwamba, wengi wao ni vijana, ambao wakipata fedha kidogo wanachangamka halafu wakati mwingine wanasahau. Kwa hiyo, ni muhimu kuwatengenezea haya mashirikisho, lakini pia kuwapatia elimu mara kwa mara na kushirikiana na kuhimiza sekta binafsi kuingia katika haya masuala, kwa sababu kwa kweli kiujamii hasa bado hatujajikita na kutambua umuhimu wa haya masuala ya sanaa au masuala ya utamaduni kwamba ni kiwanda kikubwa ambacho tukkiangalia vizuri, kwa kutokea jamii lakini pia kwa sekta binafsi pamoja na Serikali, inaweza kutuletea kipato lakini pia ikapandisha Taifa letu katika ngazi tunazozihitaji.

Wasanii na dawa za kulevyta ni suala lingine ambalo limezungumziwa na Serikali inakubaliana na wito wa Kambi Rasmi ya Upinzani kutumika katika ubebaji na uuzaji wa dawa za kulevyta. Aidha, Serikali inatoa wito kwa wazazi na walezi kuwahimiza wasanii na vijana kiujumla kutokujilingiza katika masuala haya na kuhakikisha kwamba wanajilingizia kipato kwa kutumia na kufanya kazi zilizo halali. Hoja nyingine inahusu utengenezaji makala ya filamu na matumizi ya wasanii kutoka Kigoma. Wizara haijapokea Muswada wowote unaohusu utengenezaji wa makala ya filamu, documentary, inayowashirikisha wasanii kutoka Kigoma. Vilevile kwa mtengenezaji yeoyote wa filamu, makala ya filamu na picha jongefu, inapaswa kwa mujibu wa sheria kuwasilishwa maombi yake kimaandishi na kuridhiwa kupewa kibali husika.

Umuhimu na umiliki binafsi; Serikali inakubaliana na maombi ya Kambi ya Upinzani kuhusu umuhimu wa kuzingatia suala la umiliki bunifu katika sheria zote

Nakala ya Mtando (Online Document)

muhimu zinazohusiana na tasnia ya ubinifu. Kama nilivyokwisha kueleza hapo awali, tuko katika kutengeneza Sera ya Utamaduni ambayo inabeba masuala haya mengine yote katika kusimamia haya mashirikisho lakini katika sehemu hizi tofauti tofauti. Sera ya Utamaduni pia inabeba na kutambua na kuelekeza uwezekano wa kuja kutengeneza sheria itakayosimamia masuala ya umiliki na ubinifu.

Mheshimiwa Spika, mmonyoko wa maadili nchini, hili tumekwisha lizungumzia na hili limechangiwa na wachangiaji idadi yao ni sita ingawa hapa majina sikuyapata. Katika kudhibiti suala hili la mmonyoko wa maadili, Wizara imendelea kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuvaa mavazi yenye staha na pia kuzuia ngoma zisizozingatia maadili ya Tanzania kama vile kigodoro na khanga moja, ndembendembe na laki si pesa. Wanaokaidi na kukiuka maagizo haya, huchukuliwa hatua za kisheria. Aidha, idadi ya uwasilishwaji kwa ukaguzi na uwekaji wa madaraja ya filamu umeendelea kuongezeka. (Makof)

Katika hotuba yangu asubuhi nimeonesha ni filamu ngapi zimeweza kuwasilishwa na ngapi zimeweza kukataliwa. Ukiangalia ni idadi ndogo ambayo imekataliwa kupidishwa kuoneshwa, ni chache pia zilirudishwa kurekebishwa. Kwa hiyo, hii inaonesha kabisa kwamba, tunaanza kupiga hatua kuanza kutengeneza filamu ambazo zinazingatia maadili kwa kiasi kikubwa. Vilevile wanaanza kukubaliana na sheria ya kuhakikisha kwamba, wanawakilisha hizo kazi zao sehemu ambazo inatakiwa ili ziweze kufanyiwa kazi.

Sasa suala la maadili ni mtambuka na linamgusa kila mwanajamii. Kwa hiyo, Wizara inasisitiza kwamba, malezi yanaanza ngazi ya kaya na inashauri wazazi na walezi kuwalea watoto na vijana wao katika maadili na hasa vijana wa kisanii, wanaoingia katika masuala ya usanii; kwa sababu dhana nzima ya usanii ni suala la masuala ya kuburudika na kuburudishana na inachukua muda mrefu sana hata kutengeneza wimbo, wazo, mfikiriane, mkae pamoja watatu, wanne na ile inatoa mazingira ambayo hayajakaa vizuri kwa vijana wetu hasa katika miaka yao ya mihemko. Kwa hiyo, ni muhimu sana wazazi kuwasimamia vijana wao wenye kuingia hasa katika masuala haya ya usanii ili tuhakikishe kwamba, wanasmamia na kufuatilia maadili ya zile tasnia zao ambazo wanataka kuziendeleza.

Mustakabali wa Vazi la Taifa huu umekwishalizungumzia na lilichangiwa na watu watano. Maendeleo ya Kiswahili, Kitaifa na Kimataifa, Mheshimiwa Nkamia ameshalizungumzia na wachangiaji watatu wamelizungumzia.

Ulinzi wa haki na masilahi ya wasanii nayo imegusiwa, tumeshazungumzia. Majina ya filamu kuandikwa kwa Kiswahili nayo imekwishazungumziwa. Utambulisho wa Utamaduni wa Tanzania. Mimi nadhani hili limegusiwa na

Nakala ya Mtando (Online Document)

mchangiaji mmoja tena kwa maandishi. Wizara yangu imekuwa ikielimisha jamii kupitia semina mbalimbali, makongamano na Mkutano Mkuu wa Sekta ya Utamaduni kuhusu umuhimu wa kulinda na kuendeleza utamaduni wa Taifa ikiwemo ngoma ya asili; hivyo, kuheshimu na kuthamini mila na desturi za Kitanzania. Hata hivyo, suala la kuheshimu na kuzingatia mila na desturi mbalimbali ni mtambuka, linagusa sekta mbalimbali kama vile elimu na mafunzo ya ufundi, maendeleo ya jamii, jinsia na watoto na jamii kwa ujumla. Sera ya Utamaduni inasilitiza kwamba, malezi yanaanza ngazi ya kaya; hivyo, inasilitiza wazazi au walezi kuwalea vijana wao katika kuheshimu, kukuza na kuenzi mila na desturi nzuri za Kitaifa.

Maonesho ya Utamaduni, ni kweli kumekuwepo matamasha. Hoja hii ingawa haikuelezea kuhusu hasa nini, imezungumziwa na mchangiaji mmoja. Ni kweli kumekuweko na matamasha ya mashindano mbalimbali ya sanaa na utamaduni, lakini mengi huendeshwa na asasi na mashirika binafsi. Mfano, Tamasha la Kiangazi Morogoro, Makuu ya Mtwara, Muziki na Sigogo Chamwino Dodoma, Bulabo Mwanza, Tamasha la Ngoma la Kanda ya Ziwa na kadhalika. Wizara inahimiza Halmashauri kwa kuwatumia Maafisa Utamaduni, kuratibu na kufanya matamasha ili kukuza na kurithisha utamaduni wetu.

Katika hili niendelee kusema tu kwamba, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi na asasi zisizo za kiserikali, tumeponga kuanzisha pia Siku ya Msanii. Wizara huwa kuna ile Siku ya Utamaduni kama hii tuliyotoka kuisherehekeea tarehe 21 Mei na tumeanza kupanua kuhakikisha tunashirikiana na Wizara ya Viwanda pamoja na sekta binafsi ili kuhakikisha tunawavuta vijana, kwanza, kuenzi na kupenda masuala ya utamaduni, lakini kuyabebesha masuala ambayo yanawapa vijana masuala ya kuwajibika na jukumu la kuijendeleza kimasomo, lakini pia kibiashara na kibunifu.

Urejeshaji wa somo la muziki shulen, hoja hii imechangiwa na mtu mmoja. Niseme tu kwamba, Serikali imeshatoa maelekezo na utekelezaji umeshaanza. Ushiriki wa vijana katika shindano na katika hili pamoja na muziki, tumeomba pia kuhakikisha kwamba hata yale mashindano ya masuala ya utamaduni katika mashule ni muhimu pia yaanze kuwekwa katika mashindano mbalimbali ambayo shule inafanya kama wanavyofanya mashindano ya michezo.

Ushiriki wa vijana katika Shindano la *Big Brother Africa*, hili limechangiwa na mchangiaji mmoja. *Big Brother Africa* ni shindano linaloendeshwa nje ya Tanzania, washiriki huomba kupitia mitando na huenda kushiriki bila kupewa vibali vinavyotolewa na Kamati ya Vibali vya Wasanii wanaotoka na wanaoingia nchini.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Vijana wanaoshiriki, mbali na kuitangaza nchi wanayotoka, mara nyingi huhitaji kuongelea masuala au vivutio vya nchini mwao na hivyo hutangaza vituo vya utalii vya nchini kwao. Kutokana na taarifa zinazotolewa na washiriki wa *Big Brother Africa*, huwawezesha kujifunza na kuonesha mambo mbalimbali muhimu katika jamii kama vile jinsi ya kuvumiliana, kujaliana na kujenga urafiki mionganoni mwao licha ya kuwa na tamaduni zinazofautiana. Kwa hiyo, katika hili tunahimiza vijana wale ambao wanakwenda katika *Big Brother*, basi wawe wanakwenda wamejipanga sawa sawa, wakitambua kwamba wanakwenda kwa malengo chanya kama wanakwenda kule wanakwenda kutuwakilisha kama nchi, lakini kwa vile hatuiratibu kama Serikali, ni jambo ambalo tunawahimiza tu waende wikitambua kwamba, wanatakiwa kwenda kule kama wazalendo na vijana ambao wana mitazamo chanya ya kuijendeleza.

Kuongezwa Bajeti na Watumishi kwenye Bodi ya Filamu na BASATA, hii imezungumziwa na mchangiaji mmoja. Mimi nikubali tu kuwa Serikali imeendelea kuziongezea bajeti asasi hizi na kadiri hali ya uchumi inavyokuwa bora, Wizara itaendelea kuzitengea fedha zaidi na kuongeza Watumishi.

Kwa kiasi kikubwa wengine walichangia kuhusu hatua gani imefikiwa katika urasimishaji wa kazi za Wasanii wa Filamu na Muziki na urasimishaji huu umesaidiaje kudhibiti uharamia wa kazi zao. Kwa muda mrefu kama nilivyoeleza, wasanii wamekuwa wakilalamika kuwa hawapati mapato stahiki ya kazi zao, kutokana na kukithiri kwa wizi unaofanywa na maharamia wa kazi hizo. Serikali ilisikia kilio chao na tayari hatua stahiki kama alivyoeleza Mheshimiwa Nkamia na mimi hapo nyuma na wachangiaji mbalimbali na kama nilivyogusia, tumekwisha shughulikia hilo. Tumefanya hivyo kwa kupitia huu urasimishaji wa tasnia ya Filamu. Serikali ina nia ya dhati kabisa ya kuikuza, kuindeleza na kuisimamia tasnia ya filamu nchini. Hatua ya kuzirasimisha tasnia za filamu na muziki ni mojawapo ya jitihada za Serikali kutekeleza matakwa ya wadau wenyewe.

Malengo ya Urasimishaji unaofanywa na Serikali pamoja na mambo mengine, ni kurejesha nidhamu katika tasnia ya Filamu na kuwezesha uwepo wa takwimu sahihi kuhusu tasnia hii, ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wadau wa filamu kuweza kutambulika na kushirikishwa katika masuala muhimu kupitia kazi zao hususan kukopesheka na kufanikisha ulinzi wa kazi zao wenyewe na kuzifanya tasnia za Filamu na Muziki kuwa rasmi. Kupitia urasimishaji huo, hususan stempu zinazobandikwa kwenye kazi za Filamu na Muziki, Serikali sasa inaweza kuzitambua kazi ambazo siyo halali na ambazo siyo halisi. Zile ambazo ni feki, pia Wizara ikishirikiana na asasi zisizo za kiserikali, kwa kushirikiana na TRA na COSOTA, tuna mpango pia wa kuhakikisha tunazitoa katika masoko ili ziweze kuachia zile kazi ambazo ni halali ziweze kupata haki yake kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa kama nilivyokwishakueleza, zimetolewa stampu zaidi ya elfu sita pointi saba, kwa kazi za Filamu na Muziki ambapo zaidi ya Stemptu laki nane na sitini elfu zimekwishatolewa. Serikali inaendelea kufanya operesheni kuziondoa zile kazi zote ambazo hazijabandikwa Stemptu husika, kwa sababu wakati tulipokuwa tunatangaza kuanzisha huu mpango, tulitoa muda ambao tutaachia grace period ya kuachia wale ambao wanafanya kazi feki waweze kujirudi. Kwa hiyo, sasa muda umefika ambapo tunaingia sokoni na kuweza kuchukua zile kazi ambazo ni feki na kuweza kuziharibu.

Kwa mantiki hiyo, urasimishaji ni njia mahususi ya kusaidia kuondokana na kilio cha muda mrefu cha wasanii na unasaidia kutambua bidhaa stahiki kwa idadi wanayoitoa wasanii wenyewe kwenda sokoni. Kwa hiyo, msanii atakapofanya kazi yake, ile ambayo atatoa Stamp zake atakazonunua, ndizo atakazoweza kutengeneza kopi ya vile vitu vyake na kuweza kuuza. Hata yule ambaye anamuuzia au yule promota wake, hatokuwa na *rights*, labda yeze mwenyewe akiuke aanze kuharibu huu mpango mzuri ambao umefanywa wa kuweza kuwanufaisha wao wenyewe.

Suala lingine ambalo lilijitokeza, hoja hii inaonekana ni hoja kutoka katika Kamati ya Kudumu, ni mkakati wa kupambana na Ugonjwa wa UKIMWI na Vijana. Wizara imeanzisha Programu ya Stadi za Maisha kwa vijana walio nje ya shule, imeweka ujumbe wa kudumu wa UKIMWI katika Mbio za Mwenge kila mwaka na elimu kupitia Maadhimisho ya Wiki ya Vijana kila mwaka. Tunahimiza kila mahali wakati ambapo kunakuwa kuna mkusanyiko wa vijana katika mtamasha mbalimbali, lakini pia katika mikutano mbalimbali ya asasi mbalimbali Serikalini na sekta binafsi, kuhakikisha watu wa AMREF wanakuwepo na watu wa TACAIDS wanasaidia ku-monitor na kusaidia na kutoa elimu nasaha na pia kuweza kupima na kuhimiza watu waweze kupima kwa hiari.

Mheshimiwa Spika, hoja nyininge iliyojitokeza inahusu kutokuzingatia maadili kati filamu na hili limezungumziwa na watu watatu. Lipo tatizo la kuwepo kwa filamu zisizozingatia maadili yetu hususan zile zinazotengenezwa nje na kuuzwa hapa nchini. Katika kukabiliana na changamoto hii, Serikali imehakikisha maadili wanayostahili yanazingatiwa katika filamu zetu kwa kuhakikisha kuwa, filamu zote za ndani ya nchi na zinazotoka nje ya nchi zinakaguliwa, zinapewa madaraja yanayoonesha ni kundi la umri upi linalostahili kuitazama filamu husika.

Kwa kutekeleza azma hii, Serikali kupitia Bodi ya Filamu, kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 hadi Aprili, ilikagua na kuwekea madaraja filamu 458. Kwa majina ni sawa na CD 916. Zilifanyika operesheni ambazo zilibaini filamu 299 zilizoingizwa sokoni bila kufuata taratibu na filamu za zamani 202, sawa na

Nakala ya Mtando (Online Document)

filamu 501 na kuzichukulia hatua za Kisheria ambapo watusika waliziwasilisha na kupewa makaripio makali.

Bodi pia ilifanya vikao 35 na Wadau mbalimbali wa Filamu, ambao filamu zao zilihitaji marekebisho hususan yale yaliyolenga uzingatiaji wa maadili kabla ya filamu hizo kwenda sokoni.

Mustakabali wa soko la filamu na vikao vya utoaji elimu hususan urasimishaji wa tasnia ya filamu, utengenezaji wa filamu na makala za filamu, umeendelea kuongezeka kwani watengenezaji kutoka nje ya nchi wameendelea kuitumia mandhari ya Tanzania na kuendelea kuhimiza kizingatia maadili na Utamaduni wa Mtanzania. Kwa hiyo, maadili na kutokizingatia maadili kwa kifupi ni suala ambalo Wizara imeliona na inalifanyia kazi, tena siyo kazi kwa maneno isipokuwa kazi kwa matendo na tumeweza pia kutoa elimu kwa Wadau na jamii ambayo pia itakuwa ni endelevu; hivyo, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa Wadau wote wa Filamu ili wazingatie utu na hadhi zao na kuepuka kutumiwa kwa njia zinazowadhalilisha.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara inahimiza jamii kununua filamu kwa kizingatia madaraja kulingana na umri wa kundi husika. Wizara yangu pia katika kudhibiti suala la maadili katika filamu, imeendelea kukemea uoneshaji na uuzwaji wa filamu zisizozingatia maadili, ikiwa ni pamoja na kusimamia maadili, weledi na ubora katika tasnia ya filamu ya michezo ya kuigiza kwa kupitia Miswada kabla ya utengenezaji wa filamu, kukagua filamu na kutoa ruksa ya kuonesha hadharani na kupitisha Miswada na kuratibu maonesho ya michezo ya kuigiza.

Kwa wale waliokiuka, Wizara yangu imeendelea kutoa makaripio, ushauri wa ana kwa ana, vikao na hata kuzuia filamu zinazokiuka maadili. Kupitia Sheria ya Mwaka 1976 ya Filamu na Michezo ya Kuigiza na Kanuni zake, Wizara yangu imeendelea kushirikiana na TAMISEMI hususan Halmashauri za Wilaya na Sekretarieti za Mikoa, kusimamia utekelezaji wa Sheria hiyo. TCRA kupitia Kamati ya Maudhui, imeendelea kusimamia maadili ya kazi mbalimbali kupitia vyombo vya habari na wale wanaokiuka, hatua zimechukuliwa dhidi yao.

Kwa upande wa Sekta ya Habari, tatizo la uandishi usio na weledi na wenye upotoshaji, uchochezi, uzushi na chuki, ni suala ambalo kwa kiasi kikubwa amelizungumzia Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kifupi ni kwamba, tasnia ya habari nchini tumekuwa nayo kwa muda, imekua kwa haraka tangu mwaka 1962 pale Serikali iliporuhusu mfumo wa soko huria kufanya kazi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Tumeshuhudia ongezeko la vyombo vyahabari nchini, kuanzisha magazeti ya kila siku, vituo vyaredio na televisheni, mathalani ongezeko la magazeti yanayotoka kila siku. Magazeti kwa siku unaweza kukuta wakati mwingine kuna magazeti 12 na ipo siku ndani ya wiki magazeti yanaweza kufikia hata 27. Leo hii tunazo redio 93 na Televisheni 26.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kutoa hoja. Ahsante. (Makofij)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono. Katibu, hatua inayofuata!

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 96 – Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

Kifungu 1001 - Administration and HR
ManagementTshs. 4,003,824,000/=

MHE. SALUM KHALFAN BARWANY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi, nimetaka kujua kauli ya Serikali juu ya usikivu wa TBC. Hii hoja ni ya muda mrefu, tumejitahidi kuielekeza Serikali kama Bunge kuangalia ni namna gani inaweza ikaboresha usikivu wa Redio ya Taifa na Televisheni yake.

Nchi yoyote Duniani, watu wake hujivunia vyombo vyake vyahabari, baadaye hufuata hivi vyombo vya private kwa maana ya binafsi. Imeonekana kwa muda mrefu, TBC pamoja na malalamiko yao kutaka kuongezewa bajeti yake, lakini Serikali imekuwa kiziwi juu ya hoja hiyo. Katika bajeti iliyopita waliomba shilingi bilioni kumi na moja, hatimaye wakakubaliwa kupewa shilingi bilioni sita. Kwa mujibu wa pesa ambazo wamepewa katika bajeti ambayo inaishia, wamepewa shilingi bilioni moja tu. Hii inaonesha dhahiri kabisa kwamba, hakuna nia nzuri ya dhati katika kuimarisha TBC ili upatikane usikivu wa kutosha.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Katika maeneo mengi sasa hivi wanasikiliza radio za nje na Televisheni za nje; kwa mfano, katika mipaka ya Malawi na Zambia, husikiliza radio za nje kuliko radio zetu. Sasa hata kwa ulinzi wa Taifa na amani ambayo tunaizungumzia hapa, kama hatuna Redio ya Taifa na Televisheni yake, hatuwezi kusimamia amani pindi hali ya machafuko ikitokea. Kwa maana hiyo, pamoja na majibu mazuri lakini ni majibu ya Kisera tu, hayajaonesha mkakati wa makusudi ni namna gani Serikali imejipanga sasa. Kuonesha kwamba haijajipanga, ni bajeti hii finyu ambayo imetolewa kwa chombo hiki ambacho ni matarajio ya Watanzania wengi.

Mheshimiwa Wabunge, tusipoelezwa vizuri sisi kama Wabunge wasimamizi wa Serikali hiyo, tutashika shilingi mpaka pale Serikali itakapotuthibitishia kwamba, usikivu wa TBC kuanzia sasa, umetengenezewa mazingira gani. Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Niseme tu kama tulivyofafanua ni kwamba, uwezo wa kifedha au wa bajeti wa kuendesha TBC, fedha inayopangiwa ni kidogo. Sisi kwa upande wa Serikali na bahati nzuri Mheshimiwa Barwany ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, ambayo inaisimamia TBC, tunaangalia ni namna gani sasa TBC iweze kubuni vyanzo vingine vya mapato. Kama nilivyosema kwamba, wana *investment areas very strategic*; kwa mfano, Mwanza pale unapotoka Airport kushoto, wana eneo kubwa sana, ambalo wakifanya *investment still wanaweza ku-generate a lot of funds*, wakapunguza vitu vingine vidogovidogo ili wasiitegemee Serikali hundred percent. Nyerere Road pale, wana *strategic area* kubwa sana, tatizo lao lilikuwa ni hati za viwanja. Hati wameshapata, sasa wanajaribu kuzungumza na makampuni ama Wadau wengine ili wafanye *investment pale*. TBC ipate fedha hizo ili kupunguza matatizo haya madogo madogo.

Suala la usikivu ni kweli lipo katika maeneo mengi, lakini hata katika *Policy* ya TCRA hivi sasa wanatakiwa kuweka mtambo wa 2KV. Mtambo wa 2KV wa FM, coverage radiance yake ni ndogo sana na inapokutana na milima ina-hinder ile penetration ya ule mtambo. Sasa ni haya mambo ambayo lazima tukae na watu wa TCRA, tuone ni namna gani badala ya kutegemea hii mitambo ya 2KV angalau pengine tu-move kwenda kwenye mitambo ya 5KV ili usikivu uweze kuongezeka. Ahsante.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia suala zima la fedha ambazo zinakwenda katika Mfuko wa Vijana. Fedha ambazo tunapangiwa kwa ajili ya kuhakikisha vijana wanakopeshwa ili kuweza kujikwamua na tatizo kubwa la ajira na kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe ni shahidi, Wabunge wote Vijana humu ndani, tumekuwa tukizungumzia suala la ajira kwa vijana tangu tumefika.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Tunajua kabisa Serikali haina uwezo wa kuajiri watu wote na vijana wanajua hilo. Sasa wamehamasika kujajiri wenyewe, lakini kwa masikitiko makubwa sana Serikali bado haitengi fedha za kutosha kuhakikisha hizo fedha zinawafikia vijana wote mpaka kule kwako Njombe. Vijana wanapata tabu, wanaambiwa tu kuna fedha lakini kiuhalsia fedha hizo hazipo.

Vijana wanaendelea kuahangaika, sasa sisi humu wawakilishi wao tunapata tabu, tunashindwa jinsi ya kwenda kuwajibu huko. Mwaka jana zimetengwa shilingi bilioni sita, shilingi bilioni mbili tu kwa 61% ya Watanzania *it is not fair*. Sasa sisi tunahitaji Serikali itupe majibu ya kina; kwa nini fedha za vijana hazitolewi kama ambavyo zinapitishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaweka angalizo, nisipopata jibu nitaondoa shilingi.

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, fedha inayotengwa kwa vijana haitoshi hasa Mfuko wa Vijana. Asubuhi umeipata Hotuba yangu, makadirio ambayo tunayo kwa sasa hivi tuna maombi ya vijana vikundi zaidi ya bilioni nane, tunaendelea kuchambua. Sasa hivi tuna bilioni mbili ambayo tumeshatumia kama milioni mia moja na kitu.

Sasa sababu za kutopata hela ya kutosha kwa Mfuko wa Vijana, ninadhani ni sababu ya kiujumla tu ambayo Kiserikali ndilo gawio ambalo tumelipata na ndiyo mpango tuliowekewa na bado tunaendelea kujaribu kuomba, tuweze kuongezewa, lakini hatuna uhakika wa kuweza kupata hizo za ziada. Kwa kiasi kikubwa, tunatumia hicho kidogo tunachokipata na tunachojitahidi kwa huu muda uliobakia angalau zile bilioni sita tulizokwa tumeahidiwa mwaka jana, tunategemea kwamba tutazipata katika kipindi hiki kilichobakia.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu kama hayo wawakilishi wa vijana humu ndani tumeyazowea na hayaturidhishi.

MWENYEKITI: Sasa unasema nini?

MHE. ESTER A. BULAYA: Ninaondoa shilingi sasa.

MWENYEKITI: Usiseme namna hiyo.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu kama haya yanatolewa kila siku, Vijana wa Taifa hili wanahangaika. Nami kwa confidence ninasema wana imani na Serikali yao. Sasa ni kwa nini hamwoni umuhimu wao?

Nakala ya Mtando (Online Document)

Kwa nini fedha za vijana zisiwekwe kwenye *ring-fenced* kwamba, zikitolewa kama zinazotengwa, aidha iwe ndogo mmebungukiwa huko Wizarani, fedha zetu msiziguse zote ziende kwa vinaja, ndiyo hizo tunazotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwenye Wizara ya Fedha wote ni vijana. Mheshimiwa Mwigulu nimekuona hapo, ulipokuwa back bencher ulikuwa unawatetea sana vijana. Vijana wana imani na wewe. Tunakuomba utoe hapo tamko, ninahitaji *commitment* ya Serikali, fedha za vijana zinazotengwa zote zitolewe. Mheshimiwa Mwigulu, tulikuwa tunatetea wote huku, sasa kwa nini umeeenda huko unanyamaza! Vijana wana matumaini na wewe, ninahitaji *commitment* yako hapo leo hii, bila hivyo sirudishi shilingi. Nikirudisha hii shilingi, Vijana wa Tanzania hawatanielewa na mimi 2015 ninataka kurudi. (Makofi)

MWENYEKITI: Hoja ni nini?

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni fedha za vijana ziwekewe utaratibu maalumu na hizo bajeti zao ndogo zinapotengwa zitolewe zote.

MWENYEKITI: Mnasikia hoja ndiyo hiyo, sasa msije mkatengeneza hoja zingine. Ngoja nitafute, Mheshimiwa Kamili!

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Kicheko)

MWENYEKITI: Kwani vijana mngezaliwa bila wao? (Kicheko)

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi ya kuchangia. Napenda kuwaeleza kwamba, sisi ndiyo tumewazaa hao vijana na ndiyo tuna huruma na vijana wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja ya kutolewa shilingi na Mheshimiwa Bulaya, kwa kuwa mimi ni Mwanakamati wa Wizara hii. Niliwaeleza na niliwaauliza maswali hawakuyajibu na nimeandika kwa maandishi hawakunijib. Fedha za vijana zimetolewa bilioni mbili, lakini wamepatiwa milioni 172 tu; je, niambieni bilioni 1.8 zipo wapi?

Katika randama yenu mlionesha kabisa kwamba, zimetumika, tukawaambieni mtuambie mmetumiaje, kwa sababu mmetumia kwa ufuatiliaji, kuelimisha na kadhalika. Sasa mimi naomba Mheshimiwa Waziri utueleze hapa fedha hizo zimekwenda wapi? Kwa nini fedha zingine pia hazikutolewa na Wizara ya Fedha mtuambie kama fedha ziliikuwa zimepangwa bilioni 6.1 leo zikatoka bilioni mbili, zingine ziko wapi mtuambie leo?

Nakala ya Mtando (Online Document)

Sisi tunaungana na Mheshimiwa Bulaya kwamba hizo fedha zipatikane bilioni sita na hizi zinazotengwa safari hii pia ziongezwe siyo bilioni nne tu peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Hoja ya mtoa hoja mmeielewa siyo kusema kila kitu hapa. Huyu hoja yake na kusema fedha za vijana ziwe *ring-fenced*, basi. Sasa ninyi maneno mengine yote yanatoka wapi?

Mheshimiwa Jafo!

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, hoja ya Mheshimiwa Ester Bulaya naiunga mkono moja kwa moja. Tukubali kwamba, hii fedha yenyelewe iliyotengwa mwaka jana ni kidogo. Kwa hiyo, katika ya bilioni sita na milioni 100 kutolewa shilingi bilioni mbili maana yake jambo haliwezekani.

Hoja ya Mheshimiwa Ester Bulaya kusema kwamba, ziwe *ring-fenced* ni jambo la uhakika na ni jambo ambalo halihitaji mjadala hapa. (Makofii)

Kwa hiyo, kwanza, tunaomba Serikali ihakikishe katika kipindi hiki kilichobakia, maana yake mwaka wa fedha tunaenda kuumaliza hivi sasa, hizo pesa ambazo zimetengwa ziweze kutolewa. Hali kadhalika, kwa bajeti ambayo tunaijadili hivi sasa, pesa hizo ziwe zimetengwa maalumu kwa ajili ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ester Bulaya, kwa asilimia zote mia moja. Ahsante. (Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Catherine!

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana mkono na kijana mwenzangu Mheshimiwa Ester Bulaya, kwa hii pesa iliyotolewa kwa ajili ya vijana na vijana wamepewa ni ndogo sana. Tunaomba kwanza hii ya bajeti ambayo inaisha, vijana wapewe na hata hii iliyopo iongezwe maana haitoshi. Serikali mmekuwa hamtukumbuki vijana mnatusahau. Kwa hiyo, tunaombeni bajeti ya vijana iongezwe na hii nyingine ambayo hawakupewa tunaomba vijana wapewe bajeti yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofii)

MWENYEKITI: Jadilini hoja, hoja ya mwenye hoja siyo kuongeza au nini iwe *ring-fenced*; ndio hoja yenyelewe. Wale wasiozungumza kule nyuma nani, Mheshimiwa Mgaya!

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. NEEMA M. HAMID: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kuungana na Mbunge mwenzangu wa vijana, Mheshimiwa Ester Bulaya, Serikali ihakikishe fedha za vijana hazitumiki katika masuala mengine. Ninaunga mkono kwamba, pesa zetu zitumike kwa matumizi yetu tu na si vinginevyo. Vilevile zile za mwaka jana tupewe na za mwaka huu tupewe kama zilivyo. Kwa hiyo, bilioni nane tunahitaji ziende kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nchemba Mwigulu!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. NCHEMBA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Ester Bulaya, kwa hoja yake ya vijana na utetezi wake wa vijana tangu aingie Bungeni. Vijana wanamwamini yeye siyo tu wa Bunda hata wa maeneo mengine ya Tanzania nzima. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii ya kuziweka fedha maalumu kwa ajili ya vijana ni hoja ambayo inatakiwa itekelezwe kuanzia kwenye chanzo cha fedha. Mtakumbuka katika maeneo mengine ambayo tuna *ring-fence* fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali, tuna *tuna-ring fence* kuanzia kwenye chanzo chake; kwa mfano, za barabara kuna chanzo maalumu ambacho fedha yake ni maalumu kwa ajili ya Mfuko wa Barabara. Vivyo hivyo na kwa ajili ya REA na fedha ambazo zinaenda kwenye Mfuko wa Elimu ya Juu. (Makofii)

Kwa hiyo, kauli ya Serikali niseme tu kwamba, sisi kama Wizara tumeliona jambo hili na tunategemea tutakapoleta *Finance Bill*, tunategemea tuangalie uwezekano wa kubainisha chanzo ambacho kitaenda moja kwa moja kwa ajili ya Mfuko wa Vijana. Tukiendelea na utaratibu huu wa kutenga tu fedha halafu mgawanyo wake utegemee kipato, ni kweli zitakuwa zinatoka kufuatana na fedha iliyopatikana, kwa sababu tukiweka kwenye Mfuko mmoja tunalazimika kugawanya kidogo kidogo kwenye mahitaji mengine ya Serikali, ambayo nanyi mnatambua kwamba tuna ufinyu wa bajeti.

Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Ester, arudishe tu Shilingi ya Waziri wa Wizara hii na tumpe *commitment*. Naliomba Bunge tutakapoleta mapendeleko ya vyanzo vya mapato wakati tunajadili Muswada wa Fedha, basi tubainishe na chanzo maalumu ambacho kitakuwa kinaelekea kwenye Mfuko wa Vijana na hiyo itakuwa tiba ya kudumu ya fedha kuwafikia vijana.

Tatizo la vijana na mimi linanigusa, nilipomaliza Masters nilifanya kazi ya kupakia tofali na kubeba zege. Kwa hiyo, natambua sana uhitaji wa kuwa na chanzo cha kuwapatia mfuko ili waweze kuendeleza ujasiriamali. (Makofii)

Nakala ya Mtando (Online Document)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Bulaya!

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri, lakini kama Naibu Waziri anzeni kufikiria huko chanzo cha upatikanaji wa fedha za vijana, mkituletea *draft* hapa sisi tuboreshe; lakini siyo sisi humu ndani tuanze kufikiria, ninyi huko muanze kufikiria halafu sisi tuje kuboresha. Hili suala limekuwa la muda mrefu na kwa *commitment* ya Serikali, narudisha shilingi, tutakutana katika Wizara ya Fedha.

MWENYEKITI: Wizara ya Fedha au ile *Finance Bill*?

MHE. ESTER A. BULAYA: *Finance Bill*.

MWENYEKITI: Tuendelee, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, hayupo! Mheshimiwa Josephat Kandege!

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi na tangu Mheshimiwa Waziri alipokuwa Naibu Waziri, nimekuwa naongelea kwa muda mrefu sana, juu ya kutopatikana kabisa kwa mawasiliano ya TBC pamoja na Televisheni yake.

Wengine wanaongelea juu ya kutosikika, mimi kwangu haipatikani kabisa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kandege, naomba unisikilize. Hiyo hoja imeletwa na Mheshimiwa Barwany, kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni zetu, huwezi kurudia jambo ambalo limeshasemwa tayari. Kwa hiyo, hoja yako imekwisha. Huwezi kurudia jambo ambalo limeshasemwa na mtu mwingine. (Makofii)

Mheshimiwa Martha Mlata!

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa naomba ieleweke kwamba, kwenye suala la sanaa kuna mashirikisho ambayo yamekuwa yakishughulikia shughuli zote za sanaa mbalimbali. Wizara imekuwa ikionekana haishirikiani na mashirikisho haya na wala haitekelezi yale ambayo mashirikisho yamekuwa yakipendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kumekuwa na mchakato wa Stika za TRA ambazo ni wazi kabisa stika zile zimekuwa kwa ajili ya kukusanya mapato

Nakala ya Mtando (Online Document)

na wala si kwa ajili ya kulinda kazi za wasanii. Bado stika zile namna ya kupatikana, ukimchukua mtu anayetoka Kigoma au Tarime ni vigumu sana kuweza kuzipata. Mfumo ule wameuanzisha juu badala ya kuanzia chini.

Kuna mapendekezo mazuri sana ambayo yanaweza yakatekelezeka, yanaanza kwenye mashirikisho. Hivyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri, anisaidie ni lini Wizara yake itayatambua mashirikisho haya na kusikiliza yale ambayo mashirikisho yanapendekeza kwa ajili ya kuboresha shughuli na kazi za sanaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitapata majibu mazuri, mimi leo kwa mara ya kwanza, naomba niondoke na Shilingi ya Waziri. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Martha Mlata na msanii, kwa juhudzi zake anazofanya kuwatetea wasanii wenzie. Niseme tu kwamba, Serikali haishindwi kutambua mashirikisho na inayatambua kabisa, lakini kuna juhudzi mbalimbali zimefanyika. Tangu Mheshimiwa Makala akiwa kwenye Wizara hii, amekutana nao, wakabadilishana mawazo na BASATA, sasa *from there* ndiyo unapoanza sasa uone namna gani unaweza kutoa mchango wako katika kuboresha hizo kazi.

Nataka niseme tu kwamba, kwa kweli Serikali inatambua kuwa sanaa ni biashara. Sanaa pia inajumuisha fani mbalimbali kama vile muziki, filamu, uchongaji, uchoraji, mitindo na hata ngoma. Sasa juhudzi za Serikali kwa mfano, kupitia COSOTA, BRELA, Shirika la Milki Bunifu Duniani (WIPO), wamefanya utafiti kama unakumbuka mwaka 2012, ambao unaonesha jinsi gani sanaa inachangia katika kuendeleza na kukuza Uchumi wa Taifa letu.

Kwa mujibu wa utafiti huo, sekta hii inachangia ajira kwa asilimia 5.6 na mchango wake kwenye GDP ni almost 4.6. Kwa umuhimu huo, Serikali inachukua hatua kubwa sana, kurasimisha kwanza ile kazi yenye kazi ya sekta ya muziki na filamu, ambayo inajumuisha Wizara tatu; Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Fedha kupitia TRA.

Kwa hiyo, Serikali inafanya juhudzi sana za kilitambua hili jambo. Nasi tuseme tu kwamba, kwa kweli tunatambua na tunashirikiana nao na ndiyo maana hata leo wengi walikuwepo hapa kuona namna gani Wizara hii ambayo ndiyo mlezi wao Mkuu, inatoa mchango gani katika kuwasaidia.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Kuwa hiyo, nikuombe tu, kwa kweli ukiondoa Shilingi ya Mheshimiwa Waziri au ya kwangu, nami jirani yako bwana, please!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mlata!

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naondoa shilingi, kwa sababu haya mambo anayazungumza ndiyo ambayo yamekuwa yakizungumzwa takribani miaka karibu tisa sasa niko ndani ya Bunge hili. Ni kweli kabisa kwamba, Serikali imechukua hatua madhubuti katika kuhakikisha kazi za wasanii zinawekwa katika hali nzuri, lakini bado. Huwezi ukataja hela zinazochangiwa na wasanii hapa wakati bado hujawatambua hata kisheria. Ule ni utamaduni, lakini bado unaenda kukusanya kodi kwa mtu ambaye hujamtambua kisheria.

Ndiyo maana tunasema, hamtaki kukaa na yale mashirikisho. Hamtaki kukaa na sisi mtusikilize tunataka nini. Wasanii wamekuwa wakiumizwa, mtu anaingia studio anarekodi, anakuja mwenye pesa zake anachukua kazi ya sanaa anaipeleka COSOTA eti ni ya kwakwe. Ninyi mko wapi? Hakuna Wanasheria, wala vyombo ambavyo vinaweza vikasimamia kwa sababu ninyi mmewaacha.

Ukienda BASATA, vile Vyama vimeshafukuzwa mpaka kwenye zile ofisi. Kuna Chama cha Wasanii Wanawake wameshafukuzwa BASATA. Waziri unalijua hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Wizara hii haijatoa kipaumbele katika kazi za wasanii. Tunataka itambuliwe kwamba, ni kazi kama kazi nyingine siyo utamaduni. Ndicho ninachokitaka hapa, ni lini mtatambua kazi za sanaa kwamba ni ajira kama kazi nyingine? Siyo utamaduni kama ambavyo mnamatamka hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nasema hivi, ukiangalia katika Sheria ya COSOTA, tangu miaka nenda rudi, Sheria zile zimetekelezeka vipi? Hakuna hata kimoja ambacho kinatekelezeka. Hata hizo stika tunazosema za kuzuia piracy, hakuna Sheria yoyote ile inayomfanya mtu amshitaki mtu aliyemkamata na kazi haramu za Msanii. Sana sana akienda Mahakamani atachajiwa laki mbili na kazi yote ya mamilioni anapewa anarudishiwa. Wizara hii ipo.

Mimi naomba jamani mnisaidie, leo niondoke na Shilingi ya Waziri nikagawane na Wasanii wezangu. Watu wanakufa wakiwa maskini na vipaji wanavyo. Naomba wengine wanisaidie.

Nakala ya Mtando (Online Document)

MWENYEKITI: Hoja ni nini?

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni kwamba, Wizara hii kwa nini isikae chini ishirikiane na yale mashirikisho ili waweze kutengeneza Sera itakayosaidia kukuza na kulinda haki na kazi za Wasanii.

MWENYEKITI: Kuna tofauti kati ya Sera na Sheria. Sasa wewe unasema Sera ama Sheria?

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyote kwa sababu unapokuwa na Sera ndipo unapokuwa na Sheria.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ridhiwani!

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kuwapa pole Wasanii kwa sababu mkasa walionao ni mkubwa sana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa lililokuwepo hapa nafikiri ni kukosekana kwa Sera ambazo zinaweza kuongoza utekelezaji mzuri wa majukumu haya. Nasema hivi kwa sababu mimi binafsi yangu kwa tafsiri ya Stika za TRA, maana yake ni kwamba, Serikali inajipa nafasi ya kutambua ni kazi ngapi ziko mtaani na kiasi gani wanaweza kupata, lakini ulinzi wa kazi za Wasanii bado kabisa na hapa ndiyo kwenye tatizo. (Makofii)

Tatizo hili ni kubwa sana. Leo hii tunashuhudia, unakwenda kufanya duplication ya kazi zako unatoa kazi 200, lakini baadaye kuna mtu anapiga kazi nyingine mia mbili zinatoka zinakwenda kwenye njia za panya. Hata huyo Askari anayekwenda kukamata kazi hizo anaanzia wapi? Sheria inayomwongoza ni ipi? (Makofii)

Leo hii nasikia sijui kuna kitu kinaitwa Kamisheni ya Kukamata. Nimeona juzi kwenye TV wamekamata watu Kariakoo kule, lakini ukiangalia kwa upande wa Sheria si kazi ya Kamisheni ile ukaangalia hizo kazi wanazozifanya. Kazi yake ni kuangalia quality. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niungane na dada yangu Mheshimiwa Martha, lakini kwangu mimi ni ushauri kwa Serikali kwamba, sasa muda umefika wa kuliangalia jambo hili katika uzito huu, ili tuweze kuwalinda watu hawa, waweze kupata stahiki ya kazi yao na siyo Serikali kupata mahitaji ya kodi yao. (Makofii)

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja ya Dada Martha. (Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kafulila!

Mhe. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia naungana na mtoa hoja kwamba, tuna tatizo kubwa kama nchi, kutazama sura nzima ya masuala ya sanaa kwa maana ya sanaa kwa ujumla wake kama sura ya tamaduni.

Kimsingi, huu ni ulimwengu wa biashara. Kwenye ulimwengu wa biashara, sanaa ni uchumi. Wizara nadhani hakuna shaka kwamba, inakubaliana na sisi kwamba, Wasanii bado hawajatazamwa katika sura ya kazi ya kiuchumi. Hili nimelieleza hata wakati nachangia Hotuba ya Viwanda na Biashara kwamba, ukiangalia taarifa za Serikali katika maeneo ya uchumi, eneo la sanaa halitazamwi katika sura ya uchumi. Kwa hiyo, matokeo yake ni rahisi kusahaulika. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokionba sisi ni kwamba, Serikali ni lazima iwe na Sera, Sheria na Mkakati ambao unaonesha sanaa katika sura ya kibiashara na kiuchumi. Hiyo ndiyo njia pekee ya kuondoa Wasanii wa Tanzania katika lindi la umaskini na majina makubwa. Wanafanya kazi kubwa, jasho lao linaliwa, kwa sababu tu mfumo uliopo siyo mfumo wa kibiashara, bado tunatazama sanaa katika sura ya mambo ya kiutamaduni zaidi kuliko uchumi na biashara. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri akubaliane na atuambie sisi kama Bunge anafanya nini.

MWENYEKITI: Muda wako umeisha; Naibu Waziri wa zamani wa Habari, Mheshimiwa Makalla!

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Martha Mlata ina mashiko na kwamba, nia ya Serikali ya kwanza ilikuwa ni kuhakikisha inalinda haki za wasanii mbali ya mapato. Serikali imefanya jitihada nyingi, katika kufikia hatua hii, tumeshakutana na mashirikisho mbalimbali katika Wizara yetu, tumefanya mikutano na walitoa *input* nyingi sana ambazo zimetusaidia angalau kuboresha. Nataka niseme, zipo changamoto ambazo Serikali nasi tunazipokea, tutaendelea kukutana nao ili tuweze kukabiliana na tatizo hili ambalo linapelekea kupotea kwa mapato kwa wasanii wengi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hoja ya msingi na Serikali tunaichukua, tutashirikiana nao na kuifanyia kazi na kwamba, ushauri uliotolewa ni wa msingi utatekelezwa.

Nakala ya Mtando (Online Document)

MWENYEKITI: Waziri wa Habari, huyu anachangia wewe ndiye Waziri mwenyewe. I hope mnailewa hoja ya huyu jamaa. Kabla ya hapo, hoja yake siyo suala la mapato, anataka Sheria na Sera.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. NCHEMBA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wasanii wa Tanzania wangepata kipato kinachostahili wangekuwa na uchumi tofauti na walivyo sasa; na ni kweli wasingevunjwa moyo kwa kazi yao kupotea hata Serikali ingepata kipato kikubwa zaidi kwa sababu wangekuwa wanalipa zaidi ya sasa ambavyo kazi nyingi inapotelea kwa wasiohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mlata amekuwa akilirudia hili jambo na nimpongeze kwa hilo. Niseme tu sisi kama Wizara ya Fedha kupitia Mamlaka ya Mapato, tutakutana na wenzetu wa Wizara inayohusika, kuishirikisha COSOTA ili kuweza kupata mawazo yao tuweze kuboresha sasa wazo hili ambalo kwa sasa limeonekana bado lina upungufu, kutengenezea Sheria pamoja na Sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Wabunge tusiishie tu kwenye Sera ambayo italinda namna ya kutengeneza Stika, nitawaomba tutakapofika wakati huo, hata adhabu kwa wale ambao watafanya kosa hilo, kwa kweli inatakiwa iwe kali ili kuwafanya wale watu waweze kuogopa kufanya kitendo hicho ambacho kimekuwa kikiwahujumu watu hawa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Mlata, achukue commitment ya Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Habari ambayo ina bajeti leo, kwamba, jambo hili tutahusisha wadau wote ambao amewataja ili tuweze kupata kitu ambacho kitawahakikishia wasanii kwamba, hawatapita kwenye mlolongo wa tatizo la aina hii ambalo amelipata.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, hoja yake anasema iwepo sheria, habari zingine zitakuwa after.

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninaungana na wasemaji waliopita; Naibu Waziri wa Fedha pamoja na Naibu Waziri wa Maji, katika kusisitiza hii hoja ambayo ameizungumzia Mheshimiwa Mlata. Ni kweli kwa kiasi kikubwa, tunatambua hilo tatizo na tulijitahidi kukutana na mashirikisho mbalimbali na tunashughulikia Sera ya Utamaduni tunaibadilisha ili iweze kutoa nafasi ya kuhakikisha zile sheria mbalimbali zinabadilishwa ili kuweza ku-facilitate haya mashirikisho mbalimbali.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelizingatia hilo na hata COSOTA na TRA ndiyo wanaoshughulikia hilo kwa kiasi kikubwa.

MWENYEKITI: Huyu anasema anataka Sheria, ninyi mnazunguka vipi?

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria itakuja baada ya Sera ya utamaduni kupita. Sera ya Utamaduni inatoa nafasi kwa Sheria kuweza kutengenezwa itakavyoweza kufocus katika fani zote za sanaa.

MBUNGE FULANI: Lini?

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Swali la nini hiyo inategemea na ratiba mbalimbali za kiserikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mlata ndiye mwenye hoja, usiwajibu watu ambao hawana hoja.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninamshukuru Naibu Waziri wa Fedha, kwa commitment yake alioitoa, kwa mipango mizuri ambayo ameahidi kwamba itafanyika; inaleta matumaini. Pia naomba nimshukuru Waziri, isipokuwa tu nimwambie kwamba, Sera ya Utamaduni hairuhusu kuwa biashara. Kwa hiyo, ninaomba kwenye Sera ya Utamaduni kwa sababu sisi kama shirikisho tulitengeneza Sera ya Kazi za Sanaa; ndiyo maana nimeomba mkutane na yale mashirikisho ili kuweza kutofautisha utamaduni na hii inakwenda kwenye ajira. Hapo litakuwa limeeleweka na litakaa vizuri ili kupelekea kupatikana Sheria itakayoweza kusimamia kazi zetu za sanaa, zikiwemo alizotamka adhabu na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya hayo, ninaomba nirudishe shilingi ili haya mambo yaweze kutekelezeka vizuri. Ahsante. (Makofii)

MHE. JOSEPH D. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka maelezo na very seriously vinginevyo nitatoa shilingi. Nataka Waziri au Naibu Waziri waniambie ni lini Muswada wa Sheria ya Habari, by timeline utaletwa hapa? Muswada huu mimi nimeanza kuusikia toka nimeanza kuingia kwenye Bunge hili na kabla hata sijaingia huko nje ninasoma kwenye magazeti. Toka Gazeti la Mfanyakazi lipo wanaandika kuhusu Muswada huu utakuja na uzuri Naibu Waziri ameelezea imani yake kwa

Nakala ya Mtando (Online Document)

Muswada huu na ameelezea matumaini yake kwa Muswada huu. Ninataka kujuua Muswada huu utakuja lini?

Muswada huu ni tatizo. Tutakaporekebisha hii sheria ndipo tutakapoweza kufanya tasnia hii ya habari, wanahabari na wafanyakazi wengine kwenye hii tasnia, wafanye kazi kwa uhuru, kwa amani na kwa weledi kuliko ilivyo hivi sasa; usalama hakuna, watu katika mazingira ya sheria hii wanang'olewa kucha, wanang'olewa meno, hamna namna yoyote ya kujisaidia, magazeti yanafungiwa kiholela kwa sababu anayetafsiri sheria ni mahakama. Sasa iwapo Sugu ametukanwa au mtoto wa Rais kaandikwa kwa ujisadi, inatakiwa yeze ndiyo aende Mahakamani kushtaki na siyo Waziri au Wizara kuchukua sheria mkononi kwa kuamka asubuhi tu na kulifungia gazeti kama walivyolifungia Gazeti la Mwanahalisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anayekashfiwam Wizara siyo Mahakama, kama kuna kashfa kwenye vyombo vya habari, anayetakiwa kutafsiri ni mahakama na siyo Wizara. Kwa hiyo, nataka commitment vinginevyo nitatoa shilingi leo na nitatoa seriously. Nataka commitment, lini; timeframe; Muswada huu utakuja lini ili tubadilishe chapter? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoeleza wakati tunajibu hoja, Muswada huu wa Sheria lengo lake kubwa ni kuwasaidia Waandishi wa Habari, wala siyo Mbilinyi, siyo mimi wala siyo mtu mwagine.

Sasa hawa walengwa ni lazima wafaidike, lakini kabla hawajafaidika na Muswada huu ni lazima Muswada huu uhakikishe kwamba maeneo yote ambayo yana upungufu katika tasnia ya Habari katika nchi hii yanawekwa sawa. Utakuja hapa Bungeni, ukiniambia lini hata ukiniwekea kisu hapa siwezi kukwambia kesho.

Ninachosema ni kwamba, Kamati ya Maendeleo ya Jamii ilikwenda India imekusanya, imepeleka maoni yake, watu wengine wamekwenda UK wamekusanya maoni, wengine wamekwenda South Africa wamekusanya maoni, ile draft imeshatengenezwa kinachosubiriwa sasa ni kuletwa hapa.

Mheshimiwa Mbilinyi, lakini ngoja nikwambie Mheshimiwa Mbilinyi, nchi hii ndiyo nchi yenye uhuru wa Vyombo vya Habari kuliko nchi nyingine yoyote Duniani

MWENYEKITI: Unamwambia Mwenyekiti siyo Mbilinyi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ina uhuru mkubwa wa Vyombo vya Habari na ndiyo nchi inayoongoza kwa kuwa na Magezeti mengi Duniani. Wewe unasema aah kwa sababu hujui, inawezekana haujatembea. Jinsi Vyombo vya Habari vya nchi hii vinavyoandika, uhuru huu haujawahi kuonekana Duniani kote, *trust me, believe me or not!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu utakapokuja inawezekana kabisa baadhi ya magazeti yakapungua au redio zikapungua, lakini lengo lake ni kuwasaidia hawa Waandishi wa Habari. Leo kuna baadhi ya Waandishi wa Habari wanafanya kazi hawalipwi mishahara, wanalipwa per piece; mimi nimetoka huko ninajua, Sheria hii ndiyo itakayowasaidia hawa.

Kwa hiyo, Joseph nikueleze tu...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mbilinyi.

MWENYEKITI: Mwenyekiti, wala siyo Joseph wala siyo Mbilinyi.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Ninaomba rafiki yangu ajue kwamba, kweli Muswada huu unakuja. Nami nina imani kubwa sana kwamba, Muswada huu utakapokuja ndiyo utakaokuwa mkombozi wa tasnia ya habari katika Taifa letu. Lini? Be patient, tayari ugali upo jikoni tusubiri usogezwe mezani tuje tule, hatuna sababu ya kusema lini, lakini I am sure kwamba utakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanahabari mimi ni Mwanahabari mwenzao na ningependa pia na mimi kuwa na legacy kwamba, kwa kipindi kile na Waziri wangu tulitengeneza kitu hiki, kimejenga mazingira mazuri kwa Waandishi wa Habari ili na wao wafaidike.

MWENYEKITI: Si hivyo tu, hata Bunge liliagiza hivyo kwamba, amendment iliyokuwa imeletwa hapa ilahirishwa ili kusudi kije kitu kimoja complete. Mheshimiwa Mbilinyi!

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, seriously nakusudia kutoa shilingi.

WABUNGE FULANI: Toa!

MWENYEKITI: Endelea.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri amesema tuwe patience, patience is no more Mzee. Muda mrefu sana patience no more, tumekaa kwenye viti mpaka viti vinakuwa na moto. Naomba nikwambie kwamba, natoa shilingi ili ushindwe kwenda kuhiji tena.

MWENYEKITI: Ukishatoa shilingi unajenga hoja.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo najenga hoja zangu hivi. Waziri amesema kwamba, Muswada huu ni kwa ajili ya kuwasaidia Waandishi, hamna aliyekataa. Mimi ni Waziri Kivuli wa Habari na haya ninaongea hapa kwa kuwatetea Waandishi ambao anasema wapo kwa ajili ya huu Muswada, ndiyo maana wadau wenyewe wa Habari walitaa *input* zao. Anasema michakato inaendelea, michakato ilishakwisha miaka mingi; MCT na Vyombo vingine vyote vya Wadau wa Habari, walishatoa *input* zao kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia kuhusu uhuru, kwamba, magazeti yapo mengi sasa; uhuru hautakiwi uwe kwa huruma na busara za Rais Kikwete sasa, atakayekuja tutajuaje kwamba atakuwa na huruma. Kuna haja gani unakuwa na magazeti 1,000 ambayo kesho asubuhi unaweza ukaamka ukakuta yote yamefungiwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka mambo yawe kisheria, Muswada uje ili hayo magazeti mengi tuwe na uhakika kwamba, mimi nasoma Mwanahalisi kila siku, kila Jumatano au kama linatoka Alhamisi, kila Alhamisi nitapata Gazeti la Mwanahalisi. Unajua kufungia magazeti kwa mfano, Waziri tu ana tatizo na Mhariri anafungia gazeti, utafikiri Mhariri ndiye anayeendesha lile gazeti peke yake. Utakuta behind kuna watu kama 200, 300 kwenye lile gazeti, mpaka venders wa magazeti wanasomesha watoto kwa ajili ya kuuza hilo gazeti ambalo ninyi mmeilifungia kiholela kwa sababu sheria hamna. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi na ninaomba Bunge zima liniunge mkono kwa ajili ya Waandishi wa Habari.

MWENYEKITI: Ngoja kwanza, shilingi neno lenyewe shilingi ni hoja. Inatakiwa yule mtu anayetoa hoja sisi tumuelewe tunamuunga mkono nini. Hayo mengine ni maudhui, lakini hoja ni ipi. Muswada umefanyaje? Hoja ni ya Mbilinyi, ninyi wengine wote siyo hoja yenu.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nipewe date, timeframe, kwamba, Muswada huu wa Sheria ni lini utaletwa Bungeni kwa

Nakala ya Mtando (Online Document)

sababu Mheshimiwa Waziri amesema tuwe patience, patience no more, viti ni vya moto tumekaa mpaka tumechoka. (Kicheko)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha mbwembwe za kijana mwenzangu pale, hoja yake ina mashiko.

MWENYEKITI: Mbona ninyi mna maneno maneno tu, hamuwezi kuvumiliana hata kidogo, hebu endelea Ester. (Kicheko)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema ukiacha mbwembwe na swaga zake Mheshimiwa Mbilinyi, hoja yake ina msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Muswada wa Habari, nakumbuka tangu aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mama Jenista Mhagama, ambaye leo hii ni Naibu Waziri, amelizungumzia sana kwa uchungu na kila siku alikuwa akiihoji Serikali ni lini mtaleta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umetoka kutukumbusha hapa kwamba, tulimkatalia Mwanasheria Mkuu, tukishirikiana na Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Tundu Lissu, walete Muswada uliokamilika. Walete msumeno utakaong'ata kotekote, ambao utajali masilahi ya Waandishi wa Habari na utaweka misingi ya imara ya kuhakikisha Waandishi wa Habari wanafuata ethics za Uandishi wa Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala tumeliongelea muda mrefu, tangu tumeingia Bungeni hapa mwaka 2011, mchakato gani usioisha? Wanasema subira yavuta heri, lakini heri hii sasa inavuta shari. Serikali ni lazima iji-commit, bajeti iliyopita mlisema Muswada upo katika hatua ya Baraza la Mawaziri, leo hii mnatuambia muanze kuwashirikisha wadau, lakini kila mwaka mnasema mnashirikisha wadau; wadau gani hao wasioisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waandishi wanaendelea kuteseka. Kuna wengine wanatumia fursa hiyo kuandika habari za uchochezi, ndiyo tunataka chombo sasa cha kuwabana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na mbwembwe za Mbunge mwenzangu wa Mbeya Mjini, hoja yake ni ya msingi na ninaiunga mkono. Serikali leo iji-commit ni lini italeta Muswada wa habari?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mkosamali!

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la Muswada unaletwa lini, tumeshauliza maswali kwenye Bunge hili zaidi ya mara 40. Mheshimiwa Lukvi alishajibu, Mheshimiwa Nchimbi alishajibu, Mheshimiwa Makalla alishajibu, kila mtu alishajibu, Mheshimiwa Jenista akiwa huko hadithi za Muswada unakuja lini, hawana majibu hawa watu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameshajibu Mawaziri zaidi ya kumi swali hili wanasema tutaleta, sisi hatuko huko. Tunajua kwamba, Serikali makini inakuwa na ratiba. Sasa mambo ya uwongo, juzi nilisema hapa kwamba, uwongo wa Muswada huu tumeshachoka, wadau waliandaa Muswada huu tangu mwaka 2007, watu wamezungumza. Sasa hawa hata tukiwaambia jibu la lini, hawawezi kujibu. Jambo la msingi kwa sababu Bunge lilishaagiza, baada ya ile Amendment kuletwa Bunge, liliagiza kwamba uletwe Muswada. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba wewe mwenyewe, uwaagize siku ya kuleta huu Muswada. Wewe ndiyo uwaagize, hawana jibu hawa la kuleta. Ukiwaambia lini ni kujikanyagakanyaga tu na kutupotezea muda. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waagize walete lini, lakini ukisema wajibu wale, tunapoteza muda, jibu la lini hawana hawa! (Kicheko)

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi ninataka niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Mbunge. Hoja hii ni ya msingi sana. Ulipokuwa ukizungumza hapa ulieleza kwamba, hili ni Azimio la Bunge na kwamba, tunaomba wenzetu wasiendelee kuja na Muswada binafsi ili Serikali itemize wajibu wake wa kuleta Muswada ambao utalinda masilahi ya Wadau wote wa Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha na pengine Bunge letu lifike mahali sasa kuwa na Kamati inayofuatilia Maazimio ya Bunge. Bunge haliwezi kuazimia jambo halafu likaendelea kubaki na maelezo ambayo hayajitoshelezi kama haya ambayo Naibu Waziri ameyaeleza hapa. Tunataka Serikali iseme imekwama wapi? Kama mmekwama mtueleze sisi tulete Muswada huo hata katika Mkutano ujao wa Bunge. Hali yetu ni mbaya na sjui kwa nini watu hawataki kuona. Ukiacha kwamba vyombo vingine vya habari vimefungiwa ambavyo hata mimi sifurahii, lakini ukweli ni kwamba, kuna uandishi usiokuwa wa kizalendo na ambao ni wa kulinda masilahi ya makundi na usioheshimu, usioandika na kuanika uhalifu wa rasilimali za nchi, kwa sababu tayari vyombo vya habari vingine vinasimamia maslahi ya wale wanaomiliki na wale ambao wanawaunga mkono. Leteni Muswada turekebishe wadau wote wapate haki

Nakala ya Mtandao (Online Document)

yao. Simameni tuelezeni mmekwama wapi, mlipokwama tutawasaidia kukwamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mbilinyi. (Makofi)

MWENYEKITI: Sasa hapa ni *commitment*, Serikali mnahitajika. Naomba mseme, ni utaratibu! Naomba mjibu ni lini mnaleta Muswada huu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri kwenye ukurasa wa 9, paragraph ya kwanza, naomba kunukuu: "Mheshimiwa Spika kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara imekamilisha maandalizi ya Muswada wa sheria ya kusimamia vyombo vya habari na sasa uko katika hatua nzuri. Kwa kuzingatia utaratibu uliopo, Muswada huu utafikishwa katika Bunge lako tukufu lijalo la kutunga sheria". Mwisho wa kunukuu. (Makofi)

Kwa maana hiyo, Bunge litakalokuja la kutunga sheria, siyo Bunge la Katiba, maana siyo kuja hapa tena Bunge la Katiba mkaanza kuuliza. Ni Bunge la kutunga sheria. Kwa hiyo, tutauleta.

MWENYEKITI: Kutokana na kuingiliwa na Bunge la Katiba, leo saa mbili tutakutana na Kamati ya Uongozi kuangalia ratiba mpya ya vikao vya Bunge kipindi kinachokuja. Sasa ni kweli kwamba hamuwezi kupilisha Bunge hili. Bunge la Kumi na Tano ni la Bajeti. Sasa kule atakwenda Mheshimiwa Lukuvi tutakapopanga atatuambia ni hoja gani zinaingia katika kipindi hicho tutakachokubaliana. Mheshimiwa Lukuvi! Mheshimiwa Lukuvi. (Kicheko)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuja na hiyo orodha ya Miswada kwa ajili ya huo Mkutano, kwenye Kamati ya Uongozi.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, wote wana hata upande wa pili wanahudhuria, watashuhudia huko, kikao baada ya saa mbili tukitoka hapa tuna kikao Kamati ya Uongozi kupanga mikutano iliyobaki baada ya hapo, maana yake tukitoka hapa kutakuwa na Bunge la Katiba. Kwa hiyo, ratiba tunabadilisha kidogo. Mheshimiwa Mbilinyi ndio hoja yako bado. Usimuulize Mchungaji, bwana wee! (Kicheko)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, no, no, no, simuulizi Mchungaji. Kwa sababu hapa nimechanganyikiwa kidogo, Mheshimiwa katoa maelezo na Kiti kimetoa maelezo. Sasa unaweza kunipa option nichukue

Nakala ya Mtandao (Online Document)

maelezo ya Kiti chako na uyarudie tena kama maagizo kwa Serikali, tafadhalii Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Sawa, kwa hiyo umerudisha shilingi?

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Bado, naomba msaada huo tu kidogo, yaani sielewi maelezo nichukue yepi, aliyotoa Mheshimiwa Lukuvi, aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri, maana yake Naibu Waziri kasema kwanza tuwe patient. Lakini, baadaye anasema kila kitu kiko sawa kwenye kitabu. Halafu wewe umetoa maelezo kwamba baadaye saa mbili kuna Kikao.

Sasa mimi ningependa nichukue maelezo yako Kiti, kwa sababu maelezo haya ya Mawaziri kama alivyosema Mheshimiwa Mkosamali, zaidi ya Mawaziri 13 wameshatoa majibu hapa ambayo hayajafanya kazi na mimi nakuamini Kiti, kwa sababu ndiye Boss wangu.

MWENYEKITI: Ninachokisema ni kwamba, tuna ratiba mpya ya vikao kwa sababu zamani tulikuwa na miezi ya vikao, lakini safari hii kidogo ndiyo hicho kikao tunaenda kufanya jioni hii. Ndiyo maana nikamwingiza Mheshimiwa Lukuvi. Hizo siku mnazosema iko katika hiyo hatua, vinaweza kuingia katika vikao hivyo mwaka huu? Maana yake hivi vikao ni vya mwaka huu. Ndiyo hicho nilichokuwa nasema na bahati nzuri pande zote hata upande wa Kambi ya Upinzani wanashiriki kikao hicho. Kwa hiyo, watashuhudia maneno yatakayozungumzwa huko. Kwa hiyo, naomba urudishe kusudi tusimamie kwa mtindo huu.

Ni kweli kwamba hiki kitu ni cha miaka mingi. Ni cha miaka mingi. Mimi nimekuwa Naibu Spika, nimeshiriki katika mkutano mmojawapo uliokuwa wa Waandishi Habari wanazungumzia Muswada huo. Ni ya siku nydingi, kwa hiyo tutasimamia. Mheshimiwa Mbilinyi, naomba ukubali hiyo.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima yako Kiti, none of these Ministers ambao nachukua kauli yao, nachukua kauli ya Kiti. Asante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla!

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote niweke wazi kwamba nitatoa shilingi endapo sintopata maelezo ya kueleweka.

Hoja yangu inayonifanya nisimame hapa ni kutaka kupata ufanuzi kutoka kwa Serikali kuhusiana na hoja ya kuanzisha mpango maalum wa maendeleo ya vijana ambapo ndani yake kulikuwa kuna mambo yafuatayo:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mpango huu ni Azimio la Bunge la tarehe 4 Februari, 2013. Katika Azimio lile, tulianzimia...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, limezungumzwa mpaka tumepiga kura. Mpaka tumepiga kura!

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Hapana, ni kitu tofauti.

MWENYEKITI: Aaa, sipendi kubishana na wewe. Hivyo ndivyo tumezungumza, hoja imeletwa na Mheshimiwa Ester Bulaya, tumelizungumza, tena kwa kuondoa shilingi, siyo tu hivi hivi, kwa hiyo limezungumzwa. Mheshimiwa Gekul.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti,...

MWENYEKITI: Naomba nisimame sasa, Mheshimiwa ulikuwa haupo, nilikuita, hukuwepo, bahati mbaya unasema kitu ambacho tayari kimeishapita. Mheshimiwa Gekul tuendelee na kifungu ulichosema.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba tu ufanuzi, mimi langu siyo mshahara wa Waziri per se, lakini ni kifungu kidogo kwenye Subvote hiyo...

MWENYEKITI: Naomba tumsikilize, huyu siyo mshahara wa Waziri, anaulizia kifungu kidogo hapa, mki-note.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sub-vote 1001, item 220700 – rent expenses. Mwaka huu zimetengwa shilingi 1,237,015.000/=. Naomba nipate ufanuzi wa kina, fedha zote hizi ni za nini katika Wizara yenye bajeti ya bilioni 35 na majibu yasiporidhisha, niondoe tu shilingi. Naomba ufanuzi kwanza.

MWENYEKITI: Ahsante. Mmesikia hilo swali? Mmekiona kifungu? Mmekiona?

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki ni kwa ajili ya gharama za pango la ofisi na nyumba za viongozi za Dar es Salaam na Dodoma. Ongezeko ni kutokana na ongezeko la bei ya nyumba na pango lenyewe.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani nilitoa hoja.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Tumemaliza, hakuna namna. Huwezi kutoa hoja. Maana yake ni *rent*. Ni *rent*, kwa hiyo kama ni *rent* ukitoa shilingi inakuwaje? Kifungu hiki kinaafikiwa? Tuendelee.

Kif. 1002 - Finance and
Accounts.....Tsh.286,932,000/=

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa nakushukuru. Mheshimiwa Mwenyekiti, niko katika Sub-vote 1002 item 230400 *Routine Maintenance and Repair of Vehicle and Transport Equipment*. Mheshimiwa Mwenyekiti mwaka jana katika kifungu hiki kulikuwa na shilingi 7,200,000/= mara hii kuna shilingi milioni 21,420,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Randama wanaeleza katika mgao wao na mchakato wao shilingi 16,300,000/= zitatumika kwa ajili ya matengenezo na ununuzi wa vipuri na gari la Kitengo. Shilingi 5,120,000 watanunua matairi na betri, kwa mujibu wa Randama walionayo wao Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu shilingi 16,300,000/= juu ya matengenezo na ununuzi wa vipuri vya gari, 16,300,000/= kwa mujibu wa Randama mliyo nayo na mimi Randama ninayo. Kwa hiyo, ununuzi wa vipuri vya gari la Kitengo, siyo magari ya Kitengo, gari moja kuna ununuzi wa vipuri milioni 16. Napata mashaka kwamba kuna harufu ya ubadhirifu na ufisadi wa fedha.

Wanielimishe na waelimishe Watanzania wanaonisikiliza. Gari la Kitengo siyo magari ya Kitengo kama Randama inavyoeleza milioni 16, kuna kipuri gani au cha ndege?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi!

MWENYEKITI: Haya! Mheshimiwa, mmekiona kifungu anachouliza?

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinatumika kulipia gharama za matengenezo ya magari na ununuzi wa vipuri, ongezeko ni kutokana na mabadiliko ya bei katika soko na uchakavu wa magari ya Vitengo, siyo gari moja, nasema magari na ununuzi wa vipuri, siyo gari moja. Typing error mimi nadhani.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Nakala ya Mtando (Online Document)

Kif. 1003 – Policy and
Planning.....Tsh. 494,999,000/=

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye Sub-Vote 1003 – Item 221000 juu ya safari za ndani. Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na shilingi 29,186,000, mara hii kuna shilingi 47,680,000 kuna ongezeko la shilingi 18,500,000. Sasa tatizo lipo kwamba ongezeko hili na kwa mujibu wa Randama hakuna ongezeko la wafanyakazi na hakuna ongezeko la mambo mengine ambayo yangeweza kupelekeea ongezeko la shilingi 18,500,000. Naomba ufanuzi juu ya ongezeko kubwa la safari za ndani za kikazi za wafanyakazi hawa wakati mmeonesha kwamba hamtaajiri wafanyakazi wengine kwa mujibu wa shughuli hizi. Naomba ufanuzi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinatumika kulipia gharama za usafiri na posho ya kujikimu ndani ya nchi. Ongezeko hili ni kutokana na ongezeko la bei za tiketi, na watumishi watakaosafiri katika safari mbalimbali za kikazi kufuatilia majukumu mbalimbali ya Wizara.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1004 – Government Communication
Unit.....TSh.128,460,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1005 – Procurement Management
Unit.....TSh.222,255,000/=

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko katika Sub-Vote 1005 niko kwenye item 221400 - Hospitality supplies and services. Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana kulikuwa na shilingi 4,900,000, mara hii kuna shilingi 9,110,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika fedha hizi kwa mujibu wa Randama imeeleza kwamba shilingi 500,000 tu ndiyo zitatumika kwa ajili ya kutoa zawadi kwa mfanyakazi bora. Zizobakia zote ni kwa ajili ya chakula na chai. Ningombaa ufanuzi wa ziada kwamba hii chai ambayo mnataka kunywa

Nakala ya Mtando (Online Document)

mara hii mara mbili na chakula mara mbili zaidi kuliko mwaka jana ni chai ya aina gani? Naomba ufanuzi.

MWENYEKITI: Waheshimiwa, mmekiona kifungu chenyewe? Mmekiona? Haya maelezo.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki ni kwa ajili ya chakula na viburudisho wakati wa vikao vya kazi vya Kitengo. Vikao vyote, siyo kikao kimoja, kwa mwaka nzima, *financial year* nzima ile na pia hiyo zawadi ni kwa ajili ya mfanyakazi bora wa hicho Kitengo, tena ni nyingi na ongezeko ni kutokana na mabadiliko ya bei katika soko.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1006 – Internal Audit
Unit.....Tsh.198,500.000/=

Kif. 1007 – Information and Communication Tech
Unit.....Tsh.87,419,000/=

Kif. 1008 – Legal Service
Unit.....Tsh.85,588,000/=

Kif. 6001 – Culture Development
Division.....Tsh.2,897,977.000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 6002 – Youth Development
Division.....Tsh.995,234,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Mnyika. Mheshimiwa Jafo!

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kupata ufanuzi katika kasma namba 221400 ambapo mwaka huu bajeti hapo imeshuka karibu kwa milioni 100 ukilinganisha na mwaka uliopita.

Sasa najua Kitengo hiki ndiyo Kitengo kinachohusiana na suala zima la vijana. Kwa nini hapo bajeti imeshuka kiasi hicho, Je, zile zinazokusudiwa zinaweza kufanyika vizuri?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Hebu turudie kasma. Ni namba ngapi?

MHE. SELEMANI S. JAFO: Kasma namba 221400, kifungu hicho kimeshuka karibu kwa wastani wa shilingi milioni 100 uki-compare na mwaka wa jana. Kwa nini tofauti imekuwa kubwa kiasi hicho?

MWENYEKITI: Zima ya kwako. Okay, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kutokana na ukomo wa bajeti tu.

MWENYEKITI: Umemwelewa swali lake?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa kwamba ufinyu wa bajeti umefanya kuwe na *dundling* ya hiyo fedha.

MWENYEKITI: Samahani, bado, Mheshimiwa Mnyika nilimwita. Naomba Mheshimiwa Mnyika!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii. Nasimama kwa kasma 210300 – *Personal Allowance Non – Discretionary*, hiki kifungu cha posho ambacho mwaka jana kilikuwa na milioni 101. Mwaka huu kimeongezewa mpaka milioni 113 na Mheshimiwa Mwenyekiti nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 103, Kanuni ndogo ya 3 kutoa hoja ya kueleza kutokuridhika juu ya utekelezaji unaohusu kifungu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa mazungumzo juu ya kifungu hiki kwenye Mkutano wa Bunge uliopita, tulielezwa kwamba kifungu hiki pamoja na mambo mengine kina fedha kwa ajili ya vikao vya uanzishwaji wa Baraza la Vijana, Benki ya Vijana na Tathmini juu ya Mwenge wa Uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 103, naomba kutoa hoja ambayo nitaomba Wabunge wenzangu waniunge mkono ya kueleza kutoridhika na utekelezaji wa Serikali kwenye kifungu hiki. Matumizi ya pesa hizi na utekelezaji wa Serikali kwenye kifungu hiki.

MWENYEKITI: Kifungu namba gani?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu...

MWENYEKITI: Aaa hicho cha hoja!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kifungu cha Kanuni?

MWENYEKITI: Ndiyo.

MHE. JOHN J. MNYIKA: 103, Kanuni ya 3. Kwa madhumuni ya hoja ya aina hiyo 103 (2) na 103(3). "Vilevile Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja ya kuondoa shilingi moja katika kifungu chochote". (3) Madhumuni ya hoja ya aina hiyo ni kuwezesha Mbunge aliyetoa hoja aweze kueleza kutokuridhika kwake na utekelezaji wa jambo fulani mahsus ambalo ni dhahiri linahusika na kifungu hicho".

Mheshimiwa Mwenyekiti, na jambo mahsus ambalo nataka kulitolea hoja ya kutoridhika utekelezaji wake ni namna gani Wizara inatumia kasma za pesa kwenye kifungu hiki kwa ajili ya mchakato wa uundwaji wa Baraza la Vijana pamoja na Benki ya Vijana Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba niendelee kuitoa hoja hiyo.

MWENYEKITI: Ngoja tu niwaelekeze. Ndugu anawazungusheni tu, hapa ni kuondoa shilingi basi, ndicho anachokifanya. Hapa amewazungusha, lakini ni kuondoa shilingi. Sasa utupe exactly unauliza nini sasa?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri kuanzia ukurasa wote unaohusika na masuala ya vijana ukurasa wa 14 mpaka ukurasa wa 18. Hakuna mahali popote ambapo Mheshimiwa Waziri baada ya kumtengea pesa hizi za vikao vya kazi hii, ametoa mrejesho Bungeni ni hatua hatua gani imefikiwa katika mchakato wa uundwaji wa Baraza la Vijana Tanzania? Hili ni jambo ambalo haliridhishi kabisa. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata katika suala muhimu ambalo kama tungelifanikisha, leo vijana wangekuwa na pesa nyingi zaidi kuliko hata za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana la uundwaji wa Benki ya Vijana Tanzania, nalo Bunge halijaelezwa utekelezaji wake kwa kamilifu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba maelezo ya Wizara juu ya utekelezaji wa masuala yanayohusu uundaji wa Baraza la Vijana la Taifa na masuala yanayohusu uanzishwaji wa Benki ya Vijana Tanzania haturidhiki na utekelezaji wake na tunataka majibu ya msingi na naomba Wabunge wenzangu waniunge mkono kwenye jambo hili. (Makofii)

MWENYEKITI: Naomba kwanza, Randama inasema nini juu ya kifungu hicho? Si kwamba unabambikiza hoja kwenye kifungu chochote!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi simbakizi hoja.

MWENYEKITI: Aaa ngoja kwanza. Mbona wewe unaharaka hivyo!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Nataka kunukuu Randama.

MWENYEKITI: Naomba ukae, tumsikilize anisomee Randama kifungu *item* hii inasema nini. Nisomee *item* hii inasema nini? *Item* yenye? Atasoma mwenyewe anayehusika.

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yake ni kwamba, kifungu hiki hukutumika kwa ajili ya posho za ajira za lazima kama vile likizo, kazi za ziada, posho za vikao, posho za kukaimu, matibabu, bima, posho ya kujikimu na mavazi kwa wakimbiza mwenge wa uhuru. Ongezeko linatokana na mabadiliko ya bei katika soko hasa kwa vifaa na shuguli za Mwenge wa Uhuru. Kwa mwaka huu hizi hela tunazoomba zitafanya kazi hii.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni Kitabu cha...

MWENYEKITI: Hoja yako rudia tena tuielewe vizuri, habari ya Benki haipo hapo wala nini.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki iko hapo; hiki kifungu kwenye kitabu kikuu kinaonesha 210300, kwenye mchanganuo 210300 imegawanyika katika kasma ndogondogo mbalimbali.

Ndani ya hizo posho anazozzungumza Mheshimiwa Waziri, kuna kasma inaitwa 210314, ndani ya hiyo 310, yaani 310 kuna 310 moja, 310 na kuendelea. 210314 inasema hivi, posho za vikao imetengewa shilingi milioni 20.1 ina maelezo yafuatayo:-

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mwaka 2013/2014 shilingi milioni nne tu zilitengwa. Hadi Machi 2014 shilingi milioni 2.3 zimepokelewa na kutumika. Mwaka 2014/2015 shilingi milioni 20.1 zinaombwa kwa ajili ya kazi ya vikao vya uanzishwaji wa Baraza la Vijana, Benki ya Vijana pamoja na tathmini ya Mbio za Mwenge wa Uhuru. Kwa hiyo, naomba niendelee sasa kutoa Hoja yangu?

MWENYEKITI: Sawa.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa hoja kwamba, Wizara hii haioni kipaumbele, umuhimu wa kuwaunganisha vijana wote Tanzania bila kujali vyama kuwa na Baraza ambalo litawaunganisha vijana wote, Baraza ambalo vilevile litafuatilia maslahi yanayowahusu vijana, iwe ni fedha zao za maendeleo, iwe ni miradi mbalimbali! Wizara hii vilevile hailipи kipaumbele suala la kuundwa kwa Benki ya Vijana ambayo itatupatia ufumbuzi endelevu juu ya mikopo kwa vijana na mitaji kwa vijana kwa masharti nafuu! (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kasma hii tulitenga milioni nne, Wizara imetoa milioni mbili peke yake. Na siyo imetoa pesa kidogo tu, haikutoa hata maelezo kwenye hotuba ya Waziri na hata kwenye majibu ya majumuisho nini wamefanya na pesa walizopewa. Na safari hii wametenga pesa kidogo pamoja na umuhimu wa mchakato huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi siridhiki na jambo hili na nawaomba Wabunge wenzangu wote wasioridhika na utekelezaji wa jambo hili waunge mkono na wachangie hoja na baadaye nitajibu baada ya majumuisho ya Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Unatanguliza, wewe una Muswada. Unao Muswada unasubiri ratiba yetu tukupangie na hatuwezi kupanga sasa hivi. Sasa huwezi kuniambia mimi hela hii inaweza kutengeneza Muswada wako wala hela hii inaweza kujenga Benki. Kwa hiyo, hili tunaliondoa, wewe una Muswada na Muswada wako unakuja. Na kwa maana hiyo, hiyo shilingi yako siikubali, naomba tuendelee.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unisikilize. Kuna mambo mawili hapa, kuna Baraza la Vijana na Benki ya Vijana. Muswada wangu hauhusu uanzishwaji wa Benki ya Vijana Tanzania.

MWENYEKITI: Haya, naomba na wewe ukae sasa unisikilize mimi. Hela hizi haziwezi kujenga hicho unachokisema. Hili ni suala ambalo ultakiwa utuambie wakati ule tunapozungumza pamoja mambo ya sera, pale lilikuwa sahihi kwa

Nakala ya Mtando (Online Document)

sababu, ni jambo kubwa ambalo linahitaji utaratibu mkubwa. Hizi ni pesa tu milioni 20, tutatengeneza nani... Kwa hiyo, shilingi siikubali.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 6004 - Sports Development.....Tsh. 3,015,683,000/=

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi. Kwa mujibu wa Randama na kwa mujibu kwanza wa kitabu, kineneza kwamba, mwaka jana katika kifungu kidogo cha 221400 - Hospitality Supplies and Services ni kwamba, kulikuwa na 3,500,000/= mara hii kuna 15,200,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Randama ya Ukarimu wanasema, fedha kwa ajili ya chakula na viburudisho. Ukiacha fedha 500,000/=, lakini wanasema fedha zilizobaki zote milioni 14 na, watanunulia chakula, maji na vinywaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu yangu mimi, ikiwa kulikuwa na 3,500,000/= vinywaji gani, viburudisho gani, vinywaji baridi gani vimezidi mara nne mwaka huu? Mara nne, hata kama kuna ongezeko la bei kiasi gani na hakuna taarifa ya maelezo mengine tangu mwanzo ya ongezeko la ajira, nayo mnataka kusema kwamba, kuna ajira ya watu wapya. Lakini mara nne unaongeza, yaani vinywaji baridi, vitafunwa na chakula, Wizara hii mara hii mmekusudia mle tu nyie? Naomba ufanuzi! (Kicheko)

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Masoud, hiyo pesa yenye hiyo hata ukituambia sisi kuwa tunataka kula tu kwa kweli, unatuonea. Hii Idara ya Maendeleo ya Vijana ina mambo mengi na sasa hivi tuna program nyingi za maendeleo ya michezo. Wageni wengi wanakuja, wakati mwingine hata mgeni akija pale, hata wewe ukija kweli, tukakuacha hivi, utakuja hapa tena utesema ile Wizara gani jamani. Tusamehe bwana, ni hela yenye hiyo kidogo tu hii.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko yoyote)

SPIKA: Mheshimiwa Gekul, kaa kwanza, inasomwa figure, halafu unasi mama.

Kif. 7003 - Information Services.....Tsh.7,954,973,000/=

Nakala ya Mtando (Online Document)

SPIKA: Mheshimiwa Gekul?

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi naomba nipatiwe ufanuzi kwenye kifungu kidogo cha 220700 ambacho kinahusika na *Rental Expenses*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nililisema mwanzoni, lakini cha kusikitisha kwenye Randama nimesoma hizi fedha ni kwa ajili ya kulipia pango la Idara, lakini ufanuzi huu kwenye Randama hautoshelezi.

Na hoja yangu inaendana na ile ya mwanzo kabisa kwamba, Wizara hii imetenga bilioni 1.5 kulipia tu jengo la ofisi yake. Na inasemekana ofisi zake ziko PSPF pale na hili jengo ni ghali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Wizara ya Ujenzi tu wanatumia milioni 700, Wizara ya Uchukuzi milioni 700, Wizara ya Ardhi milioni 36. Ni kwa nini ofisi hii au Wizara hii inatumia bilioni 1.5 wakati kuna matatizo ya mikopo ya vijana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kama hawatanieleza ni kwa nini wamesambaza hizi pesa, lakini wametenga fedha nyingi sana, naomba nitoe Hoja ya Kuondoa Shilingi, ili Wabunge wenzangu tujadili kwamba, Wizara hii ihame kutoka kwenye hilo jengo na wahamie eneo lingine. Haiwezekani bilioni 1.5 ni fedha za ofisi. Naomba *justification*, kwa nini mnaendelea kukaa kwenye hilo jengo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi. Baada ya hapo nimeshatoa hoja hiyo ya kuondoa shilingi.

MWENYEKITI: Lakini siyo kuhamisha jengo. Mheshimiwa eleza maelezo kwa nini hizi hela zimepanda hivi?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu dada yangu Gekul, jirani yangu kama ifuatavyo:-

Ni kwamba, hii Wizara ina sekta nne ambazo ni kubwa na zimesambaa na zimeanza upya. Kwa mfano Idara ya Vijana imeanza upya, yaani ndio kujipanga upya, Maelezo wana sehemu yao, Wizarani pia kule, Utamaduni. Kwa hiyo, hiyo fedha unayoisema hapa na kwa Dar-es-Salaam ni hela nyingi kwenye maandishi, lakini kwa pango inatosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe tu dada yangu, hata ukitingisha kichwa, ukifanya nini, wewe mwenyewe unajua. Hata pale Babati tu, ukipanga chumba pale hela nyingi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kwa hiyo, utusamehe tu, siyo kwamba, ni lengo letu namna gani, bali Idara hii ina maeneo manne ambayo yote yanatakiwa yawe accommodated.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul, nisingeruhusu kwa sababu, tuko kwenye nguzo ya kifungu kwa kifungu. Huwezi kutoa shilingi, maelezo yanatosha. Kwa hiyo, na wengine nani nilimkuta?

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Kanuni ya 103!

MWENYEKITI: Halafu leo, naomba msikilize, leo tunaingia Wizara nyingine kwa hiyo, nina dakika 10 natakiwa kuingia kwenye Guillotine sasa hivi. Ehee, Mheshimiwa Gekul, malizia.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni kwa sababu tu ya muda, lakini Kanuni inaruhusu. Nimesema kwamba, Wabunge wenzangu tujadili na nimetoa hoja hiyo. Mheshimiwa Waziri, majibu yako hayatoshelezi kwa sababu, nilivyosoma Randama ni kwamba, hizi fedha mmesambaza ofisi zingine Dar-es-Salaam, zingine Dodoma.

Mhesimiwa Mwenyekiti, Bunge hili linashauri kwamba, Serikali ihamie Dodoma au Dar-es-Salaam. Kutenga bilioni 1.5 kwa pango tu la ofisi; Mheshimiwa Naibu Waziri amesema hata Babati tunahitaji hizi fedha ni kweli, vijana wangu wa Babati kwanza wamerushwa na Halmashauri shilingi milioni 8 za kwao na bado Serikali haijapeleka.

MWENYEKITI: Hapo unaenda nje ya hoja, unaenda nje ya hoja!

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba fedha hizi Bunge lisipitishe, Kamati ya Bajeti ikae tufanye re-allocation hizi fedha; ninyi Wizara hii mtafute ofisi nyingine popote kwa sababu, jengo hili ni ghali. Kwa hali yetu ya Tanzania hatuthubutu kulipa *1.5 billion* pango la ofisi, ni kufuru. Vijana hawana ajira, vijana hawana mikopo, naomba Wabunge wenzangu mniunge mkono hii Wizara ihame hapa, ndiyo hoja yangu.

MWENYEKITI: Wala hamruhusiwi kwa sababu, ni mambo yaliyo obvious.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi Bila Mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 96 - Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

Kif. 1003 - Policy and
Planning.....Tsh.150,000,000/=
Kif. 6001 - Culture Development
Division.....Tsh.1,520,000,000/=
Kif. 6002 - Youth Development
Division.....Tsh.4,600,000,000/=
Kif. 6004 - Sports Development.....Tsh.7,280,000,000/=
Kif. 7003 - Information Services.....Tsh.1,450,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya
mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Hamkunisikia kwamba, tunaingia kwenye guillotine, 10
minutes before?

(Bunge lilirudia)

TAARIFA

SPIKA: Waheshimiwa tukae, hatujamaliza kazi hii.

Mheshimiwa Mtoa Hoja, Taarifa?

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa, Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, kifungu kwa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote, hivyo basi naliomba Bunge lako tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Naafiki!

SPIKA: Naomba mkae kwanza, hoja imeungwa mkono.

Kifungu cha 220700, hesasbu yake ni milioni 105,750,000 siyo bilioni, ni 105,750,000. (Makofi)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni naMichezo kwa Mwaka 2014/2015
yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Tunapenda kuwapongeza Wizara, lakini kuna suala la Sheria ya Waandishi wa Habari, hilo mmeshindwa. Fanyeni hiyo kazi kwa sababu, hatuwezi kuwa tunarudia hapa kila wakati, mkafanye hiyo kazi, hiyo sehemu tumeshindwa, kwa hiyo, mfanye kazi. Lakini tunawapongeza kwa kazi nyingine zote mlizozifanya na mfanye kazi kwa pamoja na hili swali liondoke katika nyumba yetu hapa. Baada ya kusema hivyo, Katibu?

HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

SPIKA: Mheshimiwa Mtoa Hoja? (Makofi)

Mkumbuke saa mbili tutakuwa na Kikao cha Kamati ya Uongozi.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2013/2014 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini, Mashirika na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka 2014/2015. (Makofi)

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kulipatia Taifa letu uongozi imara, wenyewe dhamira ya kujenga uchumi imara, wenyewe kutoa ajira mpya na matumaini mapya kwa vijana na maskini wa nchini mwetu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za kipekee kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa uongozi wao wenyewe ubunifu na tija kubwa kwa maendeleo ya Taifa letu.

Nampongeza kwa dhati Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kupewa Tuzo ya Utumishi Bora kwa kuwa Kiongozi mwenye mchango mkubwa zaidi katika maendeleo ya Bara za Afrika kwa mwaka 2013. Hii ni heshima kubwa sana kwa Taifa letu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuliongoza Bunge letu kwa hekima, busara na umahiri mkubwa sana. Vilevile namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa kuishauri na kuisimamia Wizara kwa manufaa ya Watanzania wote. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2014/2015. Naomba kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge kuwa, ninachokiwasilisha ni muhtasari wa kitabu cha hotuba yangu ya bajeti mllichogawiwa au ambacho mtagawiwa. Aidha, naomba hotuba yangu kamili ya bajeti iingizwe kwenye Hansard kama ilivyo kwenye kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, Ukusanyaji Mapato: Mwaka 2013/2014 Wizara ya Nishati na Madini ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 220. Hadi kufikia tarehe 03 mwezi huu, jumla ya shilingi bilioni 147 zilikusanywa, sawa na 67% ya lengo. Juhudi zinaendelea kuwekwa ili kuhakikisha kuwa lengo la ukusanyaji linafikiwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mwaka huu tunaomaliza, kwa mwaka 2013/2014 Wizara iliidhinisha jumla ya shilingi trilioni 1.3, kati ya fedha hizo shilingi trilioni 1.2 zilikuwa ni fedha za maendeleo na shilingi bilioni 110 zilikuwa matumizi ya kawaida.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Hadi kufikia tarehe 23 Mei Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 660.73 sawa na asilimia 31.3 ya bajeti iliyoidhinishwa mwaka huu tunaoumalizia.

Mheshimiwa Spika, kutokana na usimamizi mzuri wa matumizi ya fedha za umma, naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Wizara ya Nishati na Madini ilipata hati safi ya hesabu ya mwaka 2012/2013 pasipo na suala lolote. Wizara itaendelea kuhakikisha fedha za walipa kodi zinatumika kwa manufaa yao na si vinginevyo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato mwaka 2014/2015: Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 240.59. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 9.36 ya lengo la mwaka huu tunaoumaliza. Mipango na mbinu zitakazotumika katika ukusanyaji wa mapato ni pamoja na kuboresha mfumo wa utoaji na usimamizi wa leseni za madini, kuongeza udhibiti na kuimarisha usimamiaji mzuri wa ukusanyaji wa mapato yanayotokana na madini, gesi asilia na mafuta.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Nishati: Dira ya maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 ilianza kutekelezwa mwaka 2000. Kwa kutumia dira hii Serikali ya Chama cha Mapinduzi imedhamiria kujenga uchumi wa kisasa na imara utakaoiwezesha nchi yetu kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja (GDP per capita) kutoka wastani ya dola za Marekani 640 hadi dola 3,000 ifikapo mwaka 2025. Ili kufikia leongo hilo, nishati ya kutosha ya uhakika, safi na ya gharama nafuu inahitajika.

Mheshimiwa Spika, sambamba na azma hiyo, sekta ya nishati imejumuishwa kwenye Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN). Katika Sekta hiyo miradi inayohusisha ufuaji, usafirishaji, usambazaji umeme pamoja na miradi wa ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia inatekelezwa. Utekelezaji wa miradi ya BRN utachangia kwa kiasi kikubwa kufikiwa kwa malengo ya dira yetu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hali ya uzalishaji umeme: Mwaka 2013/2014 hali ya upatikanaji wa umeme ilikuwa ya kuridhisha ambapo hapakuwa na mgao wa umeme kama tulivyoahidi mwaka 2012/2013. Na ninarudia, hakuna mgao labda uwe ni mgao wa magazetini au wa kwenye mitandao. Hadi mwishoni wa mwezi Aprili 14 uwezo wa mitambo yetu ya kufua umeme (*total installed capacity*) ulifikia megawati 1583. Uwezo huu mpya ni sawa na ongezeko la asilimia 78 ikilinganishwa na megawati 891 zilizokuwepo mwaka 2005 wakati Serikali ya awamu inaingia madarakani. Hili ni jambo la kujivunia kwa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. (Makofii)

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, hii ni Wizara ya miradi wala siyo mipango. Nakuja kwenye miradi ya kufua umeme. Mradi wa megawati 60 Nyakato Mwanza: Serikali imekamilisha mradi wa ujenzi wa mitambo ya megawati 60 inayotumia mafuta mazito katika eneo la Nyakato Jijini Mwanza. Mradi huo ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wetu tarehe 8 Septemba mwaka jana. Mitambo hiyo imeimarisha upatikanaji na usambazaji wa umeme kwenye Kanda ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Kufua Umeme ya Kinyerezi I, II, III na IV: Miradi ya kufua umeme kwa kutumia gesi asilia eneo la Kinyerezi ipo katika hatua nzuri za utekelezaji. Kwa upande wa mradi wa Kinyerezi I wa megawati 150 mitambo miwili yenye uwezo wa kufua megawati 75 katil ya mitambo minne, imewasili nchini mwezi Februari mwaka huu. Katika mwaka 2014/2015 ufungaji wa mitambo, ujenzi wa njia za kusafirisha umeme na kituo cha kupoozea umeme vitakamilishwa. Fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya mradi huu ni shilingi bilioni 90.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya Kinyerezi II megawati 240, Kinyerezi III megawati 300, Kinyerezi IV megawati 300, Rusumo megawati 80, Mtwara megawati 600 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Vile vile Serikali inaendelea kusimamia miradi ya kufua umeme wa makaa ya mawe ya Kiwira megawati 200, Mchuchuma megawati 600, Ngaka megawati 400.

Vile vile miradi ya nishati jadidifu (*renewable energies*) ya tungamotaka (*biomass*), umeme juu, upepo, joto ardhi (*geothermal*) inaendelea kuongezeka nchini ikiwa ni vyanzo vipyta vya nishati nchini mwetu.

Mradi wa kuzalisha megawati 600 Mkoani Mtwara: Katika kuhakikisha kuna upatikanaji wa umeme wa uhakika kwenye Mikoa ya Lindi na Mtwara, TANESCO kwa kushirikiana na Kampuni ta Simbion zinatekeleza mradi wa megawati 600, upembusi yakinifu wa mradi huu utakamilika mwezi Julai mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, mradi wa ORIO. Mradi huu unahusisha ufungaji wa generator zenyе uwezo wa megawati 2.5 kila moja katika Wilaya za Biharamulo, Mpanda na Ngala. Vilevile kuna ujenzi wa njia mpya za usambazaji umeme katika Wilaya hizo. Jumla ya shilingi bilioni 22.5 zimetengwa kwa mwaka mpya wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha njia za kusafirisha na kusambaza umeme: Mbali ya kutekeleza miradi mikubwa ya kufua umeme ambayo tunataka tufikishe megawati 3000 mwakani mwishoni, Serikali imeanza kutekeleza miradi

Nakala ya Mtando (Online Document)

mikubwa yenyewe uwezo wa kusafirisha umeme mwingi kwenye umbali mrefu. Miradi hiyo ni ifuatayo:-

Mradi wa Iringa - Shinyanga kilovoti 400, back born inaitwa. Mradi huu ni wa kilomita 670 na msongo wa kilovoti 400 kutoka Iringa kuitia Dodoma na Singida hadi Shinyanga. Mradi unagharimu shilingi bilioni 367.36. Wafadhili wa mradi huu ni Serikali yetu, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Maendeleo la Japan, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya na Shirika la Maendeleo la Korea.

Jumla ya shilingi bilioni 2.5 zimetengwa kwa mwaka mpya wa fedha ikiwa ni mchango wa Serikali. Mradi utakamilika mwaka 2015/2016. Wale wanaotaka *time table* za miradi kukamilika wanisikilize kwa makini mimi, miradi yetu ina tarehe. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, mradi wa Makambako – Songea KV 220: Mradi huu ni wa kilomita 250 za njia za kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 kutoka Makambako hadi Songea. Vituo vipyta vyta kupooza umeme vitajengwa Madaba na Songea na kile cha Makambako kitapanuliwa. Lengo la mradi huu ni kuunganisha Wilaya za Ludewa, Mbinga, Namtumbo, Njombe, Songea Mjini na Songea Vijiji kwenye grid ya Taifa.

Hakuna Mikoa iliyosahauliwa. Mradi utaanza kutekelezwa katika katika mwaka huu mpya wa fedha na utakamilika mwaka 2015/2016. Jumla ya shilingi bilioni 16.3 zimetengwa.

Mradi mwingine mkubwa wa *transmission*, mradi wa *North East Grid* wa kilovoti 400. Mradi huu ni wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 yenyewe urefu wa kilomita 600 kutoka Kinyerezi hadi Arusha kuitia Chalinze na Segera. Jumla ya shilingi bilioni 1.5 zimetengwa kutekeleza mradi huo. Miradi yetu yote ina *deadline*, mradi unatarajiwa kukamilika mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, *North West Grid* kilovoti 400: Mradi huu ni wa ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Mbeya, kuitia Sumbawanga, Mpanda, Kigoma hadi Nyakanazi yenyewe urefu wa kilomita 1148. Fedha za ndani ni shilingi bilioni 1 zimetengwa mradi huu utakamilika mwaka 2016/2017. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, mradi wa Singida – Arusha – Namanga, tunataka kuza umeme Kenya. Ibara ya 63 ya llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010/2015 inatoa msisitizo kuhusu kuunganisha *grid* yetu ya Taifa na nchi jirani ili kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mradi wa Singida – Arusha - Namanga ni sehemu ya mradi wa Zambia, Tanzania, Kenya Interconnector yenye urefu wa kilomita 2047. Fedha za nje ambazo ni mkopo wa ADB na JAICA zilizotengwa kwa ajili ya mradi huu ni shilingi milioni 500. Mradi umepangwa kukamilika mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, sambamba na jithada hizo, TANESCO itatekeleza mradi wa upanuzi wa njia ya usambazaji umeme ya Tunduma hadi Nakonde, Zambia ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa mita 100. Katika mwaka 2014/2015 Serikali imetenga bilioni 5 kwa utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, mradi mkubwa wa sita, mradi wa Bulyanhuru Geita kilovoti 220. Mradi huu ni wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 55 kutoka Bulyanhuru hadi Geita gharama za mradi ni shilingi bilioni 21, jumla ya shilingi bilioni 2.5 zimetengwa kwa mwaka 2014/2015. Fedha za nje zitatoka BADEA (*Bank of Arab for Economic development in Africa*). Mradi umepangwa kukamilika mwaka ujao wa fedha. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Electricity 5, mradi wa saba huu: Narudia hii siyo michakato, mipango, ni miradi. Mradi huu ni kwa ajili ya usambazaji umeme kwa wakazi wa Wilaya za Bukombe, Busega, Kwigwa, Magu, Mbogwe, Misungwi na Sengerema.

Vilevile kuna ukarabati wa vituo vya kupoozea umeme vya Ilala na Sokoine katika Jiji la Dar es Salaam pamoja na upanuzi wa kituo cha kupoozea umeme cha Njiro Mkoani Arusha. Gharama za mradi huu ni shilingi bilioni 78.8, jumla ya shilingi bilioni 4 zimetengwa ili kutekeleza kazi zilizopangwa, fedha za nje zitatoka African Development Bank, mradi umepangwa kukamilika mwaka huu wa fedha tutakaouanza.

Mheshimiwa Spika, mipango ya kuboresha umeme Jiji la Dar es Salaam: Mradi huu unafadhiliwa na Serikali za Finland na Japan na unahusu ujenzi wa kituo kipyaa cha kupoozea umeme mkabala na kituo cha Ilala City Centre. Ujenzi wa njia za usafirishaji umeme na kuweka mfumo mpya wa kuunganisha vituo vya umeme vya kupoozea umeme vya City Centre, Kariakoo, Railway na Sokoine.

Lengo la mradi huu ni kuboresha miuondombinu ya umeme ili kuboresha upatikanaji wa umeme wenye ubora na uhakika zaidi katika Jiji la Dar es Salaam. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 123, fedha zilizotengwa kwa mwaka huu tunaanza wa fedha ni bilioni 1.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, umeme Bihamula, Mpanda na Ngara - mradi wa ORIO. Mradi huu unahusisha ufungaji wa generator zenyе uwezo wa megawati 2.5 kila mmoja katika Wilaya za Bihamulo, Mpanda na Ngara, pia ukarabati wa njia zilizopo na ujenzi wa njia mpya za usambazaji umeme zenyе msongo wa kilovoti 33. Lengo la mradi huu ni kuongeza uwezo wa ufuaji na usambazaji umeme katika Wilaya hizo. Garama za mradi ni shilingi bilioni 81.55. Jumla ya shilingi bilioni 22.5 zimetengwa kutekeleza huu mradi na mradi umepangwa kukamilika mwaka wa fedha unaokuja. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, miradi ya TANESCO na REA. Serikali imeendelea kutekeleza ibara ya 23 ya llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 hadi 2015 inayohamasisha kuongeza idadi ya wananchi waliounganishiwa umeme vijijini na mijini. Wakati Serikali ya awamu ya nne inaingia madarakani, kiwango cha uunganishwa (*connection level*) nchini kilikuwa asilimia 10 tu.

Kiwango cha uunganishwaji umeme vijijini kimeongezeka kutoka asilimia 2 mwaka 2005 hadi asilimia 7 mwishoni mwa mwaka jana. Hadi kufikia mwezi Machi mwaka huu watu wanaopata huduma ya umeme (*access level*) walifika asilimia 36 kwa Tanzania Bara. Hivyo Wizara ya Nishati na Madini imekamilisha lengo lililowekwa na Chama Tawala. Na wana-CCM naomba mtupatие malengo mapya uwezo tunao. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya yametokana na miradi ya REA na uamuzi wa Serikali wa kupunguza gharama za kuunganisha umeme wateja wa njia moja (*single phase*) mijini na vijijini kwa wastani wa kati ya asilimia 77 na 30 ulioanza kutekelezwa Januari mwaka jana.

Kwa miradi ya sasa ya REA awamu ya pili ya umeme vijijini, gharama za kuunganisha umeme *single phase* ni shilingi 27,000 tu, na vijijini ninapotembelea wanasema hii ni bei sawa na jogoo wawili wa vijijini. Hii inadhihirisha uamuzi wa dhati wa CCM na Serikali yake wa kufanya mageuzi makubwa sana ya uchumi nchini mwetu. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba mwaka 2013/2014 bajeti ya REA iliyopitishwa ilikuwa jumla shilingi bilioni 333.90. Hadi leo hii Wizara imeshapokea jumla ya shilingi bilioni 225.82, sawa na asilimia 66.4 ya bajeti yote na tumefanya majadiliano fedha mpya zinatoka mwezi wa Juni, kwa hiyo wakandarasi niwakute site mwezi wa Juni. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, mradi wa kusambaza umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. REA inaendelea na utekelezaji wa miradi 52 ya kusambaza umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Gharama ya kuunganisha umeme kwenye Mikoa hiyo ni shilingi 99,000 kwa umbali usiozidi mita 30.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kwa kupokea na kutekeleza ombi la Wabunge wa Lindi na Mtwara, Serikali imeamua kwamba gharama ya uunganishaji umeme kwenye Mikoa hiyo itaendelea kuwa shilingi 99,000 hadi mwakani mwezi Juni. Ndugu zangu wa Mikoa ya Lindi na Mtwara tumieni fursa hii kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji huduma za wateja, Serikali kupitia TANESCO imeendelea kuhakikisha kwamba vifaa vyote muhimu vya kuunganishia umeme wateja vikiwemo nguzo mita na nyaya vinapatikana kwa wakati. Pamoja na uchakavu wa miundombinu ya umeme nchini, naipongeza sana TANESCO kwa kuendelea kuboresha miundombinu hii chakavu na kwa ujenzi wa miundombinu mipyä ya kisasa na kwa utoaji huduma ya umeme vizuri kuliko siku za nyuma. Hongera sana Bodi ya TANESCO, hongera sana Menejimenti, hongereni sana watumishi wa TANESCO. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya gesi asilia: Kufikia mwezi Mei, mwaka 2014 kazi ya ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Songosongo kupitia baharini hadi Somanga Fungu lenye urefu wa kilomita 25.6 ilikamilika kwa asilimia 100 na hivyo kufanya kiwango cha utekelezaji wa ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam kufikia wastani wa asilimia 78. (Makofii)

Aidha, maandalizi ya ujenzi wa mitambo ya kusafirisha gesi asilia yamekamilika kwa asilimia 90 kwa upande wa Mtwara, na asilimia 78 kwa upande wa Lindi. Serikali imedhamiria kwa dhati, kukamilisha ujenzi wa bomba hili ifikapo mwezi Julai, 2014 na mitambo ya kusafirisha gesi asilia ifikapo mwezi Desemba, 2014. Napenda kurudia, mtu apende asipende hili bomba ndiyo roho ya nchi hii na litakamilika. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, usambazaji wa gesi asilia Lindi – Mtwara na Pwani: Serikali itawezesha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kwa ajili ya mitambo ya kufua umeme, matumizi ya viwandani, kwenye taasisi majumba na kwenye magari katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani. Aidha, TPDC imeanza majadiliano na baadhi ya viwanda vya uzalishaji saruji kama cha Dangote cha Mtwara na Meis cha Lindi na Kilwa Energy cha Kilwa kwa ajili ya kufua umeme.

Mheshimiwa Spika, utafutaji wa gesi asilia na mafuta: Mwezi Oktoba, mwaka jana Serikali ilifanya uzinduzi wa dulu ya nne ya kuitisha zabuni za utafutaji mafuta (*forth petroleum licensing round*) kwenye vitalu saba katika Bahari kuu na kimoja kwenye Ziwa Tanganyika Kaskazini. Zoezi hilo lilifanyika nchini mwetu kwa mara ya kwanza baada ya kufanyika nchi za nje mara tatu

Nakala ya Mtando (Online Document)

mfululizo na kwa mara ya kwanza kampuni tano zimerudisha nyaraka za zabuni ilipofika tarehe ya mwisho ya tarehe 15 Mei, 2014. Hili halijawahi kutokea kwa round zote za awali zilizofanyika nje ya nchi. Tanzania ni nchi inaaminika na tuna uwezo wa kukaribisha wawekezaji tusijidharau. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Taifa ya Mafuta: Serikali imeendelea kuratibu uanzishwaji wa Hifadhi ya Taifa ya Mafuta kwa kuandaa rasimu ya kanuni za uratibu wa mafuta ya akiba. Aidha, kampuni ya *Oman Trading International* ilishinda zabuni ya kuiuzia *TPDC* mafuta na imekubali kuleta mafuta kwa mkopo na itakuwa inalipwa baada ya *TPDC* kuuza mafuta hayo. Na mwaka huu wa fedha unaonza tunakamilisha taratibu hizo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, sera, sheria katika sekta ndogo ya gesi na mafuta: Kama nilivyoahidi katika hotuba yangu ya mwaka jana mbele ya Bunge hili tukufu, napenda kutoa taarifa bungeni, Serikali imeidhinisha Sera ya Gesi mwezi Oktoba, mwaka jana ili itumike kuimarisha usimamizi wa sekta ya gesi asilia kwa manufaa ya Watanzania wote. (Makofii)

Aidha, Muswada wa Sheria ya Gesi asilia utaletwa bungeni mwezi Novemba, 2014. Sera ya uvezeshaji, naomba mnisikilize kwa makini hapa, sera ya uvezeshaji na ushirikishaji wazawa (*local content policy*) itakamilika ifikapo Desemba, 2014. Lengo kuu la sera hii ni kuhakikisha kuwa Watanzania wanashiriki ipasavyo katika shughuli zote za rasilimali ya gesi asilia na mafuta kwa manufaa ya Watanzania wote bila upendeleo au ubaguzi wa aina yoyote. Rasimu hiyo imesambazwa kwa wadau ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge ili tupate maoni yenu kabla ya tarehe 15 Juni, 2014.

Mheshimiwa Spika, muundo wa *TPDC*, mwezi wa Aprili, mwaka huu, Serikali kupitia Msajili wa Hazina iliidhinisha muundo mpya wa *TPDC* ili kuliwezesha shirika hilo kushiriki kikamilifu kwenye shughuli zote za uzalishaji na usambazaji wa gesi asilia na mafuta. Ushiriki wa *TPDC* katika maeneo hayo utaimarisha mapato ya Serikali kwenye shughuli za rasilimali hii kwa niaba ya Watanzania wote. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, EWURA na kampuni ya *PICL* kwa pamoja waliendelea kutimiza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka jana jumla ya lita bilioni 4.66 za aina mbalimbali za mafuta ziliingizwa nchini kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Aidha, kutokana na kuimarika kwa mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja wastani wa ghamrama (*weighted average premium*) za uagaziji wa mafuta ya *petrol* zimeshuka kutoka dola za Marekani 59 kwa tani mwezi Novemba, 2011 hadi dola za Marekani 36 kwa tani mwezi Aprili, 2014. (Makofii)

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini: Mwaka 2013/2014 Serikali imeendelea kusimamia ukusanyaji wa mapato ikiwemo ushuru wa huduma (service levy).

Migodi ya Geita, Bulyakhulu, Buzwagi, North Mara, Resolute na mgodi wa Almasi wa Mwadui imelipa jumla ya shilingi bilioni 17.35 kwa Halmashauri za Geita, Kahama, Kishapu, Nzega na Tarime. Tumieni vizuri hizo fedha watu wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, majadiliano na kampuni za madini: Katika hotuba yangu ya mwaka jana niliahidi kwamba Wizara itafanya majadiliano na baadhi ya wamiliki wa migodi mikubwa nchini wenyewe mikataba ya uendelezaji migodi. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa kutokana na majadiliano hayo. Kampuni ya African Barrick Gold imekubali kuanzia Julai, 2014 kulipa asilimia 0.3 ya mapato yaani ya turnover kama ushuru wa huduma service levy kwa Halmashauri husika, badala ya malipo ya dola laki mbili kwa mwaka yaliyokuwa yanalipwa hapo awali. Napenda kuipongeza kampuni ya ABG na kusisitiza kwamba Wizara inaendelea kujadili na kampuni zingine zifanye hivyo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo nchini mwetu: Katika kutekeleza ilani ya uchaguzi ya CCM, ibara ya 56 ambayo inasisitiza juu ya kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata mitaji, Wizara imetoa mikopo ya masharti nafuu na ruzuku kwa wachimbaji wadogo kuitia Benki ya Rasilimali. Mwezi Aprili, 2014, Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu alikabidhi hundi zenye jumla ya shilingi milioni 88 kwa miradi 11 kwa wachimbaji wadogo ambayo ilikidhi vigezo vya kupata ruzuku. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, wachimbaji wadogo wamepewa milioni 88 vikundi 11 ikiwa ni ruzuku, hatuwadai. Kuendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo kwa mitaji na mikopo, Wizara imetenga bilioni 2.5 kwa mwaka 2014/2015 kwa ajili ya mikopo yao.

Pamoja na fedha za mikopo, Serikali kuitia mradi wa Benki ya Dunia imetenga jumla ya shilingi bilioni 5.74 kama ruzuku kwa wachimbaji wadogo na kiasi cha shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya kununua mitambo miwili ya kuchoronga miamba (*drill and leads*). Mitambo hiyo itapelekwa katika ofisi za madini za Kanda ya Ziwa Mwanza, na Kanda ya Kusini Magharibi Mbeya, ili itumike kwenye utambuzi wa kiasi cha mashapo yaliyopo katika maeneo ya wachimbaji wadogo.

Kwa hiyo jumla ya fedha zilizotengwa kwa mwaka 2014/2015 kwa ajili ya wachimbaji wadogo ni shilingi bilioni 10. Waheshimiwa Wabunge, kabla ya

Nakala ya Mtando (Online Document)

mwisho wa mwezi wa Juni haujaisha, naenda tena kuwapa ruzuku ya kila mtu kutoka na dola 50,000. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2013, jumla ya maeneo kumi yenye ukubwa wa hekta zaidi ya 67,000 yametengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Hii inafanya jumla ya maeneo yaliyotengwa hadi sasa kwa ajili ya wachimbaji wadogo kufikia ukubwa wa kilomita za mraba zaidi ya 2000. Wizara itaendelea kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo ili kutoa ajira mpya kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, kuboresha utoaji na usimamizi wa leseni za madini: Katika kuboresha mfumo wa utoaji wa leseni za madini, Wizara iliwezesha wamiliki wa leseni kupata taarifa kupitia tovuti maalum ya leseni na pia kuwawezesha wateja kupokea taarifa za maombi kupitia ujumbe mfupi wa simu na barua pepe. Hatua hizi zinalenga kuwawezesha waombaji wa leseni kuwasilisha maombi na malipo yao wa njia ya mtando, na hii ni njia moja ya kupunguza rushwa hii. Hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu leseni tulizonazo ni 39,958.

Mheshimiwa Spika, wakati sekta ya madini ikiendelea kukua imejengeka dhana kwamba wawekezaji wageni wanamiliki maeneo mengi na makubwa kuliko Watanzania. Aidha, ipo fikira kwamba Serikali hajachukua hatua ya kuwawezesha Watanzania kushiriki kikamilifu katika uwekezaji kwenye sekta hii muhimu. Ukweli ni kwamba Watanzania wanamiliki asilimia 70 ya leseni zote za madini. Wageni wanamiliki asilimia 25 tu na asilimia tano ni za ubia kati ya wageni na Watanzania. Naomba nirudie Watanzania ndiyo wenye leseni nyingi kwa asilimia 70 na nina majina, kesho nitawasomea. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuchukua hatua dhidi ya wamiliki waliohodhi maeneo makubwa ya leseni za madini bila ya kuyaendeleza. Hadi kufikia mwezi Aprili, mwaka huu hati za makosa 336 zilitolewa zikihusisha leseni 253 za utafutaji wa madini na leseni 83 za uchimbaji madini. Aidha, jumla ya leseni 174 za utafutaji madini na leseni moja ya uchimbaji mkubwa wa madini zilifutwa.

Pamoja hatua ya kufuta leseni, Wizara pia imechukua hatua ya kutomilikisha leseni mpya 214 kwa kampuni zenye leseni zinazozidi ukomo wa eneo la leseni la kilomita za mraba 2000. Hatua hii imechukuliwa ikiwa ni sehemu ya usimamiaji mzuri wa sheria za madini wa mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Madini: Chuo cha Madini Dodoma kimeendelea kutoa mafunzo katika fani ya jiolojia, uhandisi, uchimbaji na uchenjuaji madini, sayansi za mafuta na gesi asilia na uhandisi usimamizi wa

Nakala ya Mtando (Online Document)

mazingira migodini katika ngazi ya cheti na stashahada. Chuo hiki kitakabidhiwa eneo la migodi uliofungwa wa Resolute ili ijenge campus nyingine huko Nzega.

Kampuni ya Resolute imetoa shilingi bilioni 1.64 kwa ajili ya kukarabati miundombinu na kuimarisha ulinzi katika eneo. Aidha, Serikali imeanza utaratibu wa kukigeuza hiki chuo kuwa polytechnic ili vyeti vyake vitambulike kimataifa. Na wameanza mazungumzo na Chuo cha Montreal, Canada. (Makof)

Mheshimiwa Spika, STAMICO: Katika mwaka 2013/2014 STAMICO iliajiri watumishi wapya 78 ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kwa mwaka 2014/2015 shirika litakamilisha kujaza nafasi za menejimenti na kuanza kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo ya Bacliff, Buhemba, Kiwira, Mererani na Tulawaka. Pia shirika litaanza kununua na kuchenjua madini ya bati katika mkoa wa Kagera na kufanya utafiti wa rare earth metals katika maeneo yenye leseni zao. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ukaguzi wa Madini (TMAA): Katika kipindi cha kuanzia Julai, mwaka jana hadi Aprili mwaka huu, TMAA imehakikisha kampuni ya Resolute inalipa bilioni 3.38 na kampuni ya Geita inalipa bilioni 50.6, ikiwa ni kodi ya mapato.

Waheshimiwa Wabunge mnakumbuka huko nyuma tulikuwa hatukusanyi kodi ya mapato, tumeanza. Aidha, ukaguzi ulifanywa wakala umewezesha jumla ya shilingi bilioni 4.9 kulipwa Serikalini na baadhi ya wamiliki wa migodi mikubwa na ya kati. Kwa mwaka 2014/2015, Serikali itaimarisha ukaguzi wa migodi ili kuhakikisha Taifa linanufaika ipasavyo na rasilimali yake ya madini. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Jiolojia: Kwa mwaka 2013/2014 wakala umeendelea kufanya utafiti wa jiolojia kwenye Wilaya mbalimbali, uchoraji wa ramani unaendelea vizuri na wakala pia utachora ramani nne za jiolojia za Wilaya za Kilwa, Liwale, Nachingwea na Ruangwa pamoja na ramani mbili za jiomeria za Wilaya ya Liwale na Ruangwa. (Makof)

Mheshimwia Spika, Kamati Tekelezi ya TEITI ilikamilisha rasimu ya sheria itakayosimamia shughuli zake. Maoni yaliyopatikana kutoka kwa wadau yametumika kuboresha rasimu hiyo. Muswada wa sheria hiyo unatarajiwa kuwasilishwa katika kikao cha Bunge cha mwezi Novemba mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, rasilimali watu: Katika mwaka 2013/2014 jumla ya watumishi 227 wa kada mbalimbali wameajiriwa na Wizara, Mashirika na taasisi

Nakala ya Mtandao (Online Document)

zake. Vilevile Wizara imefadhili wanafunzi 214 wa Kitanzania wanaosoma katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi kuitia mpango wa Wizara unaojulikana *the martial plan on capacity building and development in oil and gas industry.* (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa kimataifa: Hii ni Wizara ya uhakika, sikiliza orodha; Wizara...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, naambiwa kwamba mengine unatumbukiza, hayamo kwenye hotuba.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Aaa, hilo nalitoa, hilo nalitoa.

Mheshimiwa Spika, Waziri ya Nishati na Madini, inashirikiana na wadau mbalimbali kutoka kila pembe ya dunia. Kwa niaba ya Serikali napenda kutoa shukrani kwa Serikali za Algeria, Brazil, Canada, China, Finland, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Sweden, Thailand, Trinidad and Tobago, Uingereza, Ujerumani na Urusi.

Vilevile natoa shukrani kwa Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya EXIM ya China, Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini, Benki ya HSBC, Benki ya BADEA, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, Umoja wa Ulaya, pamoja na taasisi na Mashirika ya FD - Ufaransa, CIDA - Canada, DANIDA Denmark, DFDI - Uingereza, ECDF - Marekani, Korea Kusini, FINIDA - Finland, JAICA - Japan, MCC - Marekani, NORAD - Norway, OFID - Saudi Arabia, ORIO - Uhlanzi, SIDA - Sweden, IFC, UNDP, Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola, Climate Investement Fund, USAID - Marekani na JBIC - Japan. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, shukrani: Napenda kuwashukuru sana Manaibu Mawaziri wa Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Stephen Julius Maselle, Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini na Mheshimiwa Muhangwa Kitwanga, Mbunge wa Jimbo la Misumbwi.

Nakiri wazi kabisa kuwa Naibu Mawiziri wangu hawa wamekuwa nguzo kubwa na msaada mkubwa kwangu na kwa Taifa letu katika kutekelezaji wa majukumu yetu kwenye Wizara yetu. (Makofii)

Pia napendea kumshukuru sana Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Jimbo la Kibakwe kwa utendaji kazi na ushirikiano wake mzuri wakati alipokuwa nasi Wizarani. Namtakia mafanikio makubwa kwenye kituo chake kipyaa cha kazi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nawashukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, ndugu Eliakim Maswi na Naibu wake Mhandisi

Nakala ya Mtando (Online Document)

Ngosi Mwihava, kwa ushirikiano wanaonipa na kwa utendaji kazi wao mahiri, hawa ni watu wa kujituma, watu makini, watu wabunifu, wachapakazi mahiri kwenye timu yangu mimi ya ushindi ya Wizara ya Nishati na Madini. (Makofii)

Aidha, nawashukuru Makamishina wote, wakuu wote wa idara na wafanyakazi wote wa Wizara kwa kutekeleza majukumu yao kwa umakini na ubunifu mkubwa. Hakuna kushindwa, hakuna kukatishwa tama. Hakuna kushindwa, hakuna kukatishwa tama. Mara ya tatu, hakuna kushindwa, hakuna kukatishwa tamaa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Wenye viti wote wa Bodi za Wakurugenzi, Wenye viti wote wa Bodi za Ushauri na wafanyakazi wote wa mashariki na taasisi zilizo chini ya Wizara yetu kwa utendaji kazi wao wenye tija unaotanguliza mbele maslahi ya Taifa letu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza viongozi wote wa madhehebu ya dini nchini kwa kukubali kushirikiana na Wizara katika kuelimisha jamii kwa kaulimbiu isemayo “uendelezaji wa rasilimali za gesi asilia, mafuta na madini kwa amani na maendeleo ya nchi yetu”.

Kupitia viongozi hawa Wizara imeendelea kuelimisha jamii juu ya faida zitokanazo na rasimali zetu kwa manufaa ya Watanzania wote na siyo kwa wateule wachache. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru familia yangu, ndugu na rafiki zangu kwa kuendelea kuboresha ubunifu wangu, utendaji wangu mahiri wenye weledi mkubwa na wenye manufaa makubwa kwa Watanzania bila upendeleo au ubaguzi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hitimisho: Bajeti ya mwaka 2014/2015 inalenga kuimarisha kuendeleza sekta za nishati na madini ili kuongeza zaidi mchango wake katika kukuza uchumi imara wa Taifa letu wenye kutoa ajira mpya, matumaini mapya na kupunguza umaskini nchini. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe bajeti ya jumla ya shilingi 1,082,555,622,000/=) kwa mchanganua o fuataao:- Bajeti ya maendeleo ni shilingi 957,177,170,000/= sawa na asilimia 88.4 ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo 652,805,000,000/= ni fedha za ndani

Nakala ya Mtandao (Online Document)

sawa na asilimia 68.2. Fedha za ndani asilimia 68.2 ya fedha za maendeleo na shilingi 304,372,170,000/= sawa na asilimia 31.8 ni fedha za nje.

Matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 125,378,452,000/= sawa na asilimia 11.6 ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo, shilingi 26,912,948,000/= ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara, mashirika na taasisi sawa na asilimia 2.4 ya bajeti yote, ndiyo mishahara yetu na shilingi 98,465,504,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengine ya OC, sawa na asilimia 9.11 ya bajeti yetu.

Hii ni bajeti ya upendo, hii ni bajeti ya maskini. (*Makofij*)

HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI NA MADINI MHE. PROF. SOSPETER MWIJARUBI MUHONGO (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA

MWAKA 2014/15 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

DIRA

Kuwa Taasisi yenye ufanisi na inayojali tija ili kuhakikisha kuwa Rasilimali za Nishati na Madini zinachangia ipasavyo katika maendeleo ya nchi kijamii na kiuchumi.

DHIMA

Kuendeleza, kuwezesha, kudhibiti na kusimamia matumizi endelevu ya Rasilimali za Nishati na Madini kwa manufaa ya Watanzania.

ORODHA YA VIFUPISHO

ABG - African Barrick Gold

ADUC - Africa Down Under Conference

AFD - French Agency for Development

AfDB - African Development Bank

ARGeo - African Rift Geothermal

BADE-Bank of Arab for Economic Development in Africa

BPS - Bulk Procurement System

BRN - Big Results Now

CAMARTEC - Centre for Agriculture Mechanization and Rural Technology

CCM - Chama Cha Mapinduzi

Nakala ya Mtandao (Online Document)

CFL - Compact Fluorescent Light
CIDA - Canadian International Development Agency
CIF - Climate Investment Fund
CPI - China Power Investment
DANIDA - Danish International Development Agency
DBSA - Development Bank of Southern Africa
EDCF - Economic Development Cooperation Fund
EIB - European Investment Bank
EITI - Extractive Industries Transparency Initiative
ESIA - Environmental and Social Impact Assessment
EU - European Union
EWURA - Energy and Water Utilities Regulatory Authority
EXIM - Export Import Bank
FDI - Foreign Direct Investment
FINIDA - Finland Department for International Development Agency
FSL - Full Supply Level
GDP - Gross Domestic Product
GIT - Geological Institute of Thailand
GST - Geological Survey of Tanzania
GWh - Gigawatt Hour
HSBC - Hong Kong and Shanghai Banking Corporation
IDA - International Development Association
IED - Innovation Energy Development
IFC - International Finance Corporation
ISO - International Standard Organisation
JBIC - Japan Bank for International Cooperation
JICA - Japan International Corporation Agency
JV - Joint Venture
KEMCO - Khalid Electrical and Mechanical Company
KIA - Kilimanjaro International Airport
kV - Kilovolt
Kva - Kilovolt-Ampere
LUKU - Lipa Umeme Kadri Unavyotumia
Mb - Mbunge
MCC - Millennium Challenge Corporation
MCIMS - Mining Cadastral Information Management System
MDU - Ministerial Delivery Unit
ML - Mining License
MMSCF - Million Standard Cubic Feet
MoU - Memorandum of Understanding
MPSA - Model Production Sharing Agreement
MRI - Mineral Resource Institute
MSL - Minimum Supply Level

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MVA - Mega Volt Ampere
MW - Megawatt
NDC - National Development Corporation
NEMC - National Environment Management Council
NORAD - Norwegian Agency for Development Cooperation
OC - Other Charges
OFID - OPEC Fund for International Development
ORIO - Facility for Infrastructure Development (The Netherlands)
OTI - Oman Trading International
PAYE - Pay as You Earn
PDAC - Prospectors and Developers Association of Canada
PE - Personal Emolument
PICL - Petroleum Importation Coordinator Limited
PL - Prospecting License
PPA - Power Purchase Agreement
QDS - Quarter Degree Sheet
REF - Rural Energy Fund
RFP - Request For Proposal
SAGCOT - Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania
SDL - Skills Development Levy
Sida - Swedish International Development Cooperation Agency
SMBC - Sumitomo Mitsui Banking Corporation
SML - Special Mining License
SPPA - Standardised Power Purchase Agreement
SREP - Scaling-Up Renewable Energy Program
SSMP - Sustainable Solar Market Packages
STAMICO - State Mining Corporation
TAMIDA - Tanzania Mineral Dealers Association
TANESCO - Tanzania Electric Supply Company Limited
TAZAMA - Tanzania - Zambia Pipeline Limited
TCF - Trillion Cubic Feet
TEITI - Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative
TGDC - Tanzania Geothermal Development Company Limited
TGJTA - Thai Gem & Jewelry Traders Association
TIB - Tanzania Investment Bank
TIPER - Tanzania International Petroleum Reserve
TMAA - Tanzania Minerals Audit Agency
TPDC - Tanzania Petroleum Development Corporation
TRA - Tanzania Revenue Authority
UNDP - United Nations Development Programme
USD - United States Dollar
VAT - Value Added Tax
VETA - Vocational Education Training Authority

Nakala ya Mtandao (Online Document)

VVU - Virusi vya UKIMWI

WB - World Bank

WDL - Williamson Diamonds Limited

WHT - Withholding Tax

ZTK - Zambia – Tanzania – Kenya

A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji ya Mwaka 2013/14 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka 2014/15.
2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.
3. **Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wa Rais, Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal na Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb.) kwa uongozi na juhudzi zao katika kuleta maendeleo ya Taifa letu na kwa ushirikiano wanaonipa katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini.
4. **Mheshimiwa Spika**, naomba kumpongeza kwa dhati Rais wetu Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kupewa Tuzo ya Utumishi Bora kwa kuwa Kiongozi mwenye mchango mkubwa zaidi katika maendeleo ya Bara la Afrika kwa Mwaka 2013.
Hii ni heshima kubwa na Tunu kwa Watanzania wote kwa ujumla kwa kuthaminiwa na kutambuliwa kwa kiongozi wetu katika medani za kimataifa. Tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu ili azidi kumpa nguvu na hekima zaidi ya kutekeleza majukumu yake.
5. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa hekima, busara, umahiri na bila kuyumba katika kusimamia Kanuni tulizojiwekea sisi wenywewe.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Vilevile, namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa (Mb.), Makamu Mwenyekiti Mhe. Jerome Dismas Bwanausi (Mb.), na wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuishauri na kusimamia Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake, pamoja na kuchambua na kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2013/14 na Makadirio ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2014/15.

Napenda kulihakikisha Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Nishati na Madini imezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Nishati na Madini katika kuandaa Bajeti inayowasilishwa kwenu.

6. **Mheshimiwa Spika**, naomba vilevile kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapongeza Mhe. Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Jimbo la Kalenga na Mhe. Ridhiwan Jakaya Kikwete, Mbunge wa Jimbo la Chalinze kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa wawakilishi wa wananchi katika Majimbo hayo.

Aidha, napenda kuwapa pole familia, ndugu, jamaa na wananchi kwa kuondokewa na wapendwa wetu, Mhe. Dkt. William Augustao Mgimwa, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kalenga na Waziri wa Fedha; Mhe. Said Ramadhani Bwanamdogo, aliyekuwa Mbunge wa Chalinze; na Mhe. John Gabriel Tupa, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mara. Tunaomba Mwenyezi Mungu awarehemu na awapumzishe kwa amani.

7. **Mheshimiwa Spika**, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2013/14; na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2014/15.

B. TAARIFA YA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2013/2014 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2014/2015

8. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2013/14 katika Sekta za Nishati na Madini ulilenga kufanya yafuatayo: kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika; kuongeza wateja wanaotumia umeme hususan vijiji; ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia; kuongeza kasi ya upelekaji umeme katika Makao Makuu ya Wilaya ambazo hazijapatiwa umeme; kusimamia na kudhibiti biashara ya mafuta; kuvutia uwekezaji katika Sekta za Nishati na Madini; kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali; na kujenga uwezo wa usimamizi na ufuatiliaji katika Sekta za Nishati na Madini ili kukuza uchumi na kuharakisha maendeleo ya Taifa letu.

Nakala ya Mtando (Online Document)

9. **Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine zilizotekeliza ni pamoja na: kuboresha utoaji na usimamizi wa leseni za madini; kuendeleza uchimbaji mdogo wa madini; kuimarisha usimamizi wa afya, usalama na utunzaji wa mazingira migodini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; na kuziwezesha Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Nishati na Madini kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa manufaa ya Watanzania wote.

10. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2014/15, pamoja na masuala mengine, Wizara imelenga kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia inayojumuisha ujenzi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam na mitambo ya kusafisha gesi asilia; kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kipaumbele chini ya mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa (Big Results Now - BRN); kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme vijiji na Makao Makuu ya Wilaya; kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli katika Sekta za Nishati na Madini; kuendeleza uchimbaji mdogo na wa kati wa madini; kuimarisha usimamizi wa biashara ya madini; na kuvutia uwekezaji katika Sekta za Nishati na Madini, hususan nishati jadidifu (renewable energies) na makaa ya mawe.

Taarifa ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka 2013/14

11. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka 2013/14, Wizara ya Nishati na Madini ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 220**. Hadi kufikia tarehe 23 Mei, 2014 jumla ya **Shilingi bilioni 147.14** zilikusanywa, sawa na **asilimia 67** ya lengo. Juhudi zinaendelea ili kuhakikisha kuwa lengo la ukusanyaji linafikiwa kama ilivyopangwa na hivyo kuongeza mapato ya Serikali.

Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2013/2014

12. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14, Wizara iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,289,329,129,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 110,216,384,000** zilikuwa ni Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,179,112,745,000** zilikuwa ni fedha za maendeleo.

13. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 23 Mei, 2014 jumla ya **Shilingi 83,202,288,459** sawa na **asilimia 75** ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa. Aidha, jumla ya **Shilingi 577,526,232,810** sawa na **asilimia 49** ya Bajeti yote ya Maendeleo zilipokelewa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **431,010,106,443** ni fedha za ndani, sawa na **asilimia 58** ya fedha za ndani zilizotengwa na Shilingi **146,516,126,367** ni fedha za nje, sawa na **asilimia 34** ya fedha za nje zilizotengwa. Hivyo, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi**

Nakala ya Mtandao (Online Document)

660,728,521,269 sawa na **asilimia 51** ya Bajeti yote iliyoidhinishwa kwa Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2013/2014.

14. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na usimamizi mzuri wa matumizi ya fedha za Serikali, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Nishati na Madini ni mionganoni mwa Wizara zilizopata Hati Safi ya Hesabu za Mwaka 2012/13 isiyokuwa na swali lolote.

Wizara itaendelea kusimamia ipasavyo Sheria mbalimbali ili kuhakikisha fedha za walipa kodi zinatumika kwa manufaa ya Taifa letu na kwa Watanzania wote bila upendeleo wa aina yoyote.

Malengo ya Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015

15. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2014/15 Wizara ya Nishati na Madini inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 240.59**. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la **asilimia 9.36** ya lengo la Mwaka 2013/14 la **Shilingi bilioni 220**.

Mipango na mbinu zitakazotumika katika ukusanyaji wa mapato ni pamoja na: kuboresha Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini; kuhakikisha kuwa wamiliki wote wa leseni za madini nchini wanatimiza masharti ya leseni zao; na kuimarisha ushirikiano na taasisi nyingine za Serikali katika kuzuia utoroshaji wa madini.

16. **Mheshimiwa Spika**, mipango mingine ni kuongeza udhibiti katika kukusanya mapato yatokanayo na madini ya ujenzi na viwandani; kuimarisha usimamizi wa wachimbaji wadogo kwa kuwatambua na kutoa huduma za ugani ili kuongeza tija katika uzalishaji madini; na kuwahamasisha Wananchi kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Sekta za Nishati na Madini kuhusu umuhimu wa kulipa kodi na ada mbalimbali.

SEKTA YA NISHATI

UKUAJI WA SEKTA YA NISHATI

17. **Mheshimiwa Spika**, Dira ya Maendeleo ya Taifa (Tanzania Development Vision, 2025) ilianza kutekelezwa Mwaka 2000. Kupitia Dira hiyo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) imedhamiria kujenga uchumi wa kisasa utakaoiwezesha Tanzania kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja (GDP per

Nakala ya Mtando (Online Document)

capita) kutoka wastani wa **Dola za Marekani 640** hadi **3,000** ifikapo Mwaka 2025. Ili kufikia lengo hilo, nchi inahitaji kuwa na nishati ya kutosha, yenye uhakika na ya gharama nafuu. Kwa kutambua hilo, Serikali imeendeleza jitihada za kuboresha upatikanaji wa nishati bora vijiji na mijini kwa kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya nishati ikiwemo ya umeme, gesi asilia na mafuta.

18. Mheshimiwa Spika, sambamba na azma hiyo, Sekta ya Nishati imejumuishwa kwenye Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) ulioanzishwa na Serikali Mwaka 2013/14. Katika Sekta hiyo, miradi 29 ilianishwa ambayo inahusisha miradi 7 ya ufuaji, miradi 7 ya usafirishaji na miradi 14 ya usambazaji umeme pamoja na mradi mmoja wa miundombinu ya gesi asilia. Utekelezaji wa miradi ya BRN utachangia kufikiwa kwa malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025.

19. Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeendelea kudurusu na kuandaa Sera na Sheria mbalimbali katika Sekta ya Nishati ikiwemo Sera ya Taifa ya Nishati. Lengo ni kujenga mazingira yanayochochea uwekezaji kwa kushirikisha Sekta Binafsi, na hivyo kuongeza ufanisi na ushindani wa kibashara katika Sekta ya Nishati.

Mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Nishati

20. Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Nishati kwa Mwaka 2013/14 ni pamoja na:

Kuongezeka kwa idadi ya Watanzania waliunganishiwa umeme (**connection level**) kutoka **asilimia 21** Mwaka 2012/13 hadi kufikia **asilimia 24** Mwezi Machi, 2014.

Ikumbukwe kwamba kiwango cha uunganishwaji wa umeme kilikuwa **asilimia 10** mwaka 2005 wakati Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipoingia madarakani.

Mafanikio mengine ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya watu waliofikiwa na huduma ya umeme (**access level**) kufikia **asilimia 36** Mwezi Machi, 2014; kukamilika kwa ujenzi wa mtambo wa kufua umeme MW 60 huko Nyakato, Mwanza; kufunga vipozea umeme (transformers) vyenye uwezo wa MVA 15 katika vituo vya Bahari Beach, Gongolamboto, Kigamboni na Kunduchi; kufunga vipozea umeme viwili vyenye uwezo wa MVA 90 kila kimoja katika vituo vya Kipawa na Ubungo; kusainiwa kwa mikataba 35 ya utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijiji (Turnkey Phase II); kuwasili kwa mitambo miwili ya kufua umeme yenye uwezo wa MW 75,

Nakala ya Mtando (Online Document)

kati ya mitambo minne ya mradi wa MW150 wa Kinyerezi – I; na kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme nchini na hivyo kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii.

21. **Mheshimiwa Spika**, mafanikio mengine ni pamoja na: kupertishwa kwa Sera ya Gesi Asilia Mwezi Oktoba, 2013; kukamilika kwa ujenzi wa Bomba la kusafirishia gesi asilia kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam kwa **asilimia 77.8**; kukamilika kwa maandalizi ya kufunga mitambo ya kusafisha gesi asilia kwa **asilimia 44.8**; kugunduliwa kwa gesi asilia inayofikia **futi za ujazo trilioni 4.8** kwenye visima vilivyopo kina kirefu cha Bahari na hivyo kufanya jumla ya kiasi cha gesi asilia kilichogundulika hapa nchini hadi sasa kufikia **futi za ujazo trilioni 46.5**; kuzinduliwa kwa duru ya nne ya utafutaji mafuta na gesi asilia katika kina kirefu baharini na Kaskazini mwa Ziwa Tanganyika; na kuanzishwa kwa kitengo maalumu (Ministerial Delivery Unit - MDU) cha kufuatilia utekelezaji wa miradi ya BRN katika Sekta ya Nishati.

22. **Mheshimiwa Spika**, mafanikio yote hayo ni matokeo ya utekelezaji thabiti wa llani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 - 2015 inayositiza upatikanaji wa nishati ya uhakika kwa ajili ya kujenga uchumi wa kisasa na imara unaozingatia maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Ukuaji wa uchumi imara ndio utakaotoa ajira mpya na matumaini mapya kwa vijana na maskini katika nchi yetu.

SEKTA NDOGO YA UMEME

Hali ya Uzalishaji Umeme

23. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14, Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha upatikanaji wa umeme nchini. Hadi mwishoni mwa mwezi Aprili, 2014 uwezo wa mitambo yote ya kufua umeme (total installed capacity) ulifikia **MW 1,583** (majji - **asilimia 35**, gesi asilia - **asilimia 34** na mafuta - **asilimia 31**). Uwezo huo wa mitambo yote ni sawa na ongezeko la **asilimia 78** ikilinganishwa na **MW 891** zilizokuwepo mwaka 2005 wakati Serikali ya Awamu ya Nne inaingia madarakani. **Hili ni jambo la kujivunia kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi.**

24. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013 kiasi cha umeme kilichoingizwa kwenye Gridi ya Taifa kiliongezeka na kufikia GWh 5,997.41 ikilinganishwa na GWh 5,760 za Mwaka 2012, sawa na ongezeko la **asilimia 4**. Aidha, mahitaji ya juu ya matumizi ya umeme kwa Mwaka 2013/14 yalifikia wastani wa **MW 898.72** ikilinganishwa na **MW 851.35** kwa mwaka 2012/13, sawa na ongezeko la **asilimia 6**.

Miradi ya Kufua Umeme

Mradi wa MW 60 Nyakato - Mwanza

25. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imekamilisha mradi wa ujenzi wa mitambo ya MW 60 inayotumia mafuta mazito katika eneo la Nyakato, Jijini Mwanza.

Mradi huo ulizinduliwa rasmi na Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 8 Septemba, 2013. Kuzinduliwa kwa mradi huo kumeimarisha upatikanaji wa umeme katika Kanda ya Ziwa Victoria.

Mradi wa Kinyerezi I - MW 150

26. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14 utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa MW 150 kwa kutumia gesi asilia katika eneo la Kinyerezi, Jijini Dar es Salaam unaendelea vizuri. Mradi huo utakapokamilika utapunguza utegemezi wa mitambo ya kukodi inayotumia mafuta kufua umeme ambayo ni ghali. Pia, mitambo miwili yenye uwezo wa kufua MW 75 kati ya mitambo minne (4) iliwasili nchini Mwezi Februari, 2014. Aidha, ujenzi wa misingi ya kuwekea mitambo na matenki mawili (2) ya kuhifadhi mafuta kwa matumizi ya dharura umekamilika. Kazi nyingine zinazoendelea ni ujenzi wa jengo la utawala, karakana pamoja na miundombinu ya barabara na maji.

27. **Mheshimiwa Spika**, kazi zilizopangwa katika Mwaka 2014/15 ni pamoja na kukamilisha ufungaji wa mitambo ya kufua umeme; kujenga kituo cha kupozea umeme chenye uwezo wa kV 220/kV 400; kujenga njia ya kusafirishia umeme ya msongo wa kV 220 kutoka Kinyerezi hadi Kimara; na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 132 kutoka Kinyerezi hadi kituo cha kupozea umeme cha Gongolamboto. Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 183** sawa na **Shilingi bilioni 301**. Katika Bajeti ya Mwaka 2014/15 **Shilingi bilioni 90** sawa na **Dola za Marekani milioni 55** ikiwa ni fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha mradi huu. Mradi unatarajiwa kukamilika katika Mwaka 2014/15 ikiwa ni sehemu ya kutekeleza uamuzi wa Serikali wa kuondoa kero ya umeme nchini.

Mradi wa Kinyerezi II - MW 240

28. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14, Serikali ilikamilisha majadiliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika ya Kusini (DBSA), ambapo mkopo wa **asilimia 15** ya gharama ya mradi uliidhinishwa. Aidha, majadiliano kwa ajili ya mkopo wa **asilimia 85** ya gharama za mradi, kati ya Serikali na Benki za Sumitomo Mitsui

Nakala ya Mtando (Online Document)

Banking Corporation (SMBC) na Japan Bank of International Cooperation (JBIC) za Japan yamekamilika.

29. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2014/15, Serikali itaanza kutekeleza mradi huo ikiwa ni pamoja na kuagiza mitambo na kuandaa eneo itakapofungwa mitambo hiyo. Mkandarasi wa mradi ni Kampuni ya Sumitomo Corporation kutoka Japan. Gharama za mradi huo ni **Dola za Marekani milioni 344**, sawa na **Shilingi bilioni 564**. Ili kuanza utekelezaji wa mradi, fedha za nje **Shilingi bilioni 1**, sawa na **Dola za Marekani 609,756** zimetengwa. Ujenzi wa mradi umepangwa kukamilika katika Mwaka 2015/16.

Mradi wa Kinyerezi III - MW 300

30. **Mheshimiwa Spika**, makubaliano ya ubia (Joint Venture Agreement) kwa ajili ya kuendeleza mradi wa Kinyerezi III kati ya TANESCO na Kampuni ya China Power Investment (CPI) yamekamilika na kusainiwa Mwezi Oktoba, 2013. Taratibu za uundwaji wa Kampuni ya ubia zimekamilika, ambapo Serikali kupitia TANESCO itamili **asilimia 40** ya hisa na CPI **asilimia 60**. Katika Mwaka 2014/15, TANESCO na CPI zitateua wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi kwa ajili ya kuanza kusimamia utekelezaji wa mradi huo. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa ni **Dola za Marekani milioni 389** sawa na **Shilingi bilioni 638**.

Mradi wa Kinyerezi IV - MW 300

31. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TANESCO iliingia Makubaliano ya Awali (MoU) na Kampuni ya Poly Technologies kutoka China Mwezi Septemba, 2013 kwa ajili ya kuendeleza mradi wa Kinyerezi IV. Mradi utatekelezwa kwa njia ya ubia utakaozihusisha Kampuni za Golden Concord Development Limited (**asilimia 40**), China – Africa Development Limited (**asilimia 30**) za China na TANESCO (**asilimia 30**).

32. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2014/15, kazi zitakazofanyika ni pamoja na kukamilisha upembizi yakinifu wa mradi na Tathmini ya Athari za Mazingira na Kijamii (ESIA); kukamilisha mkataba wa ubia na uundwaji wa Kampuni ya ubia; pamoja na uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi.

33. **Mheshimiwa Spika**, miradi niliyoieleza hapo juu inatekelezwa kupitia mfumo mpya wa usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya kimkakati ya Kitaifa yaani BRN.

Mradi wa Kuzalisha MW 600 Mkoani Mtwara

34. **Mheshimiwa Spika**, Mwezi Novemba, 2013 Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO iliidhinisha utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa MW 600 Mkoani

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mtwara. Mradi huo utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa KV 400 kutoka Mtwara hadi Songea.

Kampuni ya Symbion ya Marekani inayotekeleza mradi huo imeajiri Kampuni ya MPR Associates kutoka Marekani kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa mradi. Kazi hiyo imeanza na inategemewa kukamilika Mwezi Juni, 2014. Baada ya kazi hiyo kukamilika Kampuni ya Symbion na TANESCO zitaanza majadiliano kuhusu masuala ya kiufundi na fedha. Utekelezaji wa mradi huo utaimarisha upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma pamoja na kuingiza katika Gridi ya Taifa. Aidha, ujenzi wa mradi huo utawezesha kuuza umeme wa ziada nchi jirani zikiwemo Malawi na Msumbiji.

Mradi wa Kufua Umeme wa Rusumo – MW 80

35. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa Rusumo unatekelezwa kwa pamoja na nchi za Rwanda na Burundi. Mradi pia unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa KV 220 kutoka Rusumo hadi kwenye mifumo ya usafirishaji umeme kwa nchi husika. Kwa upande wa Tanzania njia ya kusafirisha umeme itaunganishwa katika Gridi ya Taifa katika kituo cha Nyakanazi.

Kazi zilizokamilika katika Mwaka 2013/14 ni zifuatazo: upembuzi yakinifu; Tathmini ya Athari ya Mazingira na Kijamii (ESIA); kusainiwa kwa Mkataba wa Utekelezaji Mradi (Implementation Agreement); na Mkataba wa Wana Hisa (Share Holding Agreement).

Aidha, majadiliano ya mkopo kati ya Serikali za Burundi, Rwanda na Tanzania, pamoja na Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika yilikamilika. Mradi utaanza kutekelezwa Mwaka 2014/15, na utagharimu kiasi cha **Shilingi bilioni 164**, sawa na **Dola za Marekani milioni 100**. Fedha za nje zilizotengwa na Serikali ni **Shilingi bilioni 2**, sawa na **Dola za Marekani milioni 1.22** kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huu.

Miradi ya Kufua Umeme Kutokana na Makaa ya Mawe

36. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kusimamia uendelezaji wa miradi ya kufua umeme kutokana na makaa ya mawe ya Kiwira - MW 200, Mchuchuma - MW 600 na Ngaka - MW 400. Miradi ya Mchuchuma na Ngaka inatekelezwa na Wizara ya Viwanda na Biashara kuitia Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC). Kwa upande wa mradi wa Kiwira unaosimamiwa na STAMICO, kazi zilizofanyika Mwaka 2013/14 ni kudurusu taarifa za kitaalamu za utafiti, upembuzi yakinifu na mazingira zilizofanyika miaka ya nyuma.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kazi zilizopangwa kufanyika katika Mwaka 2014/15 ni pamoja na: kufufua mgodi wenyewe uwezo wa kuzalisha tani 150,000 za makaa ya mawe kwa mwaka; kukarabati mtambo wa kufua umeme uliopo mgodini wa MW 6; kukamilisha upatikanaji wa mbia kwa ajili ya mradi mkubwa wa kuzalisha MW 200; na kulipa fidia kwa watakaopisha mradi na njia ya umeme wa msongo wa KV 400 wa urefu wa kilomita 100 kutoka mgodini hadi eneo la Uyole, Mbeya ili kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 400**, sawa na takriban **Shilingi bilioni 656**. Katika Mwaka 2014/15, **Shilingi bilioni 5** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza baadhi ya kazi zilizotajwa hapo juu.

Ukarabati wa Mitambo ya Kufua Umeme katika Kituo cha Hale

37. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu wa ukarabati wa mitambo ya kufua umeme katika kituo cha Hale unaofadhiliwa na Serikali ya Sweden. Lengo ni kuwezesha kituo hicho kufua umeme kufikia uwezo wake wa juu kabisa wa MW 21 badala ya MW 10 zinazofuliwa sasa. Katika Mwaka 2014/15 **Shilingi bilioni 3**, sawa na **Dola za Marekani milioni 1.83** zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa mitambo hiyo.

Kuimarisha Njia za Kusafirisha na Kusambaza Umeme

(i) Mradi wa Iringa - Shinyanga KV 400 (Backbone)

38. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa kilomita 670 za usafirishaji umeme wa msongo wa KV 400 kutoka Iringa kupitia Dodoma na Singida hadi Shinyanga. Aidha, vituo vya kupozea umeme wa msongo wa KV 400/220/33 pamoja na njia za usambazaji umeme za msongo wa KV 33 zitajengwa. Mwezi Novemba, 2013 TANESCO ilisaini mikataba ya ujenzi na Kampuni za KEC International Limited na Jyoti Structures Limited za India.

TANESCO pia ilisaini mikataba na umoja (consortium) wa Kampuni za GS Engineering and Construction na Hyosung kutoka Korea Kusini kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Kazi nyingine iliyofanyika ni ulipaji wa fidia katika maeneo ya Igunga, Kishapu na Shinyanga. Pia, kazi za upimaji (detailed survey), utayarishaji usanifu na uidhinishaji wa michoro zinaendelea.

39. **Mheshimiwa Spika**, kazi zilizopangwa kufanyika katika Mwaka 2014/15 ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya mradi; maandalizi ya usambazaji wa umeme

Nakala ya Mtandao (Online Document)

wa Gridi katika vijiji zaidi ya 90 ambako mradi utatekelezwa; na kuanza ujenzi wa njia za usafirishaji umeme.

Jumla ya **Shilingi bilioni 2.50** sawa na **Dola za Marekani milioni 1.52** zimetengwa kwa Mwaka 2014/15 ili kutekeleza mradi huu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 500** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 2** ni fedha za nje kutoka Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo la Japan (JICA), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) na Shirika la Maendeleo la Korea (EDCF). Mradi utagharimu **Dola za Marekani milioni 224** sawa na **Shilingi bilioni 367.36** na unatarajiwa kukamilika Mwaka 2015/16.

(ii) Mradi wa Makambako - Songea kV 220

40. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Ibara 63 (u) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 - 2015, Wizara inaendelea na taratibu za kuanza utekelezaji wa mradi huo. Mradi utahusisha ujenzi wa kilomita 250 za njia za kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 kutoka Makambako hadi Songea; kujenga vituo vikuu viwili (Madaba na Songea) vya kupozea umeme wa msongo wa kV 220/33 na kuongeza uwezo wa kituo cha kupozea umeme cha Makambako; ujenzi wa kilomita 900 za njia za usambazaji umeme za msongo wa kV 33.

Lengo la mradi huu ni kuunganisha Wilaya za Ludewa, Mbinga, Namtumbo, Njombe, Songea Mjini na Songea Vijiji katika Gridi ya Taifa. Mradi pia utahusisha kuwaunganishia wateja wa awali 30,000 ambao watatakiwa kulipia kodi ya ongezeko la thamani (VAT) pekee.

41. **Mheshimiwa Spika**, Mwezi Januari, 2014 TANESCO ilisaini mkataba na Kampuni ya Isolux kutoka Hispania kwa ajili ya kutekeleza mradi wa usambazaji umeme. Aidha, uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya ujenzi wa njia ya usafirishaji umeme umekamilika na maombi ya "no objection" yamewasilishwa Shirika la Maendeleo la Sweden (Sida). Vilevile, ulipaji fidia kwa watakaopisha mradi katika maeneo ya Mkoa wa Ruvuma umekamilika kwa **asilimia 95** na uhakiki wa malipo kwa Mkoa wa Njombe unaendelea.

42. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2014/15, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kuanza ujenzi wa njia ya usafirishaji umeme na vituo vya kupozea umeme pamoja na njia za kusambaza umeme.

Jumla ya **Shilingi bilioni 16.30** sawa na **Dola za Marekani milioni 9.94** zimetengwa ili kutekeleza kazi zilizopangwa. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni **Shilingi milioni 300** na fedha za nje ni **Shilingi bilioni 16**. Mradi umepangwa kukamilika Mwaka 2015/16.

(iii) **Mradi wa North - East Grid kV 400**

43. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu ni wa ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme wa msongo wa kV 400 yenyeye urefu wa kilomita 664 kutoka Kinyerezi hadi Arusha kupidia Chalinze na Segera. Pia, mradi utahusisha ujenzi wa njia za kusafirishia umeme wa msongo wa kV 220 zenyeye jumla ya kilomita 104 kutoka Segera kwenda Tanga na kutoka Kibaha kwenda Bagamoyo.

Aidha, vituo vikubwa vya kupozea umeme vya Bagamoyo, Chalinze, Segera na Tanga vitajengwa kwa ajili ya kuwezesha usambazaji umeme katika Wilaya na Miji Midogo ambayo njia za umeme zitapita. Kazi zilizokamilika Mwaka 2013/14 ni upembuzi yakinifu wa mradi; Tathmini ya Athari za Mazingira na Kijamii (ESIA); na upimaji wa awali wa ardhi. Aidha, kazi za usanifu wa michoro ya mradi na uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya kumpata mshauri wa mradi zinaendelea.

44. **Mheshimiwa Spika**, kazi zilizopangwa kwa Mwaka 2014/15 ni pamoja na kukamilisha upimaji wa ardhi na kuweka mipaka ya eneo la mradi; kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha eneo la mradi; na kumpata mshauri kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.50** sawa na **Dola za Marekani 914,630** zimetengwa ili kutekeleza mradi huu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 1.0** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 500** ni fedha za nje. Mradi unatarajiwa kukamilika Mwaka 2016/17.

(iv) **Mradi wa North - West Grid kV 400**

45. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 400 kutoka Mbeya kupidia Sumbawanga – Mpanda - Kigoma hadi Nyakanazi yenyeye urefu wa kilomita 1,148. Awamu ya kwanza ya mradi itahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme yenyeye urefu wa kilomita 340 kutoka Mbeya hadi Sumbawanga, na vituo vikubwa vipyta vya kupozea umeme vya Uyole (Mbeya) na Sumbawanga.

46. **Mheshimiwa Spika**, kazi zilizofanyika kwa Mwaka 2013/14 ni pamoja na kutathmini upya Athari za Mazingira na Kijamii (ESIA); kudurusu upembuzi yakinifu baada ya kubadilisha njia ya kusafirisha umeme kutoka msongo wa kV 220 kwenda kV 400; upimaji wa mkuza itakakojengwa njia ya kusafirisha umeme; na kutathmini fidia kwa watakaopisha awamu ya kwanza ya mradi.

47. **Mheshimiwa Spika**, kazi zilizopangwa kufanyika Mwaka 2014/15 ni pamoja na kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi ili kuwiana na mahitaji ya sasa ya msongo wa kV 400; upimaji wa mkuza itakakojengwa njia ya kusafirisha umeme kutoka Mbeya hadi Sumbawanga; na kulipa fidia kwa watakaopisha

Nakala ya Mtandao (Online Document)

mradi. Fedha za ndani **Shilingi bilioni 1.0**, sawa na **Dola za Marekani 609,756** zimetengwa. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwaka 2016/17.

(v) Mradi wa Singida – Arusha - Namanga kV 400

48. **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 63 (b) na (t) ya llani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 - 2015 inatoa msisitizo kuhusu kuunganisha Gridi yetu ya Taifa na nchi jirani ili kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika. Mradi wa Singida - Arusha - Namanga ni sehemu ya mradi wa Zambia – Tanzania – Kenya (ZTK interconnector) yenye urefu wa kilomita 2,047. Kwa upande wa Tanzania, mradi utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 400 kutoka Singida hadi Arusha na kutoka Iringa hadi Mbeya.

49. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14, kazi zilizofanyika ni zifuatazo: kukamilika kwa upembusi yakinifu wa mradi na Tathmini ya Athari za Mazingira na Kijamii (ESIA); na upimaji wa mkuza kwa ajili ya njia ya kusafirisha umeme.

Kazi zilizopangwa kufanyika Mwaka 2014/15 ni pamoja na kukamilisha tathmini ya mali na kulipa fidia; ujenzi wa kituo kipyaa cha kupozea umeme katika eneo la Kisongo, Mkoani Arusha na upanuzi wa kituo cha kupozea umeme Mkoani Singida. Kazi nyingine ni kuajiri mshauri wa mradi na kupata wakandarasi wa ujenzi wa vituo vya kupozea umeme na njia ya kusafirisha umeme; na kuandaa mpango wa kusambaza umeme kwenye vijiji vilivyo kando kando ya njia ya kusafirisha umeme. Fedha za nje zilizotengwa ni **Shilingi milioni 500**, sawa na **Dola za Marekani 304,878** ambazo ni mkopo kutoka AfDB na JICA. Mradi umepangwa kukamilika Mwaka 2016/17.

50. **Mheshimiwa Spika**, sambamba na jitihada hizo, Serikali kuitia TANESCO itatekeleza mradi wa upanuzi wa njia ya usambazaji umeme ya Tunduma hadi Nakonde (Zambia) ya msongo wa kV 33 na urefu wa mita 100. Mradi pia utahusisha ufungaji wa kipozea umeme chenye uwezo wa kVA 200 na ukarabati wa njia ya kusambaza umeme kutoka Mbeya hadi Tunduma yenye urefu wa kilomita 40. Katika Mwaka 2013/14, upimaji na tathmini ya njia ya usambazaji umeme vilikamilika.

Aidha, Kitengo cha kusimamia mradi kimeundwa na taarifa ya Tathmini ya Athari za Mazingira na za Kijamii imewasilishwa Baraza la Usimamizi wa Mazingira la Taifa (NEMC) kwa ajili ya kupata idhini ya utekelezaji wa mradi. Katika Mwaka 2014/15, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 5**, sawa na **Dola za Marekani milioni 3.05** ili kuendelea na utekelezaji wa mradi huu.

(vi) Mradi wa Bulyanhulu – Geita kV 220

51. **Mheshimiwa Spika**, mradi unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa KV 220 yenye urefu wa kilomita 55 kutoka Bulyanhulu hadi Geita.

Mradi pia unahusisha ujenzi wa kituo cha kupozea umeme cha Geita chenye uwezo wa KV 220/33, usambazaji umeme katika vijiji vilivyopo ndani ya eneo la mradi na kubadilisha mita za umeme za kawaida (conventional meters) zipatazo 2,000 Mkoani Geita kwa kufunga mita za LUKU.

Kazi zilizofanyika Mwaka 2013/14 ni pamoja na: kuundwa kwa Kitengo cha usimamizi wa mradi (Project Implementation Unit) na kuanza kwa taratibu za upimaji wa eneo la mradi. Aidha, tathmini ya zabuni ya kumpata mshauri wa mradi inaendelea.

52. **Mheshimiwa Spika**, kazi zitakazofanyika Mwaka 2014/15 ni zifuatazo: kukamilisha upimaji wa eneo la mradi; kulipa fidia kwa watakaopisha mradi; kumpata mshauri na mkandarasi wa mradi; na kuanza utekelezaji wa mradi. Gharama za mradi ni **Shilingi bilioni 41** sawa na **Dola za Marekani milioni 25**. Jumla ya **Shilingi bilioni 2.50** sawa na **Dola za Marekani milioni 1.52** zimetengwa ili kutekeleza mradi huu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 2** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 500** ni fedha za nje kutoka Bank of Arab for Economic Development in Africa (BADEA). Mradi umepangwa kukamilika Mwaka 2015/16.

(vii) **Mradi wa Electricity V**

53. **Mheshimiwa Spika**, mradi unalenga kuunganisha wateja wa awali 8,600 kwenye Wilaya za Bukombe, Busega, Kwindu, Magu, Mbogwe, Misungwi na Sengerema katika Mikoa ya Geita, Mwanza na Simiyu. Ujenzi wa njia za usambazaji wa umeme wa msongo wa KV 33 zenye urefu wa kilomita 480, KV 0.4 zenye urefu wa kilomita 231 na ufungaji wa vipozea umeme 109 utafanyika chini ya mradi huu.

Shughuli nyingine ni ukarabati wa vituo vya kupozea umeme vya Ilala KV 132/33/11 na Sokoine KV 33/11, katika Jiji la Dar es Salaam pamoja na upanuzi wa kituo cha kupozea umeme cha KV 220/132/33 Njiro, Mkoani Arusha.

54. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kuanza kwa ukarabati wa kituo cha kupozea umeme cha Sokoine Drive, Ilala (Dar es Salaam); kukamilisha ukaguzi wa maeneo na michoro ya kazi za usambazaji umeme; kukamilika kwa utafiti wa udongo kwenye vituo vya kupozea umeme vya Sokoine Drive, Ilala (Dar es Salaam) na Arusha; kuanza kwa ulipaji fidia kwa watakaopisha mradi; kuwasili kwa vifaa vya usambazaji umeme ikiwa ni pamoja na nguzo 890 katika maeneo ya mradi; na kuendelea kwa kazi ya usanifu wa mradi.

55. **Mheshimiwa Spika**, kazi zitakazotekelawa katika Mwaka 2014/15 ni zifuatazo: kukamilisha ukarabati wa kituo cha Sokoine Drive, Ilala (Dar es Salaam) na Arusha. Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 45** sawa na **Shilingi bilioni 73.80**. Jumla ya **Shilingi bilioni 4**, sawa na **Dola za Marekani milioni 2.44** zimetengwa ili kutekeleza kazi zilizopangwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 3.50** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 500** ni fedha za nje kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Mradi umepangwa kukamilika Mwaka 2014/15.

Mradi wa Kuboresha Upatikanaji wa Umeme Jijini Dar es Salaam

56. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unafadhiliwa na Serikali za Finland na Japan na unahu ujenzi wa kituo kipyaa cha kupozaa umeme mkabala na kituo cha City Centre cha msongo wa KV 132/33/11, ujenzi wa njia ya usafirishaji umeme wa msongo wa KV 132 kutoka kituo cha Ilala na kuunganisha mfumo wa vituo vya kupozaa umeme wa KV 33/11 vya City Centre, Kariakoo, Railway na Sokoine.

Lengo la mradi huu ni kuboresha miundombinu ya umeme ili kuwezesha upatikanaji wa umeme wenye ubora na uhakika zaidi katika Jiji la Dar es Salaam.

57. **Mheshimiwa Spika**, kazi zilizotekelawa kwa Mwaka 2013/14 ni zifuatazo: kupatikana kwa eneo la ujenzi wa kituo cha kupozaa umeme cha City Centre; kukamilisha upembuzi yakinifu wa mradi; ulipaji fidia kwa watakaopisha mradi; na kuanza kwa ujenzi wa kituo.

Kazi zifuatazo zitatekelezwa kwa Mwaka 2014/15: kuendelea na ujenzi wa kituo cha City Centre na njia za usafirishaji na usambazaji umeme. Gharama za mradi ni **Shilingi bilioni 123** sawa na **Dola za Marekani milioni 75**. Fedha za nje zilizotengwa ni **Shilingi bilioni 1.0** na mradi umepangwa kukamilika Mwaka 2014/15.

Mradi wa Ufuaji na Usambazaji Umeme – Biharamulo, Mpanda na Ngara (ORIO)

58. **Mheshimiwa Spika**, mradi unahusisha ufungaji wa jenereta zenyе uwezo wa MW 2.5 kila moja katika Wilaya za Biharamulo, Mpanda na Ngara na hivyo kufanya jumla ya uwezo wa MW 7.5. Pia, ukarabati wa njia zilizopo na ujenzi wa njia mpya za usambazaji umeme zenyе msongo wa kV 33 utafanyika. Lengo la mradi huu ni kuongeza uwezo wa ufuaji na usambazaji umeme katika Wilaya hizo.

59. **Mheshimiwa Spika**, kazi zilizofanyika katika Mwaka 2013/14 ni pamoja na: kusainiwa kwa mkataba kwa ajili ya ufungaji jenereta hizo kati ya TANESCO na Kampuni ya M/s Zwart Techniek B.V. ya Uholanzi Mwezi Oktoba, 2013; kusainiwa kwa mikataba kati ya TANESCO na Kampuni ya Nakuroi Investment ya Tanzania kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa mifumo ya usambazaji umeme Mpanda; na Kampuni ya NAMIS ya Tanzania kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa mifumo ya usambazaji umeme katika Wilaya za Biharamulo na Ngara. Mikataba husika ilisainiwa Mwezi Desemba, 2013.

60. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2014/15 kazi zitakazofanyika ni zifuatazo: kufunga jenereta katika Wilaya za Biharamulo, Mpanda na Ngara; kukarabati na kujenga njia mpya za usambazaji umeme katika Wilaya za Mpanda, Biharamulo na Ngara; na kutoa mafunzo kwa ajili ya usimamizi wa miradi kwa wajasiriamali na watumiaji wa umeme katika Wilaya hizo. Mradi huo utakapokamilika unatarajiwa kuwaunganishia umeme wateja wapya zaidi ya 100,000.

61. **Mheshimiwa Spika**, gharama za mradi huo ni **EURO milioni 33.15** sawa na **Shilingi bilioni 81.55**. Jumla ya **Shilingi bilioni 22.50** sawa na **Dola za Marekani milioni 13.72** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu Mwaka 2014/15. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 22** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 500** ni fedha za nje kutoka Serikali ya Uholanzi. Mradi umepangwa kukamilika Mwaka 2015/16.

Usambazaji Umeme kupitia TANESCO na Wakala wa Nishati Vijijini (REA)

62. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza Ibara ya 63 (c) ya llani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 – 2015, inayohamasisha kuongeza idadi ya wananchi waliouanganishiwa umeme mijini na vijijini. Wakati Serikali ya Awamu ya Nne inaingia madarakani kiwango cha uunganishwaji (**connection level**) nchini kilikuwa **asilimia 10**.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kufuatia jitihada mahsusi za Serikali ikiwemo punguzo la ghamama za kuunganisha umeme pamoja na uwezeshaji chini ya Mfuko wa Nishati Vijijini (Rural Energy Fund - REF), kiwango cha uunganishwaji umeme kimeongezeka na kufikia **asilimia 24** Mwezi Machi 2014. Lengo la Serikali ni kuwawezesha Watanzania **asilimia 30** kuunganishiwa umeme (**connection**) ifikapo Mwaka 2015/16. Aidha, kiwango cha uunganishwaji umeme vijijini kimeongezeka kutoka **asilimia 2** Mwaka 2005 hadi **asilimia 7** mwishoni mwa Mwaka 2013.

63. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Mwezi Machi, 2014 watu wanaopata huduma ya umeme (**access level**) walifikia **asilimia 36** ya Watanzania waishio Bara.

Hivyo, Watanzania wanashauriwa kutumia fursa ya huduma ya umeme ili ichangie katika shughuli za kiuchumi na kijamii na hivyo kuinua hali ya maisha yao mijini na vijijini na kuanza kupunguza na hatimaye kutokomeza umaskini.

64. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na juhudhi nyingine, mafanikio hayo yametokana na utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini uliokuwa na miradi midogo 41 katika Mikoa 16 ya Tanzania Bara (Arusha, Dodoma, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Pwani, Rukwa, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga). Kuanzia Mwezi Julai 2013 hadi Aprili 2014, wateja wapya 15,817 walikuwa wameunganishiwa umeme kati ya wateja 22,000 waliotarajiwa. Aidha, kuititia lengo la BRN la kuunganisha wateja 150,000 kwa mwaka, jumla ya wateja wapya 138,931 waliunganishiwa umeme sawa na asilimia 92.62 ya lengo hilo. Ongezeko hili linatokana na uamuvi wa Serikali kupunguza ghamama za kuunganishia umeme wa wateja wa njia moja (single phase) mijini na vijijini kwa wastani wa kati ya asilimia 30 hadi 77 ulioanza kutekelezwa Mwezi Januari, 2013.

65. **Mheshimiwa Spika**, REA imesaini mikataba na wakandarasi 35 wa kutekeleza Awamu ya Pili ya Mradi Kabambe wa Usambazaji Umeme Vijijini katika mikoa mbalimbali Tanzania Bara. Utekelezaji wa mradi huo utaendelea katika Mwaka 2014/15, ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 290.20** sawa na **Dola za Marekani 176.95** zimetengwa kutekeleza miradi hiyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 269.20** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 21** ni fedha za nje kutoka Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD).

Mpango wa Kitaifa wa Kuhamasisha Uwekezaji kwenye Usambazaji Umeme

Nakala ya Mtandao (Online Document)

66. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeandaa Mpango wa Usambazaji Umeme Nchini kwa kipindi cha miaka 10 kuanzia Mwaka 2013 hadi 2022 (The National Electrification Programme Prospectus).

Katika kipindi hicho, Mpango huo utakuwa ndiyo mwongozo wa miradi ya Serikali ya kusambaza umeme vijijiini. Maandalizi ya Mpango huo yamefadhiiliwa na Serikali ya Norway.

Mradi wa Kusambaza Umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara

67. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia REA inaendelea na utekelezaji wa jumla ya miradi 52 ya kusambaza umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Hadi Mwezi Aprili, 2014 miradi 47, sawa na **asilimia 97** ilikamilika, ambapo wateja 1,925 waliunganishiwa umeme. Kati ya hao wateja 1,135 ni kutoka Mkoa wa Lindi na wateja 790 ni kutoka Mkoa wa Mtwara. Gharama za miradi hiyo ni **Shilingi bilioni 6.10**, sawa na **Dola za Marekani milioni 3.72**.

Katika Mwaka 2014/15, Serikali itakamilisha miradi mitano (5) iliyobaki. Gharama ya kuunganisha umeme kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara ni **Shilingi 99,000** kwa umbali usiozidi mita 30. Gharama hizi zitatumika hadi kufikia Mwezi Juni, 2015. Natoa ushauri kwa wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara kutumia fursa hiyo kuunganishiwa umeme ili kuboresha maisha yao kupitia shughuli endelevu za kiuchumi na kijamii.

Tanzania Energy Development and Access Expansion Project (TEDAP)

68. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu ni wa uboreshaji wa mifumo ya Gridi (on-grid) na kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu kama vyanzo mbadala vya kufua umeme nje ya Gridi (off-grid). Kazi zilizotekelawa Mwaka 2013/14 kwa upande wa Gridi ni zifuatazo: kukamilika kwa ufungaji wa vipozea umeme viwili vyenye uwezo wa MVA 20 katika kituo cha umeme cha Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA). Kukamilika kwa kazi hiyo kumeboresha upatikanaji umeme katika maeneo ya Mererani, Usa River na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro. Gharama za mradi huo kwa upande wa on-grid ni **Dola za Marekani milioni 114.50** sawa na **Shilingi bilioni 187.78**.

Aidha, kwa upande wa mifumo ya nje ya Gridi, kazi zilizofanyika ni zifuatazo: kuwezesha ukamilishaji wa mradi wa maporomoko madogo ya maji wa Mapembasi (Njombe) unaotekelawa na Sekta Binafsi; kuwezesha wafuaji wa umeme wa uwezo mdogo (small power producers) kutumia mkopo kutoka Benki ya Dunia (IDA Credit Line); kugharamia ukamilishaji mradi wa pamoja na kufunga mifumo ya Umeme Jua katika Wilaya za Bunda, Geita na Tandahimba; na kukagua mifumo ya Umeme Jua katika Wilaya ya Sumbawanga chini ya

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Awamu ya Kwanza ya Sustainable Solar Market Packages (SSMP). Gharama za mradi kwa upande wa off-grid ni **Dola za Marekani milioni 47.50** sawa na **Shilingi bilioni 77.90**. Mradi huu unafadhliliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Benki ya Dunia na Serikali ya Korea ya Kusini.

69. **Mheshimiwa Spika**, kazi zitakazotekelawa kwa Mwaka 2014/15 ni zifuatazo: kuendelea kuboresha miundombinu ya umeme katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Kilimanjaro; kuendelea kuhamasisha na kuwezesha matumizi ya nishati bora; na kufadhili ujenzi wa mitambo ya kufua umeme kwenye maporomoko madogo ya maji. Aidha, Awamu ya Pili ya SSMP itahusisha ufungaji wa mifumo ya Umeme Jua kwenye taasisi za kijamii, makazi ya watu na sehemu za biashara. Wilaya zitakazonufaika ni Biharamulo, Bukombe, Chato, Kasulu, Kibondo, Namtumbo, Sikonge na Tunduru. Jumla ya **Shilingi bilioni 4.7**, sawa na **Dola za Marekani milioni 2.87** zimetengwa ili kutekeleza kazi zilizopangwa. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni **Shilingi milioni 700**, sawa na **asilimia 15**; na fedha za nje ni **Shilingi bilioni 4**, sawa na **asilimia 85** ya gharama zote za mradi.

70. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuhamasisha uendelezaji wa miradi ya kufua umeme kwa kutumia maporomoko madogo ya maji. Katika Mwaka 2013/14, Serikali kuitia EWURA ilitoa leseni tatu kwa Kampuni za Mwenga Hydro Limited ya Mufindi (MW 4); Ngombeni Power Limited ya Kisiwani Mafia (MW 1.5); Mapembasi ya Njombe (MW 10); na Tangulf Express Limited ya Njombe (MW 10).

71. **Mheshimiwa Spika**, ili kuboresha mazingira ya uwekezaji katika miradi midogo isiyozidi MW 10 ya kufua umeme kwa kutumia nishati jadidifu, katika Mwaka 2014/15, Serikali kuitia EWURA itakamilisha durusu ya Mwongozo wa mikataba ya kuuziana umeme (Standardised Power Purchase Agreement - SPPA) na Kanuni ya kukokotoa bei ya kuuziana umeme kwa miradi yenye uwezo wa kufua umeme kati ya kW 100 mpaka MW 10. Kukamilika kwa Kanuni na Mwongozo huo kutaimarisha uwekezaji nchini kwani bei itazingatia gharama halisi za kufua umeme pamoja na aina ya teknolojia itakayotumika. Lengo ni kuongeza kasi ya kuwapatia wananchi huduma ya umeme, hususan vijijini.

Ujenzi wa Miundombinu ya Umeme Kilombero na Ulanga

72. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekelezwa chini ya Mpango wa Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT) katika maeneo ya Kilombero na Ulanga. Katika Mwaka 2013/14 upembusi yakinifu ulikamilishwa. Katika Mwaka 2014/15, kazi zitakazofanyika ni pamoja na zifuatazo: kusimamia utekelezaji wa ujenzi wa njia kubwa ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV

Nakala ya Mtando (Online Document)

220; ujenzi wa kituo cha kupozea umeme cha kV 220/33 chenye uwezo wa MVA 20; na ujenzi wa njia za kusambaza umeme. Ili kutekeleza mradi huu, jumla ya fedha za nje **Shilingi bilioni 1.0**, sawa na **Dola za Marekani 609,756** zitazolewa na Umoja wa Nchi za Ulaya.

Kuboresha Upatikanaji wa Umeme

73. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa huduma ya umeme katika shughuli za kiuchumi na kijamii, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kuiwezesha TANESCO kutoa huduma bora. Miradi hiyo ni ya kipindi cha mpito wakati Serikali inakamilisha ujenzi wa miundombinu ya umeme wa gesi asilia. Katika Mwaka 2014/15, jumla ya **Shilingi bilioni 145**, sawa na **Dola za Marekani milioni 88** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 20**, sawa na **asilimia 14** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 125**, sawa na **asilimia 86** ni fedha za nje kutoka Benki ya Dunia.

74. **Mheshimiwa Spika**, Serikali pia imeendelea na zoezi la kutathmini muundo wa TANESCO na kuandaa Mwelekeo Mpya wa Sekta Ndogo ya Umeme (Electricity Supply Industry Reform Roadmap). Vilevile, Serikali imempata mshauri Kampuni ya PriceWaterCoopers (PWC) kutoka Uingereza, ambaye ametoa ushauri kuhusu zoezi hilo. Serikali inategemea kutangaza Roadmap hiyo ifikapo Mwezi Juni, 2014.

75. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii **kuupongeza vongozi wa TANESCO na watumishi wote kwa mabadiliko ambayo wameanza kuyatekeleza katika Shirika hilo na matokeo kuanza kuonekana**. Mabadiliko hayo ni pamoja na kuhamisha shughuli za ununuzi, utekelezaji wa Bajeti na Mipango kutoka Makao Makuu kwenda Ofisi za Kanda na Mikoa kwa nia ya kuboresha huduma zinazotolewa kwa wananchi. Utaratibu huu utasaidia kuongeza kasi ya kupeleka umeme wilayani na vijijini pamoja na kuharakisha matengenezo na ukarabati wa miundombinu ya umeme.

Uboreshaji wa Huduma kwa Wateja

76. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mahitaji ya juu ya umeme (Maximum Demand) kuongezeka kwa asilimia 8 kati ya Mwaka 2011 na 2013, TANESCO imehakikisha kuwa huduma ya umeme inaendelea kupatikana nchini. Sambamba na jitihada za TANESCO, inatarajiwa kuwa umeme wa uhakika utaendelea kupatikana kwa Mwaka 2014/15 kama ilivyokuwa kwa 2013/14.

Pamoja na kuwa na changamoto mbalimbali, naipongeza TANESCO kwa kuboresha utoaji huduma ya umeme nchini na hivyo kuimarisha shughuli za kiuchumi na kijamii.

77. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TANESCO inaendelea kuhakikisha kuwa vifaa vyote muhimu vya kuunganishia umeme wateja vikiwemo nguzo, mita na nyaya vinapatikana kwa wakati.

TANESCO pia imeendelea kuboresha huduma mbalimbali kwa wateja zikiwemo: kutumia mtandao (on-line) kupata fomu za maombi ya mwanzo ya kuunganishiwa umeme na kulipia ankara kwa wateja wanaolipa baada ya kutumia umeme; utoaji wa taarifa za katizo la umeme kwa ujumbe mfupi wa simu (sms); kuanzisha vituo maalum (point of sales) vya kulipia umeme karibu na wanachi; kulipia umeme kupitia benki; mpango wa kuwaunganishia wateja majumbani na Ofisi za Serikali mita za LUKU utakaotekelawa na kukamilishwa ndani ya kipindi cha miaka mitatu pamoja kuongeza matumizi ya mita za kisasa zifulikanazo kama Automatic Meter Reading (AMR).

SEKTA NDOGO YA NISHATI JADIDIFU

(i) Uendelezaji wa Umeme wa Jua

78. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14, wasambazaji wa mifumo ya Umeme wa Jua nchini waliongezeka kufuatia kukua kwa mahitaji na matumizi ya aina hiyo ya nishati. Aidha, wawekezaji wengi walionesha nia ya kujenga mifumo ya Umeme wa Jua yenye uwezo wa kuanzia MW 50 hadi MW 500 kwa ajili ya kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa. Katika Mwaka 2014/15, Serikali itaendelea kuhamasisha matumizi ya Umeme wa Jua.

79. **Mheshimiwa Spika**, Mwezi Januari, 2014 Serikali ilisaini Mkataba na Kampuni ya Elektro-Merl kutoka Austria kwa ajili ya kuleta na kufunga jenereta 14 za Umeme wa Jua (Photovoltaic Generators) zitakazotumika kusambaza umeme vijiji. Mradi huo utatekelezwa katika Mikoa ya Dodoma, Katavi, Ruvuma na Tabora. Gharama za mradi huo ni **Euro milioni 5.38** sawa na **Shilingi bilioni 14.20**.

(ii) Uendelezaji wa Nishati ya Upopo

80. **Mheshimiwa Spika**, taratibu za uendelezaji wa nishati ya upopo kupitia Sekta Binafsi zipo katika hatua mbalimbali. Majadiliano ya kuuziana umeme (Power Purchase Agreement - PPA) kati ya TANESCO na Kampuni ya Geo Wind Power (Singida) yanaendelea.

Katika awamu ya kwanza (2015/16), Kampuni hiyo inatarajia kufua umeme wa MW 50 ambapo **Dola za Marekani milioni 136**, sawa na **Shilingi bilioni 223** zitatumika. Aidha, Kampuni ya Wind East Africa Limited (Singida) iliendelea na maandalizi ya kufua umeme wa MW 100 na kulipa fidia kwa watakaopisha mradi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Vilevile, Kampuni ya Sino-Tan Renewable Energy Limited inatarajia kutekeleza mradi wa kufua umeme MW 100 katika eneo la Makambako, Mkoani Njombe. Kwa sasa Kampuni hizo zinatafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi yao. Katika Mwaka 2014/15, Kampuni hizo zitakamilisha mikataba ya kuuziana umeme na TANESCO pamoja na taratibu za kupata mikopo.

(iii) Uendelezaji Tungamotaka (Biomass)

81. **Mheshimiwa Spika**, Watanzania wengi bado wanategemea tungamotaka hasa kuni na mkaa kama chanzo cha nishati ya kupikia. Katika Mwaka 2013/14, Serikali ilikamilisha Mpango wa Kuendeleza Tungamotaka, ambao unalenga kuboresha matumizi ya nishati hiyo. Katika Mwaka 2014/15, kazi zitakazofanyika ni pamoja na kukusanya taarifa kuhusu viwanda vinavyofua au vinavyoweza kufua umeme kutokana na mabaki yatokanayo na shughuli za viwanda vya sukari, mbao na karatasi.

(iv) Uendelezaji wa Bioenergies

82. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeandaa Rasimu ya Sera na Sheria ya Bioenergies, na kufanya tathmini ya kina kuhusu uzalishaji wa bio-diesel kwa kutumia mafuta ya mimea. Katika Mwaka 2014/15, utekelezaji utalenga kuhamasisha uendelezaji wa Bioenergies na kukamilisha Sheria ya Bioenergies. Jumla ya **Shilingi milioni 800**, sawa na **Dola za Marekani 487,805** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 300**, sawa na **asilimia 37.5** ni fedha za ndani; na **Shilingi milioni 500**, sawa na **asilimia 62.5** ni fedha za nje kutoka Sida (Sweden) na NORAD (Norway).

83. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14, Serikali kwa kushirikiana na Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia (CARMATEC) ilitekeleza Mpango wa uendelezaji wa **biogas** katika ngazi ya kaya. Kupitia Mpango huo, jumla ya mitambo 9,000 ilijengwa katika Mikoa 22 nchini. Katika Mwaka 2014/15, Serikali itaendelea kuhamasisha matumizi ya **biogas** majumbani, vituo vya afya, zahanati na katika shule mbalimbali.

(v) Uendelezaji Jotoardhi (Geothermal)

84. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanzisha Kampuni inayoitwa **Tanzania Geothermal Development Company Limited** (TGDC). Kampuni hiyo itaratibu utafiti, uchorongaji visima, uendelezaji wa jotoardhi na kutoa ushauri wa kitalaamu. Serikali pia inatekeleza Mpango unaoitwa Scaling-Up Renewable Energy (SREP) unaofadhiliwa na mfuko wa Climate Investment Funds (CIF) na kuratibiwa na AfDB. Serikali imepata **Dola za Marekani 700,000** sawa na **Shilingi bilioni 1.15** kwa ajili ya maandalizi ya mradi huu. Miongoni mwa shughuli zitakazotekelawa ni uendelezaji wa nishati jadidifu vijijini (Renewable Energies

Nakala ya Mtando (Online Document)

for Rural Electrification) pamoja na matumizi ya jotoardhi kama chanzo kipywa cha nishati nchini. Thamani ya mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 50**, sawa na **Shilingi bilioni 82**.

85. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2014/15, Serikali kupitia TGDC itachoronga visima vyenye kina kifupi katika Mkoa wa Mbeya kwa ajili ya kupima mwongezeko wa joto chini ya ardhi. Aidha, Mpango wa kuendeleza Jotoardhi nchini utaandaliwa. Katika kuendeleza ushirikiano na nchi wanachama wa African Rift Geothermal (ARGeo) pamoja na kuhamasisha uendelezaji wa jotoardhi nchini, Serikali kwa kushirikiana na UNEP inaandaa kongamano la kikanda kuhusu Jotoardhi litakalofanyika Jijini Arusha Mwezi Oktoba, 2014. Katika Mwaka 2014/15, **Shilingi bilioni 11.0**, sawa na **Dola za Marekani milioni 6.71** zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 10.0**, sawa na **asilimia 90.9** ni fedha za ndani; na **Shilingi bilioni 1.0**, sawa na **asilimia 9.1** ni fedha za nje.

(vi) **Matumizi Bora ya Nishati**

86. **Mheshimiwa Spika**, matumizi bora ya nishati (Energy Conservation and Efficiency) ni mpango muhimu katika kuhakikisha upatikanaji wa nishati na kupunguza uharibifu wa mazingira. Jitihada za kuendeleza matumizi bora ya nishati zimeelekezwa katika sekta za kiuchumi zikiwemo: afya, biashara, elimu, makazi, migodi, kilimo, usafirishaji na viwanda. Lengo la mradi huu ni kupunguza upotevu wa nishati hasa ya umeme.

Katika Mwaka 2014/15, Serikali kupitia TANESCO itatekeleza mradi wa kusimamia matumizi bora ya umeme (Demand Side Management) katika Taasisi za Serikali kwa kubadilisha jumla ya taa milioni 3.2 zitumiazo umeme mwangi (Incandescent bulbs) na kuweka taa zitumiazo umeme kidogo (Compact Fluorescent Light - CFL) na hivyo kuwezesha kuokoa takriban MW 37.9 baada ya mradi huu kukamilika. Kiasi hiki cha umeme kinaweza kutosheleza mahitaji ya Mkoa wa Mbeya. Mradi huu utatekelezwa katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na Tanga ambapo matumizi ya umeme ni makubwa. Gharama ya kutekeleza mradi huu ni **Shilingi bilioni 24**, sawa na **Dola za Marekani milioni 14.63**.

87. **Mheshimiwa Spika**, sambamba na mradi huo, TANESCO pia inafanya juhudzi za kupunguza upotevu wa umeme katika njia za usafirishaji na usambazaji umeme (Supply Side Management), kwa kuboresha miundombinu yake. Katika Mwaka 2014/15, Serikali inakusudia kufanya yafuatayo: kujenga uwezo wa kitaasisi katika masuala ya matumizi bora ya nishati; kuratibu tafiti za kupunguza upotevu wa nishati; na ukaguzi wa matumizi ya nishati (Energy Audit) kwa kushirikiana na Kampuni ya KEMCO kutoka Korea Kusini ambayo imesaini Makubaliano ya Awali (MoU) na Wizara ya Nishati na Madini. **Shilingi milioni 600**,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

sawa na **Dola za Marekani 365,854** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu, ambapo **Shilingi milioni 400**, sawa na **asilimia 66.67** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 200**, sawa na **asilimia 33.33** ni fedha za nje kutoka Sida (Sweden).

SEKTA NDOGO YA GESI ASILIA NA MAFUTA

Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Gesi Asilia kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam

88. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Mwezi Aprili, 2014 mabomba yote **45,693** kwa ajili ya ujenzi wa Bomba la kusafirishia gesi asilia kutoka Mtwara (Madimba) na Lindi (Songo Songo) hadi Dar es Salaam yalikuwa yameletwa nchini. Ufukiaji wa mabomba hayo umekamilika kwa umbali wa kilomita 182 kati ya 542 sawa na **asilimia 34**.

Kazi ya ujenzi wa Bomba la kutoka Songo Songo kupitia baharini hadi Somanga Fungu, lenye urefu wa kilometra 25.6 imekamilika kwa **asilimia 100**. Kwa ujumla ujenzi wa Bomba la gesi asilia umekamilika kwa **asilimia 78**. Kazi ya kuweka mkongo wa mawasiliano (Fibre Optic Cable) inafanyika sambamba na ufukiaji wa Bomba. Aidha, mitambo wa kuchimbia mabomba katika Mto Rufiji (horizontal drilling) uliletwa nchini Mwezi Aprili, 2014.

89. **Mheshimiwa Spika**, shughuli za ujenzi wa mitambo ya kusafisha gesi asilia katika eneo la Madimba, Mtwara na Songo Songo, Lindi zinaendelea. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2014 ujenzi wa nyumba za kuishi wafanyakazi kwa eneo la Madimba ulikuwa umekamilika kwa **asilimia 90** na Songo Songo kwa **asilimia 78**.

Aidha, ujenzi wa misingi (foundations) ambako mitambo ya kusafisha gesi asilia itafungwa umekamilika. Vilevile, utengenezaji (manufacturing) wa mitambo yote ya kusafisha gesi asilia umekamilika kwa **asilimia 60**. Mitambo hiyo itaanza kuwasili nchini kuanzia Mwezi Julai, 2014 kutoka Jamhuri ya Watu wa China. Kwa ujumla maandalizi ya kufunga mitambo ya kusafisha gesi asilia yamekamilika kwa **asilimia 45**.

90. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imedhamiria kwa dhati kukamilisha ujenzi wa Bomba ifikapo Mwezi Julai, 2014 na mitambo ya kusafisha gesi asilia ifikapo Mwezi Desemba, 2014. Mradi huu utagharimu **Dola za Marekani bilioni 1.2**, sawa na takriban **Shilingi trilioni 2**. Fedha za ndani zilizotengwa kwa Mwaka 2014/15 ni **Shilingi bilioni 148**, sawa na **Dola za Marekani milioni 90**.

Usambazaji wa Gesi Asilia Lindi, Mtwara na Pwani

Nakala ya Mtandao (Online Document)

91. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa Bomba la gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam umeweka matoleo (tie - out) kwa ajili ya kusambaza gesi asilia katika miji mikubwa yote ambapo Bomba hilo linapita ikiwemo miji ya Mtwara, Lindi, Kilwa na Kisarawe. Serikali itawezesha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kwa ajili ya mitambo ya kufua umeme, matumizi viwandani, Taasisi mbalimbali, majumbani na kwenye magari katika Mikoa hiyo.

Katika Mwaka 2013/14, zabuni ilitangazwa kwa ajili ya kumpata Mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu wa mradi na Tathmini ya Athari za Mazingira na Kijamii (ESIA) kwa ajili ya usambazaji wa gesi asilia katika miji ya Mtwara, Lindi, Kilwa na Kisarawe. Mshauri amepatikana na anatarajiwani kuanza kazi Mwezi Juni, 2014 na kukamilisha kazi hiyo baada ya miezi mitatu (3). Kazi zitakazofanyika katika Mwaka 2014/15 ni pamoja na utafiti wa mahitaji ya gesi asilia katika viwanda, Taasisi mbalimbali, magari na majumbani; na mfumo na miundombinu ya kufikisha gesi asilia katika maeneo yatakayoainishwa. Aidha, baadhi ya viwanda na kampuni mbalimbali zimeanza majadiliano ya mikataba na TPDC ili kupatiwa gesi asilia. Kampuni hizo ni pamoja na Dangote (Mtwara) na MEIS (Lindi) kwa ajili ya uzalishaji wa saruji; na Kilwa Energy (Kilwa) kwa ajili ya kufua umeme.

92. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2014/15, Serikali itaendelea kusimamia ukamilishaji wa upembuzi yakinifu wa mradi. Vilevile, Serikali itampata mshauri atakayefanya usanifu na michoro (Detailed Engineering Design and Drawings) ya miundombinu pamoja na vituo vya kujazia gesi asilia iliyoshindiliwa (Compressed Natural Gas) kwenye magari.

Mshauri huyo ataongoza zoezi la kumpata mkandarasi na atasimamia ujenzi wa mradi. Fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo ni **Shilingi bilioni 5**.

Shughuli za Utafutaji wa Mafuta

93. **Mheshimiwa Spika**, utaratibu wa awali wa kupata Kampuni za kuja kufanya utafiti wa mafuta na gesi asilia nchini toka miaka ya 1952 ulikuwa kwa Kampuni husika kuomba eneo inalolitaka kufanya utafiti na kupewa bila ushindani. Kwa wakati huo, maeneo yaliyohusika yalikuwa ya nchi kavu na siyo kwenye kina kirefu cha Bahari.

Kuanzia Mwaka 1973 hadi 1999, TPDC ilianza kujitangaza Kimataifa kwa nia ya kupata wawekezaji na kushawishi Kampuni za nje zenye uwezo, kuja nchini kwa ajili ya utafutaji mafuta. Kampuni zilizojitokeza ni: Agip ya Italia; Aminex, BP, Heritage, Petrodel, Tullow za Uingereza; Ammoco na Exxon za Marekani;

Nakala ya Mtando (Online Document)

Artumas ya Canada; Beach Petroleum, Ndovu Resources na Swala za Australia; Bubin ya Ireland; KUFPEC na IEDC za Kuwait; Maurel and Prom ya Ufaransa; Motherland ya India; Shell ya Uhlanzi; na Tanganyika Oil ya Misri yalikuja nchini kufanya utafiti katika nyakati tofauti. Tafiti hizo zilifanyika nchi kavu na Bahari ya kina kifupi.

94. **Mheshimiwa Spika**, vitalu kwenye kina kirefu cha Bahari vilianza kutangazwa Mwaka 2000. Katika zabuni ya kwanza, **Kampuni moja** ilipatikana ambayo ni Petrobras ya Brazil. Katika Duru ya Pili iliyofanyika Mwaka 2001, **Kampuni moja** ilipatikana ambayo ni Shell ya Uhlanzi. Katika Duru ya Tatu iliyofanyika Mwaka 2004, **Kampuni tatu** zilipatikana ambazo ni Ophir (Uingereza), Statoil (Norway) na Petrobras (Brazil). **Duru zote hizo tatu zilifanyika nje ya nchi.**

95. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14, Serikali ilidurusu Mwongozo wa Mkataba wa Uzalishaji na Ugawanaji Mapato yatokanayo na Mafuta na Gesi Asilia (Model Production Sharing Agreement – MPSA, 2013).

Kufuatia Mwongozo huo, uzinduzi wa Duru ya Nne ya Kuitisha Zabuni za Utafutaji Mafuta (Fourth Petroleum Licensing Round) kwenye vitalu saba (7) katika Bahari Kuu na kimoja (1) kwenye Ziwa Tanganyika Kaskazini ulifanyika hapa nchini Mwezi Oktoba, 2013. Shughuli hiyo ilizinduliwa rasmi na Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Zoezi hilo lilifanyika kwa mara ya kwanza nchini baada ya kufanyika nje ya nchi mara tatu mfululizo.

Kampuni za ndani na nje ya nchi zilizokidhi vigezo zilishiriki, ambapo hadi Aprili, 2014 kampuni 19 zilinunua taarifa za vitalu vilivytangazwa. Zoezi hilo lilifungwa tarehe 15 Mei, 2014 ambapo kampuni 5 zilirudisha nyaraka za Zabuni (bidding documents), limesaidia kuitangaza Tanzania kimataifa na kutoa fursa ya Watanzania kushiriki. Katika zabuni hiyo, Kampuni za kitanzania zilipewa upendeleo maalum wa kisheria wa alama za ziada. Hata hivyo, hakuna Kampuni ya Kitanzania ilijoitokeza kushiriki.

Nitoe wito kwa Kampuni za Kitanzania kujitokeza kushiriki katika fursa mbalimbali zilizopo katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia. Hii itaondoa dhana kwamba uwekezaji katika sekta hiyo ni kwa ajili ya kampuni za nje pekee. Nashauri Kampuni nyingine za kitanzania ziige mfano wa Kampuni za Swala Energy na Petrodel za nchini mwetu ambazo zinafanya shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia nchini.

96. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14, jumla ya futi za ujazo **triliioni 4.8** za gesi asilia ziligungnduliwa katika visima vya Mkizi – 1, Ngisi – 1, Tangawizi – 1, na Mlonge – 1. Hadi kufikia Mwezi Aprili 2014, kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa nchini ni futi za ujazo **triliioni 46.5, sawa na mapipa ya mafuta bilioni 8.37**. Kiasi hiki ni **takriban mara tano ya gesi asilia** iliyokuwepo Mwaka 2005 wakati Serikali ya Awamu ya Nne inaingia madarakani. Kati ya kiasi hicho, **asilimia 83** ni kutoka kina kirefu cha maji Baharini na **asilimia 17** ni nchi kavu.

Mradi wa Uzalishaji Mbolea kwa Kutumia Gesi Asilia

97. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza kauli mbiu ya "Kilimo Kwanza" Serikali itawezesha uanzishwaji wa kiwanda cha mbolea kitakachotumia malighafi ya gesi asilia inayopatikana hapa nchini. Jitihada hizi ni katika kuhakikisha upatikanaji mzuri na wa uhakika wa mbolea ili kuboresha kilimo chetu. Mwezi Agosti, 2013 Serikali kupitia TPDC ilitangaza zabuni ya kujenga kiwanda cha mbolea na kampuni 19 zilionesha nia. Kati ya Kampuni hizo, 12 zilikidhi vigezo na hivyo kupelekewa Request for Proposal (RFP) ili ziwasilishe project write-up kwa ajili ya uchambuzi. Kampuni 6 zimeleta mapendekezo ya utekelezaji wa mradi na uchambuzi unaendelea wa kumpata mshindi. Taratibu za kumpata mwekezaji kwenye kiwanda cha mbolea zitakamilika kabla ya Julai, 2014 na maandalizi ya ujenzi yataanza Mwaka 2014/15.

Hifadhi ya Taifa ya Mafuta

98. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuratibu uanzishwaji wa Hifadhi ya Taifa ya Mafuta kwa kuandaa Rasimu ya Kanuni za Uratibu wa Mafuta ya Akiba (National Strategic Petroleum Reserve Regulations). Kampuni ya Oman Trading International (OTI) ilishinda zabuni ya kuiuzia mafuta TPDC. Kampuni ya OTI imekubali kuleta mafuta kwa mkopo, ambapo TPDC itailipa Kampuni hiyo fedha baada ya kuuza mafuta hayo. Lengo la utaratibu huu ni kuhakikisha nchi yetu inakuwa na mafuta ya akiba wakati wote. Katika Mwaka 2014/15, Serikali itakamilisha maandalizi ya Kanuni za Uratibu wa Mafuta ya Akiba na kuanza utekelezaji wake.

Hisa za Serikali katika Kampuni ya Puma Energy Limited, TAZAMA na TIPER

99. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14, Serikali iliendelea kusimamia na kushiriki katika shughuli za uendeshaji wa Kampuni za Puma Energy Tanzania Limited (**asilimia 50**), Tanzania Zambia Pipeline Limited (TAZAMA, **asilimia 30**) na Tanzania International Petroleum Reserve (TIPER, **asilimia 50**).

Gawiwo litakalolipwa Serikalini katika kipindi husika kutoka Kampuni ya Puma Energy Tanzania Limited ni **Shilingi bilioni 3.28**. Kampuni za TAZAMA na

Nakala ya Mtandao (Online Document)

TIPER hazijawasilisha gawiwo Serikalini kwa kuwa bado hazijakamilisha hesabu zake za Mwaka 2013. Serikali itaimarisha usimamizi wa Kampuni hizo ili kuongeza gawiwo katika miaka ijayo. Kufuatia kumalizika kwa vipindi vya Wajumbe wa Bodi hizo tatu (3), Serikali imeteua wajumbe wapya wa Bodi hizo Mwezi Machi, 2014.

Sera na Sheria katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia

100. **Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoahidi katika Hotuba yangu ya Mwaka 2013/14 mbele ya Bunge lako Tukufu, **Serikali iliidhinisha Sera ya Gesi Asilia Mwezi Oktoba, 2013 ili kuimarisha usimamizi wa Sekta Ndogo ya Gesi Asilia**. Aidha, Rasimu ya Sera ya Uwezeshaji na Ushirikishaji Wazawa (Local Content Policy) ziliandaliwa.

Lengo la Sera hiyo ni kuhakikisha kuwa Watanzania wanashiriki ipasavyo katika shughuli zote za rasilimali za mafuta na gesi asilia kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vijavyo. Rasimu ya Sera hiyo imesambazwa kwa wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Wizara, Taasisi za Serikali na Washirika wa Maendeleo ili kupata maoni yao. Wizara ingependa kupata maoni yenu kabla ya tarehe 30 Juni, 2014.

101. **Mheshimiwa Spika**, Vilevile, Serikali imekamilisha Rasimu ya Kwanza ya Sera ya Petroli itakayotoa mwongozo kuhusu usimamizi wa shughuli za utafutaji, uzalishaji na ugawanaji mapato yanayotokana na Mafuta na Gesi Asilia pamoja na usafishaji, uhifadhi, usafirishaji na usambazaji mafuta.

Katika Mwaka 2014/15 Rasimu hizo zitawasilishwa katika Mamlaka husika kwa ajili ya kuidhinishwa. Kukamilika kwa Sera husika kutaimarisha usimamizi wa Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia kwa maendeleo ya kizazi cha sasa na vijavyo.

102. **Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Rasimu ya Sheria ya Gesi Asilia imekamilika. Rasimu imepelekwa kwa wadau ili kupata maoni yao kabla ya kuikamilisha na kuiwasilisha katika kikao cha Bunge cha Mwezi Novemba, 2014.

Kudurusu Muundo wa TPDC

103. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na kuongezeka kwa shughuli za utafutaji mafuta na gesi asilia, uendelezaji wa matumizi ya gesi asilia na kusudio la kuongeza ufanisi katika utendaji wa TPDC, Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya TPDC iliwasilisha Serikalini mapendekezo ya muundo mpya wa Shirika Mwezi

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mei, 2013. Serikali ilitathmini mapendekezo hayo kwa kuangalia miundo na uzoefu kutoka nchi mbalimbali zilizonufaika na uwepo wa rasilimali ya mafuta na gesi asilia. Baada ya tathmini hiyo Mwezi Aprili, 2014, Serikali kupitia Msajili wa Hazina iliidhinisha muundo mpya wa TPDC ili kuliwezesha Shirika hilo kushiriki kikamilifu kwenye shughuli zote za utafutaji, uzalishaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia (Upstream, Mid and Down-streams).

Ili kutekeleza majukumu hayo, TPDC itaanzisha kampuni tanzu zikiwemo Kampuni ya Usafirishaji na Usambazaji wa Gesi Asilia (GASCO) na Kampuni ya Mafuta (COPEC). Ushiriki wa TPDC katika maeneo hayo utaimarisha mapato ya Serikali kwenye shughuli za mafuta na gesi asilia pamoja na kuboresha usimamizi wa Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia.

Shughuli za Udhibiti wa Sekta ya Nishati

104. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14, EWURA iliendelea kusimamia shughuli za udhibiti katika Sekta Ndogo za Umeme, Mafuta na Gesi Asilia. Serikali kupitia Kampuni ya Petroleum Importation Coordinator Limited (PICL) iliendelea kusimamia Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (BPS). Kati ya Mwezi Julai, 2013 na Aprili, 2014 mafuta yaliendelea kupatikana kulingana na mahitaji yetu.

Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2013 jumla ya lita bilioni 4.66 za aina mbalimbali za mafuta ziliingizwa nchini kupitia Bandari ya Dar es Salaam. Kati ya kiasi hicho, lita bilioni 2.76 sawa na **asilimia 59** yalikuwa ni mafuta kwa matumizi ya ndani na kiasi cha lita bilioni 1.90, sawa na **asilimia 41** yalikuwa kwa ajili ya nchi jirani. Aidha, kutokana na kuimarika kwa mfumo huo, wastani wa gharama (**weighted average premium**) za uagizaji mafuta ya petroli zimeshuka kutoka **Dola za Marekani 59 kwa tani** Mwezi Novemba, 2011 hadi **Dola za Marekani 36 kwa tani** Mwezi Aprili, 2014.

105. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14 Serikali kupitia EWURA iliendelea kudhibiti ubora wa bidhaa za mafuta ya petroli nchini na kuchukua hatua stahiki za kisheria kwa wale waliothibitika kutozingatia viwango viliwyowekwa. Aidha, EWURA iliendelea kusimamia bei za mafuta katika soko la ndani ili kuhakikisha bei hizo zinaendana na mabadiliko ya bei katika Soko la Dunia na mwenendo wa thamani ya Shilingi ya Tanzania ikiwianishwa na Dola ya Marekani. Bei ya mafuta ya petroli nchini imeendelea kushuka kutokana na kuimarika kwa Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja na shughuli za udhibiti.

106. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14, Idara ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilifanya tathmini kuhusu manufaa ya uwekaji vinasaba

Nakala ya Mtandao (Online Document)

katika mafuta, uanzishwaji wa matumizi ya Kanuni ya Kukokotoa Bei Kikomo pamoja na Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja. Matokeo ya tathmini hiyo yanaonesha kuwa nchi imenufaika na shughuli za udhibiti wa Sekta Ndogo ya Mafuta kwa kupunguza uchakachuaji ambapo kati ya Mwaka 2010 na 2011, mapato ya Serikali yameongezeka kwa **Shilingi bilioni 33.5**. Aidha, kutokana na udhibiti wa uuzaji mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya nchi jirani (transit) mapato ya Serikali yameongezeka kwa **Shilingi bilioni 468.5** kwa kipindi cha kati ya Mwaka 2010/11 na 2012/13. Vilevile, shughuli za udhibiti zimeongeza ufanisi katika uagizaji mafuta na matumizi ya miundombinu bandarini; pamoja na kuondoa upandaji holela wa bei za mafuta nchini.

107. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2014/15 EWURA itaendelea kuboresha usimamizi na udhibiti wa ubora wa mafuta pamoja na Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja. Aidha, katika Mwaka 2014/15, Serikali itaboresha muundo wa PICL ili kuongeza ufanisi kwa kuzingatia uzoefu wa nchi jirani za Kenya na Msumbiji zinazotumia mfumo kama huo.

Changamoto katika Sekta ya Nishati na Mipango ya Kukabiliana Nazo

108. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Sekta ya Nishati imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo upatikanaji wa fedha za kutosha kutekeleza miradi; mahitaji makubwa ya umeme; kupunguza upotevu wa umeme; vivutio mwafaka kwa wawekezaji; gharama kubwa za umeme unaofuliwa kutokana na mafuta; uzingatiaji matumizi bora ya nishati; na mabadiliko ya tabia nchi.

109. **Mheshimiwa Spika**, Mpango na Bajeti ya Mwaka 2014/15 katika Sekta ya Nishati unalenga kukabiliana na changamoto hizo kwa kutekeleza mipango na miradi iliyotajwa katika Hotuba hii, pamoja na kudurusu, kutunga na kusimamia Sera na Sheria zinazohusu Sekta ya Nishati kwa manufaa ya Watanzania wa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

SEKTA YA MADINI

Mafanikio katika Sekta ya Madini kwa Mwaka 2013/14

110. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka 2013/14, Wizara iliendelea kutekeleza vipaumbele vyake katika Sekta ya Madini. Mafanikio yaliyopatikana katika Sekta hii ni pamoja na yafuatayo: kukamilika kwa zoezi la high resolution airborne geophysical survey katika Mikoa ya Dodoma, Manyara, Mbeya, Morogoro, Pwani, Singida, Tabora na Tanga Mwezi Oktoba, 2013; kukamilika kwa ground geophysical survey (kwenye Quarter Degree Sheet (QDS) - 7, geological mapping kwa QDS 18 na geochemical mapping kwa QDS 7) katika

Nakala ya Mtandao (Online Document)

maeneo ya Dodoma, Mbeya, Morogoro, Njombe, Pwani, Singida na Tanga; na kusainiwa kwa Makubaliano ya Awali (MoU) na Serikali ya Finland kwa ajili ya mkopo nafuu kuwezesha utafiti wa kijosayansi na maeneo yenye madini katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani utakaoanza Mwezi Agosti, 2015.

111. **Mheshimiwa Spika**, mafanikio mengine ni kukamilika kwa Rasimu ya Sheria ya kusimamia shughuli za Mpango wa Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Tasnia ya Uziduaji (TEITI); kusainiwa kwa makubaliano kwa STAMICO kumiliki mgodi wa dhahabu wa Tulawaka (Biharamulo) kutoka Kampuni ya African Barrick Gold; kutolewa kwa leseni nane (8) za uchenjuaji madini katika Wilaya za Bunda (2), Misungwi (1), na Mkoa wa Geita (5); Serikali kukusanya **Shilingi bilioni 50.6** kama Kodi ya Mapato kutoka Kampuni ya Geita Gold Mining Limited na **Shilingi bilioni 3.38** kutoka Kampuni ya Resolute Tanzania Limited; na malipo ya jumla ya **Shilingi milioni 178.9** kwa Serikali kama Alternative Minimum Tax kutoka Kampuni ya *Williamson Diamonds Limited*.

112. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kusimamia upatikanaji wa malipo ya ushuru wa huduma (service levy) kwa Halmashauri za Geita, Kahama, Kishapu, Nzega na Tarime. Mapato yaliyolipwa tangu migodi hiyo ianze hadi Aprili, 2014 kwa Halmashauri hizo ni jumla ya **Dola za Marekani milioni 10.58**, sawa na **Shilingi bilioni 17.35** kwa mchanganuo ufuatao: Mgodi wa Geita **Dola za Marekani milioni 1.6**, sawa na **Shilingi bilioni 2.62** kwa Halmashauri ya Geita; Mgodi wa Bulyanhulu **Dola za Marekani milioni 2.53**, sawa na **Shilingi bilioni 4.15** kwa Halmashauri ya Kahama; Mgodi wa Buzwagi **Dola za Marekani 800,000**, sawa na **Shilingi bilioni 1.31** kwa Halmashauri ya Kahama; Mgodi wa North Mara **Dola za Marekani milioni 2.4**, sawa na **Shilingi bilioni 3.94** kwa Halmashauri ya Tarime; Mgodi wa Resolute **Dola za Marekani milioni 3.04**, sawa na **Shilingi bilioni 4.99** kwa Halmashauri ya Nzega; na Mgodi wa Almasi wa Mwadui **Dola za Marekani 202,469** sawa na **Shilingi milioni 332.05** kwa Halmashauri ya Kishapu.

113. **Mheshimiwa Spika**, Mafanikio mengine ni kukusanya kwa mrabaha wa **Shilingi bilioni 116.64** kutokana na madini yaliyozalishwa na kuuzwa; kukamilika kwa Mpango wa Uendelezaji wa Uchimbaji Mdogo wa Madini; kuandaliwa kwa Mtaala wa utafiti wa madini na programu za uchimbaji mdogo wa madini; kufadhili mafunzo ya wanafunzi 148 katika ngazi ya cheti na diploma katika fani za Madini, Petroli na Gesi Asilia; kuanza ujenzi wa madarasa mawili (2) katika Chuo cha Madini Dodoma kila moja likiwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 140; na kuanzishwa kwa ofisi mbili za Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA) katika Mikoa ya Arusha na Mbeya.

114. **Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka 2013/14, Serikali kwa upande wa Sekta ya Madini iliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kufuata Mpango Kazi uliowekwa na Wizara. Katika Mwaka 2014/15 maeneo mahsusni yatakayoleta

Nakala ya Mtando (Online Document)

matokeo makubwa katika Sekta hii ni pamoja na: kuimarisha makusanyo ya maduhuli yatokanayo na madini; kuendeleza shughuli za uchimbaji mdogo; kuboresha utoaji na usimamizi wa leseni za madini; kuimarisha usimamizi wa afya, usalama na utunzaji wa mazingira migodini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuimarisha usimamizi wa biashara ya madini; kuwezesha Mashirika na Taasisi za Serikali katika Sekta ya Madini; na kuendelea kuboresha mazingira ya kazi katika Ofisi za Madini za Kanda.

Mauzo na Thamani ya Madini yaliyouzwa nje ya Nchi

115. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14 Wizara iliendelea kusimamia shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini nchini kwa lengo la kuongeza mchango wa Sekta hii kwenye Pato la Taifa. Kutokana na mipango na miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa na Serikali, Sekta ya Madini imeendelea kuwa chachu katika ukuaji wa uchumi nchini. Hata hivyo, Sekta ya Madini ni mojawapo ya sekta zilizoathiriwa kwa kiasi kikubwa na mtikisiko wa uchumi Duniani ambao uliambatana na kushuka kwa bei ya madini mbalimbali, hususan dhahabu na pia kushuka kwa upatikanaji wa mitaji ya nje (FDI).

116. **Mheshimiwa Spika**, thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi yaliyouzwa na Migodi Mikubwa ya Dhahabu iliongezeka kutoka **Dola za Marekani milioni 640** Mwaka 2005 hadi kufikia **Dola za Marekani bilioni 1.79** Mwaka 2013. Uzalishaji wa madini ulipungua kutoka wakia 1,398,406 Mwaka 2005 hadi wakia 1,244,743 Mwaka 2013, sawa na punguzo la **asilimia 10.9**. Aidha, **asilimia 69.27** ya mauzo ya madini yote ya migodi mikubwa nje ya nchi kwa Mwaka 2013 ilitokana na mauzo ya dhahabu.

117. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa uzalishaji na mauzo ya madini katika migodi mikubwa nchini katika kipindi cha Mwaka 2013, jumla ya wakia milioni 1.24 za dhahabu, wakia 380,000 za fedha na ratili milioni 17.70 za shaba zilizalishwa na kusafirishwa nje ya nchi kutoka migodi mikubwa ya Bulyanhulu, Buzwagi, Geita, Golden Pride, New Luika, North Mara na Tulawaka. Jumla ya thamani ya madini hayo ni **Dola za Marekani bilioni 1.79** pungufu kwa **asilimia 17.7** ukilinganisha na mauzo ya madini yaliyofanywa na migodi hiyo kwa Mwaka 2012 ya Dola za Marekani bilioni 2.17.

Vilevile, jumla ya karati 158,562 za almasi na gramu milioni 3.24 za Tanzanite zilizalishwa na migodi ya Mwadui na TanzaniteOne, sawia. Mauzo yote ya almasi na Tanzanite yaliyofanywa na migodi hiyo kwa Mwaka 2013 yalifikia **Dola za Marekani milioni 50.53**.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mrabaha uliolipwa Serikalini na wamiliki wote wa migodi mikubwa nchini katika kipindi hicho ni **Dola za Marekani milioni 72.90**, sawa na **Shilingi bilioni 116.64**. Mgodi wa Tulawaka uliopo Wilaya ya Biharamulo, Mkoa wa Kagera ulifungwa rasmi Mwezi Julai, 2013.

Aidha, mgodi wa Golden Pride uliopo Wilaya ya Nzega, Mkoa wa Tabora ulifungwa rasmi Mwezi Februari, 2014. Ni wazi kuwa, kufungwa kwa migodi hiyo kutapunguza uzalishaji wa dhahabu na mapato ya Serikali.

Kuimarisha Makusanyo ya Maduhuli Yatokanayo na Madini

118. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha makusanyo ya maduhuli ya Serikali yatokanayo na madini, Wizara ililenga kukusanya kiasi cha **Shilingi bilioni 199.96** katika Mwaka 2013/14. Hadi kufikia tarehe 23 Mei, 2014 kiasi cha **Shilingi bilioni 137.9** kimekusanya, sawa na **asilimia 69** ya lengo. Kushuka kwa makusanyo hayo kumetokana na kushuka kwa bei ya dhahabu katika Soko la Dunia.

119. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2014/15 Serikali inategemea kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 209.96** kutoka katika Sekta ya Madini. Ili kufikia lengo hilo, Wizara itaimarisha ukaguzi na usimamizi wa Sekta ya Madini ili kuhakikisha kwamba wachimbaji wakubwa, wa kati, wadogo na wafanyabiashara wa madini wanalipa ada za leseni na mrabaha stahiki.

Pia, Wizara itafungua ofisi mpya mbili (2) za Kanda ambazo ni Kanda ya Ziwa Viktoria Mashariki, ambayo Makao Makuu yake yatakuwa Musoma; na Kanda ya Ziwa Nyasa ambayo Makao Makuu yake yatakuwa Songea. Aidha, Ofisi nne (4) za Maafisa Madini Wakazi zitafunguliwa huko Bariadi, Moshi, Nachingwea na Njombe. Kufunguliwa kwa Ofisi hizo kumelenga kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

120. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia itaendelea kutekeleza mpango wake wa kuanzisha vituo vya ukaguzi wa madini ya ujenzi na viwandani katika Kanda zote za Madini nchini. Mpango huo umewevesha jumla ya **Shilingi bilioni 1.71** kukusanya Mwaka 2012/13 kutoka Kanda za Mashariki, Ziwa Viktoria, Kati na Kusini ikilinganishwa na wastani wa **Shilingi milioni 4** kwa mwaka zilizokuwa zinakusanya hapo awali katika Kanda hizo kabla ya mpango huo kuanzishwa. Aidha, Wizara itaimarisha usimamizi wa uchimbaji na biashara ya Tanzanite ili kuhakikisha kuwa Taifa linapata manufaa stahiki ya uvunaji wa madini hayo yanayopatikana Tanzania pekee.

Majadiliano na Kampuni za Madini

Nakala ya Mtando (Online Document)

121. **Mheshimiwa Spika**, katika Hotuba yangu ya Mwaka 2013/14, niliahidi kuendelea kufanya majadiliano na baadhi ya wamiliki wa migodi mikubwa nchini wenye Mikataba ya Uendelezaji Migodi (Mineral Development Agreements – MDAs). Majadiliano hayo ni kuhusu kubadilisha baadhi ya vipegele vya mikataba ili kuleta mapato zaidi ya fedha kwa Taifa.

122. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imefanikiwa kujadiliana na Kampuni ya African Barrick Gold (ABG) inayomiliki migodi mikubwa ya Bulyanhulu katika Halmashauri ya Msalala, Wilaya ya Kahama, Buzwagi katika Halmashauri ya Mji wa Kahama na North Mara katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime.

Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kutokana na majadiliano hayo, Kampuni hiyo imekubali kuwa kuanzia Julai, 2014 italipa asilimia 0.3 ya mapato (turnover) kama ushuru wa huduma (service levy) kwa Halmashauri husika, badala ya malipo ya Dola za Marekani 200,000 kwa mwaka iliyokuwa inalipwa hapo awali kulingana na MDA.

Napenda kutumia fursa hii kuipongeza Kampuni ya ABG kwa uamuzi huo na kuzishauri Kampuni nyingine kuiga mfano huo.

123. **Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya ABG itaendelea kulipa moja kwa moja Dola za Marekani 200,000 kwa Halmashauri husika na ziada ya malipo yatakayotokana na asilimia 0.3 ya mapato itawekwa kwenye Mfuko Maalum utakaoanzishwa na kusimamiwa na Halmashauri husika. Mfuko huo utatumika kwa ajili ya kuendeleza miundombinu kwenye maeneo ya Halmashauri hizo katika nyanja za afya, barabara, elimu, maji na nishati. Ili kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatumika kama ilivyokusudiwa, Halmashauri husika italazimika kuwasilisha kwa Wizara ya Nishati na Madini Mpango wa utekelezaji kwa ajili ya idhini. Lengo ni kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatumika kwa miradi ya maendeleo tu.

Kuendeleza Shughuli za Uchimbaji Mdogo wa Madini

124. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14, shughuli za uchimbaji mdogo zimeendelea kukua na kutoa mchango mkubwa katika kupunguza umaskini, ambapo zaidi ya Watanzania milioni moja wamejajiri katika shughuli hizo.

Katika kutekeleza llani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 – 2015, Ibara ya 56 (d) ambayo pamoja na mambo mengine, inasisitiza juu ya kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata mikopo na mitaji, Wizara imeendelea kutoa mikopo ya masharti nafuu na ruzuku kwa wachimbaji wadogo kuitia Benki ya TIB.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mwezi Aprili, 2014 Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alikabidhi hundi zenyé jumla ya **Dola za Marekani 537,000** sawa na **Shilingi milioni 880.68** kwa miradi kumi na moja (11) ya wachimbaji wadogo ambayo ilikidhi vigezo vya kupata ruzuku.

Vilevile, Wizara inatarajia kuipatia miradi mingine 18 ya wachimbaji wadogo mikopo yenyé jumla ya **Shilingi bilioni 2.3** ifikapo mwishoni mwa Mwezi Juni, 2014. Nawasihi wachimbaji wadogo kuandaa michanganuo yao ya miradi kwa ajili ya kuomba mikopo na ruzuku kupertia TIB ili watakaokidhi vigezo wapate ruzuku ama mikopo kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za uchimbaji mdogo kwa tija.

Wachimbaji wadogo wanashauriwa kupata ushauri wa bure wa kitaalamu kutoka Shirika la Taifa la Madini (STAMICO). Wizara itaendelea kushirikiana kwa karibu sana na wachimbaji wadogo waaminifu watakaotumia vizuri ruzuku wanazopewa, na watakaorejesha mikopo na kulipa kodi za Serikali.

125. **Mheshimiwa Spika**, ili kuendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo kwa mitaji na mikopo, Wizara imetenga kiasi cha **Shilingi bilioni 2.5** katika Bajeti yake ya Mwaka 2014/15 kwa ajili ya kukopesha wachimbaji hao.

Pamoja na fedha hizo za mikopo, Serikali, kupertia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia imetenga jumla ya **Dola za Marekani milioni 3.5**, sawa na **Shilingi bilioni 5.74** kama ruzuku kwa ajili ya wachimbaji wadogo, na kiasi cha **Dola za Marekani milioni 1.1**, sawa na **Shilingi bilioni 1.8** kwa ajili ya kununua mitambo miwili (2) ya uchorongaji miamba (drilling rigs).

Mitambo hiyo itapelekwa katika Ofisi za Madini za Kanda ya Ziwa (Mwanza) na Kanda ya Kusini Magharibi (Mbeya) ili kuwezesha utambuzi wa kiasi cha mashapo yaliyopo katika maeneo ya wachimbaji wa kati na wadogo yaliyogunduliwa kuwa na madini. Kiasi hicho kinafanya jumla ya fedha zilizotengwa kwa Mwaka 2014/15 kwa ajili ya wachimbaji wadogo kufikia jumla ya **Shilingi bilioni 10.04**.

126. **Mheshimiwa Spika**, katika juhudzi za kuendeleza shughuli za uchimbaji mdogo, kwa Mwaka 2013/14 Wizara iliendelea kutoa mafunzo kwa nadharia na vitendo kwa wachimbaji wadogo ambapo jumla ya wachimbaji wadogo 420 walipatiwa mafunzo katika maeneo ya Handeni na Kiliindi (250), Musoma (90) na Tunduru (80).

Pia, katika kupanua wigo wa kutoa elimu kwa wadau wengi zaidi, vitabu 2,000 vya kuelimisha wachimbaji wadogo vilichapishwa na kusambazwa. Kwa Mwaka 2014/15, Wizara imepanga kutoa mafunzo kwa nadharia na vitendo

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwa wachimbaji wapatao 1,000. Vilevile, Wizara itaendelea kutoa huduma za ugani ili kuboresha utendaji kazi wa wachimbaji wadogo nchini.

127. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14 jumla ya maeneo 10 yenye ukubwa wa hekta 67,677.61 yametengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Maeneo hayo ni Nyamwironge (Kakonko), Ibaga (Mkalama), Makanya (Same), Mwajanga (Simanjiro), Itumbi B na Saza (Chunya), Ilujamate (Misungwi), Kalela/Kigogwe/Samwa (mpakani mwa Wilaya za Kasulu, Buhigwe na Kigoma Vijiji), Maguja (Nachingwea) na Nyangalata (Kahama/Nyang'hwale).

Jumla ya maeneo yaliyotengwa hadi sasa kwa ajili ya wachimbaji wadogo ni 25 yenye ukubwa wa kilomita za mraba 2,166.24. Aidha, jumla ya viwanja 8,800 vyenye ukubwa wa jumla ya kilomita za mraba 2,047.14 vimegawiwa kwa wachimbaji wadogo.

128. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2014/15, Wizara itaendelea kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo kadri itakavyoonekana inafaa. Pamoja na kuongeza ajira kwa wachimbaji wadogo, utengaji wa maeneo unalenga kupunguza migogoro ya maeneo kati ya wachimbaji wadogo na wakubwa na kati ya wachimbaji wadogo na wadogo (wenyewe kwa wenyewe). Vilevile, Wizara itafanya tathmini maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo na yatakayobainika kuwa hayafanyiwi kazi yatatenguliwa na kugawiwa kwa waombaji wengine kwa mujibu wa Sheria.

Kuboresha Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini

129. **Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mfumo wa utoaji wa leseni za madini, Wizara iliwezesha wamiliki wa leseni kupata taarifa za leseni kuitia tovuti maalum ya leseni (Mining Tenements Portal) na pia kuwawezesha wateja kupokea taarifa za maombi kuitia ujumbe mfupi wa simu (sms) na barua pepe. Hatua hizi zimelenga hatimaye kuwawezesha waombaji wa leseni kuwasilisha maombi kwa njia ya mtandao (on-line applications of mineral rights and payments). Pamoja na maboresho hayo, Wizara imeendelea kuhakiki taarifa za leseni kwenye mfumo wa utoaji wa leseni (data cleaning), kuondoa mlundikano wa maombi ya leseni na kuimarisha miundombinu ya mfumo wa leseni (MCIMS).

130. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kati ya Julai, 2013 na Aprili, 2014 jumla ya **maombi 7,640** ya utafutaji na uchimbaji madini yaliyopokelewa na kuingizwa kwenye Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini, ikilinganishwa na **maombi 9,889** katika Mwaka 2012/13.

Kati ya maombi yaliyopokelewa, 715 ni kwa ajili ya leseni za utafutaji wa madini; 6,909 yalikuwa ni ya uchimbaji mdogo; na 16 ni ya uchimbaji wa kati.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Jumla ya maombi 3,994 ya leseni yalikataliwa kwa sababu ya kushindwa kutimiza masharti ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. Aidha, jumla ya leseni 5,418 zilitolewa, kati ya hizo 482 kwa ajili ya utafutaji wa madini; 4,913 za uchimbaji mdogo; 22 za uchimbaji wa kati; na moja (1) ya uchimbaji mkubwa.

131. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Mwezi Aprili, 2014 jumla ya leseni hai za madini nchini zilikuwa ni **39,958**. Kati ya hizo, leseni za uchimbaji mkubwa ni 13; uchimbaji wa kati ni 381; uchimbaji mdogo ni 36,094; na leseni za utafutaji madini ni 3,470. Eneo la leseni hizo zote ni kilometra za mraba zipatazo **240,000** sawa na **asilimia 27** ya eneo lote la nchi kavu ya Tanzania Bara.

132. **Mheshimiwa Spika**, wakati Sekta ya Madini ikiendelea kukua na kuongezeka kwa uwekezaji, imejengeka dhana kwamba wawekezaji wageni wanamiliki maeneo mengi kuliko Watanzania. Aidha, ipo fikra kwamba Serikali haijachukua hatua ya kuwawezesha Watanzania kushiriki kikamilifu katika uwekezaji kwenye Sekta hii muhimu. Ukweli ni kwamba, Watanzania wanamiliki asilimia 70 ya leseni za madini, wageni asilimia 25 na asilimia 5 ya leseni hizo zinamilikiwa kwa ubia kati ya Watanzania na wageni.

133. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha usimamizi wa leseni za madini, Wizara imeendelea kuchukua hatua za kutoa Hati za Makosa (Default Notices) kwa wamiliki wa leseni za utafutaji na uchimbaji madini ambao hawatimizi masharti ya leseni. Aidha, Wizara imechukua hatua dhidi ya wamiliki waliohodhi maeneo makubwa ya leseni za madini nchini. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2014 Hati za Makosa 336 zilitolewa zikihusisha leseni 253 za utafutaji madini na leseni 83 za uchimbaji madini. Aidha, jumla ya leseni 174 za utafutaji madini na leseni moja ya uchimbaji mkubwa wa madini zilifutwa.

Vilevile, leseni 78 za utafutaji madini na leseni 34 za uchimbaji wa kati ziko katika utaratibu wa kisheria wa kufutwa. Kati ya leseni zote zilizofutwa na zinazotarajiwa kufutwa, **leseni 67 ni za wamiliki 10** waliobainika kuhodhi maeneo makubwa ya leseni za madini. Pamoja na hatua ya kufuta leseni, Wizara pia imechukua hatua ya kutomilikisha leseni mpya 214 kwa kampuni zenye leseni zinazozidi ukomo wa eneo la leseni la kilomita za mraba 2,000. Hatua hii imechukuliwa ikiwa ni sehemu ya usimamiaji wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010.

134. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2014/15, Wizara itaendelea kuimarisha Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini ikiwa ni pamoja na kukamilisha uanzishwaji wa Data Recovery Center mjini Morogoro. Kituo hicho kitaimarisha usalama wa taarifa za leseni. Aidha, Wizara itaanza kupokea maombi ya leseni na malipo ya ada za leseni kwa njia ya mtandao. Utaratibu

Nakala ya Mtando (Online Document)

huu utapunguza muda wa kushughulikia maombi ya leseni na kuongeza mapato ya Serikali. Vilevile, utapunguza ushawishi wa rushwa na upendeleo kwa waombaji wa leseni za madini. Wizara pia itaendelea kuwachukulia hatua za kisheria wamiliki wanaokiuka masharti ya leseni zao na wale wanaohodhi maeneo makubwa ya leseni bila kuyaendeleza.

Kuimarisha Usimamizi wa Afya, Usalama na Utunzaji wa Mazingira Migodini

135. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14 Wizara iliendelea kuhakikisha kuwa shughuli za uchimbaji madini zinaendeshwa kwa kuzingatia Kanuni za Usalama, Afya na Utunzaji wa Mazingira. Hadi kufikia Mwezi Machi 2014, jumla ya migodi 351 ilikaguliwa, ikijumuisha migodi mikubwa mitano (5); migodi ya kati 56; na migodi midogo 290. Kagazi hizo zimesaidia kuimarisha usalama na afya migodini.

Wizara itaendelea kusimamia Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Kanuni zake kwa kuimarisha ukagazi katika migodi mikubwa, ya kati na midogo.

Aidha, ukagazi utafanywa katika maeneo ya uchenjuaji na leseni za utafutaji wa madini. Pia, leseni za biashara ya madini na maduka ya usonara yatakaguliwa kwa lengo la kuhakiki ulipaji wa maduhuli ya Serikali.

136. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha utunzaji wa mazingira katika migodi mikubwa nchini, migodi ya Bulyanhulu, Buzwagi, Golden Pride, North Mara, Tulawaka na WDL imekamilisha Mipango ya Ufungaji Migodi (Mine Closure Plans) kwa mujibu wa Kanuni za Usalama, Afya na Utunzaji wa Mazingira na imeidhinishwa na Kamati ya Kisekta ya Ufungaji Migodi. Migodi ya Geita na TanzaniteOne imewasilisha Mipango ya Ufungaji Migodi ili kupitiwa na Kamati ya Kisekta kwa ajili ya uidhinishaji. Migodi ya El Hilal, New Luika na TANCOAL inatarajiwa kuwasilisha Mipango ya Ufungaji Migodi kabla ya mwisho wa Mwaka 2014.

137. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia kufungwa kwa shughuli za uzalishaji katika migodi ya Tulawaka na Golden Pride, Wizara ilisimamia taratibu za makabidhiano ya mgodi wa Tulawaka kwa STAMICO kupitia Kampuni yake tanzu ya "STAMIGOLD Mining Company Ltd" ili kuendelea kuchimba mashapo ya dhahabu yaliyobaki baada ya Kampuni ya ABG kufunga shughuli za uchimbaji. Pia, taratibu za kufungwa na kukabidhi eneo la mgodi wa Golden Pride kwa Chuo cha Madini Dodoma zinaendelea. Ukarabati wa maeneo yote yaliyoathiriwa na shughuli za mgodi huo unaendelea na utakamilika ifikapo Mwezi Desemba, 2014.

Aidha, maandalizi katika eneo la mgodi wa Golden Pride yataanza Mwezi Agosti, 2014 ili kuwezesha Wanafunzi 200 kuanza mafunzo katika eneo hilo. Baada ya majadiliano ya kina na Serikali, Kampuni ya Resolute imekubali kukipatia Chuo cha Madini Dodoma **Dola za Marekani milioni 1.0**, sawa na **Shilingi bilioni 1.64** ili kuendeleza miundombinu ya kuanzisha Kampasi ya Chuo cha Madini kwenye eneo la mgodi wa Golden Pride na kuimarisha ulinzi. Kwa upande wake, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1.0** katika Bajeti ya Mwaka 2014/15 kwa ajili hiyo.

138. **Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka 2014/15, Wizara itaendelea kukamilisha mikataba ya uwekaji wa Hati Fungani ya Ufungaji Migodi (Rehabilitation Bond for Mine Closure) kwa ajili ya migodi mikubwa nchini. Aidha, wachimbaji wadogo wataendelea kupewa elimu ya namna ya kuandaa mipango ya utunzaji wa mazingira (Environmental Protection Plans) ili kutimiza matakwa ya Sheria ya Madini ya Mwaka, 2010.

139. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kusimamia shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini ya Urani nchini. Hata hivyo, kumekuwapo na mtazamo hasi kuhusu utafutaji na uchimbaji wa madini ya Urani nchini. Kutokana na hali hiyo, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilitekeleza mpango wa elimu kwa umma kuhusiana na madini ya Urani na shughuli za uchimbaji wa madini hayo. Elimu hiyo ilitolewa kwa njia ya makongamano katika maeneo ya Bahi na Namtumbo ambako shughuli za utafutaji zinaendelea. Kutolewa kwa elimu hiyo kumeweza jamii husika kuwa na taarifa sahihi juu ya madini hayo na faida zake. Katika kipindi cha Mwaka 2014/15, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa jamii kwa njia ya semina na vyombo vya habari kuhusu uvunaji, uhifadhi, usafirishaji, matumizi ya madini ya Urani.

Usimamizi wa Shughuli za Baruti Nchini

140. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka 2013/14, Wizara iliendelea kuimarisha usimamizi wa uingizaji, usafirishaji, uhifadhi na matumizi ya baruti nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, katika kipindi cha kuanzia Julai 2013 hadi Machi 2014, **jumla ya tani 15,628.8 za baruti na fataki 2,177,062** ziliingizwa nchini kwa ajili ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia na uchimbaji wa madini. Vibali 114 vilitolewa kwa ajili ya kuingiza baruti nchini; vibali 44 vilitolewa kwa ajili ya kusafirisha baruti nje ya nchi; vibali 85 vya kulipulia baruti; na vibali 12 vya maghala ya kuhifadhia baruti. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo wa madini wanaotumia baruti wapatao 420 katika Mikoa ya Mara (90), Ruvuma (80) na Tanga (250). Mafunzo hayo yalihusu utaratibu wa kisheria wa upatikanaji, usafirishaji, utunzaji na matumizi salama ya baruti.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Lengo ni kuwaelekeza na kuwaelimisha watumiaji wa baruti juu ya mambo muhimu ya usalama katika kufanya shughuli za uchimbaji wa madini kwa kutumia baruti.

141. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka 2014/15 Wizara itaimarisha mipango na taratibu za usimamizi wa masuala ya baruti kwa kuzingatia Sheria ya Baruti ya Mwaka 1963; kuendelea kutoa elimu na mafunzo kwa wachimbaji wadogo wapatao 1,000 kuhusu matumizi bora na salama ya baruti; na kuendelea kufanya kagazi mbalimbali kwenye maghala ya kuhifadhia baruti. Pia, Sheria ya Baruti ya Mwaka 1963 itaboreshwa ili iendane na wakati.

Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini

142. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka 2013/14, Wizara iliendelea kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini ambapo hadi kufikia Mwezi Machi, 2014 jumla ya leseni 32 za uchenjuaji wa madini ya dhahabu (Vat Leaching), leseni 1 ya uchenjuaji wa madini ya coltan na leseni 1 ya uyeyushaji wa madini ya shaba (copper smelter) zimetolewa. Pia, viwanda vitatu (3) vya kuchenjua madini ya shaba vyenye uwezo wa kuchenjua wastani wa tani 90,000 za shaba ghafi (Copper Oxide) kwa mwaka vimeanzishwa. Viwanda hivi viwo Dar es Salaam (Danformation), Mkuranga (Horus) na Mpanda (TPM Mining).

Viwanda hivyo vina uwezo wa kuzalisha shaba katika kiwango cha ubora wa kati ya **asilimia 80 hadi 95**. Maeneo yanayozalisha shaba ghafi kwa wingi kwa sasa ni Mbesa (Tunduru); Dreef, Kapanda, Kasakalawe na Sikitiko (Mpanda); Burega, Gagwe, Ilagala, Lusunu, Kabulanzwila na Mkanga (Kigoma); Ibaga na Ilangida (Mkalama); na Sufu (Chamwino). Makisio ya uzalishaji wa shaba ghafi kwa mwaka ni **tani 1,200**.

143. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeanza kukarabati na kukiboresha kituo cha Jimolojia kilichopo Arusha (Tanzania Gemological Centre) ili kiwe cha kisasa zaidi ikiwa ni pamoja na kununua vifaa vya ukataji wa madini ya vito (lapidary) na usanifu wa mawe (carving).

Aidha, katika kukiimarisha kituo hicho, Wizara imenunua mashine 37 za aina mbalimbali zikiwemo faceting machine 20, triming machine 4, stone carving machine 4, bead making machine 6 na carbochon machine 3 kwa ajili ya kutoa mafunzo ya ukataji na usanifu wa vito kwa vitendo. Pia, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini imesaini makubaliano ya ushirikiano na Chuo cha Jimolojia cha nchini Thailand (GIT) kwa kipindi cha miaka miwili (2) kuanzia Mwezi Julai 2013 hadi Juni 2015. Aidha, Chama cha Wafanyabiashara wa Madini Tanzania (TAMIDA) kimesaini hati ya ushirikiano na Chama cha

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Wafanyabiashara wa Vito na Usonara cha Thailand (TGJTA) Mwezi Februari, 2014 ili kusaidia maendeleo ya tasnia ya vito nchini mwetu.

144. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuendesha maonesho ya Vito na Usonara huko Arusha yakiwa na malengo ya kuvutia masoko ya uhakika hapa nchini; fursa ya kutangaza rasilimali za madini ya vito yapatikanayo Tanzania; kukuza kazi za uongezaji thamani madini nchini kupitia programu mbalimbali kwa kutoa elimu ya uongezaji thamani madini kwa vikundi mbalimbali vya kinamama wanaojishughulisha na biashara ya madini ya vito; wazalishaji na wafanyabiashara wa madini wa ndani kupata fursa ya kupata masoko ya kimataifa; kuifanya Arusha kuwa kituo cha biashara ya vito na usonara barani Afrika; na kukusanya mapato ya Serikali.

Katika maonesho yaliyofanyika Arusha kuanzia tarehe 28 hadi 30 Oktoba 2013, nchi 29 zilishiriki ambapo jumla ya washiriki walikuwa ni 550 wakiwemo waoneshaji, wageni waalikwa na wanunuzi. Aidha, madini yenye thamani ya **Shilingi bilioni 6.9** yaliuzwa na kuiwesha Serikali kukusanya kiasi cha **Shilingi milioni 227.4** ikiwa ni mrabaha. Ili kuboresha zaidi maonesho yajayo, Wizara ilishiriki kwenye maonesho ya vito nje ya nchi yakiwemo Maonesho ya 53 ya Bangkok, Thailand; na Maonesho ya Tucson, Marekani. Ushiriki huo umesaidia kujifunza namna bora ya kuandaa maonesho ya vito na kuwashawishi wafanyabiashara wakubwa kuja kushiriki kwenye maonesho yajayo ya vito ya Arusha ambayo yamepangwa kufanyika Mwezi Novemba, 2014.

145. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2014/15, Wizara itaendelea kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini hapa nchini yakiwemo madini ya shaba, vito, dhahabu na madini ya viwandani ili kuongeza ajira, kipato kwa wananchi na mapato kwa Serikali. Aidha, Wizara itakamilisha Sheria na Kanuni za Uongezaji Thamani Madini ili kusaidia kukuza na kusimamia shughuli za uongezaji thamani madini hapa nchini.

Pamoja na juhudi hizo, baada ya kukamilisha ukarabati wa kituo cha Jimolojia kilichopo Arusha, Wizara itatekeleza mpango wa mafunzo ya uongezaji thamani kwa vitendo kwa Watanzania na hivyo kuifanya fani hiyo kuchangia ipasavyo katika ukuaji wa Sekta ya Madini na upatikanaji wa ajira mpya kwenye tasnia hiyo.

Kuimarisha Usimamizi wa Biashara ya Madini

146. **Mheshimiwa Spika**, katika juhudi za kuimarisha usimamizi wa biashara ya madini nchini, Serikali imeendelea kusimamia shughuli hizo kwa kukagua na kuhakiki madini yanayozalishwa, kuthaminisha, na kutoa vibali vya kuruhusu kusafirishwa kwenda nje. Katika kutekeleza lengo hilo, jumla ya leseni 621 za

Nakala ya Mtando (Online Document)

biashara ya madini (dealers - 361 na brokers - 260) zimetolewa kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010.

Aidha, katika kupambana na wimbi la utapeli na udanganyifu katika biashara ya madini, Wizara imeanzisha mpango wa kutangaza wamiliki wa leseni halali za biashara ya madini kupitia tovuti yake ili kusaidia wanunuvi wa madini kuwafahamu wafanyabiashara halali wa madini.

147. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2014/15 Wizara itaimarisha ukaguzi wa biashara ya madini ili kupunguza udanganyifu unaoikosisha Serikali mapato. Pia, Serikali itakamilisha mazungumzo na nchi za India, Kenya na Marekani ili kuzishawishi kukubali kutambua Certificate of Origin ya Tanzanite. Hatua hii itapunguza utoroshaji wa madini.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za umma itaimarisha msako kwa ajili ya kuwabaini na kuwakamata wanaojihusisha na utapeli katika biashara ya madini.

Kuendelea Kuvutia Uwekezaji katika Sekta ya Madini

148. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14, Serikali imeendelea kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Madini kwa kushiriki kwenye warsha na maonesho ya ndani na nje ya nchi yanayokutanisha wawekezaji katika Sekta ya Madini, kwa mfano INDABA (Afrika Kusini), PDAC (Canada) na ADUC (Australia). Kupitia fursa hii, Serikali imetoa taarifa mbalimbali kuhusu mazingira wezeshi ya uwekezaji katika Sekta ya Madini ikiwa ni pamoja na taarifa za kijiolojia ili kuvutia wawekezaji.

149. **Mheshimiwa Spika**, ili kuendelea kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Madini, kwa Mwaka 2014/15 Wizara itaendelea kushiriki katika warsha na maonesho mbalimbali ya ndani na nje ambayo huhudhuriwa na wawekezaji mbalimbali. Aidha, Wizara itaendelea kutoa taarifa za kijiolojia kupitia Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST) zinazohitajika katika shughuli za utafutaji wa madini pamoja na kuboresha huduma za utoaji wa leseni ili zipatikane kwa wakati.

Kuimarisha Mazingira ya Kazi katika Ofisi za Madini za Kanda

150. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuimarisha Ofisi za Madini za Kanda ikiwa ni pamoja na kujenga ofisi za kudumu. Katika Mwaka 2013/14, taratibu za kujenga Ofisi za Dodoma, Mpanda na Mtwara zimeanza. Lengo la Wizara ni kuboresha mazingira ya kazi ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji

Nakala ya Mtando (Online Document)

majukumu likiwemo ukusanyaji wa maduhuli. Kwa Mwaka 2014/15, Wizara itaendelea kuimarisha na kuboresha vitendea kazi kwenye Ofisi zote za Madini za Kanda na Maafisa Madini Wakazi na kukamilisha ujenzi wa ofisi za Dodoma, Mpanda na Mtwara.

Asasi ya Uwazi katika Tasnia ya Uziduaji (Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative – TEITI)

151. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14 Kamati Tekelezi ya TEITI ilikamilisha rasimu ya Sheria itakayosimamia shughuli zake. Nchi wanachama wa EITI ambazo tayari zina Sheria hiyo zilishirikishwa katika maandalizi ya rasimu hiyo. Nchi hizo ni Ghana, Liberia na Nigeria. Lengo lilikuwa ni kupata maoni na uzoefu wa nchi hizo katika utekelezaji wa Sheria hiyo. Maoni yaliyopatikana Mwezi Oktoba, 2013 yametumika kuboresha rasimu hiyo, na taratibu za maandalizi ya muswada zinaendelea ili uwasilishwe katika kikao cha Bunge kabla ya Mwezi Novemba, 2014.

152. **Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za Serikali za kuweka wazi mapato yanayotokana na shughuli za kampuni zinazofanya utafutaji na uchimbaji wa madini, mafuta na gesi asilia, TEITI iliendesha warsha kwa Waandishi wa Habari, Asasi za Kiraia na wananchi juu ya matokeo ya Ripoti ya Tatu ya TEITI katika maeneo yenye uwekezaji. Jitihada hizi zinalenga kuwajengea wananchi uwezo wa kuhoji Serikali katika usimamizi wa rasilimali hizo. Warsha hizi zilifanyika tarehe 28 Juni, 2013 na 03 Julai, 2013 Jijini Dar es Salaam; tarehe 03 - 05 Julai, 2013 Jijini Arusha; tarehe 30 Septemba - 02 Oktoba, 2013 Jijini Mwanza; na tarehe 04 - 06 Novemba, 2013 Lindi na Mtwara.

153. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa asasi ya EITI imefanya marekebisho ya masharti ya uanachama ili kuongeza kasi ya kuleta mabadiliko yanayokusudiwa katika kuongeza manufaa ya uvunaji wa rasilimali kwa wananchi kwenye nchi wanachama. Kuanzia Mwezi Julai, 2013 utekelezaji katika nchi wanachama ulianza kupimwa kwa kutumia viwango (EITI Standard) badala ya Kanuni za Mwaka 2011.

Katika mabadiliko hayo, nchi wanachama zinatakiwa pamoja na hatua nyingine kuweka wazi rejista ya majina ya watu na kampuni zinazomiliki leseni za utafutaji na uchimbaji wa madini, mafuta na gesi asilia.

154. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mpango wa EITI umekuwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na utoaji wa takwimu zilizo nje ya kipindi husika na ucheleweshaji wa upatikanaji wa takwimu hizo kutoka kampuni za uchimbaji wa madini na gesi asilia; na kutoka katika Taasisi za Serikali zinazokusanya mapato, na hivyo kuathiri utoaji wa ripoti za TEITI kwa wakati. Ili kuondoa tatizo hili, natoa wito kwa kampuni na Taasisi za Serikali kuwasilisha takwimu sahihi na kwa wakati.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

155. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2014/15, Kamati Tekelezi ya TEITI itaendelea kuandaa Sheria ya TEITI pamoja na kujenga uwezo juu ya uendeshaji wa EITI kwa wajumbe wa Kamati na Sekretarieti Tekelezi ya TEITI. Katika kipindi hiki Kamati imepanga kuelimisha na kuhamasisha wananchi juu ya maeneo yafuatayo: utekelezaji wa EITI kwa kuchapisha na kusambaza taarifa za TEITI kwa Mwaka 2011/12 na 2012/13; kukamilisha matayarisho ya Taarifa ya Tano ya TEITI inayohusisha malipo ya kodi na mapato ya Mwaka 2012/13; kusimamia tafiti mbalimbali za kupanua wigo wa utekelezaji wa EITI; kutekeleza mpango wa mawasiliano na kuendesha warsha na semina juu ya utekelezaji wa mpango wa TEITI; na kuiwezesha kifedha Sekreterieti na Kamati Tekelezi ya TEITI. Aidha, Kamati itazijengea uwezo Asasi za Kiraia, Idara za Serikali na kampuni za uziduaji juu ya utekelezaji wa mpango wa TEITI.

Uchambuzi na Uthamanishaji wa Madini ya Vito Kupitia TANSORT

156. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai 2013 hadi Machi 2014, TANSORT ilithamini na kusimamia uuzwaji wa karati 128,000 za almasi zenyet thamani ya **Dola za Marekani milioni 33.3**, sawa na **Shilingi bilioni 54.61**. Mauzo ya almasi hizo yaliingizia Serikali mapato ya **Dola za Marekani milioni 1.7**, sawa na **Shilingi bilioni 2.79** ikiwa ni mrabaha. Aidha, Kitengo kilithamini tani 24,000 za madini ya mapambo; gramu milioni 10 za vito ghafi; na karati 166,000 za vito vilivyochochongwa vikiwa na thamani ya **Dola za Marekani milioni 25.2**, sawa na **Shilingi bilioni 41.33**.

Mauzo ya madini hayo yote ya vito yaliingizia Serikali mapato ya **Dola za Marekani milioni 0.98**, sawa na **Shilingi bilioni 1.61**.

157. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2014/15, TANSORT itaendelea kutekeleza majukumu yake yakiwemo: kuthamanisha almasi na madini ya vito ili kuwezesha Serikali kupata malipo stahiki ya mrabaha; kutayarisha miongozo ya bei ya almasi na madini ya vito; kutoa huduma za kijemolojia kwa wachimbaji wadogo na wa kati; kusimamia mauzo ya almasi na madini ya vito ndani na nje ya nchi; kufanya tafiti za masoko na bei za vito; na kutoa ushauri kwa wachimbaji wadogo na wa kati kuhusu masoko, ukataji na ukadiriaji thamani ya vito.

Kuwezesha Mashirika na Taasisi za Serikali katika Sekta ya Madini

Chuo cha Madini cha Dodoma - MRI

Nakala ya Mtandao (Online Document)

158. **Mheshimiwa Spika**, uamuzi wa kukigeuza Chuo cha Madini Dodoma kuwa Polytechnic umeanza kutekelezwa katika Mwaka 2013/14. Jambo muhimu katika hatua hii ni kukipa Chuo mamlaka ya kijiendesha (autonomy), ambapo Wizara ya Nishati na Madini imewasilisha mapendekezo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa hatua zaidi.

Aidha, maandalizi ya kukikabidhi Chuo cha Madini eneo la Mgodi wa Golden Pride (Nzega) uliofungwa yanaendelea ambapo makabidhiano rasmi yatafanyika Mwezi Desemba, 2014. Pamoja na juhudhi hizo, Chuo cha Madini kimeandaa Makubaliano ya Awali (MoU) yatakayowezesha kushirikiana na Chuo cha Southern Alberta Institute of Technology (SAIT Polytechnic) cha Canada. Lengo la hatua hii ni kuwezesha Chuo hiki kupata uzoefu wa kimataifa.

159. **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Madini Dodoma kimeendelea kuongeza idadi ya wanafunzi kutoka 35 Mwaka 2005/06 hadi 547 kwa Mwaka 2013/14 katika ngazi ya Cheti na Stashahada.

Chuo hiki kinatoa mafunzo katika fani za Jiolojia na Utafutaji Madini; Uhandisi Uchimbaji Madini; Uhandisi Uchenjuaji Madini; Sayansi za Mafuta na Gesi Asilia; na Uhandisi Usimamizi wa Mazingira Migodini. Aidha, katika Mwaka 2014/15, Chuo kitaanzisha kozi mpya ya Upimaji Migodi (Mine Surveying) na Jimolojia (Gemology) katika ngazi ya Cheti na Stashahada.

160. **Mheshimiwa Spika**, kuanzia Mwaka 2012/13 Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini iliamua kwa makusudi kudhamini wanafunzi wa Tanzania kusomea fani za mafuta na gesi asilia ndani na nje ya nchi. Lengo ni kuhakikisha kwamba Wataalam wa Kitanzania wa kuhudumia Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia wanapatikana. Hadi sasa, wanafunzi 109 wanapata udhamini katika Chuo cha Madini katika ngazi ya Stashahada.

Aidha, katika kujenga uwezo wa Chuo hicho, jumla ya Wakufunzi 6 wanahuduria mafunzo ya Shahada za Uzamili na Uzamivu katika nchi za Australia, Kenya, Sweden na hapa nchini. Aidha, Chuo kitaendeleza watumishi kitaaluma na kitaalamu ili waweze kutoa mafunzo yaliyokusudiwa ipasavyo kwenye Sekta za Nishati na Madini.

Shirika la Madini la Taifa - STAMICO

161. **Mheshimiwa Spika**, katika Hotuba yangu ya Mwaka 2013/14 niliahidi kuwa Serikali itafanya kila linalowezekana ili kuimarisha utendaji wa Shirika hilo. Miiongoni mwa hatua zilizochukuliwa na Wizara ni kuwezesha STAMICO kuajiri watumishi wapya 78 ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Aidha, Shirika liliendeleza mradi wa Buckreef kwa ubia na Kampuni ya TANZAM 2000 kwa kukamilisha utafiti wa kimaabara wa njia bora za uchenjuaji miamba (metallurgical studies) katika maeneo ya Bingwa, Buckreef na Tembo Mines katika Mkoa wa Geita. Taratibu za uagizaji wa vifaa na mitambo kwa ajili ya uchimbaji na uzalishaji dhahabu zimeanza kwa lengo la kuanza uzalishaji Mwezi Novemba, 2014.

162. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na kukamilisha utafiti wa Buckreef, Mwezi Aprili, 2014 Shirika lilianza maandalizi ya kuchenjua mabaki ya uchimbaji wa zamani (tailings) katika eneo la Buhemba. Aidha, mkataba rasmi wa ubia kati ya STAMICO na TanzaniteOne Mining Limited ulisainiwa Mwezi Desemba, 2013. Chini ya ubia huo, mgawanyo wa faida ni **asilimia 50 kwa 50** na watumishi wa STAMICO wamepelekwa mgodini kusimamia maslahi ya Taifa. Vilevile, STAMICO kupitia Kampuni yake tanzu ya STAMIGOLD imeshaanza uendelezaji wa maeneo ya "West Zone na Moja Moja" kwa kujenga barabara inayounganisha maeneo hayo na mitambo ya uchenjuaji ya mgodi wa Tulawaka uliopo Wilaya ya Biharamulo.

163. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2014/15 STAMICO imepanga kufanya yafuatayo: kuendeleza migodi ya Buckreef (Geita), Buhemba (Butiama), Tulawaka (Biharamulo) na TanzaniteOne (Simanjiro). Aidha, Shirika litaanzisha ununuzi na uchenjuaji wa madini ya bati (tin ore) katika Mkoa wa Kagera na kufanya utafiti wa madini Rare Earth Metals katika leseni zake zilizopo Wilaya ya Nkasi.

Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania - TMAA

164. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2013/14, TMAA ilitekeleza majukumu yake na kuwezesha kupatikana mafanikio mbalimbali. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2013 hadi Aprili 2014, baadhi ya migodi mikubwa iliendelea kulipa kodi ya mapato kutokana na ukaguzi uliofanywa na TMAA kwa kushirikiana na TRA. Baadhi ya Kampuni hizo ni Resolute Tanzania Limited (Nzega, Tabora) iliyolipa **Shilingi bilioni 3.38** na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (Geita) iliyolipa **Shilingi bilioni 50.6** kama kodi ya mapato.

Aidha, ukaguzi uliofanywa na Wakala umewezesha **jumla ya Shilingi bilioni 4.86** kulipwa Serikalini na baadhi ya wamiliki wa migodi mikubwa na ya kati. Malipo hayo yanajumuisha mrabaha, ushuru wa huduma, ada ya mwaka ya leseni na kodi ya zuio.

165. **Mheshimiwa Spika**, ukaguzi uliofanywa na TMAA uliwezesha kukusanywa kwa mrabaha kutokana na madini ya ujenzi na viwandani katika Kanda za Mashariki, Kusini, Magharibi, Kati na Ziwa Victoria ambapo jumla ya **Shilingi**

Nakala ya Mtandao (Online Document)

bilioni 1.72 zililipwa kama mrabaha katika kipindi cha Julai 2013 hadi Aprili 2014. Malipo hayo yametokana na uzalishaji wa jumla ya tani milioni 5 za madini ya ujenzi na viwandani yaliyokaguliwa na Wakala yenye thamani ya **Shilingi bilioni 56.8.**

166. **Mheshimiwa Spika**, Serikali iliendelea kupata mrabaha na takwimu sahihi za madini yaliyozalishwa na migodi mikubwa kutokana na ukaguzi na uhakiki wa madini yaliyozalishwa na kuuzwa na migodi mikubwa ya Bulyanhulu (Shinyanga), Buzwagi (Shinyanga), Geita (Geita), Golden Pride (Tabora), New Luika (Mbeya), North Mara (Mara), Mwadui (Shinyanga), TanzaniteOne (Manyara) na Tulawaka (Kagera). Ukaguzi huo ulisaidia kujua kiasi na thamani halisi ya madini yaliyozalishwa na kuuzwa katika kipindi husika. Ukaguzi huo umewezesha kukusanywa mrabaha wa jumla ya **Dola za Marekani milioni 72.90**, sawa na **Shilingi bilioni 119.56** kwa Mwaka 2013.

167. **Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti utoroshaji wa madini na ukwepajji wa mrabaha, Wakala umeendelea kufanya ukaguzi kuitia madawati maalum kwenye Viwanja vya Ndege vya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Mwanza. Kwa Mwaka 2013, ukaguzi huo umewezesha kukamatwa kwa watoroshaji wa madini katika matukio 32 yaliyopotiwa katika viwanja hivyo. Matukio hayo yanahusu utoroshaji wa madini nje ya nchi yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.1. Wahusika wamefikishwa mahakamani na baadhi yao wamehukumiwa na madini yao kutaifishwa na Serikali kwa mujibu wa Sheria za nchi.

168. **Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka 2014/15, Serikali itaendelea kuimarisha ukaguzi wa shughuli za uzalishaji na biashara ya madini kwa migodi mikubwa, ya katika midogo kuitia Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA) ili kuhakikisha kuwa Taifa linanufaika ipasavyo na rasilimali yake ya madini.

Aidha, Wizara kuitia TMAA itaendelea kuchukua hatua za makusudi kuelimisha umma kuhusu manufaa yanayopatikana kwenye Sekta ya Madini kama njia ya kukabiliana na udanganyifu unaofanywa na baadhi ya watu kwa lengo la kupotosha umma.

169. **Mheshimiwa Spika**, Wakala pia utaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa kununua vitendea kazi vinavyohitajika na kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma na kujenga uwezo katika kubainisha maoteo ya mapato ya Serikali kutoka kwenye Sekta ya Madini kwa kutumia mfumo wa kisasa (revenue forecasting model) ili kuwa na takwimu za uhakika za mapato ya Serikali kutokana na Sekta ya Madini. Aidha, Wakala utakamilisha taratibu za usajili wa Maabara ya Wakala katika Shirika la Viwango vya Kimataifa (ISO 17025) ili iweze kutambulika kimataifa.

170. **Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka 2013/14, Wakala umefanya utafiti wa kijolojia na upatikanaji madini katika QDSs kumi na nane (18) kwenye Wilaya za Bagamoyo, Chamwino, Chunya, Dodoma, Handeni, Ikungi, Iramba, Kilindi, Ludewa, Makete, Mbinga, Mkalama, Mvomero, Singida na Songea Vijiji. Uchoraji wa ramani hizo unaendelea kukamilishwa. Aidha, Wakala umekamilisha utafiti wa jiomeria katika QDSs saba (7) kwa ajili ya utafutaji madini kwenye Wilaya za Dodoma, Ikungi, Iramba, Manyoni, Mkalama na Singida.

171. **Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza Sekta ya Madini nchini, Wakala pia ulifanya utafiti wa kina wa kijofizikia (ground geophysical surveys) kwenye QDSs saba (7) katika Wilaya za Bagamoyo, Handeni, Iramba, Kilindi, Mkalama na Singida kwa ajili ya kufuatilia maeneo yaliyoonesha kuwa na viashiria vizuri vya kuwepo madini kutokana na utafiti wa kijofizikia kwa kutumia ndege. Matokeo ya utafiti huo yanaendelea kutafsiriwa na taarifa zake zinaandaliwa na zitakamilishwa kabla ya Mwezi Januari, 2015.

172. **Mheshimiwa Spika**, ili kujimarisha kiutendaji, Wakala umebadilisha mfumo wa kuhifadhi na kusambaza taarifa na takwimu za jiosayansi kwa kuziweka kwenye Computer Based Centralized Geo-Scientific Data and Information Management Systems. Mabadiliko hayo yanawezesha kuwa na takwimu za uhakika, zinazopatikana kwa urahisi na kwa wadau wengi zaidi.

173. **Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka 2014/15, Wakala umejipanga kuendeleza tafiti za kijiosayansi za upatikanaji madini, hususan technology metals, upatikanaji wa nishati ya jotoardhi, gesi za Helium (Mara) na Carbon Dioxide (Mbeya) na kuchora ramani 4 za kijolojia katika Wilaya za Kilwa, Liwale, Nachingwea na Ruangwa pamoja na ramani mbili (2) za kijiomeria katika Wilaya za Liwale na Ruangwa.

Changamoto katika Sekta ya Madini

174. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Sekta ya Madini imekabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo: upatikanaji wa masoko ya uhakika ya baadhi ya madini yanayozalishwa na wachimbaji wadogo; kiwango kidogo cha uwekezaji wa mitaji katika uchimbaji mdogo wa madini; kiwango kidogo cha fungamanisho la Sekta ya Madini na sekta nyingine za uchumi; utoroshaji wa madini nje ya nchi; na upungufu wa watumishi wenye ujuzi katika kusimamia Sekta ya Madini.

Mipango ya Kukabiliana na Changamoto Zilizojitokeza

175. **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, Wizara itaendelea kuboresha na kuimarisha Idara ya Madini kwa kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi na watumishi katika Ofisi zake. Aidha, Wizara itaimarisha ukaguzi wa shughuli za uzalishaji na biashara ya madini nchini ili kuendelea kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini nje ya nchi.

C. AJIRA NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

176. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2013/14 Wizara imeendelea kuajiri na kuendeleza watumishi wake ili waweze kufanya kazi kwa weledi na ufanisi zaidi ikilenga kuinua mchango wa Sekta za Nishati na Madini kwenye Pato la Taifa.

Katika kipindi hicho, jumla ya watumishi walioajiriwa na Wizara na Taasisi zake katika kada mbalimbali ni 227. Kati ya hao, Wizara iliajiri watumishi 36, TMAA 11, STAMICO 78, REA 4 na TPDC 51. Vilevile, TPDC inaendelea na utaratibu wa kuajiri watumishi wapya 226.

Aidha, katika kuendeleza watumishi, Wizara ilipeleka watumishi 80 katika mafunzo ya muda mfupi na watumishi 60 katika mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi. Katika Mwaka 2014/15, Wizara na Taasisi zake inatarajia kuajiri jumla ya watumishi 508 katika kada mbalimbali. Kati ya hao, watakaoajiriwa na Wizara ni watumishi 207; TMAA 29; STAMICO 79; GST 52; MRI 74; TPDC 51; na REA 16.

177. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia kwa kutambua kwamba masuala ya mafuta na gesi asilia ni maeneo mapya nchini, itaendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Rasilimali Watu (Marshall Plan on Capacity Building and Development in Oil and Gas Industry). Hii ni mionganini mwa mipango ya Serikali kuhahakikisha kuwa nchi inakuwa na wataalamu wa Kitanzania wa kutosha katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia.

Mpango huu unashirikisha vyuo mbalimbali nchini vikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na Chuo Kikuu cha Dodoma ambavyo pamoja na fani nyininge vimeanzisha pia mitaala kuhusu mafuta na gesi asilia (BSc in Petroleum Engineering, Petroleum Chemistry na BSc Petroleum Geology).

178. **Mheshimiwa Spika**, baada ya mitaala hiyo kuanzishwa, Wizara kwa Mwaka 2013/14 ilitoa ufadhili kwa vijana wa Kitanzania 9 katika Chuo Kikuu cha Dodoma kusomea Shahada ya uhandisi wa Mafuta na Gesi Asilia; 109 Chuo

Nakala ya Mtandao (Online Document)

cha Madini Dodoma kusomea Stashahada ya Sayansi ya Mafuta na Gesi Asilia; 59 VETA – Mtwara kwa wanafunzi wanaotoka maeneo ya Lindi na Mtwara kusomea ufundi stadi ambao utawawezesha kupata ajira sehemu za uzalishaji wa mafuta na gesi asilia; na wanafunzi 9 kusomea Shahada ya Uzamili katika masuala ya Mafuta na Gesi Asilia huko Uingereza.

Aidha, Watanzania 8 walipata ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China na mmoja nchini Ufaransa kusomea Shahada ya Uzamili ya Mafuta na Gesi Asilia. Vilevile, watumishi 38 kutoka Taasisi mbalimbali walihudhuria mafunzo ya muda mfupi yaliyofadhiliwa na Serikali ya Uhlanzi ambayo yalifanyika nchini Tanzania na Uhlanzi. Vilevile, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimewezesha jumla ya wanafunzi 19 kwenda nchini Norway kusomea Shahada ya Uzamili ya Mafuta na Gesi Asilia. Kati ya wanafunzi hao, 11 wanasoma Msc. in Petroleum Engineering na 8 wanasoma Msc. in Petroleum Geology.

179. **Mheshimiwa Spika**, ili kuendelea kuimarisha utendaji wa watumishi wake, Wizara kwa Mwaka 2014/15 inatarajia kupeleka mafunzoni watumishi 246 katika mafunzo ya muda mfupi na watumishi 95 katika mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi.

Aidha, pamoja na kuendelea kuwalipia wanafunzi wa Kitanzania walioanza masomo katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi, Wizara kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo inatarajia kuwapeleka Watanzania katika nchi mbalimbali kwenye mafunzo ya Shahada za Uzamili, ambapo 10 watasomeshwa na Serikali ya Brazil; 10 Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China; na wawili (2) Serikali ya Thailand katika masuala ya mafuta na gesi asilia.

Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na nchi na mashirika mbalimbali ili kuongeza idadi ya Watanzania watakaosomeshwa katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia kwa ajili ya kusimamia Sekta hiyo.

180. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki pia, Wizara itaanzisha mpango maalum wa kutoa mafunzo ya kusimamia Sekta ya Nishati kwa kushirikisha Washirika wa Maendeleo wa Umoja wa Ulaya (EU), Serikali ya Sweden na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP). Fedha zitakazotumika kutekeleza mpango huo, ambazo zimetengwa katika Bajeti ya Mwaka 2014/15 ni **Shilingi bilioni 7.80** sawa na **Dola za Marekani milioni 4.76**.

181. **Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza tija na motisha kwa watumishi, kwa Mwaka 2013/14 Wizara iliwapandisha vyeo jumla ya watumishi 57 katika fani mbalimbali na kuwathibitisha kazini watumishi 36. Katika Mwaka 2014/15 Wizara inatarajia kuwapandisha vyeo watumishi 157 ambao wamepata sifa za

Nakala ya Mtando (Online Document)

kitaaluma na wenyе utendaji mzuri wa kazi kulingana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 1999. Aidha, ili kuongeza ufanisi wa masuala ya Sheria katika Sekta za Nishati na Madini zinazokua kwa kasi, Serikali imeboresha muundo wa Wizara ya Nishati na Madini kwa kukipandisha hadhi Kitengo cha Sheria na kuwa Idara kamili.

182. **Mheshimiwa Spika**, katika kujali afya za watumishi, kwa Mwaka 2013/14, Wizara ya Nishati na Madini imeendelea kutekeleza Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 2 wa Mwaka 2006 kwa kuwashudumia watumishi wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU) na wenyе Ukimwi waliojitekeza kwa kuwapa lishe na madawa maalumu.

Katika Mwaka 2014/15, Wizara itaendelea kutoa elimu mahali pa kazi ili kuzuia maambukizi mapya na kuwashudumia waathirika wa Ukimwi kadri watakavyojitekeza. Sambamba na jitihada hizo, Wizara pia itaendelea kuhamasisha watumishi kupima afya hususan kuhusiana na magonjwa ya shinikizo la damu (blood pressure), kisukari na saratani.

Elimu kwa Umma kuhusu Rasilimali za Nishati na Madini

183. **Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza uelewa kuhusu masuala mbalimbali katika Sekta za Nishati na Madini, kuanzia Mwaka 2013/14 Wizara imeweka Mpango wa kutoa elimu kwa wananchi. Ili kuwafikia wananchi wengi zaidi, Wizara inatumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na vyombo vya habari na Viongozi wa aina mbalimbali wakiwemo Viongozi wa Dini. Mpango huo ulizinduliwa rasmi Jijini Dar es Salaam na Mhe. Dkt Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwezi Januari, 2014.

184. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza mpango huo, kati ya Mwezi Januari na Machi 2014, Wizara imefanikisha kufanyika kwa makongamano matatu (3) katika Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Pwani kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kuhusu Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia pamoja na Sekta ya Madini, yakilenga pamoja na mambo mengine, kuonesha faida zinazopatikana kwa Watanzania katika uwekezaji kwenye rasilimali hizo. Katika Makongamano hayo jumla ya **washiriki 605** walihuduria, kati ya hao 209 walikuwa katika Kongamano liliofanyika Dar es Salaam, 227 Lindi na Mtwara na 169 Pwani.

185. **Mheshimiwa Spika**, kimsingi makongamano hayo yamekuwa na mafanikio makubwa, ikiwa ni pamoja na washiriki kupata ufanuzi ulio sahihi katika masuala yanayohusu Sekta za Nishati na Madini. Washiriki wengi wamekiri kuelimika na kuahidi kueneza elimu sahihi katika maeneo yao. Aidha, kupitia makongamano haya, washiriki hao kwa niaba ya Watanzania walishuhudia kwa vitendo juhudzi zinazofanywa na Serikali katika kuendeleza Sekta hizo kwa manufaa ya Watanzania. Moja ya ushuhuda ni ule uliotokea wakati Washiriki wa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kongamano la Mikoa ya Mtwara na Lindi walipotembelea eneo la Madimba panapojengwa mitambo ya kusafisha gesi asilia, ambapo mmoja wao alitamka wazi kuwa "kumbe Serikali inafanya mambo makubwa lakini wananchi kwa kutoyajua, wanaendelea kudanganywa kila siku kwa kupewa taarifa zisizo sahihi".

186. **Mheshimiwa Spika**, ili kuendeleza mafanikio hayo, Wizara katika Bajeti yake ya Mwaka 2014/15 imeamua kwa dhati kuanzisha programu maalum ya kuelimisha umma (Public Awareness Program), ambayo itawezesha Wizara kutoa elimu juu ya utekelezaji wa shughuli zake kwa kutumia njia mbalimbali zikiwemo luninga, magazeti, redio, makongamano, tovuti na mihadhara. Lengo la Wizara ni kuendelea kutoa elimu kwa Watanzania juu ya Sekta hizo ili kuwa na taarifa sahihi za shughuli zinazotekelawa na Serikali yao na faida zinazopatikana.

D. USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

187. **Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa shughuli zake, Wizara ya Nishati na Madini inaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali. Kwa niaba ya Serikali napenda kutoa shukrani kwa Serikali za Algeria, Brazil, Canada, China, Finland, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Sweden, Thailand, Trinidad na Tobago, Ujeruman na Urusi.

Vilevile, natoa shukrani kwa Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Exim ya China, Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini (DBSA), Benki ya HSBC, Benki ya BADEA, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Umoja wa Ulaya (EU), pamoja na Taasisi na Mashirika ya AFD (Ufaransa), CIDA (Canada), DANIDA (Denmark), ECDF (Korea Kusini), FINIDA (Finland), JICA (Japan), MCC (Marekani), NORAD (Norway), OFID (Saudi Arabia), ORIO (Uhulanzi), Sida (Sweden), IFC, UNDP, Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola, Climate Investment Fund (CIF), USAID (Marekani) na JBIC (Japan).

E. SHUKRANI

188. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru Naibu Mawaziri wa Wizara ya Nishati na Madini, Mhe. Stephen Julius Masele, Mbunge - Jimbo la Shinyanga Mjini, anayesimamia masuala ya Madini; na Mhe. Charles Muhangwa Kitwanga, Mbunge - Jimbo la Misungwi, anayesimamia masuala ya Nishati.

Nikiri wazi kuwa Naibu Mawaziri hao wamekuwa msaada mkubwa kwangu katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini. Aidha, namshukuru kwa dhati aliyekuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mhe. George Boniface Simbachawene, Mbunge - Jimbo la Kibakwe kwa mchango

Nakala ya Mtando (Online Document)

mkubwa alioutoa akiwa Wizara ya Nishati na Madini. Namtakia mafanikio katika majukumu yake mapya aliyoominiwa na Mhe. Rais katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

189. **Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Mwenyekiti, Makamu na wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwanza kwa ushauri na maelekezo yao wanayoyatoa katika kuongeza ufanisi wa Wizara yangu. Kamati hii imekuwa chachu muhimu katika kutoa miongozo ya kusaidia kutatua matatizo na changamoto zinazoikabili Wizara. Nawashukuru viongozi na wajumbe wote wa Kamati hii na ni matumaini yangu kuwa wataendelea kutoa ushirikiano ili kuendeleza Sekta za Nishati na Madini kwa faida ya Watanzania wote.

190. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee nawashukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Bw. Eliakim C. Maswi, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Mhandisi Ngosi X. Mwihava kwa ushirikiano wanaonipa na kwa utendaji wao mahiri ambao unaiwezesha Wizara hii kusonga mbele siku hadi siku. Nakiri kuwa viongozi hawa wamekuwa kiungo muhimu na wenye umakini mkubwa katika timu yangu ya ushindi ya Wizara. Aidha, nawashukuru Kamishna wa Nishati na wa Masuala ya Petroli; Kamishna wa Madini; Wakuu wa Idara, Sehemu na Vitengo.

191. **Mheshimiwa Spika**, nawashukuru sana Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi za EWURA, PICL, PUMA, REA, STAMICO, TANESCO, TIPER na TPDC; Wenyeviti wa Bodi za Ushauri za GST, TMAA na MRI pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Madini kwa ushirikiano wanaonipa katika kuongoza Wizara. Ili Bodi hizi zifanye kazi vizuri zinahitaji Menejimenti nzuri na yenye mwono wa mabadiliko.

Nawapongeza sana Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara; na watumishi wote kwa ujumla kwa ushirikiano wao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ndani ya Wizara, Taasisi na Kampuni zetu.

192. **Mheshimiwa Spika**, kwa unyenyekevu kabisa napenda kuwashukuru na kuwapongeza Viongozi wote wa Dini nchini kwa kukubali kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini katika kuelimisha jamii kwa kauli mbiu isemayo "**Uendelezaji wa Rasilimali za Gesi Asilia, Mafuta na Madini kwa Amani na Maendeleo ya Nchi Yetu**". Kupitia viongozi hawa Wizara imeendelea kuelimisha jamii juu ya rasilimali zake katika makongamano mbalimbali nchini. Aidha, navishukuru vyombo vya habari na wadau wengine kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini katika kutoa habari na kuelimisha wananchi juu ya uendelezaji wa rasilimali zetu kwa manufaa ya Taifa letu. Nawaomba Viongozi wa Dini na wadau wengine tuendelee kushirikiana ili kuleta maendeleo endelevu kupitia rasilimali za nishati na madini. Napenda kuwahakikisha kuwa Wizara ya Nishati

Nakala ya Mtandao (Online Document)

na Madini haitarudi nyuma katika kutafuta ufumbuzi wa matatizo na changamoto mbalimbali zinazoikabili na itaendelea kushirikisha jamii na wananchi kwa ujumla katika hatua zake za utekelezaji.

193. **Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa namshukuru sana mke wangu Bertha Muhongo pamoja na wanangu Godfrey Chirangi, Dkt. Musuto Chirangi, Dkt. Bwire Chirangi, Rukonge Muhongo, ndugu, marafiki na Wananchi kwa ujumla kwa msaada mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kusimamia Wizara ya Nishati na Madini kwa umakini na ubunifu wa hali ya juu.

F: HITIMISHO

194. **Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Mwaka 2014/15 inakusudia kuimarisha na kuendeleza Sekta za Nishati na Madini ili kuongeza zaidi mchango wake katika kujenga uchumi imara wa Taifa utakaota ajira mpya kwa Watanzania na kupunguza umaskini nchini.

195. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe Bajeti ya jumla ya **Shilingi 1,082,555,622,000.00** kama ifuatavyo:

(i) Bajeti ya Maendeleo ni **Shilingi 957,177,170,000.00** sawa na **asilimia 88.4** ya Bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 652,805,000,000.00** ni fedha za ndani, sawa na **asilimia 68.2** ya fedha za maendeleo na **Shilingi 304,372,170,000.00** sawa na **asilimia 31.8** ni fedha za nje; na

(ii) Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 125,378,452,000.00** sawa na **asilimia 11.6** ya Bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo **Shilingi 26,912,948,000.00** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara, Mashirika na Taasisi zake (sawa na **asilimia 21.47** ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida au **asilimia 2.49** ya Bajeti yote) na **Shilingi 98,465,504,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C), sawa na **asilimia 78.53** ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida au **asilimia 9.1** ya Bajeti yote.

196. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja hii imeungwa mkono. Kwa sababu muda uliobaki siwezi kuwaita Wenyeviti wa Kamati na nini, basi tutaendelea nao kesho. Ningependa kutumia nafasi hii kuwatambua watu walioko humu ndani, wengine sitasoma majina yao kwa sababu yako mengi. Kwanza kabisa Wizara hii imekuja na wataalam wake wote maana wakuu wote wa taasisi na mashirika na bodi

Nakala ya Mtandao (Online Document)

mbalimbali wakiongozwa na Katibu Mkuu ndugu Eliakim Maswi, asimame alipo. Anasaidiwa na Naibu Eng. Ngosi Mwihava, Naibu Katibu Mkuu, naomba asimame. Halafu tuna wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ambapo ipo familia yake ikiongozwa na mke wake mama Bertha Mamuya, naomba asimame hapo alipo na familia yake wako wapi, sijui. (Makof)

Wageni wa Mheshimiwa Charles Kitwanga, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, wapo familia yake ikiongozwa na mke wake Mrs. Matilda Kitwanga na watoto wake, naomba wasimame walipo. Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri, Madiwani 20 wakiongozwa na Mheshimiwa Diwani Halid Bintihazana Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya naomba hao wote wasimame madiwani kama wapo hapa naona labda kesho.

Tuna wageni nane kutoka jumboni kwake Mheshimiwa Kitwanga wakiongozwa na Katibu wa umaja wa vijana wilaya Mohamed Nassoro, hawa na wenyewe hawajaingia nafikiri watakuwepo kesho.

Pia tuna wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Stephen Masele, wapo wanafunzi watano kutoka Chuo cha Madini Dodoma, naomba wasimame waliopo, Chuo cha Madini, naona wengi wanakuja kesho, ukumbi ulikuwa umejaa. Na kuna wageni wengine wanne kutoka Jimbo la Shinyanga Mjini na wenyewe kama wapo wasimame. Lakini na wale wengine wa habari nadhani wameshaenda, labda sijui wapo!

Kuna wageni kumi wa Mheshimiwa Ole Sendeka wakiongozwa na Ndugu Sami Mollel, Mwenyekiti wa Wanunuzi na Wauzaji wa Madini ya Tanzanite (TAMIDA), hawa wapo pia, kama hawapo tatarudia kesho. Naona wageni hawa nitawasoma tena kesho kwa sababu wengine hawapo.

Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema, naomba Kamati ya Uongozi sasa hivi tukakutane, lakini wengine wote niwashukuru sana kwa kazi mliyofanya leo, niombe kwamba kesho tatarudia tena kazi kama kawaida. Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. (Makof)

(Saa 1.48 Usiku Bunge lilahirishwa hadi siku ya Ijumaa
Tarehe 30 Mei, 2014 Saa Tatu Asubuhi)